

Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya UNESCO kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika

# HISTORIA KUU YA AFRIKA •

Juzuu  
Lililofupishwa

## I Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika

MHARIRI J. KI-ZERBO



TUKI • CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM • UNESCO

Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (UNESCO)

---

Historia Kuu ya Afrika · I

---

# Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika

---

MHARIRI J. KI-ZERBO

---

Toleo Lililofupishwa

**Jina la Asili: GENERAL HISTORY OF AFRICA, VOL I**

© UNESCO 1999  
ISBN 9976 911 40 8

*Maelezo yaliyotolewa na uwasilishaji wa matini zote kwenye chapisho hili haumaanishi maoni yoyote yale kwa upande wa UNESCO kuhusu sheria ya nchi yoyote ile, mji au eneo au mamlaka yake, au kuwekea mipaka eneo lolote lile. Waandishi wanahusika na uteuzi na uwasilishaji wa taarifa za kweli zilizopo kwenye kitabu hiki na kwa maoni yaliyoelezewa ndani, ambayo si lazima yawe yale ya UNESCO na hayalifanyi Shirika liwajibike.*

*Toleo la Tafsihi ya Kiswahili limechapishwa kwa msaada wa kifedha wa UNESCO.*

---

## Historia Kuu ya Afrika · I

---

# Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika

---

---

### Toleo Lililofupishwa

#### UNESCO Historia Kuu ya Afrika

- |           |  |
|-----------|--|
| Juzuu I   | <i>Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika</i><br>Mhariri J. Ki-Zebro                                     |
| Juzuu II  | <i>Staarabu za Kale za Afrika</i><br>Mhariri G. Mokhtar  |
| Juzuu III | <i>Afrika kuanzia Karne ya Saba hadi ya Kumi na Moja</i><br>Mhariri I. Hrbek                           |
| Juzuu IV  | <i>Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Mbili hadi ya Kumi na Sita</i><br>Mhariri J. Ki-Zerbo na D.T. Niane |
| Juzuu V   | <i>Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Sita hadi ya Kumi na Nane</i><br>Mhariri B.A. Ogot                  |
| Juzuu VI  | <i>Afrika kwenye Karne ya Kumi na Tisa hadi miaka ya 1880</i><br>Mhariri J.F. Ade Ajayi                |
| Juzuu VII | <i>Afrika Chini ya Utawala wa Kigeni 1880 - 1935</i><br>Mhariri A. Adu Boahen                          |

### Toleo Lisilofupishwa la Jalada Jepesi

- |            |   |
|------------|---|
| Juzuu VIII | <i>Afrika Kuanzia 1935</i><br>Mhariri A.A. Mazrui<br>Mhariri Msaidizi C. Wondji |
|------------|---|

**Toleo lililofupishwa la  
HISTORIA KUU YA AFRIKA YA UNESCO  
Limechapishwa na:**

**Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam  
S.L.P. 35110  
Dar es Salaam, Tanzania**

**Pamoja na:  
UNESCO Publishing  
7 Place de Fontenoy, 75700, Paris**

**Kimepangwa na kuchapwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha  
Dar es Salaam, S.L.P. 35110, Dar es Salaam, Tanzania.**

---



# YALIYOMO

---

Dibaji na Amadou-Mahtar M'Bow, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO (1974-87)	vii
Wasifu wa Mradi na B.A. Agot, aliyekuwa Mwenyekiti, Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawadi Historia Kuu ya Afrika	xii
Maelezo ya Wendo	xv
Wanakamati wa Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawadi Historia Kuu ya Afrika	xvi
Orodha na Wasifu wa Waandishi waliochangia kwenye juzuu kuu.	xviii

<i>Utangulizi wa Jumla</i>	<i>1</i>
1. <i>Maendeleo ya uandikaji historia wa Afrika</i>	<i>11</i>
2. <i>Nafasi ya historia katika jamii za Kiafrika.</i>	<i>17</i>
3. <i>Mielekeo mipya katika taaluma ya uandishi wa historia ya Afrika na mchango wao katika historia kwa jumla</i>	<i>24</i>
4. <i>Marejeo na mbinu maalum zilizotumiwa katika historia ya Afrika</i>	<i>30</i>
5. <i>Marejeo ya kimaandishi kabla ya karne ya kumi na tano</i>	<i>35</i>
6. <i>Vyanzo vya kimaandishi kuanzia karne ya kumi na tano na kuendelea</i>	<i>44</i>
7. <i>Mapokeo Simulizi na mbinu zake</i>	<i>55</i>

8.	<i>Mapokeo hai</i>	63
9.	<i>Akiolojia ya Kiafrika na mbinu zake pamoja na ukadiriaji umri</i>	74
10.	<i>Historia na isimu na nadharia kuhusu mbari na historia ya Afrika</i>	90
11.	<i>Uhamaji na upambanuzi kiisimu na kimbari</i>	103
12.	<i>Uainishaji wa lugha za Kiafrika na ramani ya lugha</i>	112
13.	<i>Jiografia ya kihistoria: Vipengele vya maumbile</i>	122
14.	<i>Jioografia ya Kihistoria: Vipengee vya kiuchumi</i>	131
15.	<i>Mbinu za taaluma fungamano zilizotumika katika historia</i>	139
16.	<i>Kiunzi cha kikronolojia: enzi za mvua na barafuto za Afrika</i>	146
17.	<i>Asili ya binadamu: Matatizo ya jumla</i>	188
18.	<i>Binadamu wa mwanzo Afrika</i>	196
19.	<i>Historia ya Afrika Mashariki ya kipindi kabla ya historia.</i>	210
20.	<i>Historia ya kusini mwa Afrika ya kipindi kabla ya historia</i>	221
21.	<i>Historia ya Afrika ya Kati ya kipindi kabla ya historia</i>	240
22.	<i>Historia ya Afrika Kaskazini ya kipindi kabla ya historia</i>	250
23.	<i>Historia ya Sahara ya kipindi kabla ya historia</i>	263
24.	<i>Historia ya Afrika Magharibi ya kipindi kabla ya historia</i>	274
25.	<i>Kipindi kabla ya historia katika bonde la mto Nili</i>	284
26.	<i>Sanaa za Kiafrika za kipindi kabla ya historia</i>	298
27.	<i>Chimbuko, maendeleo na kuenea kwa mbinu za kilimo</i>	
28.	<i>Uvumbuzi na ueneaji wa metali na maendeleo ya mifumo ya jamii karne ya tano kabla ya Kristo</i>	307
	<i>Hitimisho: tokea mwanzo kabla ya ustaarabu hadi binadamu aliyejikomboa</i>	314
	<i>Bibliografia</i>	323
	<i>Farahasa</i>	329
	<i>Sherehe</i>	351

---



## Dibaji

**AMADOU - MAHTAR M'BOW**

*Mkurugenzi Mkuu wa Zamani wa UNESCO (1974-1987)*

---

Kwa muda mrefu, aina zote za uzushi na kashfa zilificha historia halisi ya Afrika kwa dunia nzima. Jamii za Kiafrika zilionekana kama jamii zisizoweza kuwa na historia. Licha ya kazi muhimu zilizofanywa na waasisi kama Leo Frobenius, Maurice Delafosse na Arturo Labriola tangu miongo ya mwanzoni mwa katne hii, wataalamu wengi wasio Waafrika hawakuweza kuondoa fikra fulani za awali walizozishikilia na wakadai kwamba kukosekana kwa kumoukumbu za maandisni kulifanya isiwezekane kufanya utafiti wowote wa kisayansi wa jamii kama hizo.

Ingawa tenzi za *Iliad* na *Odyssey* kwa usahihi zilichukuliwa kama kumbukumbu muhimu za historia ya Ugiriki ya kale, mapokeo simulizi ya Kiafrika, ambayo ndiyo kumbukumbu za pamoja za watu yanayunganisha matukio mengi yenye kuonyesha maisha yao, yanakataliwa kuwa hayana thamani. Kwa kuandika historia ya sehemu kubwa ya Afrika, kumbukumbu tu zilizotumika ni zile za kutoka nje ya bara. Matokeo yake ni kuwa kile walichoandika kilitoa sura ambayo sio ya njia halisi walizopita Waafrika, bali zile ambazo waandishi walifikiria kuwa pengine ndimo walimopita. Kwa kuwa Enzi za Kati za Ulaya mara nyingi ndizo zilizotumika kama kipimo, njia za uzalishaji, mahusiano ya kijamii na asasi za kisiasa zilitazamwa tu kwa kurejelea zama za Ulaya.

Kwa hakika, waandishi hao walikataa kuwachukulia Waafrika kama waumbaji wa tamaduni za asili ambazo zilichanua na kudumu kwa karne nyingi katika ruwaza walizozibuni na ambazo wanahistoria hawawezi kuzibaini isipokuwa pale tu watakapokubali kuachana na mawazo yao ya kashfa.

Zaidi ya hayo, bara la Afrika halikutazamwa hata kidogo kama eneo moja kihistoria. Kinyume chake, mkazo uliwekwa kwenye kila kitu kilichoelekea kuhalalisha wazo kwamba mgawanyiko ulikuwepo toka zama za kale, kati ya 'Afrika ya weupe' na 'Afrika ya Weusi', kila upande ukiwa haujui kuwa kuna watu wa upande mwingine. Mara nyingi Sahara ilielezewa kama eneo lisilopitika na hivyo kuzuia kuchanganyikana kwa makundi ya kimbari na watu au mabadilishano ya bidhaa, imani, desturi na mawazo baina ya jamii zilizozidi kukua katika kila upande wa jangwa. Mipaka iliyofungwa kabisa iliwekwa baina ya staarabu za Misri ya Kale na Unubi na ile ya watu wa kusini mwa Sahara.

Ni kweli kwamba historia ya Afrika kaskazini mwa Sahara imehusishwa kwa karibu



inno na ile ya nchi za bonde la Bahari ya Mediterani kuliko ilivyokuwa kwa historia ya Afrika Kusini mwa Sahara, lakini hivi sasa inafahamika zaidi kwamba staarabu mbalimbali za bara la Afrika, pamoja na tofauti zao za lugha na tamaduni, zinawakilisha, kwa kiasi kikubwa au kidogo, michepuo ya kihistoria ya makundi ya watu na jamii yanayounganishwa na mahusiano ya karibu yenye umri wa karne nyingi.

Jambo jingine ambalo halikutendea haki utafiti wa uhakika wa Afrika ya Kale ilikuwa ni tokezaji wa ubaguzi wa rangi, ikiwa ni pamoja na biashara ya utumwa na ukoloni, ambao ulizaa dharau na kutokuelewana na hata kupata mashiko kiasi kwamba hisia hizo kuvuruga hata dhana za msingi za uandikaji historia. Tokea wakati dhana za "mweupe" na "mweusi" zilipoanza kutumika kama vitambulisho vya jumla na wakoloni, ambao walichukuliwa kuwa watu wa daraja la juu, ilibidi Waafrika waliotawaliwa wapambane dhidi ya utumwa wa kiuchumi na wa kisaikolojia. Waafrika walitambuliwa kwa rangi ya ngozi zao, walifanywa kama bidhaa, walitayarishwa ili kufanya kazi ngumu na hatimaye, katika fikra za waliowatawala, waliishia kuashiria mbari ya *kinegro* ambayo ilibuni wa na kudaiwa kuwa mbari duni. Ruwaza hii ya utambulisho wa uwongo ilidhalilisha historia ya watu wa Afrika katika fikra za watu kufikia kiwango cha historia ya kimbari, ambamo ufahamu wa ukweli wa kihistoria na kitamaduni ulikuwa lazima upotoshwe.

Hali imebadilika vya kutosha tangu mwishoni mwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia na hasa toka nchi za Kiafrika zipate uhuru na kuanza kushiriki kikamilifu katika maisha ya jumuiya ya kimataifa na katika mabadilishano ambayo ndiyo sababu ya kuwepo kwake. Idadi kubwa ya wanahistoria wamejitahidi kukabili utafiti wa Afrika kwa mtazamo thabiti, usiopendelea na wa wazi kwa kutumia - pamoja na tahadhari zote - kumbukumbu halisi ya Kiafrika. Kwa kutumia haki yao ya kuchukua jitihada za kihistoria, Waafrika wenyewe wameihisi haja kubwa ya kuanzisha upya ukweli wa kihistoria wa jamii zao kwenye misingi thabiti.

Katika muktadha huu, umuhimu wa majuzuu haya nane ya *Historia Kuu ya Afrika*, ambayo UNESCO inachapisha unajieleza wenyewe.

Wataalamu kutoka kwenye nchi nyingi ambao wanashughulikia mradi huu walianza kwa kuweka misingi ya kinadharia na ya kimbinu kwa ajili ya *Historia* hii. Wamekuwa katika hali ngumu ya kuutilia shaka urahisishaji inno wa historia ya Afrika unaotokana na dhana ya wazo la upande mmoja na finyu kuhusu historia ya dunia na kuanzisha upya taarifa za kweli kila ilipolazimu na ilipowezekana. Wamejitahidi kuonyesha bayana data za kihistoria zinazotoa picha ya wazi kuhusu mabadiliko ya watu tofauti wa Afrika katika mandhari yao maalum ya kijamii na kitamaduni.

Ili kuikabili kazi hii kubwa, ambayo ilifanywa kuwa yenye utata na ngumu zaidi na wingi wa kumbukumbu za aina nyingi na ukweli kwamba nyaraka zilikuwa zimesambaa sana, imebidi UNESCO iende hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza, kuanzia 1963 hadi 1969, ilikuwa ni ya kukusanya nyaraka na kutayarisha mpango wa kazi. Migawanyo ya kazi ilifanyika uwandani na ilijumuisha kampeni za kukusanya mapokeo simulizi, uundaji wa vituo vya nyaraka vya kikanda kwa ajili ya mapokeo simulizi, ukusanyaji wa miswada isiyochapishwa ya Kiarabu na Kiajemi (lugha za Kiafrika zilizoandikwa kwa hati za Kiarabu), utengenezaji wa orodha ya kumbukumbu za kale na utayarishaji wa

Kiongozi cha Kumbukumbu za Historia ya Afrika (*A guide to the sources of the History of Africa*) kutokana na hifadhi za nyaraka na maktaba ya nchi za Ulaya na baadaye kuchapishwa katika majuzuu kumi na moja. Zaidi ya hayo, mikutano iliandaliwa kuwawezesha wataalamu kutoka Afrika na mabara mengine kujadili inasuala ya mbinu, na kuweka misingi wazi ya utekelezaji wa mradi huu baada ya uchunguzi makini wa kumbukumbu zilizokuwepo.

Hatua ya pili, ambayo ilianza 1969 hadi 1971, ilihusika na uwekaji sawa wa *Historia* na kuunganisha schemu zake tofauti. Madhumuni ya mikutano ya kimataifa ya wataalamu iliyofanyika huko Paris mwaka 1969 na Addis Abbaba mwaka 1970, yalikuwa ni kuchunguza na kufafanua matatizo yaliyopo kwenye kusawidi na kuchapisha *Historia*; kuitoa historia hiyo katika majuzuu manane, kuwa na chapa kuu katika Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, kuitafsiri katika lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili, Kihansa, Kifulfulde, Kiyoruba au Kilingala, matarajio ya chapa za baadaye kwa Kijerumani, Kirusi, Kireno, Kihispania na Kichina na vilevile chapa zilizofupishwa kwa ajili ya umma mpana wa Kiafrika na Kimataifa.

Hatua ya tatu imehusu usawidi wenyewe na uchapishaji. Hatua hii ilianza kwa kuteuliwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi yenye wajumbe 39, theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja wasio Waafrika, ambayo ndiyo Kamati inayochukua jukumu la kitaaluma kwa *Historia* hii.

Mbinu iliyotumika ni ya taaluma fungamano na imekitwa kwenye mkabala wenye jiha za namna tofauti na kumbukumbu za aina nyingi. Ya kwanza miongoni mwa hizi ni akiolojia, ambayo ndiyo taaluma yenye ufumbuzi kwa mambo mengi ya historia ya tamaduni na staarabu za Afrika. Kutokana na akiolojia, inakubalika sasa kuwa Afrika huenda ndio ilikuwa chanzo cha wanadamu na eneo - katika kipindi cha Neolithi - la moja ya mapinduzi ya kiteknolojia ya kwanza katika historia. Akiolojia pia imeonyesha kwamba Misri ilikuwa mahali ambapo kulikuwa na mojawapo ya tamaduni za kale maarufu mno duniani. Lakini kumbukumbu nyingine muhimu sana ni inapokeo simulizi ambayo baada ya kudharauliwa kwa muda mrefu, sasa yameibuka kama chombo muhimu cha kuvumbulia historia ya Afrika, kwa kufanya iwezekane kufuatilia mijongeo ya watu wake mbalimbali katika kitambo cha nafasi na wakati, kuelewa maono ya Kiafrika kuhusu dunia kutokea ndani mwake na kuzingatia sifa za asili za amali ambamo ndimo zilipokitwa tamaduni na asasi za bara hili.

Tunaishukuru Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi inayosiinamia *Historia Kuu ya Afrika*, na kwa Waandishi, Wahariri na Watunzi wa majuzuu mbalimbali na sura zake, kwa kuipatia mwanga mpya ukale wa Afrika katika uasilia na muundo wake mzima na kwa kuepukana na inadi katika utafiti wa masuala muhimu. Miongoni mwa masuala haya tunaweza kutaja: biashara ya watumwa, "jeraha lisilopona", ambayo ilisababisha mojawapo ya uhamishaji wa kikatili wa watu wengi katika historia ya mwanadamu, ambao ulifyonza uhai wa bara la Afrika na papo hapo kuchangia sana katika upanuzi wa uchumi na biashara huko Ulaya. Masuala mengine ni ukoloni na athari zake zote kwa idadi ya watu, uchumi, saikolojia na utamaduni, mahusiano kati ya Afrika kusini mwa Sahara na ulimwengu wa Kiarabu; na mwisho, harakati za kutokomeza ukoloni na za

ujenzi wa taifa ambazo ziliamsha akili na hisia za watu ambao baadhi yao wangali hai na pengine wangali wakiendesha harakati. Masuala haya yote yametajwa kwa kuzingatia ukweli na umakini ambazo ni sifa kubwa za *Historia* hii. Kwa kuchunguza ujuzi wetu wote wa Afrika, kutoa mawazo ya namna mbalimbali juu ya tamaduni za Afrika na kwa kutoa mtazamo mpya wa historia, *Historia* hii ina faida ya pekee ya kubainisha mwanga na kivuli na ya kudhihirisha wazi tofauti za maoni ambazo yawezekana zikawepo kati ya wataalamu.

Kwa kuonyesha kasoro katika mikabala ya kimbinu iliyotumika kwa muda mrefu katika kufanya utafiti kuhusu Afrika, *Historia* hii inadai kufanyike utafiti mpya na wenye uangalifu kwa maeneo ya matatizo ya namna mbili ya uandikaji wa historia na mahusiano yaliyopo kati yake, namna ambazo zinaunganishwa na uhusiano wa kutegemeana. Kama vile ilivyo kazi yoyote ya kihistoria yenye thamani, *Historia* hii inaandaa njia kwa ajili ya utafiti mwingi zaidi kuhusu mada za aina mbalimbali.

Ni kwa sababu hiyo kwamba Kamati ya Kisayansi ya Kisayansi, ikishirikiana kwa karibu na UNESCO, iliamua kuanzisha tafiti za ziada katika kujaribu kuyaingia kwa kina masuala kadhaa yatakayowezesha kueleweka kwa vipengele fulani vya kale ya Afrika. Matokeo ya tafiti hizo yanayochapishwa katika mfululizo wa *Mitaala na Nyaraka za UNESCO- Historia Kuu ya Afrika*<sup>1</sup> yatakuwa kijalizo muhimu kwa *Historia* hii kama zitakavyokuwa pia kazi zilizopangwa kufanyika juu ya vipengele vya historia ya taifa au ya majumbo ya Afrika.

*Historia Kuu* inatoa mwanga kuhusu umoja wa kihistoria wa Afrika na pia mahusiano ya bara hili na mabara mengine, hasa Amerika na Caribbean. Kwa muda mrefu mambo ya kibunifu ya vizazi vya Waafrika katika Amerika yalilundikwa pamoja na baadhi ya wanahistoria kama mkusanyo wa mambo mchanganyiko wa *Uafrika*. Kwa hakika huu si mtazamo wa wandishi wa *Historia* hii ambamo upinzani wa watumwa waliosafirishwa kwenda Amerika, kushiriki mfululizo na kwa wingi kwa vizazi vya Waafrika katika mapambano kwa ajili ya uhuru wa mwanzo wa Amerika na katika harakati za ukombozi wa kitaifa, yanatazamwa vizuri kama yalivyokuwa: utetezi wa dhati wa kujitambua, uliosaidia kuunda dhana ya kilimwengu ya jamii ya watu. Ingawa jambo hili linaweza likatofautiana katika sehemu mbalimbali ni dhahiri sasa kuwa namna za kuhisi, kufikiri, kuota ndoto na kutenda katika mataifa fulani ya magharibi zimeathiriwa na urithi wa Kiafrika. Urithi wa kitamaduni wa Kiafrika unaonekana kila mahali kutoka kusini mwa Marekani hadi kaskazini mwa Brazil, katika Caribbean na kwenye pwani ya Bahari ya Pacific. Katika sehemu fulani urithi huo ni msingi wa ubainisho wa kitamaduni wa baadhi ya vipengele muhimu kabisa vya watu.

*Historia* hii pia huonyesha dhahiri mahusiano ya Afrika na kusini mwa bara la Asia

<sup>1</sup> Majuzuu kumi na mbili yafuatayo yamekwishachapishwa katika mfululizo huu: *Kukaliwa kwa Misri ya Kale na ufasihi wa hati za Kimeroi; Biashara ya Utumwa Afrika tangu karne ya kumi na tano hadi karne ya kumi na tisa; Mahusiano ya kihistoria katiwa Bahari ya Hindi. Uandikaji wa historia wa Kusini mwa Afrika; Kuondoka kutoka ukolori Afrika Kusini mwa Afrika na Pembe ya Afrika; Majina ya mbari na ya sura ya nchi ya Afrika; Mahusiano ya kihistoria kijamii na kitamaduni baina ya Waafrika wengi na Waarabu tangu 1935 hadi leo; Mbinu za historia ya sasa ya Afrika; Afrika na vita vya Pili vya Dunia; Uelimishaji na uandikaji historia Afrika Kale ya Libya; Dhima ya Vyoma vya Wanafunzi wa Kiafrika kwenye mabadiliko ya kisiasa na kijamii ya Afrika kuanzia 1900 hadi 1975.*

kupitia Bahari ya Hindi na michango ya Kiafrika katika staarabu nyinginezo kutokana na mabadilishano baina yake na maeneo hayo.

Nina hakika kuwa juhudi za watu wa Afrika za kutwaa kwa nguvu au kuimarisha uhuru wao, za kupata maendeleo yao na kutetea maumbile yao ya kitamaduni lazima zitokane na utambuzi wa kihistoria uliohuishwa, wenye kushabikiwa na wa kuzingatiwa na kila kizazi.

Kwa kuangalia historia ya maisha yangu, uzoefu nilioupata kama mwalimu na kama mwenyekiti, toka siku za awali za uhuru, wa tume za mwanzo zilizoundwa kurekebisha mitaala ya historia na jiografia katika baadhi ya nchi za Afrika Magharibi na Kati, ulinifundisha jinsi ilivyokuwa muhimu kwa eliniu ya vijana na kwa taarifa kwa watu wote kwa jumla, kuwa na vitabu vilivyochapishwa na wataalamu wenye ujuzi wa ndani kuhusu matatizo na matumaini ya Afrika na wenye uwezo wa kuyaelewa mambo yote ya bara zima.

Kutokana na sababu zote hizi, shabaha ya UNESCO itakuwa ni kuhakikisha kwamba hii *Historia Kuu ya Afrika* inasambazwa katika lugha nyingi na kutumiwa kama msingi wa kuandaa vitabu vya watoto, vitabu vya kiada na vipindi vya radio na televisheni. Hivyo vijana wakiwa watoto wa shule au wanafunzi, na watu wazima katika Afrika na penginepo, wataweza kupata picha kamili ya kale ya bara la Afrika na wipengele vinavyoelezea picha hiyo na vilevile kuelewa vizuri urithi wake wa kitamaduni na mchango wake katika maendeleo ya jamii ya watu. Kwa hivyo, *Historia* hii itaweza kuchangia katika ushirikiano bora wa kimataifa na mshikamano imara miongoni mwa watu katika matumaini yao ya kupata haki, maendeleo na amani. Hii, walau, ndio tumaini langu kubwa.

Kinachobakia ni kwa mimi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kainati ya Kimataifa ya Kisayansi, mwandishi, wahariri wa majuzuu mbalimbali, waandishi na wale wote walioshiriki katika kazi hii kubwa. Kazi waliyoikamilisha na mchango waliuotoa unadhihirisha jinsi watu wenye usuli tofauti lakini wenye moyo mmoja wa ridhaa na hamasa wa kuhudumia ukweli wa kilimwengu wanavyoweza, ndani ya kiunzi cha kimataifa kilichotolewa na UNESCO, kufanikisha mradi wenye umuhimu inkubwa kisayansi na kitamaduni. Notoa shukrani pia kwa mashirika na serikali ambazo ukarimu wake umeiwezesha UNESCO kuchapisha *Historia* hii katika lugha tofauti na hivyo kuhakikisha kwamba itapata uzito inaostahiki duniani kote, na kwa jinsi hiyo kuhudumia jumuiya nzima ya kimataifa.

## Wasifu wa Mradi

B.A. OGOT'

Rais wa Zamani, Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi  
kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (1978-1983)

Mkutano Mkuu wa UNESCO katika Kikao chake cha 16 ulimwagiza Mkurugenzi Mkuu kushughulikia usawidi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kazi hii kubwa ya kutekeleza mradi ilikabidhiwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ambayo ilianzishwa na Bodi ya Utendaji mnamo 1970. Kamati hii kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bodi ya Utendaji ya UNESCO mnamo mwaka 1971, ina wajumbe thelathini na tisa (theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja ni watu wengine wasio Waafrika) wanaoshiriki kwa nafasi zao binafsi na kuteuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO kwa kipindi ambacho Kamati itadumu.

Kazi ya kwanza ya Kamati ilikuwa ni kufafanua sifa kuu za kazi hii. Hizi zilifafanuliwa katika kikao cha kwanza cha Kamati kama ifuatavyo:

- (a) Ingawa lengo lake ni kiwango cha juu kabisa cha kisayansi, Historia hii hainuii kuwa timilifu na ni kazi ya usawidi inayoepukana na inadi. Katika hali zake nyingi, historia hii ni tamko juu ya matatizo yanayoonyesha hali ya sasa ya maarifa na mikondo mikuu ya utafiti, na haisiti kuonyesha hitilafu za mtazamo pale ambapo zipo. Kwa namna hii inaweka msingi kwa kazi za siku zijazo.
- (b) Katika kazi hii Afrika inatazamwa katika ujumla wake. Nia ni kuonyesha mahusiano ya kihistoria kati ya sehemu zote za bara ambazo mara nyingi lutengwa katika kazi ambazo zimechapishwa hadi sasa. Mahusiano ya kihistoria ya Afrika na mabara mengine yanashughulikiwa ipasavyo kwa kuchanganuliwa kuzingatia mabadilishano baina yake na athari kutoka pande zote na kudhihirisha, katika mwananga halisi, mchango wa Afrika kwa historia ya mwanadamu.
- (c) Kwa mahususi, *Historia Kuu ya Afrika* ni historia ya mawazo na staarabu, jamii na asasi. Imetegemezwa kwenye vyanzo vingi vya aina mbalimbali ikiwa ni panaoja na mapokeo simulizi na namna za sanaa.
- (d) Kimsingi, *Historia* inatazamwa kutokea ndani. Ingawa ni kazi ya kitaalamu, pia kwa kadri kubwa, inaakisi kwa uaminifu jinsi waandishi wa Kiafrika

Wakati wa Mkutano Mkuu wa Sita wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi historia Kuu ya Afrika (uliofanyika Brazaville Agosti 1983), uchunguzi wa wajumbe wapya ulifanyika na nafasi ya Profesa Ogot ilichukuliwa na Profesa Albert Adu Boahen.

wanavyotazama ustaarabu wao wenyewe. Pamoja na kuandaliwa kwa mtazamo wa kimataifa, na ikichota maarifa yote ya kisayansi yaliyopo wakati huu, yapaswa pia iwe kipengele muhimu kabisa katika utambuzi wa urithi wa Kiafrika na yapaswa kudhihirisha vipengele vinavojenga umoja barani. Juhudi hii ya kutazama mambo kutokea ndani ni sifa mpya ya mradi huu na pamoja na thamani yake ya kisayansi, inapaswa kuipatia mradi umuhimu wa kujadiliwa vipana. Kwa kuonyesha sura halisi ya Afrika, *Historia* inaweza, katika enzi iliyozama kwenye mapambano ya kiuchumi na kiufundi, kutoa dhana mahsusi ya amali za mwanadamu.

Kamati imeamua kuwasilisha kazi ya miaka milioni tatu ya historia ya Afrika katika majuzuu manane, kila moja likiwa na karibu kurasa mia nane za matini na mifano, picha, ramani na michoro.

Mhariri Mkuu akisaidiwa, pale inapolazimu, na wahariri wasaidizi wawili, ana jukumu la kuandaa kila juzuu. Wahariri wanachaguliwa na Kamati ama kutokana na wajumbe wake au kutoka nje kwa wingi wa theluthi mbili. Hawa wana jukumu la kuandaa majuzuu kulingana na maamuzi na mipango iliyokubaliwa na Kamati. Kuhusu mambo ya kisayansi wanaiwajibikia Kamati, au kati ya mikutano miwili ya Kamati watawajibikia Idara kuhusiana na maudhui ya majuzuu, miswada ya mwisho ya matini, mifano na kwa jumla, vipengele vya kisayansi na kiufundi vya *Historia*. Idara mwishowe huhabitisha muswada wa mwisho. Inapooni kwamba muswada uko tayari kuchapishwa inaukabidhi kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Hivyo, katika kipindi kati ya Vikao Viwili, Kamati au Idara huendelea kusimamia mradi.

Kila juzuu lina kama sura thelathini. Kila sura ni kazi ya mwandishi mkuu, akisaidiwa, inapolazimu, na mshiriki mmoja au wawili. Waandishi wanachaguliwa na Kamati kutokana na sifa na uzoefu wa kitaaluma. Waandishi wa Kiafrika hupewa upendeleo alimradi wawe na sifa zinazohitajika. Juhudi maalumu pia hufanywa kuhakikisha kwamba kila inapowezekana kanda zote za bara na vile vile kanda nyingine zenye historia au utamaduni unaohusiana na Afrika zinapata uwakilishi sawa miongoni mwa waandishi.

Pale mhariri wa juzuu anapothibitisha matini za sura, zinapelekwa kwa wajumbe wote wa Kamati kwa uhakiki. Zaidi ya hayo, matini ya mhariri wa juzuu inawasilishwa kwa uchunguzi, kwa Kamati ya Wasomaji, iliyoundwa ndani ya Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kulingana na uwezo wa wajumbe wake katika uwanja wa kitaaluma. Kamati ya Wasomaji inachanganua sura kimaudhui na kimuundo. Kisha Idara hutoa uthibitisho wa mwisho kwa miswada.

Utaratibu kama huu unaonekana mrefu na mguumu, unaonekana kuwa wa lazima kwani unatoa uthibitisho bora kabisa wa uhakika wa kisayansi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kwa hakika, kumewahi kuwepo inatukio ambapo Idara inekataa miswada au kusisitiza ifanyiwe marekebisho makubwa au hata mwandishi mwingine kuombwa asawidi sura. Hutokea pia wataalamu wenye ujuzi wa kipindi fulani cha historia au wa swali fulani mahsusi kuombwa ushauri ili kukamilisha juzuu fulani.

Kazi hii itachapishwa kwa mara ya kwanza katika matoleo ya jalada gumu kwa lugha

za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu na baadaye katika matoleo ya jalada laini kwa lugha hizo. Matoleo yaliyofupishwa kwa lugha za Kiingereza na Kifaransa ndiyo yatatafsiriwa kwa lugha za Kiafrika. Kamati imechagua lugha za Kiswahili na Kihausa kama lugha za kwanza za Kiafrika za kufanyia tafsiri za kazi hii.


Aidha, kila juhudi itafanywa kuhakikisha *Historia Kuu ya Afrika* inachapishwa katika lugha nyingine kubwa kimataifa kama vile Kichina, Kireno, Kirusi, Kijerumani, Kiitaliano, Kihispania, Kijapani, n.k.

Hivyo, ni dhahiri kwamba hii ni kazi nzito inayotoa changamoto kubwa kwa wanahistoria wa Kiafrika na kwa wasomi kwa jumla, na vilevile kwa UNESCO ambayo kazi hii inafanywa chini yake. Hii ni kwa kuwa ni jukumu kubwa mno kuandika historia ya bara la Afrika ya miaka milioni tatu iliyopita kwa kutumia kanuni makini kabisa za kitaaluma na kulazimika kuwahusisha wataalamu kutoka nchi, tamaduni, itikadi na mahusiano ya kihistoria tofauti. Mradi huu unabeba peo kubwa za mambo ya bara, ya kimataifa na ya taaluma mbalimbali.

Kwa kuhitinisha, ningependa kusisitiza unuhimu wa kazi hii kwa Afrika na dunia. Katika kipindi ambamo watu wa bara la Afrika wanajitahidi kuunda umoja na ushirikiano mkubwa ili kutoa niwelekeo kwa mwenendo wa maisha yao, uelewa muafaka wa kale ya Afrika na utambuzi wa uhusiano miongoni mwa Waafrika na baina ya Afrika na mabara mengine, usingekuwa tu mchango mkubwa kwa maelewano miongoni mwa watu duniani bali pia chanzo cha maarifa ya urithi wa kitamaduni ambacho ni cha wataalamu wote.

---

*Maelezo kuhusu Wendo*



---

Imekubaliwa kufuata utaratibu ufuatao wa kuandika tarehe. Ama kuhusu kipindi kabla ya historia, tarehe zinaweza kuandikwa kwa njia mbili.

Njia ya kwanza ni kwa kurejea enzi ya sasa yaani tarehe KS (Kabla ya Sasa), mwaka unaorejewa ukiwa ni + 1950; tarehe zote zinakuwa hasi kuhusiana na + 1950.


Njia nyingine ni kwa kurejea mwanzo wa enzi ya Ukristo. Kuhusiana na enzi hii, tarehe huwakilishwa kwa kutumia alama + au - kabla ya tarehe. Zinaporejewa karne, vifungu KK na WK nafasi yake huchukuliwa na 'kabla ya enzi ya Ukristo' na '-a enzi ya Ukristo'.

Baadhi ya mifano ni kama hii Ifuatayo:

- (i) 230 KS = - 350
- (ii) 2900 KK = - 2900  
1800 WK = + 1800
- (iii) Karne ya tano KK = Karne ya tano kabla ya enzi ya Ukristo  
Karne ya tatu WK = Karne ya tatu ya enzi ya Ukristo.



---



*Wanakamati wa Kamati ya  
Kimataifa ya Kisayansi ya  
Kusawidi Historia Kuu ya Afrika*

---

*Tarehe zilizotajwa zinawakilisha tarehe za wanachama.*

Profesa J.F. Ade Ajayi  
(Nigeria), tangu 1971  
Mhariri Juzuu VI

Prof. F.A. Albuquerque Mourão  
(Brazil), tangu 1975

Profesa D. Birmingham  
(Uingereza), tangu 1985

Profesa A. Adu Boahen  
(Ghana), tangu 1971  
Mhariri Juzuu VII

Hayati H.E. Boubou Hama  
(Niger), 1971-8 (alijiuzulu 1978);  
alifariki 1982

Dakta (Bibi) Mutumba M. Bull  
(Zambia), tangu 1971

Hayati Profesa D. Chanaiwa  
(Zimbabwe), tangu 1975;  
alifariki 1993

Profesa P.D. Curtin  
(Marekani), tangu 1975

Profesa J. Devisse  
(Ufaransa), tangu 1971

Profesa M. Difujita  
(Angola), tangu 1978

Profesa H. Djait  
(Tunisia), tangu 1975

Hayati H.E.M. El Fasi  
(Morocco), tangu 1971; alifariki 1991  
Mhariri Juzuu III

Profesa J.D. Fage  
(Uingereza), 1971- 81 (alijiuzulu)

Hayati Profesa J.L. Franco  
(Cuba), tangu 1971; alifariki 1989

Hayati Bw. M.H.I. Galaal  
(Somalia), 1971 - 81; alifariki 1981

Profesa Dakta V.L. Grottanelli  
(Italia), tangu 1971

Hayati Profesa E. Haberland  
(Ujerumani Magharibi), tangu 1971; alifariki 1992

Dakta Aklilu Habte  
(Ethiopia), tangu 1971

Hayati H.E.A. Hampaté Bâ  
(Mali), 1971 - 8; (alijiuzulu); alifariki 1991

Dakta I.S. El-Hareiri  
(Libya), tangu 1978

Hayati Dakta I. Hrbek  
(Czechoslovakia), tangu 1971; alifariki 1993  
Mhariri Msaidizi Juzuu III

Hayati Profesa Cheikh Anta Diop  
(Senegal), 1971- 86; alifariki 1986

Hayati Abbé Alexis Kagame  
(Rwanda), 1971 - 81; alifariki

Profesa I.N. Kimambo  
(Tanzania), tangu 1971

Profesa J. Ki-Zerbo  
(Burkina Faso), tangu 1971  
Mhariri Juzuu I na IV

Bw. D. Laya  
(Niger), tangu 1979

Dakta A. Letnev  
(Urusi), tangu 1971

Dakta G. Mokhtar  
(Misri), tangu 1971  
Mhariri Juzuu II

Profesa P. Mutibwa  
(Uganda), tangu 1975

Profesa L.D. Ngcongco  
(Botswana), tangu 1971

Profesa D.T. Niane  
(Senegal), tangu 1971  
Mhariri Juzuu IV

Profesa T. Obenga  
(Jamhuri ya Watu wa Kongo),  
tangu 1975

Profesa Bethwell A. Ogot  
(Kenya), tangu 1971  
Mhariri Juzuu V

Profesa C. Ravoajanahary  
(Madagascar), tangu 1971

Dakta (Bibi) A. Jones  
(Liberia); tangu 1971

Hayati Profesa W. Rodney  
(Guyana), 1979 - 80; alifariki 1980

Hayati Profesa M. Shibeika  
(Sudan), 1971 - 80; alifariki 1980

Profesa Y.A. Talib  
(Singapore), tangu 1975

Hayati Profesa A. Teixeira da Mota  
(Ureno), 1978 - 82; alifariki 1982

Mgr T. Tshibangu  
(Zaire), tangu 1971

Profesa J. Vansina  
(Ubelgiji), tangu 1971

Hayati Mheshimiwa Dakta E. Williams  
(Trinidad na Tobago), 1976-8;  
alijiuzulu 1978; alifariki 1980

Profesa A.A. Mazrui  
(Kenya)  
Mhariri Juzuu VIII.  
Siyo Mwanakamati

Profesa C. Wondji (Côte d'Ivoire)  
Mhariri Msaidizi Juzuu VIII  
Siyo Mwanakamati

*Ukatibu wa Kamati ya  
Kimataifa ya Kisayansi*  
Schemu ya Ushiriakiano wa Kimataifa wa Utamaduni,  
Hifadhi na Ukuzaji wa Utambuzi wa Tamaduni  
UNESCO  
1, rue Miollis, 75015 Paris

*Wasifu*  
*wa waandishi waliochangia*  
*makala katika nakala kuu*

*Toleo lililofupishwa lilitayarishwa kutokana na matini za  
toleo kuu lililoandikwa na waandishi wafuatao:*

- UTANGULIZI D.T. Niane (Guinea); Mtaalamu wa Mandingo; amechapisha kazi nyingi kuhusu Afrika Maghaibi wakati wa himaya kuu, kuanzia karne ya kumi na moja hadi ya kumi na sita; alikuwa Mkurugenzi wa Mfuko wa L.S. Senghor, Dakar, mchunguzi.
- SURA 2 O. Saidi (Tunisia); mtaalamu wa historia ya Waalmohad; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya zamani ya Maghrib, na hususan Tunisia, anafundisha historia kwenye Kitivo cha Sanaa na *Ecole Normale Superieure* ya Chuo Kikuu cha Tunus.
- SURA 3 M. Talbi (Tunisia); mtaalamu wa Uislamu; amechapisha kazi nyingi na makala kwenye maeneo mbalimbali ya dini ya Kiislamu na Utamaduni, anafundisha kwenye Kitivo cha Sanaa, Tunis.
- SURA 4 I. Hrbek (Jamhuri ya Czech); mtaalamu wa kumbukumbu za Kiarabu za historia ya Afrika, hususan Afrika Magharibi; pia ni mtaalamu wa Uislamu; amechapisha kazi nyingi na makala katika nyanja hizi; ni mchunguzi katika Taasisi ya Taaluma za Mashariki, Prague.
- SURA 5 R. Idris (Ufaransa); mtaalamu wa lugha na fasihi ya Kiarabu; alifundisha historia ya Magharibi ya Uislamu; amefariki.
- SURA 6 D.T. Niane
- SURA 7 M. Ly-Tall (Mali); mtaalamu wa historia ya Mali; amechapisha kazi zinazohusu himaya za Mali, anafundisha kwenye *Ecole Normale Superieure*, Bamako; Mchunguzi.
- SURA 8 S.M. Cissoko (Senegal); mtaalamu wa historia ya Timbuktu ya Kale; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Afrika Magharibi; inhadhiri msaidizi kwenye Kitivo cha Sanaa, Dakar.
- SURA 9 M. Izard (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya bonde la Volta na hasa lile la falme za Mossi; amechapisha kazi nyingi kuhusu kipindi kabla ya ukoloni; historia ya ukoloni na historia ya kisasa ya eneo hili; Mchunguzi Mwandamizi katika Kituo cha Taifa cha Utafiti wa Kisayansi, Paris.
- SURA 10 D. Lange (Ujerumani); mtaalamu wa historia ya Sudan ya kati kabla ya ukoloni; amechapisha kazi nyingi kuhusu kipindi hiki; anafundisha kwenye Chuo Kikuu cha Niamey.
- SURA 11 M. Adamu (Nigeria); mtaalamu wa historia ya Wahausa; amechapisha kazi zinazohusiana na somo hili; Mkurugenzi wa Kituo cha Taaluma za Utamaduni wa Nigeria cha Chuo Kikuu cha Ahmadu Bello, Zaria.
- SURA 12 A. Salifou (Niger); mtaalamu wa historia ya Wahausa; amechapisha kazi nyingi kuhusu Niger na Nigeria; anafundisha Niger.
- Y. Person (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya Afrika, hususan Mandingo; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Afrika; Profesa kwenye Chuo Kikuu cha Paris I, Pantheon - Sorbonne; amefariki.

- SURA 13 P. Kipre (Côte d'Ivoire); mtaalamu wa historia ya kisasa na ya sasa ya Côte d'Ivoire; amechapisha makala mengi kwenye masimulizi; anafundisha *Ecole Normale Supérieure*, Abidjan.
- SURA 14 A.F.C. Ryder (Uingereza); mtaalamu wa historia ya Afrika Magharibi; amechapisha kazi nyingi kuhusu kipindi kabla ya ukoloni na wakati wa ukoloni wa eneo hili; Profesa kwenye Chuo Kikuu cha Bristol.
- SURA 15 J.C. Garein (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya Misri ya Kiislamu; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Misri chini ya Mamluki na Misri ya Juu ya Waislamu; anafundisha Chuo Kikuu cha Provence, Aix-en-Provence.
- SURA 16 L. Kropáček (Jamhuri ya Czech); mtaalamu wa historia ya jamii, siasa na dini ya Sudan, amechapisha kazi nyingi kuhusu Darfur, anafundisha katika Idara ya Taaluma za Asia na Afrika ya Chuo Kikuu cha Charles, Prague.
- SURA 17 T. Tamrat (Ethiopia); mtaalamu wa historia ya kale ya Ethiopia; amechapisha kazi nyingi juu ya kipindi hiki; anafundisha kwenye Chuo Kikuu cha Addis Ababa.
- SURA 18 V. Matveiev (Muungano wa Urusi); mwanahistoria na ethnolojia; amechapisha kazi nyingi juu ya kumbukumbu za Kiarabu za historia ya Afrika; Mchunguzi Mwandamizi kwenye Taasisi ya Ethnolojia, Akademia ya Sayansi ya Urusi, St. Petersburg.
- SURA 19 C. Ehret (Marekani); mwanaisimu na historia ya Afrika Mashariki; amechapisha kazi nyingi na makala kuhusu historia ya kabla na wakati wa ukoloni wa Afrika Mashariki; anafundisha kwenye Chuo Kikuu cha California, Los Angeles.
- SURA 20 B.A. Ogot (Kenya); mtaalamu wa Afrika na hususan historia ya Afrika Mashariki; amechapisha kazi nyingi na makala juu ya historia na akiolojia ya Afrika Mashariki; mwalimu, mchunguzi; alikuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Kimataifa ya Kumbukumbu ya Louis Leakey kuhusu Historia ya Awali ya Afrika; Mkurugenzi, Taasisi ya Utafiti na Taaluma za Uzamili, Chuo Kikuu Kishiriki cha Maseno, Kenya.
- SURA 21 B.M. Fagan (Uingereza); mwanaanthropolojia, mwanaakiolojia; amechapisha kazi nyingi kuhusu tamaduni za Enzi ya Chuma na Enzi ya Mawe Afrika Mashariki na Kusini; Profesa wa Anthropolojia katika Chuo Kikuu cha California, Santa Barbara.
- SURA 22 J. Vansina (Ubelgiji); mtaalamu wa simulizi; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Ikweta ya Afrika na Afrika ya Kati; anafundisha Chuo Kikuu cha Wisconsin, Marekani.
- SURA 23 L. Ngongco (Botswana); mtaalamu wa historia ya Kusini inwa Afrika kabla ya ukoloni; amechapisha kazi nyingi kuhusu Botswana kabla ya ukoloni; alifundisha Chuo Kikuu cha Botswana; Mkurugenzi wa Taasisi ya Taifa ya Uchunguzi Gaborone.  
J. Vansina.
- SURA 24 F. Esoavelomandroso (Madagascar); mtaalamu wa historia ya Madagascar; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Madagascar kuanzia karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane; anafundisha kwenye Kitivo cha Sanaa, Antananarivo.
- SURA 25 D.T. Niane
- SURA 26 J. Devisse (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya Kaskazini Magharibi ya Afrika kuanzia karne ya nne hadi ya kumi na sita; mwanaakiolojia; amechapisha makala mengi na kazi juu ya historia ya Afrika. Profesa wa Historia ya Afrika, Chuo Kikuu cha Paris 1, Panthéon - Sorbonne.
- S. Labib (Misri); mtaalamu wa historia ya kale ya Afrika; amechapisha makala mengi kuhusu historia ya jamii na uchumi ya kipindi hiki; anafundisha Chuo Kikuu cha Utah (Marekani) na Chuo Kikuu cha Kiel (Ujerumani).
- SURA 27 D.T Niane

## Utangulizi wa jumla

Afrika ina historia yake. Kwa bahati mbaya sana kwa muda mrefu ni kiasi kidogo tu cha historia hiyo kimefahamika; na hata hicho kidogo hakikufahamika vilivyo. Baada ya majilio na marcejo ya wasafiri wengi, wafanyabiashara ya utunwa, wafanyabiashara ya kawaida, askari, watawala na wanazuoni wa kila aina, kwa kipindi cha maelfu ya miaka, picha ya Afrika katika mawazo ya watu wengi iliharibiwa na maelezo potofu yaliyokuwa yakielezea umaskini, ushenzi, kutokuwajibika na ghasia katika bara hili.

Walakini basi, historia ya Afrika, kama ilivyo historia ya mwanadamu, ni hadithi ya mzinduko. Hadithi hii inahitaji kuandikwa upya kwani imcharibiwa nuno kutokana na kutokujua na ubinafsi wa watu walioandika.

### *Kwa nini?*

Lengo letu hapa siyo kuandika historia ya kulipiza kisasi bali kufanya kazi ya kisayansi, katika jitihada za kuleta mwanga kwenye kiza ambamo bara la Afrika - pamoja na shajara zake zisizokamilika, miundo yake mbalimbali isiyocleweka vizuri, tarehe zake ambazo ama hazikuonyeshwa au siyo za kutegemewa - limegubikwa. Katika kutokujua kwao historia ya Afrika watu hufanya hitinisho la haraka na kijinga kwamba Afrika haina historia. Lakini kila mwaka, mlolongo wa vitabu na makala mbalimbali juu ya Afrika na uvumbuzi wa hati na vitu mbalimbali vya kiakiolojia, vingine vikiwa vya kustaajibisha kabisa, vinafanya watu waanze kusaili maana ya batua fulani fulani katika historia ya mwanadamu kwa jumla.

Kwa hiyo ni muhimu kufanya uchunguzi mwafaka wa habari usiokuwa na upendeleo au ila ya aina yoyote. Uchunguzi huo ulifanywa na makundi mbalimbali ya wanazuoni, Waafrika na wasio-Waafrika, chini ya ufadhili wa UNESCO, na waliongozwa na Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa pamoja na wahariri wa Kiafrika. Hili ni jaribio kubwa katika ushirikiano wa kimataifa ambao sasa unafanya iwezekane kuwarejeshea watu wa Afrika historia yao si kwa kujifurahisha tu bali kwa miujili ya kuwafanya waiclewe hali ya sasa, na waweze kuondokana na kujihisi wanyonge ili wasonge mbele na kujenga hali njema ya baadaye.

### *Kwa vipi?*

Sharti pawe na kila hadhari ili kuhakikisha kwamba ukweli wa kihistoria unatambuliwa tena. Mbinu mujarabu itakayotumiwa katika zoezi la nanua hiyo si lazima ifofautiane kimsingi na ile iliyotumika kwingineko. Kanuni zilezile hutumika ulimwenguni kote ili kuwawezesha

wachunguzi wapate matokeo thabiti. Lakini kwa kuwa hakika ya mambo hutofautiana ni dhahiri kwamba kuyaclewa mambo hayo pia kutatofautiana. Kwa mfano uamuzi uliochukuliwa na Mfalme Napoleon<sup>1</sup> au amri iliyotolewa na Churchill<sup>2</sup> haviwezi kutafsirika kwa namna sawa na utenzi wa kumsifu Sundjata.

Ama kwa hakika matatizo mahsusi juu ya historia ya Afrika budhahirika zaidi tunapozingatia jografia ya maumbile ya bara hili. Kama ramani mpya ya "Peters" inavyoonyesha,<sup>3</sup> Afrika si bara lililotengwa katika anga la sayari yetu; lakini bara hili laonekana kuwa limejitenga lonyewe. Ingawa limeunganishwa na Mashariki ya Kati na shingo ya nchi ya Suez lakini limezungukwa na pwani za bahari ambamo mito huingia kwa kupitia maporomoko ya maji ambayo huabirika kwa shida sana. Eneo kubwa pekee la kupitia kati ya Sahara na milima ya Ethiopia nalo limefungwa na mabwawa makubwa ya matope ya Bah-el-Ghazal.

Theluthi moja ya eneo la bara hili imechukuliwa na majangwa mawili: Jangwa la Sahara, jangwa la majangwa; na Jangwa la Kalahari. Tukijumlisha "jangwa la kijani" la msitu wa ikweta ambalo linachukua sehemu isiyopitika katikati ya bara hili, tutakuwa tumekwishacleza nusu ya umuhimu wa mapengo ya asili ambayo yanajenga ujia mwembamba unaoanzia kaskazini kuelekea kusini kama vile Kihori kikuu cha Bonde la Ufa, au kutoka Mashariki kwenda Magharibi kama vile bonde la Mto Niger. Halikadhalika tunaclewa kwa nini falme za kwanza za Afrika ya wesi zilikuwa tu katika mipaka ya maeneo ambayo yalikuwa yamejifunga na hususa katika maeneo ambayo hayakuwa na vizuizi vya usafiri kama vile Sahel.

Zaidi ya hayo, ukweli kwamba idadi ya watu katika Afrika ilikuwa kidogo ni mojawapo, ya ufumbuzi wa matatizo yake ya kihistoria kwani, kama anavyosema F. Braudel, "Ustaarabu huzaliwa na idadi ya watu." Vita na magonjwa mbalimbali, ya kuambukiza na yasiyoambukiza, haviwezi kuchukuliwa kwamba ndivyo vilivyosababisha matatizo hayo kwani mabara mengine pia yamewahi kuathiriwa navyo. Hata hivyo kupungua sana kwa watu kutokana na biashara ya utumwa pamoja na ukoloni bila shaka kulizuia bara hili kufikia kiwango cha mkusanyiko ambacho huleta mabadiliko muhimu ya kiuchumi na ya kijamii na kisiasa. Mazingira magumu ya tabia ya hali ya nchi pia yalichangia katika matatizo haya. Haya yote ni mambo halisi yasiyohusiana na imani zisizo na msingi za Waafrika kujihisi dhalili kutokana na rangi yao, migananyo ya kizamani ya kinbari au wao kujiona kuwa wanyonge wa kuzaliwa.

### *Tatizo la Vyanzo*

Kuna vyanzo vitatu muhimu vya uchunguzi wa kihistoria katika Afrika: hati za kimaandishi, akiolojia na mapokeo sinulizi. Hivi vinakamilishwa na isimu na anthropolojia. Lakini hakuna hata kimoja kati ya vyanzo hivi ambacho chaweza kuscmwa kuwa na unuhimu zaidi kuliko vingine.

### *Vyanzo vya Kimaandishi*

Ingawa baadhi ya vyanzo vya kimaandishi vipo lakini havikujigawa katika uwiano mzuri wa muda na wakati. Karne ambazo angalau tunapata mwanga juu yake kutokana na vyanzo vya

<sup>1</sup> Napoleon: mfalme wa Kifaransa wa mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa

<sup>2</sup> Churchill: mtawala wa Kiingereza aliyechukua dhima ya kukata shauri wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia

<sup>3</sup> Arno Peters: Mwanahistoria wa kisasa wa Kijerumani aliyekamilisha ramani kulingana na eneo halisi la ardhi.

kimaandishi isipokuwa kuhusiana na Afrika Kaskazini, ni zile ambazo zatangulia au zafuatia kuzaliwa kwa Ukristo.

UNESCO imeanzisha Kituo cha Ahmed Baba, huko Timbuktu, ili kukusanya hati zinazolusika. Idadi kubwa ya hati hizi bado zinaweza kupatikana katika maktaba mbalimbali za Afrika Kaskazini, Ulaya, Mashariki ya Kati na Armenia, na hata majumbani mwa raia na wanazuoni maarufu wa Kiafrika katika Sahel. Uvumbuzi wa hivi karibuni wa miswada uliofanyika Moroko na katika Istanbul (Uturuki) ni ushuhuda wa jambo hili; ushuhuda mwingine ni zile hati zilizogunduliwa na vyuo vikuu vya Afrika Magharibi au katika Vituo vya Mitalaa ya Kiafrika. Miongozo mipya kuhusu vyanzo vya maandisli, kama ile iliyochapishwa na *International Council of Archives*, itakuwa na manufaa inakubwa kwa wachunguzi, ambao pia watahitaji kazi za kitaalamu zitakazochapishwa upya na tafsiri za kazi muhimu ambazo kwa hakika kwa sasa hivi kupatikana kwake ni shida. Mwisho, miswada katika hati za kusini mwa Sahara kama vile Vai, Bamum na Ajami pia haina budi kuzingatiwa<sup>4</sup>.

### Akiolojia

Tunaweza kusema kuwa Akiolojia hutoa hati ambazo haiziwezi kujieleza zenyewe. Hata hivyo kuna kitu yakiniifu na halisi kuhusu lugha katika vitu vilivyochinbuliwa kutoka ardhini. Kila kitu hutegemea jinsi ya kuzifasiri habari zipatikanazo kutokana na ushuhuda sukutu na vidokezo juu ya ustaarabu, iwe ni vyakula, zana au vifaa, au vifaa vilivyotengenezwa kutokana na chuma, kioo au ufuyanzi. Kwa kulinganisha vitu hivyo tu iliwezekana kuonyesha uhusiano wa kale uliopo baina ya watu walioishi katika Bonde la Chad kabla ya historia -Wasao-na jamii zilizoishi katika bonde la Mto Nili na jangwa la Libya. Kutokana na gharama kubwa za utafiti wa kiakiolojia ni vema kwanza mipango ya kimataifa Kiafrika ibainishe na kuainisha maeneo muhimu ya utafiti kabla mipango ya machimbo hajafanywa.

### Mapokeo simulizi

Mapokeo simulizi ni inakumbusho hai ya mkusanyiko wa inatokeo ya utamaduni wa jamii yaliyohifadhiwa na watu ambao yasecekana hawakuwa na kumbukumbu za kimaandishi., Wazee ambao ndio wenye kuhifadhi matokeo hayo ya utamaduni wa jamii ndio waliobaki katika mandhari ya kale ambayo wanahistoria wanajaribu kuyarejesha. Chambilecho methali ya Kiafrika: "Kinywa cha inzee hunuka, lakini ndani mwake nina mambo mazuri na marudi mema". Mapokeo simulizi huvisha nguo, huremba na kuitia nyama mifupa ya wakati uliopita. Kama kawaida ni lazima pawe na hadhari kubwa kuhakikisha kwamba mambo yaliyomo katika mapokeo hayo yanachanganuliwa na kuchujwa kwa uangalifu.

Imewahi kudaiwa kwamba mapokeo simulizi si mambo ya kuaminiwa sana kwa sababu niamilifu, yaani yanafuata jinsi jamii inavyotaka -kana kwamba taarifa zote zinazowahusu binadamu siamilifu, pamoja na nyaraka kuukuu ambazo inara nyingine huficha ukweli wa mambo ndani yake. Ni kweli kwamba tenzi karibu ni uhuishaji wa ki-kisaasili wa wakati uliopita unaonua kurejesha asili za kihistoria za watu kwa kutumia nguvu ya masimulizi. Lakini hata kumbukumbu za kimaandishi nazo wakati mwingine hufanya hivyo.

Hapana shaka, kuna haja ya kuongeza kwamba udhaifu mkubwa wa masimulizi ya tenzi uko katika marejeo yake ya kikronolojia. Kwa mafano matunizi ya wastani wa urefu wa

<sup>4</sup> Vai ni lugha ya Liberia; Babum ni lugha ya Kameruni; na Ajami ni lugha ya Kiafrika iliyoandikwa kwa hati za Kiaarabu.

kipindi cha utawala au vizazi mbalimbali kupiunia kiwango cha wakati uliopita kwa kukadiria tu kutokana na wakati wa leo yamepingwa sana kwa sababu huenda yametokea mabadiliko ya hali ya maisha katika jamii pamoja na mabadiliko mengine. Wakati mwingine unaweza kukuta mfalme fulani maalumu amepwa sifa zote za wafalme wengine waliotawala katika nasaba yake kama vile Da Monzon, Mfalme wa Segou aliyetawala katika miaka ya mwanzo ya karne ya 19 na ambaye anapewa sifa zote za ushindi muhimu wa ufalme luo na mayeli na malenga.

Tena basi maelezo ya masimulizi hupoteza umuhimu wake iwapo yatakuwa yamefungwa katika mazingira ya hadhira iliyoyapa uhai. Lakini yakiachwa huria katika jamii inayoyakuza hukua mthili ya lugha hai, hujinasibisha katika hadhira mpya na hukubali kuchukua michango mipya. Ilivyo siku liizi mafungu ya matini ya maandishi ambayo baadhi ya "manluki" wa mapokeo simulizi hujifunza kwa ghibu yanaingizwa tena katika masimulizi ya zamani.

Hata maudhui ya ujumbe mara nyingi hayawi dhahiri. Kwa Waafrika usemaji ni jambo lenye uzito. Kwa kadri mtu anayesema alivyo maarufu ndivyo pia ujumbe anaotoa unavyozidi kuwa muhimu na ndivyo unavyozidi kupambwa na methali na mafumbo mbalimbali. Hali hii ya ujumbe kutokuwa dhahiri kufanya iwe vigumu zaidi kuyatafsiri maudhui ya mapokeo simulizi ya Kiafrika katika lugha ya nchi ya kitasnia. Mapokeo ni magumu kutafsirika na baadhi ya makosa ambayo yamesemwa kuwa ni ya mapokeo yametokana na wafasiri wenyewe.

Hata hivyo, namna ya maelezo ya mapokeo simulizi, iwe ni ya tenzi au ya nahari, iwe ni ya kinafunzo au ya kimaadili, unaweza kuwa na umuhimu wa kihistoria katika namna tatu. Kwanza huakisi mila na desturi za jamii. Kwa mfano Da Monzon anapoitwa "bwana wa inji na bwana wa wanaume" inaashiria kwamba alikuwa na mamlaka ya juu kabisa. Wimbo wa kumbukumbu ya Sundjata unaposema "*Saya Kausa malo yé*" (Ni bora kufa kuliko kufedhheka) unaonyesha wazi kwamba katika karne ya 13 heshima ilikuwa ni mojawapo ya mambo yaliyoathaminiwa sana katika jamii ya Malinke. Silamaka anaposema: "Bahati yako, siruhusiwi kuu wajumbe", tunapata ushuhuda wa mojawapo ya sharia za kimatifa katika Afrika ya kabla ya ukoloni.

Pili, mapokeo simulizi hutupatia maelezo nasibu ya mambo yakini na vitu ambavyo hutujengea hali ya mazingira na hali ya kijamii ambavyo kwamo maisha yaliendeshwa. Kwa mfano katika utenzi wa Da Monzon, wa ufalme wa Ki-Bambara wa Segou, tunapewa maelezo ya makubadli ya ngozi, ngalawa ambazo kila moja iliweza kuchukuwa watu sitini, mbinu za kuteka miji ambapo mishale ya moto ilikuwa ikitupwa ili kuwasha moto na kuzitia maji baruti zilizokuwa zikitumiwa na askari wa adui. Ndiyo maana idadi ya tafsiri mbalimbali za mapokeo simulizi, kinyume na fikra kwamba zinaweza kuwa kizuizi, zinampa faida mtu yeyote ambaye anauclewa vema muundo wa kifasihi unaotumika pamoja na ishara zake, taratibu zake zisizobadilika na mbinu za usemaji zinazotumika kuongezcaongezca labari ili kuufanya ufane zaidi; na pia ambaye anazielewa vema jamii zinazohusika, tabaka zao mbalimbali za kijamii na koo mbalimbali zenye kupingana na zinazotoa tafsiri mbalimbali. Inapokuwa maelezo yanakubaliana, kama ilivyo katika mayeli wa Kibambara na wa Kifula ambao wako katika vikundi viwili vinavyopingana ukweli wa maelezo hayo huwa madhubuti zaidi.

Tatu, katika sehemu nyingine kuna mapokeo yaliyoasisiwa rasmi na ambazo muundo wake umefundishwa katika shule kama ilivyo huko Keyla, Kita na Nyani nchini Mali. Mapokeo haya rasmi huandamana na muziki unaopigwa kwa kutumia ala ambazo ni



maalumu kwa cneo hilo kama vile *balla* au marimba katika nchi ya Mali, ngoma ya *bendre* ya Wamossi wa Burkina Fasso au kinubi cha *mvé* cha Wafangi. Kutokana na kuwepo kwa lugha zenye toni ala hizi huweza kuchukua nafasi ya maafisa wa kitala au washairi ambao huzifanya ala hizi zitoe ujumbe bila wao wenyewe kutanika neno lolote. Hali hiyo hiyo pia hujitokeza katika sanaa ya plastiki ambayo ni maelezo ya moja kwa moja ya watu wenyewe, matukio au ruwaza za kijamii, kama ilivyo katika sanaa za nakshi za Abomey na Benin na uchongaji vinyago wa Kuba.

Kwa hiyo mapokeo sinulizi ni chanzo maalum kinachofanya historia ya bara hili iwe na uasili.

### Isimu

Isimu ni uwanja ambao umepata kiwango cha juu cha usahihi ambao unauwezesha kutumiwa katika kuupima na kuuchunguza wakati uliopita. Hata hivyo kabla lugha hazijalinganishwa ili kuwekwa katika makundi ya aina na vikoa vya asili moja - ambapo lugha moja huweza kusemwa kuwa ilizungumzwa kabla ya lugha nyingine kuwepo, na kwa hiyo watu wenye lugha hiyo waliwatangulia wale wa lugha nyingine - shurti kwanza zitambuliwe na zielezwe kisayansi. Hili ni jambo amalo mara nyingine linazusha ubishi baina ya wataalamu. Kwa mfano baadhi ya watu hudai kwamba asili ya Kibantu ni bonde la Kongo, ambako ndiko ilikoinukia, na baadhi hudai kwamba asili ya lugha hii ni lugha za Kisudani. Hata hivyo mwanaisimu anapoonyesha kuwa maneno yenye maana ya kondoo yanafanana yanapotumiwa kaskazini mwa msitu wa Ikweta na katika msitu wenyewe fasiri tunayoweza kutoa ni kwamba yamkini kufikuwa na kondoo katika cneo lililokuwa sambamba na ukingo wa msitu hadi hapo msitu ulipoinalizikia. Ama kwa hakika hii inathibitishwa na hali ilivyo katika Afrika Mashariki ambako kundi la maneno yanayohusiana yenye maana ya kondoo lina uelekeo wa Kusini-Kaskazini, ikiwa katika usawa wa pembe uraba katika uelekeo wa katikati ya bara lenyewe.

Greenberg anconyesha mchango wa Kikanuri kwa Kihausa kuhusiana na maneno yanayohusu utamaduni, teknolojia na vyoo vya kisiasa. Uchunguzi makini wa majina ya mahali (toponomia) na watu (anthroponomia) yanaweza kutoa data za kihistoria kwa mwelekeo wa Kiafrika.

Kwa mfano utafiti kuhusu msamiati wa Kiswahili, ambao unejaa maneno mengi ya asili ya Kiarabu au utafiti juu ya lugha za watu waishio katika pwani ya Bukini, ambao nao waliathiriwa na Waarabu unaweza kuwa wenye manufaa makubwa kwa wanahistoria. Lakini awali ya yote isimu lazima iondokane na nadharia za kibaguzi kama zile za akina A.W. Schlegel ambazo zinaziweka lugha za Kiafrika 'chini kabisa ya ngazi ya lugha za ulimwengu'.

### Anthropolojia na Ethnolojia

Kwa muda mrefu taaluma hizi mbili zilikuwa zinetumiwa katika huduma za kuendeleza ukoloni na utawala: kwa kuonyesha jamii za Kiafrika na nyinginezo kama jamii za kishenzi na zisizoendelea, na kwa kuzitenga jamii hizi iliwezekana kabisa kuzitawala kama jamii zilizowategemka wakoloni au, kwa maneno mengine, ilichangia kwenye 'kuendeleza hali ya kutoendelea'.

Nadharia ya Darwin juu ya maendeleo ya mabadiliko ya viumbe vyenye uhai na kutawanyika kwavyo ikiandamana na fikra kwamba vitu vyote vizuri katika Afrika vilitoka katika scheimu nyingine za ulimwengu, pamoja na nadharia ya uamili ambayo inaandamana

na mada! kwamba miundo mbalimbali ya ulimwengu wa Kiafrika ilifuata utaratibu usiobadilika na ambao haukuwa na mwendelezo wa kihistoria - zote zilikuwa nadharia ambazo ama kwa makusudi au vinginevyo ziliundezeza na kuupa nguvu ukoloni. Waliwatumia watu wa hali za chini kabisa katika uchunguzi wao na kuwachukulia kwamba ndio waliokuwa wakiwakilisha watu na maisha halisi ya dunia ya Mwafrika.

Hata hivyo, mwishoni ukoloni ulifaulu kuwazindua wazalendo ambao baada ya kujinyakulia uhuru wao walikuwa raia kamili. Kutokana na hali hiyo wazalendo hao sasa wamewania kutafiti habari juu ya jamii zao wenyewe na kukataa kutumiwa kama vyombo vya kustajabiwa na watu wa Magharibi walio na uchu wa kutafuta mambo ya kuajabia.

Kwa bahati nzuri wachunguzi kama vile Barth, Frobenius, Delafosse na Evans-Pritchard walikwishaonyesha njia ya kuzitunika sayansi za jamii katika mazingira ya Kiafrika; hii ikiwa imejengwa kwenye msingi kwamba Waafrika ni sawa na watu wengine isipokuwa tu wametokea kuwa katika mazingira tofauti.

Mbinu ya Ki-Marx, mradi tu haing'ang'aniwi bila sababu makini, na mbinu ya kuclunguza miundo ya vitu vinaweza kuwa na manufaa makubwa ingawaje njia hizo zitafautiana katika mikabala yake ya kuangalia uhalisi.

U-Marx, ambao unaangalia historia kama dhamira ya pamoja katika utendaji hutilia mkazo nguvu za kuzalisha mali na uhusiano wa kuzalisha mali. Kwa hakika ni mbinu ya kihistoria. Mbinu ya kuclunguza miundo imejengwa kwenye msingi kwamba uwezo wa kuelewa jambo umu katika miundo ya jambo hilo, ambayo ama kwa makusudi au vinginevyo ndiyo utendajikazi wa kimantiki unaosababisha matendo ya vikundi vya binadamu.

Ili anthropolojia iweze kuwa yenye manufaa shurti izingatie kanuni za kimatendo na kinadharia pia ikitupilia mbali fikra za upendeleo au chuki zinazoweza kuyapotosha maendeleo ya kisayansi. Na hapo ndipo tunapoweza kupata uwiano wa maana ambao utamulika wakati uliopita. Kwa mfano njia za kibiasara ambazo kwazo baadhi ya bidhaa zilikuwa zinahodhiwa na koo za kifalme zilipata tu kutokoa wakati mmoja\* na taratibu za kisiasa za kuniliki nchi nyingi katika Ghana ya Kale na Mali na zile za Dola ya Ashanti, Ufalme wa Lunda, n.k. Hali hii pia ilijitokeza katika utawala a Kingonde na Kizulu. Lakini watu wenyec uhusiano kama Wanyakyusa na Waxhosa, ambao walikuwa mbali na njia hizo hawakuanzisha miundo ya utawala wa kifalme. Yawezekana kuchukulia hali kama hii kuwa msingi wa kuunda namna fulani ya kanuni ya maendeleo ya kihistoria katika Afrika.

Aidha, inewahi kuonekana kwamba taratibu za ndoa katika makundi ya binaadamu mara nyingi ndizo zinazoamua ni lugha za makundi yapi zitakuwa na umuhimu zaidi kuliko nyingine kwani lugha za upande wa mama huweza kudumu tu iwapo wanawake watachukuliwa kama wake na wala sio kama watumwa au masuria. Hii imejitokeza wazi miongoni mwa Wangoni wa Kusini mwa Afrika na wafuata wa Ouassoulou.

Kwa kuhitunisha, basi, tunaweza kusema kuwa haiwezekani kuvianisha vyanzo vya historia ya Afrika, kama ilivyodokezwa hapo juu, kwa kufuata "utaratibu wa ubora." Kila kimoja kinawezeka kuwa na umuhimu mkubwa kutegemkana na hali ya mambo. Vyanzo hivi huwa thabiti tu vinapowekwa pamoja au vinapotofautishwa. Kwa mfano, mapokeo simulizi huweza hata kuvisalimhisha vyanzo vya kimaandishi: mmojawapo wa watu maarufu, Ibn Khaldun katika kitabu cha *History of the Berbers* alieleza yafutayo kuhusu Sundjata: "Ufalme wake ulirithiwa na mwanaye, Mansa Uli. Katika lugha yao "*Mansa*" ina maana ya sultani na *Uli* ni kisawe cha Ali." Lakini mapokeo simulizi huthibitisha tena ukweli kwa kuonyesha kwamba katika lugha ya Kimande neno *ule* lina maana ya "wekundu." Hivyo Mansa Ule au Uli lina maana ya "Mfalme mwenye ngozi ya rangi ya inaji ya kunde."

## Msingi ya Utafiti

Misingi minne imewekwa ili kuhakikisha kwamba utafiti wa historia katika Afrika unakuwa wa kiwango cha juu.

### Kuzingatia Taaluma Fungamano

Mkabala unaozingatia taaluma fungamano huvikuzia vyanzo mbalimbali kwa kuviunganisha na vingine. Kwa mfano, Ufalme wa Wabambara wa Segou unaweza kueleweka vema kwa kuichunguza sosiolojia ya kisiasa ambayo ndani mwake mmeconckana afama za mfumo wa himaya kubwa ya Mali. Vilevile mapokeo simulizi ya nchi za delta ya Niger yanaonyesha kwamba historia ya enco hilo haitokani tu na athari za biashara ya utumwa na mawese, tunaweza vile vile kubainisha mambo mengine ya asili ambayo hayakutiliwa maanani na mwandishi wa Kireno, Pacheco Pereira, lakini ambayo pia yamechangia katika maendeleo ya haraka ya enco hili.

Uchunguzi wa anthropolojia ya kitamaduni miongoni mwa Wafulani wa Ico unewawezesha Hampaté Bâ na Germaine Dieterlen kutoa mwanga juu ya michoro ya ajabu ya nakshi za Tassili.

Kuenca kwa Wabantu kumefuatiwa mwanzo wake kwa kutumia vyanzo vya upatanisho wa kisarufi katika isimu, inapokeo simulizi, anthropolojia na maelezo ya kimaandishi ya Kiarabu, Kireno, Kiingereza na Kiafrikaans; na hivi karibuni kwa kutumia akiolojia. Maelezo ya kiisimu vile vile hukubaliana na yale ya kiteknolojia katika kushauri jinsi patu za kifalme au kengele pacha za sherche zilivyoenca kuanzia Afrika Magharibi hadi Kongo ya Chini, Shaba na Zambia.

Umuhimu wa kuvitumia vyanzo vyote hivyo kwa pamoja hudhihirika zaidi tunapolazimika kutatua matatizo ya kikronolojia. Kwa bahati mbaya luwa si rahisi kukadiria umri kwa kutumia kaboni-14 wala kupata vipande vingi vya vyungu kama ilivyo kaskazini mwa Chad ambavyo vinaweza kutumiwa kuainisha ruwaza zinazofuatana (mwainisho wa kibistoria). Katika baadhi ya sehemu ramani za kupatwa kwa mwezi (jua) ambako kunajulikana kuwa kulipata kutoka katika maenco maalumu na kwa wakati maalumu huweza kuwianishwa na kipindi cha ufalme fulani maalumu; hasa kwa kuwa kwa namna fulani ni hatari kufanya mahitimisho ya kikronolojia kutokana na urefu wa wastani wa vipindi vya ufalme au vizazi mbalimbali kwa sababu tu mabadiliko makubwa hutokea kadri wakati unavyokwenda.

Hakuna sababu ya kuiamania kronolojia na kufanya kila juhudi kuikita katika misingi thabiti, hata kama ingekuwa na umuhimu wa kuwa uti wa mgogo wa historia. Tarehe ni njia tu ya kulifikia jambo na wala sio jambo lenyewe. Iwapo hatujui ni mwaka gani hasa Kumbi Saleh aliposhindwa tunaweza bado kusema "mwishoni mwa karne ya kumi na moja." Zaidi ya hapo basi, mwendelezo mzima ulioundwa upya na historia hauna budi kuingizwa tena katika muktadha wa wakati wa Kiafrika kadri iwezekanavyo. Hatuwezi kuukana ukweli kwamba wakati wa Kiafrika umekitwa katika misingi wa baadhi ya mambo kutangulia na kufuatiwa na mengine; unaosukumwa na nguvu ya chanzo cha matukio, lakini unaodhoofishwa kwa kuingiliwa na kisaasili.

Maendeleo yalifikia kiwango kilichoondoa haja ya kuwa na kalenda za tarakimu na za kidhahania. Kwa hiyo marejco kuhusu wakati yalifuata tu utaratibu wa mambo yalivyokuwa kufuatana na usili wake na yalihusu vitu kama jua, majira na miguro ya watu na wanyama wa porini; la sivyo ulihusu matokeo fulani yasiyokuwa ya kawaida, hasa maafa ya kinaumbile ambayo yaliacha athari za kudumu katika fikra za watu. Hata hivyo mtazano

huu wa wakati ulikuwa wa kihistoria kwani jamii za Kiafrika mara nyingi ni zenye mtazamo wa kuyaangalia mambo kiumri na wazo la kutangulia kwa kitu ni la muhimu kabisa katika kuangalia haki za jamii. Aidha kutokana na kukuzwa nguvu za mtu binafsi na kundi lote ukiwa ndio msingi wa falsafa ya maisha ya Mwafrika, isingeweze kana kutazama dhana ya wakati kuwa kitu tuli.

Katika hali nyinginezo pia mkabala wa kuangalia kronolojia ulikuwa dhahiri na wa kisayansi. Mbali na ufundi wa kushangaza ulioonekana katika Misri ya Mafarao na falme za Kiislamu kulikuwa na uchongaji uliokuwa unafanywa kwenye vipande maalumu vya mbao katika nchi ya Wadogon; au vibonge vya dhahabu vilivyokuwa vikiwekwa mwenye chombo katika nyumba-ya -vigoda ya wafalme wa Bono Mansu. Wakati mwingine tarehe iliyoundwa na mgeni aliyeshuhudia tukio inaweza kuwa marcejeleo muhimu ambayo yanatoa mwanga mkubwa juu ya utawala wa mtu mashuhuri.

Dhana za kimapokeo kuhusu wakati zilianza kuundwa upya baada ya kuingia maaandishi, kuenea kwa dini ambazo zilihusishwa zaidi na historia ya kikalenda, na kuingia kwa Afrika katika ulimwengu wa faida iliyopatikana kwa kutumia wakati kwa ufanisi zaidi.

Hitajio la pili muhimu ni kwamba Historia ya Afrika haina budi kutazamwa *katika mtazamo wa Kiafrika* badala ya kufasiriwa kwa kurejelea jamii nyingine au mawazo ya wengine na upendeleo wao. Hii haina maana ya kutaka kulipiza kisasi au kujivisha kilemba cha ukoka bali itahusu kuonyesha ukumbusho wa jamii. Mielekeo ya watu wengine inara nyingi hutufanya tuwe na wasiwasi na tena tujione katika hali ya unyonge. Wakati sasa unefika kwetu kuutazama kwa undani utambulisho wetu na mwamko wetu wa kujitambua.

Katika bara kama Afrika, ambako majina yanapewa umuhimu mkubwa kiasi kwamba baadhi ya watu wanaotukuzwa hawatajwi majina, ni muhimu kuona kwamba historia yetu inaelezwa kwa mfululizo wa maneno na dhana zilizotoka Ulaya au mabara mengine na ambazo hutafsiri - mara nyingi hubetua- ukweli wa manbo na miundo iliyoundwa katika muktadha mwingine wa kisimu na kijamii. I.A. Akinjogbin amelidhihirisha jambo hili kulusia na ebi au mfumo wa kiukoo katika ufalme wa Oyo. Hii ndiyo maana istilahi za Kiafrika zinazohusu miundo ya Kiafrika shurti ziachwe jinsi zilivyo, kwa kadri inavyoweze kana, pale ambapo hakuna visawe vyake mwafaka katika lugha nyingine.

Bila shaka hatuwezi kukana athari za kigeni, hasa pale ambapo zimeleta mabadiliko mazuri ambayo yaliharakisha maendeleo ya historia ya Afrika. Kwa mfano kuanza kutumiwa kwa bunduki katika Sudani ya kati katika karne ya kumi na sita kuliwaweka askari wapanda farasi wa kikabaila katika hali duni dhidi ya jeshi la askari wa miguu wenye bunduki lililoundwa na watumwa na watu wa chini. Matokeo yake yakawa kubadilika kwa miundo wa utawala katika Sudani ya kati; *kacella* au *kaigamma*, ambaye hapo awali aliandikishwa kutokana na watumwa akachukua nafasi ya waziri wa daraja la juu, Ciröma, katika mahusiano yake na mfalme. Hata hivyo ni muhimu kwanza kuchunguza utaratibu wa mfumo wa ndani kabla ya kutafuta athari za nje.

Msingi wa tatu kwa historia mpya ya Afrika ni kwamba shurti iwe *historia ya watu wa bara la Afrika kwa jumla*; na bara la Afrika linajumuisha visiwa, kama vile Bukini, na eneo la Afrika ya kaskazini, ambako nchi za kusini mwa Sahara zimekuwa na uhusiano nao wa karibu na wenye faida kwa muda mrefu. Haina budi kuwa historia ya watu kwani ingawa kulikuwa na falme na temi mbalimbali yawezekana kwamba umbali uliokuwepo, ukosefu wa mara kwa mara wa inagari na maandishi vilipunguza nguvu za utawala dhalimu katika vijiji vya ndani. Tena basi, hata wale wafalme na watemi waliokuwa na mamlaka ya mwisho kabisa nao walifungwa na mila, na ndiyo kusema basi walifungwa na namna fulani ya sharia

zilizowekwa na vyombo vya mamlaka vilivyokwisha kuwepo kama vile halmashauri mbalimbali, makasisi, watabiri, n.k. Pia ni lazima iwe historia ya watu kwani ingawa kuna historia ya ukoloni na mipaka iliyoletwa nao katika nchi ziundazo umoja wa nchi huru za Afrika (OAU) watu wa Afrika hawafungwi na mipaka hiyo. Mifano mwili, miongoni mwa mingine mingi, ni kama vile Wasenoufo, ambao wako Mali, Burkina Fasso na Ivory Coast na Wahausa ambao huishi Niger na Nigeria.

Ni dhahiri, basi, kwamba kuanzia kipindi kabla ya historia hapakuwa na vita tu bali pia kulikuwa na mwingiliano wa kijamii, kuchukua mila na dini za wengine na mambo mengine mengi kama yanavyojitokeza katika ramani ya Afrika. Mtawanyiko wa Waluo kati ya bonde la Naili na Afrika Mashariki, kuenca kwa Wabantu kati ya Sudani na Afrika ya Kati na kusini mwa Afrika, biashara ya kuvuka bara, kati ya pwani ya Atlantiki na pwani ya mashariki ni sehemu muhimu tu ya kuchanganyikana kwa watu kulikoendelea kwa maelfu ya miaka. Wala uhamaji au uvamizi wa kudumu siku zote laukuwa katika umbo la mawimbi yasiyoshindika ya kihistoria kama inavyodhihirika katika mfano wa Chaka. Kwa mfano kuishi kwa Wamossi katika nchi wanayokalia leo ya Burkina Fasso kulitokea taratibu, kadri makundi ya askari wapandaji farasi yalivyochukua wanawake katika makundi ya watu waliokutana nao, lakini wakaacha madaraka juu ya vitu kama kuabudu ardhi na haki za makazi katika mikono ya watemi wa sehemu hizo. Hivi ndivyo Ubri, mshindi mkuu wa Wamossi alivyokuwa chotara. Mwendelezo huu wa kuchanganyika taratibu ndio uliokuwa wa kawaida sana na ile picha tunayopewa ya wimbi la usongaji mbele wa uvamizi kama inavyojitokeza katika maandishi yanayocheza kutoka ghafla kwa Beni Hilal katika Afrika kaskazini kwa mfano hailingani na ukweli wa kihistoria.

kwa muda mrefu anthropolojia ya maumbile ilitumiwa kuwagawanya watu kwa namna ambayo iliwadhuru na kuwatia dosari watu weusi ambao waliitwa washeenzi "waliostarabishwa" na watu waliodaiwa kuwa wa "mbarikuu bora" kama vile Wahamiti. Wanazuoni kama vile J. Hiernaux wamconyesha upofu wa mengi ya mawazo haya ambayo yamecgmeczwa kwenye msingi wa ubaguzi wa rangi. Kwa mfano, Wafulani, ni kundi la kitamaduni na wala sio la kibiolojia. Kushabihiana kwa Wamoor na Wawarsingili wa Usomali kunatokana na kurithi na hali ya mazingira yabisi na yasiyo na rutuba ambayo yameathiri makundi yote na yamesababisha maumbo yao kuwa marefu zaidi, nyonga zao kuwa pana zaidi na vichwa vyao kuwa vyembamba na virefu. Hivyo basi, tukiacha baadhi ya sehemu za Afrika Kaskazini ambako neno *kabila* linatumika, neno "kabila" halitaingizwa katika historia hii kutokana na hisia za dharau ziandamanazo nalo.

Msingi wa nne unaotuongoza ni kwamba laihalisi historia kuwa jambo la masimulizi tu ambalo linazingatia tu vitu na unyonyaji uliofanywa na watu fulani maarufu. Ni lazima ishughulikie vilevile mambo muhimu ya *ustaarabu*, *taasisi*, *miundo mbalimbali ya maisha*, *mbinu*, na *taratibu za kijamii, kisiasa, kitamaduni na kidini*.

Kwa kuhitimisha pengine inaweza kuulizwa kwa nini ni muhimu kufanya jitihada kubwa kuunda upya historia ya bara letu. Jibu la kwanza ni kwamba pasipo historia ya Afrika historia ya ulimwengu kwa jumla ingebaki katika hali isiyu dhahiri, kwa namna nyingi. Zaidi ya hapo mbinu iliyotumiwa kwa historia hii itatoa mchango mkubwa wa kisayansi katika uandikaji wa historia kwa jumla; hasa kwa upande wa mkabala wa kuzingatia taaluma fungamano. Si hivyo tu, kuishi bila historia ni kama kipande cha ubao kinachoelea majini au kama mti uliokatwa na ambao unatafuta njia ya kujiunganisha na mizizi isiyu yake.

Hata hivyo, kimsingi, kuandika upya historia hii ni wajibu kwa sababu kwa watu wa Afrika hii ni haki yao. Wao ndio walioiunda historia yao na wanaendelea kujenga. Sharti paundwe timu mbalimbali ambazo zitajaribu kuokoa mabaki ya historia ya wakati uliopita kadri iwezekanavyo na majumba ya makumbusho hayana budi kujengwa ili kuyahifadhi mabaki hayo. Sharia shurti zitungwe kuyalinda, misaada ya masomo itolewe kuwafunza wataalamu mbajimbali, mihutajari ya masomo na kozi za shahada shurti ziundwe katika mtazamo wa Kiafrika. Historia itunike siyo tu kama kioo ambamo tunatambua sura zetu bali pia iwe ni msukumo utakaotupeleka mbele katika barabara ya maendeleo na ufanisi.

# I

## Maendeleo ya uandikaji historia wa Afrika

Hati za mwanzo juu ya kale ya Afrika zilitokoa wakati uandishi ulipoanza. Ikiwa kama sehemu halisi ya dunia ya Mediterani ya kale na ya ustaarabu wa Kiislamu, Afrika Kaskazini daima imetoa mchango wake kwa historia ya Afrika pamoja na ile ya maeneo yaliyoko kusini mwa Sahara. Hata hivyo kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na nane hadi 1930 au karibu hapo, uandikaji historia ya Afrika Kaskazini ulitawaliwa na mtazamo wa wakoloni wa Kizungu hadi mwamko wa kizalendo katika kanda hii ulipojumuisha mitaala ya kihistoria katika mipango yake kuanzia tarehe hiyo ya nyuma na kuendelea.

Kwa hivyo, sura hii inajihusisha na uandikaji historia wa Afrika kusini mwa Sahara, 'Ethiopia' ya kale ya Bilad al-Sudan ambayo mawasiliano kati yake na sehemu nyingine yalikuwa madogo kidogo na kufanya maandishi ya kihistoria kuwa machache. Mbali na hati za maandiko-picha, vyanzo vilivyopatikana mwanzo vilikuwa na maelezo ya juu juu na vilirejelea Afrika kusini mwa Sahara kwa njia ya ngano au maelezo ambayo mara nyingine hayakuwa ya moja kwa moja na pengine yasiyokuwa dhahiri. Kwa mfano Herodotus, Pliny Mkubwa na Strabo walitoa masimulizi ya safari au mashambulizi kupitia Sahara au katika sehemu za 'mwanambao'. Maeneo - ya kibiashara ya wafanyabiashara wa Alexandria katika Bahari ya Shari na katika Bahari Kuu ya Hindi zilitoa msingi wenye hakika zaidi kwa kazi zilizoshughulikia kanda hiyo kama vile Periplus of the Erythraean Sea (karne ya 1 enzi ya Kristo) na maandishi ya Cladius Ptolemy (nusu ya karne ya pili ya enzi za Kristo).

Karibu zaidi na wakati wa sasa biashara za kawaida za kupita Sahara kwa ngamia na mashambulizi Magharibi ya Bahari Kuu ya Hindi yiliwawezesha wanaojiografia na waandishi wa Kiarabu walioishi kati ya karne ya tisa na ya kumi na tano kama vile al-Bakrī, al-Idrīsī, Yāqūt, al-Umari, Ibn Battuta na leo Africanus (Hassan ibn Muhammad al-Wuzza'n) kutupa mwanga kuhusu kanda za Saheli za Sudani na mwanambao wa Afrika Mashariki. Tatizo lililolotwa na hizi kazi zenye thamani kubwa ni lile la kuhakikisha ukweli halisi wa vyanzo vyao ambavyo hutofautiana sana kwa ubora: wakati mwingine vina taarifa zilizosluhudiwa ambapo wakati mwingine zimekusanywa na katika hali nyingine ni mchanganyiko wa njia hizo mbili kama ilivyo kuhusiana na kazi za Leo Africanus.

Hata hivyo, miongoni mwa waandishi hawa yuko mahiri mmoja anayejitokeza kuliko wote: Ibn Khaldun (1332-1406), 'baba wa historia ya sasa', aliyezaliwa Tunis. Falsafa yake

1 Herodotus alikuwa mwanahistoria na mwanajiografia wa Kigiriki wa karne ya 5 kabla ya Kristo. Pliny Mkubwa alikuwa mwanazuoni wa Kirumi, aliyeishi karne ya kwanza ya enzi ya Kristo; alikamilisha kazi yeye majuzuu 37 juu ya sayansi ya mambo ya asili. Strabo alikuwa mwanajiografia wa Kigiriki kutoka Asia Ndogo, aliyeishi karne 1 kabla ya enzi ya Kristo.

ya historia hutazama mwendelezo mzina kama namna ya mbembeo ambamo wanomadi wakisukumwa na nguvu za mshikamano walioukata jangwani, kwa kawaida hunyakua ardhi inayolimika na miji, lakini hatimaye hudhalilika kutokana na maisha ya kutamakani na kunyinwa uongozi na wanomadi wengine. Ruwaza hii ambayo ilizingatiwa na Marc Bloch kuhusiana na Ulaya mwanzoni mwa enzi za kati, huonyesha uwezo wa kubashiri wa Ibn Khaldun ambaye, kwa hakika, ndiye alitoa itikadi za uyakinifu wa kihistoria miaka mingi kabla ya Karl Marx. Sura mojawapo katika kazi yake muhimu zaidi inahusu Miliki ya Mali ambayo wakati huo ilikuwa katika kilele chake.

Hatimaye tamalaki za Saheli na Sudan ziliwapata waandishi wao wenyewe ambao miongoni mwa kazi zao zilikuwa vitabu maarufu vya *Ta'rikh al-Sudan* na *Ta'rikh al-Fattash* ambavyo vyote viwili vilitungwa huko Timbuktu katika karne ya kumi na saba. Kwa upande mwingine, *Kilwa Chronicle* ambayo huenda ni ya kuanzia karne ya kumi na tano na *Kano Chronicle* ambayo yaonekana iliandikwa mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa ni mikusanyo ya mapokeo simulizi. Hivi karibuni, katika karne yetu hii, idadi kubwa ya miswada iliyogunduliwa inaonyesha kwamba Waafrika wasemao Kiarabu walitaka kuandika maelezo kuhusu nchi zote walimoishi au walizopitia, kama ilivyo kuhusu *Gonja Chronicles* (*Kitab al-Ghunja*) inayoelezea habari za Ufalme mdogo uliokuwa kaskazini mwa sehemu ya kati ya Ghana ya leo.

Yafaa pia kutaja kazi zilizoandikwa kwa hati za Kiarabu, lakini katika lugha za Kiafrika kama vile Kihauza, Kiswahili na Kifulfulde ambazo nazo zilikuwa nyingi katika kipindi hicho hicho. Isisahauliwe pia kwamba kwa miaka elfu mbili au zaidi Ethiopia ilikuwa na mfululizo wa desturi ya uandishi mwanzoni kwa Kige'ez na baadaye kwa Kiamhara iliyoweza kutoa kazi maarufu kama *Wars of Amda Sion*.

Kuanzia karne ya kumi na tano na kuendelea, kanda za Afrika zilizotembelea mara nyingi na wazungu kama vile miamba ya Guinea, kanda ya Zaire ya chini na Angola, nchi ambamo Mto Zambezi hupitia na Ethiopia zilikuwa mada katika mitaala mbalimbali na maeneo yaliyoshughulikiwa kwa makini na wanahistoria. Tukianza na Cadmosto katika mwaka 1460 hadi kuwafikia Barbot na Busman katika karne ya kumi na nane, bila kumsahau Dapper na mkusanyo wake mkubwa (1688), waandishi kadha waliacha maandishi kuhusu miamba ya Guinea ambayo ni viashirio muhimu kuhusu maendeleo katika sehemu hii ya Afrika Magharibi.

Udadisi kuhusu Waafrika kwa jumla ulikuwa wa kijuujuu miongoni mwa wafanyabiashara lakini ulikuwa wa namna iliyo wazi miongoni mwa wamisionari ambao walitaka kujifunza zaidi kuhusu jamii walizokuwa wamenuia kuzibadilisha. Katika Ethiopia, ambako data za kimaandishi zilikwishakuwapo, ziliwasaidia wamisionari wa karne ya kumi na saba Pedro Paez na Manoel de Almeida, wakifuatwa na mtaalamu wa mamba ya Mashariki Job Ludolf, ambao walitoa kazi za kwanza za kihistoria. Katika Congo, Angola na bonde la Zambezi upinzani wa Waafrika dhidi ya unyimivu wa wafanyabiashara ulisababisha visa vikubwa vinavyogusiwa katika kazi za waandishi kama Pigafetta na Lopez katika karne ya kumi na sita na Cavazzi katika karne ya kumi na saba, wakati ambapo Cardonca pia aliandika kitabu chake cha *History of the Angolan wars*.

Ilipofikia karne ya kumi na nane kulikuwa na ongezeko kubwa la kazi zilizokuwa na maeneo makubwa zaidi kama vile historia na jioografia za kilimwengu. Ama kwa hakika, maandishi ya awali yalitumiwa kama vyanzo na mabishano kuhusu biashara ya watumwa yalikuwa yamekwishaanza kushitadi. Kazi za kuanzia kipindi hiki ni kama vile *Universal History*, *History of Angola* iliyoandikwa na Silva Corrcia, *Some Historical Account of*



Guinea' iliyoandikwa na Benezet, *Memoirs of the Reign of Bossu Ahalee* iliyoandikwa na Norris na *the History of Dahomey* iliyoandikwa na Dalzel.

Kipindi hiki pia kilishuhudia kutokeza kwa tabia ya kujihisi bora ambayo wazungu walianza kuionyesha kuhusu mabara waliyokwisha yanyonya kwa karne kadha. Mwelekeo wao huu ulitokana na mageuzi makubwa ambayo tangu mapinduzi ya kisayansi na kitasua, yaliipa Ulaya nyenzo kubwa. Lakini wazungu walisahau ukweli kwamba sehemu ya nguvu yao ilitokana na biashara ya utumwa ambayo ilikuwa imezidhoofisha jamii katika Afrika.

Hegel (1770-1831) hakusita kusema katika kitabu chake *Philosophy of History* kwamba Afrika 'si bara la kihistoria; halionyeshi mabadiliko wala maendeleo' na kwamba watu weusi hawakuwa na uwezo wa maendeleo wala elimu. Hivi walivyo leo, ndivyo walivyokuwa siku zote." Mtazamo huu wa kifidhuli kuhusu Waafrika uliendelea hadi katika karne ya ishirini ambapo Profesa wa Oxford aliweza kusikika akisema: "Huenda katika wakati ujao, kutakuwa na kiasi fulani cha historia ya Afrika cha kuweza kufundishwa. Lakini kwa wakati huu hakuna historia yoyote: historia iliyopo tu ni ile ya Wazungu katika Afrika. Kilicho baki ni kiza... na kiza si sono la historia... Kwa hiyo haituhalisisi kujifurahisha na mwinginyo isiyoyona faida ya makabila ya kishenzi yanayoishi katika maeneo ya dunia yenye kuvutia macho lakini yasiyo na umuhimu wowote."

Hata hivyo, kutokana na uvumbuzi na unyanganyiro wa Afrika katika karne ya kuini na tisa, idadi kubwa ya vitabu juu ya bara hili viliandikwa, vikiwa pamoja na vitabu kama vile vya akina James Bruce cha *Travels to Discover the Source of the Nile; Mission from Cape Coast Casile to Ashantee* cha Bowdich, kazi za Mvumbuzi Mkuu Heinrich Barth; *Documents sur l'histoire, la géographie et le commerce de l'Afrique orientale* cha M. Guillain; na *Sahara und Sudan* cha Gustav Natchigal. Minojawapo wa wasafiri wakubwa wa kipindi hiki alikuwa Richard Burton, ambaye alikuwa mtaalamu maarufu wa inambo ya Mashariki mwenye kupenda kudadisi. Katika kitabu chake *Mission to Glele, King of Dahomey* (1864) anaandika: "Katika jamii ya binadamu Mnegro halisi yu chini ya mbarikuu mbili za Kiarabu na Kiarya.... Mnegro, kwa jumla, hawezi kuendelea kuvuka kiwango fulani, ambacho nacho hakistahili heshima; kiakili hubakia mtoto daima."

Wasomi fulani wa Kiafrika kama James Africanus Horton, waliingia kwenye injadala nikali juu ya mada hii na London Anthropological society, bila inafanikio yoyote. Mambo yalikuwa mabaya zaidi wakati kikundi cha wanahistoria wa Kijerumani walipodai kwamba vyanzo vya kimaandishi tu ndivyo vinavyoweza kutoa nisingi unaostahili wa historia. Huko London Profesa A.P. Newton alikariri nadharia hii alipodai kwamba Afrika "haina historia kabla ya majilio ya Wazungu. Historia huanza tu watu wanapoanza kuandika"... "desturi za kishenzi"... ziliwahusu "wanaakiolojia, wanaisimu na wamaanthropolojia." Matokeo ya fikra hizi ni kwamba katika kitabu cha *Cambridge Modern History* kilichochapishwa mwanzoni mwa karne ya ishirini kilipuuza Afrika kabisa, na uandishi wa historia ya bara hili ukabakia mikononi mwa watu kama Sir Charles Lucas na Gabriel Hanoloux. Kwa hiyo historia ya kikoloni na ya kibeberu ilichukua nafasi ya historia ya Afrika. Hata hivyo, miongoni mwa majuzuu manane ya *Cambridge History of the British Empire*, ni moja tu lililohughulikia Afrika na hasa Afrika Kusini, yaani historia ya walowezi katika eneo hilo. Ni sura ya utangulizi tu iliyoandikwa na mwananthropolojia, ndiyo inayogusia watu wa Afrika. Kwingineko, historia ya Afrika ilitokeza kidhaifu katika machapisho ya hivi karibuni zaidi kama vile *Peoples et Civilisation* au *Histoire Générale* kilichoandikwa na Glotz na kuchapishwa Paris; *Historia Mundi* kilichotokoa Berne; *Vsemirnaja Istorija*, kilichochapishwa Moscow na *Storia d'Etioopia* kilichohaririwa na C. Conti Rossini. Hata

wanaakiolojia hawakuslughulikia sana Afrika kwa kuwa, katika wakati huo, nao pia walivutiwa na vyanzo vya kinaandishi na uvumbuzi wa maandishi-nakshi ya kale. Ni magofu makubwa tu ya Kiafrika kama yale ya Aksum na Zimbabwe ndiyo yaliwapendeza wanazumi, ambapo machimbo yaliyofanywa kutafuta asili ya binadamu yaleleka yalikuwa ya kijiolojia zaidi kuliko ya kihistoria, pengo kubwa la wakati liliwatenga hawa wanadamu wa kwanza na watu wengine historia halisi.

Ni kweli kwamba katika karni ya ishirini wanaanthropolojia na wanaisimu walivutiwa na ukubwa wa aina mbalimbali za maumbile ya wanadamu jamii na lugha za bara na wakaanza kwa shauku kufanya kazi anzilishi za uwandani. Wakati mwingine walijaribu kueleza hali iliyokuwapo. Matokeo yake wakati mwingine yalikuwa mabaya sana. Hii ni kweli hasa kuhusiana na kitabu *Races of Africa* kilichoandikwa na mwanaanthropolojia C.G. Seligman ambacho kilichapishwa mwaka 1930 na ambamo aliandika "Staarabu za Waafrika ni staarabu za Wahamiti". Alihitimisha kwa kusema kwamba maendeleo yaliyofanywa na makundi mengine - Mnegro na Mtukoko - yalitokana na athari za "kabila" bora la Kihamiti. Haya madai ya bure na ya majivuno yalikanushwa na baadhi ya waandishi, miongoni mwao akiwa J.H. Greenberg, ambaye alionyesha kwamba istilahi Hamiti haikuwa na inana yoyote isipokuwa kama mwainisho wa kiisimu, ambao haukuwa na maana ya upangaji wa mbarikuu kulingana na ubora wao. Kama mfano, alikariri "Wakulima wa Kihausa wameka Kihamiti... chini ya utawala wa Wafulani wafugaji wanaosema.... lugha ya Ki-Niger-Congo (yaani Kinegro)." Hata hivyo, katika enzi zake Seligman alichukuliwa kama bingwa katika uwanja wake na kazi yake ilichukuliwa kama kazi ya kirasini. Ama kwa hakika mwelekeo wake uliakisi kashfa na uliokuwa wa kawaida katika mazingira alimoishi ambamo watu weupe waliotamalaki na kutawala Afrika katika karni ya kumi na tisa walikuwa wakiendeleza tu mwendeleo wa kustaarabisha, ambao watu wengine ngozi ya maji ya rangi ya kunde waliojulikana kwa jumla kama Wahamiti, walikuwa wamekwishauanza kabla yao. Mkabala huu wa kibaguzi unaweza kuonekana katika kazi kubwa zilizofanywa na baadhi ya waandishi waliofuata, kama vile Sir Harry Johnston katika muhtasari wake mkuu *A History of the Colonization of Africa by Alien Races* na Maurice Delafosse katika utafiti wake *Haut Sénégal-Niger*. Kwa mfano, katika maoni ya Delafosse, Himaya ya Ghana ilikuwa imeanzishwa na wahamaji wa Kiyuda-Kisiria. Vivyo hivyo, Flora Shaw, katika kitabu chake *A Tropical Dependency* (1906) alishikilia sana athari za Waarabu Waislamu kusini mwa Sahara, ambapo Yves urvoy katika kazi zake kubwa *Histoire Populations du Soudan Central* (1936) na *Histoire du Bornou* huona tu athari moja wa wanomadi wa Sahara juu ya Wanegro watamakani. Mwanaakiolojia Sir Richard Palmer (*Sudanese Memoirs 1928 na The Bornu Sahara and Sudan 1936*) hufika hadi Tripoli na Yemen kutafuta nguvu iliyosukuna historia ya watu wa Nigeria.

Kisaasili cha Kihamiti kiliachwa kidogokidogo lakini hata hivyo, hapakutokca mkabala linganifu. Ama kwa hakika, kati ya mwaka 1930 na 1950, wanaanthropolojia waamili kama A.R. Radcliffe-Brown na B. Malinowski waliathiri sana fikra za wakati huo. Walizipa unuhinu mkubwa changamizi thabiti na elezi, bila kuziingilia hakika za kihistoria za hali iliyoelezwa. Kazi zilizowakilisha mtazamo huu ni *The King of Ganda* (1944) kilichoandikwa na Tor Istain, *The Trade of Guinea* (1965) cha Lars Dunstrom, *Völkerkunde Afrikas* (1940) cha Herman Baumann, na *Geschichte Afrikas* (1952) cha Dietrich Westermann. Mwandishi aliyetajwa mwisho alikuwa mwanaisimu maarufu aliyeshiriki katika kazi-anzilishi ya kutengeneza ensiklopedia kubwa ya Baumann ingawaje yeye pia hakuweza kujepusha na dhana hii ya Kihamiti. Kazi kubwa ya G.P. Murdock, *Africa: Its People and*

*Their Cultural History* (1959) ina dosari kwa sababu mwandishi hakuwahi kufika Afrika.

Inawezekana pia kutaja *The Zimbabwe-Monomotapa Culture* (1948) kilichoandikwa na H.A. Wieschoff, aliyekuwa mfuasi wa Leo Frobenius ambaye ni mwanaanthropolojia wa kitamaduni, mwanaakiolojia na mwanahistoria yote kwa pamoja. Frobenius alikuwa mwandishi mashuhuri aliyetoa ripoti kuhusu kazi kubwa za uwandani alizozifanya katika inaeneo mengine kote barani. Pia alitoa nadharia asilia kadhaa ambazo baadhi yake zilikuwa nzuri hali nyingine kama zile kuhusu athari za Atlantis na Etruscan juu ya utamaduni wa Afrika zilikuwa za kilimbwende. Vyovyote vile tutakavyoyafikiria makusudio makubwa ya Frobenius yaliyochochewa na shauku isiyopungua na fikra zake za kutaka kujitambulisha na Afrika, aliweza kukusanya taarifa nyingi ambazo ingefaa zitaluminiwe tena na ambazo bila shaka zinaceza sababu za watu kuvutiwa tena na kazi yake hivi leo.

Hata hivyo, hatuna budi kukiri kwamba hamu ya wataalamu wa historia katika Afrika ilikuwa ndogo mno mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Kwa bahati nzuri, kama ilivyokuwa kuhusiana na *Ta'riki* katika karne ya kumi na sita, Waafrika wenyewe walijitokeza kuokoa mambo. Wakiwa wamekwishajipatia ujuzi wa lugha za Kiuroopa, walizitumia kuweka pamoja ushahidi kuhusu kale ya watu wao. Miongoni mwa vitabu vinavyofaa kutajwa ni *A History of the Gold Coast and Asante* (1895) kilichoandikwa na Carl Christian Reindorff na *History of the Yorubas* kilichoandikwa na Samweli Johnson, ambavyo vyote hadi leo hii bado vinaaminika na ni inarejco muhimu ya historia ya watu wao.

Kulikuwapo pia na kazi nyingi za mane-wazalendo wa kwanza ambao mara nyingi walitumia historia kutetea msimamo wao na kuvunja kisaasili kuhusu unyonge wa utamaduni wa mtu mweusi. Waandishi katika kikundi hiki walikuwa akina J.A.B. Horton, E.W. Blyden, J.M. Sarabah, J.E. Casely-Hayford na J.B. Danquah, na wenyewe kujulikana zaidi ni J.O. Lucas aliyandika *Religion of the Yoruba*, J.W. de Graft Johnson aliyandika *African Glory* na Eva L.R. Meyrowitz aliyandika *The Sacred States of the Akan; the Akan Traditions of Origin* (1952). Baadhi ya waandishi waliotajwa mwisho walijaribu kufuatilia nyuma historia ya watu weusi hadi kwa wazazi wa zamani wa Bonde la Nili.

Mara nyingine kutokana na uchochezi wa Wamisionari, kazi za kihistoria ziliandikwa kwa lugha za Kiafrika, kama katika Uganda na Yorubaland. Mfano mmojawapo ni kazi mashuhuri *A Short History of Benin* ya J.V. Egharevba (1934).

Aidha ukoloni uliingia na matakwa mapya ya kiutendaji. Ili kuwa watawala bora, iliwasaidia wazungu kujifunza mambo fulanifulani ya kale ya Afrika, uhusiano kati ya makundi tofauti na taasisi zao za kale. Zaidi ya hayo, misingi ya historia ya mahala pale, ilifundishwa katika shule zilizoanzishwa ili kuwafunza wasaidizi wa baadaye wa watawala wa koloni, ingawa pengine kwa nia tu ya kuwaamsha hamu kwa kile kilichofikiriwa kuwa cha muhimu zaidi yaani ujuzi wa historia ya watawala wao. Hata hivyo kazi za baadhi ya waandishi hawa zilitokeza kutokana na ubora na uyakinifu wa maelezo yao, au walau na usahihi wa mambo waliyoyakusanya. Mifano ni *The Land of Zinj* (1913) kilichoandikwa na C.H. Stigand, *Caravans of the Old Sahara* (1933) cha E.W. Bovill, *Les Empires du Mali* (1929) cha Charles Monteil, kazi za Georges Hardy na Henri Labouret na kazi ya kuvutia *Tableau géographique de l'Ouest Africain au Moyen Age* (1961) ya Raymond Mauny.

Polepole iniundo rasmi ilianzishwa, hasa katika makoloni ya Kifaransa, kwa kuanzishwa *Comité d'études historiques et scientifiques de l'Afrique Occidentale Française* iliyoitangulia *Institut français de l'Afrique Noire* (IFAN) iliyoundwa Dakar mwaka 1938 na ambayo machapisho yake *Bulletin* na *Memoires* yaliongoza njia ya utafiti. Kuanzia 1947

na kuendelea, *Societe Africaine de Culture* na jarida lake *Présence Africaine* vilitoa mchanganyiko mkubwa, ambapo wasomi wa Kiafrika waliojifunza mbinu za kihistoria, walitumia mbinu hizo katika bara lao, kurejesha uyakinifu na kujalizia mbinu hizo hasa kwa matumizi mapana na makubwa ya

vyanzo kama vile mapokco sinulizi, isunu na kahalika. Katika muktadha huu twawcza kutaja kongamano juu ya matatizo ya kutamakani kwa watu katika Misri ya Kale, lililoandaliwa huko Cairo na UNESCO.

Mwisho, lakini muhimu pia ni vyuo vikuu, vituo vilivyotukuzwa vya uchunguzi, vilivyoanzishwa polepole. Katika jambo hili makoloni ya Kiingereza yaliongoza njia baada ya kuundwa kwa *School of Oriental and African Studies*. Chuo cha Liberia huko Monrovia na Chuo cha Fourah Bay katika Sierra Leone vilikuwepo tangu karne ya kumi na tisa, lakini kuanzia mwaka 1948 na kuendelea milolongo ya taasisi za Chuo Kikuu zilianzishwa katika Gold Coast na Nigeria na huko Khartoum na Kampala (Makarere College), na huko Dakar (1950) na Leopoldville (Lovanium 1954).

Wataalamu wa historia kutoka katika vyuo vikuu hivyo na kutoka katika nchi zilizoendelea waliwawezesha Waafrika kushika nafasi zao ingawaje kulihitajika kuwashawishi kidogo. Mnaino mwaka 1956 katika Chuo Kikuu cha Ibadan Profesa K.O. Dike alikuwa Mkurugenzi Mwafrika wa kwanza wa idara ya historia.

Tangu kumalizika kwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, uandikaji historia wa Afrika ulizidi kufanana na ule wa schemu nyingine yoyote duniani, ingawaje, japokuwa misingi ya jumla ya uhakiki wa kihistoria imezingatiwa, imebidi ukubali mikabala mbalimbali mahsusi ya kifundi ili kukabiliana na matatizo fulani. Lakini yafaa isisitizwe kwamba maendeleo haya yasingepatikana kama Mwafrika asingejikomboa kutoka katika nira ya ukoloni; mapambano ya silaha ya Madagascar mnamo mwaka 1947, uhuru wa Morocco mwaka 1955, vita vya kishujaa vya watu wa Algeria na inapambano ya uhuru kote katika makoloni barani Afrika yaliwawezesha Waafrika wenyewe kuifikiria kale yake.

# 2

## *Nafasi ya historia katika jamii za Kiafrika*

Binadamu ni kiumbe mwenye historia. Huiangalia historia yake kana kwamba ni mfululizo wa matukio ambayo yalishapita kuwa kumbukumbu iliyojaa maana, yaani kama "ruwaza". Hivyo, wakati uliopita hukumbukwa kulingana na aina ya wakati wenyewe na aina ya kila hatua ambamo wakati huo umcepita. Jamii ambayo imekuwa ikipata ushindi mara nyingi, hukumbuka kale yake kwa namna tofauti na jamii ambayo imekuwa ikikandamizwa. Mazingira ya jiografia nayo pia luathiri jinsi watu wanavyoona mambo. Kwa hiyo kwa namna fulani, Waafrika huangalia wakati kama jambo la visaasili na la jamii. Hata hivyo, itaonekana kuwa Waafrika wanaamini kuwa wanaendesha kikamilifu historia yao wenyewe na wakati wa Kiafrika utaoonekana kuwa una misingi ya Kihistoria.

### *Wakati katika Visaasili na katika Jamii*

Visaasili vilikuwa na nafasi muhimu katika jinsi Waafrika walivyotazama jamii. Mara nyingi desturi zilipangwa kwa ajili ya wale wenye dhima maalum katika jamii: watu wote kuanzia kiongozi walipaswa kufuata mienendo ya mhenga aliyestahili kufuatwa na ambaye asili yake ilikuwa katika gubiko la wakati. Kisaasili kilitawala historia na papo hapo kuithibitisha.

Sifa mbili hutokea katika aina hii ya fikra ya kihistoria: kutofungwa na mipaka ya wakati na umuhimu wake kijamii. Pale ambapo wakati hauhesabiwi hujumuisha umilele wa wakati uliopita na ule wa wakati ujao. Wakati luafanani na into ambao unachimbuko na mkondo ila luafanana zaidi na bahari isiyo na mipaka kamili. Hivyo kitendo kinaweza kuanzia mahali popote na athari zake zikafika mahali popote. Mansa Musa, mfalme wa Mali (mwaka 1312-1332) alipomwomba Mfalme wa Yatenga abadihishe dini na kuwa mwislamu, mfalme huyo wa Yatenga alijibu kuwa alipaswa kwanza kuomba ushauri kwa mababu zake kwa kutambika. Mfano huu unaonyesha jinsi mambo ya kale yanavyoathiri mambo ya sasa moja kwa moja. Ndoto za wafalme kama zilivyofafanuliwa na mawaziri walioteuliwa maalumu kufanya kazi hiyo zilisababisha vitendo halisi vya siku za mbele ambavyo havikusababishwa na matukio halisi ya wakati uliokuwapo. Katika namna hii ya wakati uliosaki luku na luuko, huenda hata wakati wa sasa ukaathiri wakati uliopita ambao kwa kweli unaweza ukabaki wakati uliokuwepo. Damu zinazotambikwa sasa huweza kuwasaidia mababu waliokufa.

Maendeleo yaliyotokoa katika wakati wa historia yanahusishwa na maelezo katika visaasili. Kwa vile wakati wa historia huangaliwa kwa namna tofauti, na kila mtu, badala yake hutokoa kumbukumbu za jamii zisizo za kihistoria. Mfano munojawapo ni ngano ya

Wakikuyu inayosimulia jinsi watu walivyogundua mbinu ya kufua chuma. Ngai (Mungu), alikuwa amewagawia wanyama, wanaume na wanawake. Lakini wanawake walikuwa katili sana na wanyama wao walikimbia na kuwa wanyama pori. Kwa niaba ya wake zao, wanaume walimwomba Ngai na kusema: "Tuko tayari kutoa sadaka ya kondoo kwa leshima yako lakini hatupendi kutumia kisu cha mti tusije tukapatwa na yale yaliyowapata wake zetu." Ngai aliwampigeza kwa busara yao na akawafundisha kufua chuma ili waweze kupata silaha nzuri zaidi.

Dhana hii ya visaasili na jamii ilifanya wakati kuwa sifa ya ufalme. Huko Sudan, mfalme wa Washilluk ni mhifadhi wa kibinadamu mwenye madaraka ya kiungu, kwa sababu hujumuisha katika nafasi yake wakati wa kisaasili na wa jamii (ni mfano wa shujaa muasisi), na huhesabika kama ni chanzo cha uhai wa jamii. Hali kama hii huonekana kati ya Bafulero wa Zaire ya Mashariki, Wanyoro wa Uganda na Wamosi wa Burkina Fasso ambao wote lumwona kiongozi wao kama nguzo ya wakati wa jamii: "Mwami akiwepo: watu huishi. Mwami asipokuwepo: watu hufa". Ama kwa hakika, mfalme anapokufa, wakati unasimama na shughuli zote na mipangilio yote na kila kitendo cha uhai toka kucheka hadi kilimo na hujamiiana baina ya binadamu au wanyama. Katika kipindi cha mudakali (yaani kipindi kati ya kufariki mfalme na kutawazwa mrithi wake) wakati husunama na kila kitu kilichokuwa kinakatazwa kinaruhusiwa.

Kwa hiyo kila jambo linaonekana likifuata imani ya kuzimu ambamo schemu inaweza ikawakilisha na hata kumaanisha kitu kizima; na nywele na kucha zilizokatwa hazipaswi kuingia mikononi mwa adui kwani zaweza kumfanya amdhibiti mwenye nywele na kucha hizo.

Kwa hakika tukitaka kujua Waafrika wanavyouelewa wakati na kuona wakati una maana gani kwao, lazima tuangalie mtazamo wao kuhusu ulimwengu kwa jumla. Katika fikra za kikisaasili wakati unaopita ni schemu tu ya wakati mwingine aliotumia binadamu katika shughuli zake nyinginezo. Usiku, mtu anapolala kwenye mkeka au kitandani, kivuli chake huondoka na kufuata njia ambayo huyo mtu alifuata wakati wa mchana kwa kutembelca schemu alizotembelea na kurudia kazi na matendo aliyoyafanya wakati wa mchana. Wakati wa matembezi hayo, kivuli hukutana na mema na mabaya na wakati huo ndio kivuli hiki kinapaswa kuwa imara. Wasonghay wanaposema kuwa "bya" (kivuli) cha mtu fulani ni kizito au chepesi wanamaanisha kuwa haiba ya mtu huyo ni madhubuti au dhaifu. Mtu akitaka kufaulu katika maisha, lazima ajaribu kuwa kama kivuli chake katika kila kitu kama vile alivyofanya Si mhenga mashuhuri wa ufalme wa Songhay: "Baba wa wasi anatisha, ni baba wa radi. Anapounwa jino, anatafuna changarawe. Anapoviimba macho, hutoa miali ya moto. Anatanda ulimwenguni. Yuko kila mahali na haonekanki popote".

Wakati wa jamii, ambao ni historia ya matukio ya jamii hiyo, hulimbikiza madaraka ambayo huonyeshwa kwa kutumia kitu maalumu ambacho kiongozi hurithi toka kwa mzee au kwa mkuu wa ukoo au mfalme. Kitu hicho kinaweza kuwa ni kifute cha dhahabu kilichowekwa katika *toba* au ngoma ya vita, pamoja na mabaki ya mnyama pori. Kinaweza pia kuwekwa katika intungi kama vile mavazi rasni ya kifalme (*tibo*) ya Wamosi alivyowekwa. Wasonghay na Wazarma hutumia fumbo ya chuma. Wasorko wa ufalme wa zamani wa Gao walitumia sanamu ya samaki mkubwa mwenye pete mdomoni. Wasonianke, wazawa wa Sonni Ali wana mikufu ya dhahabu, fedha na shaba nyekundu na kila kiungo cha mkufu huo kinawakilisha mhenga mmoja na rukufu mzima unawakilisha unasaba unaorudi nyuma hadi Sonni Mkuu. Wakati wa sherche za matambiko, mikufu hiyo hutolewa kutoka kwenye midomo ya wale wanaoendesha sherche mbele ya umati uliokusanyika na kiongozi

wa Wasonianke anapofariki, anatema mkufu huo kwa mara ya mwisho na mrithi wake aliyeteuliwa huumeza mkufu huo. Kiongozi wa ukoo hufariki baada tu ya kukabidhi mkufu kwa mtu atakayeendelea uongozi. Utendaji wa wasia huu wa mwisho unaonyesha umadhubuti wa mtazamo wa Waafrika kuhusu wakati wa visaasili na wa jamii.

Labda watu wengine wanaweza kudhami kuwa msimamo wa namna hii kuhusu historia ni msimamo usio wa kimaendeleo na kuwa visaasili ndivyo husukuma historia ambayo imegota. Lakini kama tutakavyoona hapo baadaye, dhana ya historia katika jamii za Kiafrika ni pana zaidi.


Ama wa hakika kutumia visaasili kuelezea historia ni jambo la kawaida katika jamii zote. Kila historia huanza kama historia ya dini. Lakini wakati mwingine visaasili ndivyo hufumika mielelekeo, maoni au itikadi ya taifa fulani. Kwa mfano, wakati wa utawala wa Nazi huko Ujerumani, visaasili vya ubaguzi wa kitaifa kama vilivyoonekana katika matambiko ya kale viliwaingiza binadamu katika kipindi kimojawapo cha kutisha katika historia yake yote.

### *Je, Waafrika Wanatambua kuwa wanaendesha Historia yao wenyewe?*

Ni kweli kuwa kwa muda wa karne nyingi, Waafrika walinyimwa haki ya kuanzisha na kuvumbua mambo yao wenyewe kutokana na ghasia za mkengeuko zilizotokea wakati wa biashara ya utumwa na ukoloni. Pia kuna sababu za kutufanya tuamini kuwa kabla ya ukoloni, watu walioishi katika jamii ndogondogo walikuwa wakikandamizwa na madaraka ya wazee au na wakuu wa ukoo au na mfumo wa ndoa na hivyo hawakuishi kuwa wanadhiti maisha yao wenyewe. Hata hivyo ni katika kiwango hiki ndimo hisia hizi za kushirikishwa moja kwa moja katika maamuzi na kuwa mtu huru luwa kubwa sana. Kwa vile madaraka yaligawanywa miongoni mwa watu wengi katika jamii kama hizo, utamalaki wa ukoloni ulikabiliwa na upinzani nikubwa sana.

Katika jamii ambazo madaraka yalikuwa yamshikiliwa na watu wachache hasa katika jamii ambazo zilikuwa na mfumo mpana na madaraka, hatushangai kuona kwamba historia nzima ya kujitokeza kwa Himaya ya Mali hujumuishwa katika inaandishi ya *Sifa za Sundjata (Sundiata Fasa)*. Historia ya karibuni, ya kabla na baada ya ukoloni ya Afrika tangu zama za Osei Tutu na Anokye wa Asante hadi Shaka au Samory na mpaka kuwafikia wakuu wengine wa nchi za Kiafrika hivi leo, haitofautiani na dhana ya "maana" ya historia waliyonayo Waafrika. Lakini inabidi tuongeze kuwa ingawa Waafrika wanaamini kuwa kiongozi ndiye anayesababisha matukio ya historia kamwe hawamdunishi kwa kumfanya aonekane kama ndiye pekee anayeleta maendeleo ya binadamu wote. Karibu wakati wote kuna kikundi cha watu ambao ni mashuhuri katika kuleta maendeleo kama inavyochezwa katika *Sundiata Fasa*. Wasaidizi wa kiongozi huwasahauhiwi, hata wale wenye vyeo vidogo kama vile mayeli, waseinaji wa baraza na waludumu. Wao pia huingia katika historia kama mashujaa.

Wanawake pia hutambuliwa katika historia. Kinyume cha wanavyodhani watu wengi, wanawake hujitokeza zaidi katika historia ya Afrika kuliko katika historia ya bara nyingine. Katika jamii za kukeni ambamo mpwa humrithi mjomba jambo lili si la kushangaza. Kwa mfano, Wasonianke wanaamini kuwa madaraka hukabidhiwa toka kwa "titi la inama." Katika nchi nyingine pia wanawake huonekana kuwa na dhima muhimu katika mabadiliko ya kihistoria ya mataifa yao. Wakiwa binti, dada, wake na mama wa wafalme, wanawake walikuwa na nafasi nzuri ya kuathiri matukio. Kwa mfano, Luleji ambaye aianza kama binti wa mfalme kisha kuwa dada wa mfalme na baadaye kuolewa na mfalme na hatimaye kuwa mama wa mfalme ni mfano wa kiajabu wa mtu aliyestahili lakabu ya "Swana Mulunda" au



2.1 *Sanamu ya shaba nyeusi inayowakilisha nguvu ya kifalme ya wasongaji wa Dargol (A. Salifou)*



mama wa taifa la Walunda. Miongoni mwa majina mengine maelfu tunaweza kuyataja yale ya Yannenga, mama na shujaa wa Wamossi, na Annina mashuhuri wa Zaria ambaye katika karne ya kumi na tano alitamalaki miji mingi ya Wahausa ambayo mpaka leo ina jina lake. Vitendo vyao na heshima walivyopewa vinaendelea hadi leo kwa sababu ya shughuli zao katika vyama vya kisiasa na katika harakati za ukombozi. Kweli, wanawake hawa kama walivyo wanawake kila mahali walijitahidi kujipendeza na kujipamba na kutumia hila zao kuwapotosha wanaume kama vile alivyofanya dada yake Sundjata. Katika sanamu maarufu ya karne ya kumi na tisa, mfalme wa Dahomey anaonekana kwenye karamu akiwa amezungukwa na wanawake waliovalia vizuri sana na kujiremba. Lakini mfalme huyo alikuwa akihudumiwa pia na wanawake wa Kiamazoni ambao ndio walikuwa mstari wa inbele katika jeshi la mfalme lililopigana na Oyo na lililopinga wakoloni wavamizi kwenye vita vya Cana, mwaka 1892. Ingawa wanawake wa Kiafrika hawatokei hadharani ambako huenda ikadhauwa kuwa wanabaguliwa, lakini jukumu muhimu wanalolibebe katika uzalishaji wa bidhaa na vifaa vya kitamaduni huthibitisha methali ya Kiafrika isemayo: "wanawake huweza kutengeneza au kuharibu kila kitu".

Kwa jumla, kwa vile jamii zilikuwa na idadi ndogo ya watu kwa muda mrefu katika Afrika, hii ilikuwa na maana kuwa kila moja alihusika na madaraka ya historia, na hii ndiyo huweza ilhamu maarufu na ya kidemokrasia ambayo mara nyingi ndiyo huunda dhana ya Mwafrika kuhusu historia. Kila mtu alihisi kuwa aliweza kukimbia utawala wa kikatili na kwenda popote pale. Hata Shaka mwenyewe alifanya hivyo mwishoni mwa utawala wake.

Hisia hii ya kushiriki katika matukio ya historia katika mazingira ya kijiji au kusisunka na hisia ya kuwa kama chembe moja katika mfumo madhubuti wa ufalme mkubwa ni vipengee muhimu kwa mwanahistoria kwani hisia hizo ndio mada za historia na ambazo huchangia katika kuiunda historia.

### *Wakati wa Kiafrika ni wakati wa Kihistoria*

Baadhi ya watu kabla na baada ya Hegel wame dai kuwa Waafrika walichoweza kufanya ni kurudia tu mambo ya kale bila kuanzisha mambo mapya au kulea inaendeleo. Waandishi hao wamedai kuwa Waafrika wametamani mno mambo ya kale na kuhalalisha matendo yao kwa kusema: "mababu zetu walikuwa wakifanya hivyo". Hii ingalikuwa kweli, Ibn Batuta hangalikuta himaya ya Mali imejengeka ilivyokuwa bali angalikuta mapango ya kale au mabanda yaliyokaliwa na watu waliovaa ngozi. Maumbile halisi ya kijamii ya dhana ya historia ya Mwafrika huifanya dhana hiyo iwe ya kihistoria hasa maana historia ndio mabadiliko ya maisha ya jamii hiyo. Katika itikadi za jadi au katika mtazamo wa Kiislamu wa mambo ambao umecathiri maeneo mengi ya Afrika, historia imehusika katika kila jambo.

Katika mawazo ya Waafrika, wakati ni uwanja ambao binadamu huendeleza mapambano ya kulinda utu wake, afya yake na nguvu zake visidhoofishwe na huwakilishwa na familia, inashamba, vijiji, n.k. Katika imani ya kuzimu ya Waafrika, wakati ni uwanja uliozingirwa na ni kama soko ambamo mambo mbalimbali ya ulimwengu huu yanagongana na kusuluhishana. Nguvu hizo hukingwa, hukusanywa, huwelekezwa, hutuniwa na kuhamasishwa na utaalumu unaomfaida mtu mmoja au jamii nzima. Mwelekeo huu ni wa kimaendeleo. Kwa mfano, huko Niger, ukoo wa Cerco na ule wa Sonianke wa Wasonghay lupingana. Ukoo wa Cerco ambao unawakilisha wakati uliopita na unaotaribu kutawala usiku, hushambulia jamii. Ukoo wa Sonianke unaotawala mchana, unawakilisha wakati uliopo na hulinda jamii. Aina kwa hakika madaraka katika Afrika kusini mwa Sahara mara

nyingi huelezwa na neno lenye maana ya nguvu (*fanga, panga na pan* katika Kibambara, Kimore na Kisamo kwa mfuatano huo). Visawe hivi vinaonyesha umuhimu kwa Mwafrika wa nguvu pengine hata ukatili katika mwendelezo wa historia. Lakini haichukuliwi tu kama kitu alichio nacho mtu. Neno pia huwa nguvu. Ndiyo maana huko Songhay, mwishoni mwa ibada ya dini, mwendesha ibada huanza kutaja majina ya nasaba za wale wahomrithisha maenu matakatifu na humaliza kwa kusema: "Neno litokalo kinywani mwangu liwe zuri kuliko lilivyokuwa kinywani mwa babu zetu."

Kipengee kingine cha nguvu ni uadilifu wake ambao bila kuwapo kwake hakuna mwenye madaraka atakayeweza kutenda mema. Busara ya jamii huthitisha wazo hili katika hekaya nyingi ambazo huonyesha watawala dhalimu ambao hatimaye huadhibiwa na hivyo kupata fundisho la kihistoria. Vitabu vya *Ta'rikh al-Sultan* na *T'arikh al-Fattash* vinamsifu sana al-Hajj Askiya Muhammad. Ni kweli kwamba waandishi hawa walikuwa na maslahi yao katika kufanya hivyo lakini wanaonyesha kwa utaratibu mzuri uhusiano kati ya wema wa mfalme huyo na "bahati" yake nzuri. Mafundisho hayo yamo pia katika maandishi ya Muhammad Bello ambaye anamsihi Yacuba Bauchi kutafakari historia ya Songhay na hasa historia ya Askiya Muhammad kwa maneno yafuatayo: "Watu wengi wamepata madaraka makubwa lakini wameanguka sababu hawakuzingatia misingi ya haki... Kama tukitaka kudumisha utawala wetu, nguvu yetu lazima iwe nguvu ya ukweli na nguvu ya Kiislamu. Vizazi vijavyo... vitatuthamini kulingana na ukweli na haki tulivyotumia katika serikali yetu."

Mtazamo huu wa upeo wa juu wa dhima ya uadilifu katika historia unaonekana pia katika imami ya 'dini za jadi' ambazo huchukia dhambi kama kitu chochote kinachovuruga msawazo wa nguvu mhalimbali na huweza kudhuru jamii. Mtazamo huu waweza kufikiriwa kuwa ni wa kivisaasili tu lakini umeleta athari yakiniifu katika historia ya maisha halisi. Kwa mfano, katika mifumo ya jamii fulani za Afrika kusini ya Sahara, kulikuwa na vikundi maalumu vilivyokuwa na madaraka ya kiadili ya kudhibiti mwenendo wa shughuli za jamii ambavyo wakati mwingine vilikuwa vikundi vya siri kama vile vikundi vya *Lo* kwa Wasenoufo au *Waporo* wa Guinea ya Juu. Vikundi hivi vilikuwa na madaraka yaliyokwenda sambamba na yale ya viongozi wa jamii: na vilipokea rufaa. Vile vile vilichukua nafasi ya viongozi rasmi na hatimaye watu wakaanza kuwatazama kama vikundi vya siri vitovu vya kufanya maamuzi na vyenye kutisha.

Katika jamii za namna hiyo, mfumo wa rika unawawezesha watu kurudi nyuma katika rekodi za kikronolojia za maisha ya watu. Ilipolazimu, mfumo huu uliweza kutumika kutatua magomvi kati ya vizazi kwa kudhihirisha uhusiano kati yao kwa namna ambayo ilizua magomvi makali. Kizazi kilichotangulia kilituma mjumbe wake inmoja kwa kizazi kilichofuata. Dhima ya mjumbe huyo haikuwa kusimamia na kutoa adhabu bali kutoa ushauri na mwongozi ili kuhakikisha kuwa utukutu wa vijana hauleti madhara kwa jamii nzima. Waalladiani wa Moussou, karibu na Abidjan, hadi leo bado wanaendelea na mpango wa namna hii kwa shughuli za kila siku za jamii.

Utambuzi mkubwa wa wakati uliopita miongoni mwa Waafrika ambao huenda ukaonekana unaficha wakati uliopo ni kupuuza sifa zake za maendeleo, si ishara ya "maunbile" fulani ya Kiafrika, lakini ni dalili ya hatua mojawapo katika mabadiliko ya kijamii. Uthibitisho wa jambo hili unaonekana katika fikra ya "wakati ni mali" ya Waafrika wengi walioko mijini inavyotofautiana na ile ya wakati wa jamii ya jamaa zao wa vijijini.

Ngano na kisaasili ni sehemu ya juhudi ya kueleza maendeleo ya jamii, lakini juhudi pia zilifanyika za kuanza kupima wakati wa kihistoria kwa kuunganisha na kaida ya namna ya kutazama uliuwengu au ya kijamii hususa kama kaida hizi zinatokea mara kwa mara

kuunganisha watu binafsi. Jitihada zilifanywa pia kutafuta njia za kitaalamu zaidi za kupima na kuhesabu wakati. Kwa mfano, Ivor Wilks anaeleza kuwa Waakan walikuwa na kalenda changamano yenye wiki iliyo na siku saba, mwezi ulio na wiki sita na mwaka ulio na miezi tisa ambao unawiana na jua kwa kutumia njia ambazo hazijaeleweka vizuri bado. Kwa mfano, kwa kutumia kalenda ya Waakan, mtu aliweza kutaja siku ya kumi na nane ya mwezi wa nne wa mwaka wa tatu wa utawala wa Asantehene Osei Bonsu. Mfumo huu wa kuhesabu tarehe na miaka ulikuwa ukitumika bado katika nchi za Ulaya karne ya kumi na nane na hata karne ya kumi na tisa.

Hata hivyo mambo matatu yameathiri ubora wa dhana ya historia ya Waafrika. Jambo la kwanza lilikuwa ni kuenea kwa uandikaji ambao ulisaidia kuhesabu na kupima na hivyo kupanga vizuri jinsi wakati unavyopita. Jambo la pili lilikuwa ni kuingia kwa dini kubwa kama vile Uislamu na Ukristo, zenye misingi yake katika mila maalumu ya kihistoria. Kutokana na kuenea kwa dini hizi waongofu wa Kiafrika waliweza kuingiza historia yao kuwa sehemu ya historia ya jumla ya dini yao. Mwisho kuingia kwa Waafrika katika ulimwengu wa biashara na kulimbikiza mali kuliwatenganisha na dhana zao wenyewe na kuwafanya wawe chini ya mataifa yenye nguvu zaidi kiuchumi ambayo yaliwapangia kanuni na mwendo wao. Saa ya mkono inayovaliwa na wafanyakazi au wafanyabiashara wa Kiafrika ni ishara ya matakwa wanayopaswa kukidhi.

---



# 3

## *Mielekelo mipya katika taaluma ya uandishi wa historia ya Afrika na mchango wao kwa historia kwa jumla*

---

Majuzuu haya makubwa yanachapishwa katika juhudi ya kusawiri upya kale ya Afrika kwa sababu kale hiyo ni sehemu muhimu ya utambulisho na kwa hiyo ni kipengee muhimu katika maendeleo. Kwa hiyo Waafrika lazima wavuke vikwazo ambavyo historia iliyoandikwa na wakoloni imewaweka kati ya kale yao na wao wenyewe na ambayo imewazuia wasiingie katika mkondo wa historia.

Sote tunajua kuwa karne ya kumi na tisa na mwanzoni mwa karne ya ishirini, Ulaya ilitawala makontinenti mengiote yote. Hali ya kuwatawala wengine iliathiri mtazamo wake kuhusu historia ya ulimwengu na tangu wakati huo, historia ilitazamwa kwa jicho la Ulaya Magharibi ambayo iliongoza utamalaki wa nchi nyingine. Mtazamo huu wa Wazungu ulidhihirika katika makontinenti mengine kutokana na mifumo ya elimu iliyoanzishwa na wazungu hao katika makoloni.

Siku hizi msimamo wa namna hii kuhusu historia ya ulimwengu si msimamo rasmi lakini athari yake bado inaendelea. Wanafunzi wa mwongo wa kwanza wa karne hii ambao walijifunza msimamo wa namna hiyo wamefikia umri wa kustaafu kwenye miaka 1960. Walipomaliza shule, vitabu walivyokuwa wakitumia vilikuwa nyuma kwa miaka kumi hadi ishirini hivi, hivyo haikuwezekana kubadilisha msimamo potofu waliyokuwa wamefunzwa hasa kwa vile inaelezo yaliyokuwa katika vitabu hivyo yaliendelea kusambazwa na vyombo vya habari ambavyo vimebaki nyuma sana ukilinganisha na maandishi ya historia kwa jumla.

Hata hivyo, mwendelezo wa taratibu sana wa kubadili mielekeo unapaswa kutazamwa katika *uwili wa mapinduzi* ambao umeathiri taaluma za historia tangu mwisho wa Vita Vikuu vya Pili. Uwili huo wa mapinduzi umehusisha, mosi, *mabadiliko ya historia toka tarihi na kuwa sayansi ya jamii*, na pili, *ubadilishaji wa historia toka mreno wa kitaifa na kuifanya iwe na mtazamo wa kilimwengu*. Ruwaza hii ya mabadiliko imepata msukumo mkubwa kutokana na kazi zilizoandikwa na wanahistoria wa kanda zote za dunia na hususa wanahistoria wa Afrika.

Tangu karne ya kumi na tisa na kuendelea, historia haikufikiwa kama taaluma ya kisayansi bali kama sehemu ya urithi wa taifa ambayo ilipaswa kuhusishwa ili kukuza hisia za kizalendo yaani, kwa ufupi, kuwa kama "chombo cha kufunza maadili na elimu ya siasa." Kwa mfano, mtu aliweza kupata shahada za juu kabisa katika vyuo vikuu vya Ufaransa na Uingereza bila kujifunza kwa undani historia ya nchi nyingine za Ulaya na bila kujua historia ya ulimwengu kwa jumla. Huko Amerika ya Kaskazini, msimamo wao ulikuwa kujifunza historia ya utamaduni ambao ulianza tangu enzi ya Wagiriki na hatimaye kusababisha ustaarabu wa Marekani. Mabara ambayo leo hii ni maskini hayakufikiwa kuwa

yalikuwa na kale inayostahili kusimuliwa. Ndiyo maana maandishi ya wanahistoria wote waliokataa mtazamo huu wa Kizungu na kujifunza historia halisi ya kila jamii, yalionekana kuwa ni hatua ya kimapinduzi. Wanahistoria wa Afrika wametoa mchango mkubwa kuendeleza historia ya namna hii hata ikiwa kwa sababu tu kuwa Afrika ilikuwa imedhalilishwa sana kwa nadharia za kibaguzi. Ubaguzi wa rangi ni baa linaloweza kuonekana kwa namna mbalimbali toka hali ya kufichwafichwa hadi hali ya ukatili kama vile ilivyokuwa wakati wa biashara ya watumwa na wakati wa Vita Vikuu vya Pili. Ubaguzi ni kama visukuku hai vilivyolala katika dhamira ya manilioni ya watu hadi vinapoamka katika unbo la imani na madai yasiyo na misingi ya kisayansi, kwa mfano, kusema kuwa kila kitu kizuri kuhusu Afrika kina asili ya kigeni kwa sababu Waafrika wenyewe hawakuvumbua kitu chochote. Mwelekeo huu ulienea sana hata ikawa kuwa suala muhimu lililokuwa likijadiliwa kuhusu sanamu maarufu za Ife ilikuwa ni kujua wageni gani walisafiri mbali kiasi hicho na kufika Ife ili kutengeneza kazi hizo za sanaa.

Kwa vile zamani watu hawakujua kusoma na kuandika, walizuiwa kushiriki katika kuleta maendeleo yao na ndiyo maana historia ya Afrika Kusini mwa Sahara ilitengwa inakusudi na historia ya Afrika Kaskazini mwa Sahara. Ilisahuliwa kuwa Waafrika walikuwa wanajua kusoma na kuandika tangu mwanzoni mwa Enzi za Kati na kuwa wakati huo walikuwapo waandishi na makarami kama Ulaya kwa sababu mawaliu na wafanyabiashara walikwisha eneza maandishi ya Kiarabu mpaka katikati ya misitu ya Afrika ya tropiki. Huko Ulaya na nchi nyinginezo watu wengi walianza kujua kusoma na kuandika baada ya Mapinduzi ya Tasia.

*Kikwazo cha pili* katika uandishi wa historia thabiti ni kuwa hata huko Ulaya umna ulikuwa haushirikishwi kwenye mambo ya taifa. Historia iliwahusu matabaka yaliyotawala na vitendo vya tu ndivyo vilichukuliwa na wanahistoria kwa ajili ya kurekodiwa kwa vizazi vya baadaye. Huko Ufaransa, karni ya kumi na saba, maisha yalikuwa ni matendo ya kila siku ya mfalme Louis wa kumi na nne na vita alivyopigana.

Historia ya uchumi haikushughulikia mali iliyozalishwa na watu na mahitaji ya watu hao au jinsi watu walivyolazimishwa kutumikia tabaka la mabwanyenye bali historia hiyo ilishughulikia uvumbuzi wa ufundi uliofanywa na wanasayansi na sheria zilizopitishwa na mawaziri kuhusu sera za maendeleo ya taifa.

*Kwa vile historia ilihodhiwa zaidi na Ulaya na wasomi wa kinagharibi, kale za schemu nyingi za dunia hazikuandikwa.* Wanahistoria walioanza kupanua upco wa historia ili ujumuishe makontinenti mengine na wengine walioipana ili kujumuisha vikundi mbalimbali vya jamii, wote walikuwa wakipambana kuendeleza kitu kimoja lakini walikuja kuungana baadaye sana.

Wataalamu wa Kiafrika walijikuta katika hali ya kutatanisha walipoanza kutumia hoja zote zilizokuwa upande wao katika harakati ya *kuikonboa historia ya Afrika*. Kwa mfano, walipodai kuwa Afrika ilikuwa na falme na hinaya kubwa zenye mifumo na utawala madhubuti kama hinaya za huko Ulaya, walisahau kuwa mifumo hiyo ya Ulaya ilikuwa imepatikana baada ya watu wengi kupoteza maisha yao. Lakini demokrasia katika vijiji vya Kiafrika iliyokitwa katika uhuru mkubwa wa mtu binafsi huenda iliwakilisha mafanikio bora zaidi. Kwa upande mwingine, wanahistoria wa Afrika walifuma lengo zaidi walipobadilisha mtazamo wa "historia ya kikoloni" kuwa watamalaki wa Kizungu walikuwa ni mashujaa wa ustaarabu.

Katika maandishi ya wanahistoria walioeleza ukombozi wa Afrika mtazamo ulibadilishwa kabisa na kulingana vizuri na ukweli: Mashujaa walikuwa ni wapigania uhuru

wa Kiafrika ilihali wataamalaki walikuwa viongozi wa majeshi ya uvamizi na magavana wa kikoloni ambao walikuwa na siasa ya kumpisha mwenye nguvu. Sera hii ilitumiwa kwa ukatili na wakati mwingine kwa kuniwaga damu. Hatua ya pili ilichukuliwa wakati waandishi wengi walipoanza kutilia mkazo harakati za kukataa na kupinga ukoloni ambazo katika kilele cha kipindi cha ukoloni zilirahisisha uundaji wa vyama vya ukonbozi.

Polepole wanahistoria wenye mtazamo halisi wa Kiafrika waliungana na harakati ya kuwa na *historia kamili ya jamii*, inosi kwa kutumia mtazamo wa taaluma fungamano iliyojumisha historia za kilimo, uundaji miji na mahusiano ya kijamii na ya kiuchumi na pili kutokana na maendeleo yaliyopatikana katika historia iliyotokana na utafiti wa uwandani. Utafiti huu wa uwandani uliwavusha watafiti kutoka athari za nyaraka ambazo aghalabu hazikuamitika na zenye kasoro za msingi kwa sababu ya kashfa za waandishi wa nyaraka hizo tangu zama za biashara ya watunwa mpaka mwisho wa enzi ya ukoloni. Masimulizi ya mdomo moja kwa moja kutoka kwa Waafrika walioonewa na wakoloni yametoa ushahidi kinyume na ule uliomo katika nyaraka rasmi. Zaidi ya hayo, njia zilizobuniwa ili kutumia mapokco-simulizi zimewafanya wanahistoria wa Afrika wawe watu wa kwanza kuwa na taaluma liyo na wametoa mchango mkubwa kueleleza.

Kati ya mwaka 1890 na 1914, wasomi-watawala wa kikoloni alikwishaanza kukusanya mapokco ya Waafrika. Hata hivyo, mpaka mwaka 1959, G.P. Murdock akifuata mtindo ulcule wa waamili wa Kiingereza alidai waziwazi kuwa mapokco simulizi ya wa Afrika hayawezi kutegemwa hata kidogo. Miaka michache iliyofuata, kilichapishwa kitabu cha Jan Vansina kuhusu mapokco-simulizi kitiwacho *Oral Tradition: A study in Historical Methodology* (1961) ambamo mwandishi pamoja na wanahistoria wa Kiafrika na wengine wasio wa Kiafrika walionyeshwa ukubalifu wa mapokco-simulizi kama chanzo cha kihistoria mradi tu yawe yamehakikiwa vizuri. Mikutano ya wanahistoria iliyofanyika Dakar mwaka 1961 na Dar es Salaam mwaka 1965 ilitilia mkazo msimamo huu na kusisitiza umuhimu wa jimu na akilojia.

Shughuli zote hizi zilisaidia kufungua njia mpya ya historia na *kukuza sayansi nyingine za jamii*. Hata hivyo, kimsingi kilichojitokeza ni kwamba Afrika ya "asili" haiukuwa imekaa bila mabadiliko. Ama kwa hakika, wanauchumi, wanauchinu siasa na wanauchinu jamii walikuwa wamezoca kugawa mambo ya kale ya Afrika katika vipindi viwili: "kabla ya " na "baada ya" ilitumika kueleza mambo ya Afrika ya kale na "baada ya" ilitumika kueleza mambo yote yaliyotokoa tangu enzi ya maambao ambayo inasemekana iliainsha ulimwengu ambao ulikuwa bado umelala.

Ni wananthropolojia wasemaio Kiingereza ndio waliokerwa na ugunduzi kwamba kulikuwa na nguvu za mabadiliko katika jamii ya zamani ya Afrika. Kama waamili, wananthropolojia hawa waliangalia miundo ya jamii hiyo na kutenganisha vikundi mbalimbali vilivyokuwa na dhina mahsusii katika hali asilia ya jamii; na mbinu wahyotumia ilihitaji uchanganuzi wa wakati halisi uliopo na kuchuja kila kitu kilichoongezwa tangu kufika kwa wazungu ili kupata "ruwaza" ya kienyeji katika hali ya asili kwenye aina fulani ya "usasa wa kianthropolojia" usio kikomo. Ni kweli kuwa mtazamo huu ambao ulitawaliwa na maandishi ya Bronislaw Malinowski ulisaidia kuona kwa undani zaidi jinsi jamii za Kiafrika zilivyokuwa zikiendesha mambo yake. Lakini kupendelea huku Afrika ambayo ilidhaniwa kuwa na kikomo cha "ushenzi" na papo hapo kuwa imesunama katika makumbusho ya usasa wa kienthropolojia kuliwanyima Waafrika kitu mhimu walichokuwa nacho -yaani maendeleo yao ya kihistoria. Hivyo uchunguzi wa historia uliathiri kiyakinifu uamili kwa kukumbusha kuwa maana ya wakati uliopo ni kuwa wakati huo si wa kudumu.

Athari zake juu ya *Mitalaa ya kidini* pia zilikuwa na manufaa. Mwanzoni, waandishi walishughulikia zaidi dini ambazo athari za Kizungu zilielekea kuziondosha. Msimamo huu uliodumu kwa muda mrefu unaweza kufuatiwa nyuma hadi nyakati za Vita vya Msalaba. Kilichowavutia sana wanazuoni wa Uislamu hakikuwa maendeleo ya ndani ya dini hiyo bali siri ya mabadiliko yake na mwelekeo wa viongozi wake na madhehebu zake kwa mtawala wa kikoloni.

Kinyume chake katika miongo ya karibuni, uchunguzi unekuwa ukifanyika kuhusu dini unganishi na za kimasikhi za Kiafrika ambazo kwa kiasi fulani zimechepuka kutoka Ukristo na kuhusu athari zao juu ya harakati za kupinga ukoloni. Siku hizi waandishi wanashughulikia zaidi mabadiliko yanayotokea katika dini ya Kiislamu na dini za jadi ambazo imani yake ilikuwa haijafanyiwa uchunguzi ingawa vyama vya siri.

Katika *historia ya uchumi*, kitu vilivyokuwa vikiamini dini hizo vilikuwa mstari wa mbele katika kuleta maendeleo ya jamii mbalimbali cha kushangaza katika uchunguzi uliofanyika ni ukaidi wanaoonyesha waandishi katika kufikiria kuwa uchumi wa Kiafrika ulikuwa umegawanyika na usiobadilika na kwamba athari zilitokana tu na "mamboleo." Misingi ya uchunguzi huo inatokana tu na nadharia za ukuaji wa uchumi zilizofanuliwa wa W.W. Rostow. Katika nadharia hizo inaliyosiliza zisizotumika kikamilifu na misingi ya uzalishaji haina budi ikombolewe la sivo jamii zenye uchumi wa kijungumcko ndizo zinaweza kuishi. Dhana hii hupingana kabisa na hakika za kihistoria. Tangu zamani za kale, Waafrika wameungana pamoja kwa ruwaza changamano na za kukamilishana za uzalishaji na uuzaji nje wa bidhaa kama vile chumvi, ngo'mbe, samaki waliokaushwa, kola, madini na metali ambazo zilihusika katika kudumisha biashara baina ya ikolojia na uchumi mbalimbali. Kipengee cha kihistoria cha uchumi kitaongeza uwezo wa taaluma hii katika kuelewa uhalisi wa hali ya Afrika; kwa mfano, mkazo uliowekwa na wanahistoria juu ya umubimu wa biashara katika Afrika kabla ya ukoloni unesaidia kuendeleza nadharia za wana elimu-jamii na wanauchumi.

Sababu moja iliyofanya historia ya Afrika iseleo katika nchi za Magharibi, kulingana na historia ya makontinenti mengine, ni ukosefu wa wataalamu wa kihistoria ambao wangeweza kuwasilawishi wasomi wenzao. Vitabu vya historia viliandikwa na watawala wa kikoloni, wamisionari na Waafrika fulani viongozi wa dini au waandishi kama vile Shaykh Musa Kanara wa Senegal na utafiti mdogo ulifanyika katika taasisi za nchi za Scandinavia na Ulaya ya Mashariki na Kati lakini utafiti huo haukutosha kuinua hadhi ya historia ya Afrika. Mpaka mwaka 1950, hakuna Chuo Kikuu kilichokuwa na mitaala ya masomo ya historia ya Afrika kwenye kiwango cha uzamili na hakuna inhadhiri yeyote wa Chuo Kikuu ambaye alikuwa anashughulikia historia ya Afrika tu. Hata hivyo, miaka ishirini baadaye, kulikuwa na wanahistoria 500 waliokuwa wamehitimu shahada za falsafa katika historia ya Afrika. Maendeleo haya yalitokea kwa sababu ya hali nzuri zaidi ya kisiasa na kitaaluma ya wakati huo.

*Katika Afrika*, harakati za ukombozi zilizoanza mwaka 1940 zilisaidia sana kuendeleza mitaala hii hususa baada ya kufunguliwa vyuo vikuu vipya tangu mwaka 1950 na kuendelea. Nchi zilizokuwa zinatumia lugha ya Kifaransa na ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zimefungamana na infumo wa elimu wa Ufaransa zilibaki nyuma kidogo katika kukuza mtazamo huu mpya baadaye nazo zilipiga hatua lakini kubwa mbele hasa baada ya majadiliano ya mikutano mikuu miwili ya waandishi na wasanii weusi iliyofanyika Paris na Roma miaka 1956 na 1959.

Maendeleo makubwa yaliyofanyika Afrika wenyewe yalikuja wakati ulcule na maendeleo

ya uchunguzi wa historia ambao mara nyingine ulikuwa ukifanyika kwa miaka mingi katika vituo mbalimbali kwenye makontinenti mengine kama vile *School of Oriental Studies* katika Chuo Kikuu cha London, na *Ethnographic Institute* cha Leningrad ambayo ilichapisha marejio yote yaliyojulikana yaliyohusu Afrika kusini mwa Sahara tangu kame ya kuni na moja na kuendelea. Katika Chuo Kikuu cha Sorbonne, huko Paris, nafasi za kwanza za uprofesa katika historia ya Afrika zilianzishwa. Pia chuo kingine cha Ufaransa kitiwacho *Ecole Pratique des Hautes Etudes* kilishughulikia sana historia ya Afrika. Hata hivyo, katika Brazili na Carribean mitaala hii ilichelewa kuanzishwa jipokuwa kulikuwa na kazi zilizokwishaandikwa na Price-Mars wa Haiti na Nicolas Guillan wa Cuba.

Kabla ya mwaka 1960, vyuo vya Marekani havikuyapa umuhimu masomo ya historia ya Afrika na vyuo vichache vilivyofundisha historia ya Afrika vilizingatia zaidi Afrika ya Kaskazini hasa enzi za kale za wakati wa Wayunani na Wagiriki na vipindi vya ukoloni. Miongoni mwa Wamarekani weusi kikundi kilichoongozwa na W.E.B. Dubois kilijadili Afrika. Kabla ya hapo, Carter G. Woodson alikuwa ameanzisha *Journal of Negro History*, mwaka 1916 na W.L. Hansbury wa Chuo Kikuu cha Howard alikuwa amcendesha kampeni kali ya kuanzisha masomo ya historia ya Afrika katika vyuo vikuu vya Marekani.

Kupatikana kwa uhuru kwa nchi kadhaa za Afrika ya Kaskazini na Ghana kabla ya mwaka 1960, hakukubadilisha hali ya mambo mara moja. Huko kusini mwa Afrika, hali ilikuwa mbaya zaidi kwa vile katika Afrika Kusini historia bado ilikuwa na maana ya historia ya Ulaya na ya wazungu wachache waliokuwa Afrika. Huko Zimbabwe mnamo mwanzoni mwa miaka 1960 kulikuwa na jaribio fupi la kuingiza historia ya Afrika katika mitaala ya kihistoria lakini walowezi wachache walipojitangazia uhuru wa bandia mtindo huu uligeuzwa ghafla.

Katika Afrika ya tropiki nchi zilizokuwa zinatumia lugha ya Kiingereza ndizo zilikuwa za kwanza kujaribu kuleta urari mpya kati ya historia ya Afrika na ya ulimwengu, kwa kuunganisha historia ya Uingereza na ile ya Ulaya na knzingatia nchi za Kiislamu. Amerika ya Kusini na Asia, na kwa kufanya hivyo walidhihirisha kuwa kujifunza historia ya Afrika hakumaanishi kuacha historia ya nchi nyingine.

Katika nchi zilizokuwa zinatumia lugha ya Kifaransa, ni tangu mwaka 1970 tu na kuendelea ndipo idadi ya walimu wa historia Waafrika ilianza kuwa kubwa. Hata hivyo, mapema tangu mwaka 1963, mitaala iliyobadilishwa ya historia ilianza kutumika katika shule za Sekondari, na hii ilifuatiwa mara moja na utengenezaji upya wa mafunzo ya historia katika vyuo vikuu kulingana na mapendekezo ya mpango wa CAMES (Baraza la Afrika na Malagasy kuhusu masomo ya juu).

Zaidi ya hayo, tangu karibu mwaka 1955, vitu viwili vilisaidia kuendeleza mafunzo ya historia ya Afrika huko Ufaransa na Uingereza. Kitu cha kwanza kilikuwa ni kurejeshwa nyumbani kwa watawala wa kikoloni ambao baadhi yao walifanya uchunguzi mkubwa wa uwandani; na kitu cha pili ni hatua ya Afrikanaizesheni ya waalimu ambayo iliwapa fursa wachunguzi wengi wazungu kurudi Ulaya na kushika nafasi za uhadhiri na hata uprofesa katika vyuo vikuu. Kwa hiyo historia ya Afrika ilipewa nafasi maalumu katika vyuo vikuu vya Bordeaux, Aix, Lyon na hasa Paris kwenye kituo cha masomo ya Afrika kitiwacho *Centre d'Etudes Africaines* na pia huko kwenye *School of Oriental and African Studies*, London na katika vyuo vya Birmingham, Sussex na Edinburgh.


Huko Ulaya ya Mashariki, ufundishaji wa historia ya Afrika ulipiga hatua kubwa sana mbele. Hususan, wanaakiolojia kutoka Czechoslovakia na Poland, ambao waliwahi kufanya kazi Guinea, na huko Urusi ambao historia ya Afrika imcfundishwa vizuri kwa mfululizo



katika Chuo Kikuu cha Patrice Lumumba.

Huko Marekani, historia ya Afrika ilipiga hatua kubwa mbele kati ya mwaka 1960 na 1970. Mnamo mwaka 1960, muda mfupi baada ya kuanzishwa kwake chama cha *African Studies Association*, kilikuwa na wanachama wanahistoria 21 tu ambao walikuwa wakazi wa Marekani na Canada. Mnamo mwaka 1962, kwenye mkutano mkuu wa kwanza wa kimataifa wa wataalamu wa mambo ya Afrika uliofanyika Accra, Rais Kwame Nkrumah aliwahutubia washiriki wapatao 800 kwenye hotuba ya ufunguzi ambapo alidokezea majukumu ya mitaala ya historia katika Afrika mpya. Miaka michache baadaye, hapo mwaka 1970, wataalamu wa historia au akiolojia ya Afrika huko Marekani walikuwa wamefikia 350 hivi. Mielekeo miwili iliyokinzana ilisaidia katika kuleta maendeleo hayo. Mwelekeo wa kwanza ulikuwa imani madhubuti ya Wamarekani weusi kuwa historia ya Afrika ni urithi wa Waafrika wote ikiwa ni pamoja na vizazi popote pale walipo. Mwelekeo wa pili ulikuwa liamu ya kuunganisha mambo ya Afrika ambayo hayakutambulika kwa muda mrefu katika historia ya ulimwengu kwa jumla. Hivyo Afrika ikawa eneo kubwa la kitamaduni kama vile Asia ya Kusini au Asia ya Mashariki na idara nyingi za historia ziliongeza sehemu ya historia ya ulimwengu wa tatu kwenye sehemu zilizokuwapo za historia za Marekani na Ulaya.

Siku hizi historia ya ulimwengu haimaanishi tena historia ya ustaarabu wa Magharibi. Katika mpango wa muda mrefu, mafaukio ya maendeleo hayo yatategemea ubora wa kazi zitakazofanywa na wanahistoria Waafrika na wanahistoria wengine wa Afrika na upanuzi wa sayansi nyinginezo za jamii ili ziveze kuzingatia ipasavyo matokeo ya uchunguzi katika Afrika kabla ya kutoa maoni ya jumla kuhusu jamii za binadamu.



## *Marejeo na mbinu maalum zilizotumiwa katika historia ya Afrika*

Akili ya kushughulikia historia aliyonayo binadamu pekee yake bila kujali asili yake, hufanya kazi kwa kuzingatia uhakiki wa kihistoria ambao kimsingi ni mbinu ya kuzishughulikia hati. Hata hivyo ni lazima kwanza vyanzo vidhihirike. Kwa upande wa Afrika kuwepo kwa vyanzo vya namna hiyo lilikuwa jambo lenye ubishi mwingi. Lakini siku hizi vyanzo hivi hupatikana kwa wingi katika kila uwanja, iwe ni jiolojia, paleontolojia (climu ya maisha hapo kale), paleobotania (climu ya mimea hapo kale), utumiaji wa kitoo nguvu ili kupata data halisi za kikronolojia, jiografia ya maumbile, uchanganuzi wa kisosiolojia, mapokeo simulizi, isimu linganishi, hati za kimaandishi, uchumi, taaluma zinazohusu idadi ya watu, n.k. Orodha hii inazidi kuongezeka kila wakati lakini jambo jipya zuri kwa 'sasa ni yale matumizi ya vyanzo vyote hivi kwa pamoja na ambavyo kimoja kinathibitisha chenziye. Hii huwakilisha hatua zaidi ya mchango wa kiufundi tu wa mbinu za kihistoria kwa jumla. Ni namna ya nadharia mpya ya sayansi ya historia ambayo inawahitajia wanahistoria kuwa na msingi wa taaluma fungamano na kufanya kazi kwa kushirikiana na wanazuoni wa nyanja nyingine.

Kundi la kwanza kati ya wanazuoni hao ni la *wanafizikia*, kutokana na matumizi ya isotopi za kitoo nguvu kwa kuchukulia vipimo ambavyo hukatiza ubishi kuhusu umri wa mabaki ya binadamu yanayotambulishwa na akiolojia na paleontolojia<sup>1</sup>.

Watafiti wa *sayansi za dunia* pia wanatoa mchango mkubwa bila kutegeinca hati za kimaandishi. Kwa mfano Jiografia ya maumbile hutoa habari kuhusu ruwaza za maendeleo ya mwanadamu. Hii inajidhihirisha katika Chad ambako sura ya nchi ni kama ifuatavyo: chini kabisa kuna tambarare ya kati ambayo imetokana na kutuama kwa matope, na juu kabisa kuna nyanda za juu zenye mwinuko wa kadri. Kati ya hizi sehemu mbili kuna miteremko ambayo imelika kwa nimomonyoko wa udongo. Lakini miteremko hiyo ina idadi kubwa ya watu kuliko zile tambarare zinazoathiriwa na mafuriko, nazo sehemu za tambarare lukimu watu wengi zaidi kuliko nyanda za juu zilizomomonyoka. Latitudo pia ilikuwa na mchango kwani idadi ya wingi wa watu hupungua kwa kadri mtu anavyozidi kwenda kaskazini kuelekea katika sehemu ya kusini ambako maziwa na mito hunywesha ardhi. Kwa hiyo, kazi za binadamu hupangwa na mahitajio ya maumbile ya mazingira na historia pia imelazimika kufuata utaratibu huu wa maambo uliokuwepo tangu awali. Zaidi ya hayo, sehemu zenye nyanda za chini au za kati mara nyingi zililingiliwa na kutekwa na washambuliaji ambao waliwafukuza wazawa wa sehemu hizo wakakumbilia katika nyanda za

<sup>1</sup> Tazama Sura 9 juu ya suala hili.

juu sizizo na rutuba. Kwa mfano, Wafulani waliwafukuza Wabumi ambao walilazimika kukimbilia katika sehemu kame za Adamawa na pia wakawafanya Wakiroi wa Cameroon ya kaskazmi wabakie katika sehemu zenye ardhi ya changarawe za kale kwenye milina ya Madara. Pamoja na hivyo watu hawa ambao waliondoshwa kwenye ardhi zao, polepole walijifunza kujizoesha na mazingira ya ardhi mbaya walikolazimika kuishi papohapo wataamalaki pia walilazimika kukumbana na mbu pamoja na vurumai zilizoletwa na malaria na malale katika sehemu zenye unyevu walizoziteka. Mfano huu unaonyesha kwamba maelezo ya kijografia peke yake hayawezi kueleza kila kitu. Sayansi zote za dunia na za maisha shurti vitumiwe ndipo ruwaza halisi iweze kuelezwa vilivyo.

Kuhusu nyakati za kale kabisa ambako hatuwezi kamwe kupata vyanzo vya hati na ambako pia hakuna mapokeo simulizi yake wala data za kiantropolojia mbinu za akiolojia na paleobotania ndizo zinajitokeza. Chavua katika udongo maalumu huweza kutenganishwa kwa kuyeyusha sampuli ya udongo katika asidi ambayo huoneoa mboji, silika na chokaa lakini ikaacha chavua ikiwa nzima. Chavua hizi hupakazwa kwenye jelatini na kuhesabiwa ili kupata wingi wake katika udongo. Kutokana na wingi na aina ya chavua zenyewe, inawezekana kukadiria ni aina gani ya mimea iliota katika eneo hilo. Pia kwa kuchunguza tabaka za udongo tunaweza kuunda upya maendeleo ya maisha ya mimea au uzalishaji wa kilimo uliotokana na binadamu au tabia ya hali ya nchi. Uchunguzi kama huu umewezesha kufuatia nyuma historia ya upandaji wa mimea katika Afrika na kuanzishwa au kutumiwa kwake<sup>2</sup>

Masalia ya mbwa, nguruwe, kondoo na mbuzi pia yatupa mwanga kuhusu mwanzo wa ufugaji wa wanyama hawa. Matumizi ya farasi, ambayo yanaweza kuchukuliwa kuwa mojawapo ya "nguvu za msukumo" katika historia yamerkodiwa Misri wakati wa uvamizi wa Waliikso (yapata miaka 1600 kabla ya Kristo). Farasi walitumika huko Libya na Unubi katika miaka ya mwanazomwanzo ya elfia ya kwanza kablaya Kristo, lakini walifika Kusini mwa Sahara katika "Enzi za Kati"; na hata wakati huu walitumiwa zaidi katika baraza za kifalme tu - kama ilivyohibitishwa katika maelezo ya Ibn Battuta juu ya baraza la Mfalme wa Mali.

Ngamia, ambao wanaonekana katika michoro iliyo kwenye miamba huko Sahara ya Chad ambayo yamekama ni ya tangu kama tatu kabla ya Kristo, walianza kufugwa Misri ambako walitumiwa katika mawasiliano na Bahari ya Sham. Yawezekana makundi ya askari wa Kirumi waliwapelca Maghrib, ambako walitumiwa na Waberiberi ambao pia walihamia kusini kukimbia utawala wa Kirumi. Kutokana na hali hiyo idadi kubwa ya watu weusi katika oasisi za Sahara walifanywa watunwa au kusukumwa kusini zaidi.

Kwa hiyo, kwa mwanahistoria ushuhuda wa namna yoyote ile, bila kujali unatokana na sayansi gani, unaweza kuwa wenye manufaa sana; hakuna tofauti baina ya savansi za msingi na sayansi saidizi. Hata hivyo, ingawa historia ina deni kubwa kwa sayansi za ardhi na sayansi maisha bado kuna mchango nikubwa ambao umefanywa na *sayansi za binadamu na jamii* kama vile taaluma za Misri, isinu, mapokeo simulizi, uchumi na sayansi ya siasa.

Taaluma za Misri ni chanzo ambacho mpaka sasa hakijatumwa vizuri. Taaluma hii huumia akiolojia ya kihistoria na kufasiri matini mbalimbali kwa kuimudu vizuri lugha ya Kimisri ambayo imerithishwa kwetu katika maumbo matatu tofauti. Umbo la kwanza ni la maandishi. Haya yana alama ambazo zinagawanyika katika makundi mawili; alama-neno (uchoraji wa kikapu kuwakilisha neno 'kikapu' ambamo vipengele muhimu vya kifonetiki ni

2 Tazama Sura 27 juu ya suala hili.

*nb*); na alamasauti (uchoraji wa kikapu hubakia tu na thamani ya kifonetiki *nb* na huweza kutuniwa katika maneno mengine ambayo yana thamani hiyohiyo kama vile homonimu *nb* yenye kumaanisha "mwinyi" na *nb* yenye maana ya "wote". Umbo la pili ni lile lijulikanao kama maandishi-msonge; ni nainna ya maandishi-picha ya kuunganishwa, mtindo ambao ulitokea karibu katika ufalme wa tatu (yapata 2278-2423 kabla ya Kristo). Huandikwa toka kulia kwenda kushoto na ulikuwa ukiandikwa kwa kutumia kalamu ya tete kwenye karatasi ya mafunjo au kwenye vyungu. Maandishi ya watu wa kawaida, ambayo ni maandishi msonge yaliyorahisishwa sana, yalijitokeza katika ufalme wa ishirini na tano (yapata 751-656 kabla ya Kristo) na yalitoweka katika karne ya tano. Maandishi haya yanahusiana na maandishi ya Kimeroc ambayo mpaka sasa hayajaweza kufasiriwa.

Kuanza kusoma habari fulani iliyoandikwa ni kama kuanza safari ya kuelekea katika ulimwengu wa kiakili na wa kihisia wa watu. Katika safari hiyo wanahistoria na wanaisinu wanaweza kujifunza na kuelewa inambo kutokana na mifano ambayo inakaribia wakati wa leo kwani maandishi ya Kimisri yalisambaa hadi maceo ya Afrika ya watu wengi. Maandishi picha ya *Kigicandi* yanayotumiwa na Wakikuyu nchini Kenya yanafanana sana na maandishi-picha ya Misri. Kadhalika na maandishi-picha ya Nsibidi yanayotumiwa na Waefik wa Nigeria ya Kusini na alama zinazotumiwa katika maandishi ya Kinende Kusini mwa Sierra Leone na Kilima Kaskazini mwa Liberia. Ingawa kwa hakika hakuna uhusiano wa karibu sana lakini yawezekana kufanya mfananisho kati ya mitindo ya Kimisri na maandishi-picha ya Kidogon, Kibambara na Kibozo na maandishi ya Bamum wa Cameroon.

Muhimu zaidi ni wazo la jinsi nguvu ya maandishi ilivyojitokeza juu ya maisha ya watu na viumbe wengine waliopatikana Misri na Kusini zaidi ya Afrika. Kwa hiyo kuna kipindi wakati ambacho kinarejea nyuma hadi wakati wa Mafarao, kipindi ambamo ruwaza fulani za ustaarabu zilicindeleza pasipo kukatizwa kabisa.

Maarifa ya maandishi ya Kimisri hutupa anali kubwa ya maandishi ambayo mpaka sasa bado ni ya kuvutia sana kwa Waafrika wa leo, ikiwa ni pamoja na mawe yaliyotunika wakati wa maziko, maandishi ya nakshi kwenye makaburi, hati za shughuli za utawala, nyimbo za kumsifu Mungu, kazi mbalimbali za falsafa, maandiko ya kitabibu na ya kihusabati, na maandishi ya fasihi (riwaya na hadithi za masimulizi). Mfano mmojawapo ni ile barua ambayo Farao Nefertiti-Ka-Re (Pepi II) alimwandikia Herkhuf mnamo 2370 kabla ya enzi ya Ukristo, kiongozi wa msafara wa safari ya kibiashara katika Nchi iliyo kwenye ukingo wa Dunia (*Land on the Edge of the World*) schemu ambayo yasemekana kuwa pengine ilikuwa ni eneo la maziwa ya Afrika. Katika safari ya nne, kati ya msururu wa safari hizo za kibiashara, Farao alitewa mbilikimo. Matini nyingine ya Kimisri, ijulikanao kama *The Tale of the Castaway* ambayo ni ya karne ya ishirini kabla ya kipindi chetu, inatoa maelezo kamilifu juu ya maisha ya mabaharia na uhusiano wa kiuchumi kati ya bonde la Naili na Bahari ya Shari. Malkia Hatshepsut (1504-1483 kabla ya enzi ya Ukristo) alitayarisha safari za kibiashara kwenda katika nchi ya Punt, ambayo leo inaitwa Somalia. Maelezo haya yamepatikana katika sanamu mufti za kuchora katika Deir-el-Bahri, Misri ya juu.

Kuanzishwa kwa sono la Kimisri cha kale katika vyo vikiu kungeweza kuifikia tena mojawapo ya sura muhimu sana katika urithi wa Mwaafrika. Ama kwa hakika ripoti ya mwisho ya kongamano la Kinataifa juu ya Kutamakani kwa watu katika Misri ya Kale na Ufasiri wa Maandishi ya Kimeroc, (*The Peopling of Ancient Egypt and the Deciphering of the Meroitic Script*) mnamo mwaka 1974 inaeleza wazi juu ya jambo hili, inaposema: "Lugha ya Kimisri haiwezi kutengwa na muktadha wake wa Kiafrika na asili yake haiwezi kuelezwa

kikamilifu kwa kutumia mbinu na mtazamo wa Kisemiti: Hivyo halikuwa jambo la kushangaza kukuta lugha zenye kuhusiana katika Afrika."

Kwa hiyo haifai kukiainisha Kinisri cha Kale katika kundi la lugha ya "Kihamiti-Kisemiti" au "Kiafrika-Kiasia", kama ambavyo baadhi ya waandishi wamewahi kufanya. Lengo la uchanganuzi wa kijenetiki katika lugha hauna budi kutoa ufafanuzi wa Kisayansi wa uhusiano wa lugha ambao hii leo unahisiwa tu pasipokuonyesha ithubati yoyote. Hii hatimaye itawezesha kutambua vipengee vya kimuundo ambavyo vinapatikana katika Misri ya Mafarao na sehemu nyinginezo za Afrika. Hii ndiyo kazi inayowangoja wanahistoria na wanaisimu.

*Isimu*, hasa kama mbimu ya ulinganishaji itatumwiwa, husaidia sana taaluma ya historia kwani hutupa sababu za kurejea nyuma kabla ya lugha zilizopo hii leo ili kueleza "lalaja moja ya lugha" ambayo, japokuwa luenda siyo mama halisi wa lugha zote, huwezesha kuona wakati ambao lugha ambazo leo hii hazifanani zilikuwa na uhusiano. Kazi hii ya ulinganishaji imekwishafanywa kwa lugha za Kilundi-Kizungu na pia kwa lugha za "Mame-Bantu: Tatizo moja muhimu ndani ya suala hili ni lile la uhamaji, Tatizo haliko katika kuchunguza jinsi mataifa mbalimbali yalivyohamama, (kwani lugha ni jambo linalohusu mila halihusu mbarikuu) bali liko katika kung'amua mabadiliko yatokanayo na kuhamama mazingira kwa lugha. Kwa mfano, kutokana na lugha za kundi la Niger-Kongo tunaweza kuhitimisha kwamba kulikuwa na uhusiano wa kitamaduni-kijamii baina ya watu wote walioishi baina ya Atlantiki, kwa upande wa Magharibi, na bahari ya Hindi, kwa upande wa Mashariki, na kuelekea kusini hadi nchi ya Afrika Kusini.

*Mapokeo simulizi* pia yana manufaa makubwa kwa historia, hasa inapokuwa ndicho chanzo pekee ambacho kinapatikana kwa urahisi kama ilivyo kwa Wambochi wa Kongo na temi zao. Kutokana na waandishi taribi wa Kizungu tunapata habari kwamba wafahne wa Loango, huko Angola, walikuwa wakizikwa katika schemu mbili za makaburi, moja huko Lubu na nyingine huko Lwandjili, lakini hatuelezwi kwa nini. Lakini mapokeo simulizi ya Wavili hutueleza kuwa kuhamishwa kwa maziko toka eneo moja hadi jingine kulitokea baada ya kujiri mgongano mkubwa baina ya kitala cha mfahne na wakazi wa Lwandjili; na kwamba ilipotokea hivyo maziko yalihamishiwa Lubu. Katika hali kama hii mapokeo simulizi hutoa maelezo yaliyokosekana katika vyanzo vya kimaandishi. Halikahalika, katika shughuli za machimbo yao waliyofanya katika Tegdaoust, J. Devisse and D. na S. Robert walitumia maelezo kutoka tarihi za zamani za Kiarabu, lakini pia walitumia maelezo ya mapokeo simulizi ya kawaida ya sehemu hiyo.

Kwa kawaida, mayeli wa Kiafrika hawatungi mashairi yao kwa mfululizo mmoja uliokitwa kwenye kipimo cha kikronolojia bali hujenga tu maumbo ambamo nyakati au enzi mbalimbali huelezwa kwa namna isiyonyesha uhusiano wowote kana kwamba ni matukio yasiyo na kikomo. Jambo muhimu ni ile maana ya dluina za nguli mbalimbali katika utaratibu maalumu wa itikadi za watu. Historia hii ambayo kwa namna fulani ni haishi yaweza kusemwa mi historia ya kimuundo.

Mchango wa *sosiolojia* na *sayansi yaa siasa* pia hauna budi kutiliwa maanani. Kwa mfano, tunaweza kuuliza kama dhana ya ufahne, taifa, dola, miliki, demokrasia, chama cha kisiasa, n.k. zinaweza pia kutumika moja kwa moja katika muktadha wa bara la Afrika. Jibu ni hapana. Kwa mfano, tujiulize nini inaana ya "Ufalme" wa Kongo. Wananchi wenyewe hutumia maneno *nsi a Kongo*, ikiwa na inaana ya "nchi ya Wakongo". Mipaka inabadilika kwa kadri koo zinavyozidi kujongea. Hata hivyo katika kipindi hicho cha wakati, umoja wa kimbari, yaani kuwa na ruwaza za aina moja za kisumu na kitamaduni, ni muhimu. Mfahne

ndiye *mfumu* (mkuu au mjomba) wa kila familia (*nzo*) na kila ukoo unaorithi kukeni (*makanda*) wote wakiwa na nasaba moja ya mababu wa kale (*bankulu mpangu*). Ndiyo kusema mfalme ndiye mwenye madaraka ya mwisho (*utinu*) katika mfumo mzima wa koo. Ufalme wake ni sawa na dola ya Kimagharibi ambao ni mfano.

Kwa upande mwingine falme ya Danxome, katika nchi ambayo hii leo yajulikana kama Benin unaweza kulinganishwa na utaratibu wa ufalme wa Kimagharibi. Kama Maurice Glele anavyoonyesha katika ufalme huu kulikuwa na kiini cha kudumu ambacho kilikuwa ndio nguvu ya utawala chenye muundo wa mfalme, mawaziri wake na wajumbe walioteuliwa na mawaziri. Mfalme alikuwa na mamiaka ya mwisho juu ya uhai au mauti ya watu wake (*anato*, wawakilishi wa watu) ambao kutokana nao aliwachagua *gles* (wakulima), ambao walifanya kazi ya kulima katika ardhi yake, kwani mali yote (*dokunno*) ilikuwa ya mfalme. Madaraka haya yalitekelezwa kupitia kwa machifu wa sehemu mbalimbali waliokuwa chini ya himaya yake. Kidogokidogo Wafoni, Wamahi, waalda, Wasavi, Wajuda, n.k. waliingizwa katika utaratibu huo wa utawala, jeshi na uchumi kutokana na utamalaki. Lakini hata katika utaratibu huu wa kiuchumi unaoendelea na uliodhibitiwa, bado watu wa kawaida nao walikuwa na mchango wao kwa kupitia mabaraza na temi zao.

Kwa hiyo kulikuwa na tofauti ya muundo baina ya taifa linalotawaliwa na mfalme au malkia la Danxome na Ufalme wa Kongo, katika karne ya kumi na tisa. Katika taifa la Danxome uchifu ulitumika kama njia ya kugawa madaraka tu ambavyo katika ufalme wa Kongo uchifu ndio uliokuwa mfumo wenyewe wa madaraka.

Tukichukua neno "ukabaila" tutakuta kwamba bado kuna utata. Kwa wataalamu wa kipindi cha kuanzia 1100-1500 (baada ya Kristo) ambao wana mwclekeo wa kisheria, mfumo wa kikabaila umekitwa kwenye msingi wa *fief*, yaani kuishi kwenye ardhi iliyoilikiwa na mwinyi, kumheshimu na kumnyenyekea luyo mwinyi na kumpa sehemu ya mavuno yanayopatikana kutoka kwenye ardhi hiyo. Kwa upande mwingine wafuasi wa Marx wanauchukulia ukabaila kuwa njia ya uzalishaji mali iliyo baina ya utumwa na ubepari. Ndiyo kusema, kwao ukabaila ni uhusiano wa uzalishaji mali ambapo tabaka la kikabaila linatawala tabaka la kitumwa ambalo maisha yake yanategemea ardhi ya makabaila.

Hata hivyo swali la kujiuliza ni kama dhana hizi zinaweza kutumiwa kwa jamii za Ki-Afrika kabla ya ukoloni. Jibu lake linaweza kupatikana tu kutokana na utafiti wa mitaala linganishi ya jamii. Namna ya utaratibu wa "kikabaila" ya Wabariba (Jamhuri ya Benin) kimsingi imeonyeshwa kama nadharia tete. Dhana ya kutoa sehemu ya ardhi, *fief*, ili itumiwe na wale wasio na ardhi lakini wamnufaishe mwenye ardhi haielekei ilikuwako katika Afrika kama ilivyokuwa huko Ulaya. Ni mfumo wa kisiasa tu ulioegemezwa kwenye uhusiano maalumu wa uchumi wa kijamii unaooweza kuasiirika aina fulani ya utaratibu wa kikabaila.

Kwa ufupi, kuvitunika vyanzo mbalimbali hutuwzesha kugundua njia mpya ya kuandika historia kwa kutumia mbinu ambayo haikujitokeza waziwazi. Mtazamo huu uliwezesha kuonyesha kwamba ulingo wa Mdaga katika Chad ulitumiwa pasi na kuingiliwa kwa muda wa zaidi ya miaka elfu mbili kuanzia karne ya kumi na tisa na uliwadhahirisha watu maarufu wa Sao katika historia halisi.

---



# 5

## *Marejeo ya kimaandishi kabla ya karne ya kumi na tano*

Kama tukiachilia mbali taarifa za kihistoria zilizotokana na nakshi zilizotiwa katika mawe na chuma, tunaweza kuzitegemea tu zile taarifa za maandishi ambayo yamechorwa au kuchapwa, kwa alama za kawaida, juu ya kitu chochote kile kama vile mafunjo au karatasi. Ni kazi kubwa na ngumu sana kuweza kuvichunguza vyanzo vya namna hii, hasa tukizingatia muda uliopita na ukubwa wa bara hili ambamo vyanzo hivyo vinajitokeza katika lugha na tamaduni tofauti. Kabla ya kuviorodhesha vyanzo hivi, itakuwa bora zaidi kwanza kuzungumzia matatizo ya jumla yaliyoonekana.

### *Matatizo ya jumla*

Eneo lililochunguzwa ni pana na lenye vipengee vingi ambayo wakati mwingine vimegawanywa katika nyanja mahsusi za kisayansi kama vile wataalamu wa utafiti kuhusu Misri walivyoshughulikia enzi za Mafarao na warasimi walivyoshughulikia Misri na Ptolemi na Afrika Kaskazini ya Warumi na wanazuoni wa Kiislamu walivyoshughulikia Afrika Kaskazini ilivyokuwa chini ya Waislamu. Kwa upande mwingine, katika Afrika Kusini mwa Sahara, aina hizi mbalimbali za vyanzo vya kimaandishi zinaingiliana, ingawa karibu sehemu hii yote haikuwa na hati zozote za kimaandishi hadi kufikia karne ya kumi na sita. Vyanzo vichache vya kimaandishi vilivyopo katika baadhi ya kanda huwa na umuhimu mkubwa zaidi kuliko ilivyo, kwa mfano, katika Maghrib. Mgawanyo huu pamoja na upotofu unaotokana nao ni ishara muhimu kwamba vyanzo hivi vinaakisi historia halisi ya Afrika ambayo kwa namna fulani inatofautiana na kuhitilafiana. Lakini mambo mengi hayo yanayoingiana yanadokezea historia iliyokamilika ambayo yatupasa kuiumba upya ili tupate kitu kimoja.

### *Tatizo la uchanganuzi kwa kuzingatia nyakati*

Jambo la kwanza linalojitokeza ni kwamba hali ya hati za maandishi zihusuzo historia ya Afrika zinaelekea kubadilika tokea karne ya kumi na tano na kuendelea. Hadi kufikia wakati huu vyanzo hivi ni vya maandishi yanayoanzia zama za kale, na kuendelea mpaka Enzi za Kati. Kwa maneno mengine, haya ni maelezo yaliyoandikwa kwa makini na watu waliokusudia kurithisha mambo waliyoyafahamu kwa kutumia kumbukumbu za kihistoria, tarihi, taarifa za wasafiri na kadhalika. Kuanzia karne ya kumi na tano, vyanzo muhimu vilikuwa ni nyaraka za zamani ambazo hazikukusudiwa kutoa taarifa, bali kuhakikisha kuwa mfumo fulani wa jamii unaendeshwa inavyotakiwa.

Aidha, ingawa nyaraka za kirasimi na za Waarabu ndizo zinajitokeza zaidi katika kipindi cha mwanzo, ni nyaraka za Wazungu (Wareno, Wataliani, Wadachi n.k.) ndizo zinaonekana kujitokeza zaidi kuanzia karne ya kumi na tano. Vilevile katika Afrika Kusini mwa Sahara kuna ongezeko la kutosha katika idadi ya nyaraka zilizoandikwa na wenyeji. Hapa pia mabadiliko ya taratibu ya hali na asili ya vyanzo ni mwashirio wa maendeleo halisi ya kihistoria, hasa kwa sababu baadaye Afrika ya Mediterani ya karne ya kumi na nne na Afrika Kusini mwa Sahara ya karne ya kumi na tano, schemu za pwani za bara hili zilitwaliwa na Wazungu. Wareno walianza kuonekana katika pwani ya Afrika Kusini mwa Sahara mwaka 1434. Hii ndiyo maana tumeihagua karne ya kumi na tano, kama mpaka kati ya nyakati hizi mbili mradi tu mgawanyo huu usishikiliwe sana.

Isitoshe, kufuatana na hati zilizoandikwa, kipindi liiki cha mwanzo kinaweza kugawanywa zaidi kama ifuatavyo:

1. Kuanzia dola ya Misri ya Kale hadi kufikia mwanzo wa dini ya Kiislamu mwaka 622 baada ya kuzaliwa Kristo;
2. Kipindi cha mwanzo cha enzi ya dini ya Kiislamu; yaani tangu mwaka 622 hadi kufikia katikati ya karne ya kumi na moja; (1050)
3. Kipindi cha pili cha enzi ya dini ya Kiislamu; yaani tangu karne ya kumi na moja hadi kufikia karne ya kumi na tano.

Kwa hali hii, hatuna budi kueleza kwa nini tumeamua kuichagua karne ya kumi na moja kama wakati wa mabadiliko. Kwa hakika, hadi kufikia wakati huo, Afrika iliyoko Kaskazini mwa Sahara ilikuwa ikifuata mfumo wa dini ya Kiislamu na ilikuwa ikiingizwa katika himaya kuu ya makhalifa wa Umayyadi, Abasidi na Fatimidi. Tofauti na kipindi cha kwanza, kipindi cha pili kilishuhudia mwelekeo pewa iliyosababisha baadhi ya nchi kujitoka katika himaya hiyo. Huko Maghrib ulikuwa ndio wakati wa dola ya Waamoravidi na pia kilikuwa kipindi ambapo Waziridi walijinyakulia uhuru wao na kutokana na kitendo hicho Wahilali nao wakafanya mashambulizi. Polepole Misri ilianza kuaacha kufanya biashara yake na Ghuba ya Uajemi, na ikaanza kufanya biashara na nchi za Bahari ya Shamu na wakati Kusini mwa Sahara mahusiano na nchi za Kiislamu yalianzishwa. Papohapo utamalaki wa kisiasa ulizuka Saheli. Aidha, hati zinazohusu Afrika pia zilianza kuongezeka katika karne ya kumi na moja.

### *Maeneo yenye tamaduni za watu mbalimbali na aina za kumbukumbu*

Kufuatana na vyanzo vya kimaandishi ni rahisi kushawishika na kufikiri kwamba tunaweza kufanya mgawanyo wa kijuu juu wa bara hili katika maeneo mawili; yaani Kaskazini na Kusini mwa Sahara. Lakini, baada ya uchunguzi wa ndani zaidi inadhibirika kuwa mgawanyo uliopo si bainifu sana. Kwa mujibu wa vyanzo vilivyopo sehemu za Sudan Magharibi na Kati zilikuwa na uhusiano wa kutegemeana na Maghrib kuliko na maeneo ya Wabantu kwa sababu ya maandishi ya Kiislamu na yale ya kihistoria kutoka Maghrib. Je, Afrika ya jangwa la Sahara na mwambao wa Saheli ikiwemo Ethiopia; pembe ya Afrika na Pwani ya Mashariki hadi Zanzibar, itofautishwe na Afrika yenye imani ya mizimu ya Tropiki ya Ikweta na ya kuelekea Kusini? Ni dhahiri kwamba tofauti hii imekitwa katika kigezo cha athari ya dini ya Kiislamu. Hatari ya mgawanyo wa mkato nanna hii ni kule kutozingatia ukweli kwamba schemu kubwa ya Kaskazini-Mashariki ya bara la Afrika haikuingiliwa sana na elimu ya Kiarabu ama katika ukubwa wa eneo au katika kategoria



zinazohusika za jamii. Isitoshe, kueleza mambo kwa namna hii kunaweza kutufanya tuhitimishie, bila kuangalia kwa makini, kwamba ile sehemu ya Afrika ambayo haina vyanzo vya kimaandishi haiwezi kujunda upya historia yake, na vibaya zaidi, yaweza kufikiriwa kwamba sehemu hii haikuwa na matukio yoyote ya kihistoria.

### Maeneo ya taniaduni za watu mbalimbali

Tukizingatia mambo haya yote tunaweza kupendekeza mwainisho ufuatao kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo:-

- (a) Misri na Sudan inayokaliwa na Wanailoti.
- (b) Maghrib, ikiwemo ukingo wa Kaskazini wa Sahara kama vile Fezani.
- (c) Sudani ya Magharibi na Kati; kutoka Bahari ya Atlantiki hadi Ziwa Chadi
- (d) Ethiopia, Eritrea, Pembe ya Afrika na Pwani ya Mashariki.
- (e) Sehemu iliyobaki ya bara la Afrika, yaani kutoka ghuba ya Guinea kupitia kanda za ikweta na ya kati hadi kufikia Afrika ya Kusini.

Mpangilio huu una faida ya kutokitwa katika vigezo vya nje pekee ingawa huvitilia maanani. Hata hivyo, hii isifanye tuakaacha kuzingatia ukweli kwamba vyanzo hivi vinatokana na lugha chache tu; ni vya aina chache, kwaniba havitokani na maeneo ambayo vinazungumzia na kwamba aghalabu havilingani na wakati unaozungumiwa.

### Uainishaji wa kumbukumbu za vya kimaandishi

*Lugha za Kiafrika* ambazo zimeweza kutoa taarifa nyingi zaidi ni Kimisri cha zamani, Kiberiberi, na lugha za Ethiopia, Kikopti, Kiswahili, Kihausa na Kifulani. Lakini, maandishi mengi zaidi ni yale ya lugha zisizo na asili ya Kiafrika kama vile Kigriki, Kilatini na Kiarabu, ingawa Kiarabu kimetokea kuwa lugha ya taifa ya nchi kadha za Kiafrika. Vilevile kuna lugha nyingine kama vile Kiajemi, Kichina na kadhalika. Kwa mujibu wa tarihi, vyanzo vya awali vya kwanza kimaandishi ni maandishi-picha ya Kimisri kwenye mabapa ya mafunjo ambayo yanaanzia enzi za Ufalme Mpya na pengine nyuma zaidi hadi enzi za Ufalme wa Kati wa Mafarao mwanzoni mwa elfia ya pili kabla ya enzi zetu. Kwa mfano, mafunjo ambayo yalijulikana kama *Mafunjo kwa mfalme Merikere*. Kisha kuna maandishi ya mafunjo na ostrakani<sup>1</sup> ya Ufalme Mpya yakifuatia na vyanzo katika Kigriki na Kihibrania (Biblia) na matini ya kawaida ya Kimisri yanayoanzia wakati wa Ploteni, na maandishi ya Kilatini, matini ya Kikopti katika lugha ya Kimisri, ambayo yameandikwa kwa kutumia abjadi ya Kigriki, na pia hati zilizoandikwa kwa Kiarabu, Kichina, Kiajemi, Kiitaliano na Kiethiopia ambamo masimulizi ya kale ya Kimaandishi yanaanzia karne ya kumi na tatu.

Kufuatana na aina ya maandishi haya, tunaweza kuyagawanya katika sehemu mbili. Ya kwanza ni masimulizi ambayo ndiyo yalikuwa mengi zaidi hapo mwanzoni. Ya pili ni nyaraka za kale ambazo zilionekana hasa katika Maghrib tangu karne kumi na mbili, na kuendelea kwa mfano, vyombo vya enzi za Almohadi. Vyanzo hivi vilikithiri katika Misri, kuanzia karne ya kumi na mbili hadi ya kumi na tano (kwa mfano katika enzi za Wamamluki), na katika Ethiopia ambako vunchifadhiwa katika Mkusanyo wa Miswada kwenye makazi ya watawa. Katika sehemu zingine, hifadhi ya nyaraka za kale ilikuwa aijaanza, ingawa *mahram*<sup>2</sup>, au barua hataza zilizotolewa na Wafalme wa Bornu ya

<sup>1</sup> Mafunjo ni mma ambao ulitumia kama chombo cha kuandika; ostrakoni ni kipande cha mawe ya chokaa.  
<sup>2</sup> Barua za Kifalme zilizo kuwa zikitoa masahi kwa mu binafasi au kwa kikundi cha watu.

karne ya kumi na moja, bado zipo.

Vyanzo hivi vinagawanyika katika makundi mawili: hati ya masimulizi kama vile tarihi, taarifa za kila mwakana masimulizi ya safari, maandishi ya kisheria au dini na kazi ya fasihi. Aina ya pili ni ile ya hati vyanzo vya nyaraka za kale zikiwemo: (a) hati za binafsi kama vile barua na mawasiliano ya kibiashara; (b) maandishi rasmi kama vile mawasiliano ya kiutawala na matini za fedha na utungaji wa sheria' na (c) maandishi ya sheria na dini.

Vyanzo vya masimulizi ambavyo vilianza na Homer katika karne ya nane kabla ya enzi zetu, ni pamoja na maandishi muhimu yanayodhirisha kiwango kikubwa sana cha akili ya binadamu. Maandishi haya yanayaainisha mambo mbalimbali juu ya Afrika na kuunda nadharia ya ulimwengu kwa jumla. Hii inajitokeza, kwa mfano, katika maandishi ya Herodotus, Polybius, Ptolemi, Mt. Augustino, Mas'udi na Ibn Khaldun. Nyaraka za Kale juu ya Afrika, ambazo zamani zilionekana Misri peke yake, ni za zamani kuliko zote duniani. Maandishi ya awali ya mafunjo ya bonde la Mto Naili yalionekana karne ya ishirini hivi kabla ya yale ya Ulaya (yajulikana kama Mafunjo ya Ravenna). Kuanzia karne ya kumi na nne kulikuwa na ongezeko kubwa la nyaraka za kale. Nyaraka hizi ziliwekwa katika vitabu vya maarifa kabla ya kugundua njia mpya za kuzihifadhi katika majumba maalum ya nyaraka.

### *Uorodheshaji kwa kufuata nyakati*

Mambo ya kale kabla ya uislamu, (kuanzia mwanzo hadi + 622)

Kumbukumbu muhimu za wakati huu ni za kiakiolojia, lakini hata hivyo hati za kimaandishi zilikuwa zimeanza kuonekana Misri, Unubi na Afrika Mashariki.

### *Misri, Unubi, Afrika Mashariki*

Maandishi ya mafunjo au ya ostrakoni yamo katika maumbo ya picha-neno (ambayo maran yingi huchongwa) au katika maandishi-picha yakiunda hati unganishi ambazo zingefaa zaidi zichorwe kwenye ubapa. Haya ya mafunjo na ostrakoni yalilusika zaidi na mambo ya serikali au maisha ya watu binafsi, ripoti za kiutawala na kisheria, ripoti za uwekaji mahesabu, barua za binafsi, na hadithi na riwaya.

Elfia ya kwanza kabla ya enzi zetu ndiyo hasa yenye umuhimu. Mathalani, *Kitabu cha Wafalme* katika Agano la Kale kinatupa taarifa muhimu kuhusu ufalme wa ishirini na mbili wa Farao (yapata miaka 950 kabla ya kuzaliwa Kristo), na juu ya kipindi kilichofuatia hadi kufikia utawala wa kijeremi (yapata mwaka 525 kabla ya kuzaliwa Kristo). Kuanzia ufalme wa kwanza wa Saite katika Misri (yapata mwaka 800 kabla ya kuzaliwa Kristo), maandishi ya Kigiriki yalianza kutupa mwanagaza kuhusu Afrika hususani yale ya Meander na Herodotus. Kufikia wakati huu, mafunjo yalikuwa yakiandikwa katika lugha ya Kigiriki au Kimisri cha kawaida, na mara nyingi maandishi yalikuwa zaidi ya hati unganishi kuliko yale ya maandishi-picha.

Kati ya muda Ptolemi walipojiimarisha Misri mwishoni mwa karne ya nne kabla ya enzi ya Kristo na kutamakani kwa Waarabu mnamo mwaka 639 baada ya kuzaliwa Kristo, kulipita kipindi cha miaka elfu moja. Kumbukumbu zilizopakana kwa wingi katika kipindi hiki zilikuwa za Kigiriki za maandishi kama vile Polybius, Strabo na Diodorus Siculus na za mwandishi Pliny Mkubwa wa Roma ambaye kitabu chake cha *Natural History* (Historia Asili) kina habari zinazotofautiana katika ubora lakini ambacho kina maelezo ya kusesimua yanayotupa mwanga kuhusu ulimwengu wa Kiethiopia.

Miaka mia tano baada ya kuanza kwa Ukristo ni kipindi chenye utajiri wa vyanzo vya hati. Katika kipindi hiki Misri ilikuwa mojawapo ya vitovu vikubwa vya utamaduni wa Kigiriki na ikotoa wataalam wa mambo ya historia, jioografia, falsafa na viongozi wakuu wa Kanisa. Kuingizwa kwake katika dola la Kirumi, na baadaye katika dola ya Byzantium, kumeclezwa sana katika nyaraka za kale (kama vile zile za Sheria za Theodosius au *Novellae* ya Justin) Hadithi za kihistoria, au maelezo katika masimulizi, kama vile yale ya Jiografia ya Ptolemi (mwaka wa 140 baada ya kuzaliwa Kristo), katika *Periplus of the Erythrean Sea* (Habari za Bahari ya Erythrea) ambayo yaliandikwa na mtu asiyejulikana mnamo mwaka wa 230, na *Topographica Christiana* (Maeneo ya Nchi za Kikristo) ya Cosmas Indicopleutes (mnamo mwaka 535). Maandishi haya yote ni ya kimsingi kwa sababu yanatoa maelezo kuhusu Ehtiopia, Pembe ya Afrika, na Pwani ya Mashariki ya Afrika.

### *Maghrib ya Kale*

Historia iliyoandikwa ya Maghrib inalusiana sana na mgongano uliokuwepo kati ya Kariteji na Roma. Historia ya Puniki kabla ya Hannibal inategemea akiolojia na uandishi wa maneno ya nakshi. Kitabu cha *Periplus of Hanno* (Habari za Hanno) ambacho kinaongelea Pwani ya Kaskazini Magharibi ya Afrika ni cha ubini tu. Hata hivyo ilani za Juba II ambazo Pliny Mkubwa alizielezea katika kitabu chake cha *Natural History* (Historia Asili) zinapaswa kuzingatiwa. Sehemu kubwa ya taarifa tulizonazo kuhusu Maghrib katika awamu za Kariteji, Roma, Waharabu na Byzantium zimetokana na maandishi ya wanahistoria na wanajiografia walioandika katika lugha ya Kigiriki au Kilatini. Mwanzoni, wandishi hawa walikuwa wageni, lakini polepole maandishi wazalendo walijitokeza kuwa wengi kuwapita wageni.

Kuanzia mwaka wa 200 kabla ya Kristo hadi mwaka wa 100 badala ya Kristo - wanajitokeza mashahidi mashuhuri kama vile Polybius, Strabo, Diodorus Siculus, Salust, Livy, Tacitus, Plutarch na Ptolemi. Baadhi ya maandishi hawa walijihusisha sana na ukusanyaji wa data za zamani; lakini wengine hutoa taarifa asilia na za kipekee; Polybius alikuwa msiri wa Scipios na yasemekana kuwa alikuwapo wakati ilipozingirwa mnamo mwaka 146 kabla ya kuzaliwa Kristo. Katika kitabu chake kijulikana kama *Bellum Jugurthinum* (*Vita vya Jugurthinu*), Sallust anatupa maelezo ya kuajibia kuhusu falme za Kiberiberi na Kaisari, katika kitabu chake cha *Belium Civile* (*Vita vya Raia*), anajionyesha kama mtetezi na mwandishi wa historia. Polybius ambaye alizaliwa karibu miaka 200 kabla ya Kristo alikuwa inashuhuri sana wakati huo. Baada ya kuondoka kwake Misri iliyokuwa ikitawaliwa na wagiriki, maisha yake ya miaka kumi na sita akiwa mkimbizi wa kisiasa Roma pamoja na tabia yake ya kudadisi na kung'amua inambo vilimwezesha kuelewa kinaganaga ulimwengu wa Mediterani. Pia katika kipindi hicho alifanikiwa kuishi vizuri kutokana na urafiki wake na Scipios. Polybius alikuwa mtu mwenye shauku kubwa sana ya kujua mambo na pia alikuwa mtu mwenye fikia nyingi. Wa bahati mbaya, kati ya vitabu arobaini ambavyo kwa pamoja vilijulikana kama *Pragmateia*, ni vitabu sita tu ambavyo vimeweza kupatikana. Vaginevyo tungeweza kufahamu mengi zaidi kuhusu meli ambazo inasemekana Scipio Aemilianus alimpa Polybius ili akafanyic safari za uvumbuzi katika pwani ya Atlantiki ya Afrika.

Baada ya karne ya kwanza kipindi ambamo dola ya Kirumi ilifikia kilele cha ustawi wake na hatimaye kuporomoka na kudhalilika vyanzo vya kimaandishi vilianza kuadimika na zaidi yakabakia maandishi ya Kikristo, ingawa haya yanawahusisha watu mashuhuri kama vile Mt. Cyprian na Mt. Agustino (354-430). Hata hivyo, inabidi tuwe na hadhari wakati hawa Viongozi Wakuu wa Kanisa wanapojiingiza katika mikinzano kuhusu matukio ya

kihistoria ya wakati huo kutokana na kuamania kwao dini; kama vile Mt. Agustino anavyoshambulia sana mabadiliko yaliyoletwa na chama katika majuzuu kama yale yaliyoko Berlin na Vienna na vilevile mkusanyiko wa maandishi ya Migne.

Kipindi cha Waharabu katika Afrika ya Kaskazini kilichofuatiwa na kipindi cha Wabyzentine kunyakua na kutawala sehemu hiyo kimeelezwa na mwandishi wa kusisimua aitwaye Procopius ambaye kitabu chake inaaruifu kijulikanacho kama *De Bello Vandalico* (Vita vya Vandal), ni chanzo cha msingi kuhusu kipindi hiki cha mgogoro.

### *Afrika ya Sahara na ya Magharibi*

Kutokana na mbinu za uabiri wakati ulc, sehemu za mbali kabisa ambazo mabaharia wa zamani waliweza kuzifikia, mbele ya sehemu ya kusini kabisa ya Morocco ni Rasi ya Jubu na Latitudo ya Visiwa vya Canary. Kwa hivyo sehemu kubwa ya maelezo katika *Periplus of Hanno* (Habari za Hanno) ni masimulizi yaliyobuniwa tu. Kwa upande mwingine, vipande vya habari kuhusu Afrika Kusini mwa Sahara vimejitokeza hapa na pale katika masimulizi ya maandishi kadha. Herodotus anazungumzia biashara sukutu ya mali kwa mali waliyofanya Wakariteji katika Morocco ya kusini. Biashara hizi zililhusu zaidi kubadilishana bidhaa za Maghrib, zilizotengenezwa kwa mikono, kwa ungaunga wa dhahabu. Vitu hivi vililwekwa chini vikachunguzwa na pande zote mbili, halafu wahusika walibadilishana bila kuongea neno lolote. Msimulizi wa Pseudo-Scylax anataelezea mahusiano kati ya Wakariteji na Waberiberi wa Libya. Hata hivyo ni katika maandishi ya Polybius ambamo tunakuta tena mambo muhimu, kama vile kumbukumbu za kwanza za majina ya mahali katika Afrika Kusini mwa Sahara. Lakini, kwa vile anakomea Rasi ya Jubu pake yake, taarifa yake haina budi ijalizwe na ilani za Juba ya II zilizokusanywa na Pliny, Strabo na Diodorus Siculus.

Mwisho, katika karne ya pili, Ptolemy ambaye alikuwa mwana-jiografia wa Alexandria, katika kitabu chake muhimu cha *Geography*, (Jiografia) anatoa maelezo makim juu ya ujuzi wa watu wa kale kuhusu kontaa za Afrika. Ramani yake ya "Libya ya Ndani" ina majina ambayo yamebakia hadi leo, kama vile Mauretania, Libya, Garamantes, Numidia, Niger, na kadhalika. Aliweza kuichora ramani hii kwa kutumia taarifa aliyopata katika jeshi la Kirumi wakati likifuatilia maadui kuwaadhibu kuvuka mipaka (*limes*) ya dola yake. Ni kweli kwamba baadhi ya makosa katika ramani hii, hasa kwa Afrika Kusini mwa Sahara ambayo haikutiwa maanani sana yameendelea kuwapo hadi kufikia karne ya kumi na tisa; mathalani sehemu iliyopaswa kupitiwa na into Niger, kwa vyovyote vile, tunaweza kusema kuwa ramani hii ilikuwa ni mchango mkubwa sana katika kuifahamu historia ya Afrika.

### Enzi ya kwanza ya Uislamu (k. + 650-1050)

Kutamalaki kwa Waarabu ambako kulifuatiwa na kuanzishwa kwa tawala za makhalfi katika sehemu zilizotokwa kuliyaunganisha maeneo mengi ambayo hapo awali yalitengana kitamaduni na kisiasa katika dola za Kijamii na Byzantine. Kwa hivyo, iliundwa dola iliyoenea kutoka mwambao wa Atlantiki hadi sehemu za mbali za Asia yenye kuchanganya watu mbalimbali ambao hadi wakati huo hawakujua habari za kuwapo kwa wenzao. Hii ndiyo sababu kuanzia wakati huu tunakuwa na vyanzo vipya vya taarifa hasa kuhusu Afrika Kusini mwa Sahara, ingawa eneo hili lilikuwa bado ukingoni mwa dola hii. Hii pia ni mojawapo ya sababu zinazoeleza kwa nini taarifa hii si kamili na wala haina mtiririko mzuri, na mara nyingine hufanana kama masimulizi ya ngano. Kitu ambacho ni dhahiri kabisa ni kwamba mbali na vyanzo ambavyo vinahusiana zaidi na Misri kama vile

maandishi ya mafunjo, nyaraka za kale na vyombo vya Fatimidi karibu taarifa zote toka wakati huo zilikuwa zikionekana sehemu nyingine za Afrika. Kwa hivyo Afrika inaweza kuainishwa kwa kufuata aina badala ya kanda.

### Tarihi

Tukiacha kando tarihi ya Khalifa bin Khayyat hapakuwa na tarihi zozote zinazofahamika kabla ya karne ya tisa. *Tarihi* hii ya Khalifa ambayo ni mojawapo ya kumbukumbu za zamani za kihistoria za Kiarabu ina taarifa muhimu kuhusu kutamalaki kwa Maghrib. Pia ni muhimu kuzingatia kuwa Al Tabari ameandika katika *Ta'rikh* yake mojawapo ya taarifa za zamani za Kiarabu kuhusu Afrika Kusini mwa Sahara. Taarifa hiyo ilitolewa kama ushahidi na mwanahistoria mmoja, aitwaye Umar bin Shabba, na inazungumzia maasi ya "*Sudan*" huko Medina yapata mwaka 145 Baada ya Hijra au mwaka 662 Baada ya Kristo. Huu ni ushahidi kuwa kulikuwa na Waafrika wakati huo. Aidha kulikuwa na mkusanyiko wa sheria za jadi ambazo zilikusanywa na Ibn Abd al-Hakam ambazo pia zilikuwa na taarifa za kihistoria.

Baada ya kupita karne nzima bila maandishi yoyote, mnamo karne ya kumi katikati kilitokea *Kitab Wulat Misri wa Qudhatuha* kilichoandikwa na Kindi kinachoweza kuchukuliwa kama tarihi na ambacho ni muhimu sana katika kuzielewa Misri na Maghrib. Vilevile katika karne hiyohiyo ya kumi, kitabu cha Kadi Nu'man kilichojulikana kama *Iftitah al-Da'wa* kilitokea. Hiki kilikuwa kitabu cha msingi katika kujifunza habari za mwanzo wa harakati za Fatimidi.

Hata hivyo tarihi zote hizi zinazohusu Afrika hazina budi zizingatiwe kwa hadhari na makini; na ingefaa zilinganishwe na maandishi ya Kiislamu yaliyoko Mashariki ya Kati na Mashariki ya Karibu.

### Kumbukumbu za kijiografia

Kumbukumbu hizi zilikuwa nyingi na muhimu tangu karne ya tisa, na zinaonekana kama inikusanyiko ya ramani kama vile *Surat al-Ardh* chenye vielelezo vilivyotiwa na Khwarizmi, jiofrafia za tawala, maclekezo ya wasafiri (Masalik), au masimulizi ya safari ambayo yamefafanuliwa kwa viwango mbalimbali. Vitu hivi vinaonyesha jinsi kulivyokuwa na nia ya kuiunganisha pamoja dunia yote ya Kiislamu iliyokuwa ikijulikana wakati huo. Hii ndiyo sababu maelezo haya ni hati ya hali ya juu kuhusu Afrika Kusini mwa Sahara kwa wakati ule.

Orodha kamili iliyotayarishwa na Kubbel na Matveiev inatoia ushahidi mkubwa kuhusu thamani ya vyanzo hivi. Lakini hata hapa hatuna budi tuwe waangalifu katika kuamua mambo yapi ni taarifa ya kweli iliyokusanywa na mambo yapi ni ya kubuni. Aidha, ni muhimu nambo haya yatazamwe kufuatana na mbinu zilizotumiwa na vilevile msimamo binafsi wa maandishi wa Kiarabu wa wakati huo, na hasa kulingana na muktadha wa historia Kiafrika kama ilivyoandikwa upya kufuatana na hati nyingine. Lazima tufanye hivyo ili tusijikute tuna picha moja tu iliyotokana na misingi ya tarithi za Kiarabu na za kigeni peke yake.

Miongoni mwa mkusanyiko huu wa hati tunaweza kuyataja maandishi ya *Ta'rikh* na ya *Buldan* ambayo yaliandikwa na Al Biruni Ya kubi ambayo yanazungumzia Ethiopia, Unubi, Sudan, Beja, Zandj na Aghawa ya Kanem. Maandishi niakini zaidi ni yale yanayojulikana kama *Masalik* yaliyoandikwa na Ibn Hawkal ambaye alizuru Unubi na Sudan ya Magharibi, na ambayo yanatoa maelezo kuhusu biashara ya Sahara. Mwisho, kitabu cha *Fields of Gold*

(+ 965) (Nyanda za Dhahabu) cha Mas'udi kinaelezea mambo mengi kuhusu pwani ya mashariki ya bara la Afrika.

#### *Kumbukumbu za kisheria na kidini*

Maandiko ya Tabaat juu ya sheria na maisha ya wahubiri ni hazina kubwa sana ya taarifa kuhusu Maghrib. Vilevile kitabu kilichoandikwa na Ibn al-Saghir mapema karne ya kumi kijulikanacho kama *The Chronicle on the Imams of Tahert* (Tarihi ya Imamu wa Tahert) kinatoa mwanga kuhusu uhusiano wa kibiashara kati ya jamii ya ibadite na Gao, na juu ya biashara yote ya kuvuka jangwa la Sahara mradi tu pawe na hadhari juu ya baadhi ya maelezo yaliyomo na ambayo si sahihi.

#### **Enzi ya Pili ya Uislamu (1050-1450)**

Kitu kilichojitokeza zaidi katika kipindi hiki ni wingi na ubora wa taarifa, Taarifa hizi zinatokana na vyanzo vya nyaraka za kale ambazo ingawa si nyingi kuliko hati za maandishi lakini bado ni muhimu. Waandishi wa tarihi wanatoa maelezo ya hali ya juu sana kutokana na uchunguzi wao wa mambo ya wakati huo na kuandika upya vyanzo vya kale ambavyo sasa vimepotea. Kutokana na vyanzo vya nje vilivyopo na kupatikana kwa miswada ya Kiethiopia na hati mpya juu ya Afrika, tumeweza kupata maarifa ya upeo wa juu kuhusu Afrika Kusini mwa Sahara.

#### *Kumbukumbu za nyaraka za kale*

Kumbukumbu hizi zinapatikana Misri na Maghrib tu. Idadi kuwa ya hati zilizoko Cairo Geniza ni ya enzi ya Fatimidi, ingawa kuna sehemu ndogo inayohusiana na kipindi cha Wainamluki. Hati hizi ni inchanganyiko wa maandishi ya kifamilia na barua za kibishara ambazo zinaonyesha shughuli zilizokuwa zikifanywa na Wayahudi waliokuwa wakiishi Misri. Ingawa hati hizi hazina tarehe na wanahistoria hawana budi kuzitumia kwa makini, ni za kuvutia sana kutokana na taarifa zilizomo. Hatuna budi pia kutaja nyaraka za kale za binafsi na kumbukumbu za Wakfu ambazo zimehifadhiwa katika Masijala ya Cairo.

Hati za Kizungu - mikataba na barua za biashara ambazo zilitoa mwanga kuhusu sekta za kiuchumi na kijami - nazo zimchifadhiwa katika majiji kadhaa ya Italia na Uhispania.

Ama kwa hakika hakuna nyaraka za kale za kitaifa katika kipindi hiki, lakini kuna idadi fulani ya hati rasmi zinazotoa picha kuhusu itikadi ya dola za Almoravidi na Almohadi. Na kwa mujibu wa maoni ya A. Laroi hati hizi zinaonyesha mtazamo wa kigeni wa maendeleo ya kisiasa na kijamii. Katika kipindi cha baadaye huko Misri tunakuta vitabu vya mambo yote ya kihistoria na kisheria ambayo ni mkusanyiko wa maandishi mengi rasmi kuhusu taratibu za fedha na miundo ya taasisi mbalimbali. Miongoni mwa hati za aina hiyo lazima tutaje maandishi ya Maqrizi. Mojawapo ya maandishi hayo na ambayo yana thamani isiyu kifani ni yale ya karne ya kumi na tano yajulikanayo kama Khitab na ambayo hayaelezei Misri ya Uislamu tu bali pia Unubi, Sudan na Ethiopia.

#### *Kumbukumbu za masimulizi*

##### **Tarihi**

Baada ya karne ya kumi na mbili ambayo haikuwa na masimulizi ya aina yoyote, tunafikia karne ya kumi na tatu na kumi na nne ambapo tunakuta kikundi kizima cha waandishi hodari ambao, licha ya kuthibitisha inatukio ya wakati huo, wanasanisi pia matukio ya karne

zilizopita. Kwa mfano, Nuwayri anazungumzia Wamamluk na kutamalaki kwa Maghrib, Ibn al-Idhari ambaye ni maarufu kwa maandishi yake ya kale ya Afrika na kuhusu Almohadi, na Ibn Khaldun mwenye akili ya upeo wa juu aliyefanya utafiti kamambe uliomo katika kitabu chake cha *Kitab al-Ibar*.

### Jiografia

Ubora wa maandishi ya jiografia hutofautiana. Katika kitabu cha *Book of Roger* (+ 1154), Al-Ildr s anatupa maelezo ya kuhusu Ethiopia na Afrika Magharibi. Katika kitabu chake kinachoitwa *The Geography* (Jiografia) Ibn Sa id al-Gharnati anatumia maelezo ya Al-Idrisi kama chanzo chake pamoja na kuwa anatoa maelezo ya ziada juu ya Sudan. Pia kuna baadhi ya wandishi wasiojulikana sana. Waandishi hawa ni kama vile al-Zuhri (karne ya kumi na mbili), Yakut (karne ya kumi na nne), al-Baghdadi na al-Himyari, lakini ambao hutoa taarifa zenye manufaa. Lakini kuna waandishi watatu kati yao waliojitokeza zaidi; nao ni Al-Bakri (karne ya kumi na moja), al-Umari (karne ya kumi na nne) na Ibn Battuta. Kitabu cha *Masalik wa' l Mamalik* kilichoandikwa na Al-Bakri kinawakilisha upeo wa ujuzi wetu wa jiografia ya Maghrib na Sudan, ingawa mwandishi mwenyewe hakuwahi kulivuka jangwa la Sahara.

Al-Umari katika kitabu chake cha *Masalik al-Absar* amejidhihirisha kuwa mchunguzi mwenye utaalamu wa hali ya juu wa mfumo wa ndani wa utawala wa dola ya Mali na uhusiano wake na Misri na Uislamu. Kitabu hiki kijnatupa mwanga kuhusu mabadiliko kuelekea mfumo wa kitaifa wa Sudan na jinsi dini ya kiislamu ilivyoenea. Wakati Al-Bakri anaelezea biashara ya dhahabu na uhusiano na Maghrib karne tatu kabla ya wakati huo, al-Umari anatuonyesha jinsi uhusiano huu ulivyobadilika kuelekea zaidi Misri.

Mwisho tunafaidika mno na maelezo ya Ibn Battuta msafiri mashuhuri katika bara lote la Afrika juu ya maisha alivyoyaona mwenyewe huko Sudan na Mgharib. Kwa mfano maelezo aliyotoa kuhusu ufalme wa Mali na schemu nyingine zote za safari yake katika Sahel, yana thamani sana. Sura aliyoundika kuhusu "Uzuri na Ubaya wa Watu Weusi" ni maandishi yenye thamani kubwa sana katika historia kwa sababu yanatuonyesha jinsi watu wa Maghrib walivyokuwa wakiwatazama watu weusi wa wakati ule.

### Marejeo ya mwamko wa kidini na kimaandishi

Vyanzo maarufu kabisa vya aina hii vinavyofahamika sana ni maandishi ya *Tabakat* na yale ya waunini wa Kisunni, Kikhariji, Kimarabou na hata wa Kikristo vya madhehebu ya Kopti pamoja na miswada ya makanisa ya Ethiopia. Maandishi haya yanatuwezesha kuona, ingawa kwa juujuu, jinsi hisia za dini na mifumo ya jamii ilivyokuwa ikijengeka kama inavyodhihirika katika maandishi ya Maliki yajulikanayo kama Riyadh. Vyanzo vya Kikhariji na muhimu sana kwa kanda nzima ya Sahara ambayo iliyohusisha Maghrib na Sudan. Vyanzo vya kimaandishi ni vingi lakini vinahusika zaidi Maghrib na Misri. Mojawapo ya maandishi ya kimsingi ni Kamusi ya Safadi iliyojulikana kwa jina la *Al-Wafibi-L-Wafayati*.

### Hitimisho

Kipindi kinachofikia mwanzoni mwa karne ya kumi na tano hakina uhaba wa vyanzo vya kimaandishi kama inavyofikiwa na wengi. Ni kweli kwamba Misri, na hapo baadaye Maghrib, ndizo schemu zenye vyanzo vingi. Hata hivyo, katika kanda nyinginezo idadi na ubora wa Ilati zinazidi kuongezeka kwa kadri tunavyotoka kwenye kipindi cha Herodotus kuelekea kipindi cha Ibn Khaldun na Ibn Battuta kwa sababu zinapea kutoka kwenye vidokezo kuwa historia kamili. Vyanzo vya Kiarabu, ingawa asili yake ni nje ya bara hili bado vinakiuka tofauti zisizokatalika za kijamii na kitamaduni na kuanzisha mshikamano mpya na kamili wa maeneo ya Sahara ikiashiria hali ilivyokuwa katika enzi za Neolithiki.

---



# 6

## *Vyanzo vya kimaandishi kuanzia karne ya kumi na tano na kuendelea*

---

Mabadiliko makubwa yaliyotokea duniani, na hasa Afrika, kuanzia karne ya kumi na tano na kuendelea, yalisababisha mageuko dhambi katika tabia, asili na idadi ya vyanzo vya kimaandishi. Mielekeo mipya inayojitokeza ni kama ifuatavyo:

Kwanza, pamoja na kuongezeka kwa idadi ya vyanzo vya masimulizi katika umbo la tarihi, maelezo-fafanuzi na kadhalika pia tunakuta ongezeko kubwa la vyanzo vya msingi vitokanavyo na nyaraka za kale za watu binafsi na za kiserikali. Hili ongezeko kubwa la hali huwasaidia lakini pia huwatatiza wanahistoria, kwa sababu haliwezi kutumiwa kwa urahisi kuelezea picha kamili ya matukio.

Kadhalika tunakuta upungufu mkubwa wa idadi ya vyanzo vya masimulizi vya Kiarabu kuhusu Afrika, Kusini mwa Sahara. Jambo linalojitokeza zaidi hapa ni kuwa maandishi wazalendo walianza kuandika historia inayolusu maisha yao wenyewe kwa Kiarabu, hasa katika Sudan na mwambao wa Mashariki. Baadaye maandishi hawa walianza kuandika katika lugha zao wenyewe. Mwanzoni wakitumia zaidi hati za Kiarabu na baadaye alfabeti za Kilatini; lakini wakati mwingine walitumia hati walizoziunda wenyewe. Hatimaye waliandika kazi zao kwa lugha za Kizungu, na kukawa na ongezeko kubwa sana la idadi ya hati za namna hiyo katika kipindi chote cha karne ya kumi na tisa.

Hali hii iliendelea pia katika baadhi ya kanda kama vile Misri, Maghrib na Ethiopia, ambako mila za kale za utoaji wa hati za maandishi ziliendelezwa na hata kuhusishwa katika Maghrib.

Ongezeko hili kubwa la kazi za maandishi liliwezsha kugunduliwa kwa sehemu kubwa za bara hili, kadiri kazi hizo na uandishi zilivyozidi kuenea toka pwani hadi bara. Kuenea kwa kazi hizi kukaanza kidogokidogo na baadaye kwa kasi zaidi hasa kuanzia karne ya kumi na nane na kuendelea. Hii inahitabika zaidi katika kanda za Senegambia, delta ya Mto Niger na Benin na ufalme wa Kongo na Angola na pia katika pande zote mbili za Mto Zambezi hadi kufikia dola ya Mwene Mutapa na kuendelea pwani ya Kusini Magharibi na Bukini. Kwa jumla, mwambao wa Atlantiki una maandishi mengi zaidi kuliko upwa wa Mashariki.

Tukizingatia intazamo wa maandishi wa historia wa Sudan uliotapakaa kuelekea Kusini angalau hadi kufika katika msitu tunaona kwamba maeneo makubwa ya bara yameelezwa na vyanzo vya kimaandishi na kuwa kanda chache tu zilibaki nje ya mkondo huu hadi inwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Hii ndiyo sababu ni bora zaidi kulijadili suala hili kanda kwa kanda kwa kutilia maanani maeneo tofauti ya vyanzo kwa mujibu wa wakati, asili, tabia na lugha.



## Afrika ya Kaskazini na Ethiopia

### Afrika ya Kaskazini

Desturi ya kuandika tarihi ihendelea kuwepo katika kanda hii, lakini haikutoa watu mashuhuri kama wale wa karne zilizopita. Na hasa hapakuwa na wafuasi maarufu wa Ibn Khaldun wa kuendeleza fikra zake.

Kimsingi mabadiliko yaliyotokea katika kipindi tunachozungumzia, yanahusu hati za nyaraka za kale na maelezo ya Wazungu. Nyaraka za kale za Uturuki zinazoanzia karne ya kumi na sita, si haba hata kidogo zikilinganishwa na nyaraka zenye utajiri mwingi sana za Ulaya. Nyaraka hizo zinaelezea nchi kama Misri, Tipolitania, Tunisia na Algeria, ambazo zilijumuishwa katika dola moja. Morocco haikuwahi kupoteza uhuru wake na ina mkusanyo mkubwa wa maandishi ya historia yake ambao sehemu yake kubwa inahusu serikali na utawala, kabla ya karne ya kumi na tisa; hakuna maandishi mengi yanayohusu shughuli za kiuchumi, kijamii na utamaduni, jambo ambalo huenda linasababishwa na kutokuwepo kabisa kwa nyaraka za kale za watu binafsi.

Jambo linalojitokeza kuhusu vyanzo vya masimulizi vya Kiarabu ni kufikia kwake katika wingi na ubora wake isipokuwa kwa nchi ya Morocco, ambako Palme mbili za Kisharifu zimeelezwa kwa kirefu katika vitabu vya historia yakiwemo, kwa mfano, majuzuu ishirini ya Masul yaliyoandikwa na Mokhtar Sussi painoja na kazi ya Mwanahistoria mashuhuri wa Morocco tokea enzi za kati, aliyejulikana kama Al-Zayyani (aliyekufa + 1833). Pia kuna kazi ya al-Nasiri al-Slawi (aliyekufa + 1897) ambaye historia yake ya jumla kuhusu nchi hiyo inatumia mkusanyiko stadi wa mbinu za kimapokeo na za kisasa. Tunamshukuru pia kwa mchango wake wa kazi ya kijiografia yenye kutupatia habari nyingi kuhusu maisha ya kijamii na kiuchumi.

Huko Algeria kuna historia ya Kiarabu na ya Kituruki ya Aruj na Khayruddin Barabarossa zilizoandikwa na waandishi wasiojulikana na historia ya kijeshi iliyoandikwa na Muhammad al-Tilimsani. Historia ya Tunisia imegemea sana na mfululizo wa kumbukumbu za kihistoria kuanzia zile zilizoandikwa na al-Zarkashi katika karne ya kumi na sita hadi zile za karne ya kumi na tisa zilizoandikwa na Maqdish al-Safaqusi. Historia ya Tripoli iliandikwa na Muhammad Ghalbun katika karne ya kumi na nane, ambapo tarihi za Kiibadhi, wasifu, kama ule wa al-Shammakhi katika karne ya kumi na sita, zina habari muhimu kuhusu Sahara ya Sudan.

Katika inaandishi ya historia ya Misri ya Kiotoman majina maarufu mawili yanajitokeza; Ibn Lyaas, katika karne ya kumi na sita, ambaye kazi yake aliandikwa kwa kina kisicho kifani na hivyo kuwa na inambo mengi sana; na al-Jabarti katika karne ya kumi na tisa, aliyandika tarihi ya kipindi muhimu cha siku za mwisho wa utawala wa Kituruki, utekaji wa Napoleon na kujitokeza kwa Muhammad Ali.

Katika kipindi hiki, kulikuwa na ongezeko la kutosha la idadi ya maelezo ya wasafiri na mashahidi wa wakati ule wa Kizungu. Ingawa maelezo hayo yalieleka kupinga Uislamu kama ilivyodhihirika kwa mwelekeo wa waandishi wake, yana mambo mengi mazuri, na maono ambayo hayajapata kuonekana popote pale kabla. Wasafiri hao walikuwa ni pamoja na wafanyabiashara na hata na mateka, kama vile Miguel Cervantes. Kazi maarufu yenye majuzuu 24 itwayo *Description de l'Egypte* (Maelezo ya Misri) iliyoandikwa na wanasayansi waliokuwamo katika safari maalumu ya Napoleon ni chemchemi isiyosoza ya habari za Misri kama walivyokuta mwanzoni mwa enzi mpya. Kwa ufupi, ilipofikia karne ya kumi na tisa, vyanzo vya historia ya Afrika ya Kaskazini vilikuwa vingi kama vile vya uchi za Ulaya.

Mauritania na Mashariki ya Sudan hazina budi pia kuingizwa katika enco hili la jiografia. Kwa upande wa Mauritania, mambo yaliyopatikana ni pamoja na wasifu, shajara, tarihi za mahali hapo zilizo katika umbo la miswada na maelezo ya Wazungu kuhusu mwambao na selemu za mito kuanzia karne ya kumi na saba na kuendelea. Hati zisizokuwa zinajulikana hadi kufikia wakati huo zimegundulikana kutokana na utafiti wa Mukhtar Wuld Hamidun. Kadhalika inafaa pia kutaja "ensaiklopedia" ya mwanzoni mwa karne ya ishirini ya historia na utamaduni wa Kimsari uitwao *Al-Wasit* iliyoandikwa na Ahmad al-Shinqifi. Idadi kubwa ya vyanzo hivi, na hasa tarihi za Nema na Walata, inatupa mwanga mzuri juu ya Sudan ya Magharibi.

Katika Sudan ya Mashariki, uandikaji wa historia unaonyesha ulianza na *Tarihi ya Funj*, ambalo ni unukuzi wa mapokeo simulizi yanayohusu Usultani wa Funj katika karne ya kumi na tisa. Chanzo kingine muhimu kina shajara za vikundi mbalimbali vya Waarabu na kamusi maarufu ya wasifu ya wanazuoni wa Kisudan iitwayo *Tabakat*, iliyoitungwa na Dayfallah, ambayo imesheheni habari kuhusu maisha ya kijamii, kitamaduni na kidini katika ufalme wa Funj.

Mgeni wa mwanzo anayejulikana kuwa alifika sehemu hii, alikuwa David Reubeni ambaye alitembelea katika karne ya kumi na sita. Baadaye alifuatiwa na wachunguzi mahiri wa mandhari ya Sudan, kama vile James Bruce katika karne ya kumi na nane na al-Tunisi katika karne ya kumi na tisa ambaye alisonga mbele zaidi hadi kufikia Darfur. Hatimaye katika nusu ya mwanzo wa karne ya kumi na tisa, Sudan ilitembelewa na idadi kubwa ya wasafiri wa kigeni. Aidha vyanzo vya habari visivyo dhahiri kuhusu kanda hii vinapatikana katika nyaraka za kale za Cairo. Ama kuhusu miaka ishirini ya mwisho ya karne ya kumi na tisa nyaraka hizo zinapatikana katika kumbukumbu maarufu za Mahdiyya huko Khartoum.

## Ethiopia

Sura muhimu ya hali ya mambo katika Ethiopia ni ile ya mwendelezo wa vyanzo vya nje na vya ndani kadhalika. Ama kwa hakika katika baadhi ya vipindi fulani muhimu kuna vyanzo vya kimaandishi ambavyo vinakinzana. Waethiopia wanaamini kuwa uvamizi wa waislamu wa Ahmed Gran katika nusu ya mwanzo ya karne ya kumi na sita umcelezwa katika *Royal Chronicle in Ge'ez* (Tarihi ya Kifalme kwa Kigeez) ya Mfalme Lebna Dengel, ilihali Waislamu wanaamini kuwa unacelezwa na tarihi iliyoandikwa na karani wa Gran Arab-Faqili, mbali na taarifa zilizokusanywa na kuachwa na Wareno.

Kuanzia karne ya kumi na tatu na kuendelea, tarihi za kifalme za Ethiopia zina kumbukumbu za tawala za kifalme, na zinazoendelea hadi karne ya ishirini, mojawapo ikiwa ni Tarihi Kiamhariki ya Mfalme Menelik II. Pamoja na kazi hizi muhimu za uandishi wa historia, kuna maandishi mengine ambayo ni pamoja na historia za nyumba za watawa, maisha ya watakatifu, mizozo ya kidini, ushairi na ngano: *History of the Ghala* (Historia ya Wagala) iliyoandikwa karne ya kumi na sita na Mtawa Bahrey aliyeshuhudia Wagala wakiivamia, Ethiopia ni maandishi ya kipekee. Papohapo twamshukuru Hiob Ludolf, muasisi wa taaluma za Ethiopia katika Ulaya kwa kutokusanyia mojawapo ya historia kuu ya mwanzo ya Ethiopia. Ama kwa hakika Ethiopia (Ufalme wa Kikristo wa Prester John) iliwahamasisha Wazungu wengi tangu zama za Vita vya Msalaba kuzuru nchi hii wakija kama watalii, wamisionari, mabalazi, askari, wafanyabiashara, na majasiri. Miongoni mwa Wazungu hao walikuwamo Warusi, Wacheki, Waswidi na Warmenia na raia wa nchi za Ulaya zilizokuwa na nguvu zaidi.

Kuanzia nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa na kuendelea, maandishi muhimu ya kihistoria yanatokana na hati zilizokuwapo katika nyaraka za kale za nchi za Ulaya pamoja na nyaraka zilizoko Addis Ababa na hata Khartoum.

### *Afrika ya Kusini*

Huko Afrika ya Kusini pia, japo kwa sababu tofauti kabisa kulikuwa na vyanzo vya kimaandishi maridhiwa. Vipindi viwili vikuu vnaaweza kupambanuliwa. Kabla ya karne ya kumi na tisa, aghalabu vilikuwa ni vile vyenye asili ya kigeni vichache na vilishughulikia basa sehemu za pwani. Kuanzia karne ya kumi na tisa na kuendelea, vyanzo vinakuwa vingi na vinatokana zaidi na wenyeji. Vyanzo vya mwanzo kabisa vyaanzia karne ya kumi na sita na kumi na saba na vina maelezo ya mbaharia na walowezi wa Kidachii kwenye eneo la Rasi. Kisha kuanzia nusu ya pili ya karne ya kumi na nane na kuendelea, watu walianza kupenya ndani, na hii iliwezesha kupatikana kwa kazi kama ya Peter Kolb kuhusu Rasi ya Khoi. Ripoti nyingi mno zimekusanywa kama zile za L'Honore Nabcr. Kwa upande mwingine nyaraka za kale za wamissionari zinatoa maelezo ya undani zaidi ya jamii za Kiafrika. Mojawapo ya kazi hizo ambayo ni maarufu sana ni ile ya John Philip ambaye ahitumia maisha yake kutetea haki za Waafrika.

Katika karne ya kumi na tisa, kadri shughuli za kibiashara na kimisionari zilivyozidi kuenca ndivyo vyanzo vilivyozidi kuwa mahsusi. Kwa mfano Wasani, Wanama na Waherero wa Namibia walionyesha kama vile ni watu wa kushangaza! Kaskaziki mwa mto Orange, wamisionari na wavumbuzi waliokwisha kujifunza lugha za Kiafrika, waliandika kazi bora zenye ithibati ya hali kama zile za Robert Moffat na David Livingstone, na wakati huohuo G.M. Theal alitoa mkusanyo wa mambo yanayousu Lesotho. Papo hapo Waafrika wenyewe walianza kueleza mawazo yao moja kwa moja, kama vile barua zilizoandikwa na Mfalme Moshesh zinavyoonyesha. Ingawa zinatofautiapa kwa ubora, kuna idadi kubwa ya maelezo ya kigeni katika sehemu za bara za Natal na nchi ya Wazulu yakiwa ni pamoja na mkusanyo wa A.T. Bryant wa masinulizi ya mila za Wazulu.

Hata hivyo jambo linalojitokeza zaidi katika kipindi hiki ni kule kujihusisha moja kwa moja kwa kiwango kikubwa kwa Waafrika wenyewe wakiwa watendaji na mashahidi wa historia yao wenyewe. Mwanzo ya Waafrika yanadhibirika katika barua, magazeti, malalamiko rasmi na hati za kisheria, na katika juhudi za mwanzo za Waafrika kuandika masinulizi ya kihistoria. Mifano mikuu ya mwelekeo huu ni barua nyingi walizoandikiana watawala wa Kikoloni na inachifu wa Kiafrika kama vile Dingaana Catchwaye, Mzilikazi, Lobengula na wengine na vitu vingine kama sheria za wahenga za jamii ya Rehoboth na kitabu cha shajara (*diary*) cha Henrik Witbooi, ambazo ziliandikwa kwa Kiafrikaans.

Tangu mwisho wa karne ya kumi na tisa na kuendelea, magazeti ya mwanzo kwa lugha za Kiafrika yalichapishwa, ambapo mfumo wa utawala kwa makusudi kabisa ulikosolewa. Kwa mfano, gazeti la kila wiki liljulikana kama *Isidigini* (1870-188) lilikuwa chombo cha wazalendo wa awali kama vile tiyo Soga na *Inbo Zabantsundu* (Sauti ya Watu Weusi) lilianza kuchapwa 1884. Mgnoiki (tk 1924) mpiganaji wa Kiafrika dhidi ya Makaburu mwaka 1879 alichapisha ukumbusho wake huko Marekani, Hata hivyo historia za mwanzo zilizoandikwa na Waafrika wenyewe hazikutokea mpaka karne ya ishirini. Karibu historia zote kabla ya wakati ule zilikuwa za mazungumzo wahidia yaliyoandikwa na Wazungu, ambamo kurasa chache tu za ethnografia zilibusu watu weusi na zilifanywa kuwa utangulizi wa kile kilichodhaniwa kuwa historia halisi ya Afrika ya Kusini! Kwa hiyo kuna haja ya

kutumia ushuhuda mdogo wa Kiafrika uliopo, iwapo kuna azima ya kuandika historia thabiti ya kanda hii.

### *Marejeo ya nje ya masimulizi*

Jambo kubwa sana ni kule kupungua kwa vyanzo vya Kiarabu vikilinganishwa na vile vyenye asili nyingine.

#### Maandishi katika lugha ya Kiarabu na lugha nyingine za Mashariki

Leo Africanus aliandika kwa Kitahiano lakini ahijifanya Mwarabu na Mwislamu aliposafiri kuelekea Sudan ya Magharibi na ya Kati mwanzoni mwa karne ya kumi na sita. Ingawa maelezo yake kuhusu Afrika yana makosa, kwa karne tatu yalikuwa ndio marejeo pekee ambayo Ulaya ilikuwanayo kuhusu sehemu za ndani za bara la Afrika.

Maandishi ya baharia Ahmad Majid, yaliyoandikwa na rubani aliyemwongoza Vasco da Gama kutoka Malindi hadi India, pia ni chanzo muhimu cha mwanzo wa karne ya kumi na sita. Mbali na kuchora ramani ya topografia ya mwambao na kuonyesha njia za bahari, alitoa maoni makali kuhusu slughuli za Wareno katika Bahari Kuu ya Hindi. Kazi muhimu mbili juu ya Afrika Mashariki ni *Chronicles of the Fortess of Aden* (Tarihi ya Ngome ya Aden) iliyoandikwa na Abu Makhrama (k. 16) na *History of the Inlams and Seyyids of Oman* (Historia ya Maimamu na Masayidi wa Omani) iliyoandikwa na Salil ibn Razik (k. 19) Kusini mwa Sahara, hapakuwa na maandishi yoyote ya Kiarabu yenye maana hadi karne ya 19 lilipotokea juzuu la Kiarabu lililojulikana kama *Report on the Sudan* (Ripoti Juu ya Sudan) lililoandikwa na al-Tunisi, aliyetembelea Wadai.

Wanahistoria kadhaa wa Kimorocco waliandika mambo waliyoyaona kuhusu dola ya Songhai na nchi zilizopakana na sehemu za kati za Mto Niger, Idadi kubwa ya hati ambazo hapo awali zilikuwa hazijulikani zimegunduliwa katika maktaba za Kimorocco, na inaelekea kwamba pia kuna hati za namna hizo katika lugha za Kiajemi, Kituruki na katika lugha za Kihindi.

Katika karne ya kumi na tisa, mwanazuoni wa Kiazerbaijani alieleza safari yake kupitia Pembe ya Afrika na Maghribi katika kitabu kitiwacho *The Garden of Travels* (Bustani ya Safari). Hata hivyo, mapema kabla ya hapo, Waarmenia walikwishaingwa hamu ya kuvumbua bara hili, na mnano mwishoni mwa karne ya kumi na saba, mapadri wawili wa Kiarmenia walifunga safari kutoka Ethiopia hadi Morocco, kupitia Unubi, eneo la Ziwa Chad na Sudan ya Magharibi. Mmoja kati yao, Avatika Bagdasarian, aliandika maelezo ya safari yao. Pia tunamshukuru mwarmenia mwingine aliyetwa, Warga, kwa maelezo ya kusisimua ya safari aliyofanya mwaka 1821; akianzia Afrika Kaskazini, akavuka Sahara na kutokea kwenye upwa wa Ghana ya leo. Hati nyinginezo za Kiarmenia na Kijajia zimo katika maktaba na nyaraka za kale za jamhuri hizo za Kisovieti.

#### Maandishi katika lugha za Kizungu

Haiwezekani kuorodhesha japo kwa muhtsari kazi nyingi mno zilizofanywa na Wazungu kuhusu Afrika, ambazo zilitokea katika kipindi liki. Kwa hiyo ingefaa tujaribu kufanya tathmini ya jumla ya upeo na thamani ya maandishi.

Ama kuhusu insimamo wa ripoti za kijiografia zilizotolewa, hadi kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na sita. Wazungu hawakuyafahamu maeneo zaidi ya mwambao wa Afrika, falme za Kongo ya kale na Angola na nchi zilizo pembezoni mwa mto Zambezi. Katika

karne mbili zilizofuata, msisitizo uliwekwa zaidi katika kuchunguza kwa undani zaidi habari za watu wa mwambao, hasa wakati wa biashara ya watumwa, na dhamiri ikiwa hiyo tu. Baadaye, mwishoni mwa karne ya kumi na nane, Wazungu hawa walianza kusambaa barani Afrika na hatimaye kukatoka mnyang'anyiro wa Afrika.

Tukiangalia uwakilishi wa kitaifa wa waandishi wa historia ya Afrika katika karne mbalimbali twaweza kusema kwamba karne ya kumi na sita ilitawaliwa na Wareno, karne ya kumi na saba ilitawaliwa na Wadachi, Wafaransa na Waingereza; karne ya kumi na nane ilitawaliwa na Waingereza na Wafaransa zaidi, na karne ya kumi na tisa Waingereza, Wafaransa na Wajerumani. Hata hivyo nchi zote nyingine ambazo sasa zimeshaimarika kiviwanda zilishiriki katika biashara na kujihusisha katika kuifahamu Afrika, hasa Wataliano na Waadeni, na wananchi kutoka nchi kama Marekani na Brazil. Katika kutathmini maandishi yaliyotolewa na watu wote hawa, ni muhimu kutia maanani utaiifa wao na inabadiliko ya inwelekeo wa kitabia wa Wazungu kwa Waafrika.

Ingawa ni kurahisisha sana mambo, twaweza kusema kwamba waandishi wa Kireno walishawishika zaidi na hisia zao za Kikristo kuliko Waingereza wakati ambapo Wadachi walifikiriwa kwamba walikuwa yakinifu zaidi. Lakini mawazo ya Wazungu yalidhihirika kwa kiasi kikubwa baina ya karne ya kumi na sita wakati wanatariki wa Kireno walipokuwa wakiandika, na karne ya kumi na nane wakati wanazuoni wa Kidachi walipokuwa wakiandika historia. Si lazima kwamba picha waliyokuwa nayo kuhusu jamii za watu wesi ilikuwa yakinifu kadri wakati ulipopita. Mara nyingi hii ilikuwa kinyume cha ukweli. Mnamo karne ya kumi na tisa, kwa mfano, katika wakati wa Burton na Stanley, fikra zisizo na msingi wa kisayansi kuhusu majikwezo ya watu wcupe zilienea sana na mtazamo wa Wazungu wakati wa biashara ya watumwa ulipotoshwa sana. Hata hivyo mahitajio ya biashara hiyo yalifanya shughuli za Waafrika na tabia na mifumo yao ya serikali vitiwe inaanani, na ndiyo maana basi vyanzo vya nanna hiyo vina umuhimu wa pekee.

Aidha ilikuwa muhimu kuzingatia maslahi tofauti ya watu walioteka Afrika. Kwa kawaida, hadithi za wasafiri ziliandikwa na wavumbuzi au majasiri ambao katika kuridhisha wasomaji wao walielekea kusisitiza mno maajabu na hatari walizofaulu kuzivuka kwa ushujaa wao, wakitumia lugha ya kibaguzi kuelezea desturi walizozidhanika kuwa za kishenzi.

Kwa upande mwingine, wamisionari wa mwanzo walitaka sana kuzifahamu dini za Kiafrika, ili waweze kuziangamiza na badala yake kuziweka dini zao. Hata hivyo haja ya kuzimudu vizuri lugha za Kiafrika iliwapa nafasi nzuri ya kuelewa muundo wa kijamii ambao wakati mwingine maendeleo yake yalionyesha kwa kuyakusanya mapokeo simulizi. Wavumbuzi wafielekea kuwa mabingwa katika sayansi asili na walipendelea zaidi kutatua inatizimo makuu ya kijiografia ambayo yalikuwa hayajapata ufumbuzi. Kwa hivyo mbali na wavumbuzi maarufu kama Heinrich Barth na Mungo Park, waliobaki hawakutaka kujua maisha ya kijamii ya watu waliokutana nao katika safari zao. Hata hivyo historia za watu na au mataifa ya Afrika ziliandikwa na Wazungu kuanzia karne ya kumi na nane na kuendelea.

Baadhi ya mambo ya kupendeza katika vyanzo hivi vya masimulizi ya wazungu yanastahili kusisitizwa. Kwanza vinatoa incho mkuu katika uandishi wa tarehe ambapo ndipo pana udhaifu mkubwa katika mapokeo simulizi. Uamishaji sahihi wa tarehe ya mkutano mfalme na mvumbuzi waweza kusuka upya ruwaza ya kronolojia ya historia ya mtu mmoja au zaidi, ingawa wakati mwingine Wazungu wamesababisha makosa ya usibu kutokana na tafsiri zao za baadhi ya mila walizozandika kwa haraka mno.

Masimulizi pia yana umuhimu mkubwa kwa historia ya uchumi. Wazungu walihitaji ripoti yakinifu za njia za biashara, masoko, bidhaa na bei maliasili, kazi za mkono na kadhalika. Kwa upande huo ripoti za Binger ni mfano wa aina yake. Hata hivyo, kuna baadhi ya mifano ya maelezo ambayo yamekisiwa vibaya, pengine kwa kutaka kukuza umuhimu wa safari fulani.

Wazungu walikuwa katika nafasi nzuri kuelezea mambo waliyoyadhania kuwa "tabia na desturi" kama vile tambiko, mbinu za uzalishaji, mikakati na mbinu za kivita, na kadhalika. Lakini maranyingi waliyatazama mambo kijuujuu, kutoka nje. Ni hapo baadaye tu ndipo walipotambua kuwa kulikuwapo na ruwaza tatanifu ya mahusiano na wajibu wao katika muundo wa ndani na mienendo ya jamii za Kiafrika.

### *Marejeo ya ndani ya masimulizi*

Jambo lililojitokeza zaidi katika kipindi hiki lilikuwa ni kudhihiri kwa kazi zilizoandikwa na Waafrika Kusini mwa Sahara, mwanzoni kwa Kiarabu na baadaye kwa lugha za Kizungu. Desturi hii ya uandikaji historia inaonekana kutokea sawia kwenye kingo za Kusini mwa Sahara, kote katika Sahel na katika mwambao wa Bahari ya Hindi.

Tarihi ya mwanzo kati ya tarihi tatu mashuhuri za ki-Sudani ni *Ta'rikh al-futash* ambayo iliwa kazi ya vizazi vitatu vya ukoo wa Kati kutoka Jenne na ambayo inaelezea historia ya Songhay na mataifa yanayopakana nayo hadi uvamizi wa Morocco wa + 1591. Ie *Ta'rikh al-Sudan* yenye upeo na kina kikubwa iliandikwa na mwanahistoria wa Timbuktu, aitwaye al-Sa'di na inaelezea kipindi hichohicho na kuendelea hadi + 1655. Kazi zote hizi mbili ni za wanazuoni waliotopa wenye usuli mpana wa utamaduni na utambuzi mkubwa wa mambo ya kileo. Hata hivyo fikara muhimu ya kuzingatiwa ni kwamba tarihi hizo zinawakilisha mtazamo halisi wa mambo hata lau kama mtazamo huo unaathiriwa waziwazi na Uislamu.

Tuna historia yenye kina ya karne ya kumi na nane ambayo mwandishi wake hajulikani na ambayo inawahusu Mapasha wa Kimoroco walioishi Timbuktu (+ 1591-1751). Hata hivyo chanzo muhimu kilichotanguka ni kamusi ya wasifu wa wasomi wa Sudan ya Magharibi iliyotungwa na mwanazuoni mashuhuri Ahmad Baba aliyeishi Timbuktu na kufa + 1627. *Ta'rikh Say* iliyoandikwa na Ibn Adwar, ambayo tarehe ya kuandikwa kwake hajulikani kwa hakika, imejitokeza kuwa unukuzi wa mapokeo-simulizi.

Baina ya Sahel na msitu wa tropiki, wanazuoni waliendelea kutoa idadi kubwa ya kazi zilizoshughulikia tarihi, shajari za koo, wasifu na masuala ya kidini yaliyohusu eneo kati ya Sahel na msitu wa Tropiki. Mfano mmoja unaojitokeza wa kazi hizo ni *Kitab al-Ghunja* ambayo inaelezea maendeleo ya tangu mwanzoni ya Ufalme wa Gonja. Idadi kubwa ya kazi hizi zimeandikwa kwa Kiarabu, lakini nyingi ziliandikwa kwa Kiajama, yaani kwa lugha za Kiafrika kama vile Kihausa na Kidyula, kwa kutumia hati ya Kiarabu. Hali hii hii ilikuwapo katika sehemu za Fula, hasa Futa Toro na Futa Djalon. Idadi kubwa ya tarihi za Kifulfulde zimeletwa kwenye mkusanyo wa Gilbert Viellard katika IFAN uliopo Dakar au katika tarihi ya Futa ya Senegal, iliyoandikwa na Sire-Abbas Sow, mwandishi wa karne ya kumi na nane.

Huko Nigeria ya Kaskazini yafaa kutaja kazi ya kuvutia iliyoandikwa na Imam Ibn Fartuwa mwishoni mwa karne ya kumi na sita kuhusu utawala na vita vya Idris Alaoma, Mai wa Bornu. *Mahrma* ambazo ni barua za kifalme zilizotoa maslahi kwa familia za viongozi wa Kidini ni ushuhuda wa kipekee wa hali ya kiuchumi na kijamii. Tarihi nyingine

ndogondogo na shajara zinapatikana vilevile, hasa kutokana na uamsho wa kazi za maandishi katika karne ya kumi na tisa wakati ambapo lugha za Kiafrika kama vile Kihausa, Kifulfulde, K'ikanuri, Kimandara na Kikotoko zilitumika kwa wingi. Idadi fulani ya kazi hizi ziliandikwa na viongozi wa *Jihad* ya Wafulani ambayo ilikuwa ni harakati za kisiasa na kidini zilizoanzishwa na Uthman dan Fodio.

Tarihi za miji ya Kihausa ya Kano, Katsina, Abuja na kadhalika, ziliandikwa mwishoni mwa karne ya kumi na tisa lakini zinatimia data za kipindi kilichotangulia. Vile vile kuna tarihi iliyoandikwa kishairi kwa Kifulfulde inayoelezea maisha ya mgeuzi mkuu wa Kitukolor al-Hajj Umar Tall, ambaye ndiye mwandishi wa *Rimah Hizb al-Rahim* (Mikuki ya Chama cha Mungu Mwenye Huruma) ambamo mna vidokezo kuhusu maisha katika Sudan ya Magharibi.

Takriban picha hiyohiyo yaweza kuonekana kwenye mwambao wa Afrika Mashariki. *Kilwa Chronicle* (Tarihi ya Kilwa) iliandikwa katika karne ya kumi na sita, ambapo tarihi nyinginezo zina data za karibuni zaidi. Hata hivyo, hizo pia zina maana kwa sababu zimejumisha maelezo ya kipindi kabla ya majilio ya Wareno. Tangu 1965, zaidi ya kurasa 30,000 za miswada ya Kiswahili au Kiarabu zimeonekana. Hata mashairi huweza kutupa mwanga mathalani, shairi la Kiswahili la *al-Inkishafi* linaloelezea kujitokeza na kufisia kwa Pate.

Maandishi ya Waafrika kwa lugha za Kizungu yalianza kutokoa kuanzisa karne ya kumi na nane na kuendelea. Waandishi wa Fante kutoka pwani ya Ghana ya sasa kama vile Jacobus Capitein na A. William Amo, walianzisha juhudi zilizofuatwa na kazi kubwa zilizoandikwa na watumwa waliokombolewa kama Ignatius Sancho, Ottobach Cugoana na Olaudah Equino (au Gustavus Vasa) ambao walitetea ukomeshaji wa biashara ya watuniwa na papo hapo wakitoa maelezo ya kuthaminiwa kuhusu maisha ya watu weusi katika Afrika na Ulaya. Shajara ya Antera Duke, mfanayabiashara wa Calabar, imejaa maelezo yenye kina yaliyotokana na maisha ya kila siku mojawapo ya bandari kuu za watumwa za wakati huo.

Ama kuhusu Madagascar yafaa tutaje shajara iliyoandikwa kwa hati za Kiarabu (*sura-be*) na Mfalme Radama I (+ 1810-1828) na maandishi ya miaka ya kati ya karne ya kumi na tisa katika hati za Kirumi za mamwinyi wawili wa Kimcrina, Raombana na Rahaniraka ambao wanatoa picha jinsi wenyaji wenyewe walivyoona maisha ya siku hadi siku katika ufalme.

Katika muda wote wa karne ya kumi na tisa, idadi kubwa ya kazi ziliandikwa na Waafrika au Wamerikani wenye asili ya Kiafrika, ambao maelezo ya maisha ya Waafrika yaliunganishwa na malumbano ya junla. Miongoni mwa waandishi hao walikuwapo Samuel Crowther, Myoruba, Thomas B. Freeman, Suriama na Benjimini Anderson, Mlaiberia. Kundi la pekee ni lile la akina Edward W., Bluden na James Africanus ambao ni viongozi waanzilishi wa harakati za kuamsha dhamiri ya Mwafrika.

Hatimaye tunakifikia kizazi cha wanahistoria halisi. Mmoja kati yao alikuwa Abbe Boilat, chotara kutoka St. Louis, Senegal ambaye maandishi yake *Esquisses Sénégalaises*, yana liabari nyingi za kichnografia. Alifuatiwa na C.S. Reindorf, Mgâ aliyandika *History of the Gold Coast and Asante* (Historia ya Gold Coast na Asante) na Samuel Johnson, aliyandika *History of the Yoruba* (Historia ya Wayoruba).

Ingawa kazi hizi za Waafrika zilionesha kiwango fulani cha upendeleo walipozungumza kupinga ubaguzi wa rangi au mambo ya kisiasa au dini, hata hivyo ni kazi zenye umuhimu usokadirika, kwani zinawakilisha sehemu tu ya mambo yaliyojificha; sura nyingine ya historia ilifichwa na maelezo marefu ya wageni katika bara hili.

## *Marejeo ya nyaraka za kale, kumbukumbu za watu binafsi, ripoti za siri na kumbukumbu nyinginezo*

Kinyume na vyanzo vya masimulizi ambavyo huwa na madhumuni dhahiri, ushuhuda huu yakunifu una hati zisizokuwa na mapendeleo wala mabishano zifanyagwa kumbukumbu za mahusiano ya kiuchumi na kijamii zilizojengwa kutokana na mawasiliano ya barua, kumbukumbu za miamala, takwimu, mikataba na makubaliano, batli, na kadhalika. Ingawa pengine huwa vigumu kupambanua kati ya aina hizo mbili za vyanzo, maoni yaliyokita kwamba hapakuwapo na nyaraka za watu binafsi katika Afrika yamethibitishwa kuwa ni batilifu. Uchunguzi wa karibuni umegundua na kupambanua mkusanyo mkubwa wa vyanzo vya aina hiyo lakini bado kuna vingine vingi ambavyo vinaweza vikagunduliwa katika nyaraka za Afrika, Ulaya na Asia.

Hebu kwanza tutazame hati zilizoandikwa kwa Kiarabu. Kabla ya karne ya kumi na tisa, hati hizo zilikuwa adimu, ingawa tuna barua zilizoandikwa na Sultani wa Uturuki kwa Mai Idris wa Bornu (+ 1578), zilizogunduliwa katika nyaraka za kale za Kituruki na barua zitokazo kwa Sultani wa Morocco kwenda kwa Askija wa Songhay na Kanta wa Kebbi. Kiarabu kilikuwa lugha ya kibalozi sio tu katika miliki za Kiislam za Sudan, bali pia kati ya falme za Hinaya ya Waashanti ambazo ziliwatumia waandishi wa Kiislam kuwaandikia barua machifu wa Kaskazini na Wazungu wa inwainbao. Masijala haya ya Waarabu pia yaliweka kumbukumbu za utawala na maamuzi ya kisheria, mahesabu na kadhalika. Mfano mmojawapo kutoka mwambao wa Bahari ya Hindi ni wa mkataba uliofanywa + 1776 kati ya mfanyabishara wa watumwa wa Kifaransa aitwaye Morice na Sultani wa Kilwa.

Karne ya kumi na tisa ilishuhudia mwongezeko mkubwa wa barua nyingi za Kiarabu katika bara lote, kufuatia kuanzishwa kwa tawala kama zile za usultani wa Sokoto, tawala ya Liptako, dola na falme za al-Haji Umar, Ahmadu Seku, Lat Dior, Mahmada Lamine, Samori, Rabih na wengineo. Ama kwa hakika, tawala za kikoloni ziliwasiliana na nchi hizi za Kiarabu. Kuna barua zilizopo hadi sasa walizoandikiana Pasha wa Uturuki aliyekuwa Tripoli na Masheche wa Bornu, Sultani wa Darfur na Misri na Timbuktu na Morocco. Nyaraka za kale zenye barua za aina hiyo zipo Zanzibar, ingawa ni chache.

Matini yaliyoandikwa kwa hati za Kivai yamo katika kundi hilo. Aina hii ya mwandiko ilivumbuliwa kiasi cha + 1833 na Momolu Duwela Bukele na ulienca haraka miongoni mwa Wavai hata ilipofikia mwisho wa karne karibu wote walizijua hati hizo na walizitumia wakati luo kwa mawasiliano yao rasmi na ya kibinafsi, vilevile katika kutunza mahesabu na kuziandikia sheria za jadi, methali na hadithi. Majirani kama Wamende, Watoma, Wagueze na Wabassa walitohoa hati za Kivai katika lugha zao wenyewe na kuzitumia kwa madhumuni hayo hayo.

Mwanzoni mwa karne ya ishirini, Sultani Njoya wa Bamum, huko Cameroon, alivumbua hati ambazo alizirekebisha inara nne lakini kinyume na hati za Kivai hazikuenezwa sana bali zilitumiwa na kikundi kidogo tu cha washauri wa Kitala. Hata hivyo, Njoya aliandika juzuu kubwa ya historia na mila za watu wake kwa hati hizi. Hatuna budi pia kuzitaja matini za Kinsibidi, kutoka Nigeria ya Kusini Mashariki, ambazo zilikuwa na maandishi nakshi ya mahali patakatifu na katika aina maalum ya lugha iliyotumiwa miongoni mwa wanachama wa vikundi fulani vigeni.

Maandishi hayo katika lugha ya Kizungu yanaanzia karne ya kumi na sita hadi sasa. Maandishi haya yapo katika lugha kadhaa, ni mengi sana na yameenea duniani kote katika sehemu nyingi tofauti ikiwemo hifadli za nyaraka za kale, maktaba na mkusanyo ya watu



binafsi. Hali hii ya mambo inaifanya hazina hii iwe ngumu kutumika, hasa pale panapokuwa hapana mwongozo wala katalogi. Hii ndiyo sababu Baraza la Kimataifa la Hifadhi za Nyaraka za Kale (*International Council of Archives*) chini ya fadhila za UNESCO, lilijitolea kutayarisha miffululizo na miongozo ya vyanzo vya historia ya Afrika, ili kuongeza upatikanaji wa mkusanyo wote wa vyanzo vilivyopo kwa kuonyesha vipindi vinginevyo mbali na vile vya ukoloni. Miffululizo hiyo ina inajuzuu kumi na mawili yenye vyanzo vya kimaandishi kuhusu historia ya Afrika Kusini mwa Sahara katika nchi za Ulaya Magharibi na Marekani. Kama ambavyo Joseph Ki-Zerbo alivyosema kwa usahihi katika utangulizi wake wa miffululizo hiyo 'katika mapambano ya kugundua upya kale ya Afrika, *Guide to the Sources of the History of Africa* (Mwongozo wa Vyanzo vya Historia ya Afrika) ni silaha mpya ya kimkakati na kimbinu'. Miongoni mwa juhudi nyingine maarufu za aina hiyohiyo ni miongozo mitano ya historia ya Afrika Magharibi yenye kuelezea hifadhi za nyaraka za kale za Ureno, Utaliano, Ubelgiji na Uholanzi, Ufaransa na Uingereza.

Mikusanyiko mikubwa na yenye manufaa zaidi ni inatoleo ya nyaraka za kale zilizo kamili. Panoja na kazi ya Paiva na Mansu katika karne ya kumi na tisa, kuna mikusanyo mikubwa ya hati za kimisionari, hasa kutoka katika nyaraka za kale za Kireno zilizokusanywa na A. da Silva Regon na A. Brasio. Mkusanyiko wenye sifa ya kudumu uliokusanywa kwa juhudi za pamoja baina ya Ureno za Zimbabwe (zamani Rhodesia) umejumuisa hati za Wareno kuhusu kusini-mashariki ya Afrika zilizokamilika na zenye tafsiri ya Kiingereza. Vile vile kuna mikusanyo mingine maalum kama vile ya *British Parliamentary Papers* (Karatasi za Bunge la Uingereza) zilizoandikwa na J. Cuvelier, na ya L. Jadin juu ya hati za Catican zinazohusu Kongo ya kale na uchunguzi wa sera ya Uingereza katika Afrika Magharibi na sera ya Utaliani katika pembe ya Afrika.

Mataifa yote huru ya Afrika yana hifadhi za nyaraka za kale za umma zinazohusu kipindi cha ukoloni ambazo kwa sasa hivi zinaainishwa na kufafanuliwa. Uchapishaji wa mfululizo wa miongozo kwa hifadhi za nyaraka za kale za umma na za watu binafsi katika Afrika ni jambo lenye kuhitajika haraka. Ni dhahiri kwamba kuna mapengo katika hifadhi za nyaraka za kale za Kiafrika, kwani zimeainishwa hivi karibuni tu, na vitu vingi vimepotea, lakini zina faida kubwa kwa sababu kimsingi zina hati zinazohusiana na hali ya Afrika kuliko ile ya kuhusiana na sera ya kikoloni tu. Zaidi ya hayo zina mambo yanayohusu kipindi kabla ya ukoloni pamoja na idadi kubwa ya hati zitokanazo na Waafrika wenyewe. Kwa hivyo ni za muhimu kabisa katika kujenga intazamo mpya wenye urari kuhusu Afrika ya wakati uliopita.

Kwa kuhitimisha, twapaswa kutaja aina nyingine ya vitu tukianza na hati ya kikatografia. Ramani zilizozakshiwa na kutiwa rangi zenye tarehe inayoanzia karne ya kumi na sita zimeenezwa katika maktaba nyingi na hifadhi za nyaraka za kale katika Ulaya. Ni vyanzo ambavyo haviwezi kupata badala yake katika kufuatia mwendelezo wa majina ya mahali, kwa sababu vina majina ya mahali ambapo sasa pametoweka au panajitokeza katika mapokeo simulizi tu. Kwa mfano Wabantu fulani wa Mashariki wanadai kuwa kwa mujibu wa mapokeo chimbuko lao ni mahali palipojulikana kama Stungwaya. Ingawa jina hili sasa limepotea, linaonekana katika baadhi ya ramani za zamani. Ramani kama hizo hutoa taarifa kuhusu ngawiko wa mbari, mipaka baina ya dola, majina ya mito na milima na sura ya kitopografia; vyote hivyo vikiwa na umuhimu wa kihistoria.


Hii inadhihirika katika kazi maarufu ya Yusuf Kamal, *Monumenta Cartographica Africae et Aegypti*, ambayo pia ina masimulizi yanayoishia mwanzoni mwa karne ya kumi na sita. Hii ndiyo sababu Joseph Ki-Zerbo yu sahihi anaposisitiza kwamba mkusanyo wa

ramani zote za zamani za Afrika zichapishwe katika Atlasi zikiwa na sherehe.

Data za lugha - aina nyingine ya vyanzo - mara nyingi hupatikana kwenye vyanzo vya maandishi ama kwa kuashiria tu au kwa namba iliyowazi, kama vile katika umbo la orodha za maneno kutoka Lugha za Kiafrika. Faharasa za namna hii zinapatikana kuanzia karne ya kumi na tano na kuendelea mpaka karne ya kumi na tisa. Chapisho muhimu kabisa katika uwanja huu ni mkusanyo maarufu wa Koelle wa msamiati wa takriban lugha 160.

Hati za maandishi zinazohusiana na lugha za Kikongo zilichapishwa kuanzia karne ya kumi na sita na kuendelea. Kazi kama hii zina vipengele vya kihistoria, kwa sababu, mbali na kuwakilisha mazoezi katika glotokronolojia zinawcwa kuzingatia majina ya kijamii na kitamaduni kufuata maendeleo ya historia.

Kwa ufupi, kinyume na upotofu ulionea, vyanzo vya maandishi vya historia ya Afrika ni vingi sana ingawa havijachunguzwa kwa upana. Kuna haja ya kufanya utafiti mwanana mapema.



## *Mapokeo simulizi na mbinu zake*

### *Ustaarabu simulizi*

Kimsingi staarabu za Sahara na maenco yaliyo Kusini mwake zilikuwa staarabu simulizi. Hata hivyo litakuwa ni jambo la upuuzi kuuchukulia ustaatabu simulizi kama kitu chenye kasoro eti kwa sababu hapakuwepo na maandishi. Kufanya hivyo ni sawa na kukubaliana na usemi wa Kichina kwamba "maandishi japo ya wino hafifu ni bora kuliko kauli nzito".

Katika staarabu ambazo hazikuwa na maandishi, simulizi ambazo ndizo zilikuwa chombo cha kupashiana habari muhimu katika maisha ya kundi la watu, zilikuwa, na umuhimu wa pekee; umuhimu ambao haukueleweka katika jamii zenye maandishi. Katika hizi staarabu simulizi kusema au kukipa kitu jina kulikuwa sawa na kuigiza, kumiliki au kuumba. Kwa hivyo basi matini ya msingi katika mapokeo simulizi hayawezi kufasirika kwa namna moja matini ya kimaandishi kwani matini ya mapokeo simulizi huwa yanajihusisha moja kwa moja na ujenjaji wa historia. Kama alivyosema mwanazuoni wa Zaire, Fu Kiau, iwapo tutataka kuyafasiri mapokeo simulizi vilivyo itabidi yahuishwe kama yalivyokuwa wakati wasinuliaji wake asilia walipoyasema. Hii ni fikra ambayo wana-mapokeo simulizi maarufu kama vile Amadou Hampâté Ba na Boubou Hama pia wanaiafiki.

### *Maumbile ya mapokeo simulizi*

Mapokeo simulizi yaweza kusemwa kuwa ni ushuhuda uliotolewa kwa mdomo na kupokewa toka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Sifa zake maalumu ni kule kutolewa kwa mdomo na namna yanavyorithishwa. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba mapokeo simulizi huwa rahisi kupotoshwa kuliko kumbukumbu za ki-maandishi ambazo huhifadhiwa katika vitu halisi kama vile miswada. Yafaa pia kusema hapa kwamba yawezekana kukawa na aina mbalimbali za maandishi juu ya tukio moja; na pia kinyume chake kuna aina zisizobadilika badilika za mapokeo simulizi.

Yawezekana kabisa chanzo cha mapokeo simulizi kikawa aina maelezo ya kitu ambacho mtu kashuhudia, au tetesi zisizokuwa na insingi ambazo mtu kazizusha mwenyewe tu; au pengine yawezekana chanzo kikawa ni namna tofauti ya kufasiri inasimulizi fulani kiasi kwamba inatokeo yake yanakuwa mapokeo mapya kabisa. Hata hivyo mapokeo yaliyo na umuhimu hasa ni yale tu ambayo yamekitwa katika maelezo yaliyoshuhudiwa. Wanahistoria wa Uislamu waligundua mbinu hii ya uhakiki walipokuwa wakizichunguza *Hadithi au Semi za Mtume* zilizokusanywa na wafuasi wake. Ukubalifu wa *Hadithi* lutegemea msururu wa

watu (Isnadi) walioko baina ya mwanazuoni aliyeiandika na mmojawapo wa masahaba wa Mtume. Vigezo vya kawaida vya kanuni za tahakiki za Kihistoria vilitumiliwa katika kila kiungo katika msururu mzima: Je yawezekana kweli kwamba yule anayetoa ushahidi alifahamu hadithi au mapokeo hayo? Je, alikuwa na sababu yoyote ya kuipotosha? Je, yawezekana kweli kwamba yeye aliisimulia na kama hivyo ndivyo; je aliisimulia lini, wapi kwa namna gani?

Kwa hivyo, basi, mahitaji muhimu kabisa ya mapokeo simulizi ni kwamba ni lazima yawe yametolewa kwa mdomo na yawe yamerithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine. Madhumuni ya mapokeo simulizi si muhimu. Masimulizi mengine, kama vile nyaraka za kale, hayakukusudiwa watu wa wakati luu au wa wakati ujao. Umuhimu na thamani yake vimekitwa katika ushahidi usiodhamiriwa juu ya mawazo, imani na itikadi mbalimbali, miundo ya jamii, mienendo na jinsi jamii ilivyokuwa ikiutazama ulimwengu katika kipindi fulani maalumu.

### *Mapokeo kama kazi ya fasihi*

Jambo la kwanza kuzingatiwa ni fani iliyotumiwa katika kuwasilisha ujumbe kwani kanuni zinazotumiwa katika kuunda fani zinaathiri maudhui na hatimaye huathiri thamani ya mapokeo yenyewe. Kuna tanzu nne maalumu za mapokeo kutegemeana na kufungika au kutofungika kwa maudhui na fani:

1. Inapokuwa maudhui na fani vimefungika tunapata matini zisizobadilika badilika ambazo watu huhifadhi kimoyomoyo na hurithishwa jinsi zilivyo.
2. Inapokuwa maudhui yamefungika lakini fani haikufungika, maana huwa haibadiliki lakini mpangilio huweza kubadilika mradi tu usikitie ila kiini cha hadhithi/masimulizi au maneno muhimu kama katika methali, sala au shajara za mfuatano wa watawala. Katika hali hii, [na hasa zaidi katika hali iliyoelezwa katika (1) hapoo juu] maneno halisi ambayo yanaweza kufuatiliwa chimbuko lake hadi katika masimulizi asilia yanaweza kufasiriwa kihistoria kana kwamba yalitokea katika kumbukumbu za maandishi.
3. Inapokuwa maudhui hayakufungika lakini fani inalazimika kufuata vina, mistari au beti kunakuwa na namna mbalimbali za kufasiri matini hizo. Lakini hata hivyo bado inawezekana kabisa kuunda upya kiini cha matini.
4. Kwa upande mwingine inapokuwa maudhui na fani vyote havikufungika kunatokea aina nyingi za mipangilio, fasiri mbalimbali, maumbo mbalimbali na kuendelezwa au kubadilishwa kwa matini. Hata katika hali kama hizi uhuru wa msanii au mwana-mapokeo unaweza kubanwa na nguvu za kijamii ambazo humlazimisha kwa kiasi fulani kufuata muundo fulani maalumu. Yawezekana, basi kuiondoa ile mitindo ya fasiri inayoonekana kuvutia tu kwa kutumia uhakiki uliokitwa katika kanuni za kifasili ambazo zimetumiwa katika kueleza matini. Kwa kufanya hivyo inawezekana kugundua hitilafu fulanifulani na hatimaye kupata maana halisi. Kitu muhimu hapa ni yale maneno ya msingi ambayo yanahusu sulubu za miundo na ambazo hazina budi kufasirika tu kwa kuangalia muktadha.

Wakati mwingine viko visa vinavyosimuliwa kwa namna moja kote Afrika. Kwa mfano mapokeo ya Waluba katika Zaire, Wafulani na Wamossi katika Bukina Fasso na Wahausa katika Nigeria ambayo husimulia kisa cha chifu ambaye anajaribu kumwangamiza mpinzani

wake kwa kumkaribisha akac kwenye mkeka ambao umefunika shimo lenye vyuma vilivyochongwa na vyenye ncha kali. Hii haina maana kwamba simulizi kama hizi zikataliwe moja kwa moja; tukiachilia mbali ile hila inayotuniwa, au mandhari yenyewe, kitu muhimu kinachoelezwa ni kwamba mpinzani anaangamizwa.

Uhakiki wa kifasihi utatilia maanani vikwazo vya kiumbuji ambavyo vinamkabili mtunzi. Iwapo mtunzi atavizingatia zaidi vikwazo hivi kwa kiasi cha kumfanya ashindwe kuyasimulia matukio kwa usahihi kutakuwa na mabadiliko makubwa katika ujengaji wa masimulizi. Hali hii ikitokea itakuwa inadhihirisha vionjo vya jamii na ufundi wa mtunzi. Inapokuwa kuna aina mbalimbali za simulizi, simulizi iliyo sahihi zaidi itatambulika kutokana na ukweli kwamba haifuati mtindo wa muundo wa kisanii ufiopo, kama ambavyo aina ambayo inakinzana na taratibu za mwenendo wa kimapokeo wa jamii ya wakati huo inavyoweza kuwa na ukweli zaidi kuliko aina nyingine.

### *Kiunzi cha mapokeo katika jamii*

Katika jamii zilizo na hati za maandishi kila jambo muhimu hurithishwa kwa kizazi kifuatacho kwa njia ya inaandishi; katika jamii zisizokuwa na maandishi mambo hayo hurithishwa kwa njia ya simulizi. Maelezo kama haya huwa yamekitwa katika misingi ya kuihuisha jamii na wala hayakukusudiwa kuwa burudani tu au kuwa masimulizi ya mapokeo.

Katika mwelekeo huo mtu hushawishika kutaka kutofautisha mapokeo ya jamii zilizo na muundo wa kidola na zile "zisizo na muundo huo. Lakini jaribio la mwainisho wa namna hii haliwezi kufika mbali. Hata katika jamii za makundi yadaiwayo kuwa ya aina moja kunaweza kuwa na tofauti kubwa; chukulia mfano wa jamii zenye mtindo wa "makundi ya rika" kama vile Wamasai (Kenya-Tanzania), Wacambu (Kenya) na Waoromo (Kenya-Ethiopia). Wagouro wa Ivory Coast wana mapokeo ya kinasaba lakini nao pia wana mapokeo ya kihistoria ambayo hurithishwa na jamii ya siri tu. Halidhalika Watonga wa Zambia wana utaratibu wa kurithisha masimulizi lakini nao pia wana mapokeo ya vituo maalumu vya tambiko ambavyo vinadhibitiwa na waganga wa mvua tu. Kwa hiyo mianisho ya kinadharia pekee yake haiwezi kuaminika.

Mapokeo huwa na shughuli nyingi za kijamii, nazo huathiri maudhui ya mapokeo yenyewe. Mapokeo rasmi ni pamoja na shajara mbalimbali, orodha ya wafalme na maelezo kuhusu asili ya falme mbalimbali pamoja na marupurupu ya tani mbalimbali. Mapokeo rasmi pia huweza kujumuisha haki za kumiliki ardhi, taratibu za kimila kuhusu maji, wanyama, miti, wageni, n.k. Mapokeo ya makundi binafsi kama vile familia wafuasi wa dini fulani, vyama vya mafundi, n.k. hayahifadhiwi sana lakini yanaweza kutumiwa katika kuthibitisha ni kwa kiwango gani mapokeo rasmi yanaweza kuaminika.

Kama tutazingatia vikwazo vya kifasihi vilivyopo katika dhima na fani inawezekana kabisa kutengeneza katalogi ya aina mbalimbali za ushahidi simulizi na maelezo potofu yaliyotolewa kwa kila aina. Hii yawezekana kwa kuuliza maswali mafupimafupi kama: "Tulianzaje kulima mahindi", "Je, maleba ya mchezaji huyu yalitoka wapi?" n.k.

Hata hivyo kusema kwamba kuna uwezekano wa upotoshwaji wa habari haina maana kwamba upotoshaji huo ulitokea. Thamani ya mapokeo fulani haiwezi kukataliwa bila ya kuwa na ushahidi kuwa upotoshaji ulitokea kweli au kwamba uwezekano wa kupotoshwa habari ni mkubwa sana. Haitoshi tu kudai kama walivyofanya Goody na Watt kwamba jamii simulizi huyaondolea mbali katika kumbukumbu zao za pamoja mambo yote yanayoweza kuwakashifu. Kwa mfano kuna mapokeo ambayo yanaonyesha kukiri kwa watu katika

kushindwa au kuhamia katika maeneo ambayo tayari yalikuwa na wenyeji wake, au wakati mwingine ushahidi unaoeleza mazingira ya kijiorafia ambayo hayana uhusiano kabisa na hali ilivyo hivi leo. Na zaidi ya hapo basi hali ya watu kujaribu kufuatilia mbali jambo lolote ambalo ni kinyume na mawazo na maslahi ya jamii fulani, au pengine tabaka tawala, huhitokeza yasi katika jamii zisizokuwa simulizi. Hii ni kaida ya kilimwengu. Hivyo ni mawazo yasiyopevuka kudai, kama wanavyofanya watunzi waliotajwa hapo juu, kwamba kiwango cha ujuzi alionao kila mtu mzima katika jamii simulizi karibu ni kilikile. Haya ni madai yasiyokuwa na usingi na ambayo huufumbia macho ukweli kwamba katika kila jamii kuna watu wenye ujuzi wa fani mbalimbali kama vile ufundi, siasa, sheria au teolojia ambao wanajua mambo mengi ambayo wenzi wao hawajajui kabisa. Kila mbari ina watu wenye hekima. Kwa mfano miongoni mwa Wakuba wa Zaire tulikutana na wanaume watatu ambao kwa kutumia msingi wa mfumo uleule wa ishara waliweza kuainisha falsafa za aina tatu tofauti kabisa. Miongoni mwa watu wengi, mapokeo ya siri ni mambo yanayofahamika kwa makundi fulani tu ya siri. Kwa mfano ukoo wa Kifalme wa Asante ulijua mapokeo kuhusu asili yao ambavyo watu wa kawaida hawakujua chochote kuhusu swala hilo. Huko Rwanda wataalamu wa Kibiiru ndio walijua tanbiko za Kifalme: na hata hivyo ukamilifu wa mahitajio yote ya tambiko hizo ulipatikana tu walipokuwa wamekusanyika pamoja, kwa sababu kila kundi la Wabiiru lilijua sehemu tu ya matambiko hayo. Ada ya mapokeo ya siri lupatikana karibu katika matambiko yote ya kuwatawaza Wafalme kila mahali Afrika.

Kila mapokeo yana sura yake ya kijamii ambayo sharti yafahamike vizuri ili kuweza kuifasiri matini sawasawa. Wataalamu wa kuhifadhi matini muhimu hupeua mafunzo na mbinu maalumu -mara nyingi katika mtindo wa kughani - ili waweze kuhifadhi masimulizi yaliyo marefu sana. Aidha mara nyingi watu hawa huwa wamezungukwa na watu mbalimbali ambao nia yao ni kuhakikisha kwamba wataalamu hao wanafanya kazi yao vizuri. Wanashajara, mabingwa wa kupiga ngoma, walinzi wa makaburi, wachungaji wa dini za kitaifa n.k. hua hawajifanyii kazi jinsi wapendavyo; daima utekelezaji wa shughuli zao huwa unachunguzwa kwa makini na watu wengine. Ndiyo kusema basi kwamba kwa kuvichunguza vipengece vyote vinavyoiunga jamii, viwe ni vya mbinu (ya kurithisha mapokeo) au vya kijamii (kuwepo kwa vikundi vya watu vyenye hamu na nia ya kulinda maslahi ya jamii) mwana-historia anaweza kukisia ukubalifu wa mapokeo kwa usahihi kadri iwezekanavyo.

Kigezo kingine muhimu ni kuangalia ni mara ngapi mapokeo hayo hutekelezwa. Kwa mfano tambiko la sigi lifanywalo na Wadogoni wa Mali hurithishwa mara moja tu katika kila kipindi cha miaka kama sitini hivi. Kuna uwezekano mkubwa wa kubadilikabadilika kwa maudhui yake kila tambiko hilo linapofanywa kuliko ilivyo katika mapokeo ambayo hurithishwa katika sherche ya kila mwaka kama ifanyikavyo huko Nigeria Kusini. Lakini hata hayo ya kila mwaka hutegemea mahitajio ya jamii yenyewe. Kama jamii itakazia udhibiti wa uthabiti wa mapokeo yenyewe basi utendaji wake wa mara kwa mara utaimarisha uthabiti huo. Lakini iwapo jamii haitatilia mkazo udhibiti wa uthabiti wa mapokeo basi utendaji wa mara kwa mara wa matambiko utapotosha urithishaji wake kwa haraka zaidi kuliko matambiko yale yanaotendwa mara chache. Ukweli huu hujidhihirisha katika nyimbo maarufu na katika masimulizi yahitajikayo zaidi.

### *Kiunzi akili cha mapokeo*

Kiunzi akili hiki kimeundwa na mkusanyiko wa mawazo ambayo kwa kawaida hayadhamiriwi kwa sababu yamezoclewa na yamekuwa ruwaza au mfano wa jinsi watu

wanavyofikiri katika mazungumzo. Kwa mfano wafalme wote wa ufalme fulani wataonekana kuwa na sifa za namna moja ambazo hujitokeza katika mienendo yote ya kifalme. Mfalme mmoja anaweza kuwa "mtaalamu wa mazingaombwe" mwingine akawa "mwadilifu" na mwingine akawa "shujaa" sawa na wacheza sinema wanavyojibainisha katika filamu za Kimagharibi! Matokeo yake ni kwamba sifa zote za ushindi hupewa yule mfalme shujaa hata kama aliyelea ushindi huo alikuwa yule mfalme mwadilifu, na kadhalika.

Ndiyo maana basi kuna unuhimu wa kuuchunguza kwa makini mfumo mzima unaofumbata itikadi za watu, nyadhifa zao na dhima zao ili kuweza kuupata ujumbe uliomo katika mapokeo. Kwa mfano McGaffey amegundua kwamba Wakongo wana mfumo wa msingi wenye nyadhifa nne zilizo kamili na zenye kukamilishana -wako waganga, wapiga ramli, machifu na mtume. Halikadhalika katika mapokeo ya Ghuba ya Benin; dhima inayopewa nafasi ya kudura, kuamini, ukarimu na kulaumu wivu na vidokezo vya uchawi vinavyoandamana nao, vyote ni maadili ya kifalsafa au itikadi za watu zinazotawala namna zote za mazungumzo. Mpaka hapo yatakapotenganishwa na misingi yake, katika jitihada za kujaribu kugundua ni kwa kiasi gani matini simulizi yanaakis tu kitu chenyewe, haiwi rahisi kupata fasiri ya mapokeo inayokidhi haja. Kuna maswali ya msingi ambayo hayana budi kuulizwa, kwa mfano watu wana mawazo gani kuhusu vitu kama wakati, muda, ukweli wa kihistoria na vyanzo vya matukio.

Dhana ya wakati imekwishajadiliwa katika sura ya 2. Hata hivyo inavyooleweka katika familia dhana ya wakati, ambayo huhesabiwa kwa kufuata lini mtu fulani alizaliwa na matukio gani muhimu yalikuwepo yanaweza kuturejesha nyuma vizazi vitatu au vinne tu. Kutokana na hali kama hii ni dhahiri kwamba uwezekano mkubwa wa kurejea nyuma unapatikana katika taasisi zenye wingi mkubwa wa watu kama ilivyo katika dola za Sudan. Hivyo basi namna wakati unavyotazamwa kwa kuangalia matukio mbalimbali ni muhimu sana. Katika enco la Maziwa Makuu ya Afrika Mashariki watu huutazama wakati kama imbenzo ambao baadaye huhukua umbo la mzunguko wa matukio. Zaidi ya hayo historia hufuata viwango viwili vya wakati, kimoja kikiwa cha wakati usioeleweka vizuri wa machafuko, na kingine kikiwa cha wakati halisi wa kihistoria. Katika sehemu nyingine, kama ilivyo kwa Wabatcke kwa mfano, wakati hautazamwi kama kitu kilichio katika mfululizo mmoja bali hutazamwa kama kitu ambacho hubadilikabadilika baina ya vizazi mbalimbali. Hali ya namna hii bila shaka huathiri namna mapokeo yanavyoolewa.

Namna watu wanavyoitazama dhana ya muda mara nyingi huhusiana sana na mwelekeo wa chanzo chake. Mito mara nyingi huwakilisha mhimili wa pande kuu za dira. Hata hivyo maelezo kama vile "kufuata mkondo wa mto", "kukinzana na mkondo wa mto", ukuelekea kilele" yanaweza kuleta utatanishi kutokana na jinsi wataalamu wa leo wa mapokeo wanavyoyaweka. Kitu pekee ambacho kinaweza kutusaidia kujua data ya muda ni marejeo ya mwendo wa jua.

Wazo la vyanzo vya matukio hujitokeza katika jamii zote za watu. Lakini hata hivyo halitumiliwi kwa namna moja. Kwa mfano vitu au kaida huonyeshwa kwamba vina chimbuko la mwanzoni kabisa.

Kimsingi ukweli wa kihistoria hufungamana na uthabiti wa masimulizi yaliyorithishwa. Hata hivyo ukweli huo unaweza kuwa sawa na "ukweli" wa tabaka finalotawala kama ilivyo miongoni mwa Waidoma wa Nigeria au pengine kule kukubali tu kwamba mapokeo yaliyopo yanalingana na mambo yalivyosimuliwa na kizazi kilichopita. Hapa pia hatuna budi kukiri kwamba taswira ya akili huhukua nafasi kubwa. Kwa mfano masimulizi inengi juu ya asili ya Wakuba yalikuwa hayaoleweki vizuri mpaka kilipogunduliwa kigezo cha ufafanuzi wa

namna ya kuutazama ulimwengu ambapo uhamaji hufanywa kwa mashua kuanzia kufuata mkondo wa mto (Watakatifu) kuelekea kukinzana na mkondo wa mto (wenye kukufuru). Itakuwa ni kosa kubwa kuhitimisha kama wanavyofanya waamili, kwamba hakuna chochote chenye makini katika matini za kimapokeo na kwamba eti hayo ni makisio tu ya jinsi watu fulani walivyokuwa wakifikiri au wakipanga mawazo yao; utaratibu wowote wa mazungumzo, ikiwa ni pamoja na matini za kimaandishi, hudhihirisha ulimwengu wa itikadi ya mtunzi katika namna mbalimbali. Watu wote hujieleza kulingana na mawazo wapatayo kutoka katika jamii yao, elimu raghba zao, n.k.

### *Kronolojia*

Bila ya kuwapa kronolojia, historia isingekuwapo kwa sababu isingewezekana kupambanua mambo yaliyotokea hapo nyuma na yale yaliyofuata. Mapokeo simulizi siku zote huonyesha kronolojia ya kuyahusisha matukio<sup>1</sup> ambayo huelezwa kwa kuorodhesha watu inashuhuri au vizazi mbalimbali. Katika utaratibu huu hakuna tarehe maalumu zinazohesabika. Hivyo basi kronolojia mbalimbali zinazohusishwa hazina budi kuunganisha pamoja na kujaribu kupatata tarehe zinazohesabika.

Hapa shurti tutambue mambo mawili. Kwa upande mmoja kuna mambo ambayo hutokea na ambayo huweza kupotosha kronolojia ama kwa kurefusha muda wa matukio au kwa kuufupisha kwa madhumuni ya kutaka kuhakikisha kwamba maelezo ya matukio hayo yanalingana na maadili yaliyopo ya jamii. Kwa upande mwingine katika baadhi ya unacneo kama vile Rwanda, Zaire (Ziwa Kisale) na Mauritania (Kounbi Saleh) machimbo ya kiakiolojia yaliyofanywa kwa kufuata masimulizi ya kimapokeo yamedhihirisha kuwa simulizi hizo ni vyanzo vinavyoweza kutegemewa. Ama kwa hakika katika jamii ndogondogo na pia katika falme mbalimbali upo ushahidi wa kupotoshwa kwa kronolojia. Katika jamii ndogondogo mara nyingi simulizi huwa hazitaji majina ya wahenga ambao "hawana maana", yaani wale wahenga ambao vizazi vyao hivi leo havijitokezi kama kundi maalumu linalobainika. Halikadhalika katika orodha ya wafalme huweza kuondolewa majina ya wafalme waliojitwalia ufalme kwa nguvu au wafalme wa kurithi ambao hawakupitia taratibu zote za kimila ambazo wakati mwingine huweza kuendelea kwa miaka kadhaa. Iko pia mifano ya wafalme ambao waliacha utawala kwa kipindi fulani kisha wakarudi tena kutawala lakini wakahesabiwa kuwa walitawala mfululizo. Hii yote hufupisha urefu wa mwendelezo wa historia.

Katika mazingira mengine mwendelezo wa historia hurefushwa. Kwa mfano wakati mwingine kipindi cha ufalme hurefushwa ili kuingiza watawala wengine ambao ingawa hawana uhusiano wa moja kwa moja na watawala wa awali lakini hupeva uhusiano wa baba au mwana kwa madhumuni ya kujaribu kihalalisha uhusiano huo. Mbinu hii ilitumiwa wakati wa ukoloni katika kuwapa baadhi ya uzee watu ambao walikuwa wakisernekana kuwa vyanzo vya temi mbalimbali na ambao walikuwa wakitaka kutambuliwa na kupewa staha.

Uchunguzi mwingi umeonyesha kwamba kwa wastani kizazi kimoja cha ufalme ni kati ya miaka ishirini na sita na thelathini na mbili. Ndiyo maana basi ili kuweza kufasiri kronolojia iliyohusishwa na vizazi mbalimbali katika tarehe halisi, ni lazima kutafuta wastani kati ya kirejeo cha kronolojia cha kwanza ambacho kimtolewa katika tarehe iliyoandikwa na tarehe ya leo. Iwapo wastani huo ni kati ya miaka ishirini na sita na thelathini na mbili basi

<sup>1</sup> Uaratibu wa kuweka tarehe unaowezesha tukio kulinganishwa na tukio jingine kabla au baada ya hilo pasi na kupewa tarehe maalumu kwa kutumia mfumo wa kalenda.



unaweza kutumiwa kama kigezo cha kutazamia nyuma na kukadiriwa vipindi vya utawala wa kila kizazi cha wafalme.

Lakini kama njia hii ingetumiwa kupimia wastani wa urefu wa tawala mbalimbali, matokeo ambayo yangepatikana hayangekuwa ya hakika sana kwani ingelazimu kufikiria mabadiliko katika taratibu za kurithiana na wastani wa urefu wa maisha. Ni dhahiri kwamba uwezekano wa kukosea, kwa kutumia njia hii, ni mkubwa zaidi. Usahihizi zaidi wa kronolojia unaweza pia kupatikana kwa kuunganisha kronolojia mbili zinazokaribiana zilizo na uhusiano wa namna fulani ili iwe moja. Vita baina ya wafalme wawili (A na B) ambao majina yao yanafahamika lufanya kipindi kimoja cha kilistoria. Zaidi ya hayo, iwapo A na B wote waliwali kukutana na mfalme C yawezekana kabisa kuunda kronolojia maalumu itakayowahusisha A,B na C.

Kwa hiyo iwapo mapokeo yanataja kuwa katika enzi fulani kuliwahi kutokea mabadiliko fulani ya hali ya hewa au ya kinajimu, kama vile kupatwa kwa jua, na kama habari hizo zinaweza kuonekana katika maandishi yaliyopo, ushabahi huo unaweza kutumiwa kuwa tarehe yakini za kuweka mpangilio unaokubalika na tarehe zilizopo.

### *Tathmini ya mapokeo simulizi*

Inapokuwa data za fasihi na kijamii zimekwishajinwa kwa ukamilifu inawezekana sasa kujaribu kuweka kiwango cha uwezekano wa mapokeo. Kadri tunavyogundua kwamba aina mbili za mapokeo huru zinaelekea zaidi kukubaliana ndivyo tunavyozidi kuikaribia hakika ya mambo. Hata hivyo kuna tatizo la kuhakkikisha kuwa vyanzo vilivyotumiwa ni huru, hasa tukiitilia maanani mwingiliano wa watu katika jamii mbalimbali hata kabla ya enzi ya ukoloni na pia kwa sababu ya ukweli kwamba baadhi ya habari zilizokusanywa wakati wa ukoloni zilingizwa katika masimulizi ya kimapokeo. Inapokuwa ukubalifu wa masimulizi unatokana na kulinganishwa kwa data za kiakiolojia na hati za maandishi zilizopo uthibitisho unakuwa thabiti zaidi; mradi tu vyanzo hivyo viwe huru, kama ilivyokuwa katika swala la Kounbi Saleh na Ziwa Kisale.

Inapotokea mgongano baina ya maelezo ya kimapokeo na chanzo cha kiakiolojia, chanzo cha kiakiolojia hupewa uzito zaidi labda kama nacho kiwe kimekisiwa badala ya kuchunguza kitu chenyewe. Kama hitunisho la kiakiolojia litatokana na kukisiwa tu basi vyanzo vya masimulizi vitaaminika zaidi. Inapokuwa chanzo cha masimulizi ni mujarabu basi kinaweza kukubaliwa kama vile kilivyo chanzo cha kimaandishi; tukiachilia mbali ukweli kwamba habari za kimaandishi zenye maelezo toshelevu zinategemewa zaidi. Kwa upande mwingine ni kweli pia kwamba mara nyingi maelezo yanayotokana na vichocho vya kisaikolojia na kijamii hujitokeza zaidi katika mapokeo simulizi.

### *Ukusanyaji na uchapishaji*

Hatuna haja ya kusisitiza kwamba uhakiki madhubuti wa kihistoria huhitaji kuelewa jamii inayohusika kwa undani na kwamba mwanahistoria, kwa kutumia data zilizokusanywa na wale anaofanya kazi nao, sharti awe amekwishaelewa ustaarabu wa jamii anayoishughulikia. Kwa ajili hiyo basi maelezo ya papo kwa papo kuhusu mambo ya jamii yake mwenyewe hayatoshi, sharti afanye utafiti ulio wazi kwa kuangalia mambo ya nyuma.

Ukusanyaji wa mapokeo hujitaji muda mrefu na uvumilivu. Kwa hiyo hata inapokuwa mbinu za sampuli zinatumiwa kulinganisha vyanzo mbalimbali maarufu, si rahisi kuamua ni

vigezo gani vya kuondia sampuli ambavyo vitakuwa vimckitwa katika kanuni za asili ya nanna hizo mbalimbali za vyanzo. Kumewahi kutoka nyakati ambapo watoa habari wa "kijadi" wamewahi kupotosha habari ambazo ama wamezipata katika maandishi au wamezisikia kutoka katika matangazo ya redio. Kwa vyovyote vile haitawezekana kukusanya mapokeo yote ya jamii fulani. Hivyo vyanzo lazima vitafutwe kwa kufuatia mambo maalumu ya kihistoria ambayo yalikuwa yamekwisha fasiliwa mapema. Kwa bahati mbaya wakati mwingine watu wanashindwa kuwa wavumilivu na hivyo hujaribu kukusanya habari kutoka katika enco kubwa, upesi iwezekanavyo. Inapokuwa hivyo kunakosokana maelezo mbalimbali ya kitu kimoja jambo ambalo husababisha kutofikiwa kwa mahitimisho thabiti. Kwa upande mwingine hata kama makusanyo hayo hayataweza kumpa mwanahistoria habari anayohitaji, lakini yakikusanywa vizuri, yanaweza kuwa hazina kubwa itakayotumiwa katika fafanuzi za kùsimu, kifasihi, mawazo ya pamoja na miundo ya kijamii ya kundi linatohusika.

Kwa kumalizia kazi hiyo haitaweza kuwafikia wanazuoni mbalimbali mpaka iwe imechapishwa. Vyanzo vilivyochunguzwa vyatakiwa angalau viainishwe, na kujaliziwa kwa kupewa utangulizi, vidokezo na faharasa ili viweze kuingizwa katika kumbo la nyaraka za kale zitakazoweza kutumiwa na kila mwenye kuzihitaji. Kazi hii mara nyingi huandamana na uchapishaji wa matokeo ya uchunguzi ambao umeegemezwa kwenye makusanyo ya vyanzo na ambayo shurti yaeleze jinsi mapokeo hayo yalivyokusanywa pamoja na orodha fupi ya vyanzo, na watoa habari. Hii itamwchezsha msomaji kuona ubora wa makusanyo na kutathmini uchunguzi wa namna mbalimbali za maelezo ya kitu kimoja. Uchapishaji wa matini zote kwa ukamilifu ni kitu ambacho mara kwa mara huhitaji ushirikiano wa wataalamu mbalimbali katika nyanja anuwai kama vile historia, isimu na elimujamii.

### *Hitimisho*

Mapokeo simulizi hivi sasa yanakusanywa katika sehemu zote za Afrika. Tatizo ni kwamba ukusanyaji huu mara nyingi umeelemea mno katika upande wa historia ya kisasa; na hii pia imesisitizwa zaidi katika Afrika ya Mashariki na Kati ambako mara nyingi mapokeo hayo ndiyo pekee yanayoweza kuwa vyanzo vya historia. Hata hivyo baadhi ya tenzi au masimulizi kuhusu asili na maendeleo ya ulimwengu (kosmogonia), kama vile utenzi wa Sundjata, hueleza habari za kale sana.

Wakati mwingine mapokeo yaliyokusanywa na wasafiri wa mwanzo a Kizungu, kama yale yaliyoandikwa na Cavazzi katika kiwango cha juu, yana umuhimu wake. Hii ni kwa sababu yamedokeza juu ya mbadiliko ya kijamii na kisiasa yaliyotokea kwa kipindi kirefu. Zaidi ya hayo, ukusanyaji na ufasiri wa mapokeo mara nyingi umeelekea kuwa wa kijuujuu, hasa katika kazi zilizofanywa na wataalamu wa ethnografia. Mara nyingi mapokeo haya yamechukuliwa kuwa "ubunifu au hekaya tu za asili ya mambo". Matokeo yake ni kwamba historia yote ya Afrika inabakia kuwa taswira tu ya kuja na kuondoka kwa watu; taswira ambayo imevurugwawurugwa na kurahisishwa mno. Kwa hakika hata ingawa mapokeo hayataoi maelezo mengi na yanashindwa kuonyesha mabadiliko ambayo hutokea bila watu kufahamu, kwa sababu yanatokea polepole mno, lakini bado mapokeo hayo ndiyo pekee ushahidi wa maendeleo ya kihistoria ambayo yalitokea katika staarabu mbalimbali. Pamoja na utajiri wake mkubwa wa kimaandishi historia ya kikoloni isingekuwa na ladha na ingechosha laiti kama isingepata mchango mkubwa wa watoa habari ambao, kwa kupitia njia ya mapokeo, hutoa mchango wa kintazamo wa Kiafrika juu ya vitu; intazamo ambao ni wa thamani kubwa.

---

## Mapokeo hai



8

---

Mapokeo simulizi ndiyo njia pekee inayoweza kutufikisha katika historia na hisia za watu wa Afrika. Miongoni mwetu bado wamo watu wanaohifadhi mapokeo hayo, watu wanaoweza kuchukuliwa kama ukumbusho uliyo hai wa Afrika ingawa pengine kizazi chao kitakuwa cha mwisho chenye kuhifadhi ukumbusho huo. Mapokeo simulizi ni sehemu ya urithi wa utamaduni wa mwandamu uliohifadhiwa na mchanganyiko wa mambo mengi kwa namna ya ajabu.

Baadhi ya watu huwa na wasiwasi kama mapokeo simulizi yanaweza kuaminika. Kwa hakika swali hilo halijazuiwa kuulizwa hapa. Thamani ya ushahidi wowote hutokana na uaminifu wa mtoa habari ambaye daima huwa mwanadamu mwenyewe, haidhuru ushahidi huo wneandikwa au umesimuliwa. Isotoshe, iwapo tutarudi nyuma na kufuatilia mfululizo wa ushahidi wa maandishi, tutakuta asili yake imejikita kwenye ushuhuda simulizi ambao ndio kiini cha mambo yote yanayorithishwa na kila mwanadamu. Ukweli ni kwamba anapohadithia tukio kwa maandishi, mtu hutaja shahidi na ikiwa mwenyewe alishuhudia tukio hilo hulichambua akilini mwake kabla ya kuliandika.

Kwa hivyo tatizo halisi, ni kule kuaminika kwa mtu atoaye ushuhuda na hasa, mfungamano uliopo kati ya mwanadamu na maneno, na mfungamano huo ni imara zaidi katika jamii zitumiazo simulizi. Katika jamii zisizo na maandishi kuna mfungamano mkubwa kati ya mwanadamu na maneno anayoyatamka. Neno lililoandikwa halimfungi sana mwandishi. Kwa kuwa neno linathaminiwa kuwa ni kijumbe kitakatifu cha nguvu za siri, linaheshinika na kutumika kwa uangalifu. Miiko hii ilihakikisha ukweli wa ushuhuda wa maneno halisi.

Kama mwanamapokeo halisi wa Kiafrika angeulizwa, "mapokeo simulizi ni nini?" jibu lake la mwisho lingekuwa "maarifa kamili". Licha ya imani waliyo nayo watu wengi, mapokeo simulizi hayaishii kwenye hadithi na hekaya au masimulizi ya kubuniwa au ya historia yaliyosimuliwa na mayeli au wazec wasimuliaji wa hadithi. Mapokeo simulizi ndiyo shule kubwa ya maisha: hushughulika na dini na sayansi za asili katika nyanja kama vile elimu madini, tiba, orodha ya madawa, na mafunzo ya ufundi, na historia, na michezo na burudani, na mapenzi na kifo.

Maarifa katika jamii simulizi za Kiafrika sio kitu dhahania au kilichotengwa na maisha. Yamefungamana na mwenendo dhahiri wa kijamii wa mwanadamu. Kwa kupitia neno takatifu, yanaunganishwa na dunia ya leo na chimbuko la maarifa yote.

## Asili takatifu ya Neno, wakala wa uumbaji

Komo, mojawapo ya shule maarufu za kuwafunda vijana huko Savana ya Sudani iliwaifunza wanafunzi wake kwamba Neno *Kuma*, lilikuwa sifa ya Mungu pekee ambaye alikuwa akilitumia kuumba vitu: "Neno la Maa Ngala (Mungu) huumba maisha!"

Hapo mwanzoni, palikuwepo na ombwe hai iliyokuwa katika Kiumbe Mmoja aliyejipa jina la Maa Ngala. Aliumba "Fani" yai la mwanzo lililokuwa na hali tisa za uzima kwenye migawanyo yake tisa. Yai hilo lilipoanguliwa viumbe vilivyotokoa humo havikuwa na uwezo wa kuongea. Kwa hivyo, ili apate mtu wa kuongea naye (*Kuma-nyon*), Maa Ngala aliehukua kipande kutoka kila kiumbe akachanganya pamoja halafu akapulizia moto kwenye huo mchanganyiko kukatokea kiumbe mwingine ambaye alipewa sehemu ya jina lake ambayo ina maana ya Mwanadamu. Akiwa ndiye mchanganyiko wa uzima wote, Mwanadamu ndiye kazi ya zana halisi ya uumbaji: Neno. Mwanadamu ndiye anayemjibu Mungu na ndiye yeye ambaye Mungu lumwitikia. Neno litokalo kwa Mungu ni neno la Mungu na Neno liendalo kwa Mungu ni neno takatifu.

Sifa tatu fiche alizopewa mwanadamu na Mungu ni maarifa, uia na uwezo kwa kupitia hii Neno. Kwa ki-Fulfulde neno 'usemi' (*haala*) linatokana na nizizi *hal* ukimaanisha "kutoa nguvu" na kwa kunyambuliwa "kufanikiwa". Ama kuhusu mtu wa kwanza inasemekana kuwa "kuzungumza na Mungu kulimpa Kiikala nguvu." Ama kwa hakika usemi kwa mirindimo inayosababisha nao hutendeza na kisukuma vitu vyote, hata vitu viyakiniifu kama inavyomgutua mtu yeyote jina lake linapotajwa akageuka na kujibu. Hii ndiyo sababu lugha ni kijumbe muhimu katika uchawi wa Kiafrika. Neno uchawi daima linatumiwa kwa kutweza na wanasayansi na Wazungu kwa jumla, lakini katika Afrika haina maana zaidi ya kuonyesha kumudu nguvu mbalimbali, utaratibu ambao wenyewe unaweza kuwa wa manufaa au madhara kutokana na matunizi yake. Kama methali inavyosema "uchawi na bahati vyenyewe si vibaya." Matumizi yake ndio huvisababisha kuwa vizuri au vibaya." Uchawi mwema - sio uchawi wa walizi unaodhuru bali ule wa wale wafundaji na "weledi wa maarifa" - unalenga kutakasa mwanadamu, wanyama na vitu ili kurcjesha utaratibu miongoni mwa nguvu mbalimbali kupitia lugha usemi.

## Wanamapokeo

Huko Bambara, wanamapokeo wanajulikana kama *doma* au *soma* "wajuzi wa mambo." Katika Fulfulde wanaitwa *silatigi* au *gando*. Wakati mwingine wanapewa cheo cha "Wajenzi wa maarifa." Wanaweza kuwa Wafundwaji Waliofuzu na hivyo waanzilishi wa desturi maalumu kama vile ufuaaji, usukaji, uwindaji na uvuvi au pengine waweza kuwa na maarifa kamili. Katika Savana ya Sudani kuna taasisi mbalimbali maalumu za kufunda vijana kama vile Komo, Kore, Nama, Do, Diarra wara, Nya, Nyawoole zote zikiwa huko Mali.

Lakini maarifa si kitu kilichogawanywagawanywa. Kwa kawaida Mkuu wa Maarifa ni "ntaalamu wa jumla" aliye na ujuzi wa sayansi ya mimea, ya udongo na sifa zake za kilimo na kimadawa, ya maji, na pia ya unajimu, elimu ya ulimwengu, saikolojia na taaluma nyingine. Kwa kweli hii ni sayansi itiliayo mkazo maisha ya kila siku yenye kukusanya nguvu mbalimbali zipatikanazo kwa ajili ya kukuza maisha. *Doma* wenye maarifa kamili walikuwa Fula Ardo Dembo, ndugu wa Kibambara Danfo Sine na Latif, na ambao bado wanaishi ni kwa pamoja na Banzaoumana mwanamuziki kipofu aliye maarufu.

Wakati wa ukolom athari za wanamapokeo hazikupewa nafasi kubwa kwa sababu ilidhaniwa kuwa wangukuwa kitovu cha harakati za upinzani na walijificha msitani. Kwa

niaka fshirini ifuatayo, hadi mwisho wa karne hii, wadhamini wa desturi katika sehemu hii ya Afrika huenda wakatoweka.

### *Uhalisi wa urithishaji*

Wanamapokeo halisi wanajali sana ukweli. Kwao kusema uwongo sio tu kukosa uungwana bali ni mwiko ambao ukivunjwa huweza kutokomeza kazi yao. Kama wasemavyo wahenga: "Heri dunia itengwe nawe kuliko wewe kutengwa na nafsi yako kwa sababu ya uwongo." Mkuu wa Kisu, au mtolea sadaka, Mdogoni kutoka eneo la Pignari huko Mali alilazimika siku moja kudanganya ili kuokoa maisha ya mwanamke mmoja aliyekuwa akisakwa na akajificha nyumbani kwake. Kutokana na uwongo luo Mdogoni luyo alijiuzulu wadhifa wake kwa vile alichukulia kwamba asingetimiza masharti ya miiko ya kufanikisha majukumu yake kikamilifu. Kila alipotoa hadithi, Danfo Sinc alianza kwa kusema: "Shikeni barabara hatamu za ulimi wangu, Enyi Mababu zangu, ongozeni maneno yangu yanavyotoka ili yafuate na kuleshimu mpangilio wake halisi."

Wanamapokeo wa *doma*, ambao jukunu lao ni kufundisha kwa njia isisunuayo wasikilizaji wao inapobidi, ni tofauti na mayeli manju, na wafungwa ambao jukumu lao kubwa ni kuburudisha na kwa hiyo wana haki ya kupotosha ukweli na kutunga uwongo. Mayeli, inasinekana "wanaruhusiwa kuwa na ndimi mbili". Umma huzitafautisha ndimi hizo mbili. Kila alipoongea Danfo Sinc, aliongozana na mashahidi wawili ambao aliwaomba kusimamia na kuthibitisha alichosema. Ni kawaida ya kukariri walikopata maneno wanayoyasema kwa kusema "Nimerithishwa na fulani ambaye pia alirithishwa na fulani." Wanamtolea heshima muanzilishi wa mapokeo haya, awe ama wa kihistoria au wa kubuni tu, kwa kuchutama huku wakiweka ncha ya kiko ardhini na mikono ikisimama wima. Ukumbukaji wa mfululizo huu wa urithishaji ni wa muhimu sana kwa sababu taratibu za urithishaji zisipobeshimiwa basi desturi za kichawi na za kitakatifu hazitajitokeza.

Ikiwa mshairi wa *Komo* anaongezea chochote kwenye ujumbe aliopokea, anahakikisha kwamba anaitahadharisha hadhira yake kwa kusema: "Haya nimeongezea mie. Ikiwa ninakosea, msisahau kwamba mimi, kama ninyi, ninaisli kwa fumba inoja la mtama, funda moja la maji na hewa safi. Mwandumu lakosi kasoro". Uimarisho wa maarifa hautegemci wingi wa maneno anayotamka mtu bali unategemea kiasi gani anatekeleza hayo maneno kwa vitendo.

Kwa vile mapokeo simulizi yanawakilisha maisha na uzoefu wa watu fulani, kuyarithisha kwa watu wengine luwa vigumu: hii ni kasoro mojawapo ya simulizi ikilinganishwa na maandishi. Nimakumbuka mnamo mwaka 1928 nikiwa nimepeleka kikazi huko Tougan, katika nchi ya Burkina Faso, kijana mmoja Mfaransa ambaye ni mwana-anthropolojia alikuja kufanya utafiti juu ya kuku wanaochinjwa kama sadaka kwenye sherehe za tohara. Mfaransa aliyekuwa mkuu wa wilaya aliwaita wazee wa baraza na kuwahimiza kushirikiana kikamilifu na huyu mwana-anthropolojia akisisitiza kwamba wamueleze "kila kitu". Kiongozi wa matambiko ambaye ndiye hasa aliyeombwa alijibu: "Anataka tumueleze kila kitu? Kwani amekuja kutahiriwa?" Alipong'amua kwamba huyu mwana-anthropolojia alikuwa amekuja kutafuta habari tu luyu kiongozi wa matambiko aliamua kwamba hapakuwa na njia nyingine ila kumvunga tu.

Mbali na mafunzo ya siri yanayotolewa jandoni mafunzo ya mapokeo hutolewa na jamii na familia, nayo pia huambatana moja kwa moja na maisha ya kila siku. Hadithi na hekaya zinejaa mafundisho ya inaisha ya kila siku, ambapo methali ni ujumbe ulioachiwa vizazi

vijavyo na wahenga. Michezo mingine iliyo na misingi ya kihisabati inakomaza akili huku ikiwakilisha kimafumbo maarifa ya siri: Mfano mmojawapo ni ule Mchezo wa Banangolo huko Mali, ambao umekitwa katika mfumo wa tarakimu uliofungamana na *sikiba* 266 au alama zinazolingana na sifa za Mungu.

Ikiwa mwalimu wa zamani amekuta kuchuguu huko nyikani basi anaweza kurekebisha mafunzo yake kwa watu wanaomsikiliza: aweza akaongea juu ya mchwa wenyewe, sheria zinazoongoza maisha yao na "tabaka lao la viumbe" au anaweza kutoa fundisho lenye maadili kutokana na maisha yao ya kijamii na maana yake linapokuja suala la ushirikiano na kujihidi au pengine anaweza kuingilia mambo ya ujuzi wa siri.

Katika Savana ya Sudan kila kitu kilichoko katika sayari yetu hii kimegawanywa katika sehemu kuu tatu au "tabaka ya viumbe" na hizi nazo zinagawanywa tena katika vikundi vitatu:

chini kabisa ya ngazi, ni viumbe "visivyosema", "visivyo hai" vyenye lugha inayofikiriwa kuwa ni ya siri. Hivi ni viumbe mango, majimaji na "dohari" (vya gesi).

Kwenye ngazi ya katikali ni viumbe "vyenye uhai visivyojimudu" (mimea)

Mwisho ni viumbe ambao ni wanyama wanaojimudu, wapatikano kwenye ardhi, majini na viumbe wanaopaa angani.

Katika "historia hii ya maumbile" mwanadamu anajitokeza zaidi kwa sababu yeye anaunganisha pande zote - mnyama, mimea, na madini - kwa vile yeye aliumbwa kutokana na kipande cha kila kitu kilichoishi kabla yake na pia kwa sababu yeye amejaliwa uwczu wa kuongea na hivyo kumfanya mwenzi wa Mungu na mlinzi wa maumbile. Utata wa mwanadamu unaelezwa na methali isemayo: "kuna watu wengi katika utu wa kila mtu."

### *Sanaa za kimapokeo*

Sanaa za kimapokeo na ufundi udizo njia kuu za kurithisha mapokeo simulizi. Kazi ya msanii ni muhimu kwa sababu inashabihiana na uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Mapokeo ya Ki-Banibara yanatueleza kwamba Maa Ngala alipoumba ulimwengu, aliacha mambo nusu nusu ili Maa aweze kuyamalizia, kuyabadilisha na hatimaye kuyakamilisha. Hivyo kazi ya msanii ni kurudia utaratibu wa uumbaji kwa kusema:

Mfuaji hufua Neno

Mfumaji hufufuma

Mtengeneza-ngozi hulilainisha.

Kila sanaa au ufundi umejaa ishara. Mfunaji (*naabo* kwa Kifulfulde) ndiye mwenye kufahamu maana ya sehemu zote thelathini na mbili za mtanda. Kati ya sehemu nane kuu zinazounda kiunzi sehemu nne zinazosimama wima zinaashiria mambo manne ya msingi katika maisha (ardhi, hewa, moto na maji) pamoja na pande nne za dira ambapo sehemu nne zinakingamana zinaashiria pande nne za msambamba. Akijumlisha mfunaji mwenyewe pamoja na sehemu hizi nane hupatikana sehemu tisa zinazowakilisha tabaka tisa za viumbe, matundu tisa ya mwili (milango ya kani ya maisha) aina tisa za wanaume miogoni mwa Wafulani na kadhalika.

Kabla ya kuanza shughuli mfunaji anagusa kila sehemu ya mtanda na huomba duu. Mwendo wa mbele na nyuma wa miguu yake unafikiriwa kuwa unasema hivi:

Fokonyoko! Fokonyoko! Mbili kwa mbili, mbili kwa mbili  
 Mmoja akipanda juu, mwingine huteremka  
 Mfalme hufa na mwanamfalme hutawazwa  
 Babu hufa na mjukuu akazaliwa  
 Ugomvi wa watalaka unachanganyika na vigelegele vya harusi.

Nacho kipisha mshindio husema:

Ndiini chombo cha Fate.  
 Naabiri kati ya miamba ya kamba inayowakilisha maisha  
 Toka ukiungo wa kulia ninakwenda kushoto  
 Nikikunjua utumbo wangu (uzi)  
 Kuongeza kitambaa  
 Kisha narejea kulia kutoka kushoto  
 Nikikunjua utumbo wangu  
 Daima maisha ni kwenda na kurudi  
 Tunzo ya kudumu ya nafsi.

Kipande cha nguo kinachofungiwa fimbo iliyopo pajani mwa mfunaji kinawakilisha siku za nyuma, ambapo kidonge kilichojaa uzi kinaashiria fumbo la kesho.

Ishara za ufunaji zina miendo minane ya mbele na nyuma (miguu, mikono, kipisha mshindo na mapigo ya nyuzi zinazopishana) inayoungana na sehemu nane za (miguu, mikono, ngalawa) inbaa za kiunzi na miguu minane ya buibui wa kisaasili aliyerithisha ujuzi wake kwa wahenga wa ufumaji.

Mhunzi naye hufanya kazi katika ulimwengu wa visaasili na ubunifu. Anajulikana kama "Mwana wa Kwanza wa Dunia", kiwanda chake cha ufuaji kinaitwa Fan; kimepewa jina sawa na lile la yai la kwanza, kiwanda cha kwanza kitakatifu ambako ulimwengu mzima ulitokea. Isitoshc, vitu viune vya msingi shurti viwepo katika kiwanda; maji katika chungu kidogo, moto na hewa ya mivukuto na chungu dogo la udongo.

Ishara za uume na uke zipo pia. Ie mivukuto miwili inayoendeshwa na msaidizi wa fundi inalinganishwa na mapumbu. Hewa inayojazwa ndani ya mivukuto ndio msingi wa ubai unaosafirishwa katika mrija unaofanishwa na mboo, mpaka kwenye tanuu ambalo linafananishwa na kizazi ambamo moto wa kufuma unafanya kazi yake. Kadhalika fuawe inafananihwa na uke na nyundo ndiyo uume uliokamilika.

Mhunzi anazielewa kani za maisha. Neno "fundu" kwa Kifulfulde ni *baylo* Mgeuzaji. Kama Mkuu wa Kisu hufanya kazi ya kutabiri. Fundu wa tanuu ambaye huzindua na kuyeyusha chuma huwa inwenye maarifa mengi sana. Anachanganya maarifa ya madini ya "wana wa kizazi cha udongo" na maarifa ya maisha ya minca. Anaweza kugundua tabaka la dhahabu kwa kuangalia tu minca na mbwe zilizoko juu ya ardhi.

Mali asili haikutumika kwa ajili ya kupata faida tu, bali kwa ajili ya kujumuika na ulimwengu. Katika kanda ya Baule, kuna sheria kali zinazohusu namna dhahabu, madini ya Mungu yanavyoweza kutumiwa.

Kwa ufupi, kazi ya msanii haikuwa shughuli ya ubunifu wa moja kwa moja tu. Ilikuwa hasa ya kuiumba tena duni. Kazi yenyewe haikuishia katika vitendo na ishara za uzalishaji: ilifungamana na infuno mzima wa maisha kwa kupitia miiko na wajibu unacambatana na shughuli zilizounda hadhi ya kijamii.

Hivyo kila sanaa au shughuli ilikuwa ni njia ya kufikia mafundo: njia ya mafundi (*numusira* au *munuya* kwa ki-Bambara) njia ya wakulima, njia ya wafuwaji, njia ya wachungaji wa Kifulani (*lawol fulfulde*) inawakiisha kanuni za maisha zinazoambatana na kila kikundi na zinarithishwa kwa mapokeo kwa uangalifu mkubwa sana. Hata hivyo jambo linalojitokeza ni kuwa kadiri kila njia inavyochunguzwa kwa makini ndivyo inavyoweza kuufikia umoja ambao kwao njia hiyo huwa mwashirio mahususi.

Kwa hiyo, licha ya kuwapo kwa miiko ya jinsi inayotenga vikundi (kutokuoa nje ya ukoo) na licha ya siri za matambiko mwanzoni hapakuwa na ubaguaji wa watu kwani kila njia ni tofauti na kila mtu huweza kutumia njia yoyote kufikia kilele hichohicho. Usemi usemao "Mungu alimuumba msanii" hufuatiwa na "vita na ubwana vilileta mateka." Kwa hiyo ni dhahiri kwamba dhana ya ubaguaji ilingizwa taratibu kwa kupitia mgawanyo wa kazi mbali na ile ya sanaa za mapokeo. Hapo mwanzoni koo za Wafulani ziliongozwa na *silatigi* Wafundaji waliofuzu, lakini hawa waliondoshwa na *ardo* (machifu au wafalme).

Kazi ya kupigana vita ambayo huenda ilitokana na maendeleo ya sanaa za mapokeo pengine ndiyo iliyoshusha hadhi ya sanaa hizo katika baadhi ya kanda za Savana na kuzifanya ziwe za tabaka la chini ambalo liliwekwa vikwazo fulani. Lakini badala yake wasanii katika tabaka hilo walistahili kuomba na kupata chochote kutoka kwa mabwana wao.

Katika mapokeo ya Wamende wasanii walioheshiniwa kuliko wote katika janiii ni mafundi wakifuatiwa na wafumaji, seremala, fundi ngozi na watumbuzaji. Kila kikundi nacho kina migawanyo mitatu: kwa mfano baina ya mafundi kuna mafundi tanuu, wahunzi na masonara.

Wawindaji, wavuvi na wakulima wanaambatana zaidi na mbari kuliko "tabaka". Wawindaji, ni mabingwa wa mambo ya maumbile kama walivyo waganga ambao wanaweza kutokea kwenye tabaka au mbari yoyote. Lakini baadhi ya mbari zina ujuzi zaidi wa uganga wa jadi: kwa mfano Wadogoni walikuwa stadi sana katika kuunga mifupa iliyovunjika na kutibu ukoma, kifua kikuu, kupooza na magonjwa mengine.

### *Watumbuizaji au mayeli*

Mayeli wana jukumu la kutumbuiza na kuchangamsha sherehe rasmi au za binafsi. Wanaweza kugawanywa katika makundi matatu:

- Wanamuziki, waimbaji na watunzi wa nyimbo, waweza kupiga ala mbalimbali kama vile zcze, kora na aina mbalimbali za ngoma n.k.
- Mabalizi waambata wa kitala au wa watu binafsi wakiwa washenga au wasuluhishi.
- Wanashajara, wanahistoria na watunzi wa matini simulizi ambao kwa kawaida ni wasafiri mashuhuri kwa sababu hawakujiambatanisha kwa mtu au familia maalumu.

Tofauti na mabwana (*horon* kwa ki-Bambara), mayeli hawawajibika kwa maneno wanayomtaka wala kuwa na busara au kuheshimu ukweli. Wanaweza kusema uwongo dhahiri bila kuwajibika. Watu hukubali uwongo wao bila kudanyanyika kwa sababu kila mtu anajua kwamba mayeli wanazo ndimi mbili na 'lugha ya kihuni'. Tofauti na mabwana, ambao ni lazima wawe na hadhari na maneno wanayoyanena, mayeli wanaweza kusema chochote wependacho kwa sababu wanaweza kujipinga. Wanawasemca mabwana wao katika masuala ya mapenzi, majadiliano ya kisiasa na hata katika mambo ya biashara au kusuluhisha migogoro.





8.1 Mpiga 'Valiha'. Ala hii hutengenezwa kwa ubao na uzi wa chuma cha pua.  
(Musée de l'Homme-Jumba la Makumbusho ya Binadamu)

8.2 Mwanamuziki wa Kitukuloor akipiga 'ardin' (Kayes, Mali, Na. A0-292)



Katika Kiambara neno lenye maana ya yeli, *dieli*, pia lina maana ya "damu". Ama kwa hakika mayeli, kama vile damu, luuzunguka katika jamii ambayo wanaweza kuiponya au kuidhuru kutegemea kama watasuluhisha au kuchochea migogoro.

Lazima isisitizwe kwamba sio mayeli wote ni wafidhuli, masafihi au wadukizi. Miongoni mwao kuna watu wajulikanao kama *diet-faama*, au mayeli wa kifalme. Sio watu duni wakilinganishwa na mabwana tukizingatia ujasiri, uadilifu, wema au hekima yao na ambao kamwe hatumii ovyo haki walizokabidhiwa kimila. Wanawahamasisha na kuwatia ujasiri watu wapapo shidani kwa kuwakumbusha sifa za wahenga wao na zamani hawakusita kufa vitani pamoja na inabwana wao.

Kabla ya sherche za kutahiri, wanawataka wale vijana wadhahirishe ujasiri kwa kumwanbia kila mmoja: "Babu yako" na kutaja jina lake — "aliyeuawa katika uwanja wa vita alimeza uji wa chuma kinachowaka moto (risasi) bila kuogopa. Ninatumaini kwamba kesho ninyi hamtaogopa ukali wa kisu cha fundi." Katika sherche ya Soro miongoni mwa Wafulani wa Bororo luoko Niger nyimbo za mayeli zinawapa moyo vijana, ambao lazima watabasamu wakati wote na kutolingisha hata msuli mmoja kwa kulalamika wanapopata kipigo kikali kifuani. Mayeli huonekana sio tu kwenye tafrija, ubatizo na harusi bali pia wakati mwingine jumuiya inapokuwa ikifanya kazi kwa pamoja kwa mapigo na nyimbo zao huwasisimua vijana kuiga wazee wao.

Siri ya mayeli kustahiwa na wale wa-matabaka ya juu katika jamii inatokana na maarifa yao kuhusu shajara na historia za familia. Ikiwa, kwa kuelceza historia ya ufalme au ukoo, wanafanikiwa kuamsha hisia za ufahari, basi watazawadiwa vyema na mabwana wahusika, ambao miongoni mwao wengine, bila kufikiria, huvua hata nguo au johari zao kuzawadia yeli kwa kuonyesha ustadi, hekima na usanii kiasi hicho kwa kuwasifu wahenga wao. Wakati mwingine hii hutokea mahala ambapo bwana ana hali ndogo na yeli labda ana hali nzuri kuliko yeye. Kwa hiyo kutokwa kwa baba hadi kwa mwana, mayeli wanahifadhi mambo na matukio mengi vichwani mwao na kuwa maktaba hai, watunza kumbukumbu za kale za jamii ya Kiafrika na wakati mwingine wanakuwa wanahistoria maarufu.

Hata hivyo inabidi kusesitiza kuwa wao si wanamapokeo peke yao, Wanawakilisha tawi moja tu na hata hilo tawi silo linaloaminika zaidi kwa sababu huwa ni vigumu kwao kufikia cheo cha *doma* au Wakuu wa Maarifa ambacho kinahitaji kuwa na hadhari katika mambo wanayoyasema. Lakini, kama ambavyo mwanamapokeo asiye yeli anavyoweza kuwa mwanahistoria mashuhuri, hali kadhalika yeli anaweza akapanda cheo hadi kuwa mwanamapokeo *doma* ikiwa ameshapitia mafundo ya lazima isipokuwa mafundo ya Koino ambayo ni mwiko kwake. Akisha kuwa *doma*, yeli anakuwa mwaminifu kabisa kwa kuwa anachanganya kipaji cha kutumbuiza na sifa za kujidhibiti nafsi kama vile walivyo lwa na Banzoumana wa Mali.

Lakini aina ya watumbuizaji, wanahistoria wa muda na maayari inajumuisha aina mbalimbali kama vile *bambaado*, kwa maana sisi si mtu anayebewa mgongoni, kwa sababu wao ni mzigo kwa jamii, na tiapourta, mabwana waliokuja duniani na ambao ni masafihi zaidi kuliko mayeli wabaya, kwa vile wanawaomba hata mayeli wenyewe wawape zawadi.

### *Jinsi mtu awezavyo kuwa Mwanamapokeo*

Mtu yeyote katika Savana ya Sudani angeweza kuwa Mkuu wa Maarifa au *doma* kwani mafundo yangeweza, kwa njia moja au nyingine kumpatia cheo hicho. Hapakuwepo ubaguzi

na kila kitu kilitegemea uwezo wa mtu binafsi. Maarifa yalitukuzwa juu ya kila kitu na, yaliwapatia ubwana wale waliokuwa nayo. Mkuu wa Maarifa katika uwanja wowote angeweza kuhudhuria baraza la wazee haidhuru awe bwana msanii au mateka. Kama methali isemavyo "Maarifa hayajali mbari wala ukoo; humuenzi mtu wake." Elimu katika jamii hiyo ilidumu maisha yote. Hadi kufikia umri wa miaka 42 wanaume walipaswa kujifunza mambo ya maisha na kimsingi, walitakiwa kuhudhuria mikutano na kusikiliza yanayosemwa ili kuongeza maarifa waliyopata wakati wa kufundwa. Kuanzia umri wa miaka 42 na kuendelea, bado walitakiwa kuwasikiliza watu waliokuwa na uzoe fu kuwazidi; usemi ulikuwa "Kila siku sikio husikia jipya".

Wasanii vijana, baada ya mafundo yao, walifunga safari toka kijiji hadi kijiji, wakati mwingine na vifaa vyao begani, ili kuimarisha ujuzi wao kwa kukutana na chemchem mpya za uzoe fu. Kila walipofikia walielokezwa kwenye nyumba au wilaya za wasanifu wenzao. Kama walionyesha adabu basi waliweza hata kupata siri zilizoongezea ujuzi wao kwani imesemekana kwamba "siri ya mzee inaweza kununuliwa kwa tabia njema na wala sio kwa fedha".

Horon vijana kwa kawaida hawakusafiri mbali kwani walilitajika katika ulinzi wa nchi yao. Lakini Wakuu wa Maarifa kama vile waganga kwa kawaida walisafiri sana ili kuimarisha maarifa yao. Ama kwa hakika zilikuwepo njia maalumu zilizolindwa na wafalme na miungu ambazo walizifuata ili kuepuka maharamia. Walipofika mwisho wa safari yao Mkuu wa eneo hilo, akiwa ndiye mwenyeji wao, aliwajibika kuwahakikishia usalama na mahitaji yao. Kati ya wasafiri hao mara nyingi walikuwemo wanashajara ambao wangeweza tu kuongeza ujuzi wao kwa kutafuta taarifa kutoka kwa wenyeji. Hivi ndivyo alivyofanya Molon Gaolo, mwanashajara maarufu ambaye alielewa fika historia ya familia zote za Wafulani wa Senegal. Alipozeeka kiasi cha kushindwa kusafiri, alimtuma mwanawe Mamadou Molom kuendelea na utafiti wake kote nchini Mali. Wakati nilipomfahamu Molom Gaolo, alikuwa ameishafanikiwa kukusanya na kuhifadhi historia ya vizazi arubaini vilivyopita.

### *Athari za Uislamu*

Sifa maalumu za ukumbusho wa Mwafrika na jinsi zilivyokuwa zikirithishwa kwa mdoino hazikuathiriwa na kuenea kwa uislamu ambao wenyewe ulijinasibisha na mapokeo ya Mwafrika ikiwa mapokeo hayo hayakiuki misingi yake. Wakati mwingine mnasaba huu ulikuwa mkubwa kiasi kwamba ilikuwa vigumu kutofautisha mapokeo ya Kiislamu na yale yaliyokuwa na kijadi. Katika vyyo mashuhuri vya Kiislamu dini ya Kiislamu ilifunzwa kwa mdomo kwa lugha mbalimbali za kienyeji isipokuwa Kiarabu na Swala. Mifano inayoweza kutolewa miongoni mwa mingi ni vyyo simulizi vya Djelgodji na Barani huko Burkina Fasso, Niafunke na Nara huko Mali, na vile vya Shekh Osman dan Fodio vya Nigeria, Tierno Bokar Salif huko Bandiagara na Shaykh Salah, walii maarufu wa Wdogoni. Pamoja na kuwa na maoni sawa kuhusu ulimwengu kuwa ni mahali patakatifu, na fikra sawa kuhusu dhima ya mwanadamu katika ulimwengu aina zote mbili za mapokeo hutilia maanani umuhimu wa kutaja vyanzo vyake (*isnad* kwa Kiarabu) na wa kuhifadhi maneno ya bwana bila kuyabatilisha kuheshimu mfululizo wa urithishaji wa mafundo (*silsila* = mnyororo kwa Kiarabu) na mfumo wa njia za ufundaji. Katika orodha ya aina ya Wakuu wa Maarifa ziliongezeka zile za mawalii na masheikh maarufu wa Kisufi, ingawa mnuundo wa kimsingi wa jamii, ikiwemo sanaa zake na matabaka yake viliendelea pasi kubadilika. Utamaduni wa Kiislamu ulikuwa chemchem mojawapo ya kuzidisha maarifa.

### *Jinsi masimulizi yalivyokusanywa*

Muni binafsi nilipewa mafunzo toka utotoni na, hatua kwa hatua, nilikusanya pamoja vipengee vya mapokeo vilivyonisidia hatimaye kuandika *The History of the Fulani of Macina in the 18th Century* (Historia ya Dola ya Wafulani ya Macina katika Karne ya Kumi na Nane). Kwa vile nilikuwa mwana wa ukoo wa Tidjani, mtawala wa jimbo, nilikutana na wasafiri na washauri wa kitala waliofika nyumbani. Kwa vile pia nilipendelea sana kumtembelea msimulizi wa hadithi, mwanashajara na mwanahistoria wa Kifulani aitwaye Koulel, baada ya muda si mrefu, rafiki zangu wa rika langu walianza kuniita Amkoulel au "Koulel mdogo" wazazi wangu walipohamia Bougouni, nilifahamiana na doma mashuhuri wa Bambara aitwaye Danfo Sine na halafu mdogo wake Latif.

Baadaye, huko Bamako, nilipata kukutana na makundi mbalimbali ambayo wakati mwingine yalikuwa yanachukiana kila moja likiwa na fasiri tofauti ya historia ya Dola ya Macina. Miongoni mwa makundi haya walikuwemo Wamacinanke wenyewe, Watukolor, maadui wao na mbari nyingine kama vile Wabambara, Wamarka, Wasarakole na Wasonghay ambao wote walihusika katika matukio hayo kwa viwango mbalimbali. Tangu wakati huo na kuendelea nilianza kuandika mapokeo hayo kwa namna iliyo wazi kwa muda wa zaidi ya miaka kumi na mitano, wakati ambapo nilisafiri hadi Senegal na Kano huko Nigeria nikitafuta vyanzo vya masimulizi. Niligundua kwamba kiungo cha masimulizi yaliyotolewa na maelfu ya watoa habari niliowasililiza daima kilikuwa sawa na kwamba tofauti za kina zilitokana na kushindwa kwa mtoa habari kukumbuka mambo vizuri au tofauti za tabia. Uzoefu huo ulinithibitishia kwamba mapokeo sinulizi yalikuwa thabiti katika mtazamo wa kitaaluma.

### *Sifa za ukumbusho wa Mwafrika*

Katika jamii ambazo kila kitu kinategemea neno lililorithishwa kwa mdomo, uwezo wa kuhifadhi mambo huwa wa kiwango kikubwa. Kwa mfano kuna wafanyabiashara wasiojua kuandika wala kusoma wanaoendesha biashara kubwa ambao huwakopesha watu wengi fedha na kuwakopa wengine, lakini huhifadhi mahesabu na shughuli za kibiashara vichwani mwao bila kukosea hata kidogo. Sifa mojawapo ya kukumbuka maneno ni ule uwezo wake wa kuhifadhi masimulizi toka mwanzo hadi mwisho kama yalivyopokelewa. Katika hadithi ya vita vya Watukolor, tunaenezwa ni joho gani lililotariziwa alilovaa (*bubu*) shujaa maarufu Qumarel samba Dondo katika vita fulani, nami alikuwa saisi wake na yaliyomfika, jina la farasi wake na yaliyompata. Katika hadithi simulizi hakuna habari isiyo muhimu na ndiyo maana kila kitu kinaenezwa bila kuacha chochote, la sivyo mtamba hadithi anaacha kusimulia hadithi kabisa kwa kusema: "Ikiwa huna muda wa kunisikiliza, basi nitasimulia hadithi hii siku nyingine".


Hii ni faida kubwa sana kwa mwanahistoria kwa vile uhakiki wa ndani na uje unaweza kutegemea habari fulani kuthibitisha au kutoa matini. Mathalani katika kisa cha Thianaba nyoka wa kisaasili wa Wafulani hekaya inasimulia visa na uhamaji wake kote katika Savana ya Sudani. Mnano mwaka 1921, Belime, mhandishi aliyesimamia ujenzi wa bwawa la Sansanding alivutiwa sana hata akafuatia fununu za kijiografia zilizotolewa katika hadithi hiyo na akagundua kwa mshangao kwamba kwa liakika alikuwa akifuatia bonde la zamani la into Niger.

## Hitimisho

Hapana shaka kwamba Afrika inapitia kipindi cha mabadiliko makubwa, na hii inaelezwa kupingana kunakoonekana. Viongozi au Mameneja vijana "wa kisasa" wanatumia kanuni, mielekezo ya kiakili na itikadi za kigeni ili kuongoza jamii ambazo hazijafikia ulimwengu wa kisasa na ambazo hazielewi kwa nini ziwajibike au zilaaniwe kwa sababu ya kufuata desturi fulani. Ni kweli kwamba, kwa muda mrefu sasa vijana wengi sana walioelimika wameona haja ya kuchunguza mapokeo yao na kugundua itikadi zao za msingi katika jitihada za kuelewa asili zao na siri za nafsi zao. Lakini mfumo unaotawala unawaelekeza upande mwingine. Tayari yamekwishatoka mapengo katika urithishaji kama lile lililotokana na kuandikishwa kwa askari ambao katika vita vikuu viwili vilivyopita waliacha makwao na hivyo wakatengwa na mafundo ambayo yangewaunganisha na mkondo wa mapokeo yao.

Hali kadhalika vijana waliohudhuria shule au wale watokao schemu za vijijini ambao wameathirika na mazingira ya miji au majiji. Wakati ambapo miongoni mwetu tunacho kizazi cha mwisho cha wadhamini wa kazi kubwa ya mapokeo simulizi, suala la urithishaji lina umuhimu wa pekee. Jibu mojawapo lingekuwa kufanya juhudi kamambe ya kuzikusanya data zilizopo. Watafiti katika kazi hii itabidi wawe na uvumilivu mkubwa na "moyo wa njiwa" (ili wasipandwe na mori au hamaki), wawe na "ngozi ya mamba" (ili waweze kuweka vichwa vyao mahali popote na juu ya chochote) na "tumbo la mbuni" (ili waweze kula chochote wanachopewa bila kusikia kichefuchefu au kuugua). Pia wanapaswa kukumbuka maneno ya Tierno Bokar mwenye hekima toka Bandiagara:

Ukitaka kufahamu mimi ni nani  
 Ukitaka nikufundishe ninachojua  
 Jisahau kwa muda mfupi kuwa wewe ni nani  
 Na kuwa unajua nini.



## *Akiolojia ya Kiafrika na mbinu zake pamoja na ukadiriaji umri*

Mwanaakiolojia anapogundua kifaa, kwa kawaida huanza kukichunguza kwa kutumia njia za akiolojia tu, kama vile kurekodi tabaka za ardhi ambamo kimepatikana, kufasiri matini kinachonyesha, kuelezea umbo lake, kuhakikisha vipimo vyake na kadhalika. Data inayopatikana huchunguzwa kufuatana na mitazamo ya kistaratigrafia, kifilolojia na kiuainishaji, na kutokana na haya, baadhi ya wakati, habari muhimu za kiakiolojia huweza kupatikana kuhusu umri na asili ya kifaa. Lakini mara nyingi mwanaakiolojia hushindwa kupata data inayojibu maswali yake au inayomsaidia kuweza kuhitimisha jambo lolote kutokana na habari iliyopatikana. Hali hii itokeapo inabidi auwasilishe uvumbuzi kwenye taaluma nyingine kwa ajili ya uchunguzi wa kisayansi. Uchunguzi wa aina hiyo unatarajiwa kutoa habari muhimu kuhusu viambajengo vyake, asili yake, mbinu zilizotumika katika kukiunda, umri wake, madhumuni ya kutengenezwa kwake na kadhalika. Hata hivyo ni lazima isisitizwe kwamba uchunguzi kama huu unaweza kuchukuliwa kama ni kigezo kinachomwezesha mwanaakiolojia kukabili tatizo maalum; ushahidi kwa kisayansi lazima uzingatiwe pamoja na masuala ya kimtindo, kifilolojia na kistaratigrafia.<sup>1</sup>

Mbinu nyingine za kisayansi ambazo zinaweza kusaidia katika akiolojia ni upimaji wa uwandani wa maeneo ya kiakilojia yaliyoko chini ya ardhi bila ya kuyachimbua na kuhifadhi vifaa na minara ya kale iliyovumbuliwa. Mbinu za kisayansi zilizotumika zinafaa kutumika katika akiolojia yote. Zinaweza kutumika katika akiolojia ya Ulaya, Asia na ya Marekani, ingawa mkabala utakaotumika unaweza mara nyingine kuwa tofauti. Mbinu hizi zinajumuisha vipengee vya taaluma hii ambavyo vitazingatiwa kwa utaratibu ufuatao:

1. Mbinu za uchanganuzi zinazotumika katika akiometri
2. Madhumuni ya uchunguzi na uchanganuzi wa akiometri
3. Mbinu za kukadiria umri.
4. Mbinu zinazotumika katika utafutaji wa kiakiolojia
5. Mbinu za kuhifadhi

### *Mbinu za uchanganuzi katika akiometri*

Mbinu za uchanganuzi zimeundwa kwa kiwango ambacho inakuwa vigumu kuamua mbinu gani zitumiwe kwa sampuli fulani ili kupata habari inayotakiwa. Vipengee muhimu vya swali hili vimejadiliwa hapo chini.

<sup>1</sup> E.T. Hall, 1970, uk. 135-141

### Uchaguzi wa njia ya uchianganuzi

Sampuli za kiakiolojia zina manufaa ya pekee kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza ni kwamba kiasi kinachiopatikana cha vifaa kwa kawaida huwa kidogo sana hivyo kwamba hakiwezi kutosheleza uchanganuzi munoja kamili, na iwapo kiasi chote kitatumika huenda ikawa vigumu kupata nyingine. Sababu ya pili ni kwamba sehemu fulani ya sampuli hubidi kuwekwa kwa ajili ya marejeo au maonyesho kwa siku za baadaye. Kwa hivyo lazima ichukuliwe hadhari kubwa kuhakikisha kwamba habari nyingi zinavyoweze kama zitapatikana kutokana na uchanganuzi wa kiakiometri. Vigezo vitatu vinavyoyakinisha njia ya kutumiwa ya uchanganuzi vinaweza kuelezwa kwa ufupi kama ifuatavyo:

#### *Upatikanaji wa vifaa*

Ikiwa kiasi cha kutosha cha vifaa kitapatikana uchanganuzi wa kimikali maji unafaa kutumiwa katika kutafuta asilimia ya elementi muhimu zilizomo katika sampuli, ilihali uchanganuzi wa ufyonzaji wa atomi unaweza kutumiwa katika kutafuta asilimia ya metali za alikali kama vile natiri na kali. Kwa vyovyote vile, eksirci memetuko na eksirei usambazo inafaa kutumiwa kwa ajili ya uchanganuzi wa elementi ya ukuzi na mchanganyo japokuwa uchanganuzi huu utatoa matokeo ambayo yatafikia kiasi cha asilimia 10 mpaka 20 tu ya jawabu sahihi.

Ikiwa kiasi cha sampuli kinachoweza kupatikana ni kidogo tu na elementi kadhaa zinabidi kukisiwa, ni bora kabisa kuichanganua sampuli hiyo kwa njia ya spektotometri au kwa njia ya eksirei usambazo.

Ikiwa mwanaakiolojia hataki kutoa hata kipande cha kifaa, kifaa hicho kinaweza kuchanganuliwa kwa njia ya spektometri utokezi au kwa njia ya eksirci memetuko, alinradi ukubwa wa umbo la kitu chenye unawezesha chombo kinachofaa kutumiwa.

#### *Aina ya vifaa vya kuchanganuliwa*

Aina ya vifaa vya kiakiolojia hutofautiana sana. Baadhi yao ama ni oganiki kamili au ni sehemu tu, kwa mfano vyakula, malhamu, gundi, mafuta, nta na kadhalika. Vifaa vingine kama vile, metali, rangi, vifinyange, vigac, na plasta si oganiki. Vifaa vya oganiki kwa kawaida kuchanganuliwa kwa njia za, 'mwasho, utengenezaji sabuni, uziduzi wa viyeyusho, mnururisho wa infra-red au joto.

#### *Aina ya taarifa inayotafutwa*

Ili kuokoa muda na gharama uchanganuzi lazima ufanywe kwa mujibu wa mpango mzuri uliotayarishiwa kwa kushirikiana na mwanaakiolojia kwa lengo la kutafuta majibu ya maswali maalumu. Kwa mfano kupri na shaba nyeusi za kale zinafanana kijuujuu hivyo kwamba jaribio linalohitajika ni lile tu la kugundua kuwepo kwa bati ili kuzitofautisha. Kwa kawaida jaribio hili hufanywa kwa kuweka matone machache ya asidi nitriki iliyokolea kwenye sehemu ndogo ya sampuli.

### Uhudhurishaji wa matokeo

Kwa kuwa mwanaakiolojia ambao hatimaye ndio watakaotalii ugunduzi wa uchunguzi wa kisayansi na kuutumia kutolea maoni na mahitimisho yao wenyewe kwa kawaida si wanasayansi, matokeo hayo lazima yawasilishwe kwa namna itakayoweza kueleweka kwa urahisi. Kwa mfano, matokeo yasiwasilishwe kama kisawe cha gramu ya kiambajengo fulani

katika kila gramu 100 za sampuli. Inasaidia zaidi ikiwa matokco yote yanaclezwakama asilimia ili yaweze kucleweka kila mahali, zaidi ya hayo njia hii hurahisisha ulinganishaji wa matokco yaliyopatikana katika maabara mbalimbali.

Njia ya uchunguzi na uchanganuzi

Kwa mujibu wa inawazo haya, mbinu muhimu za uchanganuzi zinazotumika katika akiometri ni hizi zifuatazo.

*Uchunguzi unaotumia kioo cha kukuza au darubini*

Uchunguzi unaotumia kioo cha kukuza (10 x au 20 x) ambao mara nyingi husaidia sana kupata taswira ya mwanzo ya kifaa cha kale au sampuli. Darubini<sup>2</sup> ni bora zaidi kwa vile inaweza kuchunguza mashimo yenye kina kirefu sana ambayo vioo vya kukuza haviwezi kuyapenya.

Picha safi zaidi inaweza kupatikana kwa kuchunguza sampuli kwa kutumia hadubini changamano, na njia hii kimsingi huweza kutunika kwa madhumuni yafuatayo:

1. *Utambulishaji.* Mara nyingi inawezekana kutambulisha sampuli fulani, yaani kama ni safi au ina michanganyiko anuai, kwa kuchunguza kwa darubini ukubwa wa chembechembe zake au sifa za kifuwele za viambajengo vyake.
2. *Uchanganuzi wa Ubora.* Hivi sasa kuna mbinu za kuendeleza uchanganuzi wa utuamaji, uyeuyushaji, uchunguzi wa mabadiliko ya gesi na micendelezo mingine juu ya sampuli ndogo mno.
3. *Uchanganuzi wa Idadi.* Utunijaji wa darubini una faida kubwa katika uchanganuzi wa idadi wenye michanganyiko changamano na ya aina nyingi. Njia hizi zinawezesha kudhihirisha idadi na ukubwa wa viambajengo mbalimbali. Ikiwa uzani wa kila kiambajengo unajulikana, asilimia ya ujazo wake katika mchanganyiko inaweza kuguzwa kuwa asilimia ya uzito inayokaribia usahihi<sup>3</sup>

*Rediografia*

Rediografia ina faida kubwa katika kuchunguza kazi za sanaa, kwa vile inawezesha kugundua, kwa mfano, kama kuna vitu vyovyote vilivyopenyczwa ndani ya mumiani aliyczongomezwa au kama kuna naksbi zilizofichika chini ya matabaka ya kutu. Habari hii ni muhimu katika kumua utaratibu sahihi wa kufuatwa wakati wa kuwafungua mumiani au kuhifadhi vifaa vya metali. Kwa mfano picha za eksirei za mumiani wa Kifalme zilizopigwa katika Makumbusho ya Cairo zimedhihirisha kwamba hata baadhi ya wale mumiani waliofunguliwa walionekana na vyombo ambavyo havikungunduliwa awali kwa sababu vilifunika na tabaka nene la sandarusi<sup>4</sup>.

*Uyakinishaji wa mvuto mahsusi*

Katika zama za kale, dhahabu ilikuwa na kiasi kidogo cha takataka za fedha na kupri. Hata hivyo, vitu vya dhahabu ni vya thamani kubwa mno hivyo kwamba mara nyingi huwa hakuna sampuli hata iwe ndogo vipi inayoweza kutolewa kwa sababu ya uchambuzi. Calcey<sup>5</sup>

2 Kioo cha kukuza chenye vioo viwili vya kutazamia

3 I.M. Kolthoff, E.B. Sandell, E.J. Meehan na S. Bruckenstein, 1969

4 J.W. Halpern, J.E. Harris na C. Barnes, 1971, uk. 18

5 E.R. Calcey, 1949, uk. 73-82



iligundua njia ya kuyakinisha mvuto mahsusi wa vitu hivyo - njia isiyoleta uharibifu kabisa - ili kuthibitisha asilimia ya dhahabu iliyomo katika vifaa hivyo. Kwa vile mvuto inahsusi wa dhahabu (19.3) ni karibu mara mbili ya ule wa fedha (10.5) au wa kupri (8.9) kuweko kwa sehemu ndogo ya metali hizo huweza kugunduliwa.

#### *Uchambuzi wa kawaida wa kemikali wa maji*

Njia hizi aghalabu hutumika katika uchanganuzi wa ubora na idadi ya chokaa, plasta, kutu ya vifaa vya metali, vyakula, mapambo, takataka za madawa ya kuhifadha maiti na kadhalika. Vitu vya chuma vilivyogunduliwa Niani, huko Guinea, na vyenye umri wa kuanzia karne ya kumi na tatu mpaka kumi na tano ya enzi zetu vimchanganuliwa kikemikali na imeonekana kwamba ndani yake mna takataka za kupri, fosfarasi, nikeli, tangsteni, titeniamu na molibdenamu ambavyo huenda vyote hivi vilikuwemo katika mtapo wa asili.<sup>6</sup>

#### *Mbinu ya spektometri utokezi*

Mbinu hii hutumika katika uchanganuzi wa shaba nyeusi, vifinyange, chokaa, rangi na kadhalika. Kuna sababu nyingi zinazoifanya spektometri utokezi kuwa ni mbinu yenye kufaa kabisa ikilinganishwa na njia nyingine za uchanganuzi wa alama. Kiwango cha unyeti kwa kawaida hutosheleza na kuwezesha kugundua sehemu kubwa (mpaka asilimia 20) ya elementi zilizokuwemo. Kwa mfano uchanganuzi wa spektrografia ya sanamu za asili ya huko Ife, Nigeria umedhihirisha kuwa zimetengenezwa kwa shaba nyeupe na si shaba nyeusi.<sup>7</sup>

#### *Uchanganuzi wa ufyonzaji wa atomi*

Njia hii inafaa kutumiwa kwa sampuli ya vitu visivyokuwa oganiki, kama vile metali, saruji, lchemu, vigae, vioo, chumvi na kadhalika. Faida ya njia hii ni kwamba ina usahili mkubwa [uwezekano kukosoa ukiwa asilimia moja (1) tu] unaoweza kupatikana kwenye sampuli za miligramu 5 mpaka 10.

#### *Eksirei memetuzi*

Kwa vile ute uwezo wa eksirei kupenya ni indogo njia hii inaweza kutumika kwa sehemu ya nje tu ya vitu. Kwa hivyo inafaa kwa kuchanganua vitu kama vigae, kaure na vioo, vyombo obsidi, na aina nyingi za mawe. Kwa vyovyote vile, vyombo vya kale vya metali, vina tabia ya kuisha, yaani sehemu fulani ya ile ya metali ya thamani ndogo iliyomo huhamia upande wa nje wa kitu. Kwa hivyo uchanganuzi wa sehemu ya nje unaotumia njia ya eksirei unaweza kutoa inatokoe tofauti na yale yanayoweza kupatikana iwapo kitu kiziama kingechanganuliwa.<sup>8</sup>

#### *Uchanganuzi wa utendezi wa nyutroni*

Mionzi ya nyutroni na ya gama ina nguvu zaidi za kupenya kuliko ile mionzi ya eksirei. Jambo hili linawezesha kufanyika kwa uchanganuzi wa vielelezo vilivyo vinene zaidi bila ya kujali athari ya kuparaganyika kwa shaba nyekundu katika metali.<sup>9</sup>

6 A. Muzur na E. Nasck, 1974, uk. 96

7 F. Willet, 1964, uk. 81-83

8 E.T. Hall, 1970, uk. 135-41

9 kama ilivyonukuliwa awali

## Madhumuni ya uchanganuzi wa akiometri

Madhumuni muhimu ya uchunguzi na uchanganuzi wa akiometri ni kama yafuatayo:

### Utambulishaji sahihi wa vifaa

Utambulishaji sahihi wa masali ya kiakiolojia ni muhimu kabisa ili kuwawezesha wanaakiolojia kutoa maelezo sawasawa ya vifaa katika majarida ya kisayansi au katika viongozi vya makumbusho. Vilevile ni muhimu kudhihirisha aina za viambajengo vilivyotumika katika kutengeneza vifaa, kwa sababu utambuzi wa maana wa kitu kinachohusika kwa kawaida hutegemea kuthibitishwa kwa aina halisi ya viambajengo hivyo. Kwa bahati mbaya makosa ya utambulishaji yanatokca sana na yamesababisha fazaa kubwa wakati mwingine. Kupri mara nyingine hufikiria kuwa ni shaba nyeusi, ingawa uvumbuzi na utumiaji wa shaba nyeusi humaanisha kuwepo kwa kiasi fulani cha mabadiliko ya kitamaduni. Kadhalika shaba nyeusi hudhaniwa kuwa ni shaba nyeupe na matokeo yake ni kwamba umri wa kitu unaweza kukosewa kwa vile shaba nyeupe kwanza ilitengenezwa mnamo miaka ya katikati ya kwanza kabla ya enzi yetu, ilihali shaba nyeusi ilikwishajulikana na kutumika kiasi cha miaka 2,000 kabla ya wakati huo.<sup>10</sup>

Kwa vile makosa ya utambulishaji hutokana na kutegemea sura ya kitu inafaa kusisitiza kwamba utambulishaji wa vifaa vya kiakiolojia unapaswa kutegemea uchanganuzi wa kikemikali au wa eksirei usambazo ili kuepukana na utambulishaji potovu.

### Tafsiri ya maneno ya kale yasiyojulikana

Utambulishaji sahihi mara nyingine husaidia kudhihirisha maana ya maneno yasiyojulikana. Kwa mfano, huko Saqqara, Misri, vyungu viwili vilionekana katika kaburi la Farao Hor'Aha (Ufalme wa kwanza kiasi miaka 3,100 kabla ya enzi zetu). Kila kimoja katika vyungu hivi kina maandishi ya picha neno yanayolingana na neno *seret* ambalo maana yake ilikuwa haijulikani wakati huo. Uchanganuzi wa kikemikali ulionyesha kwamba vyungu hivi vilikuwa na jibini na kwa hivyo ilihitimishwa kwamba *seret* maana yake ni jibini.<sup>11</sup> Mfano mwingine ni picha neno *bekhen* lililonekana katika baadhi ya sanamu za mawe. Kwa vile neno hili lilihusishwa katika mifano mingine yenye kokoto za rangi ya maziwa za miamba na madini ambayo ni aina ya mawe laini yaitwayo *shisti*, na ilivyokuwa neno hili lilitumika katika maandishi kuhusu Wadi-Hammamat ilihitimishwa kwamba inawezekana sana kwamba *bekhen* inalingana na kokoto za rangi ya maziwa za miamba na madini za Wadi-Hammamat.<sup>12</sup>

### Ugunduzi wa vyanzo vya vifaa

Kuwepo kwa vielelezo vingi vyenye asili ya kigeni kwenye enco la kiakiolojia ni alama kwamba vitu hivyo viliagizwa kutoka nchi za nje. Pale ambapo vyanzo vya vifaa vinafahamika, ruwaza za kibiashara huweza kutambulishwa. Kwa mfano, obsidi haikuwa ikipatikana huko Misri, lakini ilikuwa ikitumika tangu zama za kabla ya Ufalme, yaani kabla ya mwaka 3100 Kabla ya Enzi za Kristo. Vitu vilivyotengenezwa kwa obsidi hii vimechunguzwa na kulinganishwa na obsidi kutoka nchi jirani na vimechunguzwa na kulinganishwa na obsidi kutoka nchi jirani na vimeonekana kushabihiana na obsidi ya

10 E.R. Caley, 1948 kur. 1-8

11 A. Zaki na Z. Isikandar, 1942 kur. 295-313

12 A. Lucas, 1962, kur.416, 419-20

Ethiopia. Kwa hiyo ilihitimishwa kwamba mahusiano ya kibiashara yalikuwepo kati ya nchi mbili hizi kutoka zamani sana.<sup>13</sup>

Alama za takataka katika mitapo na vifaa vya kupri, pia huweza kusaidia kuonyesha mahusiano yaliyoko baina ya vifaa na aina ya mtapo uliotumika katika kutengeneza vifaa hivyo, na hivyo kudhihirisha njia zilizohusika za biashara.<sup>14</sup>

Kuwepo kwa nikeli katika kifaa cha kale cha chuma husaidia kudhihirisha iwapo chuma hicho kina asili ya kimondo au kimefanywa na binadamu, kwa sababu chuma cha kimondo daima huwa na kiasi cha asilimia 4 mpaka 20 cha nikeli. Jambia maarufu la chuma la Tutankhamen lilichunguzwa kwa uchanganuzi wa sprektro utokezi na kuonekana kuwa na kiasi kikubwa cha nikeli na hivyo kuthibitisha kwamba chuma hicho kilikuwa cha asili ya kimondo.

### Kulakikisha madhumuni ya matumizi ya vifaa

Wakati mwingine huwa vigumu kujua vifaa fulani vimetumiwa kwa madhumuni gani, na uchanganuzi wa kikemikali husaidia sana katika jambo hili. Kwa mfano, mtungi mkubwa wa alabasta wenye kitu cha ajabu ulionekana katika kaburi la Nefertitah (yapata mwaka 1800 kabla ya Enzi za Kristo) lililogunduliwa katika bonde la Fayun huko Misri mwaka 1956. Uchanganuzi wa kikemikali ulionyesha kwamba kitu hicho kilikuwa na sehemu sawasawa za plumbi, sulfidi na sandarusi. Kwa vile mchanganyo huu haujapata kuonekana kabla, haikuwezekana kueleza madhumuni ya kuwekwa kwake kaburini. Hata hivyo, wakati madawa yaliyoorodheshwa katika Mafunjo ya Eba yalipoangaliwa ilionekana kwamba dawa Namba 402 ilisema hivi: dawa nyingine ya kuondosha vidoa vyeupe vinavyokeza machoni: wanja mweusi (*galeja*) na Khet'wa (sandarusi) vinatwangwa mpaka viwe unga laini na vitiwe katika macho yote mawili. Kutokana na matini haya na mchanganyiko wa kemikali wa kile kitu kilichokuwemo kwenye gudulia, ilihitimishwa kwamba kitu luki ni dawa ya macho na kwamba inaweza Nefertitah aliugua ugonjwa wa ukoma kwenye jicho moja au macho yote mawili, na ndiyo maana alitiliwa dawa hiyo kwa wingi ili atumie huko ahera.<sup>15</sup>

### Kuyakiusha utimilifu wa mambo kuhusu miendeleo ya ufundi

Uchunguzi wa kisayansi wa vitu vya kale umeweza kutupa habari kuhusu mbinu zilizotumiwa na watu wa kale kwenye tasnia zao za kemikali kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo:

#### *Utengenezaji wa rangi ya bluu ya Kimisri*

Vielezo vya rangi hii ya bluu vimechanganyuliwa kwa kutumia kemikali, kwa hadubini na kwa eksirei usambazo. tafiti huu umconyesha kwamba rangi ya bluu ya Kimisri ilitengenezwa zama za kale kwa kupasha moto mchanganyiko wa mchanga, chokaa, maleketi na mycyuko wa chumvi ya kawaida.<sup>16</sup>

#### *Uchunguzi wa kihadubini wa vitu vya metali*

Uchunguzi wa metalografia wa vitu vya metali unaweza kuonyesha ikiwa vimefanywa kwa njia ya kusubu au kwa kufunda kwa nyundo au kwa njia zote mbili. Kwa mfano, msumari

13 kama ilivyonukuliwa awali

14 P.R. Fields, J. Milsted, E. Henricksen na R.W. Ramette, 1971

15 N. Farag na Z. Iskander, 1971, kur. 111-115

16 A. Lucas, 1992, uk. 416, kur. 419-420

wa kupri uliopatikana kutoka ngalawa ya Cheops iliyogunduliwa nyuma ya Piramidi Kuu la Giza mwaka 1954 ulidhihirisha kwamba ulitengenezwa kwa kufundwa kwa nyundo.

#### *Uchunguzi wa takataka za madawa ya kuhifadha maiti*

Uchunguzi wa vielelezo vya takataka za dawa za kuhifadha maiti zilizovumbuliwa Saqqara, Luxor na Mataria huko Misri umeonyesha kwamba zina kiasi kidogo cha sabuni yenye asidi mango zenye shahamu ambayo ilitokana na shahamu zilizokuwa katika mwili na zilizoguka kuwa sabuni kutokana na kitendo cha natroni — wakati maiti alipokuwa akifanywa mumiani.<sup>17</sup> Kwa hivyo ilihitimishwa kwamba kitu hiki kilitumika kwenye shughuli za mumiani kujaza mashimo katika mwili kabla ya mwili huko kukaushwa maji unapokuwa katika kitanda cha kufanyia mumiani.<sup>18</sup>

#### *Visubu vya kutengenezea vioo*

Uchunguzi wa mabaki ya kiwanda cha vioo huko Wadi-el-Natrum umeonyesha kwamba vioo vilitengenezwa ndani ya visubu huko Misri wakati wa utawala wa Warumi.

#### *Kuthibitisha uhalisi*

Kwa miaka mingi njia pekee iliyokuwepo ya kutambua uhalisi wa kitu ilikuwa ni ile ya mkabala wa kihistoria na kiumbuji. Lakini hivi karibuni kutokana na hatua kubwa zilizopigwa katika utafiti wa kisayansi, inawezekana kudhihirisha kwa uhakika zaidi iwapo vitu hivyo ni vya kweli au la. Njia madhubuti kabisa inayotumika kuthibitisha uhalisi wa vitu ni kama ifuatayo:

#### *Uchunguzi kwa kutumia nuru-zambarau*

Mbinu hii inasaidia katika kuchunguza pembe ya ndovu na marumaru, Marumaru za aina mbalimbali zikiangazwa na mwanga wa nuru-zambarau humemetuka rangi mbalimbali na schemu ya nje ya marumaru ya kale mara nyingi huwa na rangi memetuko ambayo ni tofauti na ile ya jiwe la aina ilicile. Vilevile, ingawa hayaonekani kwa macho ya kawaida mabadiliko au matengenezo yafanywayo kwenye kitu cha kale cha marumaru au pembe, au hata kwenye michoro huweza kuonekana waziwazi kitu hicho kinapochunguzwa kwa kutumia mwanga wa nuru-zambarau. Mwanga wa nuru nyekundu na eksirci pia husaidia katika kudungua vitu vya kughushi.<sup>19</sup>

#### *Uchunguzi wa kulika kwa sehemu za nje za kitu*

Metali za kale kwa kawaida hulika kidogokidogo, na utando wa kutu hufanyika baadac ya muda mwingi kupita. Kwenye vitu vya metali vya bandia, utando bandia wa kutu hupakwa juu ili kuvipa sura ya ukale. Utando huu haugandi vizuri na huweza kutolewa kwa urahisi kwa kutumia viyeyusho kama vile maji au alkoholi etheli

#### *Uchanganuzi wa kifaa kilichotumika kutengeneza kitu*

Mfano mzuri wa mbinu inayotumika ni ile ya changanua kioleza cha towe ya Misri ya Kale. Wakati kiolezo cha towe halisi ya Misri ya Kale kimetengenezwa kwa kigae cha kwartzi,

17 Natroni – fuwele za natiri kaboneti

18 Z. Iskander na A.E. Shaheen, 1964, kur. 197-208

19 E.R. Caley, 1948, kur. 1-8

kiolezo cha towe ya bandia kwa kawaida huwa cha "kaolini", na jambo hilo huwezesha uchunguzi wa haraka na wenye kuaminika na halisi. Mfano mwingine unaweza kuonekana kutokana na ukweli kwamba madini ya zamani huwa na takataka nyingi kama vile aseniki, nikeli, mangani na kadhalika, kwa sababu mbinu zifaazo kusafishia metali hazikuwcko Zama za Kale. Kwa-hivyo ikiwa sampuli ndogo iliyochukuliwa kutoka sehemu isiyojitokeza sana ya kifaa itachanganuliwa kwa kutendezwa kwa nutroni au kwa nuru ya eksirei memenuko na kuonekana haina dalili ya elementi ya ukuzi basi kifaa hicho huwezekana sana kuwa ni cha kubuni.

#### *Utambulishaji wa rangi na njia iliyotumika katika michoro*

Mbinu za mikro kemikali zinafaa katika kutambulisha kiasi fulani cha kiwango cha usahihi wa rangi zilizotumika katika michoro. Ikiwa itathibitika kwamba rangi zilizotumika ni zile zilizovumbuliwa hivi karibuni tu, basi mchoro huo ni wa kubuni.

#### *Uchunguzi wa utando wa juu na ung'aro*

Baada ya muda mrefu kupita, mawe mengi hupata utando wa juu unaosababishwa kwa kuhama kwa chumvi za chuma na mangani katika schemu ya juu ambapo hutolewa katika hali ya oksidi na kufanya aina ya utando. Kwa vile utando huu huwa sehemu halisi ya jiwe huambatana na sehemu ya juu na hauwezi kuondolewa kwa urabisi kwa kuoshwa kwa kiyeyusho huru au kwa kuparuzwa. Kwa hivyo inawzekana kutofautisha kati ya uso halisi wa kale na ule uliochongwa karibuni hata kama utapakwa utando bandia.

#### *Uchunguzi wa vyungu kwa njia ya mwanga joto*

Asilimia ndogo ya elementi za kitoa nguvu ziino katika vyungu na katika udongo ambamo vyungu vimezikwa. Elementi hizi hutoa kiasi fulani cha mnururisho ambacho husababisha elektroni kujikusanya katika vyungu kwa kipindi cha maelfu ya miaka. Vyungu vikipashwa moto kwa zaidi ya nyuzi joto 500°C zile elektroni zihzokikusanya huonyesha athari ya mwanga-joto ambayo hubadilika kufuatana na umri wa kielelezo. Kwa hivyo njia ya mwanga-joto huwapa waangalizi wa makumbusho ushahidi thabiti wa kudhihirisha iwapo kitu fulani ni cha kweli au la.

#### *Mbinu za ukadiriaji wa umri*

Kuna mbinu kadha za kisayansi za kukadiria umri wa vitu vya kale, mbinu kuu kati yazo zikiwa.

#### *Ukadiriaji wa juujuu wa umri kwa uchanganuzi wa akiometri*

Uchanganuzi wa vielelezo vinavyotokana na vifaa vya aina moja-kama vile chokaa, vigae, towe, metali na rangi - lakini zenye umri kutoka vipindi mbalimbali kunaweza kuashiiria umri wa vielelezo vinginevyo kama katika mifano ifuatayo:

#### *Ukadiriaji wa umri kwa kuchanganua shanga za vigae kutoka Afrika Magharibi*

Shanga za "Akori" zilichanganuliwa kwa kutumia eksirei memetuko na zilionekana kugawika katika makundi mawili. Kundi A lilikuwa na kiasi kidogo cha plumbi ndani yake.

Huko Afrika Magharibi shanga za kundi A hupatikana katika macneo ya ndani ya nchi yaliyo makongwe zaidi yenye umri unaoanzia miaka 430 mpaka 1290 ya Enzi za Kristo ilihali zile za kundi B hupatikana katika macneo ya hivi karibuni zaidi. Kwa hivyo ugunduzi wa shanga hizo kwenye kaburi au kwenye tabaka la ardhi unaweza kutoa njia ya ukadiriaji wa juujuu wa umri wa eneo hilo.<sup>20</sup>

#### *Ukadirioji wa umri wa michoro ya mapangoni kwa uchanganuzi wa vinatisho vya uteyai*

Umri wa michoro ya mapangoni unaweza kukadiriwa kwa kuanisha idadi ya amino asidi zilizo katika vinatisho vya uteyai vya michoro hiyo baada ya kupima mvunjo kimaji. Kadiri asidi hizi zinavyokuwa nyingi ndivyo zinazodhihirisha ukongwe wa michoro hiyo. Njia hii imetumika kuainisha umri wa michoro 113 ya mapangoni huko Kusini mwa Afrika kwa kiwango cha asilimia 20 ya usahihi.

#### *Ukadiriaji wa umri kwa uchanganuzi wa chokaa*

Uchanganuzi wa chokaa za aina mbalimbali zilizotumika Misri umconyesha kwamba hakukuwa na chokaa kabla ya wakati wa Ptolemy I (323-285 Kabla ya Enzi za Kristo).<sup>21</sup> Kwa hivyo mnara wowote ule wenye matofali au mawe yaliyonatishwa kwa chokaa unaweza kuchukuliwa kwamba umetokea baada ya kipindi hicho.

#### *Ukadiriaji wa umri kwa kutumia redio-kaboni*

Njia ya redio-kaboni iliyogunduliwa na W.F. Libby na Anderson inatokana na hakika kwamba tishu za mimea na vitu vingine vya ogani mbali ya kuwa na kaboni ya kawaida, huwa pia na sehemu ndogo kabisa ya isotopi za kaboni zenye muundo tofauti wa atomu. Isotopi hii ni kaboni 14 na hufanyika kutokana na athari ya mionzi ya ulimwengu juu ya nitrojeni iliyomo angani. Wakati wa uhai wa vitu vya ogani hali ya kitoa nguvu ya kaboni iliyomo katika tishu zake haibadiliki, lakini mara tu vitu hivyo vikifa ile hali ya kitoa nguvu luanza kufifia.

Kufifia huku hutokea kwa kiwango fulani na kwa kipindi maalum kinachojulikana kwa jina la nusu-maisha, au kwa lugha nyingine, ule muda ambao ukimalizika mwili wa kitoa nguvu huwa umechanguka na kwa hivyo ile hali ya kitoa nguvu huwa imepungua kwa nusu. Nusu-maisha ya kaboni 14 ni miaka 5,568. Kiasi cha kaboni 14 kimeodhihirishwa kuwa ni kilekile katika tishu zote, katika kanda zote na katika vipindi vyote.

Jambo linalohitajika kufanywa ni kuondoa kaboni kwenye sampuli ya mti, kitambaa, kupri, makaa, mfupa au chakula kutoka katika eneo la akiolojia na kupima masalio ya kitoa nguvu katika sampuli hizo ili kuweza kuhesabu na kujua wakati sampuli hiyo ilipokoma kuishi kulingana na nusu maisha ya isotopi ya kaboni. Kawajida utaratibu unaotumika huendelezwa kwa hatua nne: utakasaji wa sampuli, muunguzo, utakasaji wa gesi ya kabonidioksidi iliyopatikana na kuhesabu chembechembe zilizotoka.

Hadhari haina budi kuchukuliwa ili kuondoa kitoanguvu kilichotawanyika na kuacha mwanya wa kosa ambao utazidisha au kupunguza thamani iliyopatikana. Hata hivyo, ilivyokuwa nusu maisha ya kaboni 14 ni supi, njia nyingine, kama vile ukadiriaji wa umri

20 C.C. Davidson, R.D. Giaugue na J.D. Clark, 1971, kur. 645-649

21 A. Lucas, 1962, uk. 416 na kur. 419-420

Hadhari haina budi kuchukuliwa ili kuondoa kitoanguvu kilichotawanyika na kuacha mwanya wa kosa ambao utazidisha au kupunguza thamani iliyopatikana. Hata hivyo, ilivyokuwa nusu maisha ya kaboni 14 ni fupi, njia nyingine, kama vile ukadiriaji wa umri kwa kutumia kali agoni huweza kutumika kwa vipindi virefu.

Usahihi wa njia hii umejaribiwa kwa kulinganisha sampuli za kihistoria zenye umri uliokadiriwa vizuri na umri unaolingana na redio-kaboni<sup>22</sup> hasa kwa msingi wa tarihi ya ki-Misri ambayo inatanda umri mrefu na ambao unajulikana vizuri kuliko nyinginezo. Hata hivyo, sababu nyingine kama vile kudhoofika kwa uga wa sumaku wa Dunia zinaweza kuathiri usahihi wa mbinu hii.

## Ukadiriaji umri kwa kali agoni

### *Kanuni ya msingi*

Kali ya asili huwa na asilimia 93.2 ya isotopi ya kali-39, asilimia 6.8 ya kali-41 na asilimia 0.0118 ya kali -40 ilikuwa na asilimia 0.2 ya jumla yote, lakini sehemu yake kubwa ilififia na kugcuka kalisi -40 na agoni -40, hiyo agoni ikiwa katika hali ya gesi iliyokaa baina ya chembechembe za madini. Kwa vile kali -40 ina nusu maisha marefu (ya miaka milioni 1,330, imcendelea kukaa kwenye sehemu ndogo kabisa ya asilimia 0.0118.

Zaidi ya hayo, kwa vile ile njia ya redio-kaboni haiwi sahihi ikitumika kwa vipindi vinavyopindukia miaka 70,000 kabla ya enzi zetu, ina maana kwamba kuna pengo kubwa katika tarihi ya maendeleo ya kibiolojia kutoka wakati huo na kuendelea nyuma mpaka miaka milioni kumi iliyopita. Pengo hili linaweza kujazwa kwa kiasi fulani kwa kutumia mbinu ya kali agoni.<sup>23</sup>

Ukadiriaji umri kwa kali agoni hutumika sana kwa sababu zifuatazo: Kali imo katika utando wa Dunia kwa uwiano wa asilimi 2.8 kwa uzani. Kwa hivyo kali ni moja kati ya elementi zinazopatikana kwa wingi kabisa na ambayo hupatikana karibu katika michanganyo yote. Nusu maisha ya kali ni muda mrefu wa kutosha kuwezesha kiasi cha kutosha cha agoni-40 kufanyika katika baadhi ya madini katika vipindi vyenye maana kijiolojia. Kwa kupima mkusanyiko wa agoni -40 ya kirediojeni ya madini fulani na kali yote iliyomo, inawezekana kuainisha umri wake kwa kutumia mlingano wa ufifaji wa kitoa nguvu.

### *Matatizo ambayo yangeweza kujumbuliwa kwa kutumia kali agoni katika kukadiri umri*

Miongoni mwa matatizo yanayoweza kutatuliwa kwa kutumia mbinu za kali agoni ili kukadiri umri wa baadhi ya vipindi vya Pleosini na Plestosini ni kuweza kutambua kipimo halisi cha wakati kinahowezesha kutambua asili ya binadamu na umri wa visukuku vilivyokuwepo kwa wakati mmoja sehemu inbalimbali za dunia. Huko Olduvai, katika Tanzania, kali agoni imtumiwa kubainisha umri wa matabaka ya mawe incusi na ya ile miamba ya volkeno iliyofanyika juu yake, katika kujaribu kuainisha umri sahihi wa mabaki ya Zinjanthropo yaliyopatikana katika Kitalu Namba I cha tabaka la chini chenye mawe ya volkeno. Curtis na Evenden wamehitimisha kwamba mawe meusi ya Olduvai yana umri usiopungua miaka milioni nne.

22 R. Berger, 1970; I.E.S. Edwards, 1970; H.N. Michael na E.K. Ralph 1970, E.K. Ralph, H.N. Michael na M.G. Haas, 1973

23 M.J. Aitken, 1961.

## Kukadiria umri kwa njia ya akiomagnetu

Picha rahisi ya njia hii inaweza kupatikana kutokana na maelezo yafuatayo ya baadhi ya sifa zake.

### *Upaleomagnetu*

Njia hii inahusisha uchunguzi wa sumaku iliyosalia kwenye mabaki ya kiakiolojia. Msingi wa uchunguzi huu unatokana na ukweli kwamba uelekeo na nguvu za uga wa sumaku la Dunia hubadilika katika wakati. Uchunguzi wa akiomagnetu ulitokana na vipimo vya usumaku uliobakia katika vituo vilivyookwa vya kiakiolojia na katika miamba unaonyesha kwamba nguvu za sumaku ya Dunia katika muda wa miaka 8500 iliyopita zilifika kielele chake yapata miaka 400-100 kabla ya Enzi za Kristo wakati nguvu za sumaku zilipokuwa kiasi mara 1.6 kuliko sasa na kushuka hadi kufika kiwango cha chini kabisa cha kiasi cha mara 0.6 kuliko hivi sasa yapata miaka 4000 kabla ya Enzi ya Kristo.<sup>24</sup> Athari hizi au mabadiliko katika uelekeo na nguvu za uga wa sumaku ya Dunia hujulikana kwa jina la "mabadiliko ya kidunia." Mabadiliko haya huathiri eneo maalum na huwa ndiyo msingi wa kukadiria umri wa njia ya sumaku, kwa vile mabadiliko katika uga wa sumaku ya Dunia huacha alama zake katika vyungu vilivyookwa, katika umbo la usumaku wa joto baki.

### *Utumiaji wa sumaku wa joto baki ili kukadiria umri wa kiakiolojia*

Ili kutumia mbinu ya usumaku wa joto baki katika kukadiria umri udongo wa mfyanzi uliokwa uliobakia katika hali yake ileile ya asili tangu ulipochoywa, ni lazima kwanza kudhihirisha tabia ya uelekeo wa uga wa jiomagnetu kwa kuchukua vipimo vya miundo ya kiakiolojia yenye umri unaojulikana katika kanda inayohusika. Matokeo huonyeshwa kwenye tao linaloonyesha mabadiliko ya kidunia katika kanda ile kwa muda mrefu. Hapo tena tarehe ambayo kielelezo cha udongo wa kuokwa kilipochoywa huweza kudhihirishwa kwa kulinganisha kati ya uelekeo wa uga wa sumaku katika kielelezo hicho na tao la mabadiliko ya kidunia.

Kwa kadri inavyojulikana, mbinu hii bado haijatumika Afrika, lakini inatumainiwa kwamba itatumika siku za karibuni hasa kwa vile imepiga hatua muhimu katika miaka michache iliyopita.

## Kukadiria umri kwa njia ya mwanga-joto

Mwanga-joto ni utoaji wa nuru wakati kitu kinapopashwa moto. Njia hii hutofautiana na mng'aro moto sana na husababishwa na kuachiliwa kwa nishati iliyohifadhiwa katika hali ya elektroni zilizonaswa katika kifaa kilichopashwa moto.

### *Asili ya mwanga-joto*

Vyombo vyote vya udongo na kauri vina kiasi kidogo cha chembechembe za kitoa nguvu (kiasi kidogo) kwa kila milioni ya urani na toli na asilimia ndogo ya kali. Katika ufanyanzi mnururisho unaotolewa na mionzi ya ulimwengu huviza vifaa vya fuwele kama vile kwatzi. Ule ufanyikaji wa *ioni* unaotokea hapo husababisha kutoka kwa elektroni ambazo, zikipashwa moto, hutawanyika na kutoa nishati yake ya ziada katika umbo la fotoni (yaani chengachenga za mwanga).

24 V. Bucha, 1970, kur. 47-55; Bucha, 1971, kur. 57-117



Nguvu ya nuru hii, au mwanga-joto, inahusiana moja kwa moja na umri wa kielelezo cha vyungu, lakini pia inategemea vile viambajengo mahsusi vya mwanga-joto vilivyomo katika sampuli za vyungu na mazingira yake.<sup>25</sup> Kwa kupima kiasi cha urani, toli na kali zilizoomo katika vielelezo vya vyungu na udongo uliovizunguka, inawezekana kupima kiasi cha mnururisho ambacho kielelezo kinapata kila mwaka. Kimsingi umri wa kielelezo hicho hubainishwa kwa mujibu wa mlingano ufuatao:<sup>26</sup>

$$\text{umri} = \frac{\text{kiasi cha mnururisho kilichokusanyika}}{\text{kiasi cha mnururisho kwa mwaka}}$$

#### *Usahihi wa matokeo na uwezekano wa kutumia mbinu hii*

Hivi sasa usahihi halisi wa kiasi cha asilimia 10 zaidi au pungufu hupatikana kwa kutumia mbinu hii. Matokeo haya si sahihi sana kama yale yaliyopatikana kwa kutumia redio kaboni ili kukadiria umri na kasoro hiyo kutokana na matatizo mbalimbali yanayozuka, kama vile hali ya pale pahala ambamo kielelezo kinefichika na kiasi cha unyevu wa udongo uliokizunguka.

Japokuwa mbinu hii ina ushahidi mdogo tu, inaishinda ile ya redio kaboni kwa vile maeneo ya kiakiolojia kwa kawaida huwa na vielelezo vingi zaidi vya udongo kuliko mata za ogani. Zaidi ya hayo, tukio ambalo umri wake unakadiriwa ni lile la wakati ambapo chungu kilipochomwa hasa ilihali ukadiriaji wa umri wa mti au makaa kwa redio kaboni unalingana na tarehe ya kukatwa kwa mti na siyo tarehe mti ulipotumika.

Mbinu hii inaweza kutumika sana huko Misri. Mpaka sasa ukadiriaji umri wa tamaduni za Neolithi na za kabla ya Ufalme ulifanyika kwa mujibu wa aina ya vyungu vilivyotumika wakati huo, lakini sasa itawezekana kuyakinisha umri hasa wa tamaduni hizo kwa njia ya mwanga-joto.

#### *Mbinu zinazotumika katika utafutaji wa kiakiolojia*

Madhumuni ya msingi ya utumiaji wa mbinu za kisayansi za utafutaji wa kiakiolojia uwandani, ni kutafuta habari kuhusu maeneo yaliyofichika ya kiakiolojia kabla hayajachimbuliwa au bila ya kulazimika kuyachimbua kabisa. Mbinu hizi huokoa wakati, juhudi na gharama. Miongoni mwa mbinu za kisayansi zinazotumika katika utafutaji wa kiakiolojia hizi zifuatazo zinaweza kutajwa:

#### *Upigaji picha wa angani*

Kimsingi mbinu hii hutumika sana kutambulisha alama za kiakiolojia kutokana na mpangilio wake wa kijometri. Mbinu hii ina inatumizi mawili muhimu. Kwanza inaonyesha mandhari yaliyo wazi zaidi kutoka juu ya zile sehemu ambamo alama moja moja za nje huungana pamoja kufanya ruwaza ya jumla yenye maana.<sup>27</sup> Kwa hiyo picha za angani huweza kutumika kuyatambua maeneo yanayohitaji kuchimbuliwa ili picha kamili ya mchangamauo kamili wa kiakiolojia uweze kupatikana. Njia hii ilitumiwa kuyachungua mabekalu ya Karnak, huko Luxor, chini Misri kwenye eneo la ukubwa wa kiasi cha hekta 120. Matumizi ya pili ya mbinu hii yamekusudiwa kudhihirisha kuwepo kwa miundo iliyofichika ya

25 M.J. Aitken, 1970, kur 77-88; E.T. Hall, 1970, kur. 135-141

26 M.J. Aitken, 1970, kur. 77-88

27 R.E. Linington, 1970, kur. 98-108

kiakiolojia katika ardhi zilizolimwa kutokana na alama zilizofanyika katika mazao kwa sababu ya hali tofauti ya unyevu wa udongo. Mazao yanayoota juu ya ukuta wa mawe uliofichika huwa dhaifu na yenye rangi isiyokoza, wakati yale yanayoota juu ya handaki lililofichika hustawi zaidi na kwa hivyo huwa na rangi iliyokoza zaidi. Ruwaza ya kijometri inayofanywa na alama hizi huwezesha kutambulisha miundo iliyofichika ambayo baadaye huweza kuchimbuliwa.<sup>28</sup>

### Uchanganuzi wa udongo

Masalia ya miji ya kale iliyokuwa ikikaliwa na watu na makaburi huweza kutambuliwa kwa kuchanganua udongo. Kwa vile fosfati ya kalisi ndiyo kiambajengo muhimu cha kiunzi pamoja na taka nyingine za binadamu, kiasi cha fosfati ya kalisi kilichopo bila shaka kitakuwa kikubwa zaidi kwenye ardhi ambayo ilikuwa ikikaliwa na binadamu au ikitumiwa kwa ajili ya kuzikia. Kwa hivyo mipaka ya maeneo ya aina hiyo ya kiakiolojia inaweza kubainishwa kwa kupima kiasi cha fosfati iliyomo.

### Uchanganuzi wa chavuo

Mimea ya maua kwa kawaida huchavushwa na ndege, wadudu au upepo. Maua yaliyochavushwa kwa upepo hutoa chembe nyingi za chavuo ambazo nyingi yazo huanguka chini bila ya kutumika. Kwa kawaida chembe hizi huozwa, lakini iwapo itatokea zikaangukia udongo unaofaa, kama vile wenye topetope au wenye miti iliyooza huenda zikageuka visukuku na hapo tena kuweza kuchunguzwa kwa hadubini. Utambulishaji wa uorodheshaji wa aina mbalimbali za chavuo zilizomo kwenye kielelezo husaidia katika habari zinazoweza kutolewa kuhusu mazingira ya ikolojia ambamo masalia na vifaa vya binadamu vilikuwa na ujuzi wa mazingira hayo kwa upande wake, yanaweza kuashiria mtindo wa maisha kwa wakati ulc.

### Upimaji wa ukinzania wa umeme

Hii ilikuwa mbinu ya mwanzo ya kijiofizikia iliyotumiwa katika akiolojia. Mbinu hii huhusika na upelekaji wa mkondo wa umeme ardhini na kupima ukinzani wake. Hii hutegemea maumbile ya udongo wenyewe, kiasi cha maji yaliyomo katika ardhi na chumvi zinazoyeyuka zilizomo. Miamba migumu na iliyoslikamana kama vile itale na diti huonyesha ukinzani mkubwa zaidi ikilinganishwa na udongo wa mfinyanzi. Kwa hivyo upimaji wa hali ya ukinzani utatumika zaidi kugundua miundo iliyojengwa kwa mawe yaliyofika kwenye udongo wa tope au miundo iliyochongwa miambani ambayo baadaye ilijaa udongo.<sup>29</sup>

### Upimaji kwa njia ya sumaku

Hii ndiyo mbinu inayotumika sana livi sasa katika utafutaji wa kiakiolojia. Mbinu hii huhusu upimaji wa nguvu za uga wa sumaku ya Dunia kwenye sehemu zilizo juu ya ardhi katika maeneo yanayofanyiwa utafutaji. Tofauti za vipimo zinaweza kudhihirisha kuweko kwa alama za kiakiolojia. Mbinu hii inaweza kutumika kugundua masalia ya chuma yaliyofichika, miundo iliyofungwa na kuokwa kama vile majoko na matanuri, fito zilizojaa udongo na kushindiliwa miambani au miundo ya miamba iliyofichika katika udongo wa mfinyazi.

28 M.J. Aitken, 1961

29 M.J. Aitken, 1961

Mabadiliko muhimu katika nguvu za sumaku yameonekana katika vitu vya chuma vilivyofichika lakini mabadiliko haya hayana nguvu sana katika vitu vingine. Kwa hivyo upimaji wa sumaku unaweza kuwa na manufaa ikiwa tu chombo kinachotumika kina uwezo wa kutosha na kugundua mabadiliko yaliyo madogo sana kama ilivyo kwa mitasumaku ya protoni iliyovumbuliwa katika Chuo Kikuu cha Oxford.

Upimaji wa sumaku una faida nyingi kuliko ule upimaji wa ukinzani wa umeme, kwa vile upimaji wa sumaku ni rahisi na mwepesi zaidi kutumia, na matokeo yake pia ni mepesi kuyafasiri.<sup>30</sup>

### Uchunguzi wa mapiramidi ya Misri kwa kutumia mionzi ya ulimwengu

Mionzi ya anga huwa na mchirizi wa chembe chembe zilizosheheni umeme zijulikanazo kwa jina la 'numesoni' au 'muoni'. Mionzi hii huifika Dunia kwa nguvu sawa kutoka sehemu mbalimbali angani. Mionzi ya anga ina nguvu zaidi ya kupenya kuliko mionzi ya eksirei na kasi-mwelekeo wake ni karibu sawasawa na mwendo wa mwanga.

Msingi wa uchunguzi wa mapiramidi kwa kutumia mionzi hii ni kwanza muoni hupoteza nishati wakati zinapopita kwenye mata. Huko kupotea kwa nishati (au ufyonzaji wa muoni) kunawiana na uzito na unene wa mata ambamo muoni hupitia. Nguvu au kiasi cha mionzi ya anga inayopita katika mata inayochunguzwa huweza kukadiriwa kwa chombo kinachojulikana kama chembacheche ambacho huwekwa katika chumba cha chini ya ardhi udani wa mapiramidi. Muoni zilizopita kwenye nafasi tupu (au kwenye chemba au kwenye ujia usiojulikana) hupunguzwa mwendo wake kwa kiasi kidogo zaidi kuliko zile zinazopitia kwenye mwamba mgumu. Kwa hivyo mionzi ya anga inayopita kwenye nafasi tupu huwa na nguvu zaidi. Ukweli huu hugunduliwa na chembacheche. Kwa kutumia chembacheche mbili zilizopangwa kwa ulalo, moja juu ya nyingine, kwa umbali wa mita 0.3 inawezekana siyo tu kugundua kuwepo kwa chemba iliyofichika bali pia kuonyesha mahali ilipo katika eneo la mita ehache. Uchumbuaji huweza kuanzishwa kuelekea ule upande wa nafasi tupu au chemba kama ilivyoashiriwa na ile mionzi.

Mbinu hii ilianza kutumika katika uchunguzi wa Piramidi la Pili ambalo lilikuwa la Mfalme Chephren wa Ufalme wa Nne (miaka 2,600 kabla ya Enzi ya Kristo) na umewezesha kupatambua mahali hasa penye chemba alimozikwa Mfalme.

### Mbinu za kuhifadhi

Katika Afrika, tatizo la kuhifadhi limefungamana sawa na ule uhafifu mkubwa wa vitu vilivyohusika na hali ya kuharibika sana kwa minara ya mawe.

#### Uhafifu mkubwa wa vifaa

Kutokana na hali ya joto jingi na ukavu katika sehemu nyingi za Afrika, vifaa vilivyotengenezwa kwa maada za oganiki, kama vile, mafunjo, ngozi, miti, penbe za udovu na kadhalika vina tabia ya kuhafifika. Vifaa kama hivi havina budi viangaliwe vizuri la sivyo vinaweza vikavurugika. Katika tabia ya hali ya nehi yenye ukavu inabidi kwanza vitu hivyo vihifadhiwe mahali palipo ua unyevu na palipofungwa, vifungwe katika karatasi inayofyonza maji au iliyopitishwa kwenye mvuke katika chombo muafaka ili ule ulaini wa vitu hivi

30 R. E. Linsington, 1970 kur. 89-108

uweze kurejeshwa kikamilifu au walau kwa kiasi fulani. Baada ya taratibu hizi vitu hivi vinaweza kukunjuliwa bila ya kuvunjika vipande vipande.

Vikisharejea katika hali yake ya ulaini, vifaa hivi havina budi kuonyeshwa au kuwekwa katika makumbusho au mabohari yenye mitambo ya baridi kiasi cha digrii 17+ nyuzi 2C (na unyevu hewa wa asilimia 60-65) ili vitu hivi visihafufike tena kama itakavyokuwa vikiachwa kwenye hali ya hewa iliyo kavu.

### Kuharibika sana kwa minara ya mawe

Kuharibika kwa minara ya mawe ni tatizo kubwa ambalo litazingatiwa kwa urefu zaidi hapa chini:

#### *Sababu kubwa za uharibikaji*

Vitu vinavyosababisha kufisia sana kwa mawe Afrika ni hivi vifuatavyo:

#### Kuhama kwa chumvi

Kukiwa na maji au unyevu katika udongo wenye chumvi, zile chumvi zinazoyeyuka huhama katika minara ya mawe kutokana na kaida inayojulikana kama kupanda kwa kapilari. Katika tabia ya hali ya nchi yenye ukavu, chumvi hizi husafiri katika hali ya unajimaji kutoka ndani ya jiwe mpaka sehemu ya juu na kusababisha jiwe kuchanganuka, vinginevyo chumvi hizi huweza kubaki chini ya gamba la juu la jiwe na kusababisha libanduke. Taathira kama hii huonekana zaidi sehemu za chini za kuta au mihimili kwa vile jiwe hugusana moja kwa moja na udongo wenye chumvi, kama inavyoweza kuonekana katika mihimili ya hekalu la Buhén, huko Sudan.

#### Mabadiliko makubwa ya angahewa

Katika Afrika, jiwe huathiriwa sana na tofauti kubwa ya halijoto na unyevu, hali ambazo mwishowe husababisha kubanduka kwa tabaka la juu la mawe ya aina nyingi.

Katika maeneo mengi, hasa katika sehemu za mwambao, sababu zote mbili za ufisaji, kwa pamoja husababisha uharibifu mkubwa katika minara, kama ilivyo katika mahekalu ya Kirumi huko Leptis Magna na Sabratha, nchini Libya.

#### *Uhifadhi usiotosheleza wa sehemu za nje za mawe*

Majaribio makubwa yamefanywa katika juhudi ya kutengeneza sehemu za juu za mawe, kama vile kuyahifadhi kwa vikingaogani au kwa silikiti zisizo ogani. Uhifadhi wa aina hii si kama tu haufai, bali kwa hakika, ni wa hatari sana kwa vile huharakisha kuharibika kwa jiwe na kusababisha magamba kuanza kubanduka.

Katika muda unaoanzia 1962 mpaka 1975, Kamati ya Kimataifa yenye mabingwa 10 katika fani ya kuhifadhi mawe ilizingatia matatizo ya kuharibika kwa mawe na matatizo ya kuyahifadhi.

#### *Matumaini mpya ya kupata ufumbuzi*

Profesa Lewin amegundua njia mpya kuimarisha sehemu za nje za gange na marumaru.<sup>31</sup> Katika kutumia njia hii, sehemu zilizo haribika huhifadhiwa kwa mweyusho uliotengenezwa

kwa bari, urea na gliseroli. Baada ya uhifadhi huu jiwe huwa gumu zaidi na lenye uwezo wa kustahimili athari za uharibifu.

Njia hii ilitumiwa Julai, 1973 ili kuimarisha sehemu ya nje ya shingo ya sanamu ya gange ya Sphinx iliyopo Giza. Matokeo yake mpaka sasa yamekuwa ya kuridhisha, lakini sanamu hiyo itabidi iwe katika uchunguzi kwa muda usiopungua miaka kumi kabla mbinu hii ya kuzuia kuharibika kwa gange kuweza kukubalika.

#### *Hatua za kutengemaza*

Ingawa tunaweza kuwa na matunaini juu ya mbinu iliyogunduliwa na Profesa Lewin, bado tatizo lililotangamana na utumiaji wa kemikali kuhifadha minara ya mawe halijatatuliwa. Kwa sasa hatua kadha za kuimarisha miundo zinaweza kupendekezwa, nazo ni:


1. Schemu za nje za minara iliyo nje ambayo hupata mionzi ya jua moja kwa moja ihifadhiwe kwa myeyusho wenye vikinga vinavyoziba vitundu vilivyomo katika miamba, kwa sababu kwa kufanya hivyo matabaka ya nje yanaweza kukwanguka.
2. Ule udongo ambapo minara imejengwa usafishwe mara kwa mara ili kuondoa mkusanyiko wa chumvi kwa kutumia maji ambayo baadaye huondolewa kwa kuchimba mitaro.
3. Pale ambapo minara imefyonza chumvi zinazoyeyuka ambazo huweza kufanya kuvu, inapasa chumvi hizi zioshwe na kufunika sehemu zilizoathiriwa na chumvi kwa udongo mbichili wa mfinyanzi wenye mchanga mpaka karibu chumvi yote itoke.
4. Iwapo hiyo minara ni midogo, basi inaweza kuondolewa iuko nje ilipo na kuweka katika jumba la makumbusho au mahali palipohifadhika, ambapo inaweza kusalimika na taathira mbaya ya angahewa.
5. Iwapo minara hauna paa, paa halina budi lijengwe ili kuhifadhi michoro ya kuta za ndani au nakshi ili zisipate mwanga wa jua na mvua. Hii, kwa kiasi fulani, itaweza kuzuia uharibifu unaosababishwa na mabadiliko makubwa ya halijoto na unyevu.

#### *Mapendekezo kuhusu kazi ya matengenezo*

Utando wa nje wa minara mikongwe usioshwe wala kuondolewa kwa namna yoyote kwa madhumuni wa kurejesha rangi ya asili ya jiwe. Usafishaji wa sehemu ya mbele ya minara ufanywe kwa kuondoa vumbi tu bila kugusa utando huo ambao ndiyo sura muhimu kabisa ya kiakiolojia ya minara.

Minara mikongwe inapotengenezwa upya, jambo la kufanya ni kuzijenga zile sehemu zilizoanguka mahali pale pale pa asili. Ubadilishaji au uongezaji wa vitu vingine uepukwe isipokuwa kama utahitajika ili kushikilia sehemu zilizoanguka au kuhifadhi sehemu kongwe za juujuu zisiathirike na hali ya hewa.

Chokaa iliyotumika kutengeneza kuta lazina, ifanane na chokaa ya asili, isipokuwa kama ilifanywa kwa jasi. Chokaa inayopendekezwa katika kazi zote hizi za kujenga tena ni ile isiyo na chumvi na yenye mchanganyiko wa chaki na mafuta, kwa vile chokaa hii ni laitii na hupenyeka na hivyo haizuii mjongeo mdogo wa mawe unaosababishwa na mabadiliko ya halijoto. Kwa hivyo hakuna hatari kubwa ya kuvutika au kupasuka kunakoweza kutokca.



# *Historia na isimu na nadharia kuhusu mbari na historia ya Afrika*

## *SEHEMU YA 1: Historia na isimu*

*Aada koy demgna woni* (Kifuldefulde)

*Lammii ay dekkal demb* (Kiwolof)

Lugha ndiyo inayoisanifu kale

Mwafrika huona kiungo baina ya historia na lugha kila ageukapo '*Hanki koy daarol awratee*' kama wasemavyo Wafulani: "Twaona zamani katika hadithi". Wazo hili linafanana na fikra ya Wagriki na Waarabu. Lakini kwa upande wa Waafrika, kutokana na ukosefu wa maandishi mara nyingi, sifa maalumu ya kihistoria ni kwamba huonekana zaidi katika umbo la hekima kuliko sayansi kama sanaa ya maisha inayodhihirika kauka lugha.

Isimu, sayansi ya lugha, inaathiri historia kwa namna mbili. Kwa upande mmoja lugha ikiwa kama mfumo na chombo cha mawasiliano ni kaida ya kihistoria. Kwa upande mwingine historia ni zao la lugha kwa sababu mbili: kama mazungumzo na kama ushabidi wa kihistoria.

Kila lugha inaweza kutoa data ya kiufundi kutokana na muundo wa lugha yenyewe. Lakini pia inaweza kutoa data ya mambo yasiyohusu lugha ambayo yanaelezca mazingira kwa jumla. Lugha ni kioo cha maisha ya watu na ustaarabu wao.

### *Sayansi za lugha na historia*

Sayansi zote zinazohusiana na lugha zinaweza kuwa za manufaa kwa historia. Lakini baadhi ya sayansi huweza kuchangia moja kwa moja kuliko nyingine. Kwa mfano, kutalii juu ya uhusiano baina ya lugha huweza kuwapatia wanahistoria vidokezo kuhusu uhusiano baina ya jamii za watu. Lakini, ingefaa kuongezea kwamba hata ulinganishi kama huu hauwezi kufanyika isipokuwa kwa kuchunguza muundo wa ndani wa lugha zinazohusika. Hii ndiyo sababu hakuna tawi la isimu ambalo wanahistoria wanaweza kulipuza kabisa.

### *Uainishaji wa kisayansi wa lugha na historia za watu wa Afrika*

Kuainisha lugha mbalimbali ni njia mojawapo ya kutsalii uhusiano baina ya watu. Mianinisho ya aina mbalimbali inaweza kutofautishwa.

*Uainishaji wa kijenetiki*, ambao huwa ni wa kina sana unawezesha kugundua uhusiano wa kinasaba, na kwa kufanya hivyo kupata mahusiano ya asili kabisa katika kikoa cha lugha.

*Uainishaji wa kitapolojia* hukutwa kwenye kigezo cha muundo tu kama vile maumbo ya majina vitenzi. Maumbo hayo yanaweza kufanana katika lugha ambazo hazina uhusiano wowote kama vile Kiwolof na Kiingereza. Kwa hivyo kufanana kwa taipolojia hakuna maana kuwa lugha hizo zinahusiana. Lakini pia tofauti za kitapolojia hazina maana kwamba lugha zinazohusika hazina uhusiano wowote. Wakati mwingine ni muhimu kwenda nje ya msamiati na kuvitalii vipengee vya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksi ili kubainisha uhusiano wa kinasaba kama upo.

*Uainishaji wa kijografia* unawakilisha hatua ya mwanzo kabisa ambapo lugha zilizo karibukaribu hujumuisha katika kundi moja. Huu ndio mtindo wa kawaida uliotumiwa mara nyingi kuanisha lugha za Kiafrika katika makundi kama vile Atlantiki Magharibi, Senegal-Guinea, Niger-Chad na nyinginezo. Mbinu hii hasadifu kwa sababu haizingatii maingiliano ya kiisimu yanayotokana na uhamaji, uvamizi, na kadhalika.

Uainishaji wowote wa dharti sharti uzingatie vipengee vinavyojitokeza katika kila lugha na uonyeshe kwamba kufanana huko si kwa bahati wala si matokeo ya ukopaji wa maneno ya lugha nyingine. Kwa mfano katika baadhi ya lahaja za Kiswahili takriban 60% ya maneno ni ya asili ya Kiarabu. Lakini katika muundo wake ni dhahiri kuwa Kiswahili ni lugha ya Kiafrika.

Uchanganuzi wa lugha kwa ajili ya uainishaji lazima pia uzingatie mabadiliko ya kifonotiki, kimofolojia na kisintaksi ambayo wataalamu wana uwezo wa kuyagundua na ambayo si kikwazo katika uainishaji. Kwa mfano maumbo *neds* (Kimisri cha kale), *neddo* (Kifulfulde) *nit* (Kiwolof) na *ned (a)* (Kimore) lazima yanahusiana.

#### Kuunda upya lugha

Kuunda upya lugha ni dhana yenye maana ya kuchanganua lugha kwa kurudi nyuma hadi kufikia mame-lugha zinakochipukia lugha mbalimbali za kikoa kimoja. Uchanganuzi huo huweza kufanyika kwa kuchukua mabadiliko ya sauti kuwa ndio msingi. kwa mfano ikifahamika kwamba katika lahaja moja *p* inabadilika kuwa *f* na katika lahaja nyingine *u* lubadilika kuwa *o* na kadha wa kadha basi *Fa + Pa, Lu + Lo* na kadhalika. Kwa njia hiyo maumbo ya asili yanaweza kuundwa upya. Baada ya kutazama kipengee cha fonolojia twaweza kutazama kipengee cha kileksika na kuchunguza asilimia ya maneno ya aina moja katika msamiati wa lugha zinazolinganishwa. Hata hivyo ulinganishi huu pekkee hauthibitishi chochote. Mwisho, kuna mfanano wa kinuundo katika jina, kiwakilishi nafsi, kitenzi na mifumo mingine inayohitaji kuchunguzwa.

Milinganisho kama hiyo ikishafanyika kwa uangalifu, umri wa vitu na lugha inayohusiana na vitu hivyo vinaweza kukisiwa. Inawezekana pia kuonyesha uhusiano baina ya lugha hizo katika kielelezo cha mti wa lugha. Uchambuzi huu waweza kutupa mwanga mkubwa juu ya historia ya mbari na staarabu za mataifa au mbari mbalimbali.

Utafiti kama huu unakuwa rahisi ikiwa lugha zinazochunguzwa zimeandikwa kwa muda mrefu kiasi. Lakini kazi hii inakuwa ngumu sana ikiwa lugha zinazohusika zimeanza kunukuliwa hivi karibuni ingawa msamiati wa msingi wa jamii za mwanadarau hubadilika polepole sana.

Kwa mfano katika Afrika Kusini mwa Sahara, kwa kuchukua maneno ya Waafrika wengi yaliyohifadhiwa toka karne ya kumi na moja na kuendelea, kwanza katika Kiarabu na hatimaye katika matini za kizungu, imewezekana kukadiriwa kiwango cha mabadiliko ya maneno na hivyo kuwezesha maneno mengine kutumika kama ishara ya kuonyesha maendeleo ya jamii inayoyatunika.

Mtazamo huu unakwenda mbele zaidi. Watafiti kama Swadesh wamedai kwamba ingawa msamiati wa utamaduni wa jamii fulani unaweza usiwe imara msamiati wa msingi - majina ya selemu za mwili, kaida muhimu au za kimaumbile, na tarakimu toka moja mpaka tano - huwa ni imara sana. Wanadai kwamba kiwango cha kubadilika polepole kwa msamiati wa msingi ni sawasawa katika lugha zote na kwamba kunaweza hata kupimwa. Hata hivyo fomula ya hisabati alizotunga Swadesh kupima muda ambao lugha mbili zilitengana kulingana na madai yake imetumika wa lugha za Kivolita na matokeo yake hayakuhitimika pengine kwa sababu mambo mengine yaliyo nje ya lugha yanaweza kuathiri kiwango cha mabadiliko.

### *Mwainisho wa lugha na uhusiano wa kimbari na kitamaduni*

#### **Kuwepo kwa uhusiano**

Uchunguzi mbalimbali uliofanywa na wanaisimu katika Afrika umeonyesha mifano madhubuti ya uhusiano uliopo baina ya makundi kadha ya lugha; W.H.I. Bleek alionyesha uhusiano huu mnamo mwaka 1862 baina ya lugha za Wabantu. Kadhalika kazi za Mlle Homburger na Cheikh Anta Diop zimesisitiza unasaba uliopo kati ya lugha ya kale ya Misri na lugha nyingi zilizopo katika Afrika kama vile Kihausa, Kiwolof na Kisonghay.

Isitoshe lugha nyingine za Kiafrika zimesambaa kiasi cha kungilia lugha nyingine nyingi na kutumika kama njia ya mawasiliano au hata wakati mwingine kuchukua nafasi zao. Hii inadhihirika katika lugha kama vile Kilingala, Kihausa, Kiswahili, Kiyoruba, Kitwi, Kübo, Kibambara-Dyola, Kifulfulde, Kiwolof, n.k. ambazo zinazungumzwa na mamihioni ya watu wenye asili tofauti. Kutokana na mtazamo huu lugha kuu za Afrika Mashariki na Kati ni Kiswahili na Kilingala, ambapo katika Afrika Magharibi ni Kihausa na Kimbambara-Dyola. Kiarabu pia kimesambaa pembeni mwa Sahara upande wa Kusini na pwani ya Afrika Mashariki.

Waafrika wenyewe huhisi pengine bila ya kunena, unasaba katika lugha zao ambazo wao huchukulia kwamba ni dalili ya kuwapo kwa uhusiano wa kidamu kati yao, au huwa ni matokeo ya uhusiano luo. Hisia hizi hudhihirika baina ya Wafulani na Waserer, Wafulani na Watokolor, Wamarka na Wasarakole, Wabisa na Wasani; n.k. Hata hivyo iko haja ya kubainisha msingi thabiti ya kiisimu au ya kihistoria ya uchunguzi jarabati kabla ya kuthibitisha au kukataa visaasili au hekaya za asili zilizojaa maelezo na visa.

Kwa upande wa sayansi ya etimolojia, na asili za msamiati, kinyume chake, mabingwa wa Kiafrika wa historia ya maneno — wanamapokeo wa lugha — wako katika kila mbari.

Tangu karne ya kumi na tisa, lugha za Kihindi, — Kizungu zimekuwa zikifanyiwa utafiti wa ulinganishi, na wanaisimu wamefanya utafiti kama huo kuhusiana na lugha za Kiafrika. Miongoni mwao ni W.H.I. Bleek, akifuatiwa na Meinhof na baadaye Guthrie kwa upande wa lugha za Kibantu, Delofosse kwa upande wa lugha za Afrika Magharibi; C.L. Lepsius, A.N. Tucker na G.W. Murray kwa lugha za Kiniloti; Besset kwa lugha ya Kiberiberi; Bauman na Westernmann; na J.H. Greenberg, ambao walitoa mchango wao kabla ya ugunduzi madhubuti kufanywa na Waafrika wenyewe. Hata hivyo baadhi ya wanazuoni wanadai kuwa mahitimisho yaliyofikiwa, kuhusu lugha hizi yamefanywa mapema mno kwani ufafanuzi makini wa kisayansi wa lugha zote zinazohusika ndio tu hutuwezesha kufanya ulinganishi wa kitaipolojia au wa kijenetiki ambao kwa sasa bado ni wa kukisiwa tu.

#### **Haja ya utafiti zaidi**

Hata kazi ya kuorodhesha lugha zote za Kiafrika haijafanywa katika misingi ya kisayansi. Kwa kukisia katika Afrika kuna mifumo ya usemaji kati ya 1,300 na 1,500 ambayo inaweza



kuaninishwa kama lugha lakini kwa hakika nyingi kati yazo pengine ni lahaja tu za lugha mama. Tukizingatia kwamba monografu kuhusu lugha hizi mara nyingi haziwi na maneno mengi yaliyonukuliwa kwa usahihi, ni dhahiri basi kwamba wakati haujafika wa kufanya usanii kamambe wa lugha zote za bara zima. Maeneo matatu ya Kiisimu yanaweza kuchukuliwa kuwa mifano ya kiasi ambacho mahitimisho ya awali hayaaminiki madhali bado kungalipo kutokukubaliana kuhusu data na mbinu.

Kwanza uhusiano kati ya lugha zinazodaiwa kuwa za Wanegro Waafrika na Kisemeti ambazo kwa miaka mingi sana zimekuwa zikiingiliana, sio rahisi kuzitenganisha hasa kwa vile data ya Kimisri cha kale ni ya tangu miaka 4,000 iliyopita na ile ya Kisemiti ni ya miaka 2,500 iliyopita ilihali uchunguzi wa lugha za Kichadi, Kikushiti na Kiberiberi umekitwa tu kwenye taarifa za kuaminika zinazoanzia karne ya kumi na tisa na kuendelea. Mnamo 1947, M. Cohen alipotoa kitabu chake cha *Essai Comparatif Sur le Vocabulaire et la Phonetique du Chamito-senitique*, ambamo lugha ya Kimisri, Kiberiberi, Kisemitiki, Kikushiti na Kihausa zililinganishwa mara moja alishambuliwa na Leslau na Hinze. Greenberg alilitenga kundi la Kichadi ambalo mipaka yake haikuwa dhahiri kutoka kwenye kundi aliloliunda Cohen kwani baadhi ya Wanaisimu wameona kuwa kuna uhusiano kati ya kundi la "Kichadi" (Sara) na lugha zilizoanishwa kama lugha za "Atlantiki Magharibi", kama vile Kisereri, Kifulfulde, Kiwolof n.k. Ingawa hapo mwanzoni mazoea yalikuwa ni kuongezea lugha za bara la Afrika kwenye kundi la Kisemiti lililolulikana zaidi, siku hizi wanaisimu wanapendelea kuziainisha katika makundi ya lugha za "Wanegro wa Afrika" Ushahidi wa jambo hili ulionekana katika kongamano kuhusu "Uhamiaji wa Watu Katika Misri ya Kale" lililoandaliwa na UNESCO huko Kairo mnamo mwaka 1974, ambapo ilielezwa kwamba Misri ya Kale isingeweza kutenganishwa na muktadha wake wa Kiafrika na asili yake isingeweza kuelezwa kikamilifu kwa kutumia vigezo vya Kisemiti.

Pili, kuna matatizo makubwa ya uainishaji kuhusu lugha za Kikushiti (Kisomali, Kigala, Kisidamo, n.k.) ambayo yamesababisha kuwepo kwa mianisho mitatu tofauti kutegemeana na kila mwanaisimu, akiwemo mtaalam wa Kisovieti, Dolgopolskij ana uainisho wake anaongelea. Mitazamo ya tatizo hili inatofuatiana sana. Wakati milinganisho ya Greenberg ilizingatia msamiati, milinganisho ya Tucker na Bryan ilikitwa katika mfumo wa kiwakilishi nafsi na muundo wa kitenzi.

Mwisho kundi la pwani ya "Atlantiki Maghribi" kuanzia Mauritania Kusini hadi Sierra Leone bado ni swala lenye ubishi mwingi kwani Koelle ambaye mahitimisho yake yaliungwa mkono na Delafosse na Esternmann wakifuatiwa na Greenberg, alitambua sifa maalumu za kundi hili ambapo W. Wilson, D. Dalby na D. Sapir wana shaka juu ya uasili wa kundi hilo. Mabishano kama haya ambayo yanaweza kuwa yenye manufaa, yataendelea madamu monografu za maelezo zilizopo hazitoshelezi.

### Upotofu wa kiitikadi

Historia na itikadi mara nyingi huenda sambamba. Mitaala ya kwanza ya kiisimu na kihistoria yenye upeo mkubwa iliyofanyika barani Afrika ilifanyika Sadfa na wakati wa biashara ya watumwa na baadaye wakati wa ukoloni. Ndiyo maana mitaala hii ina mitazamo ya kizungu na ubaguzi wa rangi. Nadharia ya Kihamiti ilitungwa kuelezea kuwa maendeleo yoyote ya kihistoria yanayoonekana barani Afrika ni matokeo ya kitendo cha kustaarabisha cha wataamalaki wupeu au wa 'kikahawia', wa mwisho wakiwa wakoloni waliotumwa na ubeberu wa kibepari.<sup>1</sup>

Watu kama C.G. Seligman aliyeandika kitabu kilitwacho *Races of Africa* waliziona harakati za kihistoria na mahusiano ya lugha barani Afrika kwa jicho la ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa "kikabila" na alipotaka kueleza asili ya maendeleo yaliyokuwepo Afrika Mashariki na Kati miongoni mwa Bantu, hakuona njia nyingine isipokuwa kuyahusisha na "Watu weusi waliothiriwa na Uhamiti." W. Taylor alifikia hata kuandika kuwa "Kutokana na utajiri wake wa msamiati, ufasaha wake na vivuli mwanana vya maana, kwa kweli sidhani lugha hii (Kifulfulde) imo katika kikoa cha lugha za Kisudani (lugha ya watu weusi)." Kutokana na hali hii kumekuwapo na mkanganyiko mkubwa kati ya aina za watu, lugha, utamaduni, mbari, na kadhalika.

Ukweli ni kwamba, kinyume na mtazamo potofu dhidi ya lugha za Kiafrika kama ulivyoelezwa hapo juu, lugha za Senegal (Kiwolof, Kifulfulde, Kisereri, n.k.) zinakaribiana kwa kiasi kikubwa na lugha za Kibantu kuliko na lugha za Ki-Mande zinazopakana nazo. Kimisri cha kale kinakaribiana zaidi na lugha za Wanegro wa Afrika kuliko na Kisemiti au lugha zenye asili ya Kikhindi-Kizungu ambamo kunesilimishwa. Kifulfulde, lugha ya Wafulani ni lugha ya "Wanegro wa Afrika" ambapo lugha ya Kihausa iliyotumiwa na mataifa yaliyokuwa yakitawaliwa na Wafulani katika dola za Waislamu za Sudani ya Kati inahusiana na kundi linalodhaniwa kuwa ni la Kihamiti. Kwa karne nyingi tawala za Ki-Mandingo na Ki-Wolof chini ya mamlaka ya wana-ufalme wascmao lugha za "Wanegro wa Afrika" ziliwadhibiti watu ambao waliainishwa na wanaisimu wa kibaguzi kama Wahamiti, watu walioishi kabla ya Wahamiti au Waberiberi. Kwa mfano idadi kubwa ya makundi ya Wafulani walidhiarauliwa na Wamossi, Wabambara, Wasonghay na wafalme wengine wa Sudan.

## Sayansi jalizi

### Uchanganuzi wa kitaipolojia

Taipolojia ya kitamaduni, kama inavyoeleweka kwa watu wanaosema Kiingereza na fafanuzi za mibembeo ya kitamaduni zilizotolewa na Shule ya Mawazo (ya Kijerumani) ya watu kama Vile Frobenius, Bauman na Westermann zimeelekea kuficha ukweli kuhusu lugha. Hii ni kwa sababu mambo ya kitamaduni yasiyohusiana na lugha, kama vile matumizi na ufuaji chuma, miundo ya serikali, kundi la miungu na kadhalika yanaingilia na kurahisisha uchanganuzi wa kitaalamu wa lugha kiasi kwamba katika uwanja huu unasaba Kiisimu unaishia kuwa matokeo tu ya mahusiano ya jumla ya kitamaduni.

### Sayansi ya majina

Sayansi ya majina hujumuisha mitaala ya majina ya mahali (toponimia), na majina ya watu (antroponimia), majina ya mito na maziwa (hidronimia), n.k. Majina kama haya yanawakilisha mojawapo ya miongozo ambayo hutolewa na lugha katika kugundua mawasiliano, maingiliano na athari za kihistoria. Majina ya ukoo yanaonyesha mbari au tabaka ambalo shughuli zake zinaweza kufuatiliwa nyuma kutokana na kuwepo kwa majina kama haya.

Toponimia ni visukuku vinavyomsaidia mwanahistoria katika maelezo yake. Baadhi ya viambishi tamati au viambishi awali kama vile *dugu* katika lugha za Ki-Mande, *saare* miongoni mwa lugha za Kifulani *ker* miongo mwa lugha za Kiwolof na Kiarabu-Berberi, *daaru* katika Kihausa n.k. vinavyotunika kutaja vijiji au miji vindokeza moja kwa moja waasisi wanaofikiwa kuwa walianzisha makazi hayo pamoja na njia walizopitia watu.

matumizi ya alama kuwakilisha sauti (alamasauti). Mathalani mchoro wa jembe hapo mwanzoni ulimaanisha zana yenyewe. Lakini neno lililowakilisha jembe lilitamkwa *mer* ambalo pia lilikuwa na maana ya upendo. Hivyo mchoro wa jembe hatimaye ulimaanisha mapenzi na uliwakilisha homonimia nyingine zote za *mer*.

Maandishi ya picha yaliyochorwa tangu enzi za Mafarao na baadhi ya wafalme wa Kiafrika yalifuata kanuni zilcizile za kifundi za kutumia alama kuwasilisha dhana. Kwa mfano *Recade*<sup>2</sup> ya Mfalme Dakodonu au Dokodonu wa Dahomey (+ 1625—1650) inayoonyesha alama iliyo katika tumbo la picha ambayo inawakilisha jiwe la moto "*da*" na chini yake, mchoro wa dunia "*ko*" ukiwa na tundi katikati "*donon*."<sup>2</sup> Ikiwa hizi alama za kuwakilisha picha na sauti zitalinganishiwa pamoja, zitatoa jina la mfalme huyo: Dokodonu. Mbinu hii inafanana sana na ile iliyotumiwa katika *Palette* ya Farao Narmer.<sup>3</sup>

Maandishi picha hupatikana katika maumbo yanayotofautiana kisanii katika alama za kimaandishi za jamii nyingi za Kiafrika. Katika karne ya kumi na saba, Cavazzi de Montecudolo alieleza kuwepo alama za kinaandishi kama hizo miongoni mwa watu wa Kongo na Angola.

Mifumo ya alama za kuwakilisha wazo zinapatikana katika schemu nyingi. Ama kuhusu mifumo ya aina hii Wagurma wana mifumo changamani wa uaguzi. Mwanguzi, *tambipwalo*, anatia makosi katika mchanga halafu anaifasiri. Halafu anampa mteja namna ya maelezo ya tiba yaliyokatwa nakshi kwenye kipande cha kibuyu. Alama hizi za kidhania zinawakilisha madhabahu aina ya mnyama wa kutolewa sadaka, sadaka itolewe mara ngapi na kadhalika. Kwa hakika huu ni mifumo wa maandishi ya mafumbo.

Utaratibu wa uaguzi wa Kiifa nao ni wa upco wa juu pia. Majedwali ambayo yapo kwa mamia! — yaliyochorwa na mwaguzi huunda "nyuzi" au maneno ya miungu inayotawaliwa na Ifa, mungu wa majaliwa. Mfumo huu wa uaguzi, ambao unatumika kwenye mwambao wote wa ghuba ya Benin, unatokana na mchanganyiko wa Majedwali yaliyotungwa kuonyesha mbinu za kivisaasili.

Uandishi wa kutumia alama kuwakilisha wazo wa Wadogoni na Wabambara sana umekuwa maarufu zaidi baada ya utafiti uliofanywa na M. Griule na G. Dieterlen. Maandishi ya Wansibidi kati ya Waibo wa Nigeria ya Kusini pia ni aina ya uandishi kwa kutumia alama kuwakilisha wazo.

Wakati mwingine kumepigwa hatua madhubuti kwa kuingiza mifumo ya fonetiki iliyokitwa katika maneno, silabi, au foninu moja moja (sauti). Hatua hii ya mwisho na iliyofafanuliwa kikamilifu ndiyo inayounda uandishi wa kutumia alfabeti.






































































































































*Tafneq*, ambayo ni maandishi ya Kiberiberi ya Watuaregi, pengine yameathiriwa kidogo na Wapunikwa (Kathago). Mfumo wa maandishi ya Wanubi ulianza katika karne ya kumi kutokana na athari ya maandishi ya Kikopti, ilihali maandishi ya Kitigriniya na Kiamhara ya Ethiopia, yanahusiana na hati ya Kisabe ya Kusini mwa Bara Arabuni. Ni lazima pia kutaja maandishi ya Bamoun yaliyogunduliwa na Sultani Njoya katika karne ya kumi na tisa.

Mifumo ya maandishi ya silabi au alfabeti iliyoenea pwani ya Liberia na Guinea na katika kanda za Sudani toka karne ya kumi na tisa na kuendelea, huenda ilikuwa ya asilia ingawa labda katika baadhi ya mifumo hiyo palikuwa na athari zisizo za moja kwa moja zilizotokana na Wazungu au Waarabu. Ukweli huu unadhihirishwa na hati ya Kivai ya Liberia iliyotokca katika karne ya kumi na tisa kwenye enco ambalo linasemekana kwamba hapo awali liliwahi kuwa na hati ya maandishi ya picha. Katika kama huu wa kuashiria wingi lakini wenye kutumia dasi ulitumiwa katika maandishi ya enzi za Mafarao.

2 *Recade*: kinyago kilichochoywa kikiwakilisha mamlaka ya mfalme na kuthibitisha ujumbe wa matarishi wake.

3 *Palette*: jiwe la pambo ambapo kuna mchongo au mchoro.

















      	cha ché chē chi chō chō chū	      	kpa kpé kpē kpi kpō kpō kpū	      	nda ndé ndē ndi ndō ndō ndū	      	nya nyé nyē nyi nyō nyō nyū	      	zha zhé zhē zhi zhō zhō zhū
      	dha dhé dhē dhi dhō dhō dhū	      	lba lbé lbē lbi lbō lbō lbū	      	nga ngé ngē ngi ngō ngō ngū	      	sha shé shē shi shō shō shū	<i>Miscellaneous.</i>	
		      	faa hu kpna nwa nwo whew ahn						
      	gba gbé gbē gbi gbō gbō ghū	      	lda ldé ldē ldi ldō ldō ldū	      	nja njé njē nji njō njō njū	      	tha thé thē thi thō thō thū	<i>Punctuation and other Signs.</i>	
		        	bridge comma question period exclamation accent detraction nasal continuation of sound						
    	hna hné hni hnō hnū	      	mba mbé mbē mbi mbō mbō mbū	      	nkpa nkpe nkpo nkpi nkpo nkpo nkpu	      	wha whé whē whi whō whō whū		


10.2 Jedwali la kifonetiki la herufi za Kivai

*Egyptian pictograms*  
(about 4000 before our era)

*Nsibidi pictograms<sup>34</sup>*

A <sub>11</sub>		man running, an arm outstretched inw = messenger			Dayrell <sub>127</sub> , man running an arm outstretched
		mammal's stomach, <i>h.f.</i> = stomach, body			Dayrell <sub>127</sub> , symbol containing fish bones
F <sub>22</sub>		lizard; '3 3 = numerous, rich			Talbot <sub>11</sub> , lizard
I <sub>1</sub>		woman or snake ( <i>h f'w</i> ); worm ( <i>ddji</i> )			Macgregor (p. 212), snake, Dayrell <sub>102</sub> , very long snake; <i>uruk</i> = <i>ikot</i> , snake in Efit and <i>shaw</i> , in Uyanga.
I <sub>14</sub>		woman or snake ( <i>h f'w</i> ); worm ( <i>ddji</i> )			Talbot <sub>33</sub> , see sun shining, nant, <i>utinn</i> sun in Efit and in <i>duwang</i> , in Uyanga.
N <sub>6</sub>		<i>wbr</i> : to rise			Talbot <sub>33</sub> , see sun shining, nant, <i>utinn</i> sun in Efit and in <i>duwang</i> , in Uyanga.
N <sub>11</sub>		lunar crescent; <i>i' h</i> = moon			Talbot <sub>32</sub> , lunar crescent, <i>ebi</i> = moon, in Uyanga.

10.3 *Mifano ya mchoro ya Misri na Afrika Magharibi (kutoka kwa T.Obenga, 1973 Afrika ya Kale (Afrique dans l'antiquité), Présence Africaine. Tanbilu 34 inapendekeza mlinganisho na: J.K. Macgregor, 1909, E. Dayrell, 1911, na P.A. Talbot, 1923)*



10.4 Ubao wa Narmer (kutoka kwa C.A.Diop, 1955, Mataifa ya kinegro na utamaduni (Nations nègres et culture). *Présence Africaine*)

Kwa maneno mengine madai kwamba dhana ya kuandika na uandikaji wenyewe vilikuwepo katika hatua zote za historia ya Afrika yanathibitishwa na majaribio mengi yaliyofanywa na Waafrika. Mifumo mingi iliyogunduliwa haikuendelezwa sana, lakini pengine hii ilisababishwa na umbali uliokuwepo kati ya jumuiya ndogondogo zilizotawanyika katika bara la Afrika ambalo ni kubwa sana.

## *SEHEMU YA II: Nadharia za "mbarikuu" na historia ya Afrika*

Ni vigumu kueleza kisayansi ni nini hujenga mbarikuu. Tukianza kwenye asili moja ya mwanadamu tofauti za kimbari tunazoziona hivi leo zinaweza kuelezeka tu kwa kuzingatia nadharia ya mabadiliko.

Hali mbili huhitajika ili mbarikuu zitokee: kwanza kundi moja hujitenga vya kutosha kiasi kwamba katika kuoana wao kwa wao jeni moja hupata nafasi kubwa zaidi ya kucnea kuliko nyingine na hatimaye kundi hili hujibainisha na makundi jirani kwa maumbile mahsusi ambayo mwanzoni yalitokea kwa bahati tu hii ndiyo inayojulikana kama "mwachano wa kijenetiki" na huenda ilikuwa na dhima kubwa katika Afrika miongoni mwa vikundi vidogovidogo vilivyooana wao kwa wao na ambavyo kwa sababu mbalimbali vilianzisha jamii zilizojitenga misituni.

Hali nyingine ambayo huonyesha tofauti kubwa zaidi ni ile ambamo kundi fulani huhifadhi mfumo wa kijenetiki unaolifaa katika mazingira fulani. Mwendelezo huu hujulikana kama uteuzi asili na huenda ulijitokeza kutokana na hali mbalimbali za kilatitudo, unyevuhewa au ukame, mazingira ya asili (msitu au mpululu) na kadhalika. Imeonekana kwamba wastani wa urefu wa watu huongezeka katika mwezi wenye joto zaidi katika mwaka, na pua nyembamba hupasha moto vizuri zaidi hewa iliyovutwa katika tabia ya hali ya nchi yenye ubaridi. Ijapokuwa watu wengi wanayo idadi sawa ya tezi za jasho kama weupe lakini wao hutoka jasho zaidi na hii hufanya miili yao ipoe zaidi.

### *Mtazamo wa kimaumbo*

Kwa hiyo mwanzoni kabisa mbarikuu ilifafanuliwa kwa misingi ya vigezo vilivyokuwa vikionekana wazi kama vile rangi ya ngozi, aina ya nywele na maumbo ya fuvu, pua, midomo na hata matako. Hata hivyo, watetezi wa mtazamo huo hawajakubaliana kamwe juu ya vigezo muhimu au mbinu za kupipata. Kwa mfano, kuhusu rangi ya ngozi, kuna kadri kubwa ya mifanano ya rangi baina ya watu ambao kwa asili yao ni weupe na wale ambao kwa asili yao ni wengi. Ni lini mtu huacha kuwa mweusi na kuanza kuwa mweupe? Kwa hakika, tofauti hujitokeza zaidi na kwa wingi kuliko kawaida.

### *Mtazamo wa kidemografia au wa idadi ya watu*

Kwa hiyo, wanazuoni wengi wanapendelea kubainisha mbarikuu zaidi kwa kuzingatia kujitokeza mara nyingi kwa jenetiki fulani au vipengee vya kubainisha damu kama mgawanyo wa makundi ya damu kama vile A, B na O, kuliko umbo la mtu binafsi. Landman anafafanua mbarikuu kama "kundi la binadamu (isipokuwa wachache) wanaoonyesha mifanano zaidi ya aina za kijenetiki, na pia mara nyingi mifanano zaidi ya kigenotipiki baina yao kuliko na watu wa makundi mengine"<sup>4</sup>

Kwa hiyo, sifa maalum za chembechembe za uhai za damu zinaleleka kuwa kigezo bora zaidi cha kutofautisha kundi moja la wanadamu na jingine kuliko alama za maumbile ya nje.

4 Fenotipi ni alama zinazoonkana za maumbile ya nje.



Kinyume na weusi wa ngozi au nywele za msokoto ambazo huwa za namna mbalimbali, vipengee vya kubainisha damu ama vipo au havipo.

Hata hivyo tunaweza kupambanua aina tatu za vipengee vya kubainisha damu: baadhi ya vipengee vya kubainisha damu hupatikana katika 'mbarikuu' bila kukosekana. Vingine hupatikana katika makundi yote lakini hujitokeza zaidi katika 'mbarikuu' fulani. Kwa mfano kromosomu Ro yajulikana kuwa 'kromozomi ya Kiafrika' kwa sababu huonekana sana katika damu ya watu weusi wa Kusini mwa Sahara.<sup>5</sup> Mwisho aina ya tatu ya vipengee vya kubainisha damu kimsingi hupatikana katika baadhi ya makundi ya mbarikuu au kijiografia.

### Ufafanuzi wa mbarikuu

Lakini, njia hii ya kutofautisha watu pia hukabiliwa na matatizo makubwa sana; kwanza, kwa sababu kuna vipengee vingi vya kupambanua na ambavyo huleta matokeo ambayo mara nyingine si thabiti. Ufafanuzi wa "mbarikuu" kwa misingi ya kijenetiki na ufafanuzi wa "mbarikuu" kwa misingi ya sifa za maumbile ya nje huvikubaliani. Kwa mfano, mbilikino na Wafan wa Afrika ambao wanakaribiana sana na watu weusi wa New Guinea na Australia kifinotiki hufanana sana na Wazungu katika muundo wa damu na jene, ambapo wenyeji wa Australia wanafanana zaidi na Wachina na Wajapani. Kwa hiyo maumbile ya nje huenda yanaathiriwa zaidi na tabia ya hali ya nchi.

Aidha, uchunguzi uliofanywa na R.C. Lewontin kuhusu viashirio damu umeoonyesha kwamba, katika ulimwengu mzima, asilimia 85 ya tofauti hutokea miongoni mwa mataifa. Kuna asilimia 7 tu ya tofauti baina ya mataifa zinazotokana na mbarikuu moja na asilimia 7 baina ya "mbarikuu" mbalimbali. Kwa ufupi, kuna tofauti kubwa zaidi miongoni mwa watu binafsi wa kundi la mbarikuu moja kuliko ilivyo baina ya "mbarikuu" mbili.

Kwa sababu hii wanazuni wengi wanakataa kuwepo kwa mbarikuu. Kwa mujibu wa J. Ruffie mwanadamu wa kwanza alitokea katika tropiki na akaendelea kupata mabadiliko katika tabia kwa mbarikuu. Kwa mujibu wa J. Ruffie mwanadamu wa kwanza alitoka katika tropiki na akaendelea kupata mabadiliko katika tabia ya hali ya nchi ya joto kwa muda mrefu. 'Ni katika kipindi cha pili cha barafuto, kutokana na uwezo wake wa kumudu moto, ndipo homoerecto alipohamia katika tabia ya hali ya nchi ya baridi.'<sup>6</sup> Kisha wanadamu wakawa wa aina mbalimbali kutokana na mwelekeo wa aina tofauti na kujinasibisha na mazingira mbalimbali. Lakini kidogokidogo, binadamu akajifunza kujilinda dhidi ya mazingira yote maalum aliyoyakabili kwa kuendeleza utamaduni kama vile katika matumizi ya nguo, nyumba, chakula na kadhalika, kwa kiasi ambacho wanadamu wanaelekea kurudi tena katika hali ya aina moja. Baada ya kuacha kutegemea mazingira yake kutokana na mahusiano ya karibu kati ya watu, wanadamu sasa wanaelekea kuwa mkusanyiko mmoja wa jene zinazowasiliana baina yao.

Mnamo mwaka 1952 Livingstone alichapisha makala yake maarufu ya *The Non-Existence of Human Races*, ukweli ni kwamba, kutegemea vigezo vitakavyotumiwa, iwe ni rangi ya ngozi, umbo la fuvu au pua, aina ya nywele, sifa za kijenetiki, na kadhalika, picha tofauti ya mbarikuu hutokea kila wakati. Kufuatana na maendeleo ya sasa ya jenetiki ya kibinadamu, hakuna mtaalam wa biolojia leo ambaye anakubali kuwepo kwa mbarikuu miongoni mwa spishi za wanadamu.<sup>7</sup> Bentley Glass anafikiri kwamba mbarikuu nycupe hutofautiana na mbarikuu nyeusi kwa jozi za jene, mara nyingi kuna mabadilikobadiliko makubwa kuliko idadi hii miongoni mwa

5 Kromozomi ni elementi za chembechembe ya uhai yenye jene, ambayo ni njia za kupitisha urithi.

6 E. Mayr, kama inavyonukuliwa na J. Ruffie, 1977, uk. 115

7 J. Ruffie, katika "Biolojia katika Utamaduni" (De la Biologie à la Culture), uk. 110

weupe na weusi pia. Hili ilikuwa mojawapo ya sababu iliyofanya UNESCO itamke kuwa: 'Mbarikuu huwa kisaasili cha kijamii zaidi kuliko kaida ya kibiolojia.'<sup>8</sup> Kuna mfano gani bora wa dai hili unaozidi ukweli kwamba katika Afrika ya Kusini Mjapani anachukuliwa kama 'mwupe wa heshima' na Mchina kama 'chotara', wakati mtu anayechukuliwa kuwa ni mweupe huko Brazilia huchukuliwa kuwa ni mweusi huko Marekani. Ukweli ni kwamba watu wote duniani wana damu mchanganyiko na watazidi kuendelea kuwa hivyo.


Hata hivyo, kisaasili cha mbarikuu kinaendelea kuleta madhara. Tangu Hitler alipodai kwamba kati ya Waaryeni "Promethens of Mankind" na weusi ambao ni "nusu-manyani" kulikuwa na aina ya Mediterani; kisaasili hiki cha kimbari bado kinaendelea. Katika maendeleo halisi ya watu sababu mbili zinasaidia kupambanua umbo fulani la kundi la watu: urithi wa kijenetiki (urithi) na mazingira.

Kulingana na usuli huu tunaweza kusema nini juu ya mbarikuu kuhusu bara la Afrika? Kutokana na kazi nyingi za kitaaluma zilizofanywa hivi karibu imedhihirika kuwa weusi walianza kutokea barani Afrika yapata miaka 12 000 na kuwa kwa hakika rangi nyeusi ilikuwa kinga dhidi ya nuru haribifu, hasa miali zambarau. 'Weupe' walitokea duniani baadaye kabisa - yapata miaka 55 000. Waarabu-Waberiberi ambao ni wa aina ya 'Mediterani' hatimaye walienea hadi Kusini mwa Sahara, Pemba ya Afrika na pwani ya Mashariki.

Katika kanda ambako Waarabu-Waberiberi walipakana na kundi la weusi ambao miongoni mwao walikuwepo Wakhoisani-Waniloti, Wafulani na 'Waethiopia', baadhi ya watu huonyesha alama dhahiri za mchanganyiko. Hii inadhihirika katika baadhi ya makundi ya Watuaregi, Waharatini na Wasomali na pia katika baadhi ya Wafulani na Wahausa, Watukulori, Wasonrai na kadhalika, katika ukanda wa Kisudani. Katika mifano hii na mingineyo, vipengee maalum vya kupambanua ni mazingira ya kijografia na kujitenga kwa watu wenye kuchanganyika kutokana na mashambulio, uhamaji na kuoana.

Kwa jumla, tofauti kubwa katika aina za maumbo ya Waafrika ni alama ya mabadiliko yaliyodumu muda mrefu na yaliyotokea polepole katika makundi ambayo kwa muda mrefu walijitenga. Kwa hiyo ugunduzi wa kiantropolojia, kisaikolojia na kisosiolojia umeonyesha kwamba hakuna kundi moja la wanadamu au 'mbarikuu' ambalo lina akili zaidi kuliko jingine.

Umuhimu wa kihistoria wa utamaduni zaidi ya biolojia ulidhihirika tangu vizazi vya binadamu wa asili walipoanza kuwepo duniani na pengine walikiwa wametoka Afrika. Ni lini wanadamu watatambua kwamba ni utamaduni na wala sio bilojia unaowafanya wawe jinsi walivyo?



## *Uhamaji na upambanuzi kiisimu na kimbari*

Katika Ulaya wanachnolojia na wanaisimu wa Kijerumani ndio waliokuwa wa kwanza kuchunguza kwa makini tamaduni za Kiafrika. "Taasisi ya Makoloni" ilianzishwa Hamburg mapema mwaka 1907, ambapo shule ya mitaala ya mambo ya Mashariki mjini London ilianzishwa 1916 na laikuwa shule ya mitaala ya mambo ya Mashariki na Afrika, School of Oriental and African Studies Mpaka ilipofika mwaka 1947. Ufundishaji makini wa lugha za Kiafrika huko Ufaransa ulianza baadaye kabisha. Kwa hivyo, Ujerumani iliongoza katika mitaala ya mambo ya Kiafrika katika kipindi kilichofuatiwa na vita vikuu vya kwanza vya Dunia.

### *Nadharia za shule ya Kijerumani na uvumbuzi wa hivi karibuni*

Tasniifu ya Hegel, ambayo kwayo Afrika ilikuwa ndio maskani ya 'watu wasiokuwa na historia' ambao hawakushiriki katika maendeleo wa kiroho ya dunia, imekwishatajwa katika sura zilizopita. Fikira hizi ndizo zilizokuwa msingi wa uechunguzi mwingi wa kisayansi utiofanyiwa Afrika katika karne ya kumi na tisa, kama inavyodhihirishwa katika picha iliyosawiriwa na H. Schurz, aliyefananisha historia ya Afrika na usingizi mzito usioacha kumbukumbu, tofauti na mwanga wa mchana aliochukulia kama kiashirio cha njia iliyofuatwa na jamii za Kizungu.

Kulingana na mawazo ya Hegel, mwanga wa kiroho ulianza kuchomoza Asia. Mtazamo huu ulifuatwa na wanahistoria kama vile Stow aliyefikiria kuwa Wasanii wa kwanza kuishi Afrika walitokea Asia katika luja mbili za uhamiaji.

Halikadhalika, F. Stuhlmann, mwanajiografia wa shule ya Kijerumani ya utamaduni na Historia, alipinga vikali fikira kwamba maendeleo ya mwanadamu yana mfumo wa namna moja. Alitoa fikira iliyokwenda kinyume kabisa na dhana hizo, ambayo ilikitwa katika misingi ya mibembeo ya kitamaduni. Kwa mujibu wa maendeleo ya mwanadamu yana mfumo wa namna moja. Alitoa fikira iliyokwenda kinyume kabisa na dhana hizo, ambayo ilikitwa katika misingi ya mibembeo ya kitamaduni. Kwa mujibu Stuhlmann, mibembeo hiyo hutofautishwa na sifa za mambo halisi ya kitamaduni, sifa ambazo zilienea kutoka mibembeo mmoja hadi mwingine kutokana na uhamaji. Leo Frobenius na Ackermann nao walishikilia nadharia hiyohiyo. Walichukulia kuwa uhamiaji wa watu katika Afrika ulitokea kwa mifuatano maalumu: kwanza Mbilikimo na Wasani, watu wafupi walitokea Asia na ambao hawakuwa na ufundi wa kutengeneza vifaa; halafu walikuja Wenegro wenye nywele za kitani kutoka Kusini Mashariki na Asia, wakiwa na ujuzi kiasi wa kilimo, na walijenga vibanda vya duara na mraba, walitengeneza

vifaa vichache vya mbao, na walitumia mishale na mikuki kama silaha. Watu hawa walidhaniwa kuwa walizungunza "lugha tenganishi" na ilidhaniwa walifuatiwa na Wahamiti wa awali kutoka kaskazini ya Asia waliozungunza lugha ambishi zenye ngeli za nomino na ambao pia wakitumia jembe kulimia nafaka (mtama), na walifunga ng'ombe aina ya zebu. Yafikiwiwa Wabantu walitokana na kuoana kwa Wahamiti wa awali na Wanegro. Baada ya hawa kulitokea uvamizi wa Wahamiti wenyec ngozi ya rangi ya maji ya kunde ambao walikuja kupitia shingo ya Suez. Watu hawa walisemekana kuwa ndio walikuwa mababu wa Wafulani, Wamasai, Waoromo, Wasomali na Wakhoikhoi na kwamba ndio waliosambaza zaidi mambo ya utamaduni kama vile ng'ombe aina ya ankole, mikuki na ufundi wa ngozi. Luja iliyofuata ilikuwa ya Wasemiti, waliodhani kuwa ndio walianzisha Ustaarabu wa Misri ya kale, na ambao walileta mahindi, shaba, plau na kadhalika. Baadaye wakafuata Wahaiksosi na Waibrania na Wahabeshi ambao walilowea katika nyanda za juu za Ethiopia. Mwisho wakaja Waarabu katika karne ya saba ya enzi zetu. Maelezo haya mazuri yanaonyesha uwezo mkubwa wa Stuhlmann, wa kuwaza mambo yamo katika kazi iliyochapishwa Hamburg 1910 na ndiyo yaliyadhiri fikira za wanaethoholojia wengi, wakiwemo Selgman wa Uingereza na Honea wa Austria.

Katika isinu, nadharia juu ya Wahamiti iliyoelezwa na Meinhof ilijikita katika mikondo minne ya taratibu za kidhabania. Kwanza, kulikuwa na lugha za vidoko za watu walioishi katika ujima, halafu lugha tenganishi ambazo hazikuwa zimeendelea sana, zilizozungunzwa na Wanegro wa Kisudani. Hizi zilifuatiwa na lugha ambishi zilizotokana na kuoana kwa Wabantu weusi na Wahamiti. Mwishowe zikaja lugha badili maumbo zilizo bora za Wahamiti watamalaki.

Fikira hii jumuiifu yenye kutazama historia na lugha za Afrika kwa mtazamo wa wazungu ilienea karibu Ulaya nzima hadi Vitu Vikuu vya Pili vya Dunia, ijapokuwa misingi ya ubora wake ilikuwa imekwishasailiwa kutokana na uchunguzi uliothibitisha ukweli uliowavutia watu wengi. Mwaka 1924 kulivumbuliwa mabaki ya Australopithesini huko Afrika kusini na hii ilifuatiwa na uvumbuzi mwingi rwingine na anthropoidi unaoweza kunasabishwa na makundi ya mataifa yote. Kwa hivyo nadharia ya kudhania kuwa luja za uhamaji zilianzi Asia, ilitupiliwa mbali. Kama mwanapalaeontolojia. Arambog alivyosisitiza, Afrika ndilo bara peke yake ambako hatua zote za maendeleo ya binadamu - *australopithesini*, *pithekanthropi*, *Neandarthali* na homo sapieni zinaweza kuonekana kusnzia tabaka ya chini, pamoja na zana zilizotumiwa na kila moja ya tabaka hizo. Fikira hii ililubithishwa na uchunguzi wa urithi wenye kusifika sana wa sanaa ya mapangoni, ambao ni wa kipkee na unaopatikana Afrika tu. Fikira ya Darwin kuwa Afrika ndio chimbuko la binadamu wote linathibitika.

Hapana shaka yoyote kuhusu umri wa ushahidi wa kiakiolojia, kwa vile umri huo umethibitika kwa kutumia upangaji wa tarehe kisayansi kwa njia ya kaboni-14 na potasiamu - argoni. Tarehe hizi hutunukia kanda za Afrika za Saheli na Sahara dhima ya kale kulingana na au kuzidi ile iliyohusishwa na Mashariki ya Karibu. Kwa mfano huko Tassili N' Ajjer nchini Algeria, vigae vimepewa umri wa miaka 8000 kabla ya enzi zetu ambapo huko Acacus, kwenye mipaka ya Algeria na Libya, kiunzi cha Mnegro chenye alama ya mavazi ya ngozi kilichimbuliwa na kikapewa umri wa kiasi cha miaka 9000 kabla ya enzi zetu. Katika kambi za Neolithi zilizovumbuliwa huko Nubia ya chini, mabaki ya vitu vilivyokuwa na uhai yamekusanywa na yanathibitisha kuweko na uvunaji na utayarishaji wa nafaka mwituni kiasi cha miaka 13 000 iliyopita. Kwa hivyo, ukusanyaji wa mbegu kutokana na nafaka ulifanyika katika bonde la Naili kiasi cha miaka 4000 mapema kuliko ilivyofanyika katika Mashariki ya Karibu. Eneo lenye umbo la mawezi mwandamo lenye rutuba linaloanzia Mesopotamia kupitia Palestina



**11.1** *Mvolta (Picha ya A.A.A., Naud)*



**11.2** *Chifu wa kinomadi, Rkiz, Mauritania (B. Naniet)*

**11.3** *Mwanamke wa Kifulani. Bororo, Tahoua, Niger, (B. Naniet)*





**11.4** Mwanamke wa Kidjerma, Songay, kutoka Balayera, Niger (B. Nanter)

**11.6** Mwanamke wa Kizulu: (A Robillard, Makusanyo ya Musee de l'Homme Coll)



**11.5** Mbilikimo, kutoka Kongo (Danday ia Shirika la Habari, Musee de l'Homme Coll)

**11.7** Mwanamke wa Kifulani (Archives outre-mer)



mpaka Misri lilitambaa mbali zaidi ya eneo hili mpaka katika Bara la Afrika. Kiini cha eneo hilo ambacho ndicho chanzo cha watu pamoja na mbinu za kilimo na ufugaji kinaelekea kilikuwa magharibi ya Mto Naili kama ilivyodhibirika katika michoro na nakshi kwenye miamba katika Sahara. Kwa hiyo mifuatano na umuhimu wa makazi katika Afrika viligeuzwa na magunduzi yote haya: aina kwa hakika Afrika, na wala sio Asia, ndio ilikuwa chanzo cha uhamaji wa mwanzo katika vipindi vyote virefu sana kabla ya historia mpaka enzi za Mafarao wa Misri. Ndipo hapo watu wakaanza kuhamia bara la Afrika na athari za uhamaji huo zilionekana zaidi ukingoni kuliko kwenye bara lenyewe.

### *Matatizo ya kianthropolojia na kiisimu*

Yawezekana kuwa sifa za kianthropolojia kwa jumla hutoa vidokezo vinavyoweza kuaminika zaidi kuliko data ya kitamaduni kama vile lugha au mavazi ambayo mara nyingi hubadilika kwa haraka, ingawa kuna vighairi, na kuwa biolojia na utamaduni daima huingiliana.

Ijapokuwa kitamaduni watu weusi wa Marekani wamejisilimisha zaidi na nchi za Kimagharibi (mbali na muziki wao, ngoma na imani zao za kidini) kianthropolojia wamebakia Waafrika halisi. Halikadhalika Wasiddi, Waafrika weusi waliochukuliwa kutoka pwani ya Afrika Mashariki na kupelekwa India. Mwanzoni miwa karne ya kumi na tisa, watu hawa walikuwa bado wakizungunza lugha yao, lakini sasa wanazungunza lugha za watu wa India - Kigujarati, Kiurdu, na kadhalika - ambao wamechanganyika nao. Hata hivyo wamechifadhi maumbile yao kwa kiasi kikubwa. Inawezekana pia kutaja mfano wa Waberiberi ambao bado wanaonyesha maumbile yao ya asili ingawa wamesilimishwa utamaduni wa Kiarabu.

Kwa msingi huohuo, ramani ya kianthropolojia ya Afrika yaweza kuonyesha ruwaza ya kale ya makundi muhimu ya kianthropolojia ambayo wakati mwingine kwa mtazamo wa kijuujuu huitwa 'mbarikuu'. Kwa mfano kundi la Kinediterani, limesdhibirisha sifa zake za kipekee tangu zama za kale sana, pengine kutokana na kundi la 'Kiafrika' kujinasabisha na aina mpya ya kiumbile na pia kutokana na kuzaana na makundi mengine. Vivyo hivyo kwa jamii ya watu wa 'Ethiopoidi' wa pembe ya kaskazini mashariki ya bara la Afrika. Kwa upande mwingine, ncha ya Kusini ya Afrika, ambayo kwa kiasi fulani ilikuwa imetengwa na milima na jangwa la Kalahari, vilikuwa kama makiumbilio ya Wasani. Hali maalumu za ikolojia za maeneo ya msitu na kutengwa kwake ndizo zilizosababisha kuanzishwa kwa aina ya kianthropolojia inakayowakilishwa na Mbilikimo.

Si rahisi kupambanua makuundi ya kianthropolojia ya watu weusi wa Kisudani au Kikongo katika matabaka ya awali kabisa, kutokana na kuharibika kwa masafia yao kulikosababishwa na udongo wenye asidi. Hata hivyo, ushahidi wote unaonyesha kuwa watu hawa ndio waliokuwa wenyeji, na kwamba ndio waliotangulia kutamakani Sahara na kwa wingi zaidi kuliko makundi mengine. Yaelekea hivi ndivyo hali ilivyokuwa katika bonde la Naili, hasa katika Misri, ambako kumbukumbu za kihistoria zinathibitisha mwingiliano ulivyozidi kuchangamana. Kwa mfano, vyanzo vya Kiyunani vinataja Waethiopia wa Kusini mwenye ngozi nyusi na wale Waethiopia wenye ngozi ya rangi ya maji ya kunde. Hivi ndivyo hali ilivyo katika Afrika hata sasa. Kwa vyovyote vile kuzaana baina ya watu tofauti kumtokea zaidi popote pale ambapo makundi ya binadamu yalipokutania, kama katika mabonde ya mto na kandokando ya maziwa, kutokana na sababu za hali ya hewa, za kiikolojia au nyinginezo. Kila wakati sifa za kimaumbile za makundi mbalimbali ziliathiriwa na mazingira na kwa kuzaana baina ya naitaifa tofauti, na sifa hizo tofauti hatinaye zilirithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Kwa kawaida ijapokuwa kuna tofauti

hapa na pale —Mwafrika anayeishi msituni ni mfupi na mwenye rangi ya maji ya kunde, kuliko Mwafrika mrefu na wenye rangi nyeusi anayeishi katika Savana na Saheli. Athari ya mazingira ni kubwa kiasi kwamba kufanana kunaweza kuonekana kati ya makundi yanayotengwa kwa masafa marefu hali yakiishi katika mazingira ya aina moja. Kwa mfano, Wawolof wa Senegal wa Wadinka wa Naili ya Juu wote aghlabu huwa warefu na wenye ngozi nyeusi sana.

Hata hivyo, kuna hali zenye mchangamano mkubwa ambazo huwafanya wanahistoria kutumia uamuzi wao kama wanavyofanya kuhusu suala la Mbilikimo kwa Wasani. Kinyume na ilivyofikiriwa hapo awali, Mbilikimo wa Afrika na wale wa Asia ya Kusini hawamo katika kundi moja na kufanana kwao huenda kumetokana na jinsi walivyojinasibisha na mazingira ya aina moja. Yaelekea Mbilikimo wa Kiafrika, ambao kwa hivi sasa wanaishi katika vikundi vilivyotengana kwenye misitu ya Cameroon, Gabon na Jamhuri ya Afrika ya Kati, Zaire na Rwanda, walikuwa wakiishi katika maeneo makubwa zaidi hapo zamani. Ushahidi wa jambo hili unaonekana katika mapokeo ambayo husimulia habari za watu wafupi; baadhi ya vyanzo vya kimaandishi pia vinaeleza juu ya kuwepo kwa Mbilikimo mahali ambapo kwa hivi sasa hawapo tena.

Mbilikimo wanatajwa kwa mara ya kwanza kabisa katika maandishi ya Ufalme wa sita wa Mafarao. Katika ukuta wa kaburi la Herkhuf lililoko Aswan kuna mabaki ya nakshi ya barua kutoka kwa Farao Pepi wa Pili ikimshukuru Herkhuf kwa kumpelekea zawadi ya Mbilikimo aliyeitwa Deng, jina ambalo linapatikana katika lugha za sasa za Ethiopia katika maumbo ya *dank, denk, dinki, dinka*. Barua hiyo hiyo inaeleza kuwa, karne moja kabla, Mbilikimo kama huyo alitolewa zawadi kwa Farao wa Ufalme wa Tano. Kwa hivyo inawezekana kuwa Ethiopia ya leo na Sudan zilikuwa zinakaliwa kwa wakati huo na makundi ya Mbilikimo ambao polepole walirudishwa msituni katika makimbilio.

Wasani ni mfano mwingine mchangamano kwani kwa kawaida wanajumuishwa katika kundi inoja na Khoi-Khoi katika taifa linalosemwa kuwa ni "mbarikuu ya Kikhoisan." Hii imetokana na kufanana kwa mitindo ya maisha. Ama kwa hakika, katika Kikhoi-Khoi neno *Khoi* lina inaana ya mtu, ambapo neno *Sani* linatokana na *Sa* (kukusanya au kuchuma matunda, kung'oa mizizi na kukamata wanyama). Pamoja na lili "mifumo ya uzalishaji" lugha zote zina sifa ya matumizi ya konsonanti za vidoko, mbali na ukweli kwamba makundi yote haya mawili yana ngozi ya rangi ya maji ya kunde. Hata hivyo, kuna tofauti muhimu baina yao. Wakhoi-Khoi ni warefu zaidi na wanawake wao wana shuri.

Hata tukiwalinganisha kisimu, wanatofautiana kutokana na viwakilishi wanavyotumia: Viwakilishi vya Wakhoi-Khoi vina jinsi mbili na namba tatu (umoja, uwilli, na wingi) ambavyo havipo katika lugha za Kisani. Wakhoi-Khoi waliishi katika maboma wakifua vyuma na kufuga ng'ombe, ambapo Wasani walikuwa wawindaji na wakusanyaji. Kwa hiyo haielekei kama kuna sababu yoyote ya kuyaweka makundi haya mawili pamoja.

Huenda Wasani wanawakilisha vizalia vya watu asilia na upande huu wa bara, ambao waliishi katika enco kubwa zaidi kabla ya kulazimika kubaki katika maeneo yenye hali ngumu na ukame ya jangwa la Namibia na jangwa la Kalahari.

Toponimia (Taaluma ya majina ya mahali na haidronimia (Taaluma ya majina ya maji) zinaonyesha kuwa maneno ya asili ya Wasani yameenea hata mpaka Kenya. Pieha za mapango ya Afrika ya Kusini zinaonyesha Wasani wakipigana na majesiti ya watu warefu sana na weusi zaidi. Hali kadhalika, kundi la Wahadza linaloishi karibu na Ziwa Byasi (Tanzania) laelekea kuwa alama ya enco ambalo hapo zamani lilikaliwa na Wasani.

Hata hivyo, kuwagawanya Waafrika wa awali katika makundi mbalimbali kuirahisishwa mno, kiasi cha kudhaniwa kuwa Mbilikimo waliishi katika misitu na Wasani katika nchi za



Savana. Hapana shaka makundi mengine yaliishi sambamba nao, kama vile Waotavi ambao mitindo yao ya maisha inafanana na ya Wasani lakini wanatofautiana sana nao kwa vile wana ngozi nyeusi sana na midomo minene. Mfumo wao wa kuhesabu pia unatofautiana sana na mfumo wa kidesimali unatumiwa na Wakhoi-Khoi. Ramani ya kiisimu ya bara la Afrika ilichangamaa mwanzo, kama inavyohibitishwa na kuwepo kwa vienco vidogo vya wazungumzaji wa lugha ya vidoko katika ya maeneo ambayo sasa yana wazungumzaji wa lugha za Kibantu. Wakati mwingine kumetokea athari za kiisimu ambapo konsonanti vidoko zimetumika katika lugha za Kibantu. Hii inaonyesha athari ya matabaka ya Wasani au Wakhoi-Khoi waliokuwepo kabla ya Wabantu.

Ijapokuwa kutengwa kwa muda mrefu hapo awali kunaweza kuwa kulisababisha ramani za kiisimu na kiantropolojia zikubaliane, mambo haya polepole yalijitenga yakawa na mwelekeo tofauti na kuwa na hatua tofauti za mwenendo. Kutokana na hali hii kukawapo lugha nyingi kama zilivyo hivi leo. Hata hivyo, kiasi fulani cha maeneo makuu ya lugha kinaweza kubainishwa.

### *Maeneo makuu ya lugha*

#### Lugha za Kisemiti-Hamiti au Kihamiti-Semiti

Hapo awali lugha zilizungumzwa katika bara la Afrika zilijulikana kama lugha za Kihamiti ambapo zile za Mashariki ya karibu zilijulikana kama lugha za Kisemiti. Siku hizi, baada ya Cohen kuonyesha jinsi ambavyo hapakuwa na umuhimu wa kuhusisha lugha na maeneo ya kijiografia; lugha hizi zimeainishwa katika makundi matano: Kisemiti, Kikushi, Kiberiberi, Kimisri cha Kale na Kichadi<sup>1</sup>

#### Lugha za Afrika kale za Kisani na Kikhoi-Khoi

Sifa muhimu za lugha za Afrika Kale ni sauti za vidoko na muundo tunganishi. Lugha hizi ni pamoja na lugha za Kikwadi za Angola na Kihadza cha Tanzania.

Japokuwa kuna maoni tofauti ya wanaisimu kama Greenberg, lugha za Khoi-Khoi, zikiwa na muundo tofauti wa kisarufi, haziwezi kuwekwa katika kundi hili. Yaelekea wakhoi-Khoi walikuja kutoka Kaskazini Mashariki mwa Afrika na kutamalaki Wasani na yaelekea kuwa lugha yao ilipendelewa na Wasani ambao baadhi yao waliifanya kuwa lugha yao; ingawaje inaelekea pia kuwa Wakhoi-Khoi nao walichukua sauti za vidoko kutoka lugha za Wasani. Zaidi ya hayo, vikundi vidogo vinavyohusiana kiisimu na Wakhoi-Khoi, kama vile Wasandawe wa Tanzania, vinaelekea kuonyesha njia waliopitia wahamaji hao. Kama walivyo Wahadzapi na watu wanaoongea lugha za Kikushi, Wakhoi-Khoi wanathibitisha kuwepo kwa tabaka la watu waliowatangulia Wabantu.

#### Lugha zinazosemekana ni za Wanegro wa Kiafrika

Istilahi hii ambayo ilibuniwa na Delafosse maweza kuzusha ubishi kwani inatumia viashirio vya kijiografia na vya "kimbarikuu" kueleza lugha. Zaidi ya uanishaji wa kuziweka lugha za Wanegro wa Kiafrika katika makundi hayo mawili, lugha za Kisudan na Kibantu ulifanywa kwa makosa. Hata hivyo tangu uchunguzi uliofanywa na Westermann wenyewe na hasa tokca

1 Kulingana na Mkutano wa kairo wa Kuingia kwa watu katika Misri ya kale, uainishaji huu hauna maana tena. Ling. Historia Kuu ya Afrika ya Unesco, Juz. II, Sura I.

kuchunguzwa upya kwa uainishaji wa lugha za Kiafrika na Greenberg, tofauti hii imetupiliwa mbali. Mnamo 1954 Greenberg alibainisha familia kumi na sita za lugha ambazo, baada ya miaka kadha, alizipunguza na kuzifanya kumi na mbili na baadaye nne. Mfano huu unaonyesha hali ya kutokuwa na uhakika na ugumu unaotokea katika jitihada za kuainisha lugha.

Kati ya familia nne zilizobakia, kikundi cha lugha za Afrika-Asia kihajitokeza kuwa ni kilekile cha familia ya Semiti-Hamiti. Ama kuhusu lugha inayojulikana kama Kikhoisan, inaunganisha pamoja lugha za San na Khoi-Khoi, na kwa maoni yetu, haya ni makosa. Ya tatu na ambayo imeenea zaidi kupita zote ni familia ya kikundi cha Niger-Congo, ambamo Greenberg baadaye aliongezea lugha za Kikordofan. Mwisho, kwa maoni yake familia ya nne incundwa na zile lugha zinazosemekana ni za Nilo-Sahara, ijapokuwa hizi hazijafanyiwa uchunguzi wa kutosha. Mnamo 1972 Gregersen alitoa pendekezo kuwa lugha zote za familia mbili zilizotajwa mwisho — lugha za Niger-Congo na Nilo-Sahara— ziwekwe katika kundi moja, ambalo aliliita Congo-Sahara ambalo mimi binafsi napendekeza litwe *Kundi Zindj*. Kwa mfano seti nzima hii ya lugha inayobainishwa na matumizi ya toni na ngeli za majina inaonyesha mfanano sawa na ule wa lugha za Kihindi-Kizungu. Katika fungu hili mashuhuri la lugha za Kibantu zinaonyesha uthabiti wa muundo wa maneno usio wa kawaida. Papahapo lugha za Kimande zilizoko Afrika ya Magharibi ambazo zinaonyesha tofauti za mbali za Kibantu nazo huonyesha mfano wa aina hiyohiyo.

Nje ya makundi haya muhimu ya lugha, kuna masuala mengine ambayo mpaka sasa yanazusha ubishi. Kwa mfano, lugha ya Gur au lugha za Atlantiki ya Magharibi zilizotajwa na Westermann zinatofautiana sana (angalia Manesseye) na zimeainishwa na wanaisimu wa Kiingereza katika kundi la pekee waliloliita lugha za Mel. Baadhi ya lugha hizi zina uhusiano na lugha za Kibantu. Tofauti zilizomo katika msoto huu wa lugha zinaelekea kuwa ni kielelezo cha hali ya kihistoria ya eneo hili la Afrika ya Magharibi na makimbilio ya milimani ambako wahamaji mbalimbali walikutana na kuchanganyika kadri karne zilizvopita.


Lugha za Kiniloti za Sudani ya Mashariki, ambazo hazijafanyiwa uchunguzi wa kutosha, kinajipambanua kwa kuonyesha sifa na maumbo tofauti pengine kwa sababu zilijitenga na lugha nyingine kwa kipindi kirefu.

Mfanano wa lugha za familia ya Kibantu ni dalili ya uchanga wake kwa sababu lugha zinazounda familia hiyo hazijapata kuwa na mwelekeo tofauti. Nadharia tete tatu zimeundwa katika kujaribu kueleza "Chanzo cha Wabantu." Baadhi ya watu wanafikiria kuwa Wabantu walikuja kutoka Kaskazini ya Cameroon au Chad. Wale walikuwa wakihama wanafikiriwa wahambaa misitu iliyokuwa kaskazini, ili kuupita kwa upande wa Mashariki, na kisha wakapitia Afrika Mashariki na kusambaa kusini mwa Afrika. Wataalamu wengine kama vile H.H. Johnston, wanaamini kuwa Wabantu walikuja moja kwa moja kutoka kanda ya Afrika ya Kati katika bonde la Zaire. Mwisho, wanaisimu, kama vile Guthrie, wameonyesha kuwa kiini cha Wabantu kipo katika ndi ya Luba na Bemba katika Zaire ya Juu.

Wakati mwingine Wabantu huelezwa kuwa ni watu wenye asili moja ya kibiolojia na kitamaduni kama "mbari kuu" yenye ustaarabu mmoja. Ama kwa hakika istilahi Bantu ni kielelezo cha kiisimu. Baadhi ya watu huwahusisha wabantu na usambaaji wa chuma katika nusu ya Kusini ya bara la Afrika, ilihali Wabubi wa Kisiwa cha Fernando Po ambao pia ni Wabantu hawakuwa na vifaa vya chuma walipogunduliwa na Wareno mwishoni mwa karne ya kumi na tano. Ukweli ni kwamba Wabantu wanatofautiana kwa rangi, urefu na mifumo ya uzalishaji, isitoshe baadhi yao hufuata unasaba wa kuumini, ilihali wengine hufuata umasaba wa kukeni. Kwa hiyo kuwa na muundo mmoja wa lugha wenye mfumo wa ngeli za majina uliokitwa katika

sulubu moja ya sauti na mfurno mmoja wa vitenzi kusichukuliwa kuwa ndio msingi wa kuwahusisha watu kibiolojia na kitamaduni.

Hata hivyo hatutakuwa tumetia chumvi sana kama tukisema kuwa watu waliokuwa wakiongea lugha zenye ngeli za nomino walilazimika kuondoka kwenye jangwa la Sahara kutokana na ukame uliozidi, na kuelekea kwenye milima iliyo Kaskazini, bonde la Nile na bonde la Chad kale. Hawa wawindaji na wafugaji ng'ombe waliwafukuza wenyeji ambao walielekea Kusini hadi kwenye misitu. Baadhi ya Wabantu walikuwa na ujuzi wa kufua chuma. Wabantu waoishi kwenye matapo ya eneo linalojulikana hivi leo kama Shaba walizagaa na kutumia makao hayo ya kiuchumi kama ehimbuko la kuenea mbali zaidi. Huku kutawanyika kuliwafanya wakutane na watu wa aina mbalimabali na ndiyo sababu lugha za Kibantu zilizidi kupujuka kwa kadri walivyozidi kwenda nje ya kiini cha teknolojia katika nyanda za juu za Zaire. Kwa ufupi, mfumo wa uzalishaji mali huambatana na ueneaji wa lugha.



## *Uainishaji wa lugha za Kiafrika na ramani ya lugha*

### *SEHEMU YA 1: Mwainisho wa lugha katika Afrika*

Mwainisho wa lugha kijenetiki ni utaratibu wa kimantiki ambao kwao tunalazimika kurudi nyuma kufuatia chanzo cha shajara ya lugha za leo; lugha ambazo tunaweza kusema ndizo zifanyazo matawi madogo kabisa ya shajara. Matawi hayo madogo ndiyo hatua yetu ya kuanzia kurudi nyuma kufuatia matawi makubwa na hatimaye kufikia matawi makubwa zaidi ambayo yanachomoza kutoka kwenye shina. Tunaweza kusema shina ndio mame-lugha. Kutokana na meme-lugha, kwa sababu ya tofauti mbalimbali kukatokea vizalia vya lugha na hatimaye lahaja. Kwa mfano Kihindi-Kizungu kilizaa matawi mengi kama vile tawi la lugha ya Kijerumani, lugha za Kislavu na lugha za Kihindi-Kiajemi. Tawi la Kijerumani likagawanyika katika lahaja ya Kiingereza-Kifrisi (Kiingereza), lahaja ya Kijerumani cha Juu (Kijerumani) na lahaja ya Kijerumani cha Chini (Kidachi). Isimu linganishi inaweza kutumiwa kuunda upya historia na chanzo cha mwachano huu wa taratibu katika lugha za familia moja. Inaweza pia kusaidia kuelezea historia ya utamaduni wa watu.

### *Historia ya mwainisho wa lugha katika Afrika*

Haiwezekani kufanya mlinganisho wowote wa kiisimu au kufika hitimisho lolote kuhusu nafasi ambayo lugha fulani huchukua katika shajara pasipo kwanza kutoa maelezo kamalifu juu ya vipengee vya kulinganishwa. Hii ndiyo sababu uchunguzi makini haukuweza kufanywa mpaka ilipofika karne ya kumi na tisa. Hata hivyo sarufi na Kamusi za kwanza za lugha ya Kiafrika zilianza kuandikwa kuanzia karne ya kumi na saba na kuendelea, wakati Luis Moriano alipogundua kwamba lugha ya Kimeriana ya Madagascar "ilifanana sana na Kimalay, jambo ambalo linathibitisha; kwa usahihi mkubwa kwamba wahamiaji wa kwanza walitoka katika badari za malaka."

Halikadhalika ilikuwa katika karne ya kumi na saba wachunguzi wa Kireno walipotoa rai kwamba kulikuwa na mshabaha kati ya lugha za Angola na Kongo kwa upande mmoja na zile za Msumbiji kwa upande mwingine. Kwa kufanya hivyo walikuwa wameisogeza karibu dhana ya lugha za kikoa cha Kibantu. Pia kwa upande wa mshabaha baina ya lugha za Kiethiopia na lugha za Kisemiti-Kiyahudi na Kiarabu - majaribio ya kwanza ya uainishaji yalifanywa mwishoni mwa karne ya kumi na nane.

*Glossarium Comparativum Linguarum Totius Orbis* (Faharasa Linganishi ya Lugha Zote za Ulimwengu), ambacho kilichapishwa mwaka 1790 kwa msaada wa Katarina Mkuu wa Urusi, kilikuwa na lugha thelathini za Kiafrika. Katika miaka ya mwanzo ya karne ya kumi na tisa, kamusi, sarufi na orodha za maneno-linganishi vilianza kutolewa kwa wingi. Kazi ya kwanza kubwa na ambayo ilifanywa kwa utaratibu mzuri ilikuwa ni *Polyglotta Africana* ambayo ilikusanywa huko Freetown na S.W. Koelle.

Mnamo katikati ya karne ya kumi na tisa mahitimisho kadhaa yalifikwa kutokana na kazi hii. Baadhi ya mahitimisho haya bado yanakubalika mpaka leo hii ilihali mengine yalionekana kutokuwa na msingi. Ufuatao ni muhtasari wa mahitimisho hayo:

1. Istilahi ya "semiti", iliyobuniwa 1781, mpaka leo hii inatumiwa kwa maana ya mjumuisho wa lugha za Kiarabu na za Kiyahudi pamoja na tawi la lugha za Kiethiopia, yaani Ge'ez, Kiamharia na Kiitigrinya. Zaidi ya hapo lugha kama vile Kiberiberi na lahaja za Kikushiti (Somali) zilitambuliwa tangu awali kwamba zinahusiana na lugha za familia ya Kisemiti. Zilijulikana kama schemu ya lugha za Kisemiti au "Kihamiti", istilahi iliyopendekezwa na Renan mnamo 1855.
2. Katika Afrika Kusini na Kati wanaisimu walitofautisha baina ya lugha za Kikhoi-Khoi na Kisani kwa upande mmoja na lugha za Kibantu kwa upande mwingine kwa sababu katika lugha za Kibantu neno bantu lilikuwa na maana ya "watu".
3. Kwa muda mrefu lugha zilizotanda kuanzia pwani za Atlantiki hadi kufikia milima ya Ethiopia zilijulikana kama lugha za "Kinegro". Lakini wanaisimu weledi kama Askofu O.E. Vidal na W.H.I. Bleek walikuwa wamekwishagundua kwamba baadhi ya lugha hizo zinafanana sana na lugha za Kibantu. Kidokezo hiki cha msingi hatimaye kilizingatiwa na kuhibitishwa na Westermann na baadaye na Greenberg.
4. Kimeriana, lugha ya Malagasi, iliainishwa kama lugha mojawapo kati ya lugha za Kimalaya-Polinesia tangu karne ya kumi na saba.

R. C. Lepsius, F. Muller na R.N. Cust waliandika vitabu muhimu sana juu ya uainishaji wa lugha ingawa katika baadhi wa maelezo yao waliingiza vigezo vya kibaguzi katika jitihada za kuunga mkono dhana fulani zisizokuwa na msingi wala mantiki yoyote. Baadaye Lepsius alichagua jozi mbili za lugha ambazo aliziweka katika mpangilio msonge kwa kulinganisha na kundi pekee la kimsingi, Kibantu. Mpangilio huu ulizipambanua lugha hizo kama ifuatavyo:

- (a) Lugha za Kibantu na lugha mseto za Kinegro (lugha zenye ngeli za majina)
- (b) Lugha za Kisemiti na Kihamiti (lugha za jinsi)

Lugha za Kisemiti na Kihamiti zilisemekkana kuwa na uhusiano na lugha za Kibindi-Kizungu, ambazo zilidaiwa kuwa na uhusiano na Yafeti, mmojawapo wa watoto wa Nuhu. Watoto wengine wa Nuhu walikuwa Shem (ndipo basi tukapata Semiti) na Ham (ndipo tukapata Hamiti). Itaonekana dhahiri kuwa mwainisho huu wa lugha unageuka kuwa mabishano ya kinadharia ya kibaguzi. Kwa hakika Lepsius mwenyewe alisema "Yaonekana dhahiri kwamba yale matawi matatu ya lugha za jinsi hapo kale hayakuwa tu chemchemu na vyombo vya historia ya maendeleo ya ustaarabu wa mwanadamu bali pia ni tegemeo kubwa la dunia, na hasa lile tawi changa la Yafethi."<sup>1</sup>

1 R. Lepsius, 1880 uk.90.

Uanishaji wa Müller nao ulikuwa na kasoro hizohizo. Naye alianisha lugha kwa kutumia maumbile ya watu, akitumia istilahi kama vile "lugha za watu wenye nywele za singa", "watu wenye nywele za sufu na kadhalika." Kutokana na mtazamo huu lugha za Kikhoi-Khoi pamoja na lugha za Kipapua zote ziliwekwa katika kundi la lugha za "watu wenye nywele za msokoto, wakati lugha za Kinuba-Fulh zilipandishwa hadhi kuwa kundi la lugha za "watu wa Mediterani wenye nywele za mkunjo."

Matokeo ya mwainisho huo ni makundi sita ambayo yalipangwa kwa kufuata ubora kama ifuatavyo: (1) Kisemiti (2) Kihamiti (3) Kinuba-Fula (4) Kingro (5) Kibantu na (6) Kikhoisan.

Baada ya kazi za Lepsius na Müller hapakutokea kazi nyingine hadi mwanzoni mwa karne ya ishirini ambapo mianisho mingine mipya ilifanywa na Westermann na Meinhof. Katika maandishi yake juu ya "Lugha za Kisudani" Westermann (1911) alitumia istilahi hiyo kwa maana ya lugha zote za Kiafrika ambazo haziko katika kundi la Kisemiti au Kikhoisani. Hii ni kusema kwamba Westermann alizijumuisha pamoja lugha zote za makundi malatu ambayo Müller alikuwa ametenga (Kingro, Kibantu, na Kinuba-Fula). Msingi wa madai ya Westermann ulikuwa ni mfanano wa kietimolojia na maumbo ya kale. Katika kitabu chake juu ya lugha za Kihamiti, Meinhof (1912) alilipanuwa kundi hili kwa kuingiza Kifulfulde, Kimasai na Kikhoikhoi kwa msingi kwamba lugha hizi zote zilikuwa lugha za jinsi lugha ambazo yeye aliamini kuwa zilikuwa bora kuliko nyingine.

Tukiunganisha matokeo ya Westermann na Meinhof tunapata vikoa vitano vya lugha: Kisemiti, Kihamiti, Kisudani, Kibantu na Kisani. Vikoa hivi vilidondoka kufahamika hivyo hadi kukaribia mwaka 1950. Ama kwa hakika Westermann, mnamo mwaka wa 1927, alishindwa kupata hasa vigezo ambavyo vilidokeza kuunganishwa kwa lugha za "Kisudani" na lugha za Kibantu katika kikoa kimoja. Mbali na kuonyesha mifano michache ya kufanana kwa msaniati wa muundo wa kisarufi hakuna cha zaidi alichofanya, wala hakujaribu hata kuvilinganisha baadhi ya vipenge vya lugha hizo.

Kwa upande mwingine wanaisimu wengine watatu walikwishaanza kudokeza mwainisho wa lugha za Kiafrika ambao unatumika hivi leo. Katika juzuu lake kubwa juu ya lugha za Kibantu na Nusu-Kibantu Sir Henry Johnston alitumia kigezo cha ngeli za majina na kudai kuwa kulikuwa na uhusiano baina ya lugha zinazosemwa kuwa ni za Kisudani na lugha za Kibantu.

Delafosse kwa upande wake, mara nyingi akitumia vigezo vya kijiografia kuliko vya kisimu aliamua kukifanya kikoa cha lugha za Kihamiti kuwa Kiberiberi,<sup>2</sup> Kimisri na Kikushiti tu. Ndiyo kusema lugha nyingine zote ambazo hazikuwa za Kisemiti au Kikhoi-Khoi zilichukuliwa kuwa kikoa kikubwa cha lugha za Wanegro wa Kiafrika ambamo Kibantu pia ni mojawapo.

Katika mwaka wa 1941 Mlle Homburger alikwenda mbali zaidi alipoanza kwa msingi kwanba lugha zote za Kiafrika zilitokana na Kimisri cha Kale na kwamba hapo nyuina kabisa lugha hizo zilitokana na lugha za Kidrauid za huko India.

Katika mwaka wa 1949-50 J.H. Greenberg katika *Southwestern Journal of Anthropology* pamoja na kutilia maanani mianisho iliyokuwa imetangulia alitoa mwainisho ambao ulikwenda mbali ya mianisho mingine yote katika juhudi za kujaribu kuziweka lugha za Kiafrika katika kategoria chache tu. Msingi wa mtazamo wake ulitokana na kufanana kwa kiasi kikubwa katika sauti na maana, na kati ya mizizi ya misaniati au miundo ya kisarufi. Kuwepo kwa kigezo kimoja tu, kwa mfano jinsi, hakutoshiezi kuwa ushahidi wa uhusiano wa lugha.

2 Madai hayo yamekanushwa na El Fasi ambaye anayaona kuwa ni mkatikali wa kisiasa wa k. 22. Anishia Kiarabu na Kiberiberi ambacho kwa maoni yake pia ni Kisemiti halisi.

I. Kundi Kuu la Niger-Kordofan

A. Kundi la Kordofani

Vikundi vya:  
Koalib, Tegali, Talodi, Katla, Turmtum

1. Mandel { a. Kaskazini Magharibi: Kisoninke, Kimaninka, Kibambara-Dyula, Kivai-Kono  
b. Kusini Mashariki: Kimano, Kidani, Kigani, Kisani (Kisamo), Kibisa, Kibusa

B. Niger-Kongo

2. Mengine { a. Atlantiki Magharibi { Kaskazini: Kifulfulde, Kisereri, Kiwolof, Kidyula, Kibasari...  
Kusini: Kiteme, Kibaga, Kikisi.  
b. Gur Au Kivolta: { Kati: Kidagbane, Kimore, Kigurma, Kidagari, Kigrusi  
Mengine: Kibariba, Kilobiri, Kibwamu, Kikulango, Kisenufo, Kidogoni ...  
c. Kwa: { Kikru, Kiakan-Guang, Kiga-Adangme, Kiyoruba, Kinupe, Kiedo, Kiidoma, Kiibo, Kiido...  
d. Benue-Kongo: { Lugha za Bonde la Benue  
Lugha za Kibanni<sup>3</sup>  
e. Adamawa Mashariki: { Adamawa: Kimbum, Kichamba...  
Mashariki: Kigbeya, Kizande...

II. <i>Afro-Asia</i>	A. <i>Kiberiberi:</i>	Kiberiberi cha Maghrib na Mauritania, Kituareg
	B. <i>Kimisri cha Kale<sup>a</sup></i>	
	C. <i>Kisemiti Cha Kusini-Magharibi</i>	{ Kaiarabu, Kisabea Lugha za Ethiopia: Kitigrinya, Kige'ezi au Kiethiopia cha jadi, Kiamharik, Kiharari
	D. <i>Kikushiti</i>	{ Kaskazini: Kibeja... Katikati: Kiagau... Mashariki: Kisomali, Kigalla... Kusini: Kiburungi, Kigoroa, Kialawa, Kisanye Magharibi: Kiaribanana, Kisidamo
	E. <i>Kichadi</i>	{ Kihausa, Kigwandara..... Kikotoko, Kimandara, Kimusgu....
III. <i>Nilo-Sahara</i>	A. <i>Kisongay-Jerma</i>	Kikanuri, Kikanembu, Kiteda-Daza, Kizaghawa
	B. <i>Kisahara</i>	Kiberti...
	C. <i>Kimabani</i>	
	D. <i>Kifuriani</i>	
	E. <i>Kichari-Nili<sup>b</sup></i>	{ Kisudani cha Mashariki: Kinubi, Kihailsti (Kijaluo, Kidinka, Kinueri, Kishilluki, Kikaromjong, Kiturkana, Kinandi, Kisuk... Kisudani cha Kati: Kibongo, Kibagirmi, Kimangbetu...
IV. <i>Kikhoi-Sani</i>	A. <i>Kikhoi-Sani<sup>b</sup></i>	{ Kisani cha Kaskazini
	B. <i>Kihansa</i>	{ Kikhoisani cha Kati: Kikhoikhoi, Kinaroni...
	C. <i>Kisandawe</i>	{ Kisani cha Kusini

Maelezo juu ya jedwali hili yanafuata katika ukurasa 120



*Maelezo juu ya Jedwali la Kurasa 118-119*

1. *Kikundi cha Mande.* Kikundi cha Mande hutofautiana na lugha nyingine za kundi la Niger-Kongo kwa sababu hakina baadhi ya maneno yanayopatikana katika lugha nyingine na pia hakina mwainisho wa nomino. Sifa hii ya mwisho inakifanya kikundi hiki kitofautiane hata na kundi la Kordafani, kitu ambacho kimewafanya wanaisimu wengine kama vile Mukarovsky washauri kwamba lugha hii iingizwe katika kundi kuu la Nilo-Sahara.
2. *Kikundi cha Atlantiki Magharibi* Kutokana na kuwepo kwa lugha za aina mbalimbali katika kikundi hiki D. Dalby anashauri kwamba kijikundi cha Kusini, ambacho yeye anakiita Mel, kitengwe mbali. Hata hivyo Sapir yeye anafikiri kwamba hakuna sababu ya kuzitenganisha lugha za kikundi hiki, ingawa naye anasema Kibijago (lugha ya visiwa vya Bijago) kihesabiwe kuwa tawi tofauti sawa na malawi ya Kaskazini na Kusini.
3. *Lugha za Kibantu.* Kwa mujibu wa maoni ya Guthrie lugha za Kibantu haziwezi kuhesabiwa katika kundi la Niger-Kongo. Kwa maoni yake lugha za Kibantu ni kikoa kinachojitegemea kijenetiki. Guthrie anadai kwamba mshabaha uliopo kati ya lugha hizi na lugha nyingine unatokana na athari ambazo zimeletwa tu na lugha za Kibantu kwenye lugha nyingine. Greenberg anadai kwamba kitovu cha lugha za Kibantu ni katikati ya Bonde la Berae, lakini Guthrie anadai kuwa kitovu hicho kilikuwa Shaba Kusini.
4. *Kikundi cha Kimisri cha Kale.* Wazo hili ni tofauti na wazo lililojitokeza katika Kongamano la Kairo kuhusu watu walivyotamkani Misri ya Kale (ling. Sura ya 10 hapo juu). Kikopti, ambacho kilitokana na Kimisri cha Kale, ni lugha iliyokufa; imbakia tu katika muundo wa Kibohairi ambacho hadi leo hii kinatumika katika liturjia.
5. *Kundi la Kichari-Nile.* Kijikundi cha Kinailoti (Kimasai, n.k) hadi leo hii kinaleta ubishi mwingi kwa sababu mara nyingi kimcainishwa kama Kihamiti, Kiniloti, Kipar-Noloti na hata Kisemiti.
6. *Kundi Kuu la Khoisan.* Tazama maoni tofauti ya Olderogge katika sura ya 11.

## Tambili

- a. Lugha ya Kimerina ilitawi vizuri katika nyanda za juu za Madagascar, kinyume na lugha za pwani zenye asili ya Kiafrika. Ni lugha ya Kimalay-Polinesia na inahusiana hasa na Kimaanya, lugha ya Borneo.
- b. Kimeroti ni lugha iliyokwisha kufa. Ilikuwa inasemwa katika Ufalme wa Meroe. Iliandikwa kwa kutumia maandiko picha na hati linganishi. Kwa sasa Kimeroti kinaonekana tu katika maandishi yaliyoko kwenye mabaki ya kiakiolojia ambayo yamegunduliwa kati ya Aswani na Khartoum. Ni matamshi tu ya herufi hizo yanayojulikana. Hata hivyo, kwa kuwa msaniati na sarufi yake havifahamiki, na kwa kuwa hakuna maandishi ya lugha mbili kama ilivyo katika Kimisri cha Kale, lugha hii haijawahi kufasiiwa; japokuwa yawezekana siku moja fumbo hili likafumbuliwa kwa msaada wa Kompyuta. Baadhi ya Wanaisimu huanisha lugha hii kama "Kihamiti" ambapo wengine hufikiria kwamba ni lugha ya Kinubi au Kiniloti.
- c. Hatuna budi kutaja uingiaji wa lugha za Ulaya ambazo zaidi zimetokana na majitio ya ukoloni. Hizi ni lugha kama vile Kiingereza, lugha ya Wanerikani Weusi ambao walianzisha Liberia. Lugha hii pia inasemwa kama Kikrioli (Krio) katika Sierra Leone. Vilevile kuna Kiafrikaansi, lugha iliyotokana na Kidacti na inasemwa huko Afrika Kusini. Kikrioli cha Kireno kinasemwa katika Guinea Bissau na katika Visiwa vya Cape Verde. Mwisho kuna lugha zenye asili ya Kihindi (hasa Kigujerati) ambazo zinasemwa katika Pwani ya Afrika Mashariki.

*Inaendelea kutoka ukurasa 117*

Kwa upande mwingine kutokuwepo jinsi ya kiume na kike hakukufanya lugha fulani isianishwe na lugha nyingine za jinsi. Hili linethibitishwa na lugha za Kihindi-Kizungu. Kwa mfano Kifarsi (Kiajemi) na Kiarmenia hazitofautishi jinsi ya kiume, lakini huchukuliwa kuwa na uhusiano na lugha nyingine ambazo hutofautisha jinsi hizo.

Mwainisho huu mpya unajitokeza kuwa wa kijenetiki peke yake. Sifa zake kuu ni kama zifuatavyo:

1. Lugha ambazo zimedaiwa kuwa za Kisudani, ambazo zinatanda upande wa mashariki mpaka kufikia mashariki ya Adamawa, zina uhusiano mkubwa na lugha za Kibantu. Kwa pamoja lugha zote hizi huunda kikoa kimoja kijulikanacho kwa jina la 'Niger-Kongo', kilichoenea kuanzia Afrika Kusini (Kizulu) hadi kufikia Rasi ya Verde (Kiwolof) na Kameruni Kaskazini (Kifulfulde).
2. Kwa upande mwingine Kihausa na baadhi ya lugha nyingine zilizoko katika kanda hiyo zimeainishwa kwa jina la lugha za 'Kichadi.' Lugha hizi ni mojawapo ya matawi matano ya kikoa kingine kikubwa kinachojumuisha lugha za Kiberiberi, Kimisri cha Kale,<sup>3</sup> Kisemiti na Kikushiti.
3. Lugha za 'Kinegro' ambazo hazikuingizwa katika kundi la Niger-Kongo zimeainishwa chini ya Kikoa cha Nilo-Sahara.
4. Lugha za Kikhoikhoi na Kisani zimeainishwa chini ya Kundi Kuu la Khoisani.

Kwa hiyo basi uainishaji wa makundi manne usichukuliwe kuwa ndio kamili, kwani kwa vyovyote vile utarekebisha kadri utafiti unavyoendelea.

### SEHEMU YA 11: Ramani ya Lugha za Afrika


Ingawa Bara la Afrika limekaliwa na watu wachache waliotawanyika hapa na pale - Bara hili ni asilimia 20 ya eneo lote la dunia lakini lina asilimia 10 tu ya idadi ya watu wote duniani - lina utata mkubwa wa kiisimu kuliko bara jingine lolote lile. Ndiyo maana jitihada za kulifumbua fumbo lili la kiisimu hazijawahi kufanikiwa; na hata ramani ya makazi ya mataifa mbalimbali ambayo imechorwa na Warusi bado pia ina mikanganyo.

Ramani ambayo ingefaa hasa ingekuwa ile ambamo kila Mwafrika anawakilishwa kwa kitone ambacho nacho kingeonyesha rangi inayoashiria mojawapo ya lugha 1500 anayotokea kuisema wakati huo. Ramani ingeonyesha miendo katika nyakati za majira mbalimbali. Hii ingekuwa mwashirio wa hali halisi iliyoipo.

Kwa kuwa haiwezekani kutengeneza ramani kama hiyo, basi katika mwongo uliopita *School of Oriental and African Studies* na *International African Institute* zimekuwa zikitayarisha ramani yenye skeli ya 1:5,000,000 ya lugha za asili za Afrika.

Hata hivyo kuna umuhimu wa kutoa ufafanuzi kuhusu uainishaji wa lugha katika Afrika. Ingawa mtazamo wa kijenetiki ni muhimu lakini unaweza kuleta kikwazo kwani inaweza kufikirika kuwa kwa kuwa lugha zilizopo leo zimetokana na kuzagaa kwa vizazi vya lugha vilivyotoka kwa lughababu chache, kama ilivyo katika shajara, basi yawezekana kuzifuatilia lugha zilizopo hivi leo hadi kufikia mwanzoni ambapo kulikuwa na "mame-lugha" chache tu zilizokuwa zikizungumzwa kotekote katika bara zima. Hii itakuwa sawa na kulikanganya zoezi la mtenganisho wa kimantiki na uundaji upya wa hali ya awali ya lugha kwa kutumia urazini wa kiisimu pamoja na mwelekeo halisi wa kilistoria. Lugha zisizohusiana kabisa zinaweza kuanza kujenga ukaribiano kutokana na kukaribiana kwao. Ingawa ukaribiano kama huu hutumbulikana hauwezi kuhititika kwa sababu za kijenetiki tu.

<sup>3</sup> Katika Mkutano wa Cairo wa Kuingia kwa Watu katika Misri ya Kale, mtazamo huu ulipingwa. Kama Mlle Homburger, wachunguzi wa Kiafrika walijumuisha Kimisri cha Kale katika kikundi cha Kinegro cha Kiafrika. Ling. Cheikh Anta Diop.



Kwa hiyo basi furbo la hali ya isimu katika Afrika sharti lifumbuliwe kwa kutumia njia ambayo huhitajia ufafanuzi toshelevu na usahilifu. Ili kufikia lengo hili kuna haja ya kuyatenga makundi makuu ambayo kila moja lina lugha zenye uhusiano wa mali na lugha zilizo nje ya kundi hilo. Kwa mfano iwapo kundi moja lina lugha A, B na C zenye uhusiano wa karibu basi yoyote katika lugha hizo isionekane kuwa na uhusiano wa karibu zaidi na lugha nyingine. Kuliiko ilivyo na lugha za kundi lake. Makundi ya namna hii ndiyo yanaweza kuitwa jamii ya lugha changamano. Hata hivyo, kuna lugha nyingine ambazo hazina uhusiano na lugha yoyote ile; hizi huitwa jamii ya lugha sahili. Kwa misingi ya ufafanuzi hizi mbili inawezekana kabisa kuchora ramani ya mgawanyo wa lugha katika Afrika ambayo ni wazi na yenye kueleweka vizuri zaidi. Kati ya jamii changamano na sahili 120 za lugha katika bara zima zaidi ya jamii 100 zinato katika kanda moja ambayo imetanda tokea visiwa vya Cape Verde kupitia pedimenti ya Ethiopia na nyanda za juu za Afrika Mashariki. Ukanda huu mwembamba ulioko Kusini mwa Sahara, ukiwa na upana wa wastani wa kilometa 1,000, huchukua theluthi mbili ya lugha zinazosemwa katika Afrika. Kati ya lugha 1,500 za Kiafrika lugha elfu moja (ambazo ni asilimia 66) zimekaa karibukaribu katika eneo ambalo ni asilimia 20 ya eneo lote la nchi kavu katika bara hili. Eneo hili linafaa litwe ukanda wa kusini mwa Sahara wenye migawanyiko ya lugha. Sehemu yake yenye mgawanyiko mkubwa kabisa iko kwenye ncha ya Pembe za Afrika Mashariki katika eneo lenye kipenyo cha kilometa 40 ambako lugha zote zilizoanishwa na Greenberg zinasemwa. Kwa kuwa mgawanyiko wa namna hiyohiyo unapatikana katika mwinuko ya Togo, nyanda za juu za Jos, mwinuko ya Cameroon na vilima vya Nuba tunaweza kuunda uhusiano wa chanzo kati ya mifumo ya kiekolojia ambayo huweza kuchukuliwa kama mahali pa kukimbilia (k.m. maeneo yaliyo kandokando ya jangwa au milima) na migawanyiko mikubwa ya lugha.


Zaidi ya hapo istilahi "kikoa" huashiria dhana ya asili inayofungamana na uzoa wa kibijolojia. Haiwezi kuchukuliwa kwamba dhana hii inahusu lugha pekee yake. Maeneo ambayo yana "vikoa" hivi vya lugha ingesadifu zaidi kuyaita "maeneo yenye mfanano mkubwa." Hali ilivyo sasa ni kwamba maeneo makuu mawili hayo, "Afro-Asia" na "Niger-Kongo", yamepakana na yamo katika eneo la migawanyiko mingi. Tena basi lugha za eneo la Kaskazini zenye mfanano mkubwa zinategawanyika katika jamii 17 sahili na changamano. Kati ya jamii hizi 17 jamii 12 ziko katika ule ukanda wa migawanyiko ya lugha. Katika eneo la Kusini lenye lugha za mfanano mkubwa kuna jamii 58 sahili na changamano. Kati yazo 57— tukiacha kundi la Kibantu — pia zimo katika ule ukanda wa migawanyiko ya lugha. Kwa jumla maeneo yote haya mawili huchukua asilimia 80 ya lugha zote zisemwazo katika Afrika.

Kwa sasa hali ilivyo ni kwamba vile vikundi vya kati ambavyo vinajulikana kama Atlantiki Magharibi, Kwa, Gur au Benue Kongo havijapata kukubalika kwa wote. Sababu hasa ni kwamba hoja zilizotolewa kuunga mkono uainishaji kwa makundi hayo hazina uzito.

Migawanyo ya kiusimu iyokuwa na kanuni madhubuti na ambayo imefanywa na baadhi ya wachunguzi inafanana sana na migawanyo ya kikoloni ya miaka ya nyuma. Hata Greenberg mwenyewe ambaye kwa ustadi mkubwa aliivunjilia mbali nadharia ya Kihamiti, kwani iliunda kundi la lugha kwa misingi potofu, naye aliangukia katika tatizo la kujaribu kufafanua vikoa vidogo vya lugha pasi na kufuata misingi thabiti. Kikundi cha Benue-Kongo, kikundi kikubwa kuliko vyote kimekatajiwa moja kwa moja na J.M. Stewart. Hata hivyo Stewart mwenyewe pia anafanya kosa anapojaribu kuendeleza mbinu aliyotumia Greenberg kwa kuunganisha Benue-Kongo na Kwa na Gu (dhana mbili ambazo pia hazina misingi thabiti) ili kuunda mgawanyo mwingine mdogo yaani Niger-Kongo (ambayo baadaye ilijulikana kama Volta-Kongo) ambao nao haukuwa na budi ila kuakisi kutokuwapo kwa misingi thabiti ya uundaji wa vikundi vyake.

Ili kuweza kufanya utambuzi wowote wa kisayansi juu ya vidokezo muhimu vya makundi ambayo yako kati ya makundi makuu ya jamii za msingi ambavyo kwa sasa hivi ndio ushahidi pkee usiopingika kunahitajika monografu nyingi zilizo na maelezo yenye kina. Pia itakuwa kungoja mpaka hapo wazungumzaji (wascmaji) wa lugha hizi watakapokuwa wanaisimu waanze kushughulikia isimu linganishi ili waweze kuhakikisha kama kuna uhusiano kati ya lugha nyingine zinazopakana.

Ni kweli kwamba ramani ya lugha zilizoko Afrika ni hati muhimu sana katika kuelewa historia ya awali na ya leo ya bara hili. Lakini ni mchanganua thabiti wa Kiisimu tu utakaotuwezesha kuuliza maswali sahihi juu ya matatizo ya kihistoria ambayo mpaka sasa bado yapo.



## *Jiografia ya historia: vipengee vya maumbile*

Historia ya watu wa Afrika imekua katika mandhari mahsusi ya kimaumbile, tabia ya hali ya nchi na kiikolojia. Ingawa mandhari hayo si sababu ya moja kwa moja ya mwenendo wa kihistoria, ni hali mojawapo inayotawala historia.


Hali hizi si za kudumu bali daima huingiliana na mwanadamu ambaye huzitegemea na kuzipa sura tofauti. Katika muktadha huu ukweli kwamba tabia ya hali ya nchi ya Afrika inaonyesha ruwaza ambayo karibu ni linganifu katika maeneo ya kikanda yaliyo katika pande zote za Ikweta, pamoja na uasili mkubwa wa mazingira ya kimaumbile ni muhimu katika maendeleo ya kihistoria katika bara la Afrika.

### *Sifa za kiusanifu - majenzi za bara la Afrika*

#### Uasili wa Kijiolojia wa Afrika

Matabaka ya chini ya sehemu kubwa za bara hili ni ya miamba ya kale sana ukiachilia mbali milima ya Maghrib, ambayo ni sehemu ya mturno wa Milima ya Alps ya Ulaya, na misongo ya Hersini ya Rasi ya Kusini mwa bara na Atlas ya Kusini, Afrika nzima na Madagascar ni dungu kubwa lililomong'onyolewa kwa muda mrefu na ambalo takataka na mito na upepo zimerundikwa, hususa katika mabonde makuu ya mito ya bara.

Na matabaka haya hatimaye yakawa hayakuathiriwa zaidi na kukunjiana kuliko na kusawajika polepole na kubinuka. Wakati mwingine, miinuko mikubwa ambayo ilisababisha maeneo mengine kubakia chini ilifanya ruwanza ya mikunjo na mabonde au umbo la vilima na mabonde ambalo linajitokeza sana barani Afrika. Wakati mwingine hii mibimiko huwa na umbo na mifuo mikubwa inayoanzia Kaskazini hadi Mabonde ya Ufa ambamo mikono ya lava ya volkeno hububujika na kufanya sura za kuvutia za mandhari, kama vile Mlima wa Kilimanjaro, 'pea la Afrika', ambao unafikia urefu wa mita 6000. Kwa upande wa Magharibi wa bara mlipuko ya volkeno haikuwa mikubwa sana, lakini Mlima na Kameruni unaovutia macho wenye urefu wa mita 4070, unadhahirisha kuwepo kwa mlipuko wa volkeno ulitokea kwenye bonde la Ghuba ya Guinea.



13.1 *Ramani ya sura ya Afrika kutoka kwa J. Ki-Zerbo, 1978 (Historia ya Waafrika Weusi, Paris, Hatier)*

### Athari za Tabia ya Kale ya Hali ya Nchi

Mabadiliko ya kijiolojia yalilusika kwa kiasi kikubwa katika kuunda sura ya nchi barani Afrika lakini mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi hayo yalikuwa na nafasi yake. Vipindi vya mvua nyingi vilivyopishana na vipindi vya ukame vilisababisha mmong'onyoko mkubwa ambao ulifuatawa na urundikaji mkubwa wa takataka za mito na upepo, hususa kaika miaka ya hivi karibuni.

Ushahidi mkubwa wa ruwaza hii ya matukio makubwa ni jangwa la Sahara. Katika jangwa hili ambalo linatanda karibu theluthi moja ya eneo la ardhi la bara la Afrika, mmegunduliwa masalia ya zana zilizotengenezwa kwa mawe, mifupa na miti, aina mbalimbali za vito na mapambo mengine na michoro na nakshi, pamoja na visukuu vya mbegu, mimea na wanyama wakubwa. Vyote hivyo vinahitibisha kuwapo kwa viumbe vingi kwa maelfu ya miaka. Lakini hatimaye vipindi vya ukame vilizidi na jangwa kubwa kuliko yote duniani sasa linatanda katika sehemu ya bara la Afrika iliyo pana zaidi toka Magharibi hadi Mashariki. Kwa hakika jangwa la Sahara kamwe halikuwa kizuizi kisichopitika: Wanomadi na wafanyabiashara waligundua njia nyingi za kulivuka jangwa katika misafara yao. Lakini, jangwa lisingelikuwepo, ni dhahiri kuwa historia ya bara hili ingekuwa tofauti sana: lingeungana kwa karibu zaidi na-schemu nyingine za dunia na, juu ya yote, kungekuwepo mgongano zaidi kati ya sehemu zote za bara hili.

### Hali ya Ukubwa wa Bara la Afrika

Afrika ni tungamo kubwa la ardhi lililojitokeza na kutanda masafa ya kilometa 8000 kutoka Bizerta, katika Tunisia, mpaka Rasi ya Agulhas, na kilometa 7500 toka Cape Verde hadi Rasi ya Guardafui. Katika ardhi yote hiyo kubwa kuna mabadiliko ya umbo au upenyo. Bara hii ni mihili ya mnara mkubwa wa ngome ulioimarishwa, uliokuwa na pwani yenye vizingo vichache mno, kinyume na Ulaya na Amerika ya Kati au Asia ya Kusini-Mashariki. Kwa vile vilindi vya bahari huanzia karibu na upwa, kuna visiwa vichache tu.

Zaidi ya hayo ukubwa wa umbo la bara hili unadhahirishwa na kuwepo kwa nyanda za juu pana zenye maumbo yaliyolika na ambazo zimekunjana katika kingo zake na kuzuia mito kisielekee pwani. Ni Maghrib peke yake, yenye safu za milima ya Tell na Rif kwa upande wa Kaskazini na Atlas kwa upande wa Kusini ambayo imebadilisha madhari ya bara hili.

Huko katikati ya bara hili, jambo linalojitokeza sana ambalo linaonyesha tofauti kati ya bonde kubwa na uwanda wa juu wa Zaire ulio chini, na mabonde ya Ufa yanayotanda kilometa 4,000 toka Msumbuji hadi Bahari ya Sham, ni vilele vya volkeno vya Milima Kenya na Kilimanjaro. Mabonde ya Ufa yametoa mchango mkubwa wa Kihistoria katika uhamaji wa watu kutoka Kaskazini kwenda Kusini, hususa kwa vile misitu ya tropiki katika bonde la Zaire ilikuwa kipingamizi cha kulipenya bara hili na pia kwa sababu maziwa yaliyozagaa chini ya bonde - Maziwa ya Malawi, Tanganyika, Kivu Edward, Mobutu (lililojulikana kama Albert), Victoria, na Turkana (Rudolph) —yaliuvia makazi ya wanadamu kwenye kingo zayo tangu enzi za awali za kabla ya historia iliyoandikwa.

### Kujitenga kwa Afrika Kijiografia

Afrika haijawahi kujitenga kabisa na ulimwengu wa nje. Lakini kutokuwepo kwa nyanda kubwa kama ilivyo huko Asia na Amerika Kaskazini kulizua mashirikiano baina ya watu wa bara hili. Mkusanyiko wa idadi ya watu. Papo lapo viziwi kwenye kingo, kama vile majangwa na safu za milima, vilikwaza mawasiliano ya nje. Bahari Kuu ya Atlantiki haikutumiwa sana kabla ya wavumbuzi na wafanyabiashara ya watumwa kutumia balari hii mnamo karne ya kumi na tano,



bahari kuu hii iliwakwaza mabaharia ambao hawakuweza kuvuka pwani ya Sahara, kwa sababu vyoimbo vyao visingeweza kuimudu safari ya kurudi kutokana na pepo za kusi zinazovuma mara kwa mara.

Kwa upande mwingine, Bahari ya Hindi daima imokuwa ikikuza mahusiano kati ya Afrika na Bara Arabuni na hata na bara Hindi na Uchina kwa sababu safari za kwenda na kurudi kati ya Afrika na Asia zilirahisishwa na kubadilika kwa pepo za Kusi na Kaskazi. Hata hapa pia mabaharia hawakupendelea kuingia bara na badala yake walitosheka kufanya biashara kwenye mwambao.

Ukosefu wa maeneo ya asili yafaayo kuwa bandari aghalabu umechukuliwa kuwa ndio sababu ya kujitenga kwa bara hili. Ni kweli kuwa mara nyingi pwani huwa zimenyooka, za chini na zenye mchanga mwingi, au hupenyezwa na hori —yaani milango ya bahari — zilizojaa nyangwa zenye matope, kama zile zinazoonekana mara kwa mara kwenye pwani nzima kati ya Mito ya Casamance na Kongo. Zaidi ya hayo, mwambao wa Afrika wa Bahari ya Sham, mlango wa Bahari ya Msumbuji na ufuko wa Mashariki wa Madagascar zote zina miamba tumbawe. Safari za baharini katika mwambao huwa ngumu mahali pengi kutokana na mawimbi makubwa ambayo hugawanyika kuwa mawimbi madogomadogo yanayobingirira chini kwenye matuta ya mchanga. Lakini, matatizo ya kuufikia mwambao wa Afrika yasiukuzwe sana. Kuna bandari nyingi nzuri na maezi zilizozeza kufanya Afrika kushiriki katika historia ya watu wa Mediterani tangu zama za Kale. Bado kuna maeneo yafaayo kuwa bandari katika pwani zote mbili za bahari Kuu za Atlantiki na Hindi ambayo hayajatumiwa. Ukweli ni kuwa watu wa Afrika, hata wale waliokuwa chini ya himaya maarufu kama zile za Misri ya Mafarao - hata kama kulikuwa na tawala nyingine mashuhuri na za kipekee kabisa kama vile utawala wa Kariteji (Kathago) - kimsingi walibaki kuwa watu wa nchi kavu walioshughulika na kuvumbua kama siyo kutumia, eneo kubwa la ndani ya bara la Afrika.

### *Sifa za kikanda za tabia ya hali ya nchi katika Afrika*

Afrika kama bara lililo pana kabisa katika kanda iliyo kati ya tropiki mbili ndilo lenye joto zaidi kuliko mabara yote. Kadiri unavyokaribia tropiki, ndivyo joto linavyozidi kuwa kavu, na kinyume chake, kadiri unavyokaribia Ikweta ndivyo joto linavyozidi kuwa na unyevunyevu.

### **Sababu za Kilimwengu**

Kwa vile Afrika imetanda kwenye ikweta, jua halionekani kuwa chini sana kwenye upeo wa macho, na ndiyo sababu daima kuna joto. Kwenye ikweta, jua linazungukazunguka utosini, hivyo hakuna msimu halisi wa joto na halijoto daima ikuwa juu. Lakini kuelekea kwenye tropiki, tofauti kati ya mchana na usiku na kati ya msimu hujitokeza zaidi.

Kwenye nchi za Kaskazini na Kusini za bara hili, ambapo jua hutaremka chini kwenye upeo wa macho wakati wa baridi, tofauti za msimu huwa zaidi.

### **Ruwaza ya Mvua**

Sababu kuu zinazotawala hali ya hewa barani Afrika ni tungamo hewa (za tropiki, au ikweta na za bahari au bara) ambazo hudhibiti pepo na intungo wa mawingu. Vituo viwili vya kani eneo juu (vitengua kimbunga) huhusisha Atlantiki ya Kaskazini (kitengua kimbunga cha Azores) na Atlantiki ya Kusini (kitengua kimbunga cha Mt. Helena). Kwenye bara lenyewe kuna vitengua kimbunga vingine viwili, kimoja kikiwa juu ya anga ya Sahara na kingine kikiwa juu ya anga ya Kalahari, vinatazamana na hivyo vya awali. Lakini tofauti na vitengua kimbunga viwili vya

mwanzo, ambavyo ni maumbile ya kudumu, vitengua kimbunga vya bara kimsingi huwa amilifu katika msimu wa baridi.

Kwa hivyo, wakati wa msimu wa baridi katika kizio cha Kaskazini, kitengua kimbunga cha Azores huvumisha pepo za baridi - pepo za msimu za Atlantiki - kuelekea kwenye kani eneo chini la ikweta. Pepo hizo huathiri tu mwambao wa pwani ya Sahara hadi Cape Verde. Papo hapo, kitengua kimbunga cha Shara huwa chanzo cha pepo kavu za Kaskazini Mashariki ambazo huzidi kuwa za joto kila ziravyokaribia Ghuba ya Guinea. Upepo huo ndio Harmattan, ambao hukausha kila kitu kilichomo katika njia yake pote katika Savana ya Afrika na Sahel.

Wakati wa msimu wa baridi wa Kusini, mtindo huohuo husababishwa na kitengua kimbunga cha Kalahari, ambacho kinavumisha mbali pepo za joto na zilizo kavu mpaka bonde la Zaire. Huo ni wakati wa majira ya joto katika kizio cha Kaskazini na kanienco chini juu ya anga ya Sahara hufyonza pepo zenye unyevu kutoka Guba ya Guinea ambazo huanzia katika kitengua kimbunga cha Mt. Helena. Hizi ni Pepo za Kusi za Guinea ambazo huusukuma nyuma upepo wa Harmattan zinapochanganyika nao, husababisha majira ya mvua.

Vipengee kadha vya kijiografia, kama vile vya mikondo ya bahari, sura ya nchi, mwambao wa pwani huweza kuathiri tabia ya hali ya nchi ya mahali hapo, Kwa mfano, mkondo wa joto wa Kaskazini-Mashariki hupita kwenye pwani ya Somalia wakati wa majira ya joto, ilihali mkondo wa ubaridi hutoka Bara Arabu kuelekea ikweta wakati wa majira ya baridi.

Mwambao wa Guinea wenye milima nyuma ya Conakry (Mlima wa Nimba) ambao hukumbwa na pepo kali za Kusini hupata mvua kiasi cha mita tano kila mwaka. Kwa upande mwingine pwani za Togo na Benin pamoja na ile ya Somalia, ambazo ziko sambamba na pepo za Kusi na Kaskazi, hupata mvua kidogo.

## Kanda za Tabia ya Hali ya Nchi

### *Tabia ya Hali ya Nchi Katika Ikweta*

Toka Cameroon hadi bonde la Zaire, jua, ambalo takriban huwa wima, na mvua nyingi za zaidi ya mita mbili kwa mwaka, husababisha joto lenye unyevu mara kwa mara. Ruwaza kama hiyo hupatikana katika sehemu za ikweta kutokana na athari za tabia ya hali ya Bahari Kuu ya Hindi, ingawa mvua haiwi nyingi sana.

### *Tabia za Hali ya Nchi Katika Tropiki*

Katika kanda hizi kubwa zinazotanda toka maeneo ya ikweta hadi kwenye majangwa, kadiri mtu aendavyo mbali na maeneo ya ikweta, ndivyo joto linavyozidi kuongezeka na mvua huzidi kuadimika. Katika kanda ndogo ya Sudani inayoungana na kanda ya ikweta, mvua hunyesha kwa muda wa zaidi. Katika kanda ndogo halisi ya pili ya Sudani mvua hunyesha kati ya miezi mitatu na miezi sita kila mwaka, na kiasi cha mvua hutofautiana kati ya mm 600 na mm 1,500. Tofauti za halijoto huongezeka. Katika kanda ndogo ya Saheli kiasi cha mvua kinachonyesha katika kipindi cha chini ya miezi mitatu ni chini ya mm 600, na mabadiliko ya hali ya joto luwa makubwa.

Ruwaza ya mabadiliko ya aina hiyo pia hutokeza kusini mwa ikweta, lakini mabadiliko haya yanayotokea polepole hujidhihirisha zaidi kwa sababu bara huzidi kuwa nyembamba kuelekea kusini na kwa sababu ya athari kubwa zaidi ya tungamo hewa za bahari kuu na sura ya mwambao. Pwani za Msumbiji na mwambao wa mashariki wa Madagascar ni wa mteremko mkali na hupigwa na pepo ambazo huleta mvua nyingi ilihali pwani ya Atlantiki ambapo hutiririka mkondo baridi wa Benguela ni kavu na huashiria kuwapo kwa jangwa la Namib hapo.

*Tabia ya hali ya nchi katika jangwa*

Hizi tabia za hali ya nchi ni sifa za maeneo yaliyopo katika upande wa Tropiki. Kiasi cha mvua ni chini ya milimita 250 kwa mwaka, nacho hupungua hadi kufikia milimita 100 katika Sahara. Lakini, hata hivyo, kuna haja ya kutofautisha kati ya Sahara ya kaskazini yenye mvua za Kimediterani nyakati za baridi, Sahara ya kati, isiyokuwa na mvua, na Sahara ya kusini yenye mvua za kitropiki katika nyakati za joto. Kutokana na kupungua kwa tungamo ardhi ya bara hili jangwa la Kalahari huathirika zaidi na mikondo ya kusini-magharibi ya bahari.

*Tabia za hali ya nchi za Kimediterani*

Katika Maghrib na kwenye ncha ya kusini mwa Afrika, sifa kuu za tabia ya hali ya nchi ni msimu wa majira ya baridi na wenye mvua na msimu wa majira ya joto kali na ukavu.

*Mazingira ya tabia ya hali ya nchi yanayohusiana na uhai katika Afrika*

Sura na tabia ya hali ya nchi huungana kufanya mchangamano wa kiikolojia; kila mmoja ukiwa na sifa zake za kihidrolojia, udongo na kibotania.

*Mtiririko wa maji ya bara**Ruwaza ya mifumo ya kihidrolojia*

Zaidi ya nusu ya Bara la Afrika ni kame. Katika kanda kame ya Mediterani, mvua ni adimu lakini kali na zenye kusababisha mtiririko wa maji mengi ambayo wakati mwingine hukusanyika kwa muda mfupi katika Wadi. Katika maeneo ya tropiki au ya ikweta ambapo mvua huwa nyingi zaidi, mito mikuu na vijito vyake huunda mifumo mizuri, lakini mara nyingi lupata matatizo ya kuingiza maji yake baharini/ziwani. Kwa kweli, ili kuingiza maji baharini, maji ya bara yanapaswa kupita kwenye milinia ya mwambao kwa kupenya kwenye mapengo yaliyoachwa na maporomoko. Mto Zaire una maporomoko madogo thelathini na mawili kati ya Stanley (malibo) Pool na mlango wa mto. Mto Zambezi huanguka karibu mita 100 kwenye Maporomoko ya Victoria kabla ya kuingia kwenye korongo nyembamba ya Kariba na kupita juu ya maporomoko kadha ya mawe meusi magumu. Kuna maporomoko sita ya Mto Nile kati ya Khartoum na Mediterani. Mito yote mikuu ya Afrika— Niger, Senegal, Orange, Limpopo n.k.— ina maumbo ya namna ya vidato, hususa katika sehemu zake za mwisho; jambo ambalo linafanya iwe rahisi kuelewa ruwaza ya mpango wa makazi ya binadamu barani Afrika. Kati ya mito hii mikuu kuna vijito vingi, mabwawa na vinamasi visivyokuwa na mifereji ya kutolea maji mara kwa mara. Mifereji ya ndani ni ya ajabu zaidi hasa katika mabonde ya Chad na Okovango, Macina — delta ya ndani ya Mto Niger— na Bahr el Ghazal.

*Mifumo ya mito ya Afrika*

Mifumo ya mito hutawaliwa na ruwaza ya mvua. Kwenye ikweta mtiririko huwa wa kudumu kutokana na mvua kunyesha daima. Katika kanda ya tropiki, kipindi cha mfuriko wa maji ni matokeo ya msimu wa mvua wakati wa majira ya joto na hufuatiwa na kipindi cha maji mafu ya majira ya baridi ambapo wakati mwingine mifumo wa mtiririko huonyesha tofauti kubwa. Katika kanda ya Mediterani, tufani kubwa na milima hufanya mafuriko makubwa katika majira ya baridi na hupungua sana katika majira ya joto.

*Mito mikuu ya Afrika*

Kutokana na urefu wa njia zake na latitudo ambazo mito hiyo hupitia, mito hii ina mifumo changamano na ya namna mbalimbali.

Mfumo wa Mto Zaire, ambao unapita kwenye eneo la mita za mraba milioni nne na hujazwa na matawi yenye nguvu toka kizio cha kusini (Kasai na Lualaba) na kizio cha kaskazini (Shanga na Ubangi) una maji mengi yanayotirika wakati wote kwa kiwango kikubwa cha ujazo wa mita 40 000 za ukubwa wa kila sekunde, kiwango kinachopitwa na kile cha Amazoni tu.

Mto Nile ambao unatanda kwenye masafa ya kilometa 6,700 toka ikweta hadi Mediterani, hujazwa na maji yanayotiririka kutoka sehemu za ikweta. Maji hayo yanatawanyika kwenye vinamasi vya Bahr ele Ghazal. Kisha kutoka katika sehemu za tropiki, Mto Nile hujazwa na matawi mawili, Blue Nile na Atbara, ambayo hutirika kutoka nyanda za juu za Ethiopia na kuupa msukumo unahitajiwa ili uweze kupita kwenye majangwa mapana ya Unubi na Libya kabla ya kufikia Bahari ya Mediterani. Ijapokuwa nguvu ya mtiririko ya mto huu ni ya ujazo wa mita za ukubwa 3,000 tu kwa sekunde, lakini umekuwa ni mojawapo ya mito yenye manufaa kwa sayari hii tangu zama za Kale.

Mto Niger una mfumo usio wa kawaida kwa sababu ya kuruba yake kubwa. Mto huo huanzia Guinea, karibu sana na Bahari kuu ya Atlantiki. Kisha huelekea kwenye jangwa la Sahara ambalo unaliambaa kwenye kilele cha kuruba yake kwa namna tatanifu ambayo hufanya "delta ya ndani". Kinyume na sehemu zake za juu, ambazo hupata maji kutokana na unyevunyevu wa kitropiki, mkondo huu wa katika huwa mfinyu. Kwa upande mwingine, selemu ya chini inayoishia kwenye Ghuba ya Guinea huzidi kupata mvua za ikweta ndogo na maji yanayoingia kutoka Mto wa Benue. Kwa hiyo Mto Niger una schemu mbili zinazopata mafuriko ambazo kwa kiasi fulani hukutana huko chini. Lakini schemu hizo huizunguka selemu ya katikati ambapo mtiririko hufia sana kutokana na mnyweo na mvujo.

### *Aina za Udongo Katika Afrika*

Aina tofauti za udongo ni matokeo ya athari za halijoto na maji. Katika kanda za tropiki, na hususa katika macneo ya Sudani yenye msimu wa joto uliodhahiri, mvua fufutende zenye asidi lupenyeza miamba na kuyeyusha madini muhimu na kuyapenyeza ndani katika ardhi. Aina hizi za udongo huwa nyepesi na za mchangamchanga katika matabaka ya juu na udongo wa mfinyanzi katika tabaka ya chini. Udongo kwake huharibika iwapo haukufunikwa na mimea. Wakati mwingine, oksidi za chuma na alumina - yote yakiwa madini yenye faida - hutokeza juu ya ardhi na kuchanganyika na udongo wa juu na kufanya udongo mgumu usio na urutuba au *bowe* ambao haufai kwa kilimo. Aina kama hizo za udongo lupatikana kaskazini-magharibi mwa Antananarivo nchini Madagascar.

Katika mazingira ya unyevu mwingi ya ikweta au tropiki, kuoza kwa miamba kumesababisha kuwepo udongo wa kina fulani na ambao hauchukuliwi na maji au upepo kwa sababu aina hizi za udongo hazina mboji au mbolea ya kutosha.

Katika macneo yanayotangulia jangwa, ambako ule utando mgumu kwenye ardhi haufanyiki kwa urahisi, kuna udongo mwepesi na tufufu ambao ni mzuri kwa kilimo. Lakini udongo wa aina hii hauna budi kuachwa kilala kwa muda mrefu.

Katika majangwa, matatu ya mchanga (*ergs*) na maeneo mapana ya changarawe (*regs*) huwa hayana rutuba. Macneo yenye maji na yenye kutembelewa sana na watu si schemu za milima na oasisi.

Kulika kikemikali kwa miamba si jambo linalotokea sana katika mazingira ya Mediterani na udongo kwa jumla huwa wenye rutuba zaidi.

## Maeneo ya kijiografia yanayohusu uhai

### *Msitu mnene wa mvua*

Maeneo haya ni matokeo ya tabia ya hali ya nchi, hali ya kihidrolojia na ya udongo kama ilivyokwishaelezwa. Katika kila upande wa ikweta, misitu minene ya mvua huwa yenye matabaka kadha ya spishi za mimea isiyopukutisha majani. Misitu huwa miembamba kwenuye kingo zake na kufanya vichaka vyenye kinamasi na maeneo yaliyo wazi ambayo yanaashiria hali ya unyevu kidogo. Mazingira haya ni ya hatari kwa binadamu kwani yanejaa vimelca, ndege, reptila, na wanyama waishio mitini, ilihali wanyama wakubwa zaidi kama vile kiboko, tembo na chui huishi katika sehemu zisizo na misitu mikubwa sana.

Nje ya kanda ya ikweta, misitu mikubwa ya mvua huonekana kwenuye miteremko ya safu za milima inayopigwa na pepo zenye unyevu, kama vile kwenuye mwambao wa mashariki mwa Madagascar.

### *Savana na misitu yenye miti michache*

Kutoka kwenuye misitu hadi kufika Savana kuna mandhari mbalimbali yanayozidi kuwa wazi. Kwanza ni nyika za savana, yenye misitu mingi iliyo kando mwa mito, kisha kuna mbuga za savana ambamo maeneo ya miti na nyika zenye nyasi ndefu hupakana. Hii hufuatwa na nyasi za savana na vichaka vya savana ambapo miti huwa michache na midogo zaidi na ardhi wazi huonekana hapa na pale. Aina hii ya mazingira hupendelewa sana na wanyamapori walao majani na wawindaji wa wanyama hao.

### *Maeneo ya mbuga*

Sifa halisi za maeneo yenye mbuga ni kuwepo kwa wingi kwa vichungu vya nyasi na vichaka vyenuye miiba. Hali hii ndiyo inayoonekana huko Sahel, Kalahari na kusini-magharibi mwa Madagascar.

### *Mimea ya Kimediterani*

Mimea ya Mediterani huwa na miti ambayo ina majani yasiyopukutika ya aina ya inwaloni ya *Oak*, *cork-oak*, msunobari na mwerezi, ambayo yote huwa ni spishi zenye majani yasiyopukutika na kufunika magugu.

## *Hitimisho*

Ukubwa wa hara la Afrika ulimaanisha kuwa kwa muda mrefu watu wake wengi walikuwa na mawasiliano kidogo na watu waliokuwa pembezoni mwa bara hili mpaka baadaye kabisa. Alimradi hali za kiukolojia zilikuwa muafaka, maendeleo ya ndani yalipiga hatua ya kuridhisha kama ilivyokuwa katika kipindi kabla ya historia wakati Sahara ilipokuwa ikipata mvua na katika Bonde la Nile na watu wa kale. Lakini tabia ya hali ya nchi ilipoanza kuwa mbaya, Waafrika walianza kutangatanga kwa kipindi kirefu. Biashara baina ya Waafrika kati ya maeneo ambamo mazao ya kilimo na madini yalijalizana yalisababisha kuwapo kwa biashara baina ya bara hili na mabara mengine, biashara ambayo zaidi ilinufaisha mabara hayo mengine. Dhahabu ya Unubi na Ukushi iliituniwa na Misri na Mafarao. Dhahabu ya kanda ya Sudan na ya Zimbabwe ikiwa njia ya kuzipatia Magrib na Mashariki ya Karibu ufanisi na papo hapo ikinarisha dola za Sudani ya Magharibi na Monomotapa. Katika zama za kale kulikuwa na biashara ya chuma baina ya kaskazini na kusini, ambapo shaba nyekundu ilikuwa ndiyo msingi wa msafaru wa biashara kati

ya mabara kuelekea Bahari Kuu ya Hindi. Migodi ya chumvi iliyoko ukingoni mwa Sahara ilichukuwa nafasi muhimu kati ya falme zilizoko kusini mwa Sahara na Waberiberi wa Kiarabu. Tangu kame ya kuni na tano, usafirishaji nje wa bidhaa umezidi kuchukua nafasi ya mifumo hii ya biashara baina ya mabara.

## *Jiografia ya kihistoria: vipengee vya kiuchumi*

14

Waafrika walikuwa na maliasili zipi kuu tokea kipindi kabla ya historia? Ni wapi na vipi maliasili hizo zilipatikana? Na kwa namna gani zilikawiza au kuharakisha juhudi za binadamu za kulidhibiti bara hili?


### *Madini na maendeleo ya teknolojia ya binadamu*

Kati ya maliasili zote duniani kwa ajili ya matumizi ya binadamu yaelekea madini ndiyo muhimu zaidi kwa ulimbikizaji mali na kuzidhibiti nguvu za asili. Mchangamano wa tabaka la kale litokanalo na majabali ya fuwele lililofunika theluthi moja ya bara hili, limejaa utajiri mwingi sana wa madini. Ukanda wa Shaba Nyekundu ulioko katika jimbo la Shaba, wenye eneo zaidi ya kilometa 300, ndio wenye utajiri mkubwa ulimwenguni wa mtapo wa shaba. Vilevile hupatikana madini ya radumu na kobalti. Huko Transvaal, Afrika ya Kusini, kishoroba cha kilomita 500 chenye utajiri wa madini kama vile platinumu, kromiumu na asbesta kimeingia hadi Zimbabwe. Kanda yenye almasi katika Afrika haiwezi kulinganishwa na schemu nyingine yoyote ulimwenguni: inapatikana kwa wingi sana Afrika ya Kusini, lakini mashapo yapo pia katika nchi nyingine za Afrika ikiwa ni pamoja na Zaire, Angola na Tanzania. Hali ni hiyohiyo kuhusu dhahabu, bati na mtapo wa chuma— ambayo hupatikana karibu katika kila nchi — na madini ya boksiti ambayo Guinea pekee ina zaidi ya nusu ya utajiri wote wa madini haya ulimwenguni.

Milipuko mikubwa ya volkano ilitoa miamba miongoni mwa maliasili nyingine ambayo ililika na kuwa udongo wenye rutuba au kuweza kuchongwa kutengenezea zana za mawe, kama yale mawe meusi ya obsidia yaliyoko Kenya, ambayo yalikuwa na umuhimu mkubwa katika enzi za kabla ya historia.

Miamba tabaka iliyoenea karibu theluthi mbili ya tungamo ardhi ya bara hili ni muhimu sana kama chimbuko la utajiri wa madini: kwa mfano Namibia na Afrika ya Kusini zina mkusanyiko wa mtapo wa chuma, ilihali katika schemu nyingine kuna mikusanyiko mingi ya fosfeti na pale ambapo kuna upungufu wa makaa ya mawe kuna maeneo makubwa sana ya petroli na gesi.

Katika baadhi ya schemu, maliasili hizi zimekuwa msukumo wa historia ya Afrika kama ilivyo, kwa mfano, katika biashara kuu ya dhahabu iliyokuwa ikifanyika kupitia Sahara nyakati za Enzi za Kati. Kitu kilichowavutia Waarabu katika Afrika ya Mashariki kilikuwa ni kuwepo kwa dhahabu na chuma huko Zimbabwe, ilihali ukoloni ulisababisha Afrika kubaki nyuma na kuwa tu mtoaji wa malighafi.



14.1 Matisili ya madini katika Afrika (kutoka A. Journaux, 1976, "L. Afrique", Coll.Hatier)



Katika kipindi kabla ya historia, teknolojia ya msingi ya binadamu iliyokuwa inatumika barani Afrika ilikuwa ya kutengeneza zana za mawe. Teknolojia hii ilihitaji miamba iliyokuwa na umbo la namna moja, migumu na yenye kujeya kama vile vioo vya volkano vya Bonde la Ufa la Afrika ya Mashariki, ambavyo vilikuwa msingi wa viwanda vya Kapsia vya enzi za kipaleolithi vilivyotengeneza mabamba marefu na aina mbalimbali za zana ndogondogo za kimikrolithi.

Vitu vingine muhimu kwa kazi za aina hii ni pamoja na miamba ya kisilika kama vile kwatzi na miamba migumu na laini sana kama vile shisti na silikiti ambayo ilitumika katika viwanda vya Acheuli vya enzi ya mawe ya mwanzo, ilihali flinti ilikuwa ikitumika katika sehemu kubwa na watu wa Misri na wa uwanda wa juu wa Tunisia wa kipindi kabla ya historia, na chalissoni au silikiti za fuwele ambazo zilikuwa msingi wa viwanda vya Bambata vya Zimbabwe vya enzi za Kimesolithi.

Kati ya miamba ya volkano iliyoko chini sana au ile iliyo katika kina cha kati, mawe meusi, dioriti na deleriti ilitumika kutengeneza silaha, kama vile mawe ya kutupa vigumba, vyombo, sanamu na kadhalika. Hata miamba laini kama vile chokaa, au ile laini sana kama vile stetiti pia ilitumika, hasa nchini Misri. Aidha, tope ilikuwa mali ghafi kwa ufinyanzi katika bara lote.

Hapakuwepo na kikomo chochote kuhusu matumizi ya madini katika kipindi kilichotangulia historia. Yalitumika katika ujenzi wa vibanda na maskani, udongo ulitumika katika ukandikaji, na katika kujengea mapiramidi ya Misri (itale na kwatzi), na hali kadhalika kwa kutengeneza rangi kwa ajili ya michoro ya mapangoni.

Hata hivyo, mabadiliko muhimu zaidi yalitokea chuma kilipoanza kutumiwa katika miaka ya baadaye ya kipindi kabla ya historia. Mashapo mengi yenye kiasi kikubwa cha mitapo ambayo sasa hivi yanahitajika ili kutoa faida kutokana na vitegauchumi vingi vilivyocwekwa, hayakuhitajika katika kipindi kabla ya historia na kwa hiyo lateriti ya chuma ambayo inapatikana sana katika maeneo ya Savana ilitumiwa kwa wingi. Matumizi ya awali ya shaba na bati, kinyume na matumizi ya chuma (ambayo yalienea sana mara teknolojia iliyohusika nayo ilipovumbuliwa) yalibakia katika sehemu kadhaa tu kama vile Kaskazini-Mashariki mwa Ethiopia na jimbo la Shaba hivyo kwamba sehemu kubwa sana haikupitia kwanza hatua ya utamaduni wa shaba nyeusi kabla ya kupea kwenye enzi za chuma. Nebi mojawapo iliyokuwa na hali tofauti ilikuwa Mauritania, ambavyo ilikuwa na kipindi cha shaba nyingi karne tano hivi kabla ya enzi ya Ukristo.

### *Matumizi ya mimea na kuongezeka kwa idadi ya watu*

Sehemu kubwa ya Afrika ni uwanda wa nyasi ambazo zimefunika asilimia hamsini ya bara lote ukilinganisha na asilimia thelathini ikiwa ni eneo la majangwa na asilimia ishirini ikiwa ni eneo la misitu. Mimea ilikuwa ni chakula kikuu kwa viumbe vyote kwa miaka mingi: zaidi ya kuwa chakula kwa wanyama pori, mimea pia ilitoa majani, maua, matunda na mizizi inayolika; ilitoa nyanzo za kutengeneza zana, nguo na makazi na ndiyo iliyokuwa msingi na mapinduzi ya kilimo yaliyotokea wakati mbegeu na miche ilipoanza kupandwa katika kipindi cha Neolithi.

Katika muktadha huu, sehemu muhimu kwa ajili ya makazi ya binadamu zilikuwa kandokando ya mito, maziwa na bahari, katika mazingira ya savana. aina zote za rasilimali — wanyama, samaki au chaza, ama magome ya miti na mazao yake mbalimbali vyote vilikuwepo katika sehemu hizo. Kwa mujibu wa J.D. Clark, matunda mengi ya porini njugu na mimea iliyotumiwa na watu wa Nachikufa wa Zambia ya Kaskazini wa enzi kabla ya historia, kama vile matunda ya *mbuyu* na *musuku*, bado yanaliwa na wakazi wa sehemu hizo.

Hata hivyo, yafaa ikumbukwe kuwa, kanda za mimea zimekuwa zinatofautiana sana tangu zamani za kale. Kwa mfano, Sahara, ililipitia awamu kubwa za mabadiliko ya hali ya hewa yaliyoandamana na mabadiliko makubwa sana ya mandhari ya nchi. Katika kipindi cha Neolithi wanyama wengi sana waliishi katika sehemu za misitu, na mojawapo ya mabaki ya misitu hiyo ni mti uitwao Tenere ambao umehifadhiwa katika Jumba la Makumbusho la Niamey. Inasadikiwa pia kuwa misitu ya ikweta ilipitia vipindi ambavyo vilikuwa vya ukame-ukame.

Wakati huo maliasili ya mimea ilikuwa na matumizi makubwa zaidi kuliko ilivyo siku hizi. Karibu na Maporomoko ya Kalambo kusini kabisa mwa Ziwa Tanganyika, kumegunduliwa zana za miti za kuchimbia zenye ncha kali au ncha mshazari zilizohifadhiwa vyema tangu kipindi cha mwanzo wa Paleolithi.

Vikombo vizito vilivyotumiwa na Wanachikufa wa Zambia na Malawi, sawa na mawe magumu yaliyochongwa ya tasnia ya Lupemba ya misitu ya ikweta, vinadhihirisha matumizi ya zana za mawe katika kutengeneza vifaa vya miti. Kwa upande mwingine, mti ulitumika katika kukamilisha zana za mawe.

Wahenga wetu wa kipindi kabla ya historia walitumia magome na majani ya miti kutengeneza nguo, vyombo na kamba. Zaidi ya hayo, kuanzia kipindi cha Mesolithi na kuendelea, matawi ya miti, majani ya kuzekka au kusukia huenda yalitumika kutengeneza vikinga upepo, kama ushahidi unavyoonyesha katika mabaki yaliyogunduliwa katika Chemchemu za Gwisho huko Afrika ya Kusini. Ilipofikia kipindi cha Neolithi, makazi yaliyojengwa kwa miti ambayo, wakati mwingine yatikandikwa kwa tope, taratibu yalichukua nafasi ya mapango yaliyotumiwa cnzi za nyuma. Macendeleo haya yalikuwa hatua dhahiri za awali za binadamu kuanza kutamalaki mandhari ya ardhi.

Hata hivyo, ilikuwa ni upandaji wa mimea ili kuzalisha mazao anuwai ndiko kulikoleta mabadiliko makubwa na ya kudumu katika mazingira ya binadamu. Kwa hali hiyo, Afrika ilijifunza mengi kutoka Asia na Latini Amerika, lakini ilitoa mchango wake pia katika urithi wa kilimo kwa binadamu kwa kugundua vitu ambavyo baadhi yake vilienea ulinwenguni.<sup>1</sup>

Haja ya kutayarisha shamba ili kupanda mbegu ilisababisha pia mabadiliko makubwa katika hifadhi ya mimea ambayo matokeo yake bado yanathiri hadi leo. Moto ambao ulitumiwa na binadamu katika Afrika takribani miaka 60,000 iliyopita kwanza kwa kujikinga mwenyewe na baadaye kwa kuwindia na kutengeneza zana, ulisaidia pia kuondoa mimea ambayo haikuhitajika. Hii ndiyo sababu ya uharibifu wa kudumu wa nyasi na hasa miti, na kuendelea kuenea kwa uwanda wa nyasi mbuga na kuundwa kwa savana na binadamu. Kuanzia kipindi kabla ya historia na kuendelea, misitu mikubwa ya Afrika imekuwa ikipungua na kutoweka kutokana athari ya hali ya hewa na binadamu. Nyanda za nyasi zilizochukua nafasi yake zilikuwa rahisi kufyekwa kwa ajili ya kilimo na njia. Kwa hiyo, inaeleweka kuwa sehemu muhimu za makazi ya binadamu katika kipindi hicho zinaweza kuonekana hasa savana. Inafahamika pia kuwa, kutokana na athari za ongezeko la idadi ya watu, uhamaji wa mara kwa mara ungewasukuma watu hawa kuendelea mbele katika utaratibu ambao pengine haueleweki vizuri lakini ambao ushahidi wake umo katika nyaraka za akiolojia, cchinografia, lugha na historia. Hivi ndivyo mawazo mapya na ugunduzi wa kiteknolojia ulivyosambaa, pamoja na dhana mpya za kijamii na kisiasa. Vikundi vilivyoamua kukimbia mfumo wa utawala wa mabavu vilicendelea mbele zaidi vikiwa mstari wa mbele katika kuanzisha na kuniliki eneo kubwa lisilo na ukomo. Walipoandamwa walikinbililia katika sehemu za maficho kama vile kwenye mitereniko ya safu za milima, sehemu zilizo kame au kanda zenye misitu mikubwa.

<sup>1</sup> Tazama Sura ya 27 ya Juzuu hili.

Jambo muhimu lililosababisha ongezeko la idadi ya watu lilikuwa ni kuongezeka kwa kilimo ambacho walau asilimia 80 ya Waafrika wote walijishughulisha nacho hadi kufikia katikati ya karne hii. Kufuatana na Carr Saunders, hadi 1650 Afrika ilikuwa ya pili baada ya Asia katika idadi ya wakazi wake. Idadi yake ya watu milioni 100 iliwakilisha zaidi ya asilimia 20 ya idadi ya watu katika ulimwengu ilihali sasa imeshuka kufikia asilimia 10. Dola na falme ambazo zilidumisha amani na usalama ili kuweza kutawala, zililazimika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kuongezeka kwa idadi ya watu, na dalili za athari zao bado zinaweza kuonekana katika mapana ya mbuga za Sudani kuanzia Senegal hadi Chadi, katika Mali, nchi za Waniossi na Wahusa. Idadi hii kubwa ya watu ilipungua kutokana na biashara ya utumwa na ukoloni.

### *Matumizi ya wanyama na mielekeo tofauti ya kitamaduni*

Afrika ni bara lenye idadi kubwa sana ya mamalia, na kwa hakika zaidi ya familia thelathini na nane tofauti za mamalia zimekwisha bainishwa. Kanda zote za bara hili zingeweza kudai kuwepo kwa aina mbalimbali za wanyama pori wakati fulani.

Kanda ya Mediterani iliwahi kuwa makazi ya simba na tembo, kama ilivyothibitishwa na mabaki ya visukuku vya kipindi kabla ya historia, taarifa za kampeni za Hannibal dhidi ya Warumi na ripoti za safari za mashambulizi za Wakoloni wa Kifaransa za katikati ya karne ya kumi na tisa.

Hadi leo, jangwa bado linahifadhi viclelezo vya wanyama pori wengi wa zamani wenye sura za swala na choroa wa aina mbalimbali. Kwa bahati mbaya kuanzia enzi za kale na kuendelea, wanyama pori wengi walikufa katika michezo ya kikatili kwenye viwanja vya kucheza na wanyama huko Rumi.

Siku hizi nyanda za nyasi za Afrika ndizo pekee ambazo bado zinatoa mwanga wa kutosha kuhusu wingi wa wanyama ulivyokuwa hapo mwanzoni, japokuwa tabia ya wanyama na mabadiliko ya mazingira vimekuwa na athari zake. Kwa mfano, vifaru wcupe walitoweka kwenye enco kati ya Zambezi na sehemu za juu za "White Nile" kwa sababu ya mabadiliko ya tabia ya lali ya nchi na minca ambayo iliwafaa zaidi vifaru weusi waliokuwa na uwezo wa kukabili mazingira. Spishi kama vile bango, wanatoweka kadiri macueo ya makazi yao ya misitu mikubwa ya mvua yanavyopungua.

Hata hivyo, kwa maelfu ya elfia, wanyama pori walikuwa wengi kiasi kwamba baadhi ya jamaii za Kiafrika hazikuona sababu ya kutafuta chakula chao kwa njia nyingine mbali na kuwinda. Samaki walikuwa sehemu ya chakula cha Mwafrika tangu wakati wa kipindi cha Mesolithi. Mito kama vile Nile na maziwa kama vile Chad, Nakuru, Turkana na Edward yanaonyesha, katika ufuko, dalili za kusambaa sana kwa vifaa vya uvuvi vyenye umbo la chusa za mifupo na ndoana za samaki. Mitumbwi iliyotengenezwa kwa kuchonga magogo ya miti au kusuka mafunjo inatumiwa na Waafrika hata leo, japokuwa zana hizo ni duni, wanyama wakubwa kama kiboko, mamba na nguva wamekuwa wakiwindwa na kunaswa hapa Afrika.

Kuzaliana kupita kiasi kwa wanyama pori kulikuwa na faida na hasara zake kuhusiana na ufugaji wa wanyama. Kulikuwa na uwezekano mkubwa wa kuchagua aina mbalimbali za wanyama walioweza kufugwa, lakini wakati huohuo, kule kuwepo kwa wanyama pori wengi sana kulipunguza haja ya kuwafuga. Matokeo yake ni kwamba, punda, paka kanga, kondoo na ng'ombe tu ndio wanaelekea kuwa walifugwa Afrika.

Wafugaji wa kwanza wa Kiafrika walijitokeza katika jangwa la Sahara katika kipindi cha Neolithi. Japokuwa wanyama waclache mbalimbali walifugwa na jamii zote, ni jamii elache tu zilizoziya barabara mbinu za ufugaji wa wanyama wengi, na baadhi yao kama vile Watuaregi

wa Sahara, Wafulani wa Savana ya Afrika Magharibi na Wamasai wa nyanda za nyasi za Afrika ya Mashariki waliendeleza mbinu za ufugaji hadi kuifanya uwe ndio mtindo wa maisha yao. Wakati mwingine, makundi mengine yalichanganya ufugaji wa wanyama na kilimo ili shughuli hizi zifaidiane.

Swali la kujiuliza ni kama kulikuwa na vizuizi vilivyozuia ustawishaji wa mifugo ambavyo vilikuja kuathiri vibaya mapinduzi ya kilimo katika Afrika. Yawezekana kuwepo kwa spishi nyingine za wanyama wabaribifu kulifanya ufugaji usiendeleo sana. Kwa mfano mbun'go ni mdudu anayecambukiza binadamu ugonjwa wa malale na kuua wanyama. Schemu ambazo hazina ugonjwa huu ni zile za nyanda za juu na schemu za joto zenye nyasi fupi. Kwa hiyo basi kuna kipinganizi cha kikolojia dhidi ya ufugaji kinachorudi hadi enzi za kabla ya historia, kama inavyodhihirishwa na hali ya visukuku vya wadudu vilivyopo katika matabaka ya chini ya ardhi. Kupungua kwa maeneo ya ufugaji henda kulitokana na mabadilikobadiko makubwa ya tabia ya hali ya nchi yalitokea mwishoni mwa kipindi cha kabla ya historia. Kwa hali yoyote ile, kuhama kwa makundi ya mifugo toka Afrika ya Kaskazini kuelekea Kusini kulitokana na kuwepo kwa vijishehemu visivyokuwa na mbung'o na/au kuanzishwa kwa selemu zenye idadi kubwa ya watu ambazo misitu yake ilivyekwa. Mfano mmojawapo wa maeneo yaliyokuwa na idadi kubwa ya watu ni makazi ya miaka elfu moja iliyopita ya wafugaji waliochanganyika na watu wengine katika nchi zinazojulikana hivi leo kama Rwanda na Burundi. Haitakuwa ni kukuza sana mambo tukisema kuwa kama kusingekuwepo na mbung'o, historia ya Afrika ingelichukua mwelekeo mwingine. Kutotumika kwa wanyama wavuao mikokoteni enzi hizo kunaweza kuhusishwa na athari za madhara ya mbung'o. Hali hizi ngumu zinaweza kuwa ndizo zilizochochea uhasama kati ya wafugaji wao wenyewe na baina yao na makundi ambayo hayakuwa yameendelea kama wao. Katika hali kama hizi kuwepo kwa askari wapanda farasi kulisaidia sana katika uundaji wa tawala Kaskazini mwa ikweta.

Mdudu mwingine mharibifu alikuwa ni mbu wa malaria (*Anopheles Gambiae*); ambaye anapenda kufyonza damu ya binadamu, lakini kwa kuwa anafyonza damu ya wanyama pia, ni vigumu sana kumtokomeza. Kwa kawaida hupatikana katika maji yaliyotuama na schemu za joto na unyuvunyevu, lakini haonekani kwa wingi katika schemu za miinuko.

Uvimaji wa damu wa idadi kubwa ya makundi ya Waafrika ambao kwa kiasi fulani wameuzoea ugonjwa huu, unaonyesha kuwa mbu wa malaria wamekuwepo kwa muda mrefu, na kwa hakika, pengine kwa maelfu ya miaka. Kwa kuwa mbu huyu anatishia ubai wa makundi ya watu ambao hawakuyazoea mazingira haya na kwa kuwa ugonjwa huu unesababisha kupotea kwa siku nyingi zisizohesabika za kazi, malaria yanaweza yakawa ndicho kiini hasa cha historia ya bara hili, kiasi kwamba, katika kama ya kumi na tisa, kuwepo kwa mbu wa aina ya *anofeles* kulisababisha baadhi ya sehemu za Afrika kutokaliwa na wakoloni. Wazungu walipendelea kutawala sehemu hizi kwa kuwatumia wenyeji badala ya wao wenyewe kukaa humo ili kuipuka vifo vingi. Badala yake walichagua kuishi katika sehemu zilizoinuka za Kaskazini, Mashariki, Katikati na Kusini mwa Afrika.

Nzige - nzige wa jangwani, nzige-wahamaji wa Afrika na nzige wekundu - wanawakilisha moja ya mabaa makubwa ya Afrika ambayo yametajwa katika Biblia kuhusiana na adhabu ya Mungu iliyotolewa kwa Farao wa Misri. Wadudu hawa wanahitaji ardhi tupu kwa ajili ya kutagia mayai na mimea mingi kwa ajili ya chakula. Hii inaeleza kwa nini wanapenda mashamba ya mtama yaliyopatikana na kusitawi vizuri. Inapokuwa eneo la malisho yao ni dogo hujikusanya katika makundi makubwa sana na kuvamia kila kitu katika maeneo muafaka. Uvamizi wa nzige, kabla ya mavuno, ni isliara ya njaa. Baa la nzige na ukame huangamiza jamii, husababisha uhamaji wa makundi inakubwa ya watu au kuleta misukosuko katika jamii.

## *Matumizi ya maji na uhamaji wa watu*

Tatizo la maji katika Afrika ni kubwa. Kutegemea na mahali kuna sehemu za Afrika zenye kiasi kikubwa sana cha mvua na sehemu nyingine zenye kiasi kidogo sana cha mvua ulimwenguni.

Eneo kubwa sana la jangwa katika bara hili ni ushahidi mkubwa wa tatizo hili. Katika savana ya Kisudani, ambako mvua yake ni karibu sawa na ile ya Paris, watu wanataabika kwa ukame kwa sababu kiasi kidogo cha mvua inyeshayo hunyesha kwa miezi minne tu katika mwaka. Ardhi yenye rutuba iliyoko katika mabonde ya mito imejaa mbu na kwa hakika mito mingi hukauka kabisa wakati wa kiangazi. Kuna sehemu chache, kama Misri au Casmance, ambako udhibiti wa ugavi wa maji umewezesha kupatikana kwa mavuno makubwa sana. Kuwepo kwa miamba ya chini isiyopenya maji katika sehemu nyingi kunasababisha maji kupotea na mmomonyoko. Uhaba wa maji ni hali ya kawaida ya maisha barani Afrika. Uhaba huu ndicho kiini cha kutokuwepo kwa makazi ya kudumu ya binadamu, hali ambayo haiendelezi ulimbikizaji mali, tabia ya kuhamahama kwa wazalishaji mali wa vijijini ambayo haileti maendeleo na uhamajihamaji wa watu na pia na kuingia mara kwa mara kwa watu, ambao kwa kiasi kikubwa walikuwa wapenda amani lakini ambao pia wakati mwingine walikuwa wagomvi na wanyang'anyi hata kuanzia kipindi kabla ya historia.

Kinyume cha hayo, inaonekana kuwa pale ambapo utawala wenye nguvu umefanikiwa kulinda jamii imara za vijijini bila kuzinyonya kupita kiasi, kumekuwepo na mafanikio makubwa ya kijamii na kiuchumi na wakati mwingine ya kiteknolojia. Inaelekea kuwa kuanzishwa kwa mfumo imara wa kisiasa na wa kidini kwa wakulima, ni matokeo ya mfumo bora zaidi wa uzalishaji ambao unaruhusu kiwango fulani cha mgawanyo wa kazi.

## *Matumizi ya udongo na mabadiliko ya kijamii katika jumuiya*

Afrika haina nyanda tambarare pana zenye kina kirefu cha udongo, kama ilivyo katika mabara mengine hasa katika kizio cha Kaskazini. Aina tofauti za udongo zimefuatana moja baada ya nyingine na rutuba yake hutegema zaidi muundo wa ardhi yenyewe pamoja na tabia ya hali ya nchi, kwa mfano, katika sehemu za misitu yenye unyevunyevu, kuota kwa mimea kwa wingi huzuia hali ya kuvunjikavunjika kwa udongo. Mimba ikifyekwa udongo kupasuka pasuka. Rutuba hupungua haraka na inabidi kuhamia sehemu nyingine ambazo bado hazijalimwa.

Rutuba ya udongo huwa bora zaidi katika sehemu zenye kiasi kidogo cha maji, lakini tofauti kubwa za halijoto za msimu husababisha utando mgumu wa udongo mwekundu wenye madini ya chuma ambao hauna rutuba iliy katika sehemu kubwa za savana za Afrika ya Magharibi na nyanda za juu zilizoko kauka kingo za bonde la Zaire. Udongo mwingine wenye rutuba zaidi ni ule wenye kiasi kidogo cha maji wa aina ya Saheli, japokuwa wahitaji kiasi kidogo cha mvua.

Udongo ulio adimu sana katika Afrika na wenye rutuba sana ni ule ulioko nyanda za juu za Afrika ya Mashariki, ambako udongo mwekundu na wa rangi ya chokoleti una rutuba sawa na udongo wa kitope kwenye mabonde ya mto kama vile Nile. Sehemu kama hizi zikikaliwa na idadi kubwa ya watu, inaendeleo katika uvumbuzi wa teknolojia na ujenzi wa majumba huongezeka, kama invyoonkana huko Mesopotamia na nyanda kuu za India na China. Hali kama hizi zilikuwepo kwa kiasi fulani katika sehemu za katikati za Mito Niger na Senegal na ndiyo kiini cha maendeleo makubwa ya sehemu hii, iliyodhihirishwa na kuzuka kwa dola kubwa. Misukosuko iliyotoka katika karne ya kumi na sita ilikatiza maendeleo yote haya.

*Hitimisho*

Hisia aipatayo mtu anapoitazama Afrika atadhani kuwa ni bara lililobarikiwa na mali asili nyingi. Lakini ukilichunguza kwa makini, utagundua matatizo makubwa yaliyojificha katika wingi wa wanyama, mbuga kuwa zilizo wazi ambamo idadi ya watu imebakia kuwa ndogo sana na yenye kutatiza, hali ya hewa mbaya sana na maumbile ya udongo ambao hudanganya macho kuwa ni rahisi kulimika. Mambo yote haya yalisababisha kutokea kwa jamii nyingi zilizokuwa ndogo mno kuweza kuleta mabadiliko au kuhimili ushambulizi kutoka nje, wala kupambana na matatizo ambayo jamii yoyote ya binadamu inatarajia kupambana nayo ili kupata nguvu na ubora wa maisha. Kama tukiondoa bonde la Nile katika enzi za kale na mifano michache ya hapa na pale ya kipindi kabla ya historia na awamu za kipindi cha historia, funzo tunalolipata kutokana na historia Afrika na ya kipindi kabla ya historia ni kwamba watu wa bara hili hawakuwahi kupata mazingira ambayo yangefaa kuwa msingi wa kuanzisha mipango mikubwa ya kiuchumu. Huku kutokuwepo kwa shughuli za uwiano kwa muda mrefu sio matokeo ya laana fulani, bali ni matokeo ya mchanganyiko wa matendo yao, mazingira yao na unyonyaji wa wageni. Hii sio nadharia ya kuwepo na asili ya kila kitu. Kilichoumbwa na historia, historia luweza kukiambua. Kila kitu kinategemwa wiledi na utambuzi wa mambo.

*Mbinu za taaluma  
fungamano zilizotumika  
katika historia*

*Mkabala wa taaluma fungamano*

Historia andishi haina budi icleze ukweli wa mambo kama yalivyotokca. Lakini kwa namna ya historia ilivyo changamano hakuna somo moja ambalo peke yake unawcza kuzingatia vipengee vyake vyote na kuvifafanua. Kwa hiyo, inabidi wataalamu mbalimbali wakae pamoja na kusaidiana. Huo ndio utaribu uliokubaliwa na Kamati ya Kimataifa ya Sayansi ya Historia Kuu ya Afrika. Lakini, mara mkabala wa taaluma fungamano unapotajwa, kila tawi hujiweka mbele kuongoza katika kuelezea historia. Kwa hali hii, historia inaelekea kuwa kitu cha kutumiwa tu kwa kuwa ni taaluma ya kilimwengu ambayo inahitajiwa na tanzu zote za maarifa iwapo tanzu hizo zitataka kuelewa njia zilikotoka. Kuwapo kwa historia kwenye njia panda ya maarifa njia ambayo lufuluatawa na kila taaluma huifanya historia iwe madhubuti na papo hapo dhaifu.

Hadi kufikia karne ya ishirini, hati za maandishi zilikuwa ndiyo msingi wa ujengaji upya wa historia thabiti. Lakini katika Afrika, kutokana na uhaba wa hati za maandishi, historia imelazimika kukiuka mipaka yake ya desturi. Methali moja ya Kiafrika imenena kwamba 'Anayekosa la mama hata la mbwa huamwa'. Shida imesababisba kutumia mkabala wa taaluma fungamano na kwa kufanya hivyo kuepuka kuathiriwa sana na maandishi, ambayo yamegubika vyanzo vyote vingine na kuvifanya visifac.

Zaidi ya hayo, utafiti katika sayansi za binadamu na za jamii katika Afrika umehasiriwa na aina mbili za upendeleo ambazo zinakinzana na zisizoleta faida. Aina ya kwanza kati ya hizo mbili ni ile ya mkabala halisi wa kihistoria ambamo maendeleo ya binadamu huonekana kama mfululizo wa matukio wenye tarehe, mithili ya shanga zilizotungwa. Mbali na tarehe hizo vitu vyote vingine, ikiwa ni pamoja na masuala muhimu kama vile uchumi, muundo wa jamii na utamaduni, vinapuuzwa.

Kosa jingine, ambalo ni baya zaidi, ni la kudharau kabisa infaatano wa matukio na la kumulika tu miundo ambayo inapimwa kwa usasa usiomalizika wa kiethnografia. Kasoro hii inaonekana miongoni mwa wanaisimu ambao wametoepa katika somo lao na hawaoni wala kusikia mabadiliko yanayotokca katika lugha. Ukweli huo pia unawahusu wanaanthropolojia waamili ambao wameshindwa kuelewa ukweli kwanba kuwapo au kutokuwapo kwao wenyewe au wanaanthropolojia hakuvizuii vikundi vya mbari kuendelea.

Kwa bahati nzuri, suala la jinsi ya kutatua tatizo hili huchukuliwa kuwa muhimu zaidi kuliko majadiliano juu ya zana za kutumia katika kulitatua. Desmond J. Clark amcandika kuwa, 'Utambuzi kuwa wanaakiolojia, wanaisimu na wanaanthropolojia wa kitamaduni au wana-ethnografia wanakabiliwa na matatizo mengi yanayofanana na kuwa njia bora ya kuyatatua ni

kwa kufanya kazi pamoja na katika mfungamano wa taaluma ni mojawapo ya mambo ya kutia moyo na kisisimua katika mitaala ya Kiafrika hii leo'.

Kwa hiyo, aina ya historia bandia ambayo ilifuatilia tarehe moja baada ya nyingine na uchambuzi potofu wa miundo isiyohusiana na maisha halisi, vinaafikiana na fikra za wanaisimu kama Calame-Griule na Houis ambao wanarejesha tena dhana za maendeleo na kuhusiana kwake na utamaduni. Kadhalika, watetezi wa sosiolojia hai kama vile Balandier nao pia wanagundua tena vipengee vya kihistoria ambavyo huwa vya mikizano ya historia.

Hii inamaanisha kuwa hakuna taaluma ambayo peke yake inaweza kuelezea ukweli changamano kuhusu Afrika. Methali moja ya Saheli inatukumbusha kuwa intu mmoja peke yake hawezi kuuzinga msitu: hakuna kanuni moja ya maelezo ambayo peke yake inaweza kueleza sababu za kuwapo kwa jamii za Afrika. Kwa mfano, uchanganuzi wa muundo wa nasaba au wa visaasili na alama za kiitikadi hauwezi kusaidia katika kuelewa kikundi cha kijamii, isipokuwa kama mahusiano ya uzalishaji mahi yanatiliwa maanani pia. Kama Levi-Strauss anavyokiri, haiwezekani kupuza hali za kiuchumi na kijamii na kutazama ruwaza za nasaba peke yake tu.

Mara nyingi katika Afrika, kwa mfano, kronolojia, ambayo huonekana jambo la kihistoria lililo dhahiri kabisa, huweza tu kufuatiwa nyuma kwa kutumia mchanganyiko wa hati za maandishi, akiolojia, isimu na mapokeo simulizi. Hivyo ni vyanzo vinne tofauti vinavyokamilishana, kama vile kipima-maili na saa vya mwendesha gari, nguzo za mailli njiani na maelekezo anayopewa na mwenyeji wa mahala fulani vinavyompatia mwendesha gari huyo maelezo yanayoaminika kuhusu masafa aliyokwishakwenda au yaliyobaki, mbele yake.

Habari tulizonazo kuhusu Kumbi Saleh, mji mkuu wa Ghana ya kale, huthibitika kikamilifu tu iwapo maelezo yaliyomo katika masimulizi ya Al-Bakri yanajalizwa na magunduzi ya kiakiolojia, ambayo hutoa maelezo fasaha kuliko maelezo yanayotolewa na mtazamaji wa nje. Hata mapokeo simulizi nayo yalitoa mchango wake, yakasaidia katika kugunduliwa kwa magofu ya mji huu wa zamani.

Katika hali kama hizi, hakuna suala la kuwapo vyanzo bora au duni kuanzia cha juu hadi cha chini ya skeli. Katika kila mfano kuna chanzo muhimu kinachochukuliwa kuwa ni cha msingi ambapo vyanzo vingine huegemea. Afrika katika kipindi kabla ya historia au katika jamii za Mbilikimo, haiwezekani kutegemea hati za maandishi kwa kuwa hazipo. Kwa vipindi tofauti na katika maeneo mbalimbali utuuzi wa vyanzo ya kufaa hutegemea aina maalumu ya chanzo. Chanzo cha msingi si kilekile kwa Wakirudi wa Cameroon ya Kaskazini, Waasante wa Ghana, Wakabre wa Togo ya Kaskazini au Dola ya Gao. Tena, yamkini chanzo muhimu kama hicho kitabainika tu baada ya utafiti kumalizika, kwa sababu ingawa chanzo chaweza kusemekana chatawala matokeo lakini ni matokeo, yenyewe ndiyo yanathibitisha usahihi wa chanzo. Kwa hiyo, kwa mwandishi wa historia ya Afrika, mkabala wa taaluma fungamano zaidi huwa suala la lazima kuliko la hiari.

### *Jinsi marejeo yanavyokamilishana*

Aghalabu chanzo kimoja peke yake hakitoi picha sahihi ya uhalisi wa kihistoria, bali ni mchanganyiko wa vyanzo mbalimbali tu ndio huwezesha kutoa picha halisi.

Ripoti ya *machimbo* ya *kiakiolojia* inaweza kuwa orodha ya mambo yasiyowiana kama haitawekwa katika muktadha wa jumla wa maisha ambamo kwamo mahali palipochimbuliwa huwa ni sehemu ndogo tu. Matokco ya utafiti wa kiakiolojia huibua maswali kwa ajili ya taaluma nyingine na majibu yatakayopatikana yatamwczesha mwanaakiolojia kupata maelezo



kadha ambayo ni nje za taaluma yake. Mathalan, magofu makuu ya Zimbabwe yanaonyesha kuwa ngome zilijengewa kwa ajili ya ulinzi wa migodi ya dhahabu pamoja na kufanyia faradhi za kidini. Katika scheinu nyingine sababu za kuwekwa vifaa katika makaburi na namna maiti walivyokuwa wanawekwa katika makaburi hayo hazieleweki bado isipokuwa kama imani juu ya maisha baada ya kufa katika jamaa zinazohusika itatiliwa maanani. Ni dhahiri kuwa vitu vilivyofukuliwa vinasaidia kutoa picha ya dhana hizo, sawa na namna ambavyo machimbo yaliyofanywa kaskazini mwa Ghana (ambayo yamebainisha maumbo ya usanifu majenzi yanayofanana na za Saheli ya Kisudani) yanawezesha kuibuliwa au kufumbuliwa fumbo la kusisimua la athari za kitamaduni.

Kama ilivyo akiolojia, sanaa hudhahirishwa na taaluma nyingine nyingi. Sanaa, iwe ile ya kipindi kabla ya historia au la, hufichua undani wake tu iwapo itatazama kwa kuzingatia inazingira yote, kwa kutilia maanani jiolojia, hadhi ya kijamii, muundo wa kisiasa, visaasili na dini. Kwa upande mwingine, kwa kuirekodi ada, uchanjaji chale, mitindo ya ususi, mavazi na mandhari, sanaa huwa kama makumbusho ya kitamaduni na hata ya kiantropolojia ya kimaumbile.

Kwa hiyo historia ni kiini hasa cha sanaa. Kwa mfano, katika nchi ya Wayoruba ni wasanii walewale waliokata nakshi katika mbao na baadaye katika pembe za ndovu; wasanii walewale walitumia udongo wa mfyanzi na kisha shaba nyeusi. Mabadiliko hayahaya ya kuacha kutumia kitu kimoja na kutumia kitu kingine yanatuwezesha kuelewa maumbo ya kiumbuji yaliyotumika katika kukata nakshi kwenye pembe za ndovu au shaba nyeusi, kama ambavyo katika kipindi kabla ya historia kuscha kazi ya usukaji na kuingia katika kazi ya ufinyanzi mara nyingi hueleza sababu za kuwapo kwa maumbo na mapambo ya vyungu. Kwa mfano, vinyago huakisi maisha ya vijijini ambapo vinyago hutambuliwa kama kwamba ni watu, hata na watoto. Lakini vinyago hivyo pia huchangia katika kujenga historia ambayo kwayo vyenyewe ni usuhuda. Ukweli huu luonekana katika vinyago kama vile vya ndege mkubwa aitwaye Bobo, vya nyati na vya wahenga. Wakati mwingine, vinyago luombwa ushauri na hivyo kuwa wasta kwa vikundi kadha vya jamii kulingana na muktadha wa ruwaza za nguvu za jamii hizo zilizopata mashiko. Kauri zilizotajwa na Ibn Battuta katika kitala cha mfalme wa Mali mnamo mwaka 1352 zilikuwa zimokusudiwa zitumike kama sarafu, lakini pia zilitumika kama mapambo na zawadi za kifalme nyakati za sherehe za kijamii na za kidini. Kuanza kuandika historia ya jamii fulani za Kiafrika bila ya kuwa na ujuzi wa lugha tajiri ya kauri na vinyago ni mithili ya kwenda katika maktaba pasi kujua kusoma. Historia kama hiyo lazima itatoa tafsiri potofu ya mabadiliko ya jamii hizo.

Tunapoangalia *mapokeo simulizi* ambayo yameshajadiliwa katika sura zilizopita, na ambayo yameshakubaliwa kuwa ni chanzo kamili cha historia, huweza kutoa matokeo mazuri yanapotumiwa pamoja na vyanzo vingine ambavyo mapokeo simulizi yamesaidia kuvidhahirisha, kama vile maeneo ya kiakiolojia, hazina za kisanaa n.k. Ama kwa hakika, kabla ya kuanza kuchimba inafaa kukusanya mapokeo ya mahala hapo, ambazo mara nyingi husaidia kuharakisha kazi na kuelekea kwenye usahihi. Lakini kama kuna masimulizi kadhaa ya mapokeo hayohayo, vyanzo vingine, kama vile akioloji au rekodi za kupatwa kwa jua au mwezi, huweza kutumiwa ili kuamua masimulizi yapi ni sahihi kati ya hayo.

Kwa vile *muziki* unaambatana na mila, haiwezekani kuelewa bila ya kuuhusisha na vipengee mbalimbali vya utamaduni wa jamii. Ngoma ni mithili ya vitabu vikubwa hai vya Afrika. Ngoma hizi hueleza ujumbe wa wafalme, waaguzi, wajumbe, watia shime vitani au wanatarilii, na hivyo hutafsiri na kusukuma mienendo ya historia ya vijiji na ya falme pia. Kwa kweli, tendi maarufu hufuatwa na ngoma na huimbwa na vikundi vya kijamii ambavyo hutumia

ishara pamoja na sauti. Katika Afrika, mchanganyiko wa nyimbo, ngoma na muziki ni chanzo maridhawa cha maelezo kuhusu historia ya karibuni au ya zamani kidogo ya kikundi fulani, kwa sababu matukio makubwa, kama vile magonjwa ya kuambukiza ya wanyama, vipindi vya ukame au miaka ya njaa au ya neema au mafanikio au udhaifu wa wafalme, hutumika kama mada na wasanii wa mahala pale. Mwisho, ulinganisho wa ala za muziki na sifa nyinginezo za muziki huonyesha jinsi tamaduni zinavyoenezwa. Siku hizi, muziki halisi wa Kiafrika unapitwa na mwangwi wake mzuri ingawaje ni wa kupasua masikio na usiofahamika ukirindima kutoka Marekani. Muziki wa aina hii mara nyingi hauvutii sana lakini unaendelea kusitawi kwa sababu ya mifumo tajiri ya kiuchumi. Mdundo wake mkali na wenye kelele nyingi pengine huakisi mikinzano iliyopo na inayoendela kuongezeka katika jamii za Kiafrika.

*Isimu* ni chanzo kisichofuika cha historia kwani mila huhifadhika katika makumbusho hai ya lugha. Kila lugha huwa na ubalisi wa kisaikolojia na ni fenomena ya kijamii. Msamiati wake ni mithili ya miamba tabaka ambamo matokeo halisi ya historia ya watu hulimbika. Lakini, kwa upande mwingine, ni lugha, yaani 'neni', ambayo inaeleza itikadi na ujumbe wa kitamaduni au kisiasa na ambayo hujenga au hujengua historia na huisuka upya kwa kuunda mawazo na kanuni zinazotawala mwenendo. Baadhi ya dhana zinazohusika haziwezi kutafsirika kwa sababu huwakilisha utamaduni mzima. Kwa mfano, maneno *sanakaya* (Kibambara), na *rakire* (Kimore) hupoteza sehemu kubwa ya maana yake yanapotafsiriwa kijuujuu kwa neno "utani." Hayo ni maneno yanayowakilisha kaida halisi ya Kiafrika iliyomo katika mafungamano kati ya mbari na koo, ambamo 'kutaniana' huwa ni sehemu ndogo tu ya uhusiano mzima. Kadhalika ukweli huo unahusu dhana ya *dyatigui* katika Kibambara ambayo haieleziki kwa dhana sahihi ya 'mwinyi wa nyarubanja', au ya *tengsoba* inayotafsiriwa kama 'mwenye ardhi', ingawa tafsiri hii haitoi maana kamili na hupuza mamlaka ya kidini na ya kisberia ya mtu huyo. Kwa ufupi, kila istilahi ya Kiafrika inapaswa ifikiriwe upya siyo kwa maana ya neno kwa neno tu bali kulingana na dhima kamili iliyopewa kijamii na kihistoria. Kwa hiyo, uhakiki wa kisimu huwa mojawapo ya zana muhimu za wanahistoria.

Pendekezo lililotolewa kuhusu magofu ya Lobi, nchini Burkina Fasso, kwamba yana asili ya Kireno lilikataliwa baada ya kuchunguza njia zinazoclekea huko na kudhihirika kwamba kuta za hayo magofu ni za tarehe za karibuni mno. Kwa upande mwingine, jina la asili la mahali paitwapo *kol na wo*, au 'zizi la ng'ombe wa wageni' lililwaelekeza watafiti kwenye njia sahihi. Lakini mtindo wa vyungu vilivyopatikana katika magofu na kronolojia ya uhamaji katika eneo hilo ilibidi utiwe maanani kabla ya kutambua kwamba wajenzi walikuwa Wakulango. Kaida ya lugha ambayo ni kipengee cha utamaduni isichanganywe kamwe na ukabila au na kipengee cha kibiojolojia cha rangi ya mtu. Huenda lugha ya wapandafarasi wa Kidogomba ambao walivamia nchi za Bonde la Volta katika karne ya kumi na nne imekwishapotea kutokana na kufifishwa na lugha ya wanawake wa Kikusase ambao wapandafarasi hao waliwaoa na kuzaa nao. Zaidi ya hayo, historia ya mbari iliyoselea ya waamili ambao huzianisha jamii kama zina ruwaza maalumu, si ethnografia halisi wala historia halisi, hasa kwa vile mara nyingi historia hiyo lupuza tamaduni za vitu na usambaaji wa kawaida wa bidhaa - kama vile kubadilishana chumvi kwa dhahabu, kola kwa wanyama na mateka kwa bunduki - bidhaa ambazo zilikuwa muhimu sana katika kuunda falme za Afrika Magharibi na ambazo Leroi-Gourhan aliona kuwa ni asili ya ustaarabu.

Kwa hiyo inaonekana kuwa sosiolojia hai lazima iwe mojawapo ya vijenzi vya msingi vya utafiti wa historia ya Afrika. Hili si jambo la kuhamisha tu vigezo vya uchanganuzi kutoka jamii moja kwenda nyingine kulingana na wakati au muda, kwani kwa kufanya hivyo matatizo mengi

yatazuka kuliko kutatulika. Kwa mfano, katika kuhesabu wastani wa urefu wa kipindi alichotawala mfalme, hadhari lazima ifanywe ili kuweka kigezo cha wastani wa kipindi cha sasa kwa kupimia wastani wa karne zilizopita, kwani kiwango cha uthabiti wa kisiasa sio lazima kiwe sawa siku zote. Tena, mila ya kurithisha ufalme - toka ndugu mmoja hadi mwingine - katika ufalme wa Mossi wa Yatenga haiwezi kutoa wastani unaofanana na wastani wa ufalme wa Wagadugu ambako ufalme ulirithishwa kutoka kwa baba hadi kwa mtoto mkubwa wa kiume. Katika mfano huu wa pili muda wa kutawala mfalme ulikuwa mrefu zaidi na idadi ya vizazi kuwa kubwa. Lakini tukiangalia wafalme wa Gan (Gan-Massa) ambao kwa kawaida walichaguliwa miongoni mwa vijana waliokomaa, wastani wa muda wa kutawala huwa mrefu zaidi. Kwa hivyo, mahesabu ya wanahistoria hayawezi kuthibitika bila ya kuelewa wazi sosiolojia ya kisiasa ya nchi inayochunguzwa. Zaidi ya hayo, dhana halisi ya uthabiti haiwezi kuhamishwa kwa jumla kutoka kwenye jamii zisizo za Kiafrika na kupandikizwa kwenye uhalisi wa kihistoria wa bara la Afrika. Huko Ethiopia na katika ufalme wa Wagadugu kuuliwa au kufukuzwa nchini kwa wagombea ufalme kulileta namna fulani ya uthabiti lakini hasara iliyotokana na misukosuko ya muda mrefu haijawahi kupimwa kwa usahihi.

*Sayansi za asili* zilizoanza kwa kutumia kompyuta za kuchambua data fulani za tarakimu, ni sehemu ya mchanganyiko wa taaluma fungamano. Orodha hiyo ya mchango uliotolewa na sayansi kwa utafiti wa kihistoria ni ndefu na hujumuisha mbinu za fizikia, kemia, na biokemia zinazotumika katika kuhesabu umri na kuchambua madini, mimea na chakula na kuchunguza mifugo na urithi wake, pamoja na epidemolojia na utafiti wa mabaa ya asili ambao unafungamana na elimu ya tabia ya hali ya nchi. Katika mila za Afrika, gumba ni tukio la kihistoria kama vilivyo vita. Ni kawaida kwa teknolojia kuhusiana na nafasi ya matumizi ya mabavu kauka historia. Katika Afrika pia, ingawa kwa kiwango kidogo, ujuzi wa teknolojia unewasaidia sana, kwa mfano Waasiria katika Misri, wafalme wa awali wa Ghana ya kale na mfalme Shaka wa Wazulu. Kila inapowezekana, takwimu pia huweza kusaidia kuainisha hali fulani na kutathmini umuhimu wake. Idadi ya watu 10,000 haitakuwa na muundo sawa na ule wa mathalani watu milioni 10. Kadhalika, tunapozungumzia uvamizi wa majeshi ya Kiafrika au majeshi mengine ya karne ya kumi na nne, jambo la kuzingatia hapa ni kwamba majeshi ya zama hizo hayakuwa na uhamasishaji wa aina moja na ule uliopo katika majeshi ya siku hizi.

*Utafiti wa Vita vya Kiafrika* husaidia tu iwapo utafiti huo utahusishwa na maarifa ya jamii zinazohusika. Vita vilikuwa mashindano ya kidini na mapambano ya kiteknolojia pia. Sundiata na Sumaoro Kante walifanyiana uchawi kabla hawajapigana. Wapiganaji walijaza hirizi kwenye mavazi yao ya vita na desturi hii ilifuatwa na askari wa Kiafrika katika Vita Vikuu vya Kwanza na vya Pili.

Pamoja na mgogoro uliotokea kati ya wanasayansi kutokana na kisaasili cha 'Wahamiti', *anthropolojia maumbile* bado inaweza kusaidia ili iradi viashiria vyake vya kibaguzi vinaondolewa na matokeo ya utafiti wa kisosiolojia yanatiliwa maanani. Aina fulani za uumbaji wa mifupa kama ule wa kurefusha fuvu unaofanywa na Wamangbetu, zinahusiana na utamaduni na mtindo wa maisha. Kwa upande mwingine uchanganuzi wa aina za damu umeonyesha kuwa hata makundi ya damu huweza kujinasibisha na mazingira: na hii huonyesha athari kubwa ambayo mazingira huweza kuwa nayo juu ya "jamia" Kama ilivyo kila kitu kilichomo katika upco wa historia, jamia haina budi ihesabiwe kama ni mchanganyiko wa maumbile na utamaduni wa mazingira na kupita kwa wakati.

## Mbinu

Vipi taaluma nyingi namna hiyo zinaweza kutumiwa katika kazi ya kuihuisha kale? Mbinu ya kwanza ni kuunda jumuiya zizizokuwa na mshikamano mkubwa ambamo juhudi za wote wanaohusika zinakusanywa pamoja. Tangu mwanzo shabaha kadha za jumla zinapangwa na baadaye kila mwanachama wa kikundi huangalia enco la tatizo la taaluma yake mwenyewe. Baada ya kupeana taarifa mara kwa mara hatimaye kikundi hukutana pamoja kwa ajili ya kulinganisha matokeo yake. Utaratibu huo hauridhishi sana kwani huendeleza kasoro zote zilizotoo katika kila taaluma pasi kufaidika na matokeo ya mahusiano ya karibu kati yao.

Utaratibu wenye faida zaidi ni ule wa kutumia mbinu ya taaluma fungamano ambamo taaluma mbalimbali zinaunganishwa pamoja kuliko kila moja kuachiwa kufanya kazi peke yake. Mkakati wa jumla wa utafiti na hatua za kiufundi zilizo chambuliwa kwa undani zinapaswa ziainishwe kwa pamoja. Baada ya kuyaainisha masuala ya msingi, kazi inayohusika inagawanywa katika shughuli mahsusi. Matokeo hupitiwa au kulinganishwa kila baada ya kipindi fulani au wakati mwanachama mmojawapo akiomba hivyo ili tatizo liweze kuelezwa upya kutokana na maendeleo yaliyopatikana. Iwapo ni lazima, vikwazo vyovyote vitakavyoonkana vinaweza kushughulikiwa kwa mipango ya dharura ambamo juhudi zote huletwa pamoja. Aina hii ya kazi ya pamoja inaweza kuwa na mkurugenzi mmoja au wengi kwa zamu kutegemea kama hatua iliyofikiwa inamhitaji mwanaisimu, mwanasosiolojia, au mtaalamu wa aina nyingine. Utafiti utakaofanywa kwa kutumia njia hii huenda ukakuza upeo wa kila taaluma, ukasahihisha kasoro zake na kumwongoza mchuguzi kugundua mambo mapya na kufupisha hatua zitakazookoa muda wa utafiti. Hata hivyo, vituo vya utafiti vya Afrika vitapaswa kurekebisha mfumo wa uendeshaji ili ulingane na mkabala wa aina hii. Kadhalika, itawabidi watafiti wenyewe warekebisha mtazamo wao kulingana na mkabala uliopo.

Nini madhumuni ya hayo yote? Jambo linalodhamiriwa ni kuunda upya taswira ya maisha ya kijamii, hata kama si kwa ukamilifu wake wote wa maumbile, basi walau bila ya kuiharibu taswira hii kwa kuisahilisha mno. Maisha ya kijamii hujumuisha vipengee vingi pamoja. Watu hawawi na maisha mahsusi kwa ajili ya kushughulikiwa haja za kimwili, na mengine kwa ajili ya mahusiano ya kijamii na mengine zaidi ya kushughulikia sanaa, falsafa, elimu n.k. Maisha yote haya ya mtu hufumwa pamoja kufanya kitu kimoja kizima. Riwaya kama ya Steinbeck, *Grapes of Wrath*, ya Marlaux, *La Condition humaine* na ya Thomas Mofolo, *Shaka* huonyesha kwa uaminifu mchanganyiko mkubwa kama huo wa vipengee vyote vya maisha. Mwanahistoria anapaswa kufanya kazi ya kuihusisha kale kwa kushirikiana na wanasayansi wengine. Ama kwa hakika ukweli hustaajibisha zaidi kuliko ubunifu. Vilevile hakika ya kihistoria ikisukwa upya na kukamilishwa ili isiwe na mtazamo wa upande mmoja tu wa mambo husisimua zaidi kuliko riwaya. Bila shaka inawezekana kushughulikia kwa undani kipengee kimoja mahsusi na kukieleza kwa kina zaidi katika waraka mmoja mahsusi. Lakini kufanyike hivyo kwa sharti ya kuwa baadaye kipengee hicho kitaingizwa katika mfumo mpana, ambao pia utachanganywa katika picha ya jumla. Matukio makuu ya kihistoria yanatokana na mchanganyiko wa sababu na nguvu ambazo hazina budi kudhihirishwa jinsi zinavyofanya kazi. Kwa mfano, katika kuzungumzia kuenca kwa Wamande; au Wahausa katika Afrika Magharibi, kuna haja ya kuzingatia sababu kama vile teknolojia, nyenzo na vitu vilivyokuwepo, hamu ya kufanya biashara na kupata faida, kujua lugha, jumuiya zinazohusika zilizoundwa kwa misingi ya kisiasa au kiukoo, hamasa ya kidini, n.k. Juhudi za kukuza sababu moja kuu mara nyingi husababisha kujenga kiunzi safi cha nadharia kuliko kuihusisha kale.

Mkabala huo wa kuingiza kila jambo ni wa lazima katika Afrika, kwa sababu, hadi karne ya ishirini, maisha yalikuwa yamefungamana zaidi kuliko kwingincko na migogoro ya kitabaka haikuwa mikubwa. Kuwagawanya watu katika jamii zenye dola au zisizo na dola ambamo dhana ya jamii zisizo na dola hutafsiriwa kufuatana na uzoefu wa Ulaya kutapoteza uhalisi wa mambo ambayo kwayo historia imejengwa. Katika bara la Afrika, hata katika ufalme kama ule wa Mali, kutokuwepo kwa magari na utawala msonge na sera ya makusudi ya viongozi ya kuacha watu washughulikia mambo yao wenyewe kulimaanisha kuwa maisha yao ya vijijini hayakudhibitiwa na dola. Kupuza ukweli huo ni kujifunga katika kujifunza orodha tu ya watawala ambao baadhi yao walijulikana kwa tukio moja au mawili tu ya maana katika utawala ulioendelea kwa miaka kumi na mitano au ishirini, na kuwafanya wawe kielelezo cha jinsi watu walivyoishi zamani hizo. Hata katika jamii ambamo dini ya jadi ilikuwa ndiyo nguvu yake, jamii hizo zilikuwa zimeungana kwa kiwango kilekile kama ambavyo jamii zenye kufuata dini ya Kiislamu zilikuwa zimeungana. Kwa hali yoyote ile jamii hizo hazikuwa za kidunia, na itakuwa ni makosa kuzifikiria hivyo.

Ni kweli kuwa uwekaji mamlaka katika makao makuu pia ulikuwepo katika jamii hizo, lakini huo haujawa wa aina inayoonekana katika dola ya "kisasa", ambamo yaweza kudhaniwa kuwa ndiyo kafara inayotolewa ili kufanyiwa kago - kushurutisha mgawanyo wa kazi katika kila jambo. Kwa mfano, miongoni mwa Wasenufo - pamoja na chama chao cha kisiri yaani Waporo - pia miongoni mwa Walobi (Wadyoro) na Wadyola, mafundo yalikuwa na nafasi muhimu, kwa vile maisha yao ya kijamii yalikusiana sana nayo. Tena, mashirikisho yote ya vijiji yalikuwa yamekitwa katika madhabahu au madhehebu moja, kama vile ilivyokuwa katika eneo la Samo la Burkina Faso na katika nchi ya Waibo huko Nigeria.

Jamii hizo, pamoja na kudhaniwa kuwa na teknolojia kongwe, zilionyesha namna nyingi sana za sanaa ya watu, ambayo ilionekana kwenye zana na vyombo vilivyotumika sana. Hata mitindo ya maumbo ya chale za kimbari ilitimiza kazi mbili: kuashiria utambulisho wa mbari na kutosheleza hamu ya kiumbuji. Kadhalika, sarafu za chuma, au *guinze*, ambazo hapo awali zilitumiwa na watu wengi katika Guinea, Sierra Leone na Liberia, kwa wakati ule ule kama fedha, kinga ya nyumba na ardhi, na mahala pa mapumziko ya mizimu na wahenga. Iwapo tunataka tuzitendea jamii hizo, haki basi jamii kama hizo huhitaji historia itakayojumuisha mambo yote.

## *Kiunzi cha kikronolojia: enzi za mvua na barafuto za Afrika*

### *SEHEMU YA I*

Sura hii inatoa maelezo ya jumla ya baadhi ya mabadiliko yaliyotokea katika maumbile ya Bara la Afrika katika kipindi cha Pleistosini na Holosini au katika enzi ya hivi karibuni. Katika Kipindi hiki cha miaka milioni tatu hivi, tabia ya hali ya nchi na mazingira ya dunia yalibadilikabadihika sana. Mfuatano wa matukio makubwa katika tabia ya hali ya nchi yaliyotokea katika enzi hii yalisababisha latitudo za kaskazini kusogeza au kurudisha nyuma barafuto katika nyakati zilizofuatana, mabonde ya mito na matunganzi yalifanyika na miambo ya sasa ilijitokeza na mabadiliko makubwa ya wanyama na mimea yakatokea. Mame binadamu wa mwanzo kabisa walikuwa wamejitenga na wale wa wazazi wa primata baina ya mwisho wa kipindi cha pliosini na mwanzo wa kipindi cha Pleistosini, na zana za kale sana zilizotambulikana zinapatikana katika peo za kipindi cha mwanzo cha Pleistosini. Kwa kiasi kikubwa, kukua kwa utamaduni tangu binadamu atokee kama mamalia mtumia zana kunaonekana kuwa kuliathiriwa sana na sababu za kimazingira ambazo zilibainisha hatua mbalimbali za enzi hiyo ya Pleistosini.

Wazo kwamba wakati wa matukio mengi ya kipindi cha Pleistosini mabarafuto yalikuwa makubwa sana huko Ulaya kuliko ilivyo sasa limethibitika; na sasa ni dhahiri kwamba matukio haya ya Ulaya ya kuharibika kwa tabia ya hali ya nchi pia yalionekana kwingineko. Kwa mfano uchunguzi uliofanywa Afrika umeonyesha kuwa katika enzi hizo za Pleistosini, bara hili lilipata mabadiliko makubwa sana ya tabia ya hali ya nchi na ijapokuwa mabadiliko hayo hayajahusishwa kikamilifu na matukio ya upande wa kaskazini mwa dunia, yalikuwa, kwa kiasi kikubwa, yamefungamana kwa namna ambayo bado haijafasiriwa.

Matazamio ya kupata kipimo cha wakati cha historia ya baadaye ya dunia yameongezeka sana katika mwongo uliopita. Mipango ya uchimbaji kwenye vilindi vya bahari imetoa maelezo muhimu kuhusu ufanyikaji mfululizo wa matabaka ya miamba katika historia ya baadaye ya dunia. Uchunguzi wa kina wa taaluma fungamano uliofanywa juu ya violezo vilivyotokana na mipango hii ya uchimbaji, maendeleo ya jiofizikia na hasa mitaala ya paleomagnetiki na ukamilifu wa mbinu wa vipimo vya radiometriki - vyote vimechangia katika kipimo thabiti cha wakati kwa kipindi hiki cha baadaye cha historia ya dunia. Kipimo cha wakati cha jiomagnetiki cha miaka milioni tano iliyopita kinaonyesha kuwa uga wa usumaku wa dunia umekuwa ukibadilikabadihika kutoka hali ya kawaida kwenda kinyume chake. Matukio haya yanaingiliwa na vipindi vifupi ambamo kinyume cha ruwaza ya tukio hilo hutokea. Matukio haya ni: (ukianza na la hivi karibuni hadi la mwanzoni), Brunhesi (miaka 700 000 hadi sasa); Matuyama (miaka milioni 2.43 hadi miaka 700 000); Gauss (miaka milioni 3.32 hadi 2.43); Gilbert (miaka milioni 5.4 hadi 3.32).

Kipindi cha magneti cha Gilbert-Gauss kinajipambanua kutokana na kuharibika kwa tabia ya hali ya nchi kunakoonekana mahali pengi duniani. Hiki kipindi cha ubaridi kinawiana na sehemu ya chini ya barafuto ya kale ya bara ya Amerika ya kaskazini, mwanzo wa 'taka zinazoburuzwa na barafuto katika Atlantiki Kaskazini na kutokoa kwa wanyama wa bara baridi katika Ulaya. Kulingana na maandishi kadha ambao wameainisha mipaka ya kipindi cha Pliosini na Pleistosini kuwa mwanzoni mwa kuharibika kwa tabia ya hali ya nchi, hili tukio linadhihirisha mwanzo wa kipindi cha Pleistosini.

Kama ilivyosemwa mwanzoni, sura hii inajaribu kuchungua mabadiliko makubwa yaliyotokea katika Bara la Afrika kutokana na mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi ya kipindi cha Pleistosini. Bara kubwa kama Afrika huwa na mazingira kadha mbalimbali ambayo hayakuathiriwa kwa namna moja na mabadiliko makubwa ya tabia ya hali ya nchi ya kipindi cha Pleistosini. Kwa hivyo, nia ni kuchunguza mabadiliko haya kulingana na maeneo makuu ya tabia ya hali ya nchi za hivi leo katika bara hili. Maeneo haya yanaweza kuainishwa katika mafungu mawili: Kanda ya ikweta na kanda ndogo za ikweta, na kanda za tropiki na kanda ndogo za tropiki.

### *Kanda za ikweta na za karibu na ikweta*

Ukanda wa ikweta leo hii hutanda bonde la Zaire lenye joto na unyevu katika Magharibi ya Afrika na hupambanuliwa kutokana na ngurumo na mabadilikobadiliko madogo ya msimu wa halijoto na unyevu na mvua na ngurumo za mara kwa mara. Ukanda huu umetandwa na misitu minene ya mvua. Ukanda wa karibu na ikweta hutanda sehemu kubwa za katikati ya Afrika. Ukanda huu unapambanuliwa kwa kuwa na tungamohewa la kiikweta wakati wa kiangazi na tungamohewa la tropiki wakati wa baridi. Wakati wa baridi hali ya hewa huwa kavu na yenye ubaridi kidogo tu kuliko kiangazi. Sehemu kubwa ya ukanda huu ni maeneo yenye unyevu mwingi unaosaidia kuota kwa minca ya savana ya tropiki. Hata hivyo, kingo za kaskazini na mashariki husaidia kuota kwa mapululu ya kitropiki.

Kutokana na mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi ya kipindi cha Pleistosini, unyeshaji wa mvua katika kanda hizi ulibadilikobadilika sana; na enzi hii inaweza kugawanywa tena kutokana na mfuatano wa majira ya mvua na majira yasiyo na mvua. Athari za mvua hizi hudhihirishwa na kupanuka kwa mipaka ya misitu ya mvua, katika miundotope mikubwa, mashapo ya maziwa kwenye nyanda za juu na fuo zilizomezwa na maji ya maziwa yaliyopanuka. Majira yasiyo na mvua yalibainishwa na kuongezeka kwa upepo ambapo mchanga ulipeperushwa kusini ya mipaka ya chini ya matutamchanga na ambapo mabadiliko katika minca yalitokea. Mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi ya wakati wa Pleistosini pia yalileta mabadilikobadiliko katika halijoto za kanda hizi. Kutokana na mabadilikobadiliko hayo vile kadha vya milima huonyesha kuwako kwa barafuto katika nyanda za chini kuliko kwenye mpaka wa theluji ya kudumu uhivyo hivi leo.

Enco mashuhuri la akiolojia la Bonde la Olduvai lililoko Tanzania kaskazini na ambalo lina masalia ya homonidi wa zamani sana linaonyesha mfululizo wa mvua kubwa iliyochanganyikana na vipindi vya ukame katika muda wa miaka milioni tatu iliyopita. Katika sehemu liyo, mfuatano wa tabaka miamba, unonyesha mfululizo wa mabadiliko ya shoka la mkono, tangu yale ya awali kabisa hadi ya kazi maalumu ya mwanzo wa kipindi cha Paleolithi, kama inavyojulikana katika Ulaya na Asia Magharibi.

Ushahidi wa kuwako mabadilikobadiliko ya zamani ya tabia ya hali ya nchi katika Afrika Mashariki kimsingi unatokana na kuwapo kwa fuo zilizoimuka na mashapo ya visukuku vya inaziwa kwenye kingo za maziwa mengi ya enco hili. Ziwa Tana, chanzo cha Blue Nile, lina fuo kuu tano, wa juu kabisa ukiwa mita 125 juu ya usawa wa hivi sasa wa ziwa.

Maziwa manne ya Bonde la Ufa (Zawi, Abyata, Longana na Shala) yalikuwa juu kabisa wakati uliopita, hivyo kwamba inawezekana kuwa kingo zake zilifurika na kufanya maji yake kuwa utando mmoja.

Inaelekea Ziwa Viktoria, lilikuwa chini wala halikuwa na mlango wa kutolea maji kwa muda usiojulikana kabla ya miaka 14500 kabla ya sasa, wakati ambapo mimea ya mbuga za savana ilikuwako. Maji ya ziwa hili yalianza kuongezeka katika miaka -12000 kabla ya sasa; wakati ambapo misitu ilianza kutokea kwenye pambizo za kaskazini mwa ziwa lakini yawezekana kwa muda mfupi yapata miaka 10000 kabla ya sasa usawa wa ziwa ulishuka hadi kufikia mita 12 chini ya usawa wa sasa. Ziwa Victoria lilikuwa limejaa baina ya miaka -9,500 na -6500 kabla ya sasa na lilikuwa na msitu usiopukutika karibu na fuo zake. Mlango wa kutokea maji kuingia mto Nile unaonekana ulianza miaka 12000 kabla ya sasa na umekuwako tangu wakati huo isipokuwa kwa muda mfupi karibu miaka -10500 kabla ya sasa.

Historia za maziwa ya Turkana (Rudolf), Nakuru, Naivasha na Magadi katika kipindi cha Pleistosini kwa kiasi kikubwa zinafanana. Ziwa Turkana, lenye eneo la kilomita za mraba 7,500 ndilo ziwa kubwa kabisa katika maziwa yaliyokuwa na milongo ya kutokea maji katika Afrika Mashariki. Likiwa katika kanda ya chini inayopinda na iliyopakana na Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, ziwa hili hupata maji yake kutoka Mto Omo ambao chanzo chake ni nyanda za juu za magharibi ya Ethiopia. Vitalu vya kale vya mwambao, vya delta na vya mito vya ziwa hili ni vya mita 60 juu zaidi kuliko usawa wa hivi sasa na ni vya miaka 130000 kabla ya sasa. Baina ya wakati huo na miaka 9500 kabla ya sasa, ziwa lilikuwa dogo kuliko lilivyo sasa na tabia ya hali ya nchi ilikuwa kavu zaidi. Kuanzia miaka 9500 kabla ya sasa, ziwa lilijaa tena na kubadilikabadilika baina ya mita 60 na 80 juu ya usawa wake wa sasa hadi miaka 7500 kabla ya sasa ambapo Ziwa Turkana lilinywea na kuwa dogo. Hii ilifuatwa na kuongezeka kwa usawa wake mnamo miaka ya 6000 kabla ya sasa, ziwa hili lilipungua na kuwa kama lilivyo sasa.

Katika ukanda wa karibu na ikweta kuna dalili za kutosha za kuonyesha kuwa mimea ya mbugani iliyokuwako kwa wingi katika vipindi vya mvua nyingi ilibadilika na kuwa mapululu katika vipindi visivyokuwa na mvua. Bonde la Chad ni mfano mzuri wa mabadiliko ya maumbile yaliyotokea katika ukanda huu. Ziwa la sasa ni masalia ya bahari ya kale ya ndani ya bara ambayo karibu miaka 130 000 kabla ya sasa ilikuwa kubwa mara kumi na sita zaidi kuliko ziwa lilivyo sasa, usawa wa maji yake ulikuwa mita 40 - 50 zaidi ya usawa wa sasa. Mbuga za savana zilitanda karibu na ziwa. Kipindi cha ukavu kilifuata awamu hii ya mwanzo kukiwa na matuta ya mchanga katika kingo zilizokuwa wazi kililokuwa lilinywea. Kipindi hiki kilindelea hadi miaka 12,000 kabla ya sasa wakati ambapo ziwa hili lilianza kuongezeka tena mpaka likafikia usawa wa mita 12 zaidi kuliko usawa wa hivi sasa. Ziwa lilianza kunywea hadi kufikia ukubwa wake wa sasa yapata miaka 4000 kabla ya sasa.

Mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi ya kipindi cha Pleistosini pia yalifanya halijoto ibadilikebadilike na kusababisha milima kadhaa kuwa na barafuto au mipaka ya theluji kuwa chini zaidi. Isipokuwa Milima ya Atlas, nyanda zote za juu zenye barafuto ziko Afrika Mashariki karibu na ikweta. Mlima Kenya (wenye urefu wa mita 5199) kwa sasa una mpaka wa theluji ya kudumu katika mita 4,600, lakini mpaka wa juu kabisa wa Pleistosini unakisiwa kuwa ulikuwa mita 900. Mlima Kilimanjaro (wenye urefu wa mita 5895) na Mlima Elgon (wenye urefu wa mita 4321) ipo juu ya mpaka wa theluji ya kudumu wa kitabia ya hali ya nchi lakini katika kipindi cha Pleistosini milima yote miwili ilikuwa na mpaka wa theluji wa kudumu wa takriban mita 1300. Mlima Ruwenzori (wenye urefu wa mita 5109) una mpaka wa theluji ya kudumu kwenye mita 4750 kwa upande wa Magharibi na mita 4,575 kwa upande wa Mashariki (Uganda). Barafuto za Pleistosini zilitanda kufikia mita 2900 kwa upande wa magharibi na mita 2000 kwa upande wa mashariki.

Ushahidi unatufanya tusadiki kuwa kanda za Ikweta na za karibu na Ikweta za Afrika zilipitia vipindi vya ubaridi angalau mara mbili katika kipindi cha Pleistosini na kwamba halijoto



ilikuwa ya ubaridi zaidi katika kipindi cha mwisho ambacho kilifanana na kipindi cha mwisho cha barafuto katika Ulaya na Amerika Kaskazini.

### *Kanda za tropiki na za karibu na tropiki*

Uanda wa sasa za tropiki katika Afrika hupata pepo za matlai na mabadilikobadiliko ya msimu ya halijoto ya hewa. Upande wa magharibi wa ukanda huu ambao upo katika pwani ya atlantiki, hupata pepo za msimu, halijoto ya baridi, unyevu hewa mkubwa na karibu hauna mvua. Sehemu nyingine iliyobaki ya ukanda huu imo kauka majangwa makuu ya kaskazini na kusini mwa bara hili. Haya ni maeneo makavu yenye joto na hali ya hewa inayobadilika kila siku. Ukanda wa karibu na tropiki hutanda kingo za kaskazini na kusini za bara hili na hubainishwa na kuwepo kwa tungamohewa za Tropiki wakati wa kiangazi na tungamohewa ya wastani wakati wa majira ya baridi. Halijoto na mvua za msimu hutofautiana sana. Sehemu zilizo na tabia ya hali ya nchi ya Kimediterania huwa na hali ya hewa tulivu na angavu katika majira ya kiangazi na huonyesha mvua katika majira ya baridi.

Jangwa la Sahara pengine ndilo umbile linalojitokeza sana katika ukanda huu. Likiwa na urefu wa zaidi ya kilomita 5500 kutoka Bahari ya Shamu hadi Bahari ya Atlantiki na upana wa wastani wa kilomita 1700 kuanzia kaskazini hadi kusini, jangwa hili linatanda karibu robo ya bara lote la Afrika. Katika eneo hili mvua hainyeshi kwa kiwango sawa kwenye sehemu zote, na ingawa katika sehemu nyingine kiwango cha mvua hufikia milimita 100 kwa mwaka, lakini kwa wastani kiwango huwa ni kidogo zaidi kuliko hicho. Kutokana na hali hii hakuna mito ya kudumu katika jangwa la Sahara isipokuwa Mto Nili ambao hupata maji yake kutoka sehemu za mbali zaidi nje ya jangwa. Madimbwi ya muda na ya kudumu yanayotokana na mtiririko wa maji yana athari sawa kwa maisha siku hizi kama visima na chemchemi.

Uchunguzi mkubwa umefanywa na wataalamu wa jolojia na wa akiolojia kuhusu migawanyiko ya stratigrafia ya tabia ya hali ya nchi ya Sahara hasa katika Algeria, Tibesti na Misri. Wote wanakubaliana kwamba Sahara ilianza kuwa kame katika majilio ya kipindi cha Pleistosini na kwamba tangu wakati huo ilipata vipindi kadha vya mvua. Wakati wa vipindi hivi tope katika mabonde lilitokea mahali kwingi na binadamu na wanyama wakubwa katika Afrika Mashariki na Kati na sehemu za Ethiopia, walijitokeza katika sehemu ambazo sasa hazikaliki. Inawezekana kuhusisha mabadiliko haya ya tabia ya hali ya kipindi cha Pleistosini na namna ya mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi ya hivi karibuni. Inaweza kuchukuliwa kwamba kusogea kaskazini nyuzi 15 za latitudo kwa kanda za tabia ya hali ya nchi, kungeweza kuongeza mvua mahali pengi katika jangwa na hivyo kuleta tabia ya hali ya nchi inayofanana na ile ya kipindi cha mvua cha Pleistosini. Angalau vipindi vitano vya mvua vimebainishwa katika Sahara. Vipindi, hivi, kuanzia cha zamani hadi cha sasa ni:

1. *Mvua za awali za kipindi cha mwanzo cha Pleistosini:* Mvua hizi zililimbikiza mashapo ya changarawe, mchanga na vikorokoro vingine vingi vyenye rangi ya waridi vilivyolimbikizwa juu ya miamba ya zamani. Kipindi hiki cha mvua kilitokea katikati ya kipindi cha ukavu mkubwa sana wakati ambapo Sahara lilikuwa ni jangwa halisi, Mto Nile ukakauka au ukawa na maji kidogo tu.
2. *Mvua za kipindi cha mwisho za kipindi cha mwanzo wa Pleistosini:* Katika kipindi luki mvua hizi zilisababisha ulikaji mkubwa kikemikali pamoja na kulimbikizwa kwa mchanga na changarawc. Labda hiki ndicho kipindi kikubwa cha mvua katika Sahara. Hakuna vifaa vya kiakiolojia vinavyolusishwa nacho.

3. *Mvua za kipindi cha kati cha Pleistosini:* Mvua hizi zilitokea wakati wa Asheuli na kulimbikiza changarawe, mchanga na udongo. Chemchemi zilitokea katika sehemu nyingi na maziwa mengi ya ndani ya bara yalitokea. Binadamu na wanyama wakubwa wengi wa Afrika ya Kati na Ethiopia walitembea sana katika Sahara. Mimba ya Savana ilitanda katika sehemu nyingi. Muda wa kipindi hiki haujulikani lakini huenda ulikuwa wa miaka 200,000.
4. *Mvua za kipindi cha mwisho cha Pleistosini:* Kipindi hiki kilikuwa na peo mbili na kilitokea nyakati za Mosteri na Ateri. Mafuriko ya barafuto yalitokea kwa wingi na ndiyo yalisababisha sura ya sasa ya ardhi. Chemchemi zilikuwako na binadamu walijitokeza jangwani. Muda wa kipindi hiki haujulikani lakini huenda ulikuwa wa miaka 50,000.
5. *Mvua za kipindi cha Holosini:* Mvua hizi zilizotokea mwisho wa kipindi cha Plaeothi na Neolithi zilisababisha mteremko na maziwa ya muda mfupi. Muda wa kipindi hiki cha mvua haujulikani lakini huenda ulikuwa wa miaka 7,000 na kumalizika mwanzoni mwa ustaarabu wa Mafarao.


## SEHEMU YA II

Miaka milioni chache ya historia ya dunia yetu imekuwa na ruwaza na mabadilikobadiliko makubwa ya tabia ya hali ya nchi. Kaida muhimu sana katika muktadha huu na ambayo imefanyiwa utafiti wa kina kwa muda wa zaidi ya karne ni kupanuka na kupungua kusikokuwa kwa kawaida kwa barafuto katika latitudo na miihuko ya juu. Kupungua na kupanuka huku kulisababishwa na barafuto ambayo ilikuwa na athari kubwa kwa mazingira na kwa maisha ya hominidi. Katika Afrika, jambo la kuvutia sana katika mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi ya miaka ya karibuni lilikuwa ni kuenca kwa mabonde ya maziwa katika maeneo ambayo sasa ni makavu na kutokoa kwa maeneo makubwa ya matuta ya mchanga katika sehemu ambazo sasa zina tabia ya hali ya nchi yenye unyevu zaidi.

Katika miaka ishirini iliyopita maendeleo makubwa yamekwishapatikana katika kukadiria umri wa matukio ya tabia ya hali ya nchi na matumizi ya namna iliyo wazi ya kaboni-14. Kwa vipindi vya kale zaidi ukadiriaji wa umri kwa ugeuzi wa sumaku uliotokana na vipimo vya kiradiomita, kwa kutumia mbinu ya kali-agoni, huwezesha kuthibitisha uwiano na maeneo mengine ya mbali ambapo mbinu hizo zinatumika pia hasa katika maeneo ya bahari kwa miaka milioni kadha.

Kabla ya mbinu hizi za uwiano wa kikronolojia hazijaanza kutumika, stratigrafia ya miaka ya karibuni ilikitwa, kwa kiasi kikubwa, katika mfuatano wa matukio ya tabia ya hali ya nchi uliochukuliwa kama kiunzi cha kikronolojia. Uwiano kutoka eneo moja hadi jingine ulidhihirika kutokana na enzi zilizofuatana zenye tabia ya hali ya nchi zilizofanana: Kwa mfano, ilipendekezwa pasi na kutumia kigezo chochote kufananiha vipindi vya barafuto vya Ulaya na vipindi vya mvua vya Afrika. Hata hivyo, wazo hili lilipingwa sana na waandishi wengi.

Tatizo la uwiano limekuwa changamano zaidi kuliko ilivyodhaniwa awali na tumcanza kufikia ufumbuzi kwa kuwa sasa ufanyaji kazi wa elimu ya tabia ya hali ya nchi ya dunia umefahamika vizuri zaidi na mpangilio wa kiwakati wa tabia ya hali ya nchi kwa miaka elfu chache iliyopita umethibitishwa kwa utondoti. Zaidi ya hayo, sifa fulani za uga wa usumaku, kama vile mteremko na ukali, zaelekea huhusiana sana na tabia ya hali ya nchi.



16.1 Grafu zinazoonyesha analogia kati ya halijoto zilizoonyeshwa na wanyama wadogo na mwelekeo wa kisumaku katika miaka milioni mbili iliyopita (Wallin na wenzake, 1947)

### *Barafuto za kwatenari (miaka ya karibuni) na ukadiriaji wa umri*

Inawezekana kuwa karibu vipindi 12 vya mabadiliko makubwa ya ubaridi vimeonekana katika mfululizo wa mlimbikizo wa mashapo chini ya bahari wakati wa kipindi cha miaka ya karibuni. Karibu vipindi 8 tu vimedhihirika katika mashapo ya bara huko Ulaya Kaskazini. Matungazi ya mito na mashapo ya barafuto ya eneo la Alpine yanahusiana na barafuto 4 (au 6), zinazotambulikana kwa jumla: Gunz, Mindel, Riss, Wurm (na Donau, Biber), na kila moja ikiwa na hatua kadhaa.

Ushahidi wa bara unaoonekana hapa na pale tu mara nyingi hudanganya na hufanya iwe vigumu kuwianisha vipindi vya barafuto katika maeneo ya mbali inapokuwa hayathibitiki kwa kipimo cha magnetokronolojia au radiomita. Kwa hakika kronolojia inayotumika hivi sasa kwa barafuto za Alpine si wazi sana na istilahi kama Gunz, Mindel, Riss, Wurm na Biber zimetumika katika maeneo mbalimbali zikiwakilisha maumbo ambayo hayakutokea wakati mmoja.

Kuhitilafiana huku kunafanya iwe hatari kujaribu kuwianisha ushahidi wa barafuto za Alpine na mfululizo ya mabadiliko ya ubaridi katika viini vya bahari. Kila barafuto ilisababisha kurudi kwa bahari kwa karibu mita 100. Matokeo ya baadaye ya kupanuka kwa bahari kulikosababishwa na myeyuko wa barafu kunafanya iwe rahisi kuhusisha tarihi ya tabia ya hali ya nchi na stratigrafia na tarihi ya mizunguko ya bahari kuka maeneo ya pwani.

Kukiwa na uwezekano wa kufanya makosa kwa njia hizi mbalimbali zilizotumiwa kutia tarehe ya matukio kwa kutumia radiomita, imeonekana kuwa huu usawa mkuu wa bahari unawiana vizuri na vipindi vya halijoto ya juu vinavyodhihirika katika wanyama wadogo wa baharini, chavua, isotopi ya oksijeni na kemikali (takriban miaka 200 000; 124 000; 105 000; 85 000 kabla ya sasa).

### *Ufanyaji kazi wa elimu ya tabia ya hali ya nchi ya dunia*

Ujuzi juu ya ufanyaji kazi changamano wa mzunguko wa angahewa na bahari na uhusiano wake na tabia ya hali ya nchi vimedhihirisha kuwa tabia ya hali ya nchi sio tu kuonyesha uwiano wa kikronolojia. Zaidi ya hayo, mabadiliko mbalimbali ya baadhi ya vipengee vya tabia ya hali ya nchi katika miaka 25000 hivi iliyopita na ambayo umri umekadiriwa kwa usahihi yanaonyesha kasi kubwa ya mabadiliko makuu yaliyotokea, hata kwa kutumia kipimawakati hiki.

Mfumo wa tabia ya hali ya nchi, kama ilivyofafanuliwa na National Academy of Sciences ya Washington (1975) umeundwa na tabia na miendeleo ya tabia ya hali ya nchi na mabadiliko yake: halijoto, maji, barafu na udongo; tabia za mijongee ya upepo, mikondo ya bahari, mijongee ya barafu na kadhalika; tabia ya uoevu kama vile unyevu wa hewa, mawingu na maji yaliyo juu ya uso wa ardhi, maji yaliyo chini ya ardhi na barafu, tabia tuli kama vile kanieneo na uzito wa angahewa na bahari, uchumvichumvi na kadhalika; mipaka ya kijiometri ina viwango visivyobadilika vya mifumo. Mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi ni changamano zaidi kwa kuwa yawezekana kukawa na mwingiliano baina ya vipengee vya mfumo wa tabia ya hali ya nchi. Bahari pia huchukua nafasi muhimu sana kwa njia ya miendeleo kwenye mwingiliano baina ya maji na hewa ambao hutawala mabadilishano ya joto, unyevu na nishati.

Stratigrafia ya tabia ya hali ya nchi ya miaka ya karibuni inelazimika kuwa ya kukisiwa lakini polepole inapitiwa na majaribio ya kuelewa ufanyaji kazi unaohusika katika hali maalum katika vipindi mbalimbali vya nyakati.

## *Elimu ya tabia ya hali ya nchi ya Afrika ya leo na ya zama za karibuni*

Katika Afrika, mfuatano wa mabadiliko ya misimu ya kiangazi na masika katika kanda za kati ya tropiki unafungamana na msogeo wa eneo la kutanio la pepo za msimu [*Intertropical Convergence Zone (ITCZ)*]. Kama ilivyoelezwa hivi karibuni na J. Maley (1973) na L. Dorize (1974), eneo la kutanio la pepo za msimu (ITCZ) linawakilisha mahali ambapo pepo za monsuni (hewa yenye unyevu inayotoka sehemu za ikweta au pepo za bahari zinazotoka katika kizio cha kusini cha dunia) na harmattan (pepo kavu zinazotoka Sahara) zinapokutania. Kutanio hili (ITCZ) liko karibu magharibi-mashariki na husogea kutoka kusini katika miezi miwili ya msimu wa joto, halafu husogea kutoka kaskazini hadi kusini. Mbembeo huu wa misimu hutokoa baina ya 4° kaskazini na 20° - 23° kaskazini. Eneo la mwachano baina ya hewa yenye unyevu na hewa kavu huongezeka polepole kutoka kaskazini hadi kusini. Tabaka la monsuni lenye unyevu hewa ni pembe ya baridi iliyo nyembamba sana karibu na kaskazini wakati wa majira ya joto na hutoa mvua kidogo tu; unene wake lazima ufikie mita 1200 au hata mita 1500 ili mvua yoyote yenye kuhesabika iweze kutokoa. Zaidi ya hayo, mahali pa kutanio la pepo za msimu hubadilika sana, sio tu kutoka msimu mmoja hadi mwingine bali pia kutoka siku hadi nyingine kutokana na kanieneo ya uwanda wote wa Afrika na Bahari ya Atlantiki. Jangwa la hivi karibuni la tabia ya hali ya nchi lililotokea Saheli lilitokana na ukweli kwamba kutanio la pepo za msimu lilibakia kati ya 3° na 4° kusini zaidi kuliko mahali pake pa wastani. Kwa upande mwingine, katika mwongo wa masika baina ya 1950 na 1959, jangwa la Sahara lilinyewa.

Kadri hewa ya ncha ya dunia inavyozidi kuwa na nguvu ndivyo pepo za ncha ya dunia zinavyozidi kuwa na nguvu na kutambaa kuelekea ikweta. Kuhusu jambo hili, Maley (1973) alitofautisha ufanyaji kazi wa namna mbili, mmoja ukihusu kipindi kilichopo leo hii. Wakati wa vipindi vya barafuto maeneo ya barafuto katika kizio cha kaskazini cha dunia yaliongezeka sana wakati ambapo barafuto ya Antaktiki inaonekana kuwa ilibadilika kidogo sana. Pepo za ncha ya dunia ya kaskazini wakati huo zilikuwa na athari kubwa na zilisukuma pepo za monsuni kusini kabisa wakati wa msimu wa joto. Kuongezeka kwa ukame na kutanda kwa barafuto vilikwenda sambamba. Kutokana na halijoto zenye joto zaidi za kipindi cha Holosini kabla ya miaka 5000 au 4000 kabla ya sasa, nguvu za pepo za ncha ya dunia zilipungua. Katika msimu wa jua kali wa kaskazini, kusogea nyuma kwa pepo za ncha ya dunia ya kaskazini kulisaidia katika kuenea kwa pepo za monsuni kaskazini mwa ikweta wakati ambapo pepo za ncha ya dunia za kusini zilisaidia kuelekeza ikweta vitanguakimbunga vya tropiki ndogo. Katika msimu wa baridi wa kaskazini pepo za ncha ya dunia zingeweza tena kuenea athari zake juu ya Sahara na kuleta mvua. Kutokoa kwa mvua katika msimu wa joto na ule wa baridi kunaeleza sababu za kuwako tabia ya hali ya nehi ya unyevu kusini mwa Sahara na kurudi nyuma kwa jangwa hili katika nusu ya kwanza ya kipindi cha Holosini.

Zaidi ya miaka 5000 iliyopita, kurudi nyuma kwa barafuto ya Aktiki kumepunguza nguvu za pepo za ncha ya dunia ya kaskazini wakati ambapo nguvu za pepo za Antaktiki pia zimepungua. Kupungua kwa mvumo wa pepo za monsuni pamoja na kupungua kwa athari za pepo za ncha ya dunia ya kaskazini katika Sahara kunaweza kueleza sababu za kukauka polepole kwa Sahara. Njia hizi za mitorolojia zinaweza kutusaidia kuelewa mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi yaliyotokoa Afrika katika kipindi cha Kwatenari (yaani cha kurudi nyuma hadi kama miaka milioni mbili iliyopita).

### *Ukadiriaji umri na tabia za hali ya nchi katika miaka 25 000 iliyopita*

Miaka 25 000 iliyopita ya enzi ya Kwatenari (mwisho wa kipindi cha Pleistosini na Holosini) inatoa mfano wa hivi karibuni wa msogeo mkubwa mbele wa barafuto uliofuatwa na kurudi

nyuma kwake hadi kufikia kipindi cha sasa cha kati ya barafuto. Katika kipindi hiki, maeneo ya katikati ya tropiki yalipata ukame mkubwa, ikifuatwa na awamu ya unyevu halafu ukafuata ukame mwingine tena. Haya ndiyo mabadilikobadiliko ya tabia ya hali ya nchi ambayo yanaweza kufanyiwa uchunguzi katika muda wa karne kadha au milenia kadha na ambao huwezesha kulinganisha misingi ya mfumo wa vipengee vya tabia ya hali ya nchi na mabadiliko yake, katika maeneo mengi ya ulimwengu yaliyoko karibu katika latitudo zote. Katika kipindi hiki pia, maelezo yanayopatikana kutokana na uchunguzi uliofanyiwa chavua, mbelewelw na wanyama wanaofanana na spishi za kisasa unatuwezesha kuadidisha ukubwa wa mabadiliko ya mazingira ya kijiografia kwa usahihi.

Miaka 25 000 hadi 18 000 kabla ya sasa

#### *Latitudo za Juu*

Kipindi kati ya miaka 25000 na 18000 kabla ya sasa kinawiana na mwisho wa upeo wa juu wa kuenea kwa barafuto katika kizio cha kaskazini. Wakati wa mwisho wa kuenea kwa barafuto ya Wurm (Wisconsin-Weichselien-Valdai), barafu ilisambaa juu ya eneo linalowakilisha asilimia 90 hadi 95 ya ile lililofunikwa na barafuto katika vipindi vyote vya enzi ya miaka ya hivi karibuni (Flint, 1971). Hivyo, huu ni mfano wakilishi wa barafuto.

#### *Bahari Kuu*

Kupunguka kwa maeneo huru kulikosababishwa na barafu ya baharini na kushuka kwa usawa wa bahari kutoka karibu mita - 50 hadi - 100 pamoja vilipunguza zaidi eneo la bahari kuu kwa asilimi 10 hivi. Mwishoni mwa kipindi hiki visimbwi vilikwishaanza kutokea.


Katika vizio vyote viwili, uhamaji wa maji katika ncha za dunia ulikuwa ni tukio kubwa katika enzi hii ya barafuto. Kaskazini mwa Atlantiki, maji katika ncha ya dunia yalienenwa hadi kufikia latitudo ya 42 (kutoka mahali karibu na pale ilipo sasa, kama digrii 60 kaskazini) na hivyo kusababisha kuongezeka kwa joto kali kusini mwa latitudo ya 42 ambayo pengine ilikuwa ni mhimili wa pepo za magharibi katika enzi ya barafuto. Kusini mwa latitudo hii, mabadiliko yalikuwa karibu sawa na yale yaliyopo sasa, lakini mistari ainishijoto iliyopindika kuelekea upande wa pwani ya Afrika inaonyesha kuwako kwa maji baridi, kutokana na mawimbi makali, hasa wakati wa majira ya baridi (Gardner na Hays, 1975).

Pepo za ncha ya dunia na mhimili wa pepo za magharibi ulisogea zaidi ya kilomita 2000 kuelekea ikweta katika Atlantiki ya kaskazini na kilomita 600 tu katika Atlantiki ya kusini. Katika Bahari Kuu ya Pasifiki pepo za ncha ya dunia zinaonekana zilisogea kidogo sana wakati wa vipindi vya barafuto. Hii inaeleza sababu za kupunguka kwa mpenyo wa pepo za monsuni juu ya Sahara na hali ya ukame ya eneo la Saheli mwishoni mwa wa kipindi cha barafuto.

#### *Afrika*

Kusini mwa Sahara na katika maeneo ya Saheli, mabadiliko ya jumla ya tabia ya hali ya nchi katika miaka 25000 iliyopita yanaonyesha mtindo wa aina moja kutoka pwani za Atlantiki hadi Bahari ya Sham. Kipindi hiki hujumuisha mwisho wa kipindi cha joto cha Pleistosini ya juu (kilichokuwako kwa muda wa miaka 30000 hadi 20000 kabla ya sasa) na mwanzo wa kipindi cha ukame kilichomalizika miaka 12000 hivi kabla ya sasa.

Uchunguzi wa mashapo ya maziwa katika bonde la Chad unconysha kuwa uhusiano baina ya kutua maji na mnyweo ulikuwa unatosha kuwezesha maziwa makubwa kuendelea kuwapo



16.2 Ramani ionyeshayo isothemu za maji ya nchi kavu katika Februari 18 000 kabla ya sasa. Isothemu zilizoonyeshwa kwa mistari ni za kufasiri. Maeneo makuu ya matungamo-barafu makuu yameonyeshwa kwa vistari sambamba, mabonge ya barafu ya kudumu yameonyeshwa kwa mipaka ya alama-chembechembe. Ufuo wa barafuto umechorwa kulingana na usawa wa bahari - m85 kutoka ilivyo leo (McIntyre na wenzake. 1975 kur. 75 + 80).

kati ya miaka 40 000 na 20 000 kabla ya sasa. Kwa muda wa milenia nane zilizofuata, eneo la ukame liliendelea kupanuka hadi kufikia kilomita 400 ya mipaka yake ya sasa ya kusini.

Mabadiliko haya kutoka kipindi cha maziwa hadi kipindi cha ukame mkubwa yanaonekana pia katika mashapo ya maziwa ya Afar, ambapo F. Gasse alionyesha kuwako kwa vipindi vitatu vya maziwa katika kipindi cha Pleistosini ya nyuma. Baina ya miaka 20,000 na 17,000 kabla ya sasa, mazingira ya maziwani yaliharibika na kitalu kilichokauka cha Lake Abay kiliota gramina (*gramineae*) yaani moto wa nyasinyasi.

Miaka 18 000 hadi 12 000 kabla ya sasa

#### *Latitudo za juu*

Katika maeneo ya latitudo za juu kipindi hiki kinalingana na kile cha mwisho wa upeo wa juu wa barafuto na mwanzo kwa kuyeyuka kwa barafuto. Utando barafu uliofunika Mashariki ya Amerika Kaskazini na nchi ya Skandinavia ulikuwa katika upeo wake wa juu baina ya miaka 22000 na 18 000 kabla ya sasa na ukaanza kuyeyuka mara tu baada ya wakati huo. Hata hivyo, utando barafu wa safu ya milima katika Amerika Kaskazini ulifikia upeo wake miaka 14 000 tu kabla ya sasa na ukayeyuka karibu miaka 10 000 kabla ya sasa. Kwa hivyo, myeyuko wa jumla ulianza miaka 14 000 kabla ya sasa. Kwa upande mwingine katika kizio cha dunia cha kusini utando barafu wa bara katika mashariki ya Antaktiki unaonekana kuwa ulibadilika kidogo ambapo ule katika magharibi ya Antaktiki na tako lake likiwa chini ya usawa wa bahari, inaonekana ulididimia sana.

#### *Bahari Kuu*

Maeneo makubwa yaliyofunikwa na barafu ya bahari, kwa hakika yalitoweka kutokana na kupanda haraka sana kwa usawa wa bahari baada ya myeyuko wa barafuto. Wastani wa kima cha kupanda ulikuwa mita 1.5 katika kila karne baina ya miaka 15000 na 12000 kabla ya sasa, kufikia wakati huo nusu, kama si theluthi mbili, ya kupanda kulitokea. Wakati huohuo, maji ya Atlantiki ya ncha ya dunia yalirudi katika latitudo za kaskazini zaidi.

#### *Afrika*

Tukio ambalo limcwekewa kumbukumbu vizuri zaidi ni lile la ukame mkubwa wa kipindi baina ya miaka 18 000 na 12 000 kabla ya sasa, lililoathiri schemu kubwa ya Afrika kama inavyodhihirishwa na grafu zionyesha mabadiliko ya kiwango cha maji katika maziwa Niger, Chad, Afar, Sudani na kadhalika. Kutoweka kwa mimea kulifanya pepo zisukume mbele matuta ya mchanga kutoka kilomita 400 hadi 800 katika uelekeo wa ikweta na katika visimbwi vilivyojitokeza katika bara hili. Hapana shaka kwamba katika vikwi (milenia) kadhaa, Jangwa la Sahara, lilivyoenea lilikuwa kipingamizi kikubwa kwa binadamu kuliko ilivyo sasa. Ukame huu waonekana kuwa ulikuwa wa jumla na kuna dalili kuwa kanda zilizo kati ya tropiki kwa jumla zilikauka kwa kiasi fulani katika Afrika, Asia - hasa India - na katika kizio cha dunia cha kusini.

#### *Bonde la Mediterania*

Ingawa mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi wakati wa barafuto ya mwisho (yapata miaka 100000 iliyopita) yanaonekana kuwa yanatanisha, katika Bonde la Mediterania, ugunduzi wa kipalinolojia na kipedolojia unaonyesha kuwa katika upeo wa barafuto tabia ya hali ya nchi ilikuwa ya ukavu na pia ya ubaridi. Mapululu yalienea katika kanda ya Mediterania baina ya miaka 16 000 na 13 000 kabla ya sasa, na utando wa chokaa ulitokea juu ya udongo.



## Miaka 12 000 kabla ya sasa hadi leo

### *Latitudo ya juu*

Kipindi hiki kinabainishwa na mwisho wa barafuto na ongozoko dhahiri la halijoto lililofikia kilele chake baina ya miaka 7500 na 4500 kabla ya sasa (upeo wa tabia ya hali ya nchi ambao mpaka sasa unajulikana huko Ulaya kama kipindi cha Atlantiki). Utando barafu wa mlima wa Cordillera uliicyuka haraka sana na kutoweka yapata miaka 10 000 kabla ya sasa. Ule wa Skandinavia ulitoweka muda mfupi baadaye (miaka 9000 kabla ya sasa). Mabadilikobadiliko dhahiri ya haraka ya karibu kila baada ya miaka 25 000 yameonekana kama ilivyo katika upoaji wa Dryars mpya haina ya miaka 10800 na 10 100 kabla ya sasa.

Hali ya barafuto ilianza kulinganishwa na ile ya wakati wetu huko Ulaya ya Kaskazini yapata miaka 8500 kabla ya sasa na katika Amerika Kaskazini, yapata miaka 7000 kabla ya sasa. Katika wakati huo, pia, utando barafu katika magharibi mwa Antaktiki ulirudi nyuma.

### *Bahari Kuu*

Kupanda kwa usawa wa bahari, ambako kunaonyesha kuyeyuka kwa barafuto katika ulimwengu wote, kuliongezeka kwa haraka sana baina ya miaka 12 000 na 7000 kabla ya sasa (kwa wastani zaidi ya mita moja kwa kila karne lakini kwa kupungua kasi au kurudi nyuma yapata miaka 11000 kabla ya sasa). Inaelekea bahari kuu zilifikia usawa karibu na ule wa sasa baada ya miaka 6000 kabla ya sasa na karibu umebaki hapo tangu wakati huo. Hata hivyo, mbali na mwelekeo huo wa jumla, kulikuwa na mabadilikobadiliko ya usawa wa bahari ambayo yanaweza kuonekana katika grafu zinazohusika na ambayo yaliletwa na mabadiliko ya jumla ya tabia ya hali ya nchi.


### *Afrika*

Tangu miaka 20 000 kabla ya sasa na kuendelea baada ya ukame mkubwa ulitokea baina ya miaka 16000 na 14 000 kabla ya sasa, maziwa katika maeneo ya Sahara yaliongezeka kwa namna ya pekkee kutoka pwani ya Atlantiki hadi Bahari ya Sham. Mashapo ya maziwa, mara nyingi yakiwa na mbelewele, yameonekana karibu katika maeneo yote tambarare.

Huko Niger na Chad, M. Servant (1973) akizingatia vyanzo, hidrolojia na jiomofolojia ya maziwa alionyesha tao la mfululizo wa uwiano wa kutua kwa maji na mnywco wa maji (P/E), kwa msingi wa uchunguzi wa aina mbalimbali ya maziwa (Kielelezo 3). Tao hili la tabia ya hali ya nchi linaonyesha jumla ya mabadiliko makubwa yaliyotokea: kunywa kwake karibu miaka 4000 kabla ya sasa, na mabadilikobadiliko madogo baada ya miaka 3000 kabla ya sasa. Mabadiliko haya makubwa yaliathiri maziwa mengi huko Afar pia, ingawa kulikuwa na tofauti ndogo zilizosababishwa na chanzo cha maziwa hayo (picha 3). Ulinganifu dhahiri unaweza kupatikana baina ya tao la Chad na tao la unyevu la kanda ya bara la Siberia.

Uchunguzi wa maziwa mengine ya Afrika unaonyesha ruwaza ya namna hiyo ya mabadiliko. Livingstone na Vana Zinderen Bakker wanafikiri kuwa kuna usawa ulio karibu sana baina ya mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi katika Afrika Mashariki na yale ya Ulaya.

Kupanuka kwa maziwa ya Sahara kufikia miaka 8000 kabla ya sasa kunaelekea kuhusiana na kuenca kwa mvua katika mwaka mzima na kuwako kwa mawingu mazito yanayopunguza mnywco. M. Servant (1973) anadokeza kwamba mzunguko wa angahewa ulikuwa tofauti wakati huo, na kuwako kwa aina mbalimbali za mbelewele za tabia ya hali ya nchi zenye baridi vimemfanya apendkeze uwezekano wa kujipenyeza kwa hewa ya ncha ya dunia katika Sahara. Ufanyaji kazi wa sasa wa tabia ya hali ya nchi yaelekea ulithibitika baada ya miaka 7000 tu kabla ya sasa.



**16.3** Mlinganisho wa mageuko ya mnyweo wa mvua katika bonde la Chad (13-18 KZN) katika kipindi cha miaka 12000 iliyopita. Mageuko haya yamepimwa kwa kuchunguza mabadiliko mbalimbali katika viwango vya maji ya maziwa mbalimbali yanayopata maji hasa zaidi kutokana na mivilio ya chini ya ardhi na vijito na mito (M. Servant, 1973, kur. 40-52).

*Kizio cha dunia cha kusini*

Kaskazini mwa Australia na huko New Guinea, barafuto zilitoweka karibu miaka 8000 kabla ya sasa (Mount Wilhelm) ambapo kwa mujibu wa Bowler na wengine (1975), mvua iliongezeka, kukiwa na mabadilikobadiliko madogo.

Baina ya miaka 8000 na 5000 kabla ya sasa wastani wa halijoto yaelekea ulikuwa 1° au 2° zaidi kuliko sasa. Upeo wa tabia ya hali ya nchi unonekana kuwa ulikuwa ni kaida ya dunia nzima, ambapo baina ya miaka 7000 na 3500 kabla ya sasa misitu ya mvua ilipata nafasi nzuri sana ya kukua tangu kipindi cha barafuto kabla ya kufikia miaka 60 000 kabla ya sasa. Vivyo hivyo, maziwa yaliyo kusini mwa Australia ambayo yalikuwa yamekauka mnamo miaka 15 000 kabla ya sasa, yalianza kujaa tena karibu miaka 11 000 kabla ya sasa na yakafikia viwango vya juu karibu miaka 8000 na 3000 kabla ya sasa. Inawezekana kuwa halijoto zilipanda na unyevu ukaongezeka katika maeneo yote ya latitudo za chini katika nusu ya kwanza ya miaka 12 000 iliyopita na hivyo kusababisha hali zinazobainisha kipindi cha sasa cha kati ya vipindi vya barafuto.

*Hitimisho la kronolojia ya tabia ya hali ya nchi katika miaka 25 000 iliyopita*


Kipindi hiki kinatupatia picha ya mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi wakati wa upeo wa barafuto (mwishoni mwa kipindi cha barafuto) na wakati wa kuyeyuka kwa barafuto kulikosababisha kipindi cha kati ya vipindi vya barafuto (kipindi cha sasa). Ruwaza hii ya mbembeo nusu wa kipindi cha kuyeyuka barafuto unaonyesha hali ya ukame kwa jumla, inayobainisha mwisho wa barafuto na ambayo ilidumu takriban miaka 5000 katika Afrika. Ukame huu unafuatwa na enzi ya mabadilikobadiliko ya unyevu iliyodumu kwa muda mrefu na ambayo polepole ikarejea kwenye ukame.

Matukio haya ya tabia ya hali ya nchi yanaweza kuelezwa katika kipimo cha wakati cha miaka 20 000 kwa kuzingatia msogeo wa pepo za picha ya dunia na athari zake kwenye pepo za kati ya tropiki, na pia kwa kuzingatia aina mbili kubwa za mzunguko: wa kasi na wa polepole.

Inawezekana pia kuwa ruwaza hii inawakilisha hali nyingine zinazolingana kwa kiwango hichohicho kama cha Kwaternari - hali zilizofanana, katika muda na kwa ukubwa wake. Hata hivyo, hakuna sababu ya kukihusisha na ruwaza hii kipindi kizima cha barafuto kilichodumu miaka 100 000, au barafuto za enzi ya Kwaternari zilizokuwepo kwa muda wa miaka milioni kadhaa. Kwa sababu hii, kronolojia ya kipindi cha barafuto sasa itatazama kwa jumla.

*Ukadiriaji umri na tabia za hali ya nchi katika miaka 130,000 iliyopita*

Miaka 130,000 iliyopita (Pleistosini ya Nyuma) inatupatia fursa ya kuchunguza ruwaza ya tabia ya hali ya nchi na stratigrafia kwa kuangalia kipindi kizima cha barafuto na vipindi kati ya barafuto. Kronolojia ya kipindi hiki inakiuka sana ukadiriaji umri kwa njia ya radiokaboni ambao umetuwezesha kuthibitisha mfuatano ulio sahihi kwa kiasi cha kutosha (wa kukaribia karne moja au walau milenia) wa miaka 25000 iliyopita. Hata hivyo, kipindi hiki ambacho kinaungana na kipindi kikuu cha mwisho kati ya vipindi vya barafuto (Eemian) kabla ya kipindi cha sasa na barafuto kuu ya mwisho Wurm, Wisconsin, Weichelien, Valdai) kinajulikana vizuri, uwezekano wa kufanya kosa la kukadiria umri ukiwa takriban asilimia 10 au 20 kwa kipindi cha zamani kabisa. Hatimaye hasa ni mwclekeo wa jumla wa vipindi vya wastani (miaka 10 000) ambavyo vimetambulikana na vinaweza kulinganishwa toka eneo moja hadi jingine.



16.4 Mabadiliko ya usawa wa ziwa kwenye Bonde la Afar. Michoro ya mipindo ya ziwa Abey, Ziwa Hanlé-Dobi na Ziwa Asal, yaliyoko Afar ya kati inaonyeshwa kwenye sehemu ya juu ya grafu. Michoro ya mipindo kwa Ziwa Afrera ipo tofauti. Ulinganisho ungeweza kufanyika na michoro ya P/E ya Bonde la Chad

### *Latitudo za juu*

Mimea ya kipindi cha kati ya barafuto cha Eemina inaonyesha kuwa wakati wa joto sana wa kipindi hicho (baina ya miaka 125,000 na 80,000 kabla ya sasa), halijoto katika Eurasia na Amerika Kaskazini ilikuwa inalingana vizuri na ile ya kipindi cha Atlantiki (baina ya miaka 7000 na 5000 kabla ya sasa) na haikutofautiana sana na hali ilivyo sasa. Vipindi hivi viwili vya kati ya vipindi vya barafuto vilitokea ghafla, baada ya kushuka haraka kwa halijoto kilitokea kipindi cha mwisho cha baridi sana cha Riss miaka 135,000 kabla ya sasa, na kipindi cha mwisho cha baridi sana cha Wurm miaka 20,000 kabla ya sasa).

### *Bahari Kuu*

Mabadiliko katika viwango vya maji ya bahari kuu yanaakisi vizuri peo mbili za barafuto yakionyesha kushuka kwa kiasi kikubwa kwa kiwango cha maji (mita - 110 na mita +20 kwa upeo wa pili — kwa miaka 20,000 hadi 18,000). Kiwango cha juu kabisa cha maji kilichofikiwa katika kipindi kati ya vipindi vya barafuto cha Eemian na kile cha sasa vinalingana (kwa kiasi karibu asilimia 5). Kupanda kwa usawa wa bahari katika hatua za kati (baina ya miaka 45,000 na 30,000) pengine kulifikia asilimia 60 hadi 80 ya upeo wa kupanda (kwa mfano, Inchiria katika Mauritania). Viwango hivi vinathibitisha kuwa kiasi sawa cha tungamo barafu kilivyeyuka katika hatua ya kati.

### *Afrika*

Kama ilivyokuwa kwa bahari kuu, athari za tukio la barafuto katika tungamo ardhi labda hazikujitokeza sana kuelekea kwenye latitudo za kati ya tropiki. Tafouti baina ya halijoto za hatua ya barafuto na zile za kipindi kati ya vipindi vya barafuto zingeweza kuwa baina ya 5° hadi 10° katika latitudo za wastani lakini huenda zilikuwa kati ya 2° hadi 3° baina ya latitudo za tropiki. Katika Afrika athari juu ya kuenea na kiasi cha mvua ni tukio linaloweza kuonekana kwa urahisi sana.

Maeneo machache katika Afrika yana tarihi thabiti ya kiradiometa ya miaka 130 000 iliyopita. Hata hivyo, kwa kupima Ziwa Abay, F, Gasse (1975) aliweza kupata ushahidi wa hatua tatu za maziwa katika kipindi cha Pleistosini na nyuma kabla ya ukame ulitokea baina ya miaka 20 000 na 14000 kabla ya sasa. Hatua hizi za maziwa zilikuwa kama ifuatavyo: Kipindi cha kuanzia miaka 30 000 hadi 20 000 kabla ya sasa (tabia ya hali ya nchi yenye unyevu, yenye ubaridi zaidi kuliko ilivyo sasa), kilitenganishwa kutoka kwenye hatua ya awali ya unyevu kwa kusogea nyuma kidogo yapata miaka 30000 kabla ya sasa na kikiwa na mbelewele za tabia ya hali ya nchi ya fufutende; hatua ya pili ya unyevu ambayo ilianza yapata miaka 4000 kabla ya sasa, kama ile ya awali ambayo ilitokea kabla ya miaka 60000 kabla ya sasa inabainishwa na tabia ya nchi yenye joto.

Ushahidi zaidi kuhusu mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi ya wakati ambao haufahamiki katika kipindi cha Pleistosini ya nyuma ulitolewa kutokana na utafiti wa chavua katika bonde la juu la Awash (Afar) ambako R. Bonncfille (1973,1974) aligundua dalili za kuwako mapululu ya nyanda za juu na hivyo kuonyesa kuwako kwa tabia ya hali ya nchi yenye unyevu zaidi kuliko wa sasa na pengine baridi zaidi.

### *Bonde la Mediterania*

Bonde la Medeterania likiwa baina ya maeneo mawili ya kijiografia yaliyoelezwa hapo juu, ni uwanda muhimu katika tabia ya hali ya nchi na wenye mabadiliko ambayo yaonekana kuwa changamano. Hasa, vipindi vya barafuto haviwezi tena kuhesabika kuwa ndio vipengee pake yake vilivyosababisha kuwako kwa tabia ya hali ya nchi yenye unyevu.

Uchunguzi wa kipalinolojia, kimikropaleontolojia na ugunduzi wa kiisotopi uliofanyika mashariki mwa Mediterania, huko Ugiriki na Israeli unadhihirisha kuwa kushuka kwa halijoto katika kipindi cha mwisho cha barafuto huenda kilikuwa 4° kwa halijoto za anga na kutoka 5° hadi 10° kwa halijoto za baharini. Ukame ulijitokeza zaidi katika Ugiriki katika kipindi cha barafuto ambapo hali ilikuwa kinyume katika pwani ya Israeli.

Kwa upande mwingine, utafiti uliofanywa kuhusu dalili za hapa na pale za mamilia (rodenti) unaelekea kuonyesha mabadiliko ya taratibu kutoka hali ya unyevu kwenda hali ya ukame katika miaka 80000 iliyopita. Karibu miaka 20000 kabla ya sasa, kiwango cha maji katika Ziwa Lisan huko Israeli kilishuka kwa mita 190 katika muda wa miaka elfu moja kutokana na hali za ukavu (pamoja na mtitio wa dunia katika Bonde la Dead Sea) na, kama tulivyokwishaona mwishoni mwa upeo wa ueneaji wa barafuto ya Wurm, hali za ubaridi na ukame ziliendelea kuwapo katika bonde zima la Mediterania.

Kama vile ilivyo katika Afrika, mchangamano wa hali ya ardhi na tabia ya hali ya nchi katika Bonde la Mediterania unahitaji kufanyiwa utafiti wa kina ili kuweza kuelewa mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi katika kipindi cha Wurm.

**Hitimisho kuhusu ukadiriaji umri na tabia za hali ya nchi katika miaka 130000 iliyopita**


Kipindi cha mwisho cha barafuto kinatupatia ruwaza ya mzunguko kamili wa mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi kwa skeli ya miaka 100000 hivi (kipindi kati ya vipindi vya barafuto - kipindi cha barafuto - kipindi kati ya vipindi vya barafuto) na mabadilikobadiliko yake katika hatua zile zilizodumu kadiri ya miaka 10000. Katika Afrika, kipindi liki kinabainishwa na hatua za kupanuka kwa maziwa zenye muda unaolingana uliotenganishwa na hatua za ukaukaji.

Kutokana na maarifa tuliyonayo sasa, ukadiriaji umri si sahihi kiasi cha kutuwezesha kuona uwiano uliopo baina ya vipindi vya baridi au joto na vipindi vya unyevu au ukame katika Afrika. Kuna matumaini kuwa uchunguzi unaoendelea, ukisaidiwa na sehemu na sampuli zinazotoa mfuatano wa matukio, utatuwezesha kufikia mahitimisho thabiti katika siku zijazo.


**Ukadiriaji umri na tabia za hali ya nchi kati ya miaka 3 500 000 iliyopita**

Kupungua polepole kwa halijoto ambako ni sifa mojawapo katika enzi ya Kwaternari kulianza karibu miaka milioni 55 iliyopita (kipindi cha kupunguka kwa tabia ya hali ya nchi cha Cenozoic, National Academy Sciences, Washington, 1975). Utando barafu wa Antaktiki, ambao ulikwishaanza kutokoa yapata miaka milioni 25 iliyopita, ulipanuka sana karibu miaka milioni 10 iliyopita na tena karibu miaka milioni 5 au 4 iliyopita, ambapo ulikaribia kufikia ukubwa wake wa sasa. Utando barafu wa Aktiki katika mabara yaliyo jirani na Atlantiki kaskazini ulitokoa karibu miaka milioni 3 iliyopita. Kupungua kukubwa kwa halijoto ya baharini kuanza karibu miaka 1 800 000 iliyopita (Bandy, katika Bishop na Miller, 1972) muda mfupi kabla ya kiwango cha chini kabisa cha hatua ya kibahari ya Kalabria, karibu wakati mmoja na kutokoa kwa Gilsa (miaka 1 790 000 iliyopita).

Maeneo kadha ya Afrika, kwa mfano Chad na Afrika Mashariki, yametoa wanyama wengi wa aina ya vetabrata ambao hapo awali ilifikiriwa kuwa walitokana na Vilafransia (baina ya miaka 300 000 na 1 700 000 au miaka milioni moja iliyopita). Kwa kuhusisha mazingira na baadhi ya mamalia tunapata vidokezo vya kuwako kwa hali ya unyevu zaidi kuliko zile ambazo ni sifa ya mazingira ya sasa na mashapo. Kwa liyo kuhusika huku kumechukuliwa kuwa kunaonyesha 'vipindi vya mvua' katika Afrika.



16.5 Vipengele vya kiradiometra na kipaleomagnetiki za vipindi vya Pliosini/Pleistosini huko mashariki mwa Afrika; kusini-magharibi mwa Ulaya na magharibi mwa Amerika ya Kaskazini Mjiwatoano muhimu sana iliyopatikana toka Ileret na Koobi Fora, bonde la Rudolf Mashariki, bado inachunguzwa na kwa kuwa matokeo hayajakamilika; hivyo safu zinazojihusu sehemu hizi zimeachwa wazi. (F. Clark Howell, 1972:331-68).



16.6 Mielekeo ya jumla ya tabia ya hali nchi katika dunia katika kipindi cha miaka milioni moja iliyopita. (a) Mabadiliko katika wastani wa halijoto katika eneo la  $0^{\circ}$ - $80^{\circ}$  KZN katika vipindi vya miaka mitano mitano vya miaka 100 iliyopita (Mitchell, 1963). (b) Faharisi inayoonyesha hali ya ukali wa majira ya baridi huko Ulaya Mashariki kwa kipindi cha miaka 1000 iliyopita (Lamb, 1969). (c) Mielekeo ya halijoto ya hewa kwa jumla katika latitudo ya kati ya kizio cha dunia cha Kaskazini kwa kipindi cha miaka 15000 iliyopita, imeokana na mabadiliko katika mistari ya miti (Lamarche, 1974); mabadiliko madogo katika barafuu za milima ya Alps na za bara (Denton na Karlen, 1973), na mabadiliko katika ruwaza ya mimea iliyorekodiwa katika spektra ya chavua (Van der Hammen na wenzake, 1971). (d) Mielekeo ya jumla ya halijoto ya hewa (anga) katika kizio cha dunia cha askazini mwa miaka 100000 iliyopita kuokana na halijoto ya bahari katika latitudo ya kati, na rekodi ya chavua na ya usawa wa bahari katika dunia. (e) Mabadiliko ya wingi wa barafu ulimwenguni katika miaka 1000000 iliyopita kama yaliyoonyeshwa katika mabadiliko ya utungaji wa isotopu wa visukuku vya plankitoni katika vilindi vya bahari V28-238 (Shackletoni - na Opdyke, 1973).



Stratigrafia zenye maelezo ya kutosha ambazo zinatokana na ukadiriaji umri kwa kutumia kali-agoni na palcomegneti ni zile za mashapo ya Bonde la Ufa la Afrika Mashariki. Ni vigumu kuitambua athari ya tabia ya hali ya nchi inayotokana na kufanyika miambatabaka kuliko athari inayotokana na harakati za mititio ya dunia na volkano na mabadiliko ya topografia yanayotokana na harakati hizo, na kwa hivyo juhudi za kuthibitisha kuwepo kwa mfuatano wa tabia za halinchi zimeachiliwa mbali. Kwa upande mwingine, kronostratigrafia imefahamika vizuri na kuwa rejaleo la dunia.

Katika mashapo mbalimbali ya vetabrata na homonidi katika Afrika Mashariki (picha 4) mfuatano wa miamba tabaka iliyokadiriwa umri ni kama ifuatavyo:

### Omo, Ethiopia

Uchunguzi wa chavua katika ufanyikaji wa miamba yatabaka ya Shungura unaonyesha mabadiliko makubwa ya tabia ya hali ya nchi yanayoelekea hali ya ukavu karibu miaka milioni mbili iliyopita na kuenea kwa nyika za nyasi zenye *graminaeae*.

### Olduvai, Tanzania

Mfuatano wa ufanyikaji miamba unaotambuliwa pamoja na tarihi yao ni kama ifuatavyo:

Mfuatano wa ufanyikaji miamba unaotambuliwa pamoja na tarihi yao

Nduu	vitalu	miaka iliyopita	32 000
		miaka iliyopita	400 000
Masen	vitalu	miaka iliyopita	600 000
		kitalu IV	miaka iliyopita
(Kanjera ya mwanzo)	kitalu III	miaka iliyopita	1 500 000
		kitalu II	miaka iliyopita
(Kamasia ya mwanzo)	Kitalu I	miaka iliyopita	2 100 000


### Turkana Mashariki (zamani ikiitwa Rudolf), Kenya

Stratigrafia inahusu mashapo ya mita 325 yaliyotapakaa katika kipindi cha karibu miaka 3500000 hadi 1 500 000.

### Hadar (Afar ya Kati), Ethiopia

Hatimaye ufanyikaji wa miambatabaka katika Hadar, Afar ya Kati, ambayo ina hominidi na visukuku vingi ambavyo vinnechunguzwa na *International Afar Expedition* (IARE) huenda vina umri wa miaka milioni tatu.

Katika miaka michache ijayo uchunguzi ambao unacendelezwa katika sehemu hizi za Afrika Mashariki utawezesha kutoa nadharia ya mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi iliyokitwa katika sedimentolojia na ikolojia ya mimea na wanyama huku ikitiliwa maanani kuingiliwa kwake na matukio ya mititio ya dunia na volkano.



## *Asili ya binadamu: matatizo ya jumla*

### *SEHEMU YA I: Data ya kipaleontolojia*

Historia ya binadamu siyo historia ya matendo yake na maendeleo ya kitamaduni pekee, bali historia hii kimsingi ni historia ya mabadiliko ya spishi za wanyama, ambazo polepole zilianza kutofautiana na zile za maumbile ya wahenga na zikachukua sifa mahsusi ambazo zinazitambulisha. Hii ndiyo sababu binadamu wa leo hawezi kueleweka mpaka turejee nyuma kiasi cha makumi ya mamilioni ya miaka hadi tuifikie asili ya wanyama wa kundi la Primata.

### *Vigezo vya kipaleontolojia*


Primata ni mamalia, yaani viumbe vya daraja la juu kabisa miongoni mwa aina tano za vertebrata. Kwa ufasaha zaidi ni viumbe vyenye kondo ya nyuma, ambayo hulinda na kulisha mimba. Isitoshe, joto la mwili hurekebishwa kwa ndani, na huzaa kiumbe hai, yaani kiumbe ambacho tayari kinajimudu kinapozaliwa

Hata hivyo, Primata ni tofauti na mamalia wengine kwa vile akili zao hukomaa haraka, wana uwezo wa kuviona vitu katika umbo lake halisi (urefu, upana, kina/tunene), nyuso ndogo, kucha bapa badala ya makucha yanayoparura, na vidole gumba vyenye kutofautiana na vidole vingine. Sifa hizi zinajionyesha zaidi katika Primata wa daraja la juu, Masimia (manyani), ambamo mwanadamu pia hujumuishwa, kuliko katika Maprosimia. Pamoja na hayo, Masimia hubainika kwa umbo kubwa, ubongo uliokomaa zaidi, na mabadiliko ya nafasi yalipo macho kutoka pembeni mwa kichwa hadi kwenye paji la uso.

Tangu mwanzo Masimia waligawanywa katika makundi mawili: manyani wa ulimwengu mpya au Plattirina (*Platyrrhina*)<sup>1</sup> ambao walibaki na pua pana na meno 36, na manyani wa Asia na Afrika, au *Catarrhina* ambao walikuwa na pua nyembamba, na meno 32 tu sawa na binadamu.

Familia nyingi tofauti zilitokana na Katarrina (*Catarrhina*) ambao wazao wao hivi sasa wanajulikana sana, miongoni mwao wakiwemo Sekopithesidi (*Cercopithecidae*) (kama vile nyani mkubwa), Hilobatide (nyani mdogo-mdogo mwenye mikono mirefu ila hana mkia) na Pongidi (kama vile sokwe, na sokwe mtu). Miongoni mwa familia hizi, hominidi huonyesha sifa ambazo ni tofauti kabisa na zile za familia nyingine, kwa sababu ndio familia pekee ya Primata ambao hutembea wima. Kwa vile viumbe hawa wana miguu miwili, hali hii imesababisha

1 Fahaasa, kurasa 184-190, inatoa maana za istilahi mbalimbali za kisayansi zilizotumika.



## MAELEZO

- |                                       |   |
|---------------------------------------|---|
| 1. Eneo la Taung. Afrika Kusini       | 9. Eneo la Chemeron, Kenya                        |
| 2. Eneo la Sterkfontein, A. Kusini    | 10. Eneo la Chesowanja, Kenya                     |
| 3. Eneo la Swartkrans. A. Kusini      | 11. Eneo la Kanapoi, Kenya                        |
| 4. Eneo la Kromdraai. A. Kusini       | 12. Eneo la Lothagam, Kenya                       |
| 5. Eneo la Makapansgat. A. Kusini     | 13. Eneo la Turkana Matariki (Ziwa Rudolf), Kenya |
| 6. Eneo la Garusi - Laetoli, Tanzania | 14. Eneo la Omo, Ethiopia                         |
| 7. Eneo la Olduvai, Tanzania          | 15. Eneo la Afar, Ethiopia                        |
| 8. Eneo la Natron - Penini Tanzania   |   |

mabadiliko makubwa katika kiunzi kizima kuanzia kwenye miguu, miundi, kiuno, na mpindo wa uti wa mgongo hadi kugeuka umbo kwa fuvu la kichwa, kupungua kwa umbo la uso na ukubwa wa chonge, kuviringika kwa ufizi na kukomaa kwa ubongo.

Hominidi wa kale, wajulikanao kama Australopithisi (*Australopithec*) walikwishakuwa na idadi kubwa ya sifa hizi. Jamii ya jenasi ya homo ya hivi karibuni ambamo sisi tunajumuishwa hutofautiana na akina Australopithisi kwa kuongezeka kwa umbo lao, kusimama wima na kwenda kwa miguu miwili vizuri zaidi, na uwezo mkubwa wa kutumia ubongo. Wakati huohuo muundo wa meno yao ulikwishabadilika kutokana na kubadilika kwa aina ya chakula. Wahenga wetu ambao walikuwa wakila mboga za majani, baadaye walianza kula kila kitu. Matokeo yake ni kwamba meno ya mbele yalikuwa zaidi kuliko yale ya pembeni.

Kazi ya mwanapaleontolojia ni kupambanua kwa makini jinsi maumbo ya viumbe hao yalivyotokea, kugundua ruwaza zao mabadiliko na kueleza mazingira yaliyofanya mabadiliko hayo yatokee. Kwa hiyo mkabala anaotumia mwanapaleontolojia ni ule unaozingatia taaluma ya anatomia linganishi na yenye kuzingatia kimabadiliko. Wakijua kwamba mabadiliko huanzia maumbo sahili kabisa hadi kufikia yale yaliyo changamano kabisa, wanapaleontolojia hutafuta wahenga wa binadamu katika maumbo tofauti kabisa na maumbo tuliyo nayo sasa kadiri wanavyorudi nyuma kiwakati kuelekea chimbuko la asili la binadamu.

### *Miaka milioni 20 hadi milioni 70 iliyopita*

Kwa hiyo Primata wa zamani kabisa ni Maprosimia ambao walitokea yapata miaka milioni 70 iliyopita. Wanyama hao sasa wanawakilishwa na aina ya komba (*Leurus*) wa Bukini, *tarsiere* wa Ufilipino na Indonesia na *galago* wa Afrika Mashariki. Hawa ni wanyama waoga waishio mitini na kwa kawaida huonekana usiku tu. Maprosimia wa zamani waliendelea kubadilika na kunako miaka 40 milioni iliyopita walisahabisha kizazi kingine kipya cha Masimia. Kuanzia kipindi cha Iosini<sup>2</sup> na kuendelea (miaka 35 milioni iliyopita); Masimia nao waligawanyika katika Katarrina na Platirina ambao tumekwisha wataja.

Ukosefu wa ushahidi umefanya iwe vigumu kufahamu kilichotokea kati ya miaka milioni 20 na milioni 40 iliyopita, na mabaki yaliyopatikana kutokana na kipindi hicho ni haba sana, lakini ushahidi mwingi sana uliopo Fayum, karibu na Kairo huko Misri, na ambao umefanyiwa utafiti na watu kadhaa umeonyesha aina mbalimbali za Primata ambazo ni pamoja na *Parapithecus*, *Apidium*, *Oligopithecus*, *Propithecus*, *Aelophilus*, na *Aegyptopithecus*. Miongoni mwa hawa, wale wa aina mbili za mwanzo wana meno 36 kama Maprosimia na manyani wa ulimwengu mpya, lakini sifa nyingine zaidi zinawahusisha Primata na Katarrina, walio na meno 32. Huenda hawa ndio wahenga wa kina Katarrina. Aina nne za mwisho zilizotajwa ni jamii ya Katarrina wenye meno 32, na masagagego manne kama ilivyo kwa binadamu wa leo. Oligapitheko (*Oligopithecus*) ndio waliwatangulia Sesopithesidi (*Cercopithecidae*) ambapo yawezekana Aelopitheko (*Aelopithecus*) ndio waliozaa nyani ndogodogo asiye na mkia lakini ana mikono mirefu (*gibbon*), na *Aegyptopithecus* ndio waliwatangulia sokwe.

Ruwaza yoyote ile ya uhusiano iwayo, kipindi hiki kinasisimua, kwani ni ushahidi kwamba huko Kaskazini-Mashariki mwa Afrika, yapata miaka milioni 30 iliyopita, palikuwa na idadi kubwa ya Primata wadogo wa aina mbalimbali waliowatangulia wale waliopo hivi sasa,

2. Ikumbukwe kwamba kijiolojia, wakati hugawanyika katika kipindi cha kwanza, cha pili, cha tatu, na cha nne (Kwaternari). Primata waliojitokeza mwishoni mwa kipindi cha pili, yapata miaka milioni 70 iliyopita, waliendelea kukua katika kipindi cha tatu na cha nne. Kipindi cha tatu kinegawanyika katika hatua tano: hatua ya Plioceni, Iosini, Obligosini, Miosini, na Pliosini. Kipindi cha nne kina hatua mbili tu, Pleistosini na Holosini.

Sesopithecidi, Pongid: Hiliobatidi na Homidi (*Cercopothechi*, *Pongidae*, *Hylobatidae* na *Hominidae*). Miongozo ya msingi ilikwishawekwa tayari.

### *Miaka milioni 10 hadi milioni 20 iliyopita*

Tukiachilia mbali hawa Primata wa awali, liebu tuangalie sasa Masimia wengine wenye asili ya Afrika. Katikati ya miaka milioni 20 na milioni 10 iliyopita, kutokana na kupungua kwa unyevu hewa, maeneo ya mbuga za 'savana' yalienea kwa mapana zaidi katika kanda za tropiki, na hali hii ikawavuta manyani wa aina mbalimbali kuhamia kwenye maeneo mapya yenye chakula. Uendaji wima<sup>3</sup> wa muda ulisaidia kuendeleza ubongo na kupunguza uso, na hapohapo uliivzesha mikono kuwa huru ili iweze kufanya kazi nyingine. Spishi za mwanzo zilizojiingiza katika mazingira haya mapya ni Kenyapitheko (*Kenyapithecus*), Ramapitheko (*Ramapithecus*), Gigantopitheko (*Gigantopithecus*) na Oligopitheko (*Oligopithecus*).

Visukuku vya Kenyapitheko Afrikana (*Kenyapithecus africanus*) vya miaka milioni 20 iliyopita, na vile vya Kenyapitheko Wikeri (*Kenyapithecus wickert*) vya miaka milioni 14 iliyopita viligunduliwa huko Kenya na Uganda na Dkt. L.S.B. Leakey. Vinywa vyao ni vipana sana na taya za chini zimechomoza kwa mbele. Baadhi ya wataalamu humwainisha Primata huyu kama mmoja wa wale waitwao *Pongidi*. Hata hivyo, katika mkutano wa bara zima la Afrika uliofanyika Dakar, 1967, Leakey alionyesha vipande vya mawe meusi ambayo makali yake ya kukatia yalionekana kuwa yalikwishatumika. Katika mwaka 1971, alipokuwa Addis Ababa, alithibitisha kwamba mifupa mingi ya wanyama iliyogunduliwa ambayo inahusishwa na Kenyapitheko wikeri ilikuwa imevunjwa kwa makusudi tu. Hii ni nadharia tete mojawapo, ingawa ni vigumu kutoa ushahidi wa kiakiolojia kuitetea.

Mabaki ya kianatomia ya *Ramapitheko*, Primata mdogo mwenye uzito wa kati ya kilo 18 hadi 36 na aliyecishi yapata miaka milioni 8 hadi milioni 14 iliyopita yamconekana katika eneo kubwa la kijiografia, kuanzia India na Pakistan hadi Uturuki na Hungaria. Mabaki hayo yalikuwa hasa ni vipande vya mataya mafupi na vya meno ambavyo liavikuwa rahisi kuvifanua barabara. Hata hivyo mabaki hayo yanaonyesha kuwako kwa utaratibu mpya wa chakula wenye aina ngunu za mimea ambao umedhihirishwa na visukuku vya mimea na vya wanyama vilivyoonekana kando ya mabaki hayo.

Primata mkubwa, *Gigantopitheko* aliishi Uchina na India miaka milioni kadha iliyopita. Huko Uchina Primata huyo anajulikana kwa jina la Gigantopitheko blaki (*Gigantopithecus blacki*) na huko India anajulikana kwa jina Gigantopitheko bilaspurensis (*Gigantopithecus bilaspurensis*). Jina lake linadokeza ukubwa wake. Umbo la meno na sifa zake za kianatomia zinaonyesha kwamba mnyama huyo aliishi katika maeneo yaliyokuwa na miti michache. Siku hizi, wataalamu wengi wanakataa kwamba kiumbe huyo ndiye mhenga wa binadamu.

Hatimaye, kiasi cha miaka milioni 12 iliyopita kulitokea Primata mwingine aliyetitwa Oreopitheko (*Oreopithecus*) aliyekuwa anadandia matawi ya miti katika misitu ya Tuscany huko Italia na huenda pia katika misitu ya Kenya. Oreopitheko bambolii (*Oreopithecus bambolii*) aliyegunduliwa Tuscani katika mwaka 1870 ni Primata mdandaji<sup>4</sup> aliyejirekebisha kulingana na maisha ya misituni. Wakati mwingine mnyama huyo alitembeatembea kwa miguu ya nyuma, kama invyodhirishwa na urefu wa miguu ya mbele, umbo la kiuno chake hasa katika sehemu ya chini ya mgongo wake, na jinsi alivyo kiavu chake. Pamoja na bidaa za kianatomia, ukubwa wa ubongo wake uliongezeka hata kufikia sentimita za ujazo 400 na alikuwa na meno madogo.

3 Uendaji wima ni namana ya kwenda katika nchi kavu kwa kutumia miguu.

4 Mdandaji: udandaji ni aina fulani ya mwengo wa misami wa kuruka toka tawi moja hadi jingine kwa kuning'inia.

Mpaka hapa tulipofikia, miongoni mwa vile vizazi vinne vilivyotajwa hapo juu, jambo lililo muhimu si kujua nani alimzaa nani. Jambo la kuzingatia ni kwamba mitindo mipya ya maisha ilianza kujitokeza katika hayo mazingira ya misituni. Wakati huohuo ukubwa wa uso na wa meno ya mbele vilipungua, na masagagego yaliongezeka ukubwa kwa vile hayakuzuiliwa tena na chonge. Yote haya ndiyo yaliashiria umilikaji wa mazingira ya savana na papo hapo ucdaji wima wa binadamu.

### *Miaka milioni 10 hadi milioni 1 iliyopita*

Kutoka enzi za Pliosini hadi za Pleistosini, kati ya miaka milioni 10 na milioni 1 iliyopita, tunajikuta miongoni mwa Australopithecini (*Australopithecine*), kikundi ambacho kilikuwa na maumbile tofauti na kilichokuwa kinakaa mahali pamoja.

Kuanzia mwaka 1924 hadi sasa, kumetokea ugunduzi mwingi wa Australopithecini huko Mashariki na Kusini mwa Afrika ambako ndiko lilikotoka jina lao. Inaelekea walitokeza katika maeneo hayo kati ya miaka milioni 6 na 7 iliyopita; huko Kenya waliishi katika mashapo ya mabonde ya maziwa baringo na Turkana; katika Tanzania huko Lactolil; nchini Ethiopia katika bonde la into Omo na katika mkoa wa Afar, na huko Afrika Kusini katika mapango manne: Sterkfontein, Makapansgat, Swartkrans na Kromdraai katika mkoa wa Transvaal. Yaelekea kuwa walitoweka yapata miaka milioni moja iliyopita.


Sehemu hizi mbalimbali zimetoa aina kadha za hominidi, baadhi yao waliishi wakati mmoja: Australopitheko robusto (*Australopithecus robustus*), Australopitheko grasili (*Australopithecus gracil*), Homo erekto (*Homo erectus*) na Homo habili (*Homo habilis*).

### Hominidi

#### *Australopitheko robusto*

Visukuku vyenye umri wa kati ya miaka milioni 2 hadi 22 vya aina ya hominidi vimepatikana katika mapango ya Afrika Kusini na vingine vyenye umri wa miaka yapata 1,800,000 vilionekana katika bonde la Mto Omo nchini Ethiopia na katika bonde la Olduvai nchini Tanzania. Umbo la fuvu la kichwa lilionyesha kinywa madhubuti sana. Lina utaya wa chini madhubuti wenye misuli yenye nguvu kwa ajili ya kutafunia, na kijituta kidogo<sup>5</sup> katikati ya fuvu la kichwa. Uso bapa na meno ya mbele ni madogo ili kurahisisha utafunaji wa chakula wakati kiwiliwili chake kina nguvu kuliko cha spishi nyingine za Australopitheko (*Australopithecus*). Hominidi huyo alikuwa na urefu wa mita 1.5 na uzito uliokadiriwa kuwa kilo 35 – 65. Aliweza kutembea kwa miguu miwili kwa shida tu, kwani ncha ya fundabeka lake ilikuwa ndogo, ukubwa wa ubongo wake ulikuwa ni sentimeta za ujazo 530 kule Swartkrans na kule Olduvai. Kukomaa kwa ubongo kati (*cerebellum*) kunavutia, kwani kunaweza kudokeza uwezo mkubwa wa kudhibiti miondoko ya mikono na miguu tukilinganisha na ule wa Masimia wa awali.

<sup>5</sup> Kijituta kidogo hicho ni mfupa uliojitokeza juu ya fuvu la kichwa, na unafanana na kishungi cha kofia ngumu ya kuhifadhi kichwa, hehmeti.



17.2 Uundaji upya wa fuvu la Ramapitheko (J. Oster, Makambusho ya Binadamu).

17.3 Kiunzi cha Oreopitheko bamboli chenye umri wa miaka 12000 ovo kilichogunduliwa katika eneo la Grosseto, Tuscany na Johannes Huzler mwaka wa 1958 (J. Oster, Makambusho ya Binadamu).


17.4 Fuvu la Australopitheko afrikana - upande wa kulia ni fuvu la kijana (Taung Botswana), upande wa kushoto ni fuvu la mtu mzima Sterkfontein Tansvaal (Y. Coppens, Makambusho ya Binadamu).






17.5 Fuva la *Australopithecus boisei* lililopatikava Omo, Ethiopia. Machimbo yalifanywa chini ya usimamizi wa Y. Coppens, 1976 (Picha imepigwa na J. Oster, Makumbusho ya binadamu [Musée de l'Homme]).

17.6 Eneo la uclumbuji katika Olduvai (picha imepigwa na J. Chavaillon, Makumbusho ya Binadamu).










17.7 Fuvu la Austrploitheko robuto (kulia). Fuvu la Australopitheko grasili (kushoto) (Picha imepiga na J. Robenson, Makumbusho ya Binadamu [Musée de l'Homme]).

17.8 Fuvu la Homo habilis (Makumbusho ya Taifa ya Kenya)





17.9 Mojawapo ya zana za mawe za kale kabisa ulimwenguni jilizopatikana Omo, Ethiopia: uchunguzi ulifanywa chini ya usimamizi wa J. Chavaillo (makusanyo ya Makumbusho ya Binadamu) Musée de l'Homme).



17.10 Picha kamili ya sura ya nje ya udongo katika eneo la uchimbuzi la Olduvai (J. Chavaillon,, Makumbusho ya Binadamu).

17.11 Picha ya karibu sana ya sura ya udogo katika machimbuzi ya Olduvai; mfupa wa kiboko na baadhi ya palihedroni vinaonekana (J. Chavaillon, Makumbusho ya Binadamu)



*Australopitheko grasili*

Aina hii inatoka Makapansgat na Sterkfontein huko Afrika Kusini, na inafikiwa kwamba ilipatikana pia huko Omo katika Ethiopia, Laetotil katika Tanzania, katika jimbo la Afar, na huko Lothagam katika Kenya. Inakadiriwa kuwa alikuwa na urefu wa meta 1.2 na uzito wa kati ya kilo 18 hadi 31. Uso unajitokeza zaidi wake kuliko ule wa Australopitheko robusti na kijituta cha nyusi ni kikubwa kiasi na kinahimili paji la uso lililokomaa zaidi. Ijapokuwa spishi hii yaweza kuwa ilikula chakula cha aina nyingi zaidi kuliko Australopitheko robusti, chakula hicho lazima kimsingi kilikuwa cha aina ya mboga za majani. Unene wa utaya wa chini na lile gamba la jino ambalo lilikuwa limesagika hadi kwenye ufizi, uso mfupi na ukubwa wa magego na masagagego, yote haya yanadhihirisha kuwapo kwa kinywa madhubuti. Kuchelewa kuota meno pamoja na unene wa magamba ya meno kunaonyesha kuwa ukuaji ulikuwa wa polepole. Wastani wa ukubwa wa ubongo kwa ile aina ya Afrika Kusini ni sentimeta za ujazo 444. Mifupa yake mirefu hasa ile ya mikono na mtulinga ni kama ile ya wazazi wake ambao walikuwa wakidandia matawi ya miti kwa kutumia mikono. Hata hivyo, Australopitheko huyo daima alitumia miguu miwili.

*Homo habili*

Mwanadamu huyu alitambuliwa katika bonde la Olduvai nchini Tanzania mwaka 1964 na huenda alipatikana pia huko Omo katika Ethiopia, upande wa mashariki wa Ziwa Turkana na pia huko Kanapoi katika Kenya. Meno yake yalimwezesha kula aina mbalimbali za chakula kuliko yale ya Australopitheko. Chonge na meno ya kukatia yalikuwa marefu zaidi na yaliupa utaya umbo la mvingo, ambapo magego na masagagego yalikuwa madogo zaidi. *Homo habili* anakadiriwa kuwa na ubongo wenye ukubwa wa sentimeta za ujazo 680, ambapo fuvu moja kutoka mashariki ya ziwa Turkana lina ukubwa wa karibu sentimeta za ujazo 800. Ruwaza ya mabadiliko ya meno na ubongo wake yanamfanya kiumbe huyu awe karibu zaidi na binadamu wa leo kuliko *Australopitheko*. Hata hivyo, sehemu iliyobaki ya mifupa yake ni kama ile ya *Australopitheko grasili*, na hasa mtulinga unadokeza kuwa wahenga wao walikuwa wakidandia matawi ya miti, kama tulivyosema kuhusu ile aina ya *Australopitheko grasili*. Inakadiriwa kuwa *Homo habili* alikuwa na urefu wa kati ya meta 1.2 na 1.4.

*Homo erekto*

Mwisho kabisa, huko Olduvai katika Tanzania na kwenye pwani ya Mashariki ya Ziwa Turkana, kumegunduliwa *Homo erekto* walioishi yapata miaka milioni 1.5 iliyopita, na huko Melka Konture katika Bodo kwenye bonde la mto Omo nchini Ethiopia pia kumegunduliwa *Homo erekto* walioishi yapata miaka 500 000 na milioni 1.5 iliyopita. *Homo erekto* hawa yaani *Hominidi* waliendelea zaidi kuliko viumbe waliowatangulia. Maumbo yanayofanana na hayo yamepatikana pia huko Indonesia na Uchina. Maumbile ya *Homo erekto* yanaonyesha fuvu nene lililorudi nyuma, kisogo kilichogandamizwa sana (sehemu itwayo *Occipital torus*) na kutokeza kwa kijituta cha nyusi. Ukubwa wa ubongo unakadiriwa kuwa na sentimeta za ujazo 1,000. Usahibi wa vielezo viwili vilivyogunduliwa kule Olduvai si bayana, ingawa Leakey na P.V. Tobias wamevilusisha na *Homo erekto*. Huko Mashariki ya Ziwa Turkana, kupatikana na mafuvu inatatu yenye unri tofautitofauti, ni mfano mzuri wa maelekeo ya mabadiliko katika aina hii ya spishi.

Mabaki ya asili kutoka Java yamelinganishwa na yale ya Tanzania, na hii imewezesha kuhitimisha kwamba Homo habili wa zamani kabisa anafanana kimaumbile na yule aliyepatikana Uchina na Java, ambao hapo awali walifikiriwa kuwa *Homo erecto*.

### Tasnia

Kwa mara ya kwanza katika historia ya Primata mabaki ya kianatomia ya viumbe hao yalipatikana sawia na vifaa vyao. Katika sehemu za Omo huko Ethiopia na kwenye bonde la Pleistosini la Ziwa Turkana, umri wa zana zilizotengenezwa mwanzo umerudishwa nyuma kufikia miaka zaidi ya milioni mbili na nusu, pengine hata miaka milioni tatu iliyopita. Zana za mwanzo zilikuwa za vipande vingi vya miamba ambavyo ama vilitiwa makali au vilitumiwa moja kwa moja iwapo umbo lake lilifaa kwa shughuli iliyokusudiwa, kama zilivyotumiwa chonge za kiboko au za *Suidae*.

Zana hizi zinaweza kugawanywa katika aina kadhaa, kila aina ikiwakilishwa na vielelezo mbalimbali, hali inayoonyesha kwamba maumbo yake yalifanywa kwa kukusudiwa na yalikuwa ni matokeo ya uzoefu uliorithishwa.

Mabaki mengi ya visukuku vya mimea na wanyama na yale ya Hominidi yaliyoko katika bonde la Omo hutuwezesha kuisawiri upya mandhari ya ardhi ilivyokuwa miaka milioni tatu iliyopita: hali ya mazingira ya savana ambamo spishi nyingi ambazo hivi sasa zinaishi katika sehemu zenye unyevu zaidi zilikuwa zikiishi pamoja kwa usalama au kwa uhasama.

Huko Makapansgat, Afrika Kusini, tasnia ya zana zilizotengenezwa kwa mifupa, pembe na meno imekwishaonekana, ya imepewa jina la Osteodontokerati. Tasnia hii inaelekea kuwa ya zamani zaidi kuliko zile za mbwe au ujeya, ikiwa majaribio ya kuwianisha matokeo ya utafiti katika mapango ya Afrika Kusini na yale ya sehemu za Afrika Mashariki utatoa hitimisho linalokubalika.

Huko Hadar, Ethiopia, H. Rochi hivi karibuni amegundua tasnia ya zana za mbwe inayofanana na ile ya Olduvai, kwenye tabaka la mwamba ambalo umri wake unakadiriwa kuwa miaka 2,500,000 iliyopita.

Zana za aina hiyo zinapatikana kwa wingi sana kutoka katika matabaka ya miamba ya zamani kabisa ya Olduvai (miaka 1,800,000) na kuendelea juu. Kuwepo kwa kiasi kikubwa cha zana za mawe kumesababisha tasnia hii iitwe 'Utamaduni wa Mbwe' au Oldowani. Katika tabaka la zamani kabisa Dkt. Leakey alikuta duara kubwa iliyojaa malundo ya mbwe nyeusi na akapendekeza nadharia tete kwamba mbwe hizo zilitumika kusimikia nguzo ardhini, jambo linalodokeza ujenzi wa makazi.

Huko Maika Konture karibu na Addis Ababa, J. Clavaillon hivi karibuni amechimbua umbo linalofanana na lile lililo katika tabaka ya zamani kabisa ya Oldowani (miaka 1500000). Umbo hilo pia ni la duara na lina urefu wa futi moja kutoka kwenye usawa wa ardhi, na limezungukwa na mlizamu wenye urefu wa mita mbili. Malundo machache ya mawe yanaonyesha kuwapo kwa nguzo hapo zamani. Zana zinazohusishwa na eneo hili ni za aina ya Asheuli ambazo ni pamoja na mbwe, lakini hasa aina mbalimbali za mashoka (yenye nyuso mbili) na buhari.

Pamoja na mkanganyiko huu wa ukweli na matokeo ya uchunguzi, jambo moja muhimu linajitokeza, nalo ni kwamba jenasi ya Homo na zana zilizotengenezwa kwanza zilijitokeza katikati ya tabaka la Australopitthisini ambalo hapo awali liliishia Afrika Mashariki na Kusini lakini baadaye likaenea hadi Asia (pamoja na Australopitheko katika umbo lile lile au lililocendelea zaidi).

Ni kana kwamba kiasi cha miaka milioni 6 au 7 iliyopita, katika eneo la robo ya kusiri-mashariki ya bara la Afrika, kikundi cha Hominidi waliojulikana kama Australopithecisi walitokea, na kunako miaka milioni mbili iliyopita, kiombe aliyeweza kuchonga mawe, kujenga mahali pa kujisitiri na kuishi katika jamii ndogondogo, yaani Australopitheko halisi, au labda tuseme binadamu, alitokea katika kikundi hiki na kutokana na matendo yake, aliwakilisha asili ya *Homo faber*, yaani mtengeneza zana.

### *Miaka milioni moja ya mwisho*

Miaka milioni moja iliyopita ilishuhudia kuzaliwa kwa *Homo sapiens* ambaye aliongezeka kwa wingi sana baada ya miaka mia chache iliyopita. Ilichukua miaka 115 kwa idadi ya watu kuongezeka kutoka milioni elfu moja hadi milioni elfu mbili, na baadaye miaka 35 idadi hiyo iliongezeka hata kufikia milioni elfu tatu. Katika miaka 15 iliyopita, idadi ya watu imeongezeka tena hata kufikia milioni elfu nne na idadi bado inazidi kuongezeka.

## *SEHEMU YA II: Data ya kiakiolojia*

Mwanahistoria wa kipindi cha kabla ya historia hulikabili suala la asili ya binadamu katika Afrika kwa mtazamo ulio tofauti kidogo na ule wa mwanapaleontolojia ambaye huangalia asili ya binadamu kutokana na kukua kwa ubongo, kunakomwezesha mtu, kwa kutumia mbinu za hali ya juu, kubuni na kutengeneza zana anuwai na madhubuti hivyo kwamba kadiri wakati unavyopita, zana hizo humwezesha kuyamudu kwa ufanisi mazingira yake asili. Mabadiliko ya kipaleontolojia yanayoendelea hadi kufikia kutokea kwa binadamu, siyo njia pekee ya kuelezea asili ya binadamu, bali zana ya jiwe lililohongwa naye hutudhihirishia kwamba binadamu amekwishatoka.

Wakati kwa mwanapaleontolojia, asili ya binadamu ni ukubwa wa ubongo wenye sentimeta za ujazo 800, kwa mwanahistoria wa kipindi cha kabla ya historia, asili ya binadamu hutazamwa kwa kuangalia kiwango cha stadi za kiufundi ambacho pindi kikishafikiwa humfunguia njia ya maendeleo hadi kufikia wakati tulio nao. Walakini kadiri tunavyorudi nyuma katika mabadiliko ya Hominidi ndivyo inavyozidi kuwa vigumu zaidi kuamua kwamba zana fulani iliyotokana na jiwe au mfupa, ambayo ni matokeo ya stadi hizo, ilitengenezwa na spishi maalumu.

Kwa hivyo, tatizo kubwa analokumbana nalo mwanahistoria wa kipindi kabla ya historia ni lile la kuona jinsi ya kutofautisha binadamu na manyani na lini viumbe hao walitokea.

Kazi ya kwanza ni kuachana na sababu za asili zinazoweza kuingia katika utengenezaji wa kitu na kubainisha zile sifa zitokanazo na kazi ya mkono wa mtu pekee. Kazi ya pili ni kujenga kiunzi cha kronolojia kiakachotwezesha kukadiria umri wa ushahidi japo mdogo sana wa tasnia ya binadamu, walau kwa makadirio yanayoweza kukubalika. Ni Afrika peke yake iliyoweza kutoa ushahidi wa namna hii kuhusu jambo hili.

Mwanahistoria wa kipindi kabla ya historia katika Afrika anapaswa kuanza kwa kujibu maswali matatu yafuatayo:

1. Je, zana ni kigezo cha kutegemea katika kuelezea asili ya binadamu?
2. Je, zana hizo zinatuwezesha kuonyesha mwanzo wa asili ya binadamu?
3. Je, hata kama zana hizo zimehifadhiwa, zinaweza kutambuliwa kwa uhakika?

### *Je, zana ni kigezo cha kutegemewa katika kuelezea asili ya binadamu?*

Waandishi wengi wamesema kwa dhati kwamba matumizi ya zana badala ya sehemu za mwili ("zana za asili") si tabia ya binadamu peke yake, wala ya Primata kwa ujumla. Sokwe ndiye

Pimata aliye karibu sana na binadamu. Masokwe huishi katika vikundi vyenye masokwe zaidi ya thelathini na wanaweza kuchagua vijiti vya kuchimbia, hutumia fimbo kwa ajili ya kuvunja viota vya ndege au kwa kujipatia asali, hukunja majani kwa kuchotea maji, na pengine kufunga matawi pamoja kwa ajili ya kuangushia ndizi. Pia hutumiwa kama silaha za kuwatimulia wanyama walio adui zao. Masokwe pia huwasiliana kwa njia ya ishara zisikikazo. Mambo kama hayo yameonekana miongoni mwa masokwe-mtu walioko Rwanda.

Kwa hiyo, ikiwa zana zitatumia kama kigezo cha kuelezea asili ya binadamu, ile dhana ya *matumizi* ya kitu fulani kuliko zile "zana za asili" zilizoko mwilini haitoshi. Ie dhana ya *kukigeza kwa makusudi* kitu kilichotumika ili kiwe zana sharti izingatiwe.

### *Je, zana zinatuwezesha kuonyesha mianzo ya asili ya binadamu?*

Zana peke yake hazituwezeshi kuonyesha mianzo ya asili ya binadamu, kwani vitu vya kwanza vya aina hiyo—mbwe zilizokuwa zimevunjwa—kwa jumla vimetiliwa wasiwasi. Ni kweli kwamba ubwe uliyookotwa na kutupwa na mkono wa binadamu hauonyeshi dalili yoyote iliyo bayana kwamba ulipata kutumika kwa lengo lilo, lakini ubwe uliipasuka wawezekana umekuwa hivyo tangu asili. Maporomoko na mawimbi ya maji husababisha kutokea kwa mawe ambayo hayawezi kutofautishwa na yale yaliyopasuliwa na binadamu.

Ni kutokana na kosa lililofanyika katika kufasiri matumizi ya moto yalipohusishwa na Australopithecus *prometheus*; ama kwa hakika hakuna ushahidi wa kuatumika wa matumizi ya moto kabla ya kipindi cha Homo erekto na Pithecoanthropini (Pithecanthropines), hasa katika Afrika. Kwa upande mwingine, "ala za mawe" zilizopatikana kule Olduvai kwa kweli haziwakilishi hatua za mwanzo za shughuli hiyo; maumbo anuwai, idadi kubwa ya vielelezo mbalimbali, na jinsi vilivyotengenezwa, yote haya yanaashiria hatua za mwisho kuliko za mwanzo. Vyombo hivi vilitengenezwa na viumbe wadadisi na kwa kurithisha ufundi. Hata hivyo, mianzo ya tasnia iliyotumia zana za mawe imerudishwa nyuma kwa zaidi ya miaka 2,500,000 iliyopita kutokana na ugunduzi uliofanywa hivi karibuni na wanahistoria wa kipindi kabla ya historia barani Afrika katika bonde la Ono nchini Ethiopia na huko Koobi Fora nchini Kenya.

### *Je, zana zilizotengenezwa na binadamu zinaweza kutambulika?*

Swali la tatu la kujibiwa ni iwapo inawezekana kuthibitisha kwamba utashi wa binadamu ulihusishwa kuka kutengeneza zana sahili. Ni Afrika pekee inayoweza kutoa vitu vya kutosha kwa ajili ya utafiti wa suala hili. Maeneo mawili muhimu ya utafiti yanahusu vitu viwili: mfupa na jiwe.

#### Tasnia ya Osteodontokerati

Kuwapo kwa tasnia hii kulipendekezwa kama nadharia tete na Dart mwaka 1949, na pendekezo lili liliendelezwa pia na D.F. Wolberg mwaka 1970. Hii ina maana kwamba zana zilizotengenezwa kwa mfupa zilikuwapo kabla ya zile zilizotengenezwa kwa mawe. Msingi wa madai haya unatokana na ugunduzi uliofanywa katika pango la Makapansgat katika mkoa wa Transvaal, nchini Afrika Kusini. Hakuna uhakika eneo hilo ni la miaka mingapi, lakini inadhaniwa kwamba huenda lilikuwako yapata miaka milioni 2 hadi milioni 2.5 iliyopita.

Katika marundo ya mifupa ya wanyama yaliyokutwa pamoja na visukuku vya Australopitheko grasili (*Australopithecus gracili*), Dart aliweza kupambanua takataka za jikori na masalio ya chakula cha wawindaji ambao alidhani walitumia silaha na zana zilizotengenezwa kwa mifupa, pembe na meno ya tembo, ndipo neno "osteodontokerati" lilipoanza kutumika. Wawindaji hao waliweza kutengeneza hivyo vitu kwa sababu waliweza kusimama wima na kutumia mikono. Hali kadhalika katika kuchunguza mafuvu ya manyani na Australopithisini, Dart aliweza kudai kwamba viumbe hao walipatwa na mapigo ya usoni yaliyotokana na marungu yaliyotengenezwa kwa mifupa, hasa mfupa wa paja wa mnyama mwenye kwato. Isitoshe, mifupa ya wanyama iliyopatikana ndani ya pango ilionekana imevunjika kwa sababu ya kupindwa. Hii inaonyesha kwamba mambo haya yalitendwa na binadamu.

Kwa hiyo tunaweza kusema kwamba palikuwa na hatua ya osteodontokerati ambayo ilifuatiwa na ile ya mawe yaliyochongwa ya Utamaduni wa Mbwe na tasnia zilizofuata za zana zenye nyuso mbili. Hali hii yaonyesha wazi mwanzo wa utengenezaji wa makusudi wa zana. Hata hivyo, nadharia tete ya Dart ilizusha mjadala kama ni kweli Australopitheko ndiye hasa aliyeanzisha tasnia hii, na alikuwa mwindaji au, kinyume chake, alikuwa mwidwa. Baadhi ya wataalamu walikuwa na fikra kwamba mifupa yote, pamoja na ile ya Australopithisini ililetwa mle pangoni na fisi, ijapokuwa wazo hili lingepingana na tabia za mnyama huyo. Kwa kweli, kulikuwa na mifupa mchache mno ya fisi kwenye eneo la Makapansgat hata kuweza kuwa malalo ya fisi.

Hata hivyo wakati dalili za tasnia za mawe na mifupa zilipoonekana pamoja katika pango la Sterkfontein huko Afrika Kusini, ukweli wa nadharia tete ya utamaduni wa osteodontokerati ulithibitika.

Hatimaye, Mary Leakey aligundua zana za mifupa na pembe za kiboko zilizokuwa pamoja na zana za mbwe katika tabaka la kale kabisa la Olduvai, zenye umri wa miaka milioni 1.8 iliyopita. Zana hizo zilikuwa zimepasuliwa vipande viwili na pande zake zote zingeweza kutumika. Vyombo hivi vinawakilisha ushahidi usioweza kupingika kulusu kuwapo kwa tasnia ya osteodontokerati, na ingawa kuwapo kwa hatua mojawapo kabla ya tasnia ya zana za mawe hakujathibitishwa kabisa, kwa hakika hakuna ushahidi wa kabla ya hapo wa kuwapo kwa tasnia ya namna hiyo mahali pengine popote isipokuwa katika Afrika.

## Tasnia ya Mawe

Mbwe zilizochongwa ambazo kwa muda mrefu zimejulikana kama *Utamaduni wa Mbwe* zinawakilisha tasnia ya zana za kale ya zana za mawe. Istilahi za Utamaduni wa Mbwe, hatua ya kiufundi na kitamaduni ambayo ina awamu nne na Utamaduni wa Kafu, kutokana na mto Kafu nchini Uganda ziliundwa kwa mara ya kwanza mwaka 1920. Hata hivyo ilikuwa ni H. Movius katika utafiti wake alioufanya Asia alipotoa fasili sahihi ya maumbo muhimu mnamo mwaka 1944, ndipo alipoanza kutumia maneno kama vile kishoka, chombo cha kuchanja kuni na shoka la mkono. Miainisho mbalimbali ya kimofolojia iliyotokana na mbinu zilizotumika katika utengenezaji wa zana hizo ilipendekezwa na wataalamu kama vile L. Ramendo, P. Biberson na H. Roche. Utafiti huu ulionyesha haraka mambo mawili: mosi, aina tofauti za zana, ulinganifu na kuliana kwa maumbo kulionyesha kuwa Utamaduni wa Mbwe ulishafikia hatua ya hali ya juu mno, kuweza kuwakilisha mwanzo halisi wa tasnia za mawe. Pili, Utamaduni wa Mbwe ulitangulia tasnia zote za mashoka ya mikono na buchari ambazo zilitokea katika enzi za Paleolithi ya chini ya Afrika.



Utamaduni wa mbwe umechangamana mno kiasi kwamba umewashawishi wana-historia wa Afrika wa kipindi kabla ya historia kuangalia uwezekano wa kuendeleza utaratibu wa kikronolojia ili uvuke kile kiwango cha miaka milioni moja. Enzi ya Oldowani, inayokadiriwa kuwa ilidumu kati ya miaka milioni 1.85 na milioni 1.1 ilitokana na enzi ya Omo ya zana za kukatia ambayo inakadiriwa kuwa ilikuwapo kati ya miaka milioni 2.5 na 2.1 iliyopita, na ile ya Ziwa Turkana iliyokuwapo yapata miaka milioni 2.6 iliyopita. Hata hivyo maeneo mawili yaliyotajwa mwisho yalionyesha idadi kubwa zaidi ya zana za ujeya kuliko mbwe zilizochongwa, na inaweza kudaiwa kwamba uchongaji wa mbwe kwa kutengeneza zana ulitanguliwa na matumizi ya chenge zilizobanduliwa kutoka kwenye majabali.

Fikra hii ingeweza kuthibitishwa na madai ya Leakey kwamba Kenyapitheko wikeri, Primata aliyemtangulia binadamu ambaye aliishi yapata miaka milioni 14 iliyopita, ndiye aliyehusika na vipande vya mawe meusi vilivyogongwagongwa. Walakini, hapa pia alama za kuchonga na matumizi haziko wazi sana na wala hazionekani mara nyingi ili kuweza kudhihirisha kwamba njeya hizo kweli zilikuwa zimechongwa. Hata hivyo hizo njeya zipo, na ukweli kwamba huenda zilitumiwa na Kenyapitheko wikeri hauwezi kukataliwa kabisa.

Suala linalojitokeza ni jinsi ya kumtofautisha nyani na binadamu. Kwa sasa, tatizo la chanzo cha tasnia ya mifupa na ile ya mawe ni moja. Hakuna ushahidi zaidi wa kiteknolojia wala wa kimofolojia unaoweza kupatikana. Kadiri tunavyorudi nyuma kuufuata wakati, ndivyo inavyokuwa vigumu kuwa na hakika kwamba alama fulani zilifanywa kwa kazi au uchongaji wa mawe. Kwa hiyo, kwa sasa haiwezekani kuonyesha chimbuko lake halisi.

Kwa mwanahistoria wa Afrika wa kipindi kabla ya historia zana za mifupa na mawe zinathibitisha ukuaji wa ubongo wa binadamu ambao ulikwishaanza miaka milioni 2.5 iliyopita.

## Faharasa

*Abbeville* Eneo la changamano ya tasnia lililolezwa na H. Breuil huko Abbeville katika bonde la Somme kaskazini mwa Ufaransa. Changamano hii inatambuliwa kwa zana za nyuso mbili zilizochongwa kwa jiwe gumu ili kubandua ujeya. Changamano hii iliifanuliwa huko Ulaya ambako inalingana na mwanzo wa enzi ya Paleolithi ya kale. Pia tazama *Chelles*.

*Ajite* Mchanganyiko wa madini kama vile silikati ya kalisi magnesi na chuma (feri) yatumikayo kufanyiza mawe meusi.

*Amazoni* Aina ya mikrolini ya kijani.

*Amiri* Matukio ya kurudiarudia ya kontinenti yaliyotokea huko Moroko sawia na kipindi cha Mindeli cha Ulaya.

*Anfa* Inatokana na Anfa nchini Morocco. Uvamizi wa tatu wa maji ya bahari uliotokea katika kipindi cha miaka ya karibuni luko Moroko.

*Asheuli* Inatokana na Saint Acheul katika bonde la Somme, kaskazini mwa Ufaransa. Hili ndilo eneo la changamano ya tamaduni ya enzi ya Paleolithi ya kale na ilidumu tangu enzi za barafuto la Mindeli mpaka mwisho wa enzi ya Barafuto ya Riss-Würm. Zana inayojibainisha na enzi hiyo ni ile yenye nyuso mbili ambayo ni linganifu zaidi kuliko zile za Abbeville kwa vile ilichongwa kwa nyundo laini iliyotengenezwa kwa mti au pembe.

*Ateri* Inatokana na Bir el Ater, Mashariki mwa Algeria. Tasnia ya Kipaleolithi ya Afrika Kaskazini kati ya *Musteri* na *Kapsi*. Ni tasnia ambayo ina zana za chonge zenye ncha kali na vikombo na pia chonge zenye umbo la jani. Tasnia hii iliendelea wakati wote wa kipindi cha Würm na huenda sehemu yake fulani ilitokea sawia na enzi ya Paleolithi ya nyuma huko Ulaya.

*Atlanthropo* Kisukuku cha kikundi cha *Archanthropo* (*Archanthropus*) kilichofafanuliwa na C. *Arambourg* katika eneo la Ternifine nchini Algeria. Umri wake unakadiriwa kuwa mwishoni mwa zama za Pleistosini ya Kale.

*Auryaki* Inatokana na Aurignac, iliyo katika sehemu ya juu ya mto Garonne, Ufaransa. Hii ni tasnia ya kipindi kabla ya historia iliyoanza mwanzoni mwa enzi za Paleolithi ya Kale. Jina hili lililobuniwa na H. Breuil na E. Cartailhac katika mwaka 1906 hutumika kuelezea tasnia zilizopangwa kikronolojia kati ya enzi za Muster ina za Perigodi. Tasnia hizo hubainishwa na vigumba vya mikuki vilivyotengenezwa kwa pembe za paa, vikombo vinene, mabamba marefu yaliyojengwa vizuri, na baadhi ya patasi za kukatia nakshi. Tasnia hii pia ilishuhudia kazi za kwanza za kisanaa, ambazo zilikuwa na vijisanamu vya wanyama na alama nyingine ndogondogo zilizochorwa kwenye mawe ya chokaa. Enzi hiyo ilitokea yapata miaka 30,000 iliyopita.

*Australopitheko* (kutoka katika neno la Kilatini *australis*: a kusini na Kiyunani *pithekos*: Nyani). Neno la jenasi lililobuniwa na Dart mnamo 1924 kuelezea visukuku mbalimbali kutoka Afrika Kusini vyenye sifa ya Kisimia, lakini vikiwa na sifa kadhaa za kibinadamu. Uvumbuzi wa aina hiyohiyo ulifanywa baadaye Afrika ya Mashariki na ya Kusini

*Basanti* Mwamba wa Kivoikano.

*Bresia* Mwamba wenye mawe ya kawaida yaliyochanganywa pamoja na chokaa n.k.

*Buchari* Kifaa kikubwa cha ujeya chenye ncha kali ya kukatia kilichotengenezwa kwa kugonga mawe mawili. Ni cha asili ya Asheuli ya Afrika, lakini kilipatikana pia katika kipindi cha mwanzo na kati cha tasnia za Paleolithi katika maeneo mbalimbali huko kusini mwa Ufaransa na Hispania.

*Chadanthropo* (mtu wa Chad) Kisukuku cha Hominidi kilichowekwa kianatomia kati ya vipindi vya Australopitheko na Pithekanthropo.

*Diabasi* Mwamba wa jamii ya gabbro na dioriti, kwa kawaida mi wa kijani.

*Dioriti* Mwamba wenye chembechembe zinazokwaruza.

*Diskoidi* Zana ya jiwe ya kipindi cha mwisho cha Asheuli iliyochongwa pande zote mbili.

*Doleriti* Mwamba wa jamii ya gabbro wenye madini yanayoweza kuonekana kwa macho.

*Eneolithi* (Kutokana na Kilatini: *aneus*, shaba nyeusi, na Kigiriki *lithos*: jiwe). Kipindi kabla ya historia ambamo shaba ilianza kutumika kwa mara ya kwanza.

*Eosini* Kipindi cha kwanza cha Enzi za Tatu, miaka milioni 65 hadi 45 iliyopita.

*Epidoti* Madini ya siliketi asilia ya alumini, kalisi na chuma.

*Fauresmithi* Jina la mahali katika Orange Free State huko Afrika Kusini. Tasnia ya lithiki yenye vikombo na ncha zilizochongwa ukingo mmoja, nyuso mbili na mashoka madogo, na inayo wiana na Paleolithi ya Kati huko Ulaya.

*Galena* Sulfide asilia ya risasi

*Gambli* Kipindi cha IV cha mafuriko Afrika kilichobainishwa katika eneo la maziwa ya Nakuru, Naivasha na Elementeita huko Kenya. Kilitokea wakati ule ule wa kipindi cha Würm, lakini istilahi hii hivi sasa haitumiki.

*Gunzi* Kutoka katika jina la into huko Ujerumani. Kipindi cha awali cha barafu ya Kwatenari katika milima ya Alps.

*Harunia* Mafuriko ya nne ya bahari ya kipindi cha Kwatenari huko Moroko ya Atlantiki.

*Hematiti* Oksaidi asilia ya feri.

*Holosini* Kipindi cha karibuni kabisa cha Kwatenari kuanzia miaka 10000 iliyopita.

*Hominidi* Familia ya wanyama wa kundi la mamalia wa tabaka la juu, wanaowakilishwa na visukuku na binadamu wa sasa.

*Homo Jina* la jenasi katika uainishaji wa makundi ya wanyama lililotolewa kwa visukuku (vya watu wa kale) na binadamu wa sasa.

*Homo habilisi* Jina lililobuniwa na Leakey, Tobias na Napier kuonyesha visukuku ambavyo kiwango chake cha mabadiliko ya kianatomia kiko katikati ya Australopithecini na Pithecanthropi.

*Homo sapi* Istilahi hii ilibuniwa na C. Linnaeus katika mwaka 1735 na sasa hutumika kuonyesha wasifu wa binadamu wa leo, ambaye kwa kutumia akili yake amefikia hali ya kujinasibisha na mazingira, hali ambayo humwezesha kufikiri na kutafakari.

*Homofaberi* Binadamu mtengeneza zana.

*Ibero-Maurusi* Changamano ya tamaduni katika Maghrib ya enzi ya Paleolithi ya Nyuma na iliyofuatia, enzi ambazo maendeleo yake yalibainishwa kwa kuongezeka sana kwa idadi ya mikrolithi na zilidunni kuanzia miaka 12,000 hadi 7,000 iliyopita.

*Jaditi* Madini ya asili ya "alumini-silikati" ya natiri, na kiasi kidogo cha kalisi, magnesi na chuma (feri).

*Jasperi* Kalisidoni ghafi yenye vijistari au vibaka vyekundu kwa jumla.

*Kabla ya Kambria* Kipindi cha zamani kabisa cha umbo la kijiografia. Kilidumu tangu dunia ilipotokea (yapata miaka milioni 4000 iliyopita) hadi wakati wa enzi za mwanzo (miaka milioni 500 iliyopita).

*Kabla ya Soltani* Kipindi cha kikontinenti cha Moroko kinacholingana na mwisho wa kipindi cha Riss kilichotokoa kabla ya kile cha Soltani (kutokana na Dar-es Soltan).

*Kafu* Inatokana na mto Kafu nchini Uganda. Changamano ya tasnia iliyokuwepo Afrika Mashariki tangu mwanzoni mwa enzi za paleolithi ya kale. Tasnia hiyo imebainishwa na kuwako kwa mbwe bapa ambazo zilichongwa pasipo kusawazishwa. Kuna ubishi kama tasnia hiyo ilianzishwa na binadamu.

*Kagera* Inatokana na mto Kagera nchini Tanzania. Hiki ndicho kipindi cha kwanza cha mvua barani Afrika kilichotambuliwa na E.J. Wayland katika mwaka 1934. Kilitokea wakati mmoja na kipindi cha barafuto la Gunzi kwenye milima ya Alps. Istilahi hii haitumiki tena.

*Kainozoiki* Kisawe cha kipindi cha Tatu na cha Nne (Kwatenari) kuanzia kipindi cha Eosini (miaka milioni 65 iliyopita) na kufuatiwa na kipindi cha oligosini (miaka milioni 40 iliyopita), kipindi cha Pliosini (miaka milioni 11 iliyopita), kipindi cha Pleistosini, na kipindi cha sasa.

*Kalabria* Kutoka Calabria, kusini, mwa Italia. Hatua kongwe kabisa ya Kwatenari kama ilivyobainishwa na M. Gignoux mnamo 1910.

*Kalisidoni* Aina ya silika ya nyuzinyuzi inayotokana na kwatzi na opali.

*Kalsite* kalisi ya Kaboneti asilia iliyogandishwa ipatikanayo katika chokaa, marumaru nyeupe, alabasta, n.k.

*Kamasia* Inatokana na Kamasia nchini Kenya. Hiki ndicho kipindi cha pili cha mvua barani Afrika na hujulikana kama Kamasia I. Kilitokea wakati mmoja na kipindi cha barafuto la Mindeli cha Ulaya. Istilahi hii hutumika kwa nadra sana.

*Kanjera* Inatokana na Kanjera nchini Kenya. Hiki ndicho kipindi cha tatu cha mvua barani Afrika na kilifafanuliwa na L.S.B. Leakey. Kinajulikana hasa kwa jina la Kamasia II. Kilitokea wakati mmoja na kipindi cha barafuto la Riss katika milima ya Alps, lakini istilahi hii haitumiki tena.

*Kapsia* Kutoka Kapsa, jina la Kilatini la Gafsa, huko kusini mwa Tunisia. Tasnia ya Paleolithi ya nyuma ya Kiafrika iliyotambuliwa na J.de Morgan. Vifaa vya Paleolithi ya Juu vinapatikana pamoja na idadi kubwa ya Mikrolithi na inatobolea madogo manene.

ambayo labda yalitumika kwa kutobolea mashimo katika vipande vya magamba ya mayai ya mbuni ili kutengeneza mikufu. Tasia hii ilikadiriwa kuwepo kiasi cha miaka 1100 iliyopita.

**Kamelia** Kalisidoni nyekundu.

**Katarrina** Nyani wa kale duniani wenye meno 32 na utando mwembamba.

**Kerkopitheko** (kutoka katika Kiyunani: kerkos: mkia na pithekos: Nyani) Nyani wa Afrika mwenye mkia mrefu.

**Klaktonia** Kutoka Clacton-on-sea Uingereza. Tasia ya Paleolithi ya chini iliyoelezewa na H. Breuil mwaka 1932 na chenye njeya za flinti zenye sura pana na inayoteleza. Klaktonia inaonekana kuwa ya wakati ulc ule na Asheuli.

**Lapi Lazuli** Jiwe la rangi ya buluu nzito litumikalo katika kutengeneza mawe ya mapambo (*nosais*), ambapo unga wake hutumiwa kutengeneza rangi ya samawi nzito.

**Lateriti** (Inatokana na Kilatini Later: "tofali"). Udongo wa kahawia nyekundu au wekundu mng'avu wenye oksidi ya chuma na *alumini* uliofanyika kutokana na kuchujika kwa udongo wenye rutuba kulikosababishwa na tabia ya hali ya nchi ya joto.

**Levallois** Inatokana na Levallois-Perret, Ufaransa. Mbinu ya kutengeneza mawe inayowezesha njeya zenye umbo lililokusudiwa kwa kutumia kiolezo.

**-a Levallois** Changamano ya tasnia iliyofafanuliwa na H. Breuil katika mwaka 1931. Tasia hii hubainishwa kwa njeya zilizotengenezwa kwa violezo vya aina ya Levallois bila kuhitaji marekebisha mengi. Kwa sasa tasnia hii haikubaliki tena kuwa halisi.

**Lidianiti** Mawe ya sleti.

**Lupemba** Inatokana na Lupemba, Kasai, nchini Kongo. Changamano ya tasnia ya Paleolithi ya Nyuma ambayo imebainishwa na mchanganyiko wa zana kubwa za mawe yaliyochongwa (stururu na patasi) na chonge za umbo la jani zilizochongwa pande zote mbili. Zana hizo ni za umri wa takriban miaka 8,000 kabla ya enzi zetu.

**Maarifi** Kutokana na Maarif nchini Moroko. Uvamizi wa pili wa maji ya bahari uliotoka katika kipindi cha miaka ya karibuni katika selimu ya Morocco inayotazamana na bahari ya Atlantiki.

**Magosi** Kutokana na Magosi, nchini Uganda. Tasia ya mawe iliyogunduliwa na Wayland katika mwaka 1926. Ilistawi kati ya enzi ya Gabli na Makali na ilikuwa na mchanganyiko wa vitu vyenye umbo la zana za Musteri kama vile violezo, visahani na chonge, vipande vyenye umbo la jani vilivyochongwa pande zote mbili na mikrolithi za kijometri.

**-a makali-kuwili** Zana ya jiwe iliyochongwa katika pande zake mbili na kuwa na umbo la lozi. Mwanzoni zilitwa 'vichanjio' na baadaye 'shoka la mkono' na inaolekea kwamba ilitumiwa kukatia na kwa kiasi fulani kukwangulia. Zana hizi ndizo zilizotumika zaidi katika kipindi cha Paleolithi ya Chini.

**Makalia** Kutokana na mto Makalia nchini Kenya. Hiyo ilikuwa hali ya unyevu katika enzi Kwaternari Kusini mwa Afrika na ilitokea wakati mmoja na enzi zilizofuatilia barafuto kule Ulaya. Istilahi hii haitumiki tena.

**Malakiti** Madini ya kijani ambayo hutumiwa kama kaboneti ya kuanzia wakati wa utengenezaji wa shaba nyekundu (kupri).

**Mazeri** Kipindi cha kwanza cha mvua nyingi cha Sahara sawa na kile cha Kagera.

**Mesolithi** (Kutokana na neno la Kigiriki *Mesos* yaani 'katikati ya'; na *lithos* yaani "jiwe"). Neno hilo lilitumika kwa siku nyingi kueleza changamano za kitamaduni ambazo ziliwczekana kupungwa kati ya enzi za Paleolithi na Neolithi. Changamano hizi sasa huhusishwa zaidi na hatua iliyofuatia kipindi cha Paleolithi.

**Mikoki** Ni enco la kipindi kabla ya historia lililoko kaskazini mwa *Les Eyzies*, kilometa 25 kaskazini-magharibi ya Sarlat katikati ya Ufaransa. Enco hilo ndilo lililoanzisha tasnia ya Mikoki

ambayo ilikuwa ni mwendelezo wa ile ya Asheuli iliyotokea wakati mmoja wa barafuto la Würm.

*Mindeli* Jina la mto katika Bavaria. Barafuto ya Milima ya Alps ya kipindi cha pili cha enzi ya miaka ya karibuni, kipindi kinachokadiriwa kuwa kilitokea kati ya miaka 300,000 na 400,000 iliyopita.

*Miosini* (Inatokana na Kigiriki *Meon* — 'pungufu' na *Kainos* — 'a karibuni'). Yaani kipindi kina maumbo machache mapya kuliko wa mfumo uliokifuatia. Kipindi hicho na kile cha enzi za kipindi cha tatu na ufanyikaji mianiba kilichotokea kati ya miaka milioni 25 na milioni 10 iliyopita.

*Muluya* Inatokana na bonde la Moulouya, nchini Morocco. Istilahi hii ilitumiwa na Biberson. Hiyo ni selemu ya kati ya Villafransiani ya Moroko.

*Musteri* Inatokana na Musteri, Dordogne, Ufaransa. Tasia ya kipindi kubla ya historia ya maandishi iliyotokea katika enzi za kati za paleolithi, na ambayo ilienea sana katika kipindi cha nusu ya pili ya enzi za mwisho za barafuto. Ilitambuliwa na E. Lartet katika mwaka 1865 na inabainishwa na idadi kubwa ya chonge na vikombo vilivyopatikana kwa kuchonga njeya upande mmoja tu.

*Nakuru* Kipindi cha unyevunyevu kilichobainishwa na kuwapo kwa mashapo kwenye tabaka za pwani ya Ziwa Nakuru nchini Kenya chini ya kina cha mta 102. Tabaka hizo zimeonyesha kuwako kwa tasnia za mtindo wa Neolithi zilizofanyika yapata miaka 3,000 iliyopita.

*Neanderthal* Inatokana na jina la bonde lililoko Dussel Basin katika Ujerumani ambapo kielelezo cha kwanza kiligunduliwa na Dkt. Fuhlrott mnamo 1856. Kinawakilisha kundi maalumu la jenasi Homo lililoishi Ulaya Magharibi katika enzi ya Pleistosini ya nyuma na kutoweka ghafla bila ya kuacha kizazi.

*Neolithi* (Inatokana na Kigiriki *neos* - 'moya', na *lithos* - 'jiwe'). Huo ulikuwa wakati wa enzi za mawe ulioambatana na uzalishaji wa chakula (kilimo, ufugaji). Istilahi hii ilibuniwa katika mwaka 1865 na J. Lubbock.

*Obsidi* Jiwe lililogandamana lenye asili ya kivolcano ambalo lafanana na kioo cheusi.

*Oldowani* Inatokana na bonde la Olduvai kaskazini mwa Tanzania. Changamano yenye zana za kale za mawe (zana za mbwe) iliyogunduliwa na Katwinkel katika mwaka 1911. Ni katika changamano hii ndimo Leakey alitambua viwango kumi na moja vya zana za Olduvai I zinazolingana na zile za Chelles ya kale na Oldowani XI zinazolingana na zile za Asheuli VI, na pia zile zana za Levallois.

*Oligosini* Schemu ya pili ya kipindi cha tatu cha ufanyikaji miamba, tangu miaka milioni 45 hadi milioni 25 iliyopita.

*Osteodontokerati* Tasia ya kipindi kabla ya historia iliyotumia mifupa (kwa Kigiriki: *osteon*), meno (kwa Kigiriki: *odous*, *odontos*), na pembe (kwa Kigiriki: *Keras*, *Keratos*) iliyogunduliwa na R.A. Dart huko Makapansgat, Afrika ya Kusini.

*Paleolithi* (Inatokana na Kigiriki *Paleos* '-a zamani', na *lithos* 'jiwe'). Istilahi itumiwayo kuonyesha enzi ya mawe ambayo haikuwa na uzalishaji wa chakula. Ilibuniwa na J. Lubbock mwaka 1865.

*Paleozo* Sinonimia ya -a (kipindi cha) mwanzo.

*Paranthropo* Ni Australopitheko (*Australopithecus*) mkubwa aliyegunduliwa mwaka 1948 katika mashapo ya Plio-Pleistosini huko Kromdraai katika jimbo la Transvaal. Ni sawa na *Zinjathropo* (*Zinjanthropus*) na *Paraaustralopitheko* (*Paraaustralopithecus*). Kiumbe huyu wa zamani anaonyesha sifa nyingi za kinyani lakini, hasa katika umbo la meno yake, anafanana zaidi na binadamu kuliko anthropoidi wengineo.

*Pithecanthropo* (Mtu-nyani). Hivi ni visukuku vyenye sifa zinazokaribiana na zile za binadamu wa leo na ambazo zinaweza kuwaingiza katika jenasi ya Homo na sifa nyinginezo tofauti zinazomnasibisha na spishi nyingine. Kielelezo cha kwanza cha kiumbe huyu kiligunduliwa na E. Dubois nchini Java mwaka 1889. Kiumbe huyu huainishwa miongoni mwa spishi waitwao Homo erecto (*Homo erectus*).

*Platirini* Nyani wa ulimwengu mpya walio na meno thelathini na sita na septa pana.

*Pleistosini* (Inatokana na Kigiriki; *Pleistos*: '-ingi', na *kaionos* '-a karibuni'.) Mgwanyo mdogo wa kijiolojia wa kipindi cha Kwatenari ambao huanzia mwanzoni hadi sehemu kubwa ya kipindi hicho. Istilahi hii ambayo ilibuniwa na C. Lyell mwaka 1839, inalingana na vipindi vikuu vya barafuto vya enzi za Kwatenari vilivyotangulia kipindi cha Holosini ambacho kilianza miaka 10000 kabla ya sasa.

*Pliosini* Sehemu ya mwisho ya Kipindi cha Tatu cha ufanyikaji miamba kilichoanza miaka milioni 5.5 iliyopita na kumalizika miaka milioni 1.8 iliyopita.

*Pongidi* Jamii ya nyani wa aina ya anthropoidi miongoni mwao wakiwemo orangtangi (nyani anayefanana na binadamu, mwenye nywele nyekundu na hana mkia, apatikanaye Indonesia), sokwe-mtu, sokwe, na nyani mdogodogo ajulikanaye kwa jina la gibbon.

*Ramapitheko* Ramapitheko wikeri. Primata mila mimea na nyama wa enzi za Miosini, ambaye huenda alikuwa mzazi wa hominidi, aliyeishi kati ya miaka milioni 12-14 iliyopita. Aligunduliwa katika milima ya Siwaliks Kaskazini mwa India. Vielelezo vingine vya innyama huyo vilionekana huko China, Uturuki, Afrika (Fort Ternan) na Ulaya (Austria, Ufaransa, Ujerumani, Ugiriki, Hungaria na Hispania).

*Riss* Jina la mto katika Bavaria. Barafuto la milima ya Alps lililotokea kabla ya lile la mwisho wakati wa enzi za Kwatenari kati ya miaka 200 000 na 120 000 iliyopita.

*Sango Bay* Inatokana na Ghuba ya Sango katika Ziwa Victoria nchini Uganda. Ni changamano ya zana za mawe iliyogunduliwa na Wayland kunako mwaka 1920 na ambayo inabainishwa na vitu vilivyojengwa kwa kutumia mbinu ya Levallois, chonge kubwa, zana zenye nyuso mbili, na mashoka ghafi ya mawe yaliyotengenezwa kwa kiolcho. Eneo hili ni la kipindi baina ya Kamasia na Gambli.

*Sapentini* Silikati ya magnesi yenye maji.

*Saura* Inatokana na Saura, bonde la korongo katika schemu za Sahara ya Algeria. Hiki ni kipindi cha nne cha mvua katika jangwa la Sahara ambacho ni sawa na kile cha Gambli.

*Sheli* Mwamba tabaka wenye tabaka za silika-alumini ambao huweza kupasuka kwa urahisi kufanya njeya nyembamba.

*Shellea* Kutoka Chelles, Ufaransa. Tasnia changamani ya Paleolithi ya Chini ilichoelezewa na G. de Mortillet Jina la zamani la kipindi cha Abbevillian.

*Shoka la mkono* Kifaa cha jiwe chenye umbo la lozi kilichochongwa kingo zote mbili, kitumikacho kwa kuchimbia na kuchunia. Ni sawa na zana ya nyuso mbili (biface).

*Sinanthropo* (Inatokana na Kilatini: sinensis 'Uchina' na Kigiriki *anthropos* 'binadamu'. Hivi visukuku vyenye sifa zinazokaribiana na zile za binadamu wa leo na ambazo zinaweza kuwaingiza katika jenasi ya *Homo*, na sifa nyinginezo tofauti zinazowanasibisha na spishi nyingine. Eneo la Choukoutien, Kusini-Magharibi ya Beijing lilishughulikiwa tangu mwaka 1921 hadi 1939 na Dkt. Pei, M. Black, Padri Teilhar de Chardin na F. Weidenreich. Kisukuku hicho kimo katika kundi la spishi ya Homo erekto.

*Solutre* Inatokana na Solutre, Saone na Loire, Ufaransa. Tasnia ya kipindi kabla ya historia ya enzi za Paleolithi ya Nyuma inayobainishwa na visu vya mawe membamba sana. Zana asilia zilizochoongwa vizuri katika nyuso zote mbili.

*Stillbay* Inatokana na Stillbay, Cape Province, Afrika Kusini. Tasnia ya mawe iliyokuwa na mawe mengi yaliyochongwa na kuwa membamba kama yale ya Solutre nchini Ufaransa. Tasnia hiyo ilikuwepo wakati mmoja na ule wa enzi ya Gambliia.

*Tekiti* Kioo halisi chenye 'silika' na 'alunini' nyingi; huenda kilitokana na vimondo.

*Telanthropo* Istilahi ya jumla ya jamii ya viumbe iliyotumiwa na Broom na Robinson kutaja vipande viwili vya taya vilivyopatikana mwaka 1949 katika mashapo ya Swartkrans huko Afrika Kusini. Vipande hivyo vilikuwa na mofolojia inayofanana na Arkathropini (*Archanthropines*).

*Tensifti* Inatokana na bonde la Wadi Tensift, Magharibi ya Moroko. Hiki ni kipindi cha Kikontinenti cha Moroko kinachofanana na sehemu ya kwanza ya barafuto la Riss.

*Tschitolo* Istilahi iliyobuniwa kuonyesha changamano ya zana za mawe iliyogunduliwa Tschitolo, Kasai, Kongo. Hii ni changamano ya tasnia ya kipindi kilichofuatia Palclithi iliyobainishwa na zana kubwa iwapokuwa zilikuwa ndogo zaidi ya zile za Lupemba, na idadi kubwa ya vigumba vya mishale vilivyochongwa pande zote.

*Tufu* Mwamba mwepesi na laini unonyao inaji wenye asili ya volkano.

*Ugariti I* Kipindi cha pili cha mvua katika Sahara sawa na kile cha Kamasia.

*Ugariti II* Kipindi cha tatu cha mvua katika Sahara sawa na kile cha Kamasia.

*Utamaduni wa Mbwe* Hii ndiyo tasnia kongwe sana ya utengenezaji zana za mawe inayojulikana. Tasnia hii ilishughulikia hasa mbwe ambazo zilichongwa ili ziwe na ncha kali ya kukatia, kwa kubandua ujeya.

*Villafransa* Inatokana na Villafranca d'Asti, Piedmont, Italia. Kufanyika kwa tabaka za miamba ambako kunalingana na kipindi cha mabadiliko kati ya enzi za kipindi cha tatu cha ufanyikaji miamba na zile za kipindi cha miaka ya karibuni.

*Wiltoni* Inatokana na eneo la Wilton, magharibi ya Cape Province, Afrika ya Kusini. Tasnia ya mawe iliyofanyika yapata miaka 15 000 iliyopita. Tasnia hiyo ilihusika na utengenezaji wa vikombo vyenye umbo la inwezi inwandamo, mikrolithi la trapezodi na vitoboleo na vyombo vyenye pembe zenye meno. Huu ni utamaduni wa baadaye uliodumu hadi mwanzoni mwa utamaduni wa chuma.

*Würm* Inatokana na jina la ziwa na into katika Bavaria. Ndicho kipindi cha karibuni sana cha barafuto ya kwenye milima ya Alps katika enzi za miaka ya karibuni, kilichoanza miaka 75000 iliyopita na kuanalizika miaka 10 000 kabla ya enzi yetu.

Wanyama, binadamu na mimea huainishwa kwa mujibu wa spishi zao na spishi tofauti hujumuishwa pamoja katika jenera. Kazi ya mwanapaleontolojia ni kuzitambua jenera na spishi za viumbe vya zama zilizopita, kwa kuvichunguza visukuku, ili kutambua na kuzingatia mabadiliko ya viumbe yaliyotokea katika kipindi fulani.

Charles Darwin ndiye mwanasayansi wa mwanzo aliyetoa nadharia ya kisasa juu ya mabadiliko ya asili ya binadamu. Darwin ndiye aliyekuwa wa kwanza kueleza kuwa bara la Afrika ndiyo makazi ya mwanzo ya binadamu, na uchunguzi uliofanyika katika miaka mia iliyopita umedhihirisha usahihi wa mawazo yake. Vipengee vingi vya kazi iliyoanzishwa na Darwin vimethibitishwa. Kwa hiyo kufikiri kuwa mabadiliko ni jambo la nadharia tu ni fikra ambayo kwa sasa haina ukweli wowote.

Kwa kuzingatia mambo yaliyogunduliwa katika Afrika kwa kuchunguza visukuku vya miaka milioni tatu iliyopita jenera mbili, "Australopitheko" na "Homo" zimetambuliwa katika "Hominidi" kati ya jenera hizo katika rekodi ya visukuku ya miaka milioni 3 iliyopita Australopitheko alitoweka kabisa miaka milioni moja iliyopita, ambapo jenera ya pili, inawakilishwa na Homo sapi, spishi ya binadamu.


Je Australopitheko ndiye aliyemzaa Homo? Zamani jibu la swali hili lilikuwa ndiyo; lakini haiwezekani kuwa na hakika, na baadhi ya wachunguzi (akiwemo mwandishi wa makala haya) wanaelekea kuamini kuwa jenera hizi mbili zilitokana na mzazi mmoja ambaye alitofautiana nazo. Waandishi wengine wanaona kuwa jenasi ya *Homo* imetokana na Australopitheko wa awali ambapo waandishi wengine huwajumuisha hominidi hawa wote katika jenasi moja inayoonyesha tofauti kubwa za kimofolojia.

Ili kuitetea hiyo nadharia tete inayodai kuwa kulikuwa na jenera mbili tofauti zilizotokana na mzazi mmoja itahitaji kuangalia kila jenasi kulingana na jinsi kila moja inavyojinasibisha na mazingira na mtindo wake wa maisha pia, kwa kuanzia na viumbe wa zama za karibu zaidi ambavyo sasa vinawakilisha jenasi hiyo, na halafu kurejea nyuma, mpaka kufikia kwa wale ambao ndio chimbuko lao. Lakini kwanza itabidi kueleza, kwa ufupi, nafasi ya Afrika katika hadithi hii ndefu.

### *Afrika chimbuko la binadamu*

Ushahidi unaoonyesha macandeleo ya binadamu katika Afrika haujakamilika bado lakini kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita utafiti uliofanyika unaashiria kuwa Afrika ndilo bara ambapo





18.1 Afrika: maeneo muhimu ya hominidi (R. Leakey)

hominidi walitokea kwa mara ya kwanza. Hata hivyo, si hatua zote za maendeleo ya mabadiliko yao zimedhihirika katika vielelezo vya visukuku vilivyogunduliwa —kwa kweli kuhifadhika kwa vielelezo hivyo kunategemea kuwepo kwa hali maalumu ambapo mchanganyiko wa kikemikali wa udongo husababisha mifupa ya viumbe iwe migumu kabla ya kuanza kuoza. Visukuku vinavyofanyika kwa namna hii huweza kubakia vimezikwa, kwa muda usiojulikana, katika matope yaliyokusanyika kwa miaka mingi, isipokuwa kama mmomonyoko na mjongeo wa utando wa ardhi ukitokea na kuaababisha visukuku hivyo kuonekana na kuweza kuainishwa.

Sababu zinazofanya sehemu kubwa za bara la Afrika zisiweze kuonyesha kuwako kwa mabaki ya visukuku ilihali vinapatikana kwa wingi sana katika baadhi ya sehemu hizo katika sehemu nyingine, zinalhusiana sana na tabia ya hali ya nchi na hali za kijiolojia ambazo zimekuwa zikitokea katika nyakati mbalimbali.

Kwanza ni kuwa ukubwa wa bara lenyewe unaeleza kwa nini kuna tofauti kubwa za tabia ya hali ya nchi. Ikweta, milima na mabonde husababisha tofauti kubwa za tabia ya hali ya nchi. Tukiachilia mbali mabadiliko hayo ya tabia ya hali ya nchi, bara la Afrika daima lilikuwa pahala muwafaka kwa makazi ya binadamu, ambaye aliweza kwenda popote alipotaka ama katika latitudo au katika longitudo.

Isitoshе Afrika katika kipindi kabla ya historia ilishuhudia mabadiliko makubwa katika unyeshaji wa mvua, na mabadiliko hayo yaliathiri usawa wa majisafi katika chemchemi, maziwa, mito na kiasi cha maji yaliyomo ardhini. Kila mwaka maziwa ya Afrika ambayo awali yalikuwa madogo na yenye kina kifupi, yalipata matope katika fuko zake na kwenye midomo ya mito inayoingia katika maziwa hayo. Mtindo huo wa kupwa na kujaa kwa maji uliendelea kwa miaka mingi na ulisaidia kufanyika kwa visukuku na kuhifadhika kwa mabaki ya wanyama yaliyozikwa katika mashapo ya matope na mchanga uliorundikana ukingoni wakati wa mafuriko.

Kisha hasa katika Afrika Mashariki kulikuwa na jambo ambalo lilisaidia kugunduliwa kwa visukuku vya wanyama wa kipindi kabla ya historia: mijongeo ya utando wa ardhi. Katika enzi za Pleistosini na hasa katika miaka ya mwisho ya enzi hiyo, kulitokea mpasuko mkubwa wa ardhi unaojulikana kama Bonde la Ufa, unaotoka kaskazini hadi kusini ukipitia katikati ya Afrika Mashariki. Mpasuko huu uliathiriwa na mwinuko na mshuko wa safu za taka ambazo ni mjongeo unaohusiana na kupasuka kwa ardhi. Kutokana na mabadiliko haya, miamba ya kale iliyoshikamana sana na visukuku iliweza kutokeza nje. Zaidi ya hayo, mmomonyoko uliotokana na upepo na maji uliwezesha kugunduliwa kwa visukuku vya Hominidi. Hali hii ndiyo inayotokea katika bonde la Omo huko Ethiopia, ambapo matabaka ya mianba ya chini yenye upana wa mita elfu moja, huweza kuonekana kwenye miteremko ya milima. Kwa kutazama matabaka haya, kuanzia chini kabisa na kuendelea juu inaweza kukadiriwa kwamba ni umri kati ya miaka milioni 4 na milioni moja iliyopita.


Mwisho, katika Afrika Kusini mwa Sahara visukuku vya hominidi vilipatikana katika mapango na kwa baadhi ya wakati visukuku hivyo vilipatikana chini ya rundo la kifusi cha paa lililoangukia mapangoni. Mpaka sasa haijulikani kama mabaki haya yaliletwa katika mapango hayo na wanyama wawindaji au wanyama walao mizoga kama vile fisi au na hominidi wa mwanzo. Zaidi ya hayo, kutopatikana kwa mabaki ya wanyama katika stratigrafia inayoweza kutambulika ni jambo linalozidisha ugumu wa kukisia umri na viumbe hao.

Na hii ndiyo sababu utafutaji wa visukuku vya masalia katika Afrika umefanywa zaidi katika mabonde ya maziwa ya zama za kale, ambapo mashapo yalipasuka na kupanda juu, yakajitokeza kama ardhi iliyokauka. Huu ndio uwanja wa wanajiolojia na wanapalaentolojia. Hatimaye wanaakiojia nao huanza kuvishughulikia baada ya ushahidi kuhusu maisha ya hominidi kujulikana hususani ya zana zao, silaha, kambi na kadhalika.



18.4 *Australopitheko boisei*: Sura ya ubavuni mwa fuvu la kichwa kutoka bonde la Olduvai, Tanzania (OH5) (Makumbusho ya Taifa, Kenya).


18.5 *Australopitheko africana*: Sura ya ubavuni mwa fuvu la kichwa kutoka Koobi Fora, Kenya (KNM - Er 1813) (Makumbusho ya Taifa, Kenya).





18.2 *Homo habilis*: Picha ya ubavuni mwa fuvu la kichwa kutoka Koobi Fora, Kenya (KNM-ER 1470) (Makumbusho ya Taifa, Kenya).

18.3 *Homo erectus*: Sura ya ubavuni mwa fuvu la kichwa kutoka Koobi Fora, Kenya (KNM-ER 3733) (Makumbusho ya Taifa Kenya)



### *Jinasi ya Homo: Homo Sapi*

Aina tofauti za maisha yanayodhihirishwa na binadamu wa sasa, ambaye yumo katika spishi ya *Homo sapi*, yamerahisishwa na maendeleo ya kiteknolojia. Lakini aina hizo ziliweza kuonekana katika hali zote za mabadiliko ya *Homo sapi* wa mwanzo.

Katika Afrika kumekuwepo uvumbuzi muhimu mwingi ambao umeonyesha kuwa *Homo sapi* wa mwanzo aliishi katika bara hilo kwa muda wa zaidi ya miaka 100 000. Mtu wa 'Rhodesia' aliyeonekana mwaka 1920 huko Broken Hill katika Northern Rhodesia ya wakati huo (Zambia) anahesabiwa kuwa ndiye *Homo sapi* mkongwe kabisa aliyeonekana Afrika na inakisiwa aliishi takribani miaka 35 000 iliyopita. Mtu huyu amelinganishwa na Nenderthal kutoka Ulaya.

Kwa upande mwingine, mafuvu mawili ya binadamu yanayohusishwa na visukuku vya wanyama ambao waliishi katika zama za Pleistosini, yameonekana huko Kanjera, Kenya Magharibi. Umri wa makazi haya haujulikani kwa hakika lakini hivyo visukuku viwili vimeonekana kuwa vina uhusiano na *Homo sapi* ambao kwa umbo la mwili wanafanana sana na visukuku hivyo. Huenda waliishi miaka 200 000 iliyopita. Vipande vya fuvu vya tangu miaka 100 000 iliyopita, pia vimepatikana katika bonde la Omo huko kusini-magharibi ya Ethiopia.

Kwa hiyo, ingawa hakuna visukuku vingi vilivyogunduliwa kuhusu *Homo Sapi*, haitakuwa vibaya kufikiria, kuwa binadamu wa kale wa spishi hii walikuwa wametawanyika sana katika bara la Afrika na kwingineko ulimwenguni.

### *Jenesi ya Homo (kabla ya sapi): Homo erekto*

Aina ya *Homo* wa kabla ya *Sapi* inayojulikana sana ni ile ambayo imehusishwa na spishi zenye maumbo tofauti inayojulikana kama *Homo erekto*. Spishi hii ilitambuliwa awali kabisa huko Mashariki ya Mbali na Uchina, lakini aina hii imepatikana katika miaka ya hivi karibuni katika Afrika Kaskazini na Mashariki na labda katika Kusini mwa Afrika. Visukuku hivyo vimekisiwa kuwa na umri baina ya miaka 150000 na miaka 500000.

Kwa kuangalia anatomia ya *Homo erekto*, kiembe huyu alikuwa na miguu miwili iliyofanana na mguu wa binadamu wa sasa wenye dole gumba linalolingana na vidole vingine. Ukubwa wa ubongo wake ulikuwa kati ya setimita za ujazo 750 na 1000, ukilinganishwa na 1400 za *Homo Sapi*. Fuvu lake (*Homo erectus*) lilikuwa na vijituta viwili —kimoja kilikuwa juu ya macho yake, zilipotokeza nyusi, na cha pili kilikuwa juu ya ukosi, kikiashiria sehemu iliyohimili mfumo madhubuti wa misuli.

Maoni ya jumla ya kitaalamu yanahusisha shoka la mkono au tasnia ya Asheuli na *Homo erekto*. Aina hiyo ya pekee ya tasnia ya zana za mawe imeonekana Afrika, Ulaya na kwa kiasi fulani huko Asia. Hadi sasa haijulikana kwa hakika iwapo *Homo erecto* alikuwa hatua ya mwisho ya kukua kwa binadamu kabla ya kuwa *Homo Sapi*. Kwa hali hii pengine litakuwa jambo la busara kuliacha suala hilo kama lilivyo, mpaka itakapopatikana habari zaidi juu ya spishi hii.

### *Jinsi ya Homo (kabla ya sapi): Homo habili*

Mabaki ya viumbe vinavyohusishwa na ukoo wa homo lakini ambao uliishi mapema zaidi kuliko ukoo wa *Homo erekto*, kwa sasa yanapatikana Afrika ya Mashariki tu. Fasili ya spishi ya *Homo Habilis* imetokana na vielelezo vilivyopatikana katika korongo la Olduvai na pia kwa siku

za karibuni vimeonekana huko Koobi Fora pwani ya mashariki ya ziwa Turkana. Jinasi hii inaweza pia kupatikana Laetolil nchini Tanzania na Hadar katika jimbo la Afar nchini Ethiopia, ambapo vimepatikana vielelezo vilivyokuwa makini zaidi. Jinasi hii iliishi katika mbuga za majani zilizo katika kanda hizo angalau miaka milioni 1.7 iliyopita.

Sifa muhimu aliyokuwa nayo *Homo habilis* yaweza kusemwa ni kule kuwa na ubongo mkubwa kiasi hicho wakati huo wa kale ambao ulikuwa na zaidi ya sentimeta za ujazo 750 na fuvu lenye mfupa mwembamba, ambalo lilijipinda sana kwa kwenda juu, ikilinganishwa na Primata walioishi wakati huohuo. Meno ya kukatia yalikuwa makubwa lakini magego na masagagego yalikuwa madogo. Utaya wa chini unaonyesha kuwa na nguvu. Mfumo mzima wa taya ulikuwa wa duara na zilishabihwa za binadamu zaidi kuliko za manyani.

*Homo habilis* ambaye aliishi katika Afrika kwenye mazingira ya Savana (nyanda zenye majani) alikuwa pia mwindaji. Wanahistoria wa kipindi cha kabla ya historia wanafikiri kuwa *Homo habilis* alitengeneza zana za mbwe zilizopatikana katika maeneo mengi katika schemu hizo.

### Jenasi ya Australopitheko

Wakati ulcule ambapo *Homo habilis* alikuwa akiishi, na pengine mahali palepale, aliishi hominidi wa pili mwenye miguu miwili, anayejulikana kwa jina la Australopitheko.

Tatizo la kufafanua spishi ya *Australopitheko* halijafumbuliwa, lakini maoni ya mwandishi wa makala haya ni kuwa ushahidi wa spishi mbili katika jenasi hii unaweza kuthibitishwa katika maeneo tofauti. Spishi iliyo dhahiri zaidi, Australopitheko boisei *Australopithecus boisei* au (Australopitheko robusto) ina taya madhubuti sana, magego na masagagego makubwa yakilinganishwa na meno ya kukatia na chonge, ukubwa wa ubongo usiopungua sentimita za ujazo 550, na mifupa ya mgongo na ya shingo mikubwa sana ambayo inahimili misuli ya kutafunia chakula. Spishi hii ilienea katika sehemu kubwa kusini na mashariki mwa Afrika.

Spishi ya Australopitheko afrikana (*Australopithecus africanus*) inafahamika sana katika maeneo ya Afrika Kusini, na pia kutokana na visukuku kadhaa vinavyohusiana nayo katika Afrika Mashariki na ambayo kielelezo chake bora zaidi ni KNM-ER 181 kilichopatikana Koobi Fora nchini Kenya. Sifa zinazombainisha sana ni taya za wastani zenye magego na masagagego madogo, ukubwa wa ubongo wa sentimita za ujazo 600 au pungufu kidogo, na kukosekana kabisa kwa vijituta kwenye shingo. Kiunzi cha mwili wa spishi hii chaelekea kuwa ni sawasawa na kile cha Australopitheko boisei japokuwa ni kidogo na si madhubuti sana. Mojawapo ya sifa muhimu ya spishi hizi iliyo dhahiri zaidi ni ile sehemu ya juu ya mfupa wa paja: shingo la mfupa wa paja ni ndefu na imebinukia nyuma na sehemu ya juu ya mfupa huu au kichwa ni duaraduara. Sifa hii inamaanisha kuwa spishi hizi zilikwenda kwa miguu miwili. Spishi nyenbamba iliyoonekana Afrika Mashariki imefanana na ile ya Afrika Kusini ijulikanayo kama *Australopitheko Afrikana* ambayo inafanana zaidi na spishi za kaskazini.

Ni dhahiri kuwa maendeleo makubwa sana yamepatikana katika miaka hii ya karibuni katika kuthibitisha habari zilizopatikana kutokana na visukuku kuhusu hominidi wa mwanzo. Kuwapo katika Afrika Mashariki kwa spishi angalau tatu zilizoishi wakati huohuo, yaani katika enzi za Plio-pleistosen, ni jambo ambalo linaweza kuhakikishwa kwa kuzingatia mabaki ya kianatomia na ushahidi wa kitamaduni na kiteknolojia. Wazo hilo limefasiriwa kuwa ni matokeo ya viumbe vilivyokuwapo katika kipindi cha Pliosini na ambavyo vilikuwa na mabadiliko tofauti ya kukua, ambayo yaliendelea hadi kuingia katika mwanzo wa enzi za Pleistoseni. Ama kwa hakika Afrika

Mashariki pia imetoa zana za mawe zilizokuwa za zamani kabisa na alama za makazi ya kale. Maendeleo ya mara kwa mara yaliyofanywa kutoka zana za mbwca za *Australopitheko* na *Homo habilis* mpaka zana za kishoka cha pande mbili za *Homo erecto* yanaweza kuthibitishwa kwa ukamilifu katika eneo hilo.

Suala hili changamano (la kutaka kumfahamu binadamu na asili yake) linahitaji uchunguzi na mitaala ya wataalamu wengi wa jiolojia, *paleontolojia* na historia ya kipindi kabla ya historia.

# 19

## *Historia ya Afrika Mashariki ya kipindi kabla ya historia*

Kubadilika kwa binadamu na kuwa kiumbe aishiye juu ya ardhi na mwenye uwezo wa kukaa, kusimama na kujongea kwa miguu miwili tofauti na nyani au na wanyama wengine wa kundi la mamalia wenye miguu minne kuliwezesha utumiaji na utengenezaji wa zana kwa kuiachia huru mikono na viganja viweze kukamata, kubeba, kushika na kutumiwa kwa shughuli mbalimbali.

### *Kronolojia na uainishaji*

Ijapokuwa katika sehemu kubwa ya Bara la Asia, Ulaya, na kaskazini ya Afrika, Enzi ya Mawe imegawanywa katika vipindi vitatu yaani: Paleolithi, Mesolithi, na Neolithi, katika sehemu ya Afrika kusini mwa jangwa la Sahara mfumo huu haufuatwi na waandishi wengi wa kisasa. Katika sehemu hii ya Afrika, enzi ya mawe kwa kawaida hutazamwa na kuchunguzwa kuanzia mwanzoni kabisa katika vipindi vitatu vikuu: Kipindi cha Mwanzo, Kipindi cha Kati, na Kipindi cha Nyuma ambavyo hutofautiwa na mabadiliko muhimu na dhahiri ya kiteknolojia ambayo ni tofauti kabisa na yale ya kitamaduni na ya kiuchumi. Tofauti hizi za uainisho haziwakilishi njia mbili za kuelezea kitu kilekile, kwani vigezo vya kusinisha dhana na kronolojia ni tofauti kabisa.

Vipindi vitatu vya Afrika vimekisiwa kuwa vya tarehe zifuatazo:

*Enzi ya Mwanzo ya Mawe* (au Enzi ya Kale ya Mawe), kuanzia miaka milioni 3 hadi 100 000 iliyopita.


*Enzi ya Kati ya Mawe*: kuanzia miaka 100 000 mpaka 150 00 iliyopita.

*Enzi ya Nyuma ya Mawe*: kuanzia miaka 150 00 iliyopita mpaka mwanzo wa Enzi ya Chuma kiasi cha miaka 2000 iliyopita.

Ingefaa kuisitiza hapa kwamba tarehe hizi ni za makadirio ya jumla sana na zinazua mjadala mkali bado. Ama kwa hakika, tarehe nyingine za baadaye zaidi zimependekezwa kuwa ni vipindi vya mabadiliko kutoka Enzi ya Kati ya Mawe hadi kuingia Enzi ya Nyuma ya Mawe. Kwa sababu hizi, tarehe zilizopendekezwa hapa katika kugawa Enzi za Mawe katika vipindi, ni za kale zaidi kuliko zile ambazo kwa kawaida hutolewa. Zaidi ya hayo ni muhimu ijulikane kuwa mifutulizo hii ya nyakati isichukuliwe kama vipindi ambapo hakukuwa na mabadiliko yaliyokuwa yakitokea; au kuwa mabadiliko kutoka kipindi kimoja hadi kingine yalikuwa ya ghafla.

Maendeleo yalitokea katika kila mojawapo ya vipindi liavyo vitatu na pia kati ya kipindi kimoja na kingine. Zaidi ya hayo, dhana ya kipindi cha mpito kati ya vipindi viwili ni tata. Hii ndiyo sababu iliyofanya wanahistoria wengine waletе wazo la "vipindi vya kati" lakini siku hizi kuwa mwelekeo wa kutopendelea istilahi hiyo kwa kuwa haifanuliki waziwazi. Katika nyakati





- Early Stone Age (and Early-Middle Stone Age)
- ▼ Late Stone Age (and Late Middle Stone Age).

○ Land over 1,500m  
 500km

19.1 Afrika Mashariki: maeneo muhimu ya Enzi ya Mawe (J.E. G. Sutton)



zenye matukio muhimu za Enzi ya Mawe, aina mbalimbali za teknolojia huenda zilitumika kwa wakati mmoja, hata katika maeneo finyu. Tofauti hizi zaweza kuelezeka kutokana na tofauti za mazingira, ambapo chakula na njia za kukipata vilisababisha marekebisho ya kitamaduni na ya kiteknolojia. Hili ni suala lenye mjadala lakini ugunduzi wa hivi karibuni katika Afrika Mashariki unaonyesha kwamba kile kilichodhaniwa kuwa ni vipindi viwili tofauti vya Enzi ya Mwanzo ya Mawe Utamaduni wa Zana za Mbwe (utamaduni wa Oldovani) ukifuatiwa na utamaduni wa Shoka la Mkono ni tamaduni ambazo ziliingiliana kwa miaka nusu milioni. Zaidi ya hayo, nichanganyiko wa mawazo mapya na ya zamani huweza kuashiria mabadiliko ya kawaida lakini ishara za kipindi cha mabadiliko huenda zisifahamike barabara.

Katika jedwali 19.2, kielelezo kilichofafanuliwa kwa undani kimekwika ili kuonyesha jinsi tamaduni mbalimbali za Enzi ya Mawe na tasnia za zana za mawe zinavyotambuliwa na Wanaakiolojia wa Afrika Mashariki zinavyoweza kuingizwa katika mgawanyiko huu wa vipindi vitatu. Jedwali hili si lazima lichukuliwe kama kwenye ufafanuzi sahihi bali linaweza kubadilishwa kutokana na matokeo ya uchunguzi zaidi au mtazamo mpya wa kazi za zamani.

### *Enzi ya Mwanzo ya Mawe*

#### Awanu ya kwanza

Zana za kwanza kabisa zilizojulikana kuwa zilitengenezwa na binadamu zina umri kati ya miaka milioni tatu na milioni moja iliyopita na ziligunduliwa katika kingo za vinamasi na maziwa ya zamani karibu na Bonde la Ufa kaskazini ya Tanzania, Kenya na Ethiopia. Zana hizi zaweza kuwa vipande vidogo sana vya kwatzi vyenye kuonyesha dalili za kukatwa na kuchakaa, nazo zimepatikana katika maeneo mbalimbali karibu na Ziwa Turkana na katika bonde la Omo huko Ethiopia. Hata hivyo ni vigumu kusema kwa yakini zilitumika kwa kazi gani hasa. Zana za mbwe za wakati huo au baadaye kidogo zafahamika zaidi. Hizi zilikuwa mbwe za ukubwa wa kushikika mkononi ambazo ziligonganishwa na jiwe jingine, kutoa ujeya ili kutengeneza ala ghafi za kukatia. Kazi nzito kama vile ya kukata ngozi ya mnyama au kukata majani magumu, zilihitaji zana kubwa zaidi iliyoshikwa kwa mkono. Njeya nyembamba na zenye makali zingefaa zaidi kwa kazi nyepesi. Uchunguzi makini wa hivi karibuni wa zana hizi za mbwe umeonyesha kuwa kulikuwa na maendeleo zaidi ya kiteknolojia kuliko ilivyokuwa inadhaniwa hapo awali.

Watengenezaji wa zana hizo walikuwa wawindaji na wakusanyaji. Masalia ambayo yanaonkana hadi leo ni pamoja na mifupa ya wanyama iliyochanganyika na zana mbalimbali, jambo ambalo ni ushahidi wa kuwapo kwa maskani katika kipindi hiki cha mwanzo cha kuwapo kwa binadamu. Zaidi ya hayo uchunguzi wa namna zana hizi zilivyosambaa unaonyesha kuwa huenda huko Olduvai na Melka Konture kulijengwa vikingaupepo ambavyo vilitumiwa kulindia makazi.

Kutokana na umri wa zana hizi, na muhimu zaidi kupatikana mara kwa mara kwa zana hizi katika Afrika Mashariki pamoja na mifupa halisi ya binadamu, zana hizo zaweza kuhusishwa na hominidi wa mwanzo kabisa, Australopithecini au, kama ambavyo wanahistoria wengine wangesisitiza, zaweza kuhusishwa na kizazi chao *Homo habilis*.

#### *Awanu ya pili*

Utamaduni wa Asheuli (au wa shoka la mkono) umeenea sana Afrika sawa na ule wa Olduvai na inaeneo yaliyotambuliwa ni mengi zaidi. Hii inaweza kuwa imesababishwa na kuongezeka kwa

193 Kipindi Kabla ya Historia katika Afrika ya mashariki (J.E.G. Sutton)

Years ago (approx.)	Divisions	Diagnostic technological features	Main lithic industries	Rough equivalents in Mediterranean and Eurasian regions	Geological periods (approx. correlations)
3 million	EARLY STONE AGE (ESA)	chopper-tools and flakes	Oldowan (pebble-tool industry)		Lower Pleistocene
1 million	FIRST PHASE SECOND PHASE	bifacially flaked tools, cleavers, etc.	Acheulian (biface industry)	Lower Palaeolithic	Middle Pleistocene
100 000	MIDDLE STONE AGE (MSA)	flaked tools made from prepared cores	Sangcan	Fauresmith	Upper Pleistocene
40 000	FIRST PHASE SECOND PHASE	hafting; smaller, finished tools	Lupemban	Stillbay	
15 000	LATE STONE AGE (LSA)	blades and microliths with retouch; composite tools	Tschitolian	(Magosian) Wilton	Upper Palaeolithic
			Kenya Capsian 'stone bowl' cultures ('terminal LSA')	Kenya highlands	epi-Palaeolithic or Mesolithic Neolithic (in some parts)
of our era	IRON AGE				

watersides - forests  
highlands - savannahs

wakazi, au utengenezaji wa zana kubwa kama vile shoka la mkono na buchari. Kinyume na Oldowani, utamaduni wa Asheuli ulienca nje ya mipaka ya Afrika na kuingia bara la Asia na Ulaya pia. Utamaduni huu unafikiriwa kuwa ulianza Afrika zaidi ya miaka milioni moja iliyopita. Teknolojia ya aina hii iliendelea kwa zaidi ya miaka milioni moja hadi miaka ya hivi karibuni, labda kama miaka laki moja iliyopita.

Afrika ilikuwa sehemu mojawapo ambapo mtengenezaji wa zana hizi, *Homo erecto*, alitokeza. Hata hivyo, inaelekea kuwa utamaduni za kale zaidi na watu wa kale zaidi waliendelea kuishi pamoja na hawa "wanya" kwa kitambo fulani. Ushahidi unaonekana katika matabaka mbalimbali ya maziwa yaliyokauka katika bonde la Olduvai ambako kwa miaka elfu nyingi sana, zana zilizotambuliwa kuwa zilikuwa maalumu kwa Oldowani na Asheuli zilikuwa zikiundwa na kutumiwa.

Katika Afrika Mashariki, maeneo ya utamaduni wa Asheuli, mbali na eneo la Olduvai, yanapatikana huko Oloregasailie na Kariandusi katika Bonde la Ufa, Mashariki ya Ziwa Turkana, Nsongezi na maeneo yaliyo katika mpaka wa Uganda na Tanzania, huko Isimila na Lukuliro kusini mwa Tanzania, na huko Melika Konture katika Ethiopia.

Istilahi, "shoka la mkono" na "buchari" zana mbili zilizobainisha utamaduni wa Asheuli, zinatumiwa tu kuwasaidia wanaakiolojia. Mbinu za Kiasheuli za utengenezaji zana zilikuwa zenye usahili zaidi, za kawaida zaidi na zilikuwa na mtindo mmoja wa kutengeneza njeya za nyuso zote mbili kuliko mbinu nyingine zilizofahamika hadi wakati huo.

Katika kipindi chote cha Enzi ya Mwanzo ya Mawe, watu walikuwa wawindaji-wakusanyaji waliohamahama katika nyanda za majani na nyika wakiwinda wanyama na kukusanya vyakula. Inewahi kupendekezwa kuwa upatikanaji kwa wingi wa zana bora za Asheuli katika maeneo ya Isimila na Ologesailie ni dalili ya mjumuiiko wa watu hao katika sehemu hizo wakati wa sherehe za mwaka na za msimu.

Ushahidi wa kwanza kuhusu matunizi ya moto katika Afrika Mashariki, kiasi cha miaka 50000 iliyopita, unepatikana katika maeneo ya kiakiolojia ambayo yalikuwa na zana za Asheuli. Hata hivyo, tarehe hizo zaonekana kuwa za juzijuzi mno, kwani kuna ushahidi wa kuaminika wa dalili za matunizi ya moto na kupika, mambo yaliyofanywa na Homo erecto huko Asia na Ulaya, takriban miaka nusu milioni iliyopita.

## Enzi ya Kati ya Mawe


Watu walioishi katika Enzi ya Kati ya Mawe walikuwa wa spishi ya Homo sapi japokuwa huenda hapo mwanzo watu hawa walikuwa tawi dogo la Homo sapi ambao walikuwa tofauti kidogo na binadamu wa leo. Kufikia mwisho wa Enzi ya Kati ya Mawe binadamu wa kisasa, Homo sapi, hakuwa tu amekwishatoka bali pia tofauti za rangi kama zionekavyo sasa, zilikwishajitokeza bayana katika Afrika na penginepo.

### Maelezo ya 19.3

Safu mbili za kulia kabisa zinazoonyesha uwiano wa juujuu na wa vipindi vya kijiolojia pamoja na kronolojia ya Kipindi cha Paleolithi cha Mediterania na Ulaya na Asia (Ulasia) zimewekwa kwa ajili ya marejoo tu.



Istilahi 'Kale', 'Kati', na 'Nyuma' ambamo 'Kale' ina maana ya awali, hufuata desturi ya kawaida ya kijiolojia ambayo imekitwa katika mifuhulizo ya kistratigrafia.


Kama Jedwali linavyoonyesha, istilahi Paleolithi (au Enzi ya Kale ya Mawe) si kisawe cha Enzi ya Mwanzo ya Mawe ya Afrika. Istilahi Paleolithi itumikayo siku hizi huko Ulaya humaanisha 'Enzi ya Mawe isiyokuwa na uzalishaji chakula' tofauti na 'Neolithi' (au Enzi Mpya ya Mawe) yenye kumaanisha Enzi ya Mawe lityo na uzalishaji wa chakula kwa njia ya kilimo, na ufugaji. Enzi hii inahusisha ushahidi wa utamaduni wa vitu ulioendelea zaidi kama vile vyombo vya udongo na vifaa vya mawe.



19.4 Korongo la Olduvai, kaskazini mwa Tanzania. Korongo hili ambalo lina kina cha zaidi ya meta 100 na ambalo linapita katika tambarare linaonyesha mfuatano wa matabaka ya udongo (zaidi vikiwa vitalu vya zamani vya maziwa). Matabaka ya chini kabisa ambayo ni ya miaka milioni mbili iliyopita yana mabaki ya baadhi ya watu wa kale walioishi humo, zana zao (za Kiolduwani) na mabaki ya chakula. Matabaka ya juu yana mashoka ya mkono na zana nyinginezo za utamaduni wa Kiasheuli (J.E.G. Sutton)


19.5 Enzi ya Mawe ya Mwanzo, Awamu ya kwanza: Zana za asili (mbwe) za Kioulduwan (J.E.G. Sutton)






19.6 Enzi ya Mawe ya Mwanzo, Awamu ya Pili: Sura ya mbele na ya ubavuni ya shoka la mkono la Kiasheuli. 1) sururu 2) buchari 3) shoka (J.E.G. Sutton).

19.7 Isimila, nyanda za juu za Kusini mwa Tanzania-mahali hapo panapatikana kwa wingi mashoka ya mkono, buchari na zana nyingine za Kiasheuli: Kijisepeto kinachoonekana katikati ni cha kulinganishia (J.E.G. Sutton).






**19.8** Enzi ya Mawe ya Kati na jinsi zana zilvyoendelea kubadilika. Kielelezo chu zana ya nikono wa kulia ni zana yenye ncha kali inayofua katiwa katika mpini, labda kama ncha ya mikuki (J.E.G. Sutton)

**19.9** Olorgesailie iliyopo katika Bonde la Ufa la Kenya. Shughuli za uchiunbuji bado zinaendelea katika eneo la Kiasheuli (J.E.G. Sutton)







19.10 Enzi ya Mawe ya Mwisho: Zana ya kuparuru ifanunayo na ukucha wa dole gumba la mkono (juu) wenbe wenye makali kwa nyiena (kushoto), zana zenye umbo la mwezi-nwandamo iliyotengenezwa kutokana na obsidi katika Bonde la Ufa la Kenya (J.E.G. Sutton)

Katika uwanja wa teknolojia, kipindi hiki kilikuwa cha maendeleo makubwa. Utengenezaji wa zana za msingi, uliofanywa kwa kumegua njeya kutoka katika miamba ulikuwa ukipitwa na ufundi wa hali ya juu zaidi wa kutengeneza kwanza kiini cha ujeja cha kuweza kutengeneza zana kamili zenye umbo na ukubwa ulikusudiwa kabla ya kuubandua mwambani. Wakati huohuo ufundi huo ulikamilishwa kwa kupasua vibamba ambavyo baadaye vilichongwa vizuri na kutoa vifaa vidogo zaidi. Baadaye katika awamu ya pili ya kipindi hicho kulivumbuliwa ufundi ambao ulileta mabadiliko makubwa. Uvumbuzi huo ulikuwa wa kuwekea zana hizo mipini ya miti au ya vitu vingine. Zana za Stillbay ni mfano mzuri wa zana zilizowckewa mpini wa miti. Ufundi huu wa kuzichonga zana katika maumbo mbalimbali pamoja na kuzifanya kuwa bora zaidi ulirahisishwa kwa kuzitia zana katika moto kabla ya kuzishughulikia.

Wakati huohuo mabadiliko ya kiuchumi na ya kimazingira yalikuwa yakichukuana sambamba na maendeleo ya kiufundi ya kipindi hiki. Ilikuwa ni wakati huu pia ambapo mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi yahiathiri sana kupatikana kwa chakula. Inaweza kukisiwa, iogawa bila kudhibirishwa, kuwa ongezeko la idadi ya watu wakati huo lilisababisha kutafutwe njia bora zaidi za kutumia mazingira. Kwa uhakika njia hizi ziliumika wakati wa Enzi ya Kati ya Mawe. Hali hii ilisababisha kuzuka kwa shughuli mahsusi katika maeneo mbalimbali. Katika Afrika kulitokea migawanyo bayana ya kitamaduni baina ya watu walioishi katika nyanda za nyasi na nyika na wale walioishi katika maeneo ya mvua nyingi, yaliyokuwa na misitu minene. Wale walioishi katika nyanda za nyasi waliendeleza shughuli za uwindaji wa wanyama wakubwa kwa kutumia mikuki na wale wa msituni waliendeleza shughuli za ukusanyaji wa mboga na matunda na za uvuvi.

Katika nyanja za juu za Kenya karibu na ukingo wa msitu, zana za awamu ya kwanza ya Enzi ya Kati ya Mawe zijulikanazo kama "Fauresmith" zimekusanywa. Tasnia za Gondar na Graba III zilizoko Melka Konture zinahusiana na zana hizo. Kwa vyovyote vile, zana za Fauresmith ni za kiwango cha juu, zaidi ya ufundi wa Kiasheuli kwani ijapokuwa zinafanana ni ndogo zaidi na zimetengenezwa kwa makini zaidi pia.

Tofauti na zana hizi za Fauresmith ni zile za tasnia za Sango, ambazo zilitapakaa na ambazo mifano yake bora inapatikana katika maeneo ya Ziwa Viktoria na magharibi ya Bonde la Ufa kusini mwa Uganda, Rwanda na magharibi ya Tanzania. Tasnia hizi ni mchanganyiko wa zana za kiasheuli na ufundi mpya lakini msisitizo wake unatofautiana na aina ile ya Fauresmith. Zana za Sango zinalekea kuwa ghafi japokuwa hii haina maana ya kuwa utamaduni wao ulikuwa duni bali matumizi maalumu ya zana hizo ndiyo yaliyofanya ziwe hivyo. Kwa mfano huenda zilikusudiwa kuchongea miti.

Tasnia za Sango zilionekana kwa mara ya kwanza Afrika Mashariki zikiwa zimekwishaendelea na hii inaashiriwa kuwa huenda ufundi huo ulilingia sehemu za magharibi za Afrika Mashariki katika kipindi cha mvua nyingi wakati msitu wa ikweta ulipokuwa umevuka mipaka yake. Hata hivyo, katika awamu ya pili ya Enzi ya Kati ya Mawe, watengenezaji zana wa tasnia za Lupemba, ambazo zilisifiwa sana kwa mitindo inaalamu ya vigumba vya mikuki, walikuwa wanaislu katika mazingira ya msituni.

Zana nyingine za Lupemba zinapatikana kandokando ya Ziwa Viktoria na katika sehemu nyingine za magharibi za Afrika Mashariki hata katika bonde la Zaire. Zana hizo ni tofauti na zile za Stillbay ambazo vigumba vya mikuki yake vimechongoka mfano wa jani na ambazo zinapatikana katika nyanda za juu za nyasi zinazopakana na Bonde la Ufa huko Kenya na karibu na Ziwa Tana (sitara ya Gargora) na Diredawa (pango la Nungunungu) huko Etiopia. Katika maeneo mengine hasahasa kusini-mashariki mwa Tanzania, aina mbalimbali za tasnia za Enzi ya Kati ya Mawe zinapatikana kwa wingi. Baadhi ya tasnia hizi zinawakilisha kipindi cha mabadiliko kutoka aina moja ya tasnia hadi nyingine ambacho kinajulikana kama Sango-Lupemba.

## Enzi ya Nyuma ya Mawe

Badala ya kusisitiza utengenezaji wa ujeja kutokana na viini kama ilivyokuwa katika Enzi ya Kati ya Mawe, katika Enzi ya Nyuma ya Mawe msisitizo mkubwa ulikuwa kwenye utengenezaji wa nyembe kwa kupasua vipande laini vyembamba na virefu kutokana na mawe muafaka. Kisha nyembe hizo zilichongwa vizuri katika maumbo anuwai kwa matumizi mbalimbali. Kwa kawaida nyembe hizo zilikuwa ndogo sana zikijulikana kama 'mikrolithi', yaani vijawe vidogo vyenye urefu usiofikia sentimita moja. Umbo mojawapo maarufu la nyembe hizi lilijulikana kama 'mwezi mwandamo'; hili halikusudiwa kushikwa mkononi kama zana kamili bali lilikusudiwa kupachikwa mwenye vitundu vya mipini kwa mpangilio ili kutumika kama kisu au kerezo.

Kutokana na bidaa hizi za ki teknolojia yawezekana kukisia macandelco ya kitamaduni na ya kiuchumi wa wakati huo. Inaelekea kuwa katika kipindi hiki ndipo nyuta na mishale vilianza kutumiwa kuwindia. Mifupa ilitumiwa sana wakati huo na kugunduliwa kwa shazia za mifupa na mawe kunaonyesha kuwa ngozi zilishonwa pamoja kwa lengo la kutengeneza nguo au mahema. Shana za mbegu, mifupa, kaka za mayai ya mbuni au mawe zilitungwa pamoja ili kutengeneza vidani. Mawe ya kusagia yaliyotumika katika kipindi hiki cha Enzi ya Nyuma ya Mawe, yalitumika kupondea ngeu au bidhaa za mimea.

Baadhi ya makazi ya Enzi ya Nyuma ya Mawe yalikuwa katika nyanda tambarare karibu na maziwa au mito. Katika kipindi hiki pia kulikuwa na mapango mengi ambayo wakati mwingine yalitumiwa kama makazi na ambayo yalikuwa kwenye maeneo muafaka kwa shughuli za uwindaji au kwa usalama wa makazi. Katika eneo moja la Tanzania ya kati kaskazini, kuta za miamba za makazi haya zimerembwa kwa michoro ya picha za wanyama, mandhari za uwindaji na kazi nyingine za sanaa. Inawezekana kuwa usanii huu wa mapangoni ni milenia za hivi karibuni, yaani kuelekea mwishoni mwa Enzi ya Nyuma ya Mawe na baadhi ya sanaa hii huenda iliingiliana na kuenea kwa binadamu walioishi katika kipindi cha Enzi ya Chuana. Hata hivyo inaaminika kuwa chanzo cha sanaa hii ya uwindaji ni cha kale zaidi.

Uwezekano huu wa kuwapo tamaduni hizi za savana za Enzi ya Nyuma ya Mawe kwa muda mrefu kunaenea kueleza baadhi ya tofauti za kikanda zinazojumuishwa katika tasnia za Wilton. Zaidi ya hayo, katika sehemu za magharibi za Afrika Mashariki, inawezekana kupata desturi za pekee zinazohusiana na Bonde la Zaire ambapo tasnia za Tshitoli zilistawi. Desturi hizi zimetokana na utamaduni wa nyika na msitu wa Sango-Lupemba katika Enzi ya Kati ya Mawe. Hata hivyo uhusiano huo sio dhahiri isipokuwa katika Rwanda.

Nyanda za Juu za Kenya na bonde la Ufa vinaonyesha mambo tofauti kabisa na aina ya zana zilizoelezewa hadi sasa. Ni kweli kwamba baadhi ya tasnia za Enzi ya Nyuma ya Mawe zenye kufanana na zile za Wilton zinaonekana lakini kuna tasnia nyingine ambamo zana zenye nyembe ndefu badala ya zile za vijawe vidogo vimeonekana kwa wingi. Zana hizi zilikuwepo kati ya miaka 10 000 na 5000 kabla ya Kristo na zinajulikana kama zana za Kapsia ya Kenya. Ni muhimu kusisitiza hapa kuwa tasnia hii na watu walioishughulikia inawakilisha kundi la kusini-magharibi kabisa la utamaduni wa Wanegro uliotegemea sana matumizi ya maji ambayo yalitea sehemu yote ya Afrika, kusini mwa Sahara. Utamaduni huu ulitokea wakati wa kipindi kifupi cha mvua nyingi ambapo maziwa na mito vilifurika. Utamaduni huu ulifikia kilele chake katika kikwi cha saba kabla ya Kristo. Watu walioishi kando ya mito walivua samaki na wanyama wengine waishio majini kwa kutumia mikuki ya mifupa na chusa. Zana zao zimegunduliwa katika ziwa Edward huko magharibi ya Bonde la Ufa, Ziwa Turkana, na katika upwa wa awali wa Ziwa Nakuru. Watu wa wakati huo walijua kusuka vikapu na kufinyanga vyungu, na waliishi kandokando ya maeneo ya maji.

## *Enzi ya Neolithi*

Katika Afrika Mashariki, bado ni jambo ambalo halijathibitishwa iwapo wavuvi walioselea kandokando ya Maziwa Makuu mnamo milenia ya saba na ya sita na kuendelea, ndio walioanzisha ufugaji na labda pia kilimo. Inawezekana kuwa watu hawa walianzisha shughuli hizo kwa sababu za kimazingira, kama vile kuendelea kwa jangwa la Sahara, au labda kwa sababu ya maendeleo ya kiteknolojia. Hata hivyo inadhaniwa kuwa watu hao walipenda wazo la kukaa na kuzalisha chakula, liasa kwa njia ya ufugaji na kilimo, jambo ambalo lilizagaa katika enco lote kuanzia kikwi cha tatu na kuendelea.

Enco linalojulikana sana katika kipindi hicho ni Eshl Shaheinab nchini Sudani. Eneo hilo liko katika tungazi la kale kaskazini kidogo ya makutano ya *Blue Nile* na *White Nile*. Tasia ya zana za mawe zenye mawe madogomadogo yenye umbo la kijiometri, chusa zilizotobolewa chini na ndoana za kuvulia samaki zilizotengenezwa kwa kombe, ni ushahidi kwamba uvuvi ndiyo ilikuwa shughuli kubwa. Masalia ya zana hizo ni pamoja na mashoka ya mawe yaliyochongwa, tezo na vyungu. Masalia ya mifupa ni pamoja na ile ya wanyama wa porini, wengi wao wakiwa ni samaki lakini pia mbuzi na mara chache kondoo. Eneo la Shaheinabu, ambalo linakadiriwa lilikaliwa mnamo kikwi cha nne, linaonyesha kuwa ufugaji wa wanyama ulikwishitadi.

Huko Agordat, katika jimbo la Ertrea nchini Ethiopia, kuwepo kwa mawe ya kusagia, vinu na visanamu vya mawe vya ng'ombe wafananao na wale waliofugwa na Kundi-C la wakazi wa Unubi, kunaashiria kwamba kulikuwepo uchumi uliokitwa kwenye kilimo na ufugaji ingawaje ushahidi si thabiti.

Ijapokuwa ushahidi wa kuwapo kwa wakulima huko Menya bado haujapatikana, hata hivyo kuna ishara nyingi za kuonyesha kuwa wafugaji walikuwapo katika sehemu ya Bonde la Ufa ladi Tanzania na katika nyanda za juu pia. Kumepatikana masalia katika makaburi kama vile sehemu za kuchomea maiti huko katika pango la Mto Njoro karibu na Nakuru na pia katika pango la Keringet karibu na Molo. Makazi ya watu pia yamegunduliwa, kwa mfano huko katika Crescent Island karibu na Ziwa Naivasha, na huko Narosura kusimri mwa Kenya. Ushahidi wa kuwapo kwa wachungaji unaweza kuonekana kutokana na masalia mengi sana ya mbuzi na ng'ombe. Kupatikana kwa mawe ya kusagia na michi kunatoa ushahidi kwa mbali kuwa kulikuwako na kilimo wakati huo.

Kuanzishwa kwa ufugaji na ukulima katika Afrika Mashariki, ambako mara nyingi kumehusishwa na uchumi wa mseto, daima kumeelezwa kuwa kunatokana na athari mbili. Athari ya kwanza ni ile ya watu waliotoka sehemu ambayo sasa ni Sahara ya kusini wakielekea Unubi. Uwindaji na uvuvi uliendelea kama zainani na hapakuwapo na kupotea kwa utamaduni wa vitu wa vikundi vidogo vya wavuvi au vya wakusanyaji-wawindaji ambao walikwishaanza kuwa wakazi wa kudumu wa enco moja kufikia kikwi cha tatu. Kuna ushahidi kidogo wa kuwepo kwa kilimo, lakini inaelekea kuwa ufugaji wa ng'ombe ulianza kusitawi kutoka kipindi hicho na kuendelea. Enzi ya chuma ilipoanza, watu hawa wa Afrika Mashariki huenda walikwishaendelea zaidi wa wale wa kipindi cha kabla ya kilimo.

## *Utamaduni wa matumizi ya maji Afrika ya kati na mashariki*

Kiasi cha miaka ipatayo 8000–10 000 iliyopita tabia ya hali ya nchi ya Afrika ilikuwa ya umajunaji sana na hali hii ilisababisha mitindo wa maisha ambao ulihusiana sana na kuwako kwa maji katika msitu wa ikweta, uliokuwa mkubwa sana.

Kustawi kwa utamaduni wa wavuvi kandokando ya maziwa makuu ya Afrika Mashariki pamoja na Nili ya Kati na huko Sahara, kunakisiwa kuwa kulitokea kati ya miaka 8000 na 5000

kabla ya Kristo. Kugunduliwa kwa chusa za mifupa na vyungu kunaonyesha kuwa wakazi hao walijishughulisha na uvuvi. Zaidi ya hayo walijiongezea chakula chao kwa uwindaji na ukusanyaji. Hakuna ushahidi wowote uonyeshao kuwa walijihusisha na kilimo ama katika Afrika Mashariki au eneo lolote lile walimoishi.

Tangu takribani miaka 5000 kabla ya Kristo, athari za ukame uliocnca sana zilianza kuonekana. Maji ya maziwa yalipungua, na uehumi uliotegemea matunizi ya maji ulianza kufifia, ijapokuwa ulicndelea kwa muda mrefu zaidi katika Bende la Ufa, huko Kenya. Katika kipindi cha kati ya miaka 2000 na 1000 kabla ya Kristo, watu wapya waliwasili kutoka Ethiopia wakileta ng'oinbe, na labda utamaduni wa kilimo, pamoja nao.


# 20

## *Historia ya Kusini mwa Afrika ya kipindi kabla ya historia*

### *Hominidi wa mwanzo*


Kisukuku cha kwanza cha aina ya Australopithisini, kilikuwa cha kijana na kiligunduliwa mwaka wa 1924 katika kifusi kilichogandamana na chokaa, huko Taung kaskazini mwa Jimbo la Cape la Afrika Kusini. Kisukuku cha mtu mzima wa kwanza kiligunduliwa mwaka 1936 vilivile katika masalia ya zamani ya mapango huko katika eneo la Krugersdorp, Transvaal. Tangu wakati huo idadi kubwa ya visukuku vya Australopithisini na vya hominidi wengine vinconekana katika maenco ya kusini na mashariki ya Afrika. Mbali na maenco haya kisukuku kingine cha aina ya Australopithisini kilipatikana huko Korotoro katika bonde la Ziwa Chad. Hata hivyo kielelezo hiki cha Korotoro kinadhaniwa kuwa cha hivi karibuni. Ama kwa hakika, visukuku vingi vya aina ya Australopithisini vilivyopatikana hadi leo, vimetoka katika mapango ya Afrika Kusini na katika maenco ya Bonde la Ufa kwa sababu ya hali mwafaka zilizohifadhi mifupa ya visukuku. Katika Afrika Mashariki umri wa visukuku umejulikana kwa kutumia njia ya radiometa kwa sababu ya kuwako kwa mashapo ya volkano, lakini huko Afrika ya Kusini umri wa visukuku uliwca tu kukadiriwa kwa malinganisho ya kipalaeontolojia na ya jiomofolojia. Ukadiriaji wa umri wa hivi karibuni uliotokana na uchunguzi uliofanywa juu ya nguruwe, tembo na fisi unaonyesha kuwa visukuku vya mwanzo kabisa vya Transvaal ambavyo vinahusiana na wanyama hao vina miaka ipatayo walau milioni mbili na nusu. Miamba ya chokaa iliyo katika mapango ya machimbo ya chokaa huko Makapani na katika machimbo ya Sterfontein, ni masalia ya mamalia yanayofanana na yale ya wakati huohuo huko Afrika Mashariki.

Australopithisini wa kwanza kabisa huko Afrika Kusini walikuwa na umbo dogo na fuvu la sentimita za ujazo 450 hadi 500. Katika Machimbo ya baadaye ya mapango ya Swartkrans na Kromdrai, visukuku vilivyoshitadi huko ni vikubwa zaidi (*Australopitheko robusto*). Kwa muda mrefu ilidhaniwa kuwa visukuku vya awali vyote vilikuwa vidogo na vya baadaye vyote vilikuwa vikubwa lakini uchunguzi wa karibuni kiantropometa unaonyesha kuwa aina zote zilikuwa za wakati mmoja na binadamu hao waliishi na kukaa katika eneo moja la kijiografia kama machimbo ya Makapani katika Afrika Kusini yanavyoonyesha. Wanahistoria wengine wanaamini kuwa kutofautiana kwa spishi hizi mbili zinazotokana na mzazi mmoja kunawezekana kulitokea kama miaka milioni tano iliyopita. Kuna uwezekano nikubwa kwamba Homo wa mwanzo kama yule Homo habili wa Afrika ya Mashariki aliishi kusini mwa Afrika kati ya miaka milioni 2 na milioni 1.7 iliyopita ingawa mabaki ya visukuku vyake bado hayajapatikana.



20.1 Ramani ya maneno ya Asheuli Kusini mwa Afrika (J.D. Clark, 1970).

20.2 Ramani ya maeneo ya Fauresmith na Sango yaliyo Kusini mwa Afrika (J.D. Clark, 1970).



## *Maisha ya hominidi wa awali*

Ijapokuwa idadi kubwa ya visukuku vya hominidi wa Australopithisini vimepatikana katika mapango ya Afrika Kusini, haielekei kuwa mazingira vilimokutwa yanawakilisha mahali ambapo kweli hominidi hao waliishi. Uchunguzi makini katika eneo la Swartkrans umeonyesha kuwa kwa kweli kuwepo kwa lundo la masalia ya mifupa katika eneo hili kunaweza kuwa kumesababishwa na mambo mengi. Pengine sababu muhimu ilikuwa uwindaji wa wanyama walioishi kwenye mapango. Hata hivyo hapajakuwepo na makubaliano kuhusu hoja hii. Zaidi ya hayo hakuna zana zozote zilizokutwa miongoni mwa kifusi cha maeneo ya Makapani na ya Sterkfontein ambako visukuku hivyo viligunduliwa.

Kama nadharia tete ielezayo kuwa hominidi hao waliishi katika maeneo visukuku vilipogunduliwa haikubaliki na kuamini kuwa mapango hayo yalikuwa mahala wanyama wawindaji walipolia mawindo yao (ambamo hominidi walijumuishwa), basi inaelekea kuwa hao hominidi wa aina ya Australopithisini hawakuishi mbali sana. Hii ni kwa sababu zana za mawc zenye kukadiriwa kuwa za miaka milioni 1.5 iliyopita, zimegunduliwa katika kundi la mapango ya Sterkfontein (Swartkrans, Sterkfontein na Komdraai). Hata hivyo vipande vya masalia ya mifupa ya aina ya hominidi wa kisasa zaidi *Homo sapi* vimegunduliwa katika mashapo ya Swartkrans na inaelekea hominidi huyu ndiye anayehusishwa zaidi na zana hizo. Hata hivyo hii haina maana kuwa hominidi wa Australopithisini hakuwa na uwezo wa kutengeneza zana. Pengine uwindaji na ulaji wa nyama ulisababisha utengenezaji wa zana za mawe ili kupata njeya za kukatia nyama. Aidha huenda uwindaji ulihitaji mfumo bora wa uongozi na mawasiliano miongoni mwa wahusika, mambo ambayo baada ya muda yalizaa lugha.

## *Vifaa vya mwanzo vya mawe: changamano ya tasnia ya Oldowan*

Ingefaa ikumbukwe kuwa zaidi ya mawe, vitu vingine kama miti, magamba, pembe na mifupa yawezekana kuwa vilitumiwa kama vifaa. Kwa bahati mbaya, vitu vingine huoza haraka, hivyo uchongaji mawe ndipo mahala tutakapoanzia uchunguzi wetu.

Tasnia za kwanza kabisa za mawe za eneo la Kusini mwa Afrika zilitoa vifaa maalumu kabisa vya mawe kama vile vishoka, mawe ya nyuso nyingi, vikombo, ujeya na kadhalika. Ukilinganisha zana hizo na zile za Afrika Mashariki itaonekana kuwa hizo za Kusini mwa Afrika zilionyesha dalili za kufanana sana na zile zana bora zaidi za Oldowan kuliko zile za awali. Inakubalika sasa kwa jumla kuwa maeneo ya Afrika Kusini yalikuwepo kiasi cha miaka milioni moja na nusu iliyopita. Hadi kufikia wakati huo, kulikuwepo na aina mbili za hominidi: Australopithisini robusto na Homo wa hivi karibuni. Bado haijulikani ni aina ipi kati ya lizi ilianzisha tasnia hizo.

## *Changamano ya tasnia ya Asheuli*


Mikusanyo ya awali ya zana za Kiasheuli kusini mwa Afrika ilipatikana katika maeneo yaliyo katika makutano ya mto Vaal na kijito chake Klip karibu na Vereeniging. Zana hizo zimelika hivyo haziko katika hali yake ya asili. Kuna aina nyingi za zana kama vile mashoka ya mkono, buchari, mawe yenye nyuso nyingi, zana za mbwe, vikombo, na zana za ujeya. Kimegunduliwa pia zana zinazoelekea kuwa za zamani zaidi katika sehemu mbalimbali za Kusini mwa Afrika





20.3 Shoka la mkono la Kiasheuli ya Mwarizo na visaa viwili vya kuchanjia/kukatia nyuma kutoka Breccia ya Kufi, Sterkfontein (R. Mason, 1962).

20.4 Zana za Kiasheuli ya Nyuma kutoka maporomoko ya Kalambo, zana kubwa zilitengenezwa kutokana na kwatziti, zana ndogo zilitengenezwa kutokana na "cherti" 1. Kikomo mbonyeo 2. Kikombo mbinuko 3. Vikombo vyenye meno ubavuni 4. buchari zenye makali msambao 5. Kisu cha ujeya chenye makali yaityochongwa vizuri 6. Bucharu yenye makali sambamba 7. Shoka la mkono lenye umbo la mvingo ya 8. Zana yenye umbo la mvingo 9. Msharasi 10. Shoka la mkono lenye umbo la mvingo wa yai uliorefushwa. 11 Shoka la mkono lenye umbo la mkuki (J.D.Clack, 1970)



kama vile katika Jimbo la Cape na katika mji wa Livingstone huko Zambia, lakini hadi sasa imekuwa vigumu kukadiria umri wake. Inadhaniwa kuwa Homo erekto wa kusini mwa Afrika ndiye aliyehusika na utengenezaji wa zana hizi za kiasheuli, lakini hadi sasa visukuku vyake havijagunduliwa.

Ni kutokana na kupatikana kwa zana za baadaye, au zilizo bora zaidi, za Kiasheuli ndipo maeneo mengi yalipoanza kutokeza Kusini mwa Afrika ambayo yanaashiria kuongezeka kwa makundi wa hominidi. Hakuna hata moja ya maeneo haya ambalo umri wake umcweza kukadiriwa kwa usahihi kwa sababu maeneo yote hayo yako nje ya uwezo wa kukadiriwa umri wake kwa njia ya radiokaboni na kwamba miamba inayohusishwa na maeneo hayo haiwezekani kukadiriwa umri wake kwa kutumia njia ya potasi-goni.

Eneo lililo kaskazini kabisa ni lile la maporomoko ya Kalambo mpakani mwa Zambia na Tanzania ambapo masalia ya miti yamehifadhika vizuri sana na kuwa yanaweza kukadiriwa umri wake kuwa zaidi ya miaka 190 000 Kabla ya Kristo. Tarehe hii inawiana na ile ya Isimila, huko katikati ya Tanzania, na inaashiria kuwa Tasmania za Asheuli zilikuweco miaka 700 000 hadi 125 000 iliyopita. Shughuli nyingi za binadamu za maporomoko ya Kalambo zilifanyika kwenye kingo za mto. Ushahidi wa chavua unaonyesha kuwa hali ya hewa ilikuwa ya joto zaidi na mvua zilikuwa chache zaidi kuliko siku hizi. Hata hivyo, kuelekea mwishoni mwa kipindi cha Asheuli, kuna ushahidi kutokana na chavua na mabaki ya mimea unaonyesha kuwa hali ya hewa ilikuwa imepoa kidogo na kulikuwa na ongezeko la mvua, vitu ambavyo viliwezesha aina fulani za mimea kuota katika nyanda za chini zaidi kuliko inavyoota leo. Vifaa na zana mbalimbali za miti kama vile rungu, vijiti vya kuchimbia, vipande vya magome na masalia mengine, vyote viligunduliwa pamoja na inashoka ya mikono, buchari, njeya na vikombo ambavyo vyote vinatokana na tasnia ya zana za mawe kwenye eneo hilo. Baadhi ya maskani haya mapya yalitoa ushahidi mwingi wa matumizi ya moto. Zaidi ya hayo kumegunduliwa idadi kubwa ya matunda na mbegu zilizochemwa za spishi za mimea inayolika na ambazo bado zingali zinatunika katika Bonde la Mto Kalambo. Kwa vile inatunda ya mbegu hizo huiva mwishoni mwa kipindi cha kiangazi, inafikiwa kuwa sehemu hizi za kuishi za Kiasheuli ziliwakilisha kambi za majira ya kiangazi ambazo hutumiwa miezi ya Septemba na Oktoba.

Katika sehemu moja litwayo Mwanganda upande wa kaskazini-magharibi ya Ziwa Malawi inaelekea tembo mmoja alichinjwa na makundi matatu ya watu kwani mafungu matatu ya mifupa yalikutwa pamoja na zana bora zaidi za Oldowan.

Sehemu za makazi zilizopendelewa zaidi katika enzi ya Asheuli zilikuwa karibu na maji kama vile Dambos ambako wanyama pori walikuwa wakikusanyika na ambako maji yalipatikana daima. Sehemu mojawapo ya namna hii ni Kabwe (Broken Hill) karibu na mahali maarufu pajulikanapo kama *Kopje* ambako kulipatikana masalia ya fuvu la Homo rhodesia (*Homo rhodesias*). Kuna uwezekano kuwa huko Kornelia wanyama walifukuziwa katika matope ya Dambos na kuchinjwa.

Katika vichaka vya nyanda kama za Karoo katika Jimbo la Cape na huko Botswana, makazi ya Kiasheuli yalikuwa kwenye mabonde na maziwa ya kina kifupi ambapo yalikuwa yameenea wakati huo.

Binadamu wa Kiasheuli pia walipenda kuishi pwani. Hii imedhihirika mwenye matuta ya mchanga ya ufukoni katika eneo kubwa la False Bay huko Cape Hangklip ambako masalia yalionyesha kuwa chakula chao kilikuwa wanyama wa baharini na samaki.

Maeneo ya chemchemi pia yalikuwa maskani yaliyopendelewa kama vile eneo la Amanzi lililopo katika ukanda wa mvua za majira ya baridi kali kusini mwa Genge Kuu lililo karibu na

mji wa Port Elizabeth. Katika eneo hilo zilionekana zana zilizotupwa na ambazo zilikwisha kanyagwakanyagwa na tembo na wanyama wengine waliokuja kunywa maji hapo.

Hatimaye, mapango hayo pia yalicaliwa na binadamu wa Kiasheuli wa Kusini mwa Afrika. Pango la Hearth huko Makapani katika Transvaal ya kaskazini lilikuwa mojawapo ya mapango ambamo mlikutwa kipande cha masalia ya taya la kijana aliyefanana na binadamu wa Homo rodesia. Ndani ya pango hilo mlikutwa pia zana nyingi za awali na za baadaye za Kiasheuli.

Kipindi cha baadaye cha Akculi kusini mwa Afrika kilikuwa kati ya miaka 700000 na 200000 Kabla ya Kristo. Hata hivyo ili kipindi hiki kiweze kufahamika vizuri zaidi, uchimbuzi mwingine ufanywe katika maeneo mengi zaidi pia. Jambo hili litatoa mwanga zaidi kwa utatanishi uliopo kuhusu tasnia ya Kiasheuli kwani, ingawa kuna mikusanyo mingi iliyo na mashoka ya mikono na buhari, kuna mikusanyo mingine ambayo ni ya vishoka na vifaa vingine vidogo vya mtindo wa Oldowan. Zaidi ya hayo, mikusanyo mingine ilijumuisha zana hizo na kuongezea sururu na zana nyingine za kufanyia kazi nzito. Vilevile kuna aina nyingi za makazi na vifaa vya wawindaji hawa wa kipindi cha baadaye cha Asheuli.

### *Kipindi cha mwisho cha Asheuli au Fauresmith*

Baadhi ya mikusanyo imekwepo kwa muda kwenye uwanda wa juu wa bara. Sifa za zana za mikusanyo hii ni shoka ndogo za mkono zilizotengenezwa vizuri, vifaa vingi vya ujeya, vikombo vya viini na buhari chache. Mali ghafi iliyotumika ni mawe ya lidaniti katika sehemu ambapo mwamba aina hiyo unapatikana kwa wingi, lakini kwingineko mawe ya kwatzi yalitumika zaidi.


Katika mkusanyo huu, njia ya utayarishaji kiini inayojulikana kama mbinu ya kisahani cha kiini inayotoa ujeya ndogondogo nyingi, ni maarufu; kwa upande mwingine ile mbinu ya 'Levalois' inayotoa njeya mmoja mkubwa kwa kila kiini haikutumika. Tasnia hizi zimeitwa *Fauresmith* kutokana na eneo la Mto Orange ambako mashoka ya mkono ya umbo la lozi yalionekana kwa mara ya kwanza juu ya ardhi. Tasnia hizi zaelekea kuwepo baina ya miaka 115 000 na 80 000 Kabla ya Kristo.

Katika maeneo ya mvua nyingi na mimea iliyo karibukaribu, kipindi cha mwisho cha Asheuli hakifuatwi na tasnia ya Fauresmith bali na tasnia iliyozalisha sururu, mashoka na viini, vishoka na vikombo vya kiini. Changamano hii ya tasnia ya Sango inapatikana Zambia, Zimbabwe, sehemu za Afrika ya Kusini-mashariki na mwambao wa Natal. Mingi ya mikusanyo hii haikukadiriwa umri, lakini katika maporomoko ya Kalambo inwezekana kukadiriwa umri wa zana za Sango zilizopatikana pale kuwa zenye umri kati ya miaka 46 000 na 14 000 Kabla ya Kristo. Ugumu wa kupata uwiano wa tasnia za aina ya Sango umeongezeka kwa sababu za kiikolojia na nyinginezo, lakini uwiano kati ya zana za kazi nzito na sehemu zenye mvua nyingi na wingi wa mimea hauna budi kuzingatiwa.

Kwa hivyo, katika tasnia za Fauresmith na Sango, twaweza kugundua mianzo ya mgawaanyo mahsusi wa kikanda katika zana zilizotengenezwa unaoashiria ruwaza za kuchukuana na mazingira ya nyanda za nyasi tofauti na zile za nyika na misitu.

### *Enzi ya Kati ya Mawe*

Kati ya miaka 100 000 na 80 000 iliyopita, kiwango cha usawa wa bahari kilianza kushuka kutoka kile cha zamani cha kati ya mita 5 na 12. Muda mfupi baadaye mwanadamu alianza



20.5 Zana za enzi ya Lupenba ya "Kati" Maporomoko ya Kalambo, Rubble. 1 Eneo Bi, 1956:1 Kikombo chenye upande mmoja uliobinuka (cherti); 2 Kikombo chenye meno kilichopinda kwa mbele na ncha iliyochongoka (cherti); 3. Zana yenye kuchongwa upande mmoja (chert). 4 chombo cha kukatiza metali (dihedral burin) silcrete); 5 shoka la kiini (cherti); 6. Kikombo cha kiini (cherti); 7. Shoka la kukatiza nyama (kwatzi); 8 mkaiki (cherti)

20.6 Zana za utamaduni wa Kisango kutoka Bonde la Zambezi, upande wa juu. 1 na 2 ni surura; 3 na 8 ni mashoka ya viini; 4. Ni kisahani cha kiini; 5 na 6 ni zana za ujeya zilizotengenezwa kwa uzuri zaidi; 7 ni zana yenye unbo la tufe (J.D. Clark, 1950)



kutumia maeneo muafaka kwenye fuko zilizoachwa na katika mapango. Wakati huohuo ukame wa wastani ulioenea katika sehemu ya enco la ikweta, ulizua kuota kwa misitu ambayo polepole nafasi yake ilichukuliwa na nyanda za nyasi na nyika ambavyo vilisadifu makazi ya binadamu na wanyama pori.

Mbinu zilizotumika wakati huu ni mbinu ya Levallois na utengenezaji wa kisahani kiini kwa kutengeneza njeya na kuzifanya kuwa zana nyepesi kwa kuzigongagonga. Tasnia za wakati huu huko kusini mwa Afrika zinaweza kugawanywa katika makundi matatu makubwa kutegemea teknolojia iliyotumika kuzitengeneza.

Kundi la I hutambulishwa kwa njeya pana zilizotengenezwa kwa mbinu ya Levallois na mabamba marefu yaliyotengenezwa kwa kugongagonga. Ni makusanyo machache tu yaliyotawanyika ambayo yanafahamika na ambayo umri wake haujakadiriwa.

Baadhi ya makusanyo yanaelekea kuwa ya wakati mmoja na kundi I ingawa hayawezi kuhusishwa nalo. Kwa mfano, Florisbad, kwenye enco lenye umri wa miaka 48000 Kabla ya Kristo (tabaka I, la uozo wa mimea), kumegunduliwa tasnia ya njeya, vikombo, zana zenye nyuso nyingi, mafuawe na inawe ya kusagia yaliyotengenezwa kwa Doleriti. Katika tabaka hii hili kumegunduliwa ncha ya mkuki wa mti na masalia ya fuvu la kichwa cha binadamu. Huko Chavuma, Zimbabwe, tasnia hii imedhihirishwa na kuwepo kwa sururu na mashoka machache ya mkono na zana nyepesi kama vile sindano, vikombo, na nyembe zilizotengenezwa na chalisidoni, kifusi cha opali kwatzi na kwatzi. Tasnia ya *Twin Rivers* iliyo Zambia yeuye umri wa miaka ipatayo 2000 Kabla ya Kristo inafanana na tasnia ya Chavuma.

Kundi la II linajumuisha idadi kubwa ya makusanyo ya mapangoni na ya juu ya ardhi yenye umri unaokisiwa kuwa wa miaka 40 000 na 20 000 Kabla ya Kristo. Tasnia hizi zinadhihirishwa na matumizi ya mbinu mbili za kujeya, ile ya Levallois na ile iliyojulikana kama mbinu ya kisahani-kiini ambazo zote zilitumika kutengeneza njeya za pembetatu na idadi kubwa ya nyembe zinazotokana hasa na *kwatzi* na *lidianiti*. Zana hizi hupatikana katika maeneo ya mvua za majira ya wakati wa haridi kusini mwa Genge Kuu, kusini-magharibi ya Afrika, na katika Orange Free State na jimbo la Transvaal.

Kundi la III lina umri kati ya miaka 35 000 na 15 000 Kabla ya Kristo. Linapambanuliwa kutokana na idadi kubwa ya vifaa vilivyochongwa vizuri. Kwa jumla zana hizo ni ndogo na zinaonyesha kiwango kikubwa cha ubora wa uchungaji wake kuliko inakundi yaliyotangulia. Pamoja na makundi hayo matatu, Kundi la IV (inalofahamika kwa jina la *Magosi* au "Changamano Kati ya Pili") limeainishwa. Katika kundi hili inajitokeza aina ya matumizi ya mbinu za kisahani-kiini kwa kutengeneza vitu vidogo kama vile nyembe nyembamba zilizofanana na utepe kutokana na kiini kwa kutumia zana za mifupa, pembe na miti migumu. Mali ghasi iliyotumika ni miamba fuwele ya chini ya ardhi. Tasnia hizi za kundi la nne zimkuwepo kati ya miaka 15000 na 20000 iliyopita na zinapatikana Zimbabwe, Zambia, Mashariki ya Orange Free State, kusini mwa Cape Province na sehemu za Namibia.

Kwa kuchukulia tu kwamba makusanyo hayo ni ya namna moja, mwingiliano baina ya miaka iliyotajwa hapa, inaonyesha kuwepo kwa teknolojia iliyoendelea sana ya utengenezaji wa nyembe huko Afrika ya Kusini wakati mmoja na teknolojia ya ujeya ya kiasili wakati wa Enzi ya Kati ya Mawe. Hali hii huitofautiani na Afrika Kaskazini, ambako changamano za tasnia za wakati mmoja *Daba* na *Ateria* zinaonyesha tofauti za kikanda. Badala ya kutafuta sababu za hali hii katika uhamaji mkubwa wa wanadamu, ni vyeima kusisitiza uwezekano kwamba vikundi vilivyojitengatenga ambavyo viliishi katika mazingira ya namna moja vilianzisha ruwaza ya namna moja ya kujinasibisha na mazingira.

Katika jitihada za kuthibitisha wazo hili, ni muhimu kupitia kwa muhtasari ushahidi wa visukuku vya Afrika ya Kusini baada ya mwisho wa kipindi cha Kiasheuli, kipindi ambacho kinahusishwa na upatikanaji wa mafuvu ya namna moja ya Saldanha na Kabwe. Hata hivyo, wakati inaweza kufikiriwa kwamba fuvu kamili la kichwa la Saldanha na masalia yanayohusishwa nayo, yanamwakilisha homonidi aliyehusika na zana za Sango na Asheuli ya mwisho, hii haiwezi kuthibitishwa maadamu makadirio ya umri hayaaminiki. Visukuku vya Saldanha na Kabwe (Broken Hills) vinafanana kimofolojia na kisukuku kilichopatikana kwenye tabaka la IV la Bonde la Olduvai (H.12) na kile kilichopatikana Njarassi katika Bonde la Ufa la Afrika Mashariki; hii inaelekea kudokeza maumbo ya kirodesi yanayohusiana na Homo sapi yaliyochukua nafasi ya Homo erecto katika kanda ndogo ya tropiki ya Kusini mwa Sahara zaidi ya miaka 100 000 iliyopita.


Ithibati nyingine ya hominidi huyu inaweza ikapatikana kwenye fuvu la Florisbad lililokadiriwa kuwa la miaka 48 000 iliyopita na lenye mofolojia iliyo karibu na binadamu wa leo. Kiasi miaka 10 000 iliyopita, makundi makubwa ya watu yenye mnasaba wa kijenetiki lakini yanayoishi katika kanda tofauti, ambao ni wazazi wa kale wa baadhi ya watu wa leo, yalianza kutofautiana na kuzua makundi ya Wasanii wa msituni walio wadogo na wakubwa wa Afrika ya Kusini na Afrika ya Mashariki ya Kati; Wanegro wa eneo la ikweta na Afrika Magharibi, na Wanilo wa Afrika Mashariki. Ushahidi wa visukuku si kamili na mara nyingi umcelekezwa kwenye sampuli moja tu. Zaidi ya hapo, wajili wa binadamu wa leo katika kumbukumbu za kipindi kabla ya historia, unenasibishwa na mkururo wa mabadiliko ya kitamaduni na kimaumbile. Uongezekaji na usanifishaji wa aina mbalimbali za zana, wingi wa makaburi na uzikaji wa vitu pamoja na maiti na matumizi makubwa ya rangi kwa ajili ya kupamba vyote hivi ni ushahidi wa mabadiliko ya maisha ya Homo sapi yenye kuclkea mtindo wa maisha ambao ulizingatia zaidi matambiko na alama. Vifaa vya kusagia vinajitokeza kwa mara ya kwanza kwenye kundi la tatu na la nne, na hasa baada ya kiasi cha miaka 25000 Kabla ya Kristo. Seti nzima ya zana za kazi nzito iliyogunduliwa Zambia inaakisi mtindo wa matumizi ya zana hizo unaoashiria kilimo cha mazao ya chakula.

Mambo machache sana yanafahamika kutokana na maeneo ya Enzi ya Kati ya Mawe kuliko maeneo ya Asheuli. Pango la Hearths huko Makapani ni ushahidi halisi wa jinsi meko na nyumba vilivyogawanywa. Misingi kadhaa ya mawe iliyogunduliwa inaashiria kuwepo kwa vikingaupepo katika Eneo la Orange 1. Nchini Swaziland, hematiti ilianza kusindikwa na kutumiwa kama rangi zama za miaka 28 000 iliyopita. Fuawe na sakafu za moko navyo vinconekana kwenye upco wa Enzi ya Kati ya Mawe kwenye Maporoinko ya Kalambo na zinckadiriwa kuwa na umri wa takribani miaka 27 000 Kabla ya Kristo. Katika maeneo yote haya, inasalia ya wanyama mbalimbali yanadokezea kuwepo kwa maendeleo ya mbinu za uwindaji.

Ingawa Enzi ya Kati ya Mawe ya Afrika ya Kusini imetokea wakati mmoja na Enzi ya Paleolithi ya Nyuma katika Ulaya, hatua zake za awali, ingawa hazifahamiki vyema, zinaclekea zilitokea wakati mmoja na Enzi ya Musteri ya Ulaya au Enzi ya Jabrudia ya Mashariki ya Kati.

### *Enzi ya nyuma ya mawe*

Kwa kawaida, sura inayojitokeza Afrika Kusini mwa Sahara katika Enzi ya Nyuma ya Mawe ni ya tasnia zinazotengeneza zana ndogo za mikrolithi zinazojulikana kwa jina la Wilton kutokana na mapango yaliyoko magharibi ya Jimbo la Cape. Hata hivyo katika baadhi ya maeneo ya Afrika ya Kusini tasnia zinazojulikana kama za kabla ya Wilton zimetambuliwa. Tasia hizi



20.7 Zana za tasnia ya Wilton



20.8 Tezo ya nje yenye umbo la mwezi-mwandamo uliyotengenezwa kutokana na jirve la "chert" na kuchomekwa kwenye mpini wa pembe ya kijani - kutoka katika pungo moja huku Pletenberg Bay, Mashahidi ya Cape Province (J.D. Clark 1959).

zilianza kuwepo kiasi miaka 20 000 Kabla ya Kristo na zinaonyesha mapinduzi katika teknolojia ya zana za mawe. Mbinu za viini vilivyotayarishwa za Enzi ya Kati ya Mawe zimeachwa na badala yake utengenezaji wa njeya zenye umbo maalumu umetumika zaidi. Zana maalumu ni vikombo vikubwa pamoja na vijeya vidogovidogo vingi na vikombo vya mbinuko. Sampuli za vitu hivi ni maarufu katika maeneo ya mwambao wa kusini, Orange Free State, Transvaal na Namibia, ambako magunduzi hayo yananasibishwa na kuuliwa kwa tembo watatu.

Nchini Zimbabwe, tasnia za namra hiyo ziko Promongwan, zenye miaka kati ya 9400 na 12200 Kabla ya Kristo; huko Zambia zina miaka kati ya 21 000 na 23 000 kabla ya wakati tulionao. Mapinduzi haya ya teknolojia yamesambaa kati ya miaka 20 000 na 9000 iliyopita. Inawezekana kuwa matokeo ya mabadiliko ya mazingira yaliyotokea wakati huo ndiyo yaliyosababisha kuwepo kwa mbinu nyingine za uwindaji.

Tasnia hizi za kabla ya Wilton zinanasibishwa na uwindaji wa wanyama wakubwa kama vile kongoni, nyumbu, paa wa kibuluu na kwaga. Pia kuwepo kwa idadi kubwa ya wanyama pori, kunadhihirisha kuwa kuongezeka kwa kiwango cha usawa wa bahari katika kipindi hiki kumewezesha kupata chakula moja kwa moja kutoka baharini.

Desturi ya mikrolithi imenasibishwa na maendeleo ya zana bora zaidi za mchanganyiko, kama vile pinde na mishale.

Maeneo mengi ya Enzi ya Nyuma ya Mawe yanafahamika na kuna sababu ya kuamini kwamba kumekuwapo ongezeko kubwa la idadi ya watu katika kipindi hiki. Jambo hili linadhihirishwa na kupanuka kwa uwindaji na mbinu mpya zilizotumika: mapango na hifadhi nyingine zilizidi kukaliwa, maliasili nyingi zilitemiwa kwa wingi, na uwindaji ukawa maarufu na wa watu maalumu. Mtindo wa kuyakabili maisha hautofautiani sana na ule unaotumiwa siku hizi na Wasani wa Kalahari na makundi mengine ya wawindaji wanaoishi kwenye maeneo ya ukame.

Hapana shaka kuwa wawindaji hawa walikuwa na nafasi ya kutosha ya kutumia vipaji vyao kama baadhi yake vinavyojidhihirisha kwenye michoro mizuri katika miamba ya milima ya Drakensberg, Zimbabwe na Namibia. Ingawa nyingi ya sanaa hizo hazina umri unaozidi miaka 2000 hadi 3000 iliyopita, zinatoa kumbukumbu yenye ushahidi madhubuti wa mitindo ya maisha ya wawindaji hao.

Mnamo karne za mwanzo za Enzi za Ukristo, nafasi ya wawindaji na wakusanyaji wa Enzi ya Nyuma ya Mawe katika sehemu kubwa Kusini mwa Afrika ilichukuliwa na wakulima wenyewe ujuzi wa mbinu za utumiaji metali. Watu hawa yaelekea ndiyo makundi ya mwanzo ya Wabantu yaliyohamia katika sehemu hii ya bara kutoka makwao mahali fulani huko kaskazini-magharibi. Kwa hiyo hakuna ushahidi wowote wa kilimo cha mimea yoyote kabla ya kuja kwa watu wa Enzi ya Chuma, ingawa baadhi ya makundi ya Enzi ya Nyuma ya Mawe kusini-magharibi walikuwa wafuga kondoo na ng'ombe kuanzia karne ya Kwanza Kabla ya Enzi ya Kristo. Pia kuna ubishi kuhusu mahali walikopatia mifugo yao. Kwa kutumia sababu za kisumu, baadhi hudai kuwa wamecipata mashariki katikati ya Sudani. Kokote watakakokuwa wametokea, awamu hii ya wafugaji isingekuwa imeanza kabla ya kiasi cha miaka 300 Kabla ya Kristo na imeishia karne ya kumi na nane.

Kumbukumbu iliyopatikana kutokana na uchunguzi wa kipindi kabla ya historia kusini mwa Afrika inaonyesha kuwa nchi za uwanda wa juu wa bara zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya inwanadamu mtengeneza zana. Kuongezeka kwa ubingwa na ufanisi ambao vizazi vya hominidi vilitunika, na mchanganyiko wa ujinasibishaji na bidaa, kunadhihirisha ukale na uendeleaji wa sifa nyingi za kitaniaduni ambazo bado zinadumu hadi hivi sasa.



# 21

## *Historia ya Afrika ya Kati ya kipindi cha kabla ya historia*

### *SEHEMU I*

Kijiografia bonde la Kongo limeenea kutoka Ghuba ya Guinea kwa upande wa magharibi hadi sehemu za maziwa makubwa kwa upande wa mashariki. Kwa upande wa kusini bonde hili limeanzia karibu katika latitudo 10<sup>o</sup> nchini Angola na Shaba (zamani ikiitwa Katanga) na kuenea hadi kufikia mabonde ya hidrografia ya ziwa Chad na mto Kongo kwa upande wa kaskazini.<sup>1</sup>

Kwa jumla bonde hili lipo katika ukanda wa Ikweta na mimea yake inajumuisha baadhi ya misitu minene kabisa iliyoko Afrika. Yasemekana kuwa ukanda huu wa misitu ulikuwa umeenea kaskazini zaidi wakati wa vipindi vya mvua kuliko ilivyo sasa. Kwa mujibu wa utafiti uhoofanywa hivi karibuni, tamaduni za kipindi kabla ya historia hasa zile ambazo zilitokea baada ya Asheuli zinafikiwa kuwa zilitokana na sehemu hizo hizo, kwa kutegemea msitu wa kale na bila kuingiliana na wenyeji katika sehemu ambapo misitu haikuwa minene sana.

Baada ya muda mrefu kupita, uhamaji mkubwa wa wafugaji wa Kiniolithi ulitokea pembezoni mwa msitu, upande wa kaskazini, bila kuupenya msitu wenyewe. Mawasiliano yote, ambayo yatakuwa yamefanyika, yangetafutwa zaidi katika sehemu za mashariki na kusini za bara hili.

Ugumu wa kupenyeka kwa msitu umewafanya wanahistoria wengi wa kipindi cha kabla ya historia kupendekeza kwamba katika kipindi hicho sehemu hii ilikuwa na watu wachache sana. Hata hivyo, ugunduzi uliotokana na safari za hivi karibuni pamoja na idadi kubwa ya zana za bwe ambazo zimekusanywa, umeonyesha kuwa kwa hakika msitu wa kitropiki ulikuwa na wakazi wengi kama sehemu nyingine za Afrika.

Fikra zinazopinga mtazamo huu, ambazo kwa sasa zimepitwa na matukio halisi, pengine zilitokana na ukweli kuwa katika enco lenye unyevu la ikweta asidi nyingi zilizo katika udongo ilizujia masalia ya watu, vitu vyenye uhai kama vile initi, ngozi, pembe, mifupa n.k. visihifadluke. Kutokana na sababu hii, viunzi na vifaa vichache sana vimvumbuliwa kutoka katika machimbo ya kiakiolojia.

1 Istilahi "Afrika ya Kati" inatumwa kujumlisha nchi zifuatazo, Zaire, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Jamhuri ya Watu wa Kongo na Gabon na pia sehemu fulani za Angola, Rwanda na Burundi.

### *Kronolojia ya msingi*

Kutokana na utafiti wa hivi karibuni kuna uwezekano wa kutofautisha vipindi vitatu vikubwa vya mvua ambavyo vinafuatwa na vipindi vingine viwili vyenye mvua inayoongezeka lakini kwa kiasi kidogo zaidi. Vipindi hivi vilitenganishwa na awamu fupi za ukame.

#### *Kipindi cha mvua cha Kagera*

Kipindi hiki chaonekana kuwa ndicho kilichokuwa muhimu zaidi ya vyote. Kilikuwa kipindi cha machimbo mengi mabondeni ambapo matungazi ya changarawe ya zamani sana na yenye tasnia za kabla ya Asheuli ya Kale, tasnia ambazo ni za zamani zaidi katika bonde la Kongo, yalitokea. Kipindi kirefu cha ukame kilifuatia kile cha Kagera ambapo yale matungazi ya zamani yalifunikwa na tabaka nene la lateriti ambamo iligunduliwa tasnia iliyoendelea zaidi ya kipindi kabla ya Asheuli lakini ambayo umri wake haujakadiriwa kwa usahihi.

#### *Kipindi cha mvua cha Kamasia*

Kipindi hiki kilitokea mnamo mwisho wa Pleistosini ya Kale na kudumu kwa muda wote wa Pleistosini ya Kati. Kipindi kilikuwa na awamu mbili ambazo zilitenganishwa na kipindi kingine cha ukame wa kiasi ambamo katika kipindi hicho cha ukame wa kiasi sehemu (za nchi) zenye sura ya nchi ya nyanda za chini, na baadhi ya malalo ya miti yalijaa kabisa na mito ikapasua njia mpya.

Katika matabaka ya chini ya sehemu hizi za chini za miti yenye visukuku, kumegunduliwa zana za kipindi cha kabla ya Asheuli ambazo zilikuwa zimeendelezwa zaidi kuliko zile za kipindi cha Kagera, ikiwa ni pamoja na vifaa vya awali vya nyuso mbili.

Baada ya kumalizika kipindi cha mvua cha Kamasia tasnia za zana na mbwe zilizochongwachongwa ilipitwa na tasnia ya Asheuli ya Kale yenye mashoka ya mkono yaliyotengenezwa kwa ustadi zaidi.

Kilele cha kipindi cha mvua cha Kamasia kilifuatiwa na kipindi cha ukame wa kiasi ambacho ndicho kilichosababisha kufanyika kwa lateriti, matungazi ya changarawe, mchanga na matope ya mito. Tasnia ya Asheuli ya Kati ni ya kipindi cha tabia ya lali ya nchi ambacho kilishuhudia ukuaji wa mbinu maalumu ya kujeya inayojulikana kama mbinu ya Viktoria West I inayofanana na mbinu ya Levallois ya kuchonga kiini ubavuni.


Katika kilele cha pili cha Kamasia ambacho hakikujitokeza sana, tasnia ya Asheuli iliendelea kukua baada ya kuundwa kwa sururu ambayo ilitokea kuwa zana muhimu katika sehemu ya msitu.

#### *Kipindi cha ukame kilichofuata Kamasia*


Hiki ndicho kilikuwa kipindi chenye ukame zaidi katika eneo hili. Jangwa la Sahara lilienea kusini nalo lile la Kalahari likaenea kaskazini na wakati huohuo msitu wa ikweta ulitoweka kabisa. Nafasi ya tasnia ya Asheuli ilichukuliwa na tasnia ya Sango ambayo ilidhihirishwa na wingi wa sururu na mashoka ya mkononi ya kufanyia kazi nzito.







#### *Kipindi cha mvua cha Gambalia*

Katika kipindi cha mvua cha Gambalia kanda ya ikweta ilirudia hali yake ya awali, miti ikayachimba mabonde, na kurundika mashapo katika matungazi yaliyokuwa chini. Tasnia ya



21.1 Afrika ya Kati: Sehemu zilizotajwa kitabuni (F. Van Noten)



- |   |  |   |   |   |                  |
|---|--|---|---|---|------------------|
|  | Misitu minene ya mvua za Tropiki                       |  | Misitu minene mikavu                          |  | Nusu jangwa      |
|  | Misitu mchanganyiko, Misitu ya upili, Savana na Misitu |  | Muhulu: Maenco madogo ya misitu minene mikame |  | Jangwa           |
|  | Misitu mchanganyiko mikame                             |  | Mapululu                                      |  | Maenco ya mikoko |
|  | Misitu ya vilima na mbuga za nyanda za juu             |  | Misitu ya milima ya hali ya hewa ya wastani   |  | Vinamasi         |

21.2 Afrika ya Kati: sehemu ya uoto (F. Van Noten)

Sango ilielekea kukua hadi kufikia tasnia mpya ya Lupemba ambayo haikuwa kubwa sana na ambayo pia ilichukuliwa kuwa sehemu ya utamaduni wa msituni. Tasnia zinazofanana na zile za Afrika Kusini na za Kenya, ambazo zimchusisliwa na zile za Enzi ya Kati ya Mawe, zilianzishwa katika maeneo ya kusini mashariki.

### *Vipindi vya Makalia na Nakuru*


Vipindi hivi viwili vya masika ambavyo vilikuja baada ya kile cha Gambliia havikuwa dhahiri kama vile vipindi vya mvua vilivyovitangulia. Vilitenganishwa na awamu fupi ya ukame na kwa hakika kile cha Nakuru hakitofautishwi kwa wazi katika bonde la Kongo. Katika kipindi cha Makalia, mito ilichimba mabonde yenye kina kifupi ambayo yalijaa tena baadaye. Tasnia ya Lupemba ambayo ilitokana na sehemu hizo, na ile ya Tshitolo ambayo iliifuatia, zilishuhudia kuwapo kwa visu vya kuchunia ngozi na vigumba.

Wakati wa majira ya masika ya Nakuru na baada ya hapo, tasnia za Kiniolithi pamoja na ile ya Tshitolo, zilienea katika eneo lote la ikweta katika Afrika. Kwa upande mwingine Enzi za Shaba na Chuma hazikuipenya sehemu hii mpaka muda mrefu baadaye.

### *Tasnia za kipindi kabla ya historia katika bonde la Kongo*

#### *Tasnia za kabla ya Asheuli*

Huko Kongo na Jamhuri ya Afrika ya Kati tasnia hizi za zana za mbwe hupatikana katika matungazi ya zamani ya masalia ya lateriti au ndani ya mashapo ya mchanga katika sehemu za chini ya mto.



21.3 Asheuli ya Nyuma: shoka la mkono kutoka Mto Ngoere, Sangha ya Juu, Jamhuri ya Afrika ya Kati (Makumbusho ya Taifa ya Historia ya Asili)

*Tasnia ya Kafu*

Kafu ipo katika nchi ya Uganda. Tasnia ya Kafu ina mbwe za mtoni ambazo zimebanduliwa njeya tatu katika pande tatu ili kufanya makali yasiyokamilika. Tasnia ya Kafu imegawanyika katika hatua nne za maendeleo ya kiteknolojia. Hatua ya mwisho ya tasnia hii inakaribiana na ile ya Oldowani. Hata hivyo baadhi ya waandishi wanatilia shaka fikra kwamba zana za mbwe zinazopatikana katika Kafu ya zamani ziliundwa na binadamu.

*Tasnia ya Oldowani*

Tasnia hii ambayo ilionekana kwa mara ya kwanza katika bonde la Olduvai nchini Tanzania, ina mbwe za mtoni ambazo kwa wastani si bapa kama zile za tasnia ya Kafu. Mbwe hizi zilichongwa kwa kubandua njeya kutoka pande mbili tofauti ili kufanya makali yenye tao. Tasnia hii imegunduliwa huko Shaba na sehemu za magharibi za Jamhuri ya Afrika ya Kati na huenda pia ilikuwepo huko Angola, Kameruni na Gabon ijapokuwa hakuna hakika ya kuwepo kwake katika mwambao wa Guba ya Guinea.

*Tasnia ya Asheuli*

Kugawanyika kwa tasnia ya Asheuli katika hatua nne au tano kumefungamanishwa na mbinu za kusanifu zana kuliko kuzingatia mfuatano wa kikronolojia. Kwa jumla mashapo ya Asheuli huwa katika miundo ya kitope na kwa hivyo huwa nadra kuyapata katika maumbo yake ya asili ya kistratigrafia. Hali hii husababisha matatizo mengi ya kukadiria umri. Tasnia ya Asheuli bado inaendelea kutumia zana za mbwe lakini mashoka ya mkononi, buchari, na hata sururu kwa Afrika ya Kati, vinajitokeza kuwa muhimu zaidi.

*Tasnia ya Asheuli I*

Zana zilizotumiwa zilikuwa za njeya pana zilizotengenezwa kwa kugongagonga mawe inakubwa kwenye mhimili imara. Njeya hizi baadaye zilitumiwa kutengeneza mashoka ya mkononi na buchari ambazo zilikuwa zana kubwa za kufanyia kazi ngumu na zenye makali ya matao. Zana za mbwe zilizochongwa, pia zilikuwepo kwa wingi.

Hatua hii huwakilishwa katika Shaba, Angola, na Jamhuri ya Afrika ya Kati: katika matungazi yaliyoko chini kwa mbwe ghafi zilizochakazwa na maji.

*Tasnia ya Asheuli II*

Tasnia hii inafanana sana na ile ya hatua iliyotangulia, nayo pia hupatikana katika sehemu hizohizo za Afrika ya Kati. Hata hivyo, zana za hatua hii hazikumong'onywa sana na maji na zaidi ya yote, zimetengenezwa vizuri zaidi kuliko zile za Asheuli I. Dalili za urekebishaji wa zana ili kuzifanya zinyooke kwa kutumia nyundo ya mti au ya mfupa, zaweza kuonekana katika makali ya mashoka ya mkono na buchari.

*Tasnia ya Asheuli III*

Tasnia hii hupatikana karibu na uso wa ardhi kwenye mashapo ya changarawe katika mkoa wa Shaba. Ni katika hatua hii ambapo ugunduzi wa kiteknolojia ulianzishwa kwa kuwa kiini kilitayarishwa kwanza kwa madhumuni ya kutengeneza njeya pana zaidi. Mbinu hii ilijulikana kama Victoria West.<sup>2</sup> Katika hatua ya kutengeneza kiini bamba kubwa la kugongea lenye pande

<sup>2</sup> Victoria West: ni jina linalopewa mbinu mbili za kujeya za Levallois zinazopatikana hasa katika tasnia iliyogunduliwa karibu ya maporomoko ya Victoria katika mto Zambezi.

nyingi lilitokea kutokana na bamba hilo nje ya zilibanduliwa na kutengeneza vizuri zaidi ili kuzalisha mashoka ya mkono na buchari zenye sura sawa sawa na linganifu.

#### *Tasnia ya Asheuli IV*

Katika hatua hii mbinu za kuchonga na kujeya zilikuwa kama zile za hatua ya tatu lakini kiini kilifanywa mwingo zaidi na mashoka ya mkono na buchari zilichongwa vizuri zaidi. Hii tasnia ya Asheuli ya Nyuma inapatikana karibu na Mto Kamo, na katika Kasai na Shaba.

#### *Tasnia ya Asheuli V*

Hatua ya mwisho ya Asheuli hulingana na kuwepo kwa makazi ya binadamu katika sehemu za kati na za chini za matungazi ya miti yaliyokauka. Pamoja na mbinu za kusawazisha za hapo awali, mbinu ya Levallois ilitumiwa. Pia matumizi ya sururu yalienea zaidi, pengine katika kazi zilizohusiana na miti. Mabonge ya mawe yanayofanana na yale ya Amerika ya Kusini yanayoitwa *bolas* pia yamegunduliwa. Baadhi ya mifano ya tasnia hii ya hatua ya mwisho ya Asheuli imevumbuliwa katika mashapo yaliyoko katika mto Mangala katika Jamhuri ya Afrika ya Kati, kwenye mto Kamo katika Shaba na katika Angola.

Kwa bahati mbaya, hakuna lolote linalojulikana kuhusu wenye utamaduni huu katika sehemu yoyote ya Bonde la Kongo kwa sababu kutokana na asidi iliyopo katika udongo hakuna mifupa ya binadamu au masalia mengine.

#### *Tasnia ya Sango*

Enco asilia la changamano ya tasnia hii ni Sango Bay iliyoko kwenye ukingo wa magharibi wa Ziwa Viktoria. Tasnia ya Sango ilitokana na utamaduni wa Asheuli wa sehemu hiyo pasi kuwa na athari yoyote ya nje. Tasnia hii ni ya wakati mmoja na kipindi cha mwisho cha majira ya mvua nyingi na Kanjera ambayo yalidumu wakati wa awamu ya mabadiliko baina ya majira ya mvua nyingi na ya ukame. Zana za mawe zilizogunduliwa ni mashoka makubwa ya mkono, idadi ndogo ya buchari, mbwe zilizobanduliwa njeya na idadi kubwa ya sururu na zaidi ya yote zana za kazi mbalimbali kama vile sururu-patasi na sururu-randa ambazo ziliundwa kutengeneza vifaa vya miti. Kadri tasnia ya Sango ilivyoendelea ndivyo zana hizi zilivyo zidi kuwa ndogo ilihali mbinu za kujeya ziliimarika na kuwa bora zaidi.

Tasnia ya Sango imeenea sana katika bonde la Zaire kama vile katika nyika tambarare za Kinshasa na Shaba ya Juu ambapo hutofautiana na ile ya sehemu za magharibi kwa vile hakukuwepo na majambia au chonge zenye umbo la jani. Bila shaka mashapo mengi ya Kisango ni yale yanayopatikana katika Jamhuri ya Afrika ya Kati ambako yamehifadhika vizuri.

Kama ilivyokuwa kwa tasnia ya Asheuli iliyotangulia, tasnia ya Sango ilichipukia katika sehemu hizohizo bila kuathiriwa sana na ulimwengu uliokuwa nje ya mazingira yake ya msituni.

#### *Tasnia ya Lupemba*

Kufuatana na uainishaji uliopendekezwa na Mkutano wa *Pan African Congress* juu ya historia ya kipindi kabla ya historia uliofanywa mwaka wa 1955, tasnia ya Lupemba<sup>3</sup> ni tasnia ya Enzi ya Kati ya Mawe inayoonyesha maendeleo zaidi ya ile ya Sango ambayo ilitangulia. Tasnia ya Lupemba ilianza wakati ambapo ruwaza za mvua zilikuwa zimeanza kurudia hali yake ya kawaida, mwanzoni mwa kipindi cha mvua cha Gambli na ilidumu kwa muda wa karibu

<sup>3</sup> Tasnia ya Lupemba: jina hili linatokana na enco la kipindi kabla ya historia lililoko Lupemba katika Kasai. Istilahi hii ilitumiwa kwa mara ya kwanza na Abbe H. Breuil.

miaka 25 000. Mwanzoni mwa kipindi cha Lupemba mashoka machache ya mkono yalikuwa yangali yakitengenezwa lakini haya baadaye yaliacha kutumiwa kabisa na hapajagunduliwa buchari zozote. Mbinu ya Levallois ilitumiwa katika kuunda nyembe na njeya ambazo zilisawazishwa kwa nyundo. Hapo baadaye mbinu iliyokuwa thabiti zaidi ya kutengeneza nyembe kwa kutumia patasi na tindo ilitumiwa. Mbinu ya Levallois iliendelea kutumika zaidi katika kutengeneza njeya. Tasia na Lupemba inapambanuliwa katika hatua tano.

### *Lupemba I*

Mifano ya hatua hii hupatikana katika sehemu zote za magharibi ya Bonde la Kongo ambapo tasnia hii yaelekea kuwa ilitokana na ile ya Sango. Chonge, majambia na vigumba halisi vilianza kuonekana mwishoni mwa hatua hii.

### *Lupemba II*

Hatua hii ilibainishwa huko Pointe Kalina na mifano mingine inepatikana Stanley Pool. Patasi zenye umbo la jani za Lupemba I zilibadilika taratibu kuwa vishoka. Patasi zenye ncha zilizonyooka na aina mpya ya vikatio vilitumiwa badala ya inodeli za awali za Sango huku silaha zilijumuisha majambia yenye ncha nyembamba zenye umbo la jani zilizojewa vizuri sana.

### *Lupemba III*

Tasia hii imejulikana kutokana na mashapo kwenye uso wa ardhi huku Stanley Pool na katika Angola. Katika hatua hii stadi za uchongaji wa mawe zilikwisha imarika na kufikia kilele cha ukamilifu kutokana na matumizi ya mbinu ya kusawazisha kwa kutumia kanienco; mbinu ambayo ilipendelewa zaidi kuliko ile ya kugongagonga kwa nyundo. Zana za tasnia ya awali ya Lupemba kana vile sururu, patasi, mashoka madogo ya mkono, vikombo, vikatio na nyembe zimepatikana pia katika sehemu hizi lakini maumbo yake ni madogo zaidi. Idadi kubwa ya zana mbalimbali zenye umbo la jani, vigumba vyenye mipini na meno na mibonyeo vinaweza kuonekana.

### *Lupemba IV*

Habari kidogo sana hujulikana kuhusiana na hatua ya nne ya Lupemba. Sifa muhimu ya hatua hii yaelekea kuwa na mabadiliko katika mbinu ya kujeya.

### *Lupemba - Tshitolo*

Hatua hii ya mwisho yaonekana kuwa ilitokea wakati wa majira ya ukame ambayo kikronolojia yanatokea muda mfupi kabla ya kipindi cha kwanza cha masika ya Makali. Mashapo yanayojulikana yapo kwenye matope ya miti yaliyofunikiwa na clangarawe au chini ya tabaka la majumaji lililo juu yake hasa katika visiwa vya mito. Katika hatua hii mbinu ya kujeya ilikuwa bado ni ile ya Levallois. Kwa upande mwingine urekebislaji wa zana hudhihirishwa na matumizi ya nyundo, kanienco na usawazishaji mwinamo. Zana zilizokuwepo zilikuwa ni pamoja na patasi, bobari, na mashoka ya mkono. Pamoja na vikatio vya kawaida, vilikuwepo 'vijikatio' ambavyo wakati mwingine vimedhaniwa kuwa ni vigumba. Vigumba vyenyewe vilikuwa na maumbo tofauti umbo mishale. Navyo vyembe vya mishale vilitokea kuwa vya umbo la jani au umbo la ng'anda uru; umbo la miiba-miiba na mara chache, umbo la meno na mibonyeo na mipini.

Huko Angola hatua hii inafikiriwa kuwapo yapata miaka 11000 kabla ya enzi za Ursto. Ingawa kuwapo kwa hatua hii hakujadhihirishwa bado katika Jamhuri ya Afrika ya Kati na Kameruni huenda ikawa ilikuwepo Angola na Gabon.



## *Tamaduni za kipindi kabla ya historia katika mazingira yasiyo ya msitu*

Wakati ambapo tasnia ya Lupemba ilikuwa inaendelea katika ukanda wa msitu magharibi mwa Bonde la Kongo, tamaduni nyingine kama zile za Mame-Stillbaya, Stillbay na Magosi zilikuwa zikiendelea huko Shaba na Angola ya Mashariki.

### *Mame-Stillbay na Stillbay*

Hizi tasnia mbili hazikutofautiana sana baina yao. Pia katika kila tasnia zana zilizokuwapo ni pamoja na chonge zenye uso mmoja, vikombo, koleo za mishale, mawe ya kutupa, mashoka machache ya mkono na chonge nenc zenye umbo la nusu jani. Mbinu ya kurekebisha ni ile ya mwinamo na mitindo halisi ya Kistillbay huonyesha ubingwa wa matumizi ya mbinu za Levallois. Masalia ya binadamu ya kale kabisa yaliyopatikana nchini Kongo pia ni ya hatua hii ya pili. Masalia hayo ni magego mawili yaliyogunduliwa pamoja na mbwe za kwatzi na chonge za nyuso mbili ambazo zilikuwa kauka vifusi vyenye mifupa ambavyo vilipatikana katika Kakontwe.

### *Tasnia ya Magosi*

Tasnia hii iligunduliwa kwa mara ya kwanza nchini Uganda. Ni utamaduni ambao mambo kadha ya Kistillbaya hupatikana bado na pia hujumuisha zana za mikrolithi. Tasnia ya Magosi pia hupatikana huko Shaba lakini hakuna mahali maalumu ambapo tasnia hii imedhihirika.

### *Tasnia ya mesolithi: tasnia ya Tshitolo*


Vipindi viwili vya ukame wa wastani vilisababisha kupungua kwa eneo la misitu hasa katika nyanda za juu ambako binadamu wa Tshitolo alifanya makazi yake.<sup>4</sup> Idadi kadhaa ya zana mpya ilijitokeza ambapo nyingi kati ya hizo zilikuwa za aina ya mikrolithi. Kwa kuwa silaha za tasnia ya Tshitolo zilikuwa ni vigumba peke yake, tasnia hii yaweza kuchukuliwa kuwa ya utamaduni wa kabla ya Neolithi usiokuwa na vyombo vya udongo wala mashoka yaliyotengenezwa vizuri. Tasnia hii ilikuwa aina ya utamaduni wa mwishomwisho wa msitumi wa Kiafrika kabla ya kuwepo kwa utamaduni wa Neolithi wa Kongo Magharibi.

### *Tasnia ya Neolithi*

Utamaduni wa Neolithi wa Bonde la ni wa wakati mmoja na kipindi kifupi cha mwisho cha mvua nyingi kijulikanacho kama Nakuru. Tabia ya hali ya nchi ilikuwa kama ilivyo siku hizi, japokuwa misitu ilikuwa mimene zaidi, kwani haikuwa na barabara nyingi zilizotengenezwa na binadamu ili kuipenya misitu hiyo.

Wakitokea kaskazini, baada ya kuvuka Mto watu wa utamaduni wa Neolithi uliojulikana kama 'Kongo ya Magharibi' walienea polepole hadi katika eneo hili. Sifa muhimu ya utamaduni wa Neolithi ni kwamba karibu ulikuwa ukitumia miamba tu kama vile shisti, kwatzi na jadeiti ambayo ilikuwa vigumu kuchonga na ilitoa zana hafifu sana. Zana za tasnia hii zilikuwa ni pamoja na sururu ambazo hazikukamilishwa vizuri, patasi, mbwe zilizojewa ovyoovyo, mawe yaliyopekechiwa, na zaidi ya hayo mashoka mengi sana ambayo kwanza yalikatwa katika maumbo maalumu na kisha kung'arishwa vizuri. Kwa kawaida vigumba vilitengenezwa kwa kwatzi na havikuengenezwa kwa ustadi. Katika maeneo mengine kama vile Ishango, zana za

<sup>4</sup> Tshitolo: jina hili lilitumiwa zana za mbwe zilipogunduliwa Tshitolo, Kasai, Kongo.



21.4 Gudulia lenye kitako cha bapa la Neolithi kutoka Bataimo, Lobaye, Jamhuri ya Afrika ya Kati (Maabara ya Enzi za Kabla ya Historia, Makumbusho ya Historia ya Mambo ya Asili)



21.5 Minara ya Megalithi ya eneo la Bouar, Jamhuri ya Afrika ya Kati  
(R. de Bayle des Hermonet)

mulupa ambazo nyingi yazo zilikuwa ni shusa zilihusishwa na masalia mengi ya vyombo vya udongo.

Utamaduni wa Neolithi umeonckana pia huko Kwango magharibi, katika kingo za Mto Kongo baina ya Stanley Pool na Kongo dia Vanga pamoja na Gabon na Jamhuri ya Afrika ya Kati. Maeneo haya ya utamaduni wa Neolithi ni ya miaka ya hivi karibuni kwani metali ilianza kutumiwa katika sehemu za misitu baadaye sana; chuma kilianza kutumiwa mnamo karne ya tisa wa enzi za Ukristo.

### *Minara ya megalithi*

Tamaduni za kimegalithi zilikuwepo tu huko Kameruni na Jamhuri ya Afrika ya Kati.<sup>5</sup> Minara iliyo katika inkoa wa Bouar, katika Jamhuri ya Afrika ya Kati, ni ya kustaajabisha sana. Minara hii ina umbo la marundo ya udongo ya ukubwa mbalimbali na imesambaa katika eneo la urefu wa kilometa 130 na upana wa kilometa 30.<sup>6</sup> Uchimbaji uliofanywa katika minara hii haujatoa ushahidi wowote wa maana wa kiakiolojia lakini minara ya mwanzo inaweza kusemwa kuwa ina

5 Megalithi ni minara iliyojengwa kwa mawe yaliyochongwa ovyo au magogo ya mawe au mawe yaliyotiwa mahali yakasinama katika makundi au binafsi katika mpango maalumu kama vile miringo.

6 Rundo la Udongo. Fungu la mchanga au mawe linalopuhika mahali na mazishi

yake ni sehemu maalumu zilizobainishwa, wakati mwingine zikiwa na umri wa miaka 5500 kabla ya enzi ya Kristo na ile ya hivi karibuni zaidi huenda ilijengwa miaka 450 ya enzi ya Kristo. Tarehe hii ya pili inaelekea kudokeza kuwa minara hii iliitumiwa kwa mara ya pili.

## *Sanaa ya miambani*

Likiwa kati ya maeneo makubwa mawili - Sahara na Afrika Kusini ambapo sanaa ya miambani ilishitadi Bonde la Kongo lina sanaa yake ya miambani. Huko Kameruni na Angola, aina ya sanaa inayojitokeza sana ni ya michoro ya kijiometri iliyokatwa nakshi katika mabamba ya miamba. Michoro ya karibuni zaidi imepatikana katika jimbo la Shaba nchini Kongo. Sanaa ya kikundi hiki ni ya kidhania wala sio sanaa wakilishi kama ile ya Afrika Kusini.

Katika Jamhuri ya Afrika ya Kati sanaa ya miambani hupatikana katika sehemu za kaskazini na mashariki za nchi hiyo. Katika sehemu ya kaskazini makazi yaliyo katika mawe huwa na picha za ngeu zinazowakilisha maumbo ya binadamu na alama. Katika sehemu za mashariki picha za nakshi, juu ya mabamba ya miamba, ndizo zinazojitokeza zaidi na huonekana kama kwamba zilichorwa na watu waliokuwa na ujuzi wa kutumia chuma.

Sanaa hii inafanana sana na sanaa inayopatikana katika sehemu za Wabantu na kwa hivyo ni ya karibuni na pengine ni ya kipindi cha historia. Hata hivyo, sanaa hii ni kidokezo muhimu cha uhamaji wa watu katika kipindi ambacho hakijulikani sana cha mame-historia au cha historia ya mwanzo ya Afrika ya Tropiki.

## *SEHEMU II*

Katika sura hii Afrika ya Kati hujumuisha Kongo na baadhi ya nchi zinazopakana nayo yaani Jamhuri ya Watu wa Kongo, Gabon, Rio Muni, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Rwanda, Burundi na Angola.

Misitu minene, tabia ya hali ya nchi na wingi wa asidi katika udongo vinetatiza kuvumbua na kuhifadhi kwa usahihi maeneo ya kiakiolojia na masalia ambayo yamebainishwa. Katika Afrika ya Kati, pengine kwa kiasi kikubwa zaidi kuliko sehemu nyingine, ile kawaida ya mfuatano wa Enzi ya Mwanzo wa Mawe, ya Kati, na ya Nyuma ambazo zinatenganishwa na vipindi vya kati, kwa kweli haikubaliki tena kwa mujibu wa kronolojia au wa uainishaji. Kategoria hizi pana lazima zifikiriwe kuwa ni za muda tu, na pia, za kadri sana. Kwa miaka mingi historia ya Afrika ya Kati ya kipindi kabla ya historia ilikuwa ya uainishaji na kronolojia tu na binadamu hakupewa umuhimu mkubwa. Hata hivyo tunaamini kwa dhati kuwa haiwezekani kuainisha kwa uhakika maeneo dhahiri ya kitamaduni. Hatuna budi kutoshika kwa kufahamu tu kuwa binadamu alikuwepo bila kuweza kusema kama chimbuko lake lilikuwa mumu humu au alikuja kutoka mahali kwingine. Bila shaka binadamu tangu mwanzo kabisa alijinasibisha na mazingira mahsusi, kila yenye namna zake za moja yakiwa na namna yake ya tabia ya hali ya nchi, mimba, na wanyama. Matokeo sifa zinazolingana, bali pia zikionyesha tofauti za kikanda, na hata za kijanibu ambazo haziziwezi kufafanuliwa kwa kuzingatia athari za mabadiliko ya hali ya kiakiolojia tu.

## Usuli wa kijiografia

Mofolojia ya sehemu ya Afrika ya Kati ni matokeo ya mfululizo wa mititio ya dunia ambayo inaanzia mwanzo wa kipindi cha tatu cha ufanyakaji miamba<sup>7</sup> na ambacho huenda ikawa hakijaisha bado.

Bonde la Kati ambalo lializidi meta 500 kutoka usawa wa bahari limezungukwa na nyanda za juu na milima. Sura ya tabaka la kale la chini ya ardhini imeharibika sana.

Tukiacha mwambao wa kusini ya Angola na Bonde la Kuhango-Zambezi, sehemu ya Kati ya Afrika hupata mvua ya kutosha na mara kwa mara kwa mwaka mzima. Kwa hiyo msitu wa mvua uliosababishwa na hali hii hutanda kwenye Bonde la Kongo na katika sehemu kubwa ya Jamhuri ya Watu wa Kongo, Gabon, Rio Muni na Kameruni ya kusini. Msitu huu huzungukwa na msitu inkubwa wenye kiasi fulani cha miti ipukutayo majani na ambao mara nyingi humomonyoka lakini ambao unaweza kustahimili ukame wa miezi miwili au mitatu. Ikiwa na umbo la tao kuzunguka kanda ya msitu mnene wa ghuba ya Guinea, nyika na savana ya Sudani Zambezi hutanda enco linalojumuisha Kameruni ya Kati, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Sudani ya Kusini, Rwanda mashariki, Shaba, Zambia na Angola, ambapo msimu wa ukame waweza kudumu kwa muda wa hadi miezi saba katika mwaka mmoja. Mtitio wa kinamasi hupatikana katika njia za mito hasa katika Nili nyeupe, Bonde la Mto Kongo, mtitio wa Upemba nchini Kongo, na pia katika bonde la Zambezi nchini Angola na Zambia.

## Mabadiliko ya mazingira

Hata hivyo katika kipindi kabla ya historia ruwaza ya mimea ziliathiriwa na mabadiliko muhimu ya tabia ya hali ya nchi yaliyojulikana kama vipindi vya mvua nyingi na awamu za ukame zilizoviteganisha vipindi hivyo.

Vipindi vya mvua, ambavyo hufikiriwa kuwa vya wakati mmoja na awamu za barafuto katika kizio cha kaskazini, vimepewa majina kulingana na nyakati vilipotokea, Kagera (mwanzoni), Kamasia na Gambalia (mwishoni). Awamu mbili za nyuma za mvua, Makalia na Nakuru, ambazo zilitokea mwanzoni mwa enzi za Holosini ziliainishwa baadaye. Kwa hivyo mabadiliko ya mazingira katika Afrika ya Kati yameathiriwa sana na tabia ya hali ya nchi zilizokuwepo kwa muda wa milenia hamsini zilizopita, ambazo zimeweza kudhihirishwa kutokana na uchunguzi wa aina za mimea iliyopo siku hizi na ushahidi wa chavua za kale ambavyo vimewesha uundaji upya wa utanda wa mimea ya kale.

Kwa hivyo, kuanzia miaka 50 000 hadi miaka 10 000 kabla ya wakati wa sasa, Afrika ya Kati ilipitia katika awamu ndefu ya ukame iliyotokea wakati mmoja na kipindi cha mwisho cha barafuto barani Ulaya, yaani *Würm* ilihali awamu ya mvua ambayo ilianza kama miaka 12 000 iliyopita yaweza kufikiriwa kuwa hulingana na mabadilikobadiliko ya tabia ya hali ya nchi ambayo huashiria mwanzo wa enzi ya Holosini. Katika kipindi hiki kirefu cha ukame, ambacho huenda kikawa kilikatiwa na awamu yenye unyevu zaidi yapata miaka 28 000 kabla ya enzi za Ukristo, kulikuwa na ongezeko kubwa la savana ya nyika, ilihali katika kipindi cha unyevunyevu msitu mnene ulienea katika sehemu kubwa ya Afrika ya Kati. Kupungua kwa misitu hii siku hizi kumesababishwa na binadamu.

<sup>7</sup> Kipindi cha tatu cha ufanyakaji miamba huwa na hatua tano kama ifuatavyo: kuanzia ya zamani hadi ya karibuni zalki, pafcosini, losini, oligosini, miosini, na pliosini. Enzi hii imejumuisha kipindi kinachoanzia miaka milioni 65 hadi miaka 1.8 milioni iliyopita.

### *Ukaaji wa watu katika Afrika ya Kati*

Kwa kuwa hakujapatikana mifupa ya binadamu, ambayo imeharibiwa na asidi iliyoko katika udongo, yakubalika kwa jumla kuwa dalili za kwanza za kuwepo kwa binadamu zilikuwa ni mbwe zilizochongwa ambazo hujulikana kama zana za mbwe. Zana hizi zinalingana na zile zilizogunduliwa Olduvai katika Tanzania. Vifaa vya aina hii hupatikana karibu katika eneo lote la Afrika ya Kati katika bonde la Kasai na Shaba nchini Kongo; katika Kameruni na Gabon, katika Jamhuri ya Afrika ya Kati na kaskazini mashariki ya Angola. Tunahisi kwamba ni kosa kuzichukulia mbwe hizi kama zana halisi kwa sababu kwa jumla zilikuwa ni viini vya miamba ambavyo vimebanduliwa njeya. Zana halisi zilikuwa njeya ambazo ama zilitumiwa kama zilivyo au zilichongwa kutengeneza vikombo.

Katika Afrika ya Kati hakujagunduliwa makazi yoyote ya kipindi hiki, ambacho charudi nyuma hadi kufikia miaka milioni mbili, wala dalili yoyote ya zana zilizotengenezwa kwa miti au mifupa ambazo pengine zilikuwa ni sehemu muhimu ya vyombo vya homonidi wa kwanza.

Ushahidi madhubuti wa kuwepo kwa binadamu katika Afrika ya kati ni kupatikana tu kwa zana za Asheuli. hatua yake ya mwanzo kabisa, yaani Asheuli ya Kale, inapatikana katika sehemu ya Lunda tu ilihali ile ya karibuni zaidi, yaani Asheuli ya Nyuma, ambayo kwa kawaida hupatikana katika mazingira ya ukame, imegunduliwa katika sehemu nyingi za bonde la kati huko Angola, Rwanda, Kongo na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Sifa bainifu za tasnia za Asheuli ni mashoka ya mkono na buchari na juhudi mbalimbali zimefanyika kuziainisla zana hizi kwa kuzingatia maumbo yazo. Baadhi ya waandishi wamepambanua hatua tano katika eneo hili. Pamoja na zana hizi vifaa anuwai vingine vimegunduliwa, ikiwa ni pamoja na zana za nyuso tatu, sururu, visu, zana za duara dufu na zana ndogondogo kadhaa. Mojawapo ya maeneo machache ambako utamaduni wa Asheuli umepatikana ni katika kingo za Mto Kamao ulioko Shaba, mahali ambapo hufikiwa kuwa palikuwa ni karakana na makazi papohapo, yaliyotumiwa kwa msimu. Mali ghafi ya kuteugeneza zana hizi ililetwa kutoka umbali wa kilometa moja na nusu kutoka kwenye eneo lenyewe. Viini vilivunjwa palepale vilipopatikana na ni njeya pekee ambazo zilisafirishwa hadi kwenye makazi ili kutumiwa kuundia zana. Makazi haya yanafikiwa kuwa yalikuwepo yapata miaka 60 000 Kabla ya enzi za Ukristo.

Aina ya binadamu aliyehusika na tasnia hizi awcza kukisiwa tu kwa kumfananisha na binadamu katika sehemu nyingine za Afrika ambapo Homo erecto amconekana pamoja na zana za Asheuli.

### *Unasibishaji na maendeleo ya kiteknolojia*

Ingawa tasnia za kipindi baada ya Asheuli kutoka katika sehemu kadha hutofautiana, lakini bado zinaonyesha upatanifu wa kiasi fulani. Ili kurahisisha mambo, eneo la kijiografia linalozungumziwa laweza kugawanywa katika sehemu ya magharibi na sehemu ya mashariki.

Katika sehemu ya magharibi ambayo imeenea kutoka Angola hadi Gabon, kanda inayojulikana zaidi ni ile inayotanda kusini-magharibi mwa Bonde la Kongo ambapo sehemu ya mashariki hutanda kanda ya maziwa na eneo lote kutoka Shaba hadi ziwa Tanganyika.

Katika sehemu ya magharibi mkusanyiko wa tasnia umebainishwa na tasnia hizi kwa jumla zinafasiriwa kuwa zenye kufuatana kikronolojia na kiainishaji zikijumuisha Lupemba na mwisho Tshitolo. Kuna sururu ghafi kama zile zilizokwishaonekana katika tasnia ya Asheuli nazo zilidumu muda wote hadi kufikia tasnia ya Tshitolo. Kwa hivyo kifaa hiki hakiwezi

K 5 (KABLA YA SASA)	KANDA YA MAGHARIBI				KANDA YA SHABA ZIWA TANGANYIKA		KANDA YA MAENEO YA MAZIWA
	UWANDA WA KINSHASA	GOMBE	DIMBA BIIORRI MDUSSANDA	KANDA YA LUNDA	KALAMBO	KAMOA MOSE	MATUPI
1000							
2000							
3000	TASHIA YA	TASHIA YA	TASHIA YA	TASHIA YA		ENZI	
4000	TASHITOLI YA	TASHIA YA	TASHIA YA	TASHIA YA	KAPOSWAYA	YA	
5000	MWISHO	NDOLI?	TASHIA YA	SCHITOLI YA	MWISHO	MAWE	
6000	TASHIA YA	TASHIA YA	NYUMA	NYUMA	(A.P.R)	YA	
7000	TASHITOLI YA	NDOLI	TASHIA YA	SCHITOLI YA		MWISHO	
8000	MWISHO		TASHIA YA	SCHITOLI YA			
9000	TASHIA YA	TASHIA YA	KATI	TASHIA YA			
10000	TASHITOLI	DJOKOCI		LUPEMBO-	POLUNGU		
11000	TASHIA YA			SCHITOLI	(MPITO)		
12000	LUPEMBAYA			YA SCHITOLI			
13000	KATI			TASHIA YA		TASHIA YA	
14000	TASHIA YA	TASHIA YA		SCHITOLI YA		MPITO	
15000	MWANZO	DJOKOCI		MBELE			
16000	WA LUPEMBA			TASHIA YA			
17000	YA KATI			LUPEMBA YA			
18000				MWISHO AU		ENZI	
19000			LUPEMBA YA	LUPEMBO-		YA	
20000			NYUMA	SCHITOLI?		MAWE	
21000						YA	
22000							
23000							
24000							
25000							
26000	STANLEY POOLII	TASHIA YA					
27000	NA LUPEMBA	KALINI					
28000	YA MWISHO.						
29000							
30000					NAKISASA		
31000	STANLEY POOLII				TASHIA YA		
32000	NA LUPEMBA				(LUPEMBA)		
33000							
34000							
35000							
36000	?						
37000							
38000							
39000				TASHIA YA			
40000				LUPEMBA YA			
41000				MBELE			
42000							
43000		TASHIA YA			CHIPETA		
44000		KALINI			(TASHIA YA		
45000					SANGO)		
46000							ENZI
47000							YA
48000							MAWE
49000							YA
50000							KATI
51000							
52000							
53000							
54000							
55000							
56000							
57000							
58000							
59000							
60000							
-D.A.T KWA TASHIA ZA KIAKEULI							
● Ukadiriaji umri kwa kutumia Karboni-14							

MABADILIKO YA MAZINGIRA	MIMEA
<p>MAGEUKO KUELEKEA HALI YA HEWA YA SASA</p> <p>HALI YA UNYEVUNYEVU ?  MMOMONYOKO WA MARA KWA MARA; UKAME ?  HALI YA UNYEVU.  KUIKARUKA KWA MITEREMKO. KUPANYIKA KWA  PALESOLI NYEMBANDA. KUPANUKA KWA  MAZIWA.</p> <p>KIPINDI CHA UKAVU NA UKAME. KUSHUKA KWA  HALIJOTO KATIKA MAENEO YA MILIMA.  MMOMONYOKO WA VILIMA NA KANDO YA  MABONDE, KUTOKEA NA KUPOTEA KWA MITO.</p> <p>KIPINDI CHA UNYEVU (?) NA UFANYIKAJI WA MITO?</p> <p>KIPINDI KIKAVU CHA NUSU UKAME  UPANYIKAJI WA MABONDE KUTOKANA  NA ULIKAJI MIAMBA. MITO KUTOKANA  NA VIJITO NA KUTOWEKA KWAKE.</p>	<p>KUPANUKA  KWA MSITU  MNENE</p> <p>MSITU MKAVU.  SAVANA YA  AKASIA.  MAPULULU YA  SAVANA.</p> <p>* Kazi za Binadamu kupungua  kwa misitu mihene. Kupanuka  kwa misitu yenye kuona na  Savana.</p>



kufikiwa kuwa zana ya Sango pekee tu. Mara nyingine kifaa hiki huhusishwa na tasnia yenye ustadi mkubwa ambayo ilitengeneza vigumba vyenye umbo la jani na majambia marefu. Baadaye vigumba vilitokea ambavyo vinadhihirisha matumizi ya uta na mshale katika kuwinda.

Sehemu ya Mashariki huonyesha tasnia zilizo changamano zaidi. Tasnia za sehemu hii hufanana na zile za sehemu ya magharibi lakini kujeya njeya za nyuso mbili hakuonekani kwa wingi. Kwa upande mwingine mbinu za kujeya za Musteri na Levallois zimeenea sana. Katika sehemu hii tasnia za Sango na Lupemba ni uaalumu kabisa na huwezesha kubainisha maeneo mawili tofauti: lile linalotanda katika sehemu ya kaskazini au kanda ya maziwa ambalo huwakilishwa na majambia na zana zenye nyuso mbili za maumbo ya jani na mkuki na lile lililotanda katika sehemu ya kusini (yaani Shaba na ufuo wa Ziwa Tanganyika) ambalo halina chonge zozote lakini lina patasi na bobari ambazo hazipatikani katika sehemu za maziwa. Ugunduzi huu unapingana na tofauti zilizobainishwa baina ya tasnia za msituni na zile za savana. Kwa kweli, hakuna kanda yoyote ambayo yaonekana kuwa na misitu mingi zaidi kuliko nyingine katika wakati huo. Fasiri hii inathibitishwa na tabia ya hali ya nchi ambayo yaelekea ilikuwa kame zaidi kuliko ilivyo sasa. Misitu ilianza tu kuenea mwishoni mwa kipindi hicho. Japokuwa hakuna masalia ya mifupa ambayo yamewahi kupatikana yaelekea Hoino sapi ndio waliohusika na utengenezaji vifaa hivi vya utamaduni.

Kwa jumla, tasnia za Sango-Lupemba za kale zaweza kukisiwa kuwa na umri wa baina ya miaka 45000 na 26000 kabla ya sasa, zile za Tshitolo ya Kale baina ya miaka 10,000 na 7,000 kabla ya sasa, na ile ya Tshitolo ya Nyuma baina ya miaka 6000 hadi 4000 au 3500 kabla ya sasa.

### *Wawindaji-wakusanyaji maalum*

Katika kipindi fulani pengine baina ya miaka 50000 na miaka 40000 kabla ya sasa, zana ndogondogo au mikrolituli za kijiometri zenye maumbo ya duara, pembe tatu, instatili, na trapezodi, vilianza kuonekana. Zana hizi zilianza kutumiwa kwa mara ya kwanza katika Enzi ya Kati ya Mawe na kusambaa kwa wingi katika Enzi ya Mwisho ya Mawe, wakati ambapo zilitumiwa kwa vigumba, mikuki, chonge za chusa, na visu. Katika kipindi hiki pia, sehemu hii yaweza kugawanywa mara mbili yaani ya mashariki na ya magharibi.

Sehemu ya magharibi hujumuisha Angola ya kaskazini, Kasai, Kwango, Kongo ya Chini na Jamhuri ya Watu wa Kongo ambapo desturi za Lupemba bado zingalipo ingawa zilikuwa zikibadilika taratibu kuwa za Kitshitolo. Mikrolituli za kijiometri zimegunduliwa kwa wingi lakini hazikuzidi zile za sehemu ya mashariki ambapo maumbo haya yalikuwa mengi kuliko maumbo mengine. Kwa mfano, katika kanda ya Lunda kune gunduliwa mtindo wa bondeni wenye idadi kubwa ya visu vidogo vya kuchunia ngozi na mtindo wa uwanda wa juu wenye mipini ya chonge ambayo imeenea sana. Nchini Kongo, tasnia ya Tshitolo ina umri baina ya miaka 13000 na 4500 kabla ya sasa kutegemana na eneo. Swali la kujiuliza ni iwapo mitindo mbalimbali ya Kitshitolo imetokana na namna mbalimbali za kujinasibisha na mazingira tofauti. Pengine utafiti wa baadaye utatoa jibu la swali hili.

Katika sehemu ya mashariki, iliyopo pembezoni mwa msitu mnene wa Ikweta, tasnia za mwanzoni za Enzi ya Nyuma ya Mawe hazihitilafiani na zile zilizotangulia. Ni eneo moja tu, luko Matupi Cave, linalotupa habari kuhusu kipindi hiki. Pango hili lilikaliwa kuanzia miaka 40000 hadi 3000 kabla ya sasa. Mikrolituli za kwatzi zilizopatikana pale kwa maelfu zilitengenezwa kwa mbinu itwayo *bipolar*. Zana za kazi nzito au makrolituli zilizotengenezwa kwa kwatzi, mawe meroro au shisti hujumuisha vijaa, michi, fuawe, nyundo za mawe, vikombo

na patasi chache. Masalia ya mifupa huonyesha kuwa mazingira yalikuwa ya ukame zaidi katika wakati huo kuliko yalivyo sasa. Wanyama waliowindwa na wakazi wa pango hilo, walikuwa ni ng'ombe, mjusi, rodenti, nguruwe mwitu, tumbili na nungunungu. Watu hawa pia walidhaniwa kuwa waliishi katika mazingira ya savana, japokuwa ilikuwa na msitu jirani na masalia yaliyogunduliwa hapa yalikuwa ni pamoja na zana chache za mifupa, rangi, na mapambo madogomadogo.

Katika eneo la Ishango pamepatikana tasnia ya mikrolithi iliyotumia kwatzi duni lakini ilitengeneza chusa zenye mwiba mmoja na baadaye zenye safu mbili ya miiba. Tasnia hii inafikiriwa kuwa ya umri wa miaka 21 000 kabla ya sasa. Kitu cha kustaajabisha kilichogunduliwa ni ufito mdogo wa mfupa uliorembwa kwa mistari ya toja ambao ulitumika kama mpini wa njeya wa kwatzi. Wakazi wa Ishango walishi kwa kuwinda na kuvua samaki na windo lao kubwa lilikuwa viboko, ingawa ndege pia walikuwa mawindo muhimu. Masalia ya binadamu yaliyogunduliwa yameonyesha kuwa wakazi wa wakati huo hawakufanana na binadamu wa sasa hata kidogo.

Tasnia ambazo kiuainishaji zawekwa baina ya tasnia za mikrolithi halisi na tasnia maalumu kwa sehemu ya magharibi ya Afrika ya Kati ilitokea katika eneo la maziwa, Shaba na katika fuo za Ziwa Tanganyika. Kwa mfano huko Kamao katika Kongo tasnia hizi za vipindi vya mabadiliko zinakadiriwa kuwa na umri baina ya miaka 15 000 na 12 000 kabla ya enzi za Ukristo. Kwa hivyo inaelekea kuwa tamaduni hizi tofauti zilikuwepo katika wakati mmoja. Eneo la Gwisho, nchini Zambia, linatoa picha kamili sana ya maisha katika Enzi ya Nyuma ya Mawe mnamo milenia ya tano. Pamoja na zana zilizong'arishwa, idadi kubwa ya vitu vya miti na mifupa imegunduliwa na vitu hivyo vizathibitisha umuhimu uliopewa mbinu za kutengeneza zana hizi ambazo zilienea hata katika savana.

### *Mwisho wa enzi ya mawe*

Zana zilizong'arishwa hazikutokea katika kipindi cha Neolithi tu na kwa hakika zilikwisha kuwepo katika Enzi ya Nyuma ya Mawe. Ruwaza ya kusambaa kwake yaonyesha kuwa zana hizi zilikuwa zikitumiwa pembezoni mwa bonde la kati. Katika sehemu ya mashariki vitu hivi ni adininu mno. Kwa upande mwingine zana za aina hii huwakilisha kiasi kikubwa cha uvumbuzi wa kiakiolojia uliofanyika kaskazini ya msitu wa ikweta kama vile katika bonde la Uele na hata sehemu zilizo mbali zaidi kama vile Ituri. Kama machimbo ya Buru yanavyoonyesha, tasnia ya Neolithi ya Uele haiwezi kuwa ya nyuma zaidi kupita karne ya kuni na saba kabla ya enzi ya Ukristo, na kwa sababu hiyo yaweza kudhaniwa kuwa ni ya Enzi ya Chuma.

Kwa upande wa magharibi zaidi, mkusanyo mwingine wa mashoka yaliyong'arishwa umegunduliwa katika sehemu ambapo Mto Ubangi huingia msituni. Katika kisiwa cha Fernando Po, kilichoko karibu na mwambao wa pwani ya Kameruni, mashoka yaliyong'arishwa na ambayo yanahusishwa na ufinyanzi yamekadiriwa kuwa na umri wa karne ya saba ya enzi yetu na zana za aina hii zingali zinatumia mpaka sasa.

Sehemu ya mwisho huenda sambamba na mwambao wa Bahari ya Atlantiki kutoka Gabon hadi kaskazini-magharibi mwa Angola. Katika sehemu hii zana zimechongwa bila kung'arishwa isipokuwa makali yake. Huko Gabon, mashoka huwa yanakuwa na makali ya kupindapinda. Ugunduzi pekee uliopatikana katika Jamhuri ya Watu wa Kongo na Angola umepatikana katika mashapo yaliyoko juu ya ardhi.

Bila ya kuwepo na data za kiuchumi na kijamii, haiwezekani kudhani kuwa wakazi wa sehemu hii walifanya kazi za kilimo na ufugaji wa wanyama.

Ni muhimu pia kutaja megalithi zilizogunduliwa katika mkoa wa Bour katika Jamhuri ya Afrika ya kati. Hizi zimekadiriwa kuwa za milenia ya tano kabla ya enzi za Ukristo au pengine kwikwi cha kwanza, lakini hii huenda ikawa ni hali ya kutumiwa kwa mara ya pili. Sakafu ya kimegalithi iliyoko Api ni senomena ya asili na hali ni hiyohiyo kwa minara yote inayodhaniwa kuwa ya megalithi ambayo imo nchini Kongo.

Baadhi ya waandishi hufikiri kuwa hakuna istilahi yoyote kati ya zile zinazotumiwa sasa, yaani Sango, Lupemba na Tshitolo ambayo inawiana na ushahidi uliothibitishwa kisayansi. Hata hivyo, kama tulivyojaribu kuonyesha katika sehemu hii ya sura (ya 21), tunaamini kuwa kuna uwezekano wa kutenganisha tofauti za kikanda miongoni mwa tasnia za mawe za baada ya Asheuli, na pia kuzingatia jinsi tasnia hizo zilivyoendelea kubadilika. Pia, tunaamini kuwa katika kupambana na mazingira, binadamu alilazimika kuvirekebisha vyombo alivyovitumia. Hata hivyo, hatuamini kuwa mazingira yalikuwa na athari zenye uwezo mwingi zaidi juu ya maendeleo haya ya binadamu hasa katika Afrika ya Kati.

Tofauti na Afrika Mashariki, Afrika Kaskazini yaelekea ilibakia nyuma katika mambo mawili muhimu ya kipindi kabla ya historia: mbinu za uchimbuaji ambazo mara nyingi zilipuuzwa na kronolojia halisi ambayo haikukamilika kwa sababu ya ukosefu wa mifuatano ya kistratigrafia ambamo matabaka ya udongo hayakuguswa na yamebakia katika hali zao za asili. Kwa hivyo kutokana na ukosefu wa visukuku vya hominidi wa awali, mbinu za ukadiriaji umri za kutumiwa katika maumbile ya ardhini, na maeneo ya makazi ya enzi za kipaleolithi, umri wa makazi ya hominidi katika Maghrib na Shara, kwa sasa, waweza kukisiwa tu kwa kuonisha masalia ya kiakiolojia na yale ya wanyama na mimca pamoja na aina za ufundi zilizopatikana.

Mkabala wa kipaleoethnolojia shurti uzidi kutumika katika kutafiti kipindi kabla ya historia katika Afrika kwa jumla na hasa katika Maghrib; badala ya kuzingatia 'Binadamu na mazingira yake' tunapaswa kuangalia jinsi 'Binadamu anavyostahimilia mazingira hayo'.

### *Tasnia za awali kabisa za binadamu: kipindi cha kabla ya asheuli*

Kuna ushahidi wa kutosha kuhusu kuwepo kwa binadamu kauka Maghrib, lakini ushahidi huu unakuwa mgumu kuufasiri kwa namna nyingine isipokuwa kwa kuainisha tu. Tafsihi hii imekitwa katika ruwaza ya kistratigrafia ya sehemu za mwambao, hasa Moroko na pia katika paleontolojia ya wanyama. Kuna kulingana kidogo baina ya sehemu hizo na maeneo katika Tanzania, Kenya na Ethiopia.

Kutokana na magunduzi haya ya kikronolojia na kistratigrafia haielekei kama homonidi walikuwepo katika Maghrib na Sahara mapema kama vile walivyokuwa katika mashariki na kusini mwa Afrika. Hakuna alama za Australopithesini kama vile masalia ya mifupa yao au mawe yaliyojewa yanayoashira tasnia halisi ya mbwe. Hata hivyo zana za mbwe zimegunduliwa Moroko, Algeria na Sahara, na zinaelekea kuwa ni za umri wa baina ya miaka milioni moja na milioni mbili, ambao ni umri sawa na ule wa zana zilizogunduliwa katika bonde la Olduvai. Lakini hakuna mahali popote katika Maghrib na Sahara ambapo pamegunduliwa miundo ya kiakiolojia inayolingana na ile ya mashariki na ya kusini mwa Afrika.

Kwa hiyo juhudi za wanahistoria wa kipindi cha kabla ya historia ilibidi zielekezwe kwenye kuthibitisha uwiano baina ya kronolojia, mifuatano ya kistratigrafia na mabadiliko ya aina za zana hasa katika Moroko na Sahara ya kati na ya magharibi.

### *Tasnia za Kiasheuli*

Mifano ya tasnia ya Kiasheuli katika Maghrib ni mingi sana. Mbali na mashapo yaliyoko juu ya ardhi, tasnia hii hupatikana katika aina tatu mahsusi za maeneo.

1. Maeneo yanayohusiana na mwambao katika enzi za miaka ya hivi karibuni ambayo huweza kutambulishwa na usawa fulani wa zamani wa bahari. Kwa mfano katika mwambao wa bahari ya Atlantiki nchini Moroko mfuatano wa kiakiolojia umejengwa upya. Mfuatano huanzia zana za mbwe za kipindi cha kabla ya Ashculi na kufikia kilele chake katika Paleolithi ya Kati. Kwa sababu zinazohusiana na mofolojia ya mwambao, nchi za Algeria na Tunisia hazina maeneo ya aina hii katika mwambao wao.
2. Maeneo katika mashapo ya mito na maziwa. Maeneo ya mito ni adimu sana na namna ya kuyafasiri nayo huwa sio sahihi. Hali hii ndiyo inayoonekana katika maeneo mengi ya Algeria, Moroko na Tunisia, kama vile katika Redeyef, karibu na Gafsa, nchini Tunisia. Maeneo ufukoni mwa maziwa ni adimu katika nchi zote tatu. Kwa upande mwingine mikusanyiko ya tasnia ya Ashculi huwa ya kawaida katika schemu ya kusini kuanzia Mauritania hadi Libiya.
3. Maeneo yanayohusishwa na chemchemi zenye kububujika ambayo yanaelekea yaliwavutia binadamu kuanzia kipindi cha Kiasheuli hadi kipindi cha Kiateri. Maeneo ya aina hii ni pamoja na yale yanayopatikana Tit Mellil na Ain Fritissa, nchini Moroko, na pia Ternifine karibu na Mascara, nchini Algeria. Katika eneo lililotajwa mwisho, tasnia na wanyama wa Kiasheuli hupatikana kwa wingi sana, na viligunduliwa pamoja na fuvu la hominidi aliycopewa jina la *Antalanthropo* na anahusiana na *Homoerecto*.

Ama kuhusu zana za mawe tasnia ya Kiasheuli katika Maghrib na Sahara kimsingi haitofautiani na tasnia ya aina hiyo huko Ulaya. Viambajengo vikuu vyake ni njeya, mashoka ya mkono yenye nyuso mbili na zana za wajiji tatu. Lakini bila shaka, sifa yake ya asili kabisa ni umuhimu wa buchari zilizoundwa kutokana na njeya za mawe.


Kutokana na uchanganyuzi wa kiainishaji wa buchari hizi za kimaghribi mambo mawili hujitokeza, mosi, ni kuanzishwa kwa mbinu ya Kilevallois tangu enzi ya awali ya Kiasheuli ambayo ilitumiwa kutayarisha kiini cha mwamba kwa kubandua njeya mmoja mmoja (buchari zilizojulikana kama Tabelbalat-Tachenghit kutoka Sahara ya magharibi nchini Algeria ziliteugenezwa kwa mbinu hii) na pili matumizi ya mbinu ya Kombewa ya Kusini mwa Afrika ili kupata ujeya za nyuso mbili zenye makali kamili.

Hominidi waliohusika na tasnia hizi walitokana na jenasi ya *Homo erecto* na umri wao umekadiriwa kuwa wa karibu miaka 400 000 hadi 500 000 iliyopita. Huenda hominidi hawa walijua kutumia moto na, pengine, walikuwa na uwezo wa lugha.

### *Tasnia ya Musteri*


Kuwepo kwa utamaduni wa Ki-Musteri katika maghrib unaofanana na ule wa Ulaya umekuwa ukibishaniwa kwa muda mrefu. Hata hivyo tasnia zilizogunduliwa katika magharibi na mashariki ya Maghrib zinawakilisha kikamilifu mtindo luo na bado huonyesha ishara nyingi za matumizi ya mbinu ya Kilevallois. Huenda tasnia hii ya Musteri ya Maghrib ilianzia Mashariki mwa Mediterania.

Sifa muhimu zaidi ya tasnia hii ni ile namna ambayo imeweza kujiendeleza yenyewe hadi kuwa ya Kiateri (jina hilo hutokana na eneo la Bir el Ater lililoko kusini mwa Tebessa. Kiteknolojia tasnia ya Ateri ilizalisha idadi kubwa sana ya zana zilizochongoka. Teknolojia hii ilikuwa matokco ya awali ya tasnia ya Musteri; ilikuwa na maisha marefu sana na ilienea kutoka kaskazini hadi kusini kupitia Maghrib na Sahara. Kwa hivyo, kikronolojia lazima hii iliingiliana na schemu ya Paleolithi ya Kati na, angalau, mwanzoni mwa Paleolithi ya Nyuma katika Ulaya.



22.1 Zana ya Kiasheuli yenye nyuso mbili; zana bora kabisa iliyopatikana Ternufine, magharibi mwa Algeria. Uchimbuzi ulioongozwa na C. Arambourg, 1954 (Michoro, M. Dauvois)

22.2 Shoka lililogunduliwa katika eneo la Asheuli la Erg Tihodaine, Sahara ya Algeria (M. Bovis)



22.3 Mbwe zenye sura ya tufe. Ain Hanek (M. Bovis)



22.4 Zana ya Kimusteri iliyochongoka, El-Guettar, Tunisia; uchimbuzi ulifanywa chini ya usimamizi wa M. Gruet (M. Bovis).



22.5 Zana za Kiateri-Chonge ndefundefu, vikombo na violezo vya Levallois, Wadi Juf-Jemel, Mashuriki mwa Algeria (M. Bovis)

Tarehe ya awali zaidi ya mwanzo wa kipindi cha Ateri huenda ni ya milenia arobaini kabla ya enzi yetu, ingawa tarehe zilizopatikana kwenye maeneo yaliyochunguzwa katika Maghrib huonyesha kipindi cha baina ya miaka 37 000 na miaka 30 000 kabla ya enzi za Ukristo. Ni vigumu zaidi kukadiriya tarehe ya tasnia ya Ateri. Tasnia hii ilienea kote katika Sahara na pengine hata kufikia maziwa makubwa, na namna teknolojia ya Ateri ilivyobadilika inaashiria enzi ya Neolithi. Hata hivyo, hakuna ushahidi kamili wa kuonyesha kuwepo kwa teknolojia ya Ateri ya 'Kabla ya Neolithi' ingawa pia hakuna tasnia za katikati zilizogunduliwa kati ya vipindi hivi viwili.

Kuhusu binadamu wa kipindi cha Ateri, ugunduzi wa hivi karibuni katika Moroko huiongezea uzito nadharia kuwa binadamu huyo hakuwa wa aina ya *Neanderthal* kama vile alivyokuwa katika hatua ya Musteri lakini alikwishaifikia kuwa *Homo Sapi*.

### *Paleolithi ya Nyuma na Paleolithi-Juu*

Maarifa yetu ya sasa kuhusu vipindi hivi yamekitwa katika tasnia nne: Iberia Maurusi ambayo ipo katika sehemu ya mwambao, upeo wa macho wa Killoginon katika Tunisia, Kapsi iliyogawanywa katika sehemu mbili, yaani Kapsi Halisi na Kapsi ya Nyuma; na ya Neolithi ya mapokeo ya Kapsi ambayo kama jina lake linavyodokeza ilitokana na tasnia iliyoitangulia.


### Tasnia ya Iberia Maurusi

Machimbo ya karibuni kwenye eneo la Tamara Hat katika Algeria yamcwezesha kukadiriya umri wa awali sana, na pia kupatikana picha safi zaidi kuhusu Waiberia na Wamaurusi ambao walikuwa wawindaji wa kondoo wenye pembe na ambao waliishi katika mapango kwenye mwambao yaliyotenganishwa na bahari na kinamasi na mwinuko unaofanya kisimbwi kilichojitokeza chenye samaki chaza. Ama kwa hakika Tasnia ya Iberia na Maurusi ilikuwa ni utamaduni wa mwambao japokuwa ulipenya bara katika mahala fulanifulani kama ilivyodhihirishwa na eneo la Kolumnata huko Tiaret katika Algeria. Hakuna alama yoyote ya kuwepo kwa tasnia hii katika eneo la Tangiers ama katika mwambao wa Ahel ya Tunisia au katika Tunisia kwa jumla.

Hata uchanganuzi wa kina huonyesha mambo machache sana ya maana miongoni mwa vifaa vya Iberia na Maurusi. Mamia kadhaa ya burini ndogo yanatoa ushahidi wa kuwepo kwa mbinu ya asili ya kujeya na ambayo yamekusanywa kutoka kwenye maeneo kama vile La Mouillah katika Algeria na yanathibitisha kuwa burini ndogo hizi zilitumiwa kutengenezwa chonge zenye wajiji tatu zijutikanazo kama chonge za La Mouillah kuliko mikrolithi za kijiometri kama zilivyotengenezwa katika Tasnia ya Kapsi. Kuna tasnia chache sana za zana za mifupa, na vitu vya asili vinaonekana ni visu vya kuchunia ngozi. Hakuna sanaa ya binafsi au ya ukutani ingawa kipindi cha Iberia na Maurusi kilikuwa wakati mmoja na michoro ya miambani ya Lascau huko Ufaransa na Altamira, huko Hispania. Hata hivyo binadamu wa Cro magnon wa aina ya Mechta el Arbi wa Kialgeria, waliopo katika jenasi ya *Homo sapi* walikuwepo katika pande zote mbili za Mediterania katika kipindi hicho.

Fikra inayokubaliwa kwa jumla ijapokuwa hakuna ushahidi thabiti unaoiunga mkono ni kuwa utamaduni huu ulianza masbariki na kugawanyika katika matawi mawili ya Cro Magnon ya Kiulaya lililoenea kaskazini mwa Mediterania na Mechta el Arbi lililoenea kwenye mwambao wa Afrika kwa upande wa kusini. Kianthropolojia watu hawa huenda walitokana na Ncanderthal kwa kupitia Waateri lakini tasnia yao ya zana za mawe huonyesha ushahidi wa utamaduni ambazo






22.6 Zana halisi za tasnia ya Kapsi (M. Bovis)

22.7 Tasnia ya Kapsi ya Nyuma: Mikrolithi za kijometri (zana za pande nne zenye pande mbili tu zilizo sambamba, zana za pembe tatu zenye pande zisizolingana, zana zenye umbo la mwezi-mwandamo, na burini ndogo ndogo) (M. Bovis.)

22.8 Utamaduni wa Kapsi ya Kineclithi: Mawe ya kusagia yanayoonyesha alama za ngeu ya makaa ya mawe na vipande vya Kauri ya Helix vyote hivi vilipatikana Damous el-Ahmar, Al'geria mashariki (M. Bovis).



hazifanani na tamaduni za Musteri na za Waateri zilizoitangulia. Pia kuna sifa nyingine bainifu kama vile ung'oaji wa meno na makaburi ya mapangoni au makazi ya miambani kama yale ya Afalu-bu-Rhummel, nchini Algeria, na Taforalt, katika Moroko.

Kwa upande mwingine watu hawa waliishi hadi kufikia kipindi cha Neolithi na kufikia mwisho wa kwikwi cha tatu waliweza kuvifanya hata visiwa vya Kanari kuwa makoloni yao.

**Tasnia za Nyembe za 'Upeo wa Macho' wa Kollignon na nyinginezo za kabla ya Kapsi**

Ushahidi wa kistratigrafia na kijiomofolojia umeonyesha kuwa tasnia za nyembe za Tunisia ya kabla ya Sahara katika eneo la Gafsa ni wa mapema zaidi kuliko mfuatano mzima wa tasnia ya Kapsi yote. Tasnia hizi zimepewa jina la 'Upeo wa Macho' wa Kollignon. Hata hivyo haijawezekana kuthibitisha kronolojia sahihi ya tasnia hizi. Tukizitazama tasnia hizi kiuainishaji, tunaona kwamba zina idadi kubwa ya nyembe zenye makali pande zote na huenda zina asili ya mashariki kama vile Sirenaica, Misri au Mashariki ya Karibu.



Zaidi ya hayo, baina ya tasnia ya Iberia na Maurusi, ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa ni ya Paleolithi na tasnia ya Kapsi ya baadaye, kuna idadi kadha ya tasnia za sehemu hizo kama zile za Kerenii, Kristeli na Kolumnata, nchini Algeria, ambazo zote ni za kikwi cha saba liivi kabla ya enzi za Kristo.

### Tasnia ya Kapsi

Mfuatano wa tasnia ya Kapsi umefafanuliwa kwa kuzingatia mitindo mitatu ambayo huja katika nyakati tofauti. Mitindo hii ni 'Kapsi Halisi', 'Kapsi ya Juu' na Neolithi 'ya mapokeo ya Kapsi'. Katika nyakati mbili za mwanzo maeneo huwa ni marundo ya taka za majivu, mawe yaliyoungua, mamia ya maelfu ya koa za konokono, mifupa ya wanyama wanaoliwa na binadamu, zana za mawe na za mifupa, vitu vya mapambo na vya watu binafsi, masalia ya binadamu na kadhalika. Tunaweza kukisia kuwa watu waliishi katika vibanda na ndiyo sababu ya kuwepo marundo ya taka. Huenda vibanda hivyo vilijengwa kwa matete na kukandikwa kwa udongo kama ilivyothibitishwa na ugunduzi uliofanyika katika jimbo la Kenchala huko Algeria Mashariki.

Zana za Kapsi ni bora sana. Burini fupi ndizo nyingi sana lakini pia kuna nyembe ndefu zenye makali pande zote ambazo mara nyingi huwa zimepakwa ngeu. Burini ndogo hazikutengenezwa kwa 'chonge za La Mouillah' kama zile za Iberia na Maurusi bali kwa kutokana na mikrolithi za kijiometri zenye inaumbo ambayo pande zake si sawa. Tasnia ya mifupa haipo kwa wingi sana. Tasnia ya Kapsi halisi imegunduliwa katika eneo dogo kwenye mpaka wa sasa kati ya Algeria na Tunisia. Pengine tasnia hii ilikuwepo katika kikwi cha saba cha kabla ya enzi yetu na kama hivyo ndivyo, itakuwa vigumu kuthibitisha kwamba tasnia hii ilikuwepo wakati mmoja na tasnia ya Kapsi ya Nyuma ya hivi karibuni. Zaidi ya hayo hakuna lolote ambalo lajulikana kuhusu binadamu ambao waliuendeleza utamaduni wa 'Kapsi halisi'.

Tasnia ya Kapsi ya Nyuma au Kapsi Iliyoundelea hupatikana katika mitindo mingi ambayo ilisambaa magharibi mwa Algeria na angalau katika sehemu ya Sahara. Hii ni tasnia yenye vifaa vidogo na yenye mikrolithi nyingi sana zenye umbo la kijiometri zilizotengenezwa kwa hali ya juu, hasa zana za umbo la pembe tatu na trapezoidi.



22.10 Kapsi ya Nyuma·jiwe la chokaa lililonaishiwa kutoka Khanguet el-Mouhaad, Algeria Mashariki (M. Bovis)

22.9 Kapsi ya Nyuma·mfupa wa mguu (muundi) wa mwanadamu uliochongwa kuwa sime ulipatikana huko Mechia el-Arbi, Algeria Mashariki wakati wa uchumbuzi katika mwaka 1952 (M. Bovis)

Tasnia ya Kapsi ya Nyurna au, angalau tawi lake la kaskazini, ilikuwepo mpaka kufikia kikwi cha tano cha kabla ya enzi yetu na ilidumu hadi wakati wa Neolithi. Kwa hivyo mara nyingi inawezekana kuona tasnia ya 'Kapsi Halisi', 'Kapsi ya Nyuma' na tasnia ya Neolithi ya 'Mapokeo ya Kapsi' zote zikiwepo katika wakati mmoja ingawa katika sehemu tofauti.

Kwa hiyo utamaduni wa Kapsi ulidumu kwa muda wa karibu miaka 2000, muda ambao ni karne chache kidogo kuliko Misri ya Mafarao. Kuna uwezekano wa kupata vidokezo vya baadhi ya sifa za kiantropolojia za watu wanaohusika. Binadamu wa Kapsi hakuwa wa aina ya *Cro Magnon* wa Mecha-Afalou. Alikuwa binadamu wa aina ya Mediterania na mfano wake kamili ni Ain Dokkara kutoka Tebessa aliyeishi tangu kikwi cha cha saba. Mamia ya makazi ya Wakapsi yamegunduliwa. Ni jambo la ajabu kuwa watu hawa waliwahi kutamamani kabla ya kuwepo kwa ufugaji na kilimo. Hata hivyo makazi yao yalikuwa ni vibanda vilivyojengwa kwa matawi ya niti na kukandikwa kwa udongo. Uwindaji haukuwa jambo la muhimu katika maisha ya watu hawa, lakini konokono wa ardhini na mimea waliyoikusanya ilikuwa na umuhimu zaidi katika vyakula vyao kuliko wanyama. Hakuna ushahidi halisi wa kuonyesha kuwa walilima.

Wakapsi waliwazika watu wao kwa namna mbalimbali, kwa mfano wakiwa wameinama na miguu na mikono yao ikiwa imkunjiwa chini ya videvu vyao. Sababu ya kutumia ngeu nyekundu hajajulikana bado. Jambo la kushangaza zaidi ni matumizi ya mafuvu ya vichwa kama ukumbusho kama inavyoonekana katika Faid Bour, nchini Algeria. Zaidi ya hayo walikuwa waking'oa meno ya watu waliokuwa hai na waling'oa hadi makatio manane ya wanawake.

Wakapsi haohao walikuwa ndio wasanii wa kwanza katika Maghrib ambao walitengeza vitu vya mapambo ambavyo ni pamoja na vipande vya inagamba ya mayai ya mbuni vilivyonakshiwa na vilivyoanzia katika Kapsi halisi na kuendelea. Pia kulikuwepo namna kadha za vijisanamu vilivyotiwa nakshi na mawe yaliyochongwa ambayo pengine yalitangulia sanaa ya miambani.

### Uneolithishaji na mataifa ya Neolithi

Katika Maghrib kipindi cha Neolithi kilichipuka kutokana na kile cha Kapsi. Hoja inayotolwa kuwa tasnia ya "Neolithi ya Mapokeo ya Kapsi" ilikuwa imesambaa sana inathibitishwa na kuwepo kwa sifa kadha za Neolithi kama vile vyombo vya udongo, vyombo vya mawe vilivyong'arishwa na uzalishaji wa chakula. Vigumba vilivyogunduliwa kwa wingi katika Sahara ni ushahidi wa kuwepo kwa maisha ya wawindaji ambao waliyafanya makazi katika sehemu hizi. Wawindaji hao walizitumia sehemu hizi kwa uchumi wa ufugaji ambao ndio uliotangulia ule wa kilimo ijapokuwa mara nyingine walihamia milimani wakitafuta malisho ya wanyama.

Kwa hivyo baina ya milenia ya tano na milenia ya kwanza za kabla ya enzi ya Ukristo, Maghrib ilikuwa na namna nyingine za kuneolithisha kuliko zile za Neolithi halisi ya "mapokeo ya Kapsi." Kwanza sehemu ambazo hazikuathiriwa na athari za Kapsi zilipata maendeleo yao ya kipekee ambayo yaonyesha sifa mbili muhimu: maendeleo yaliyotokana na misingi ya Iberia — Maurusi na, zaidi ya yote, mawasiliano na Ulaya ya Mediterania. Hapa linazuka suala la usafiri wa baharini. Kwa hakika, ipo mitindo kadha ya mwambao ya Maghrib ya Neolithi ambayo inatoa ushahidi wa kuwepo kwa mawasiliano na Ulaya, kwa mfano vyombo vyao vya udongo na obsidi walizoagiza kutoka nje. Hivi ndivyo ilivyokuwa pia kwa mwambao wa Bahari ya Atlantiki ya Moroko.

Ni vigumu kuona kwamba utamaduni wa Neolithi ulizagaa kaskazini mwa Sahara. Sanaa ya miambani ya sehemu hizi ilianza kama sanaa ya vitu asilia na ilikuwa ya ukataji nakshi lakini

baadaye walianza kutumia rangi katika kuchora. Mwanzo wake unaonekana katika mwendelezowa neolithishaji wa utamaduni wa Kapsi. Hata hivyo, hapa pia ipo haja ya kuthibitisha uhusiano baina ya tasnia na sanaa.

Kwa mara nyingine tunaweza tu kumalizia kwa kusema kuwa kipindi kabla ya historia ya Maghrib bado hakijacleweka vizuri kwa sababu ya kutokuwa na inachimbo ya kisasa na mfuatano wa kistratigrafia unaoweza kueleza tarehe za kuaminika.

# 23

## *Historia ya Sahara ya kabila ya historia*

Sahara kwa hivi sasa ni jangwa kubwa linalotanda sehemu kubwa ya Afrika Kaskazini. Si rahisi kuelezea mipaka wala sifa zake, lakini ukame ndio ulio katika maeneo yote ya jangwa hilo. Kwa vile Sahara imeenea kilomita 5700 kutoka magharibi hadi mashariki kati ya Bahari ya Shamu na Bahari ya Atlantiki, na kilomita 1500 kutoka kaskazini hadi kusini kati ya Milima ya Atlas kabla ya Sahara na Sahel za Sudani hali za kijangwa sasa zimetanda katika eneo la takriban kilomita za mraba milioni 8.6. Lakini jangwa la Sahara kama tulijuavyo hivi leo limebadilika sana tangu zama za kabla ya historia.

Uhamaji wa watu waliokuwa wakiishi katika eneo hilo huenda ulisababishwa na ukame na joto lililozidi kuongezeka, na kutokana na hali hiyo mvua ilizidi kuwa haba zaidi, na mito na vijito vikakauka. Hali hii ilisababisha kutoweka kwa wanyama na mimea, vitu vilivyowawezesha watu kuishi. Kwa sababu hiyo, watu walilazimika kuhamia kwenye kingo za jangwa ambako hali ya kimazingira ilikuwa ya nafuu zaidi.

Kronolojia ya staarabu za kipindi kabla ya historia katika Sahara inahitaji maelezo mawili: mosi hakuna mahali popote katika Sahara ambapo ruwaza ya kistratigrafia inatuwezesha kupata picha sahihi ya hatua za kipindi kabla ya historia<sup>1</sup>. Pili, mbali na kipindi cha Neolithik hatuna tarehe sahihi ambazo zingetuwezesha kujenga upya kronolojia kamili.


Picha inayotolewa katika sura hii imerahisishwa mno. Ikumbukwe kwamba hadi sasa hapajapatikana ushahidi wa kufikiria hatua za Paleolithi ya Nyuma katika Sahara, kwani matumizi ya istilahi hiyo hayathibitishwi na hakika zilizopo. Wala haiwezekani kuongelea enzi za Mesolithi - istilahi ambayo kwa vyovyote vile inaelekea kutotumika tena.

Jangwa la Sahara halijatoa viunzi vya wanadamu pamoja na tasnia zilizoambatana navyo. Lakini viunzi vichache vilivyopatikana vinaashiria ukongwe mkubwa wa binadamu katika Sahara.

<sup>1</sup> Stratigrafia: sono na fasili ya matabaka yaliyojirundika kwa mfuatano katika mahali pamoja. Ni rahisi kuelewa kwa nini enco lililopata mabadiliko makubwa ya hali ya hewa kama Sahara haliwezi kuwa na ushahidi wa matabaka ya namna hiyo. Kwa ulakika, unapotilia maanani hali ya hewa ya maeneo madogomadogo, matatizo ya vipindi vya hali ya hewa ambayo yanaweza kugundulika kutoka na uchunguzi wa matabaka huwa changamani. Kwa kweli, mfuatano wa matabaka unaonyesha kwamba Sahara ilikuwa jangwa ilipofikia miaka 1000 kabla ya enzi ya Kristo.

<p>- 1000 hadi + 1000</p>	<p>Minara ya kabla ya Uislamu</p>	<p>Kipindi cha mwisho cha unyevunyevu.</p>
<p>- 1000 hadi - 2000</p>	<p>Neolithi ya karibuni Tichirt Fadelian Borkou</p>	<p>Kuziba vijito. Ukukaji wa vijito. Visima vya mwanzo.</p>
<p>- 2000 hadi - 5000</p>	<p>Neolithi ya Awali Meniet Guezam Tilenisi</p>	<p>Mnomonyoko wa mwisho Wa barafu za mabonde. uotaji wa matete ziwani Chungu ya mchanga ya awali aina II.</p>
<p>- 5000 hadi - 7000</p>	<p>?</p>	<p>Aukar</p>
<p>- 7000 hadi - 15000</p>	<p>Aterian. Saoura. Tidikelt. Mauritania Air.</p>	<p>Kiwango cha mwisho cha maziwa makuu yenye Niatomu Tembo, kiboko, faru.</p>
	<p>Acheulian III-VIII kama ilivyoelezwa na Biberson (1961)</p> <p>Utamaduni wa mbwe</p>	<p>Mvua kubwa. Chungu ya mchanga wa awali aina I Volcano</p> <p>Mwisho wa mmomonyoko Kuwepo na matuta ya Teffassasset</p> <p>Mtiririko wa maji ya mito makuu kutokea kwa maziwa makubwa Mnomonyoko mkali</p>

23.1 Muhtasari wa kronolojia ya Sahara ya kabla ya historia




23.2 ▲ Maeneo muhimu ya michoro na nakshi za mwambani ya Sahara (H.J. Hugot)



23.3 'Vifaa yva kukatia (Utamaduni wa mbwe) kutoka Aulef, Sahara ya Algeria (H.J. Hugot)

24.4 Shoka refu la mkono la Paleolithi ya Mwanzo - kutoka Tachenghit, Sahara ya Algeria (H.J. Hugot)






23.5 Buchari la Paleolithi ya mwanzo kutoka Tachenghit, Sahara ya Algeria (H.J. Hugot)



23.6 Chonge kubwa maradufu yenye sura mbili, tasnia ya Ateri, kutoka Timimun Sahara ya Algeria



23.7 Chonge ya Ateri kutoka Aulef, Sahara ya Algeria (H.J.Hugot)

## Enzi za Paleolithi

### Kutokea kwa Binadamu katika Sahara: Tasia na Zana za Mbwe

Tukiangalia matungazi ya mito ya zamani ambayo hivi sasa yamekwishakauka tutaona kwamba wakati mwingine yanaonyesha aina mbalimbali za tabaka ambayo kutokana na mfuatano wake kikronolojia na kistratigrafia, yameitwa matungazi ya kale, ya kati na ya nyuma.

Kwa mfano, huko Jebel Ijerane, karibu na In Salah katika Sahara ya Algeria, zana za mbwe zimeonekana katika matungazi ya kale. Tunajua, kwamba mbwe hizi ndizo zana za mwanzo ambazo zinaonyesha dalili kuwa zilitengenezwa na binadamu. Inadhaniwa kwamba zana hizo zilitengenezwa na *Homo habilis*, ingawa hakuna alama yoyote ya spishi hiyo ambayo imepata kuonekana katika Sahara.

Mikusanyiko mingine ya mbwe kama zile zilizopakana Aulef, au kwenye kingo za Mto Tefassasset na Mto Wadi Saura, yametawanyika au kuharibika.

Kwa bahati mbaya, hakuna visukuku vya wanyama au binadamu ambavyo vimeshagunduliwa kuanzia kipindi hicho na inaweza kudhaniwa tu kwamba zana hizo zisizokamilika, ambazo zinapatikana karibu pote katika Sahara, kwa hakika zilitengenezwa na walienga wetu wa zamani sana.

### *Homo erecto* mtengeneza zana zenye nyuso mbili

Utamaduni wa zana za mbwe ulifuatwa na Enzi ya Paleolithi ya Kale ambayo zana zake zilikuwa shoka la mkono na buhari. Ingawa mambo machache mno yanafahamika juu ya ekolojia ya Utamaduni wa Mbwe, tunafahamu zaidi mazingira ambamo watengenezaji wa zana zenye nyuso mbili waliishi.

Wakati huo Sahara ilikuwa eneo la maziwa makubwa yenye kiwango kikubwa cha maji na mvua zilitosheleza kuotesha aina ya mimea iliyoashiria kuwapo kwa tabia ya hali ya nchi ya ubaridi. Kutokana na mmomonyoko mkubwa uliosababishwa na athari ya upepo na maji, ushahidi wa kistratigrafia ni haba sana kwa kipindi hiki, iwapokuwa idadi kubwa ya zana zenye nyuso mbili zimeshapatikana kila mahali katika Sahara.

Huko Tihodaine, nchini Algeria, tasnia ya Asheuli imegunduliwa pamoja na mabaki ya faru, ndovu, kiboko, nyati, ngiri, pundamilia, mamba, paa, ng'ombe wa aina mbalimbali na spishi nyinginezo. Tasia ya Asheuli ya Tihodaine yaonyesha waziwazi kuwa ilikuwa imetokana na tasnia ya awali zaidi, na nyundo za mifupa na za miti zilitumika mara nyingi kutengeneza zana za ujeya. Kwa hivyo tasnia hii inawakilisha hatua ya maendeleo zaidi ya tasnia ya Asheuli na wala haikutokea mara tu baada ya Utamaduni wa Mbwe ulioitangulia.

Maeneo ya Tabelbala na Tachenghit, pia huko Algeria, yanajulikana sana kwa zana zenye nyuso mbili zilizotengenezwa kwa jiwemchanga la kwatzi lenye uwckunduwekundu, na hasa kwa aina mbalimbali za buhari zilizotengenezwa kwa mbinu ya hali ya juu ya kujeya ya Kilevallois. Katika sehemu hii ya Afrika, huko Mazer, Beni Abbes na Kerzaz, J. Chavaillon na H. Alimen wamegundua ushahidi dhahiri wa utamaduni wa Asheuli ambao ama ulitokea kabla tu ya tasnia zilizokuwa zikitengeneza zana za ujeya au ulikuwa sehemu halisi ya hatua ya Asheuli ya Kati.

Idadi kubwa ya vifaa vya Kiasheuli pia vimegunduliwa huko Aulef, Sherda, El Beyes na Esh-Shaheinab, Kharga, katika magharibi ya Sahara, na katika jangwa la Libya. Kwa hiyo

enzi ya Asheuli yaweza kusemwa kwamba ilienea katika sehemu zote za Sahara, lakini haiwezekani kukadiria umri wake kwa mfuatano kwani mbali na maeneo - manne au matano, mfuatano asilia wa kistratigrafia haupo tena. Kazi kubwa zaidi, hasa za uchimbujaji na za upimaji, zinahitaji kufanyika.

**Jambo linalohitaji ufafanuzi: tasnia za zana za ujeya.**

Ujuzi mkubwa zaidi wa sanaa ngumu ya ukataji nakshi katika mawe ulikuwa ndiyo sehemu ya sababu ya kutengeneza maumbo yaliyozidi katika ubora. Inaelekea maendeleo hayo yalitokana na utumiaji wa nyundo laini zaidi zilizotengenezwa kwa kutumia mbao au mifupa. Walakini, ingawa shoka lenye nyuso mbili linaweza kusemwa kwamba ndiyo zana iliyobainisha enzi za Paleolithi ya Kale, haikuwa ndiyo zana pekee iliyotengenezwa na *Homo erecto*. Kuna sababu nyingi zinazotufanya tuamini kwamba tangu wakati mbinu hiyo ilipoanza kutumiwa, zana za ujeya pia zilitumiwa, kama vile vyombo vilivyotokana na kubanguuliwa kwa vipande kutoka kwenye kiini cha mwamba. Ama kwa hakika kulitokeza ongezeko kubwa la zana za ujeya katika enzi za Paleolithi ya Kati. Maendeleo haya pia yaliambatana na upunguzaji wa ukubwa wa zana zenye nyuso mbili na ambazo hatimaye zikaanza kutumika kama vigumba.

Hatuna budi pia kutaja kuwapo kwa mbinu ya Kombewa huko Sahara ya magharibi ambayo inikuwa imeenea kusini mwa Afrika. Mbinu hii iliwezesha utengenezaji wa zana za ujeya zilizokuwa na makali pande zote. Zana za ujeya za aina ya Kombewa zinapatikana pamoja na zile za Asheuli katika eneo hili.

Kinyume chake ni kwamba maendeleo makubwa ya kimapinduzi yalihusu matumizi makubwa ya mbinu ya Kilevallois, ambayo ilionekana katika eneo la Sahara mapema sana; na ndiyo mbinu iliyozitangulia zile za utengenezaji wa buhari zilizopatikana pale Tachenghit na Tabelbala.

**Tasnia ya Ateri**

Katika hatua ambayo utafiti umeshaifikia hadi sasa, Tasnia ya Ateri katika Sahara inaweza kulinganishwa na ile ya Musteri katika sehemu nyingine kwa vile tasnia zote mbili zina sifa nyingi za namna moja kama vile utumiaji wa mbinu ya Kilevallois ambayo inaonekana si tu katika uchongaji mzuri bali pia katika aina ya zana zilizokamilika. Walakini, Tasnia ya Ateri inatofautiana na ile ya Musteri katika jambo moja: kuwapo kwa shina lenye kuchongoka vikombo, burini, au hata keeke. Kwa ufupi ni tasnia inayowakilisha wawindaji wanaohamahama. Yamekuwa mazoea kumhusisha *Homo sapi* na tasnia hii ya kuisimua.

Tasnia ya Ateri inakubalika kama tasnia ya Afrika Kaskazini ambayo ilienea kwenda mbali kusini na kuishia karibu na pwani za maziwa makubwa yaliyoko Sahara ya Kusini. Kadri ilivyokuwa ikielekea kusini, ndivyo ilivyozidi kuendelea kubadilika hadi kutengeneza vifaa vya kuvutia sana kama vile vya utamaduni wa Adrar Bous ainbako, pamoja na zana ambazo sasa zimegitwa za jadi kama vile violezo, nyembe, ujeya, vikombo, kolco, chonge zenye umbo la jani zilizotengenezwa kwa mbinu za utengenezaji wa zana zenye nyuso mbili na mawe ya mviringo, tunakuta pia chonge kali zilizotengenezwa kwa mbinu za utengenezaji wa zana zenye nyuso mbili.

Utamaduni wa Ateri umeenea sana. Unapatikana huko Tunisia, Moroko, katika Wadi Saura na Tidikelt huko Algeria, Mauritania ya Kaskazini, huko Ahaggar, Erg Admer, Tihodaine, Adrar Bous nchini Niger na hata katika Fezzan na Zumri nchini Libya.

Ni vigumu sana kuiweka Tasmania ya Ateri katika muktadha wake kikronolojia. Inawezekana tasnia hii ilitokea yapata miaka 35000 kabla ya enzi za Ukristo. Kwenye pwani za Ziwa Chadi, maendeleo ya tasnia hii yanaelekea kuwa yalikiwamishwa na kuongezeka kwa maji katika ziwa hilo, na kwa hiyo kutoweka yapata miaka 9000 hadi 7000 kabla ya enzi za Ukristo, ingawa hii ni nadharia tete tu.

Kwa hiyo katika juhudi za kulitatua suala la kikronolojia imependekewa kwamba Tasmania ya Ateri iwekwe chini ya kichwa cha habari kisichobishaniwa cha Paleolithi ya Mwisho. Hivi karibuni J.D. Clark alitumia istilahi ya Mesolithi ili kueleza tasnia iliyoibuka baada ya ile ya Ateri huko Adras Bous nchini Niger. Walakini, kutokana na maarifa tuliyonayo hivi sasa, si wanahistoria wote wanakubali kwamba palikuwa na kipindi cha Mesolithi au cha Paleolithi juu baina ya Paleolithi ya Mwisho na Neolithi.

### *Enzi ya Neolithi<sup>2</sup>*

Asili ya watu wa enzi ya Neolithi hajulikani sana. Inaelekea walizagaa katika eneo la Sahara kutoka sehemu tofauti. Kwa mijibu wa M.C. Chamla, inafikiwa kwamba jamii ya neolithi ya Sahara hubainishwa na mchanganyiko wa watu weusi na weupe wenye asili ya Mashariki ya Karibu, ambao kwa kawaida huitwa watu wa Mediterania.

### Waneolithi wa Kisudani wa mwanzo

Watu wa enzi ya Neolithi ya eneo la Sahara sio watu wa aina moja. Kama tukiangalia luja za makazi katika mpangilio wa ujaji wao, itaonekana kuwa makazi ya zamani kabisa ni yale yaliyokuwa kwenye kingo za Mto Nili karibu na Khartoum na Esh-Shaheinabi, na kisha yakasambaa kuelekea magharibi kwenye pwani za maziwa makubwa. Luja hii yaelekea haikuvuka sana kingo za mashariki za Aukar, nchini Mauritania, na wala haikuuingia msitu, lakini ilipenyeza mikondo miwili kuelekea kaskazini, mmoja ukielekea Ahaggar hadi kufikia ukingo wa kaskazini wa milima hiyo kabla ya kufika Tassili N'Ajjer, na mkondo mwingine uliondokea Tilemsi kuelekea Wadi Saura. Enzi hii ya 'Neolithi ya Ki-Sudani' inatambulika kwa urahisi kabisa kutokana na ufundi na pia utajiri wa mapambo yaonekanayo kwenye vyombo vya ufinyanzi. Kwa upande mwingine, ni vigumu sana kuelezea kwa usahihi tasnia za zana za mawe, kwa sababu watu wa Neolithi walikuwa stadi sana katika kutengeneza vyombo hasa kwa kutumia malighafi iliyokuwapo. Wakazi wa kwanza wa Sahara walikuwa wavuvi, wawindaji na wakusanyaji ambao hasa walipendelea nyama ya kiboko na matunda ya mwavi (*Celtis sp.*), bali pia walikula samaki kutoka kwenye maziwa, kasa wa maji baridi na matikiti. Ijapokuwa ni kweli kwamba walitengeneza vitu vingi kama vile tezo, majembe, vyombo au mawe ya kusagia, haina maana kwa walijishughulisha na aina yoyote ya kilimo. Sanasana, zana hizo zinadokezea kwamba mimea ya aina fulani ilitumiwa kwa chakula. Walitumia pinde na mikuki kwa kuwindia, kama inavyodhihirishwa na kuwapo kwa vigumba, chusa na ndoana za mifupa. Walikuwa stadi katika utengenezaji wa shanga za mawe magumu kama vile amazoniti, Kalisidoni, hematiti na akiki, na kwa ajili hiyo walitengeneza zana bora zaidi za kuchimbia, kama vile vibanzi vya burini, sindano na kekee ambazo huenda zilitumika pamoja na sandarusi na pia mchanga laini.

2 Neolithi: hii ni istilahi inayomaanisha kuzuka kwa mbinu mpya (hasa ufinyanzi ungarishaji mawe, ufugaji, kilimo na ujenzi wa miji) ambazo zilingizwa kwenye tasnia ya zana za mawe iliyostawi sana ya enzi ya Paleolithi juu.

Yaelekea watu hawa walikuwa wameshaelewa mbinu za ubaharia, na inawezekana kabisa kwamba walitumia mitumbwi ya matete kusafiria katika maziwa, kama vile mtumbwi wa aina ya kaddei ambao bado ungali ukitumiwa katika Ziwa Chadi.

### Waneolithi wa Kiguinea

Huko kusini, luja ya kwanza ya Waneolithi ilifuatiwa mara na luja nyingine yenye asili ya Kiafrika ambayo ilisambaa katika msitu, ambamo, ijapokuwa luja hiyo ilikuwa kubwa, mabaki yake yalifichwa na huo msitu kwa muda mrefu. Utamaduni huu wa Neolithi umeshabainika waziwazi nchini Guinea na ndiyo maana unseitwa wa-Neolithi ya Kiguinea, ijapokuwa pengine asili yake ilikuwa huko Afrika ya Kati.


### Utamaduni wa Neolithi wa mapokeo ya Kapsi

Baadaye kidogo, utamaduni wa Neolithi uliotokana na mapokeo ya Kapsi ambao ulikuwa matokeo ya uncolidushaji wa mahala pale wa utamaduni wa Kapsi ya Palcolithi ya Afrika Kaskazini, ulianza kuelekea Kusini. Ulifika Mauritania kutoka kaskazini-mashariki na ulienea hadi Ahaggar. Mathalani pale Manient dalili za utamaduni huo zimeonekana juu ya ardhi kwenye maeneo ambayo yalikaliliwa na Waneolithi wa mapokeo ya Ki-Sudani.

Vyombo vya ufynyanzi visivyokamilika vya utamaduni huu havikurembwa sana. Kwa upande mwingine, tasnia ya zana za mawe inatumia mbinu madhubuti, na mtindo wake katika Sahara unaonekana waziwazi kutokana na wingi wa vigumba. Zana za mawe zilizong'arishwa mara nyingi zinapendeza sana, na mabakuli ya mawe, magumu, na visanamu vya wanyama vilivyong'arishwa, ni vyombo vya sanaa ya hali ya juu ambayo inafidia ile kazi duni inayoonekana katika vyombo vya ufynyanzi. Shanga zilizotengenezwa kutokana na makaka ya mayai ya mbuni pia zimegunduliwa, ambapo mayai mazima, mengine yakiwa yamechorwa maumbo ya kijiometri, yalitengenezwa na kutumika kama chupa za maji. Matumizi ya mayai ya mbuni yaelekea yalikuwa mahususi kwa jamii za Neolithi zenye asili ya Kapsi. Mawe ya kusagia unga ambayo huenda yalitumiwa kusagia rangi, pia yamegunduliwa.

### Waneolithi wa pwani

Waneolithi wengine hasa wa pwani waliokuwa kaskazini zaidi, nao pia ni mchipuo wa Wapalcolithi. Kizazi hicho ni kile cha Waneolithi wa Iberia na Maurusi kilichoenea katika pwani ya Atlantiki ya Moroko. Pwani ya Sahara ya Mauritania nayo pia ilikaliliwa na utamaduni huu, lakini haujafanyiwa utafiti wa maana. Waneolithi wanaohusiana na mapokeo ya Iberia na Maurusi walikuwa wavuvi waliopenda sana kula samaki kombe, na kuna uslahidi kuwa walikuwepo katika eneo hilo kutokana na marundo ya makoa ya samaki kombe na ukiendelea zaidi unakuta makoa ya samaki wa aina ya *Arca senilis*. Vyungu vyao havina urembo mwingi na havikulainishwa. Zaidi ya hayo, mafiga na zana chache za mawe zimegunduliwa. Linge kuwa jambo la maana kulinganisha huu utamaduni wa kusini na ule wa kipindi kilekile uliokuwa kaskazini kwenye pwani ya Atlantiki ya Moroko.




23.9 Shoka la Kineolithi lenye mfuo kutoka Adrar Bous, Niger

23.8 Chonge za Kiateri yenye nyuso mbili na ncha mbili kutoka Adrar Bous V, Niger

23.10 Shoka la Kineolithi lilong'arishwa kutoka Faya, Chad





23.11 Ufinyanzi kutoka Akreijit, Mauritania (H.J. Hugot)

23.12 Ufinyanzi (vyungu) wa Kineolithi kutoka Dhar Tichitt, Mauritania (H.J.Hugot)



## Tasnia ya Tenere

Kwa kuangalia chonge zilizokuwa na umbo la yungiyungi, visahani, vikombe vizito vya mbonyeo, meno ya misumeno na mashoka yaliyokuwa na mipini mirefu, na pia kutokana na mwainisho wa vyombo vyake na idadi, tasnia ya Tenere yaclekea ilikuwa na mtindo asilia. Bado kuna umuhimu wa kuhakikisha ni kwa kiasi gani athari dhahiri kutoka nje ziliathiri tasnia kubwa ya Tenere, iliyokuwa na vifaa vya mawe vya kupendeza vyenye rangi ya njanonjano. Kwa vyovyote vile zana za tasnia hii zina maumbo mengi yanayokumbusha enzi ya Misri ya Kale kabla ya Ufalme. Vitu vyake vya udongo vimafanana kwa kila hali na vile vya Neolithi ya Sudani na pia vile vya Sudani ya Neolithi. Hata hivyo hatuna budi kufanya hadhari ili dhana ya "mtindo" isipotoshwe sana. Yale maeneo mawili, Adrar Bous na Gossolorum (ambako tasnia ya Tenere imehainishwa), ni ya utamaduni uleule lakini vyombo vya ufinyanzi, visahani, mashoka na zana nyingine sharti vichunguzwe kwa makini sana ili jambo hili liweze kuthibitika, kwani sifa pekee ambayo inajitokeza katika tasnia zote mbili ni kiwango cha juu cha ufundi.

## Neolithi ya Dhar Tichitt-Walata katika Mauritania

Maclezo mafupi yahitaji kutolewa kuhusu mtindo mzuri sana wa Neolithi uliogunduliwa kusini-mashariki ya Mauritania kufuatia Mto Dhar Tichitt-Walata. Uchimbuzi mwingi uliyofanyika katika sebemu kubwa ya enco hilo yameonyesha kwamba tasnia hii ambayo ni ya baadaye inahusiana na kikundi cha vijiji vilivyojengwa kwa kutumia mawe magumu, na vijiji hivyo vinavutia hasa kwa vile vilijengwa kimji, na ustadi uliotumika katika kujenga ngome. Kwa kweli, hapa tunapata ithubati kwamba jamii zilizoishi mahali pale zilianza kula ulezi yapata miaka 1500 kabla ya enzi za Ukristo, na hii inacleza sababu ya kuwapo kwa zana nyingi sana za kusagia zilizopatikana katika magofu ya vijiji hivi. Ustaarabu wa Dhar Tichitt-Walata ulikuwa wa Kiafrika, kama inavyoonekana katika ufinyanzi na sifa nyinginezo malhususi. Huenda ustaarabu huo ulitoka mashariki, na hasa pengine kutoka kwa majirani za Watilemsi, lakini hii ni nadharia tete tu.

Kwa ufupi, Neolithi ya Sahara inaweza kufikiriwa kuwa ilidumu kuanzia miaka 5000 kabla ya enzi ya Ukristo hadi mwanzoni mwa kikwi cha kwanza. Katika kipindi hiki, viwango vya maji katika maziwa viliendelea kupungua, hata kufikia wakati ambapo wanyama wakubwa waliojulikana kama wa Kiethiopia walikimbilia kwenye kingo za jangwa, mimea ikapungua, na binadamu naye akahama na mifugo yake.

## Wanyama na mimea

Wanyama walikuwepo katika Sahara tangu enzi ya Ateri, iliyomalizika wakati maziwa yalipojaa kabisa kwa mara ya mwisho, yapata miaka 8000 kabla ya enzi za Ukristo. Schemu hizi zimehusishwa na wanyama wa "Kiethiopia", kama vile faru, ndovu, mamba (*Crocodilus niloticus*), kiboko, pundamilia, twiga, nyati na ngiri. Maziwa nayo yalijaa fumi (clarias), sangara (*Lates niloticus-Nile perch*), na kasa wa maji baridi (*Trionyx*). Pia walikuwemo samaki kombe wengi, na marundo makubwa ya makaka ya kobe wa maji baridi yamepatikana katika baadhi ya schemu zilizochimbuliwa.

Mwanzoni mwa Neolithi ya Sudani maziwa yalika mbalimbali na yalibakia hivyo mpaka yakakauka kabisa. Maziwa yaliyoko Chadi hivi sasa ni ushahidi mdogo wa zama za kale.



Mimea ndiyo hasa hudhibirisha waziwazi jinsi tabia ya hali ya nchi ilivyoendelea kuharibika. Mwanzoni mwa Enzi ya Neolithi, mihazeli, midimu, miwilo, miashi na mierika ilikuwa bado inapatikana katika maeneo yenye milima. Walakini mimea hii ilififia haraka, na badala yake iliota mimea inayohimili mazingira ya ukame, ikiwemo micrezi, misonobari ya Alepo, mireteni, mizeituni na miti itoayo gundi, na miwavi, vitu ambavyo vilitumika katika kupika chakula cha sehemu ile.

### *Sahara kama chimbuko la kilimo*

Shughuli za kilimo haziwezi kusemwa zimethibitishwa na kuwapo kwa vifaa na zana ambazo huenda zilitumika kwa ajili hiyo.<sup>3</sup> Inawezekana kabisa kwamba vyombo hivyo pia vilitumiwa kwa shughuli za mimea ya porini kama ilivyotumiwa kwa mimea inayolimwa. Kuwapo kwa kilimo kunaweza kuonyesha kwa mbegu kisukuku na chavua bila kujali kama zimepatikana pamoja na vifaa hivyo au la, alimradi tu mofolojia yake ionyeshe dalili kwamba zimetokana na kilimo.

Tunachojua ni kwamba watu wa Neolithi walioishi katika Sahara walikuwa wakikusanya chakula kama vile matunda mwitu na mbegu za mjujube na miwavi na majani mwitu kwa wingi. Huko Menict na Tichitt pia kumegunduliwa mbegu za jamii ya vibuyu (*Curcubitaceae*), pengine matikiti. Mimea ya namna hii huonyesha wingi wa mavuno yaliyopatikana kwa ukusanyaji wa chakula; au huonyesha dalili za mwanzo kulima lakini siyo kilimo stadi ambacho kinahitaji kuvuruga udongo.

Kwa upande mwingine, karibu kila mahali wafugaji walichukua nafasi ya wawindaji, wavuvi na wakusanyaji tangu mapema sana. Kupungua kwa mvua hakukuwezesha kilimo kustawi, nacho kilishindikana wakati Sahara ilipokauka. Kwanza walikuwapo ng'ombe; wakafuatiwa na kondoo na baadaye mbuzi. Nadharia tete hii inaweza kuthibitika kwa vile katika sehemu nyingi za Sahara mabaki ya Neolithi yametapakaa juu ya usawa wa ardhi, na hayo yanakumbusha kuwapo kwa kambi za watu waliokuwa wakihamama kuliko wale waliojenga vijiji vya kudumu, ingawa kwa hakika vijiji kama hivyo vilikuwepo.

Wakati huohuo, huko kaskazini mwa Sahara, kile kilichojulikana kama 'enzi ya ng'ombe' kilikuwa kimeshamiri na kufikia kilele cha ustawi wake; inaclekea wafugaji walikwishapata mbinu kamili za uchungaji, jambo linaloonyesha kuwa walikuwa wamefanya kazi hiyo kwa muda mrefu. Katika Sahara michoro na nakshi ya miambani na masalia ya kiakiolojia vinadokeza kuwapo kwa ng'ombe na mbuzi yapata miaka 2000 kabla ya enzi za Kristo. Hatuna hakika kwamba wanyama hawa walikuwa wamefugwa kwa namna ya ufugaji tunavyouelewa hivi leo, lakini inaclekea kuna ushahidi kuwa baadhi ya wanyama walifugwa hasa katika Neolithi ya Ki-Sudani.

### *Hitimisho*

Utafiti unaosisimua wa hali ya zamani ya Sahara ndio kwanza umeanza na unawapa wataalamu na watu wa kawaida wanaopenda kujua habari za Sahara ya Kale, fursa nzuri ambayo sharti ichukuliwe haraka kabla inaliasili iliyosalia haijathaliwa yote na kuondoa uwezekano wa kuyafichua maajabu yanayohusu kale ya binadamu wote.

<sup>3</sup> Vifaa ambavyo huenda vilitumiwa kwa shughuli za kilimo ni pamoja na vifaa vya usagishaji, kama vile mawe ya kusagia, kuvunja, vinu, na vile vilivyotumika kwa ulimaji kama vile vijiti vya kulima, plau za kubemba, na pia schemu za misumeno na miundu.

Walakini, kipindi kabla ya historia ya Sahara hakiwezekani kuchunguzwa na mtafiti mmoja pekee. Imekuwa shughuli ya pamoja, inayohitaji kazi ya ushirikiano na kupatikana kwa fedha, na katika hali hiyo kwa bahati mbaya imepuuzwa. Wale walio na madaraka juu ya jangwa hili pana na kali wanawajibika kuwafunza watu watakaoweza kulikabili jangwa na kugundua siri zilizomo.



## *Historia ya Afrika Magharibi ya kipindi kabla ya historia*

### *Tabia ya hali ya nchi na mazingira*

Kanda kuu za tabia ya hali ya nchi kaskazini ya Ikweta huanzia mashariki kwenda magharibi kupitia eneo lote la Afrika Magharibi. Kanda hizi hulijumuisha jangwa kwa upande wa kaskazini kabisa, eneo la Saheli, na savana. Baina ya eneo la savana na ukanda wa mvua nyingi za kitropiki ulio kando ya pwani kuna eneo la savana ambalo hapo awali lilikuwa misitu lakini kwa sasa limeshakuwa mbuga halisi za savana kutokana na shughuli za binadamu.


Mabadiliko ya ruwaza ya mimea siku zote hutegemea wingi au uchache wa mvua. Hivi leo, mvua huletwa na pepo zitokazo kusini/magharibi ambazo hukusanya mvuke kutoka Bahari ya Atlantiki. Hata hivyo, maeneo ya kanda tofauti za mimea na nafasi ya pepo za kati ya tropiki vimekuwa vikibadilika huko nyuma, na hali hiyo iliyaathiri mazingira alimoishi binadamu katika Afrika Magharibi katika vipindi tofauti.

### *Binadamu wa kipindi cha kabla ya Historia*

#### *Mabaki ya awali kabisa ya kiunzi cha Binadamu*

Mpaka hivi sasa, Afrika Magharibi haijatao mabaki ya maumbo ya mwanzo kabisa ya watu au hominidi kama yale yaliyokwishapatikana Mashariki na Kusini mwa Afrika, wala vifaa vinavyowiana na tarehe za kale sana. Je, tunaweza kuchukulia kwamba vjumbe kama hao hawakuwako huko Afrika Magharibi? Swali hili hatuwezi kulijibu kwa sababu data za kiakiolojia hazitoshi. Isitoshe kuwapo kwa unyevunyevu mwingi na asidi katika udongo husababisha masalia ya kale yasihifadhike vizuri zaidi kuliko ilivyo katika maeneo yenye ukame au ukameukame.

Kwa hiyo visukuku vya wanyama na mabaki ya binadamu hupatikana kwa nadra sana. Lakini vipande vya fuvu la namna ya binadamu aitwaye *Tschadanthropus uxoris* vimepatikana karibu na Largeau, nchini Chadi, ila vipande hivi havikukamilika kiasi cha kuweza kuhusishwa kwa uhakika na jenasi ya Homo habili au Homo erekto. Hata hivyo, hamna mifano ya umbo la viumbe hawa waliotajwa mwisho huko Afrika Magharibi, ijapokuwa viumbe vinavyofanana navyo, viitwavyo *Atlantropus mauritanicus*, vimekwahi kupatikana huko Algeria.



24.1 Afrika Magharibi: maeneo ya uoto (C.T.Shaw)

## Vifaa vya mwanzo kabisa

Ijapokuwa binadamu wa kipindi kabla ya historia alitengeneza zana za mifupa na miti na pia za mawe, si rahisi kutunza vifaa vya miti, na hali za udongo huko Afrika Magharibi hazisaidii kuhifadhi mifupa. Mifano ya zana za mbwe imepatikana katika scheimu kadhaa za Afrika Magharibi, lakini kwa hivi sasa ni vigumu kuwa na hakika kwamba baadhi ya zana hizo zilitengenezwa wakati mmoja na zile za tasnia ya Oldowan ya Afrika Mashariki, ambayo inakadiriwa kuwa ilitokea kati ya miaka milioni 2 na 0.7 iliyoipita. Uchunguzi makini wa zana za mbwe zilizopatikana kando ya Mto Gambia nchini Senegal umedhihirisha kwamba baadhi ya zana hizo zielekea kuwa za enzi ya Neolithi na nyingine luenda zilikuwa za Enzi ya Mawe ya nyuma. Kutokana na Paleontolojia, kumepatikana baadhi ya makadirio ya unri wa mashapo ya Yayo nchini Chadi na mashapo hayo yamedhihirisha kuwepo kwa *Tschadanthropus*, lakini kwa bahati mbaya hapakupatikana zana alizozitumia.

## Mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi

Hivi karibuni, mambo mawili yamesaidia kuendeleza mkabala wa kisayansi katika Afrika Magharibi: kuongezeka kwa utafiti unaotakikana, na kutokea kwa nadharia mpya inayoelezea mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi katika Afrika.

Hatuna taarifa ya kuuminika ya kijiolojia au kijiomofolojia kuhusu Afrika Magharibi ambayo inaelezea mabadiliko ya awali ya tabia ya hali ya nchi. Utafiti uliofanywa kwenye ziwa la Chadi umeonyesha kuwapo kwa kiwango kikubwa cha maji kuanzia miaka 40 000 kabla ya enzi za Ukristo. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kipindi cha unyevu mwingi wakati ambapo msitu wa Afrika Magharibi ulienea kaskazini zaidi kuliko pale ulipo hivi sasa, kisha, kuanzia karibu miaka 20 000 kabla ya enzi za Ukristo, Afrika magharibi inaelekea kuwa ilipatwa na hali ya ukame mkubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Katika kipindi hicho mito ya Afrika Magharibi ilikuwa inamwaga maji katika bahari ambayo ilikuwa kiasi cha meta 100 chini ya kiwango chake cha hivi sasa kwa maji mengi yalikuwa yamekusanyika katika tando barafu za ncha ya dunia. Kwa hiyo unito ya Senegal na Niger ilipita chini kabisa ya kiwango cha sasa, na mikondo yake ilizibwa na matuta makubwa ya mchanga. Ziwa Chadi lilikuwa kavu wakati huo na matuta ya mchanga yalijaa kwenye kitalu chake katika baadhi ya scheimu za Nigeria ya kaskazini vikiashiria kiwango kidogo cha mvua kuliko ilivyo hivi sasa. Ushahidi mwingine wote unaonyesha kwamba palikuwa na hali ya ukame kwa jumla yapata miaka 18 000 kabla ya enzi za Ukristo. Ikiwa matuta ya mchanga yalikuwa yamejaa huko katika latitudo ya Kano, hapana shaka kuwa savana na kanda za misitu zilikuwa kusini zaidi. Kwa kweli inawezekana kabisa kwamba msitu ulitoweka isipokuwa katika sehemu chache zilizobakia zenye mvua nyingi kama vile kwenye ukanda wa pwani ya Liberia, sehemu ya ukanda wa pwani ya Ivory Coast, delta ya Niger na milima ya Kameruni.

Ilipofikia miaka 10 000 kabla ya enzi za Ukristo, hali ya mazingira ilianza kuwa ya umajimaji tena. Nchini Mali, Mto Niger ulifurika na kuenea katika sehemu kubwa, wakati ambapo matuta ya mchanga yalivyokuwa yamejaa katika kipindi cha ukame kilichotangulia yaligeuka kuwa mekundu kutokana na hali ya umajimaji iliyotokea kwa msimu. Katika kipindi hicho, msitu ulianza kuenea tena kuelekea kaskazini. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kwamba kipindi cha ukame huko Afrika Magharibi kilitokea karibu wakati mmoja na kile kipindi cha barafuto kilichotokea katika kizio cha dunia cha kaskazini. Wakati huohuo, hali

ya umajimaji iliongezeka huko Sahara ya Kaskazini kuliko ilivyo sasa kutokana na mvua zilizokuwa zikitokea kwenye Bahari ya Atlantiki.

Mwishowe kadiri halijoto ya dunia ilivyoongezeka, tando barafu ziliyeyuka na kurudi nyuma kaskazini. Ukame ulizidi kuongezeka katika Sahara, lakini kulikuwa na akiba ya kutosha ya maji chini ya ardhi na mimea iliyochelewesha ukaukaji wa ardhi mpaka yapata miaka 3000 kabla ya enzi za Ukristo. Walakini, jinsi eneo la Sahara lilivyoendelea kukauka, likawa halikaliki, na watu waliokuwa wanaishi huko walihamia sehemu za kusini zaidi.

### *Enzi ya Mawe*

Istilahi za Enzi ya Mawe ya Mwanzo, Enzi ya Mawe ya Kati na Enzi ya Mawe ya Nyuma zitatumiwa kuonyesha vipindi vya kabla ya historia katika Afrika Magharibi. Mipaka ya kikronolojia ya migawanyo hii ya Enzi ya Mawe kwa kiasi fulani hutofautiana kutoka eneo moja hadi jingine, lakini, kwa kukisiakisia, migawanyo hiyo inaweza kufikiriwa kuwa ya kati ya miaka 2 500 000 hadi 50 000 kabla ya enzi ya Ukristo kwa Enzi ya Mawe ya Mwanzo, miaka 50 000 hadi 15 000 kabla ya enzi za Ukristo kwa Enzi ya Mawe ya Kati, na miaka 15 000 hadi 500 kabla ya enzi za Kristo kwa Enzi ya Mawe ya Nyuma. Zaidi ya hayo, istilahi ya Neolithi inavyotumika kwa Sahara na Afrika Magharibi hutatanisha, kwani huwa haeleweki waziwazi kama inahusu kipindi, aina ya teknolojia, aina ya uchumi, au mchanganyiko wa mambo yote matatu.

### **Enzi ya Mawe ya Mwanzo katika Afrika Magharibi**

Zile zana zinazofikiriwa kuwa aina za mwanzo za nyuso mbili (zamani zikiitwa za Shele) hazipo katika eneo la Sahara ila zimedaiwa kuonekana nchini Senegal, Jamhuri ya Guinea, Mauritania na Ghana ambako zimethibitishwa kistratigrafia kuwa ziko katika hali ya mbingiriko katika matope ya mikondo ya zamani ya mito. Enco la mweneo wa zana hizo limekwishaonyeshwa katika ramani na linaelekea kuwa lilikalikiwa na watu kutoka Mto Niger kwenye safu ya milima ya Atakora na vilima vya Togo. Zana hizo na nyingine pia za mawe zimetambuliwa kuwa ni za kipindi cha Asheuli.

Zana za baadaye za Asheuli zinazodhihirishwa mashoka mazuri ya mikono yaliyotengenezwa kwa miti myepesi au nyundo za mifupa, zimeenea sana katika Sahara na zinaonekana kwa wingi kuliko katika vipindi vilivyotangulia. Labda mweneo huu unaweza kuhusishwa na kipindi kilichokuwa na mvua nyingi zaidi huko Sahara ya kaskazini na ukanda wa jangwa ulipojongea kusini na hivyo havikuwavutia sana wawindaji na wakusanyaji. Sehemu ambayo haikuhusika ni ile ya uwanda wa juu wa Jos, nchini Nigeria, ambako tabia ya hali ya nchi haikuwa ya ukame, na huenda ilisababisha kuwepo kwa mbuga ambazo zilipendelewa na binadamu wa enzi za Asheuli. Tabaka za udongo katika eneo hilo zimekadiriwa kuwa na umri wa zaidi ya miaka 39 000 kabla ya sasa.

Katika kipindi hichohicho, inawezekana kabisa kwamba eneo la Milima ya Futa Jallon nchini Guinea, pia lilikalikiwa na watu, na kiasi fulani cha zana za Asheuli kimepatikana katika eneo hilo. Mabaki ya Enzi za Kati na za Nyuma za Akeuli yakionekana yametawanyika kaskazini mwa sehemu ya juu ya Mto Senegal, eneo linaloweza kuchukuliwa kuwa linaunganisha eneo la Futa Jallon na maeneo yaliyozagaa ya Mauritania.


Alama za kuwepo kwa vifaa vya Kiasheuli zimeonekana kusini-mashariki ya Ghana na kwenye safu ya vilima vya Togo/Atakora, zikiashiria kuwa maeneo haya, ambayo yalikuwa na mazingira muafaka, yalipenywa kutoka kaskazini.



**24.2** Vidani vya mawe (basalti) kutoka eneo la Neolithi la Patte d'Oie (I. Diagne, Makumbusho ya IFAN)

**24.3** Zana ya kulainishia mifupa, iliyogunduliwa katika eneo la Neolithi la Rus Manuel (I. Diagne, Makumbusho ya IFAN)

**24.4** Jiwe la kusagia lilotengenezwa kwa mwamba wa volkano, lililogunduliwa katika eneo la Neolithi la Ngor (I. Diagne, Makumbusho ya IFAN)



*Tasnia ya Sango*

Yapo matatizo ya ufafanuzi wa changamano ya Tasnia ya Sango, na kwa hakika watu wengi wana shaka kama kweli tasnia halisi ilikuwepo huko Afrika Magharibi. Kufuatia tasnia ya Asheuli palitokea changamano ya tasnia ambazo ziliendelea kutumia baadhi ya zana za Asheuli kama vile sururu na zile zenye nyuso mbili, ijapokuwa buchari ilitoweka, na vyombo vya umbo la tufe vikaadimika. Palikuwa na sururu nyingi ambazo mara nyingi zilikuwa nzito na nene. Vishoka vilivyotengenezwa kwa mbwe za ujeja pia vilipatikana.

Huko Afrika Magharibi, zana za tasnia ya Sango zimesambaa zaidi kusini kuliko zile za Asheuli, na hii inaonyesha ruwaza mpya ya makazi, kama vile huko Cape Manuel nchini Senegal, sehemu ambayo hapo awali ilifikiriwa kama ilikuwa ya Neolithi; pia huko Bamako nchini Mali; kusini ya uwanda wa juu wa Jos nchini Nigeria; na kwenye inabonde ya mito, kama vile katika bonde la Mto Niger karibu na Bussa. Katika safu ya vilima vya Atakora Togo hadi kusini mwa Ghana, kumeonekana idadi kubwa ya vifaa vya tasnia ya Sango. Vifaa hivyo ni haba kaskazini mwa Ghana, ila vimezagaa sana sehemu za kusini.

Hata hivyo, ukadiriaji umri wa tasnia ya Sango katika Afrika Magharibi kwa kutumia radio-kaboni haujafanyika. Inawezekana kwamba mweneo wa tasnia ya Sango ulielekea kusini, ukifuata mito na misitu huko Afrika Magharibi, unawakilisha mtindo wa maisha uliojinabisha na mazingira kama yapata miaka 40 000 kabla ya enzi za Ukristo, na baada ya hapo Ziwa Chadi lilianza kujaa na kupanuka.

*Enzi ya Mawe ya Kati katika Afrika Magharibi*

Istilahi ya Enzi ya Mawe ya Kati imetumiwa kuelezea kikundi cha changamano za tasnia zilizotokea katika kipindi kinachokisiwa kuwa kati ya miaka 35 000 hadi 15 000 kabla ya enzi za Ukristo. Katika Afrika Magharibi, tasnia ziambatanazo na Enzi ya Mawe ya Kati hazikutambuliwa kwa uhakika kama ilivyo kwingineko katika Afrika, kusini mwa Sahara. Vielelezo adimu vya Tasnia ya Lupemba vimeonekana nchini Ghana na kwenye uwanda wa juu wa Jos na kwenye vilima vya Lirue nchini Nigeria. Huko Nok, hapo awali tasnia hizi zilijulikana kama za Lupemba, lakini sasa zinafikiriwa kuwa zinahusiana zaidi na tasnia za Paleolithi ya Kati zenye mapokeo ya Kimusteri. Tasnia zinazofanana nazo zimeonekana Ghana na Ivori Coast, Dakar na Sahara ya Kati.

Huko Tiemassas, karibu na pwani ya Senegal, uchimbuzi wa kiakiolojia umeonyesha chonge zenye nyuso mbili, miongoni mwa zana nyingine, pamoja na vifaa vingine vya aina ya Paleolithi ya Kati na ya Nyuma. Awali kabisa vifaa hivi vilidhaniwa kuwa viliwakilisha mchanganyiko wa vifaa vya Neolithi na vingine vya mapema kuliko hapo, lakini baadaye vilitambuliwa kuwa ni vya mapokeo ya Kimusteri. Tatizo la uainishaji wa vifaa hivi halijatatuliwa kwa vile mifuatano yake ya kistratigrafia haipo.

*Enzi ya Mawe ya Nyuma na ya Neolithi*

Katika sehemu kubwa ya Afrika Magharibi, Enzi ya Mawe ya Nyuma inadhihirishwa na kuonekana kwa zana ndogo ndogo za mawe, zijulikanazo kama mikrolithi. Na hapo ndipo tunapokabiliwa na tatizo la neno 'Neolithi' na utata wa maana yake. Katika Afrika, neno hili lapaswa kuepukwa na hasa tunapozungumzia Afrika kusini mwa Sahara.

Tukiliangalia suala hili sambamba na hali ilivyokuwa huko Afrika Kaskazini na katika eneo la Sahara, ilitokea wakati ambapo zana zilizochimbuliwa kutoka Rufisque nchini



Senegal zilihusishwa na enzi ya Neolithi ya Mapokeo ya Kapsi, lakini huenda inafaa kuziangalia zana hizo kama mwendeleo wa mikrolithi, au 'Mikrolithi ya Guinea' ambayo imeenea sana katika nusu ya mashariki ya Afrika Magharibi. Kwa upande mwingine, katika nusu ya magharibi mwendeleo huo haupo katika machimbo ya sehemu za kusini, katika enco la Liberia, Sierra Leone na kusini ya Jamhuri ya Guinea. Upo uwezekano kwamba aina fulani ya kilimo inaweza kuhusishwa na huo mwendeleo, kwa vile mpunga ulianza kuchukua nafasi ya viazi vikuu kama zao kuu la chakula katika nusu ya magharibi ya Afrika Magharibi. Huu mpunga wa Kiafrika, *Oryza glaberrina*, huenda ulianza kulimwa katika eneo la delta ya kati ya Niger. Vipande vipana na bapa vya kwatzi vilivyochongwachongwa pia vinafikiwa kuwa vilitumiwa kama majembe na kuchukuliwa kama ushahidi wa kuwapo kwa kilimo nchini Ghana; lakini hakuna uhusiano wala tarehe bayana kati ya vitu hivi viwili. Ufinyanzi unaelekea haukuwa umeneea sana katika sehemu hizi.

Kwa hiyo, inaelekea kana kwamba kulikuwa na aina fulani ya utamaduni wa Enzi ya Mawe ya Kati katika sehemu za magharibi ya Afrika ya Magharibi (ambao pia umebainika huko Dakar na Bamako), na ambao ulibakia bila kubadilika kwa kiasi cha kuonekana katika sehemu za maeneo ya kusini, na haukutumia wala kuendeleza mbinu ya kimakrolithi; sababu za tukio hili zinaweza kuwa za kiekolojia, kwa vile mbinu ya kimikrolithi inalusiana na uchumi wa kanda ya mbuga za savana ambako uwindaji ulikuwa muhimu sana. Ikiwa mtu atachora ramani ya mwendo wa maeneo ambayo hayakuwa na mikrolithi, kama vile Conakry, Yengama na Blande, na zile zenye mikrolithi - Kamabai, Yagala, Kindia, na Nhampassere - itaonekana kwamba mpaka unaozitenganisha sehemu hizi uko karibu sana na ule unaotenganisha misitu na mbuga za savana. Bidaa za kitknolojia za mashoka ya mawe yaliyochongwa na ufinyanzi hatimaye iliingia katika eneo hilo kutoka kaskazimi. Tarehe za athari hizi zimekadiriwa kuwa katikati ya kikwi cha tatu kabla ya enzi za Ukristo, wakati ambapo ukame katika Sahara ulikuwa umeneea. Inafaa kuunganisha matukio haya mawili na kuona athari ya watu waliokuwa wakihamia Sahara, ingawa mpaka sasa hakuna ushahidi uliotokana na ugunduzi wa mifupa ya binadamu.

Katika sehemu kubwa iliyobaki nchini Afrika Magharibi, awamu ya mikrolithi inazitangulia mbinu za ufinyanzi na utengenezaji wa mashoka ya mawe yaliyochongwa, mbinu ambazo zilibandikizwa kwenye mapokeo ya mikrolithi badala ya kuchukua nafasi yake.

Nchini Ghana, baada ya awamu ya awali yenye ufinyanzi na mikrolithi, utamaduni wa Kintampo ulikuwa na mashoka ya mawe yaliyochongwa, bangili za mawe - kutoka Sahara ambazo zajulikana sana - na aina ya pkee ya jiwe la kusugulia lililorembwa ambalo lilitengenezwa kwa mbinu ya kugongagonga. Awamu ya awali (Punpun) ya utamaduni huu ilitokea zaidi ya miaka 1400 kabla ya enzi za Kristo ambapo awamu iliyofuata imeonyesha kuwapo kwa mbuzi waliodumaa na ng'ombe wadogo wenye pembe fupi wanaofugwa hivi sasa huko Afrika Magharibi.

Kwenye ukingo wa kaskazini wa eneo hili, katika eneo la Saheli lililoko kusini tu mwa Sahara, palitokeza hali tofauti kidogo katika sehemu ya mwishoni ya Enzi ya Mawe ya Nyuma kutokana na kujinasibisha kwake na ekolojia ya mali ali pale kama inavyodhiliirika katika utamaduni wa zana. Huko Karkarichinkat, kaskazini mwa Gao nchini Mali, wafugaji ambao pia walikuwa wakishughulika na uvuvi, waliishi hasa juu ya vilima vilivyokuwa vimeinuka zaidi kuliko vijito vya msimu kati ya miaka 2000 hadi 1500 kabla ya enzi za Kristo. Walikuwa na vyombo vya ufinyanzi na walitumia vigumba na mashoka ya mawe yaliyochongwa pengine na mikrolithi.

Miaka elfu moja baadaye, huko Daima, kaskazini-mashariki ya Nigeria, inawezekana kabisa kwamba wafugaji wa ng'ombe pia walilima mtama kwenye udongo wa mfinyanzi uliokuwa na rutuba, ambao uliachwa baada ya kiwango cha maji kupungua katika Ziwa Chadi. Walikuwa na vyombo vya ufinyanzi na mashoka ya mawe yaliyochongwa na tasnia iliyoenea sana ya zana za mifupa, bali hapakuwa na mikrohithi.

Unasibishaji wa aina mahsusi kwenye mazingira tofauti kabisa ya kiekolojia ulitokwa upande wa pili wa eneo hilo kando ya kingo za kusini za Afrika Magharibi, kwenye pwani ya Atlantiki. Hapa watu wa Enzi ya Mawe ya Nyuma walijinufaisha kwa kufaidi samakikombe waliojaa katika wangwa na delta, ama kwa kuvua au kwa kuwakusanya ukingoni mwa pwani. Mabaki ya makoa hayo ndiyo yaliyojenga vichuguu vya makoa vilivyopatikana Ivory Coast (kuanzia miaka 1600 kabla ya enzi za Kristo hadi kufikia karne ya 16), Senegal na Nigeria (kati ya miaka 3000 hadi 1000 kabla ya enzi za Kristo).

Wakati wafugaji wa ng'ombe walipoelekea kusini kwa inara ya kwanza yapata miaka 3000 kabla ya enzi za Kristo, siyo tu kwamba walikutana na wawindaji wa enzi ya mikrolithi, bali walilihama eneo ambalo lilikuwa na mawe ya flinti, na kwenda katika eneo lililojaa mawe ya kwatzi, ambayo hayakufaa sana kutengenezea zana zenye nyuso mbili. Huko Ntereso, katika Ghana ya Kati, mahali ambapo umri wake umekadiriwa kuwa wa milenia ya pili kabla ya enzi yetu, ndilo eneo pekee lililobakia na mbinu hii ya kujeya.

Uhamaji huu wa watu unaelekea haukuwa na athari yoyote ya kuonekana juu ya maumbile ya watu kwa sababu jamii zote mbili zilikuwa za Kinegro. Kitu kilichokuwa muhimu ni upandaji wa majanipori mwafaka kwa chakula ambayo yalizia mitama inayolimwa katika Afrika. Mmea muhimu ulikuwa Sorghun bicolor au "mtama", ambao ulilimwa mnamo nusu ya kwanza ya kikwi cha pili kabla ya enzi yetu katika eneo lililo kati ya Sahara na mbuga za savana kutoka Mto Nile hadi Ziwa Chadi. Majanipori mengine yaliyoanza kulimwa ni mtama mweupe na ulezi, na hususa mpunga wa Kiafrika.

Katika seheinu zenye mvua nyingi za Afrika Magharibi, chakula kikuu kilikuwa viazi vikuu ambavyo zaidi ya aina moja ya viazi vya Kiafrika vililimwa. Walakini, hadi sasa hatuna ushahidi wa kiakiolojia wala wa kibotania kuhusu tarehe za mwanzo kabisa ambapo kilimo hicho kilianza. Tatizo ni hilohilo kwa chikichi. Hata hivyo msingi imara wa kilimo ulikwishawekwa kunako kikwi cha mwanzo cha enzi za Ukristo, ambapo kilimo kiliimarisha falme za zamani za Ghana, Mali, Songhay, Benin na Asante.

### *Kuja kwa metali*

Kwa nini hapakuwa na Enzi ya Shaba Nyeusi katika Afrika kusini mwa Sahara, na kwa nini eneo hilo halikuathiriwa zaidi na ustaarabu wa zamani wa Misri? Sababu zenyewe zinahusika kwa kiasi fulani na ule ukweli kwamba milenia ya tatu kabla ya enzi za Ukristo wakati ambapo athari hiyo ingetokea, ndiyo kikwi ambamo jangwa la Sahara lilikauka kwa mara ya mwisho, na kwa hivyo halikuendelea kutumika kama kiungo kisichokuwa cha moja kwa moja kati ya Misri na Afrika Magharibi.


### *Enzi ya Chuma ya Mwanzo (tangu kama miaka - 400 hadi kiasi cha + 700)*

Afrika Magharibi ilijifunza habari za chuma kutoka nje ya eneo hilo. Hali hii haikuishia tu katika uagizaji wa vitu vilivyokwishatengenezwa bali pia katika maarifa ya kufua chuma. Huko Taruga, Nigeria ya kati, maeneo kadhaa ya kuyeyusha chuma yamekwisha chimbuliwa na umri wake umekwisha kadiriwa, kwa kutumia radio-kaboni, kuwa ni wa kati ya karne ya



24.5 Duara la kimegalithi, Tiekere Bussura, Senegal; "kaburi la mfalme" linaonekana mbele (I Diagne, Makumbusho ya IFAN).


24.6 Chungu chenye kitako bapa cha Enzi ya Chuma (I Diagne, Makumbusho ya IFAN).



tano hadi ya tatu kabla ya enzi yetu. Machimbo yaliyofanywa katika miinuko iliyokaliwa na watu katika bonde la Mto Niger pia yanaonyesha kuwapo kwa shughuli za uyeyushaji chuma kunako karne ya pili kabla ya enzi za Ukristo.

Kadri tunavyojua inaelekea kwamba staarabu mbili ndizo zimeleta mbinu hii huko Afrika Magharibi: Wagaramante wa Afrika Kaskazini na ufalme wa Meroe, nchini Sudani. Kiwango na namna mbinu hii ilivyoletwa bado havijaeleweka. Mfano mwingine zaidi ni life eneo la Taruga, ambapo idadi kubwa ya visanamu vya udongo mwekundu vinavychusishwa na utamaduni wa Nok, vimekadiriwa kuwa vya umri wa tangu mwaka - 620. Vilionekana pamoja na vitu vya chuma na mabomba ya kuyeyushia chuma ambayo si rahisi kukadiria umri wake. Vile visanamu vinaweza kuwakilisha taswira za wahenga wa Wayoruba wa leo.

Karibu na Mto Gambia, nchini Senegal na Gambia, kumegunduliwa idadi kubwa ya nguzo za mawe zilizochongwa vizuri, ama zikiwa mbalimbali au zimepangwa kiduara. Zile zinazoonekana wazi kabisa zimekaa mbilimbili na zinafanana na umbo la kinubi. Machimbo yaliyofanywa jirani na nguzo hizo yametoa tarehe tatu za radio-kaboni katika karne ya saba na ya nane ya enzi za Ukristo. Nguzo hizo zinaelekea kama zilikuwa minara ya kaburi. Rundo la mawe la aina hiyo hiyo liligunduliwa huko Tondidaru, katika eneo la kati ambapo



24.7 Sanamu ya umbo la intu iliyopatikana katika eneo la Thiaroye, Senegal. (I. Diagne. Makunbusho ya IFAN)

Mto Niger unepinda, ila mawe hayo yamekwishaharibiwa.

Kwenye kingo za kaskazini za Afrika Magharibi, jamii za Wanegro zilikutana na zile za Waberiberi wa jangwani waliokuwa wanahamama na ambao walikuwa na ngamia na walisafirisha dhahabu kutoka Afrika Magharibi kupeleka kaskazini. Hata kufikia mwisho wa karne ya nane ya enzi yetu, umaarufu wa 'Ghana, nchi ya dhahabu' ulienca hadi Baghdad. Sehemu hizi za kaskazini za Afrika Magharibi sasa zilikwihapata teknolojia ya kilimo na ya chuma. Kusini zaidi, kaskazini mwa Sierra Leone, chuma kilianza kutumiwa baadaye kabisa, tena polepole, na siyo kabla ya karne ya nane ya enzi za Ukristo. Lakini kipindi hicho tayari kimekwishaingia katika uwanja wa historia halisi.

# 25

## *Kipindi kabla ya historia katika bonde la mto Nili*

Sudani, Nubia na Misri, ambazo ni kanda tatu tofauti zinazounganishwa na mto mmoja, zote ni schemu za bonde moja. Lakini leo, wakati hali za tabia ya hali ya nchi na za kolojia zinatofautiana, ni vigumu kufikiria kuwa jangwa kubwa linalolizingira bonde lilikuwa sehemu ya makazi na kiungo cha mawasiliano na sehemu nyingine za Afrika; au kwamba tabia ya hali ya nchi na ekolojia vilivyobadilika ndivyo jangwa lilivyozidi kuwa kikwazo kisichopitika.

Sababu za kimaumbile pia zilifanya namna ya maisha ya wakazi wa awali wa bonde hilo yawe maisha ya mapambano ya daima ya kujinasibisha na mazingira mazuri au mabaya. Kutokana na usuli huo, tunaazimia kutoa maelezo mafupi ya mabadiliko yao ya muda mrefu toka binadamu wa mwanzo hadi kufikia jaha za kipindi cha Mafarao, tukizingatia kuwa Misri lilikuwa imeshajidhihirishia sifa zake bainifu tangu enzi za Neolithi.

### *Utamaduni wa Kioldowani*

Sifa muhimu ya utamaduni huu ambayo imeenea sana ni kuwepo kwa zana za mbwe au vishoka. Tangu mwaka 1971 utafiti uliofanyika kwa namna iliyo wazi huko Thebes, Misri ya Juu, umedhihirisha matabaka ishirini na matano ya tope yaliyotoka tangu miaka ya awali ya enzi ya Kwatenari. Ugunduzi wa maeneo matatu yenye tope yaliyokuwa na zana za mbwe uliofanyika mwaka 1973 ulitoa maelezo muhimu sana ambayo yaliondoa wasiwasi kama hominidi wa awali walikuwepo Misri au la. Mikusanyiko ya zana za mbwe iligunduliwa chini ya matabaka ya Asheuli ya Awali, au Enzi ya Mawe ya Nyuma, ambayo hubainishwa na kuwepo zana za sura tatu katika sehemu zake za zamani kabisa. Hivi karibuni, jino moja la hominidi liligunduliwa pamoja na vishoka katika matabaka ya awali ya tope katika mwinuko wa Thebes, ingawa spishi yenyewe bado haijatambulika. Ugunduzi huo unathibitisha ugunduzi wa awali wa zana za mbwe uliofanywa huko Abbassia karibu na Kairo, innamo mwaka 1925, na hivi karibuni huko Adaima, katika Misri ya Juu. Haijawezekana kukadiria umri halisi wa changamano zote hizi.

### *Enzi ya Mawe ya Mwanzo*

Katika bonde la Mto Nili kuna ushahidi wa utamaduni huu unaonekana katika schemu yote toka Sudani hadi Misri bila tofauti zenye kudhihirika. Kutokana na uchunguzi uliofanyika hivi karibuni, utamaduni huo unajulikana vema zaidi Sudani kaskazini kuliko kusini zaidi. Asheuli ya Kale, inayowakilishwa na mashoka ya mkono yenye ncha za mawiombi, ambayo

baadhi yake ni ghafi, hupatikana pamoja na zana za mbwe huko Atbara, Wawa na Nuri. Asheuli ya Kati na ya Nyuma, ambazo zimefanyiwa utafiti zaidi kuliko huko kaskazini, zinajulikana sana kutokana na ustadi wake mkubwa katika kazi za mikono na kutokana na kujitokeza kwa mara ya kwanza kwa tasnia za kabla ya Levallois. Hizi baadaye zilizaa mbinu halisi ya kujeya ya Levallois, ambayo huonekana huko Khor Abu Anja. Hivi karibuni huko Khor Abu Anja na Sai, nchini Sudani kumegunduliwa vielelezo vya tasnia ya Sango ambayo hadi wakati huu ilikuwa inajulikana zaidi katika Afrika ya Kati na ya Kusini, na ambayo inaelekea kupoteza sifa zake bainifu chini ya Wadi Halfa. Buchari chache zenye nyuso mbili zilizokatwa mshazari upande wa mwisho pia zimepatikana huko Sudani.

Katika Unubi ya Misri, tasnia ya Asheuli imegunduliwa kwenye matungazi za zamani ya mito. Hata hivyo, katika Misri, maeneo yenye matabaka yaliyo Abbasia karibu ya Kairo, yaliyofanyiwa uchunguzi hivi karibuni huko Thebes, 1974, na matungazi ya kale ya Mto Nili, yameonyesha tasnia za Asheuli katika mfuatano wa tabaka. Kila mahali huko Misri na Nubia inawezekana kufuatia ruwaza ya maendeleo ya kiteknolojia na ya kitamaduni kuanzia utengenezaji wa mashoka yenye nyuso mbili hadi mbinu za kujeya za Levallois.


Eneo la Kharaga lina matabaka yaliyorundikana ya kipindi cha Asheuli cha hivi karibuni kinachoishia katika Enzi ya Mawe ya Kati. Wakati zana za nyuso mbili huonyesha maumbo ya kawaida yaliyogunduliwa kwingineko, hupatikana pia vielelezo vya zana zilizoundwa upya ili kutengeneza buhari kwenye scheinu yake ya mwisho, na kwa hakika, hivi sasa hii ndiyo aina pekee ya buhari inayojulikana huko Misri. Vilevile mashoka yanayohusiana hasa na Misri ni yale yaliyotengenezwa kutokana na mbinu inayofanana na ile ijulikanayo kama *Victoria West*. Mbinu hii inahusu ubanduzi wa ujeya mkubwa, aghalabu kutoka upande mmoja au pengine kutoka katika ncha mojawapo na baadaye kuutumia ujeya wenyewe.

### *Enzi ya Mawe ya Kati*

Mabadiliko katika mtindo wa maisha yalisababisha matumizi ya jumla ya ujeya badala ya mashoka ambayo yalizidi kuadimika na hatimaye kupotea kabisa. Zana hizi za ujeya, ambazo zilikuwa na mashina yaliyo na nyuso nyingi na ambazo aghalabu zilitengenezwa kwa mbinu za kabla ya Levallois zilizokwishatajwa, zilitokana na kiolezo ambacho kilitoa njeya za umbo lililokuwa limekusudiwa. Katika baadhi ya sehemu za Afrika, mwendeleo huo uliendelea kuwepo hadi enzi ya Neolithi. Hii inaonyesha kuwa mwendeleo huu ulitokana na fikra za kiteknolojia zilizokuwa zimeendelea sana kwa wakati huo.


Tasnia ya Musteri iliyokuwa inatumia mbinu ya kujeya ya Levallois haijachunguzwa sana katika Sudani ya kusini, ingawa yawezekana ilitumika huko Tangasi na, kwa kiwango cha juu zaidi, huko Abu Tabari na Nuri. Kwa upande mwingine, utafiti wa hivi karibuni huko kaskazini umebainisha makundi manne: *Musteri ya Kinubi*, ambayo wakati mwingine huhusishwa na zana za Paleolithi ya Nyuma (takriban - 45 000 hadi - 30 000); zana za umbo la meno za *Musteri*, Sango ya Kilupemba na katika Unubi ya Sudani, *Khormusia*, ambayo inahitilafiana na Musteri za kaskazini kwa vile ina aina za ujeya za Levallois, zilizosawazishwa, vipande vyenye umbo la meno na wakati mwingine burini. Umri wake unaweza ukawa kati ya 25 000 hadi 16 000 kabla ya sasa. Ikilinganishwa na Sudani ya kaskazini, data zilizokusanywa katika Unubi ya Misri hazitoshelezi.

Tasnia ya Ateri ambayo ni mahsusi kwa Maghrib na Sahara ya kusini, inabainishwa na njeya zenye matakao yaliyochongoka na kwa usawazishaji wa umbo la maua. Pengine mbinu hiyo ilianza katika tasnia ya Musteri na kuendelea kuwepo katika baadhi ya maeneo hadi



25.1 Vigumba vya mikuki ya aina ya flinti kutoka Mirgissa, Sudan; uchimbuzi yaliyoongozwa na J. Vercoutter (Msafara wa Wafaransa wa kiakiolojia katika Sudan)

25.2 Bonde la Malkia (J. Devisse)





enzi za Neolithi. Huko Nubia ya Misri mbinu hiyo inahusishwa na kuwepo kwa wanyama wengi: vifaru weupe, ng'ombe wakubwa, punda mwitu, spishi mbili za swala, paa, mbwa mwitu, mbweha, ngiri, mbuni, kasa na mzazi wa ngamia. Katika eneo la Kairo, tasnia ya Ateri inaelekea kuwa ya kimikrolithi.

Utafiti wote huu kwa pamoja unaonyesha kuwepo kwa kipindi cha awali cha 'aina ya Ashculi na Levallois' kikifuatwa na kingine chenye kubainishwa na kuwepo kwa violezo vikubwa ambavyo polepole vikawa vidogo na bora zaidi. Katika awamu ya baadaye, tunaona njeya zilizofanana na nyembe zikionyesha alama za kuchongwachongwa vizuri kidogo zikiashiria kuwa ni za Kimusteri, pamoja na zana nyingine kadhaa.

Kuhusu watu waliohusika na tasnia hizi, inafaa kuzingatia kuwa vipande viwili vya fuvu ambavyo huenda ni vya kipindi hiki viligunduliwa huko Silsilé mnamo mwaka 1962, lakini mpaka sasa haijawezekana kuvibainisha kwa uhakika.

### *Enzi ya Mawe ya Nyuma*

Katika bonde la mto Nili matatizo yaliyopo ya kupambanua kipindi kimoja na kingine hufanya kazi ya kuonyesha mifutulizo ya kikronolojia kuwa ngumu. Papo hapo, mabadiliko ya ekolojia yanaelekea kuathiri mahusiano kati ya wakazi wa bonde na majirani zao, kwa vile uhusiano wa zamani ulimalizika na mpya ukaanzishwa. Orodha ya aina za tamaduni zinazojulikana hivi sasa au zilizotambuliwa hivi karibuni huleta fikra kwaramba aina hizo za utamaduni ziliwakilisha mtawanyiko mkubwa. Maelezo haya pia yanahusu kipindi kilichofuata, yaani Paleolithi - juu.

Huko Sudani, Enzi ya Mawe ya Nyuma imefanyiwa utafiti hivi karibuni katika sehemu za kaskazini za nchi hiyo ambapo tasnia mbili zimedhihirika; tasnia ya Jemai karibu na Wadi Halfa (takriban - 15 000 hadi - 13 000) na tasnia ya *Sebili*<sup>1</sup>, vilevile huko Wadi Halfa (takriban - 13 000 hadi - 9600).

Tasnia mbili zimebainika katika Unubi ya Msri: tasnia ya Amodi na *Sebili* kwenye eneo la Sebuu.

Huko Misri, mitindo mitatu ya Enzi ya Mawe ya Nyuma inabairuka: mtindo wa Giza, ambao ulibainika karibu na Kairo mnamo 1938; mtindo wa Hawari ambao umeenea tangu Esna hadi ncha ya delta na huenda ukaonyesha athari za Ateri upande wa kusini, na mtindo wa *Kharga* katika Oasisi ya *Kharga*.

Mbinu ya kujeya ya Levallois inajitokeza katika mitindo yote mitatu, ingawa mitindo hii hutofautiana katika ukubwa wa vikombo, burini, nyembe, zana zenye umbo la meno ambazo hufanya zaka la zana. Ni mtindo wa Hawari peke yake ndio huonyesha mielekeo ya kimikrolithi inayoashiria kipindi kilichofuata cha Paleolithi - juu.

### *Kipindi cha Paleolithi - Juu*

Katika bonde la Mto Nili, kipindi hiki hutofautiana na kile kilichotangulia kwa vile mbinu za kujeya zilichukua nafasi ya utengenezaji wa nyembe za mikrolithi na lamela zenye nyuso nyingi. Hata hivyo, kuna mifano ya kuendelea kuwepo kujitokeza tena na tena, na kuingiliana kwa mitindo hii.

1 Sebili: Awali kipindi chote hiki kilidhaniwa kuwa kilidhihirishwa na tasnia ya Sebili katika eneo lote hili. Hata hivyo utafiti unonyesha kwamba tasnia hii ni mahsusi kwa eneo la Kom Ombo.

Utafiti uliofanywa kaskazini mwa Sudani na kusini mwa Unubi ya Misri umedhihirisha changamano ya tasnia kumi na tatu ambazo pengine zinawakilisha mitindo tofauti ya utamaduni mmoja. Mitindo hiyo ni: *Halfi* ambapo aina mpya ya mbinu ya uchongaji vizuri inatumika (takriban - 18 000 hadi - 13 000); *Ballana* (- 14 000 hadi - 12 000); Qadi ambapo katika makaburi yaliyomo majumbani kumepatikana vipande vya mafuvu ya watu waliofanana na spishi za *Cro Magnon* (takriban - 12 000 hadi - 5,000); *Akini* (7400); *El-Kabi* (takriban - 5000); *Shamaki* (takriban - 5000 hadi 3270); *Silsila*, ambayo imedhihirisha masalia ya wanadamu wa aina ya *Cro Magnon* (takriban - 13 000); *Fakuri* (takriban - 13 000); *Sebili* ambayo ilibakia na mbinu ya kujeya ya *Levallois* (takriban - 11 000); *Menchi*, *Lakeiti*, na *Helwani*. Mwisho, Natufia ambayo ni tasnia iliyoanzia Palestina na ambayo inadhaniwa kuwa iliingia Misri katika sehemu mbalimbali. Huko Halwan, awamu moja ya tasnia hiyo imegunduliwa ambayo hubainishwa na vipande vyenye migongo iliyochongwa vizuri kwa mtindo wa msalaba (takriban - 7000). Vigumba vya *El-Khiam*, vyenye vitako vilivyochongoka vizuri, ambavyo pia vilienea sana Palestina, huenda vinahusiana na mtindo huo.

### *Vipindi vya Neolithi na vya kabla ya ufalme*

Kipindi hiki kirefu kilichodumu takriban milenia mbili (tangu - 5,000 hadi - 3,000) kinahitaji uchanganuzi wa kina. Watu wa bonde la Mto Nili, ambao mwanzoni walikuwa Wanomadi au Wanomadi nusu, polepole walianza kuleta mambo muhimu ya ustaarabu kama tujuavyo leo: makazi ya kudumu, matumizi ya vyombo vya ufinyanzi, ufugaji wa wanyama, kilimo na utengenezaji wa zana mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya mwanadamu yaliyokuwa yakiongezeka.

### **Sudani**

Changamano nne za tamaduni zimetambuliwa

#### *Utamaduni wa Khartoum*

Penge huu ndio utamaduni wa awali kabisa wa kipindi hicho katika Sudani takriban - 4,000. Utamaduni huo umetambuliwa katika sehemu zaidi ya kumi na mbili kuanzia Dongola hadi Abu Hagar. Data kutoka katika uchimbuzi wa huko Khartoum huonyesha ushahidi wa makazi ya kudumu yenye vibanda vya miwati, matumizi makubwa ya vyombo vya ufinyanzi vyenye marembo ya 'mistari ya mawimbi' na 'mistari ya vitone', na matumizi ya mawe ya kusagia. Kuna aina nyingi za zana za mawe ambazo ni za kimikrolithi na kijiometri zilizotengenezwa kwa kwatzi. Chusa za mifupa zenye mistari mmoja wa miiba huashiria kuwa watu hao walikuwa wavuvi pia. Kulikuwapo pia na seti za vyombo vya kusagia. Miongoni mwa mapambo ya watu ni shanga za umbo la sahani zilizotengenezwa kwa makaka ya mayai ya mbuni, na vipuri vichache ya kuning'inia. Vilevile ngeu nyekundu na njano zilitumika kurembesha mwili. Wafu walizikwa majumbani mwao wakiwa wamelazwa kibavu. Wakazi hao walikuwa wa aina ya Kingro. Katika maisha yao waling'oa meno yao kama ilivyokuwa desturi ya Wakaspi na Waiberia - Maurusi katika Maghrib na Waneolithi wa Kenya. Miongoni mwa wanyama wanaohusishwa nao ni ny'eti, paa, viboko, paka mwitu, nungunungu na idadi kubwa ya samaki (takriban - 4,000).

#### *Utamaduni wa Shahenabi*

Utamaduni wa Shahenabi huonekana katika maeneo kadha yaliyotapakaa katika sehemu iliyo kusini mwa Poromoko la Sita. Huenda aina hii ya utamaduni inetokana na ule wa Khartoum

lakini hutofautiana nao kwa vile ulitumia udongo mwekundu kutengeneza vyombo vya ufinyanzi, patasi za *barrel-plane* na mashoka ya mifupa yaliyong'arishwa. Mikrolithi na vichwa bapa na vya mbinuko vya nyundo hujaliza zaka la zana za mawe. Chusa za mifupa bado zingalipo, lakini pia huonekana ndoana za lulu, kadhalika amezoniti na shanga za akiki na ndonya za mawe zinazopenyezwa katika midomo, ambazo huvaliwa hadi leo. Nyati, paa, twiga na ngiri waliwindwa na mbuzi waliodumaa walifugwa. Utamaduni wa Shahenabi una sifa zinazofanana, mathalan, na zile za Fayumi iliyoko Misri ya Kaskazini, pamoja na tamaduni za magharibi na magharibi-kaskazini mwa Sudani, ikiwa tutazingatia matumizi ya amazoniti na patasi. Eneo la Kadero ambalo ni mfano mwingine wa utamaduni huo, limeshahirisha makaburi ya hivi karibuni ya kuanzia takriban – 3500 hadi 3000.

#### *Utamaduni wa Abki*

Utamaduni wa Abki wa kaskazini na kusini mwa Sudani, walau hadi Sai, pengine ni wa kipindi kilekile cha utamaduni wa Khartoum na baadaye ulc wa Shahenabi (k. – 3380 – 2985)

#### *Utamaduni wa baada ya Shamaki*

Utamaduni wa baada ya Shamaki, uliostawi tangu takriban – 3650 hadi – 3270 umekonekana katika maeneo mawili tu.

#### Unubi ya Misri

Katika Unubi ya Misri, kutoonekana kwa tamaduni zilizotajwa hapo juu huenda kumetokana hasa na kutofanyika kwa utafiti wa kutosha. Utamaduni wa *Nagada I* umeonekana kwenye maeneo machache tu; ilihali utamaduni wa *Nagada II* huonekana karibu na Abu Simbel na Khor Daud, Sebua, Bahan na Ohemhit. Tangu ufalme wa kwanza na kuendelea, mawasiliano baina ya Unubi na Misri yalififia na tasnia za Kinubi, ambazo zilijulikana kwa majina ya kundi A, B na C, zilikua kwa nguvu zao wenyewe hadi ilipofikia enzi ya Ufalme Mpya.

#### Misri

Huko Misri, hali zilizotofautiana za kijiografia zilisababisha kutokea kwa makundi mawili tofauti ya kitamaduni, moja kusini na jingine kaskazini.

#### *Kundi la kusini la utamaduni (Misri ya Juu)*

Kundi la kusini limajitokeza tangu awali kuwa lenye ustaarabu wa hali ya juu, nalo limeelezwa kutokana na misingi ya utafiti uliofanyika wa makaburi mengi makubwa na masalia machache zaidi ya mahali pa makazi.

#### Utamaduni wa Tasa

Utamaduni wa Tasa, ambao mpaka wakati huu umefanyiwa utafiti wa kijuujuu tu na ambao unasailiwa na baadhi ya wataalam, hutokea katika Misri ya Kati ya huko Tasa, Badari, Mustajidda na Matmar. Vyombo vya ufinyanzi vya Tasa ni vya kahawia na mara chache sana huwa na rangi nyekundu, vikiwa na ukingo mweusi na wakati mwingine selemu ya juu huwa na mistarimistari. Vyungu hufanana na umbo la katisi. Miongoni mwa zaka la zana za mawe ni mashoka yaliyong'arishwa, vikombo na visu. Paleti mstatili za manukato, hasa za

albasta, pete, bangili za pembe na keti zilizotobolewa ni miongoni na marembo ya watu. Pia kuna vijiko na ndoana za mifupa. Makaburi ni ya umbo la yai au mstatili, pengine yenye shubaka la pembeni, yakiwa na maiti aliyelazwa kwa ubavu, na mikono na miguu iliyonyoosha, kielwa kikielekea kusini na uso ukitazama magharibi. Samani zilizomo kaburini zinafanana na zile za nyumbani.

### Utamaduni wa Badari

Utamaduni wa Badari, ambao kimsingi upo katika Misri ya Kati, huonekana huko Badari, Mustajidda, Matmar na Hamamia. Ufinyanzi wa Kibadari ambao unaonyesha ustadi mkubwa huwa wa rangi anuwai kama vile rangi nyekundu, kahawia, jivu na nyekundu yenye ukingo mweusi sehemu ya nje; pengine huwa na mistarimistari. Vyombo vya mawe vilivyong'arishwa pia vilitumika. Miiko, vitana, bangili, ndoana na vijisanamu vya mifupa au pembe za ndovu vinadhihirisha ustadi mkubwa wa usanii. Hasa vijisanamu pengine vilikuwa na nafasi muhimu katika matambiko. Mapambo ya watu ni pamoja na shanga za kwatzi zilizotungwa katika shaba, makoa na paleti mstatili za manukato zilizotengenezwa kwa sleti. Mara nyingi paleti hizo zilikuwa na tako la mbonyeo. Ngano, shayiri na kitani zililimwa na ng'ombe na kondoo walifugwa, ilihali swala, mbuni na kasa waliwindwa kwa ajili ya chakula. Nyumba ambazo pengine zilikuwa za aina ya vibanda hafifu, zimetoweka. Mila za mazishi zilifanana na zile za utamaduni wa Tasa, ingawaje makaburi zaidi luwa na umbo la yai au duara kuliko mstatili. Samani zilizokuwa katika makaburi zinafanana na zile za nyumbani. Maeneo ya utamaduni wa Badari yanaonekana katika sehemu yote ya Bonde la Mto Nili na katika jangwa la mashariki na Nubia.

### Utamaduni wa Nagada I<sup>2</sup>

Utamaduni wa Nagada I (tangu takriban – 4000 hadi 3500) umeonekana huko Misri ya Kati, Unubi na jangwa la mashariki, na ni wa karibuni zaidi kuliko ule, wa Badari. Vyombo vya ufinyanzi vya Nagada havina marembo yaliyotojwa lakini vimepakwa rangi nyeupe kwenye rangi nyekundu, pamoja na kuwepo motifu za kimistari na za kimaumbile. Vyungu vya mawe, ambavyo mara nyingi hutengenezwa kwa mawe mcuti, vina vishikio vilivyotobolewa na mara nyingi huwa na umbo la pia kwenye tako. Zana zenye sura mbili zinajumulisha vigumba, visu vya aina mbalimbali, mashoka yaliyong'arishwa na vichwa vya nyundo vycenye umbo la sahani au la pia. Picha za wanadamu na wanyama huwakilishwa kwenye paleti za manukato zilizotengenezwa kwa sleti na kwenye vitu vilivyotengenezwa kwa mifupa au pembe za ndovu. Haidhihiriki kama hivi vilitumika kwa ajili ya matambiko au uclawi, ingawa vimeonekana katika makaburi tu. Ni katika eneo moja tu, huko Mahasna, kulikopatikana ushahidi wa makazi yaliyokuwa na vibanda hafifu vyenye umbo la maboma ndani yake mkiwemo ghala za nafaka. Makaburi hayakutafautiana sana na yale ya vipindi vya awali, ingawa hapa uzikaji wa maiti wengi katika kaburi moja na uchanguaji wa maiti ulikuwa sehemu ya miviga.

Jambo moja muhimu katika kipindi cha kwanza cha Nagada lilikuwa kuongezeka kwa matumizi ya kupri.

### Utamaduni wa Nagada II<sup>3</sup>

Utamaduni wa Nagada II (tangu takriban – 3500 hadi – 3100) unaweza kuonekana kuanzia lango la bonde la Fayum huko Gerza mpaka kusini mwa Unubi ya Misri, na huko Hamamia, Mustajidda na Armant. Nafasi ya vyombo vilivyopambwa kwa rangi nyeupe ilichukuliwa na

2 Nagada I: Pengine hujulikana kama utamaduni mkongwe wa kabla ya ufalme au utamaduni wa Amrata

3 Nagada II: pia hujulikana kama Kipindi cha Kati cha Kabla ya Ufalme au kipindi cha Gerza.

vyombo vya rangi ya waridi vyenye mapambo ya kahawia yenye umbo la mitindo maalum ya kimotifu iliyowakilisha alama za mizunguko, mashua, mimea na picha zenye mikono iliyo inuhiwa juu. Pia sifa maalum ya utamaduni huo ni vyombo vilivyotuna katikati vyenye vishikio vya umbo la mawimbi, ambavyo baadaye vilikuwa vya umbo la mcheduara na hatimaye vilitengenezwa bila ya vishikio katika kipindi cha mwanzo cha historia. Vyungu vilivyotengenezwa kwa mawe yaliyong'arishwa vilifanana na maumbo ya vyombo vya ufinyanzi. Katika zaka la zana za mawe mlujumuishwa visu vyenye umbo la V mwishoni na vingine vyenye pande mbili za makali, mmoja ukiwa na mbinuko na mwingine ukiwa na mbonyeo. Baadhi ya vyombo vilikuwa na vishikio vilivyopambwa kwa dhahabu na kuwekewa njumu za pembe za ndovu. Utumiaji wa kupri ulizidi kuwa makini na zilitengenezwa chonge, pini na mashoka. Vijisanamu vya mifupa na pembe pia vilikuwa vya usanii wa hali ya juu sana. Nyumba za duara za udongo zilichimbiwa msingi kidogo katika ardhi na zilifunikwa kwa paa. Desturi za mazishi zilifanywa kuwa bora zaidi: Makaburi yalijengewa miti, tope au matofali na sadaka ziliwekwa katika mwanandani. Uelekeo wa kulazwa maiti kaburini pia ulitofautiana zaidi kuliko iliyokuwa katika vipindi vya awali.

#### *Kundi la Kaskazini la Utamaduni (Misri ya Chini)*

Kundi la utamaduni la kaskazini linatofautiana sana na lile la kusini, kwa vile maeneo ya makazi yalikuwa makubwa zaidi, vyombo vya ufinyanzi vilikuwa vya rangi moja na, katika baadhi ya vipindi, maiti walizikwa ndani ya nyumba.

#### **Utamaduni wa Fayumi B**

Utamaduni wa Fayumi B unadhaniwa kuwa ni wa kipindi cha mwisho cha Paleolithi au pengine Neolithi ya kabla ya vifinyange. Fayumi hujumuisha nyembe sahili na za mikrolithi na seti ya patasi na vigungba ambavyo huashiria kuwa huenda utamaduni huu ulikuwa na mawasiliano na Sahara (tangu takriban – 6100 hadi 5190).

#### **Utamaduni wa Fayumi A**

Utamaduni wa Fayumi A, ambao umefanyiwa utafiti kwa kina zaidi, una vyombo ghafi vya ufinyanzi vyenye maumbo anuwai ambavyo miongoni mwavyo ni vyungu vyenye miguu au kinundu kinachojitokeza ambavyo hukumbusha utamaduni wa Badari. Tasia na kutengeneza zana za mawe ni ya mapokeo ya Neolithi, lakini aina nyingi za zana za mifupa na paleti za manukato zimetengenezwa pia. Hakuna makazi yaliyojengwa yaliyogunduliwa, lakini ghala zenye vikapu zilizofunikwa na ardhi karibu na makazi hayo zimehifadhiwa. Wakazi walikula nyama ya nguruwe, mbuzi, nyama ya ng'ombe, kiboko na kasa. Hakuna makaburi yaliyokwishaonekana.

#### **Utamaduni wa Merimdi**

Utamaduni wa Merimdi (tangu – 4180 hadi – 3580) unahusishwa na sehemu moja ya makazi yenye eneo la zaidi ya hekta mbili magharibi mwa delta ya Nili. Vyombo vya ufinyanzi vimerembwa kwa kutojwatojwa, aghalabu zikiwakilisha motifu ya ukuti. Kuna vyombo vichache vya mawe na zana za mifupa na mawe hufanana na zile za Fayumi. Mapambo ya watu ni anuwai kama vile katika vipindi vya awali na hujumuisha pini, vito na paleti za manukato zilizotengenezwa kwa sleti na itale; zote mbili ziliingizwa kutoka kusini. Makazi yalikuwa ya namna mbali mbali – kuanzia vibanda vyepesi vyenye umbo la yai hadi vibanda madhubuti. Makazi hayo yaliambatana na ghala zilizosukwa ambazo baadaye zilibadiliwa na

magudulia ya udongo yaliyochimbiwa ardhini. Maiti walizikwa pasi bidhaa za makaburi, katika makaburi yenye umbo la yai yaliyojengwa kati ya makazi. Mbwa, mbuzi na kondoo walifugwa, bali viboko, mamba, na kasa bado waliendelea kuwindwa, na watu walishughulikia uvuvi pia. Huenda utamaduni wa Mernidi ulikuwa wa wakati mmoja na ule wa Fayumi kaskazini na Nagada I kusini.

### Utamaduni wa Omari A

Utamaduni wa Omari A umetambuliwa karibu na Helwan. Utamaduni huu una makazi yaliyoko kwenye kilele cha genge lenye mwinuko mkali na ndio infano pekee wa aina yake katika Misri. Vyombo vya ufinyanzi ambavyo ni vya rangi moja tu ni bora na huwa na maumbo mengi. Vyombo hivi ni pamoja na vyungu vyenye vinundu vilivyokuwa mashuhuri tangu awali kabisa. Vyungu vya mawe ya chokaa na mawe meusi navyo wakati mwingine vilitumika. Tasia ya zana za flinti kwa jumla ilitumia mbinu ya kujeya ya nyuso mbili. Kwa upande mwingine, tasnia ya nycmbe ilionyesha vipengee kadha, na kilichojitokeza zaidi kiufundi na kiumbuji, ni visu vyenye mgongo wenye kijituta na tao kwenye ncha. Chubwi za juya zilizotengenezwa kwa ujeja pia zimepatikana. Tasia ya mifupa ni ya hali ya juu lakini ndoana zilitengenezwa kwa pembe. Mapambo ya watu yalikuwa mengi na yalijumuisha kete za gastropodi kutoka Bahari ya Shamu, shanga za makaka ya mayai ya mbuni, mifupa, mawe na mifupa ya mgongo wa samaki. Kete zilizotobolewa na kisukukukete zilitumika kama herini. Galena na gundi ziliingizwa toka nje. Paleti ghafi za kusagia ngeu zilitengenezwa kwa mawe ya chokaa na kwatzi. Miongoni mwa wanyama walikuwepo ng'ombe na mbuzi ambao walifugwa, na wanyama wengine kadha na samaki walikamatwa. Ngano, shayiri na kitani zililimwa. Aidha, chakula pia kilipatikana kutokana na mimea mwitu kama vile mkuyu, mtende, majani ya tamariski na majani ya esparto. Nyumba zilikuwa za aina mbili: baadhi yazo zilikuwa za umbo la yai, zikiwa na paa lililoshikiliwa na nguzo ilihali nyingine zilikuwa duara na sehemu ya nyumba ilikuwa chini ya ardhi; kulikuwa na maghala ya nafaka kati ya nyumba hizi. Maiti walizikwa katika udongo katika maeneo ya makazi yenyewe na walilazwa ili vichwa vilekee kusini na uso magharibi.

### Utamaduni wa Omari B

Utamaduni huu unadhaniwa kuwa ulikuwepo wakati mmoja na mwanzo wa Nagada I kusini. Ulitambuliwa mashariki ya eneo la Omari A. Lakini utamaduni wa Omari B unatofautiana na Nagada I kutokana na desturi zilizofuatwa za mazishi na udogo wa zana za mawe zilizotengenezwa. Sehemu za makaburi zilikuwa mbali na makazi na makaburi yalifunikwa kwa mawc. Uchimbuzi wa eneo hili bado haujakamilika.

### Utamaduni wa Maadi

Utamaduni wa Maadi uligunduliwa kutokana na uchimbuzi ambao hayajakamilika, wa eneo moja la makazi lililounganisha sehemu mbili za makaburi huko Maadi, karibu na Kairo, na katika sehemu ya tatu ya makaburi iliyogunduliwa Heliopolis, kitongoji kimojawapo cha kusini mwa Kairo. Vyombo vya ufinyanzi vya Maadi ni vya rangi moja na mtindo wao wa ufinyanzi si makini kama ule wa Omari. Aina zinazoonekana sana ni vyungu virefu vyenye umbo la yai na ukingo uliotokeza. Vielelezo vyenye kuwakilisha vyombo vya ufinyanzi vya utamaduni huu hasa ni vyungu vyenye matak duara vimavyokumbushia vyombo vya aina hiyo vya mawe meusi. Vyungu vyenye mapambo ya kikahawia ambavyo havipatikani kwa

wingi sana huenda viliingizwa kutoka kusini, na hasa katika kipindi cha Nagada I, kama ilivyokuwa kwa vyungu vya flinti vyenye panda na umbo la V, ambavyo pia pengine viliingizwa kutoka Nagada I. Miongoni mwa vitu vingine vichache vya mapambo ya watu ambavyo pia vilitoka Nagada I ni pamoja na paleti za manukato zenye umbo la mstatili dufu.

Lakini, juu ya yote hayo, kwa mara ya kwanza katika tamaduni za Kabla ya Ufalme kuanza Kaskazini mwa Misri, utamaduni wa Maadi unatoa ushahidi wa matumizi makubwa ya kupri. Matumizi haya ya kupri yanaweza yakahusishwa na mawasiliano na maeneo ya migodi katika Sinai. Aidha, ni wakati huohuo ambapo utamaduni wa Maadi ulianza kuonyesha vipengee kadhaa vilivyofanana na tamaduni za Misri ya mashariki, hususa katika ufinyanzi mtindo wa aina hiyo hiyo umeonekana hadi huko Palestina katika zana zake za flinti, na katika matumizi yake ya mangani. Miongoni mwa rasimali za Maadi za wanyama na mimea zilikuwa spishi zinazofugwa kama vile ilivyo katika vipindi vya awali.

Idadi kubwa ya viguzo vilivyokitwa ardhini imeonekana kwenye eneo la Maadi, ikiashiria kuwepo kwa vibanda vya umbo la yai na mstatili. Vibanda vya umbo la mstatili vilitengenezwa kwa matofali makavu. Aina ya tatu ya maskani ilijengwa chini ya ardhi na kulikuwepo vidato vya kutelcmkia huko. Mabalasi ya udongo yaliyochimbiwa ardhini yalitumika kama maghala ya nafaka. Vilevile, machimbo mengine duara yameonyesha kuwa ni vyumba vya stoo. Sehemu za makaburi zilikuwa mbali na makazi ya watu na kulikuwa na makaburi ya duara na yenye umbo la yai ambamo maiti alikunjwa na kulazwa kwa ubavu ili kichwa chake kieleke kusini na uso magharibi. Wanyama waliodhariwa kuwa watakatifu, kama vile swala na mbwa, pia walizikwa katika makaburi hayo, hususa kwenye eneo la Heliopolis.

Utamaduni huu unaelekea ulikuwa katika awamu ya mpito ambayo ilitangulia enzi ya Kabla ya Ufalme na mwanzo wa kipindi halisi cha historia.

Hata hivyo, kuja kwa kipindi hicho cha historia, pamoja na kuanza kwa maandishi, kuunganishwa kwa Misri chini ya mtawala mmoja, na kuongezeka kwa matumizi ya metali, hayakubadilisha baadhi ya mitindo ya maisha ya wakazi wa awali wa bonde la Mto Nili. Waliendela kutumia zana za flinti iliyojewa ambazo zilifikia upeo wa ufundi katika enzi za ufalme za kwanza, kama inavyohibitishwa na visu vya kupendeza vya 'kafara', vilivyotengenezwa kwa ufundi mwingi na vyenye ukubwa wa kustaajabisha, vilivyopatikana katika makaburi ya wafalme huko Abydos katika Misri ya Juu, huko Sakkara na huko Helwan karibu na Kairo.

Lakini katika Nubia ya Misri na sehemu ya Nubia ya Sudani, utafiti wa kiakiolojia haukuwa umefika mbali wakati wa operesheni za kuyanusu (maeneo hayo) ziliposimama, na kale ya maeneo hayo imetupotea kabisa.

Muhtasari huu mfupi hauwezi kuwa zaidi ya juhudi ndogo ya kuunganisha vipande katika mnyororo wa historia ya Afrika kwa kutumia data iliyopatikana ya kipindi cha kabla ya ujio wa Mafarao. Jambo moja kubwa linalojitokeza linalodhihirishwa na habari zilizopo ni kuwa tangu kipindi cha Neolithi na kuendela kulikuwepo mahusiano ya karibu kati ya Misri na maeneo ya jirani ya mashariki, magharibi na kusini.

# 26

## *Sanaa za Kiafrika za kipindi kabla ya historia*

Kimsingi binadamu siku zote amekuwa mtengeneza zana na wakati huohuo pia amekuwa muumbaji wa kazi za sanaa.

Licha ya uharibifu uliosababishwa na nguvu za asili, na uporaji wa binadamu uliofanywa hasa wakati wa kipindi cha ukoloni, Afrika bado ni bara lenye idadi kubwa sana ya vielelezo vya sanaa ya kipindi kabla ya historia. Sanaa hizi zinapatikana zaidi katika sehemu za miinuko na katika safu za milima, hasa miteremko inayoenda sambamba na hiyo milima na inayoinamia mikondo ya mito yenye maji au iliyokauka. Sehemu muhimu ambapo sanaa hizi huonekana ni katika Sahara - Algeria (sehemu ya kusini ya eneo la Oranois na Tassili N'Ajjer), Moroko ya kusini, na katika maeneo ya Air na Tenere nchini Niger, katika safu za milima ya Tibesti nchini Chadi, katika Nubia na katika eneo la Dhar Tichitt nchini Mauritania - na kusini mwa Afrika katika Lesotho, Botswana, na Malawi; huko Ngwane nchini Namibia, na katika Jamhuri Afrika Kusini, hasa katika mabonde ya mito Orange na Vaal na Transvaals ambako michoro imeonekana ndani ya makazi ya mapango ya inawe na nakshi kukatwa katika sehemu za nje ya mawe hayo. Kuna nchi chache za Afrika ambako mabaki ya sanaa hayajawahi kugunduliwa, japokuwa ni kweli kwamba si mabaki yote yana asili ya enzi za kabla ya historia.

Sababu moja ya kuwepo kwa kazi za sanaa nyingi katika majangwa na mbuga za Afrika ni kwamba katika kipindi cha kabla ya historia, Afrika ilikuwa na idadi kubwa sana ya binadamu katika sayari hii, hasa katika sehemu zile ambazo sasa zimekuwa kaine. Aidha, hewa kavu katika sehemu hizi ilisaidia kuhifadhi vifaa vya binadamu kwa zaidi ya miaka elfu nyingi, wakati miteremko inayoinamia mabonde makubwa katika safu za milima au katika kingo zake zilikuwa sehemu za makazi ambayo yalikuwa rahisi kuhuda na yaliwapa wakazi wake maji na wanyama.

Kwa mfano, kwa upande wa magenge ya Tassili, kubadilikabadilika kwa hali ya hewa, mara joto mara baridi kulikoambatana na mwendo wa mawimbi ya maji, kulimomonyoa sehemu za chini za kuta za miamba na kutengeneza makazi ambayo watu waliohamia waliweza kumiliki mazingira yote yanayozunguka maeneo hayo. Schemu hii ambayo ilikuwa ulingo na ngome yenye sanaa za asili ambazo zilichongwa katika mawe ya mchanga kutokana na athari za upepo na maji, ilimpa binadamu nafasi ya uhai ya kuweza kusawiri maisha ya viumbe hai vilivyomzunguka.



## Kronolojia ya maendeleo

### Njia za ukadiriaji umri na matatizo yake

*Njia ya stratigrafia:* Njia hii ni ya kuainisha vitu kulingana na wakati na mahali vinapokatikana na mfuatano wa matabaka ardhini. Kwa upande wetu, njia hii haitufai sana, kwa sababu matabaka yalikuwepo ndani ya sakafu ya makazi yalichukuliwa na maji na nafasi yake ikachukuliwa na matabaka mengine mapya nyakati za mvua nyingi zilizotokoa katika kipindi kabla ya historia. Zaidi ya hayo, kuna uwezekano kuwa makazi hayo yalivunjwa na wakazi mbalimbali. Ushahidi pekee wa kikronolojia wa kuaminika ungekuwa kugunduliwa kwa vitu vya nywele kugeuza rangi ya ogani vilivyotoka kwenye kuta na kuangukia katika tabaka ambalo linajulikana kuwa halikupata kuguswa tangu wakati huo.

Mbinu ya kuchunguza rangi inaweza kuwa kidokezo kizuri, kwani rangi za majimaji ambazo karibu zinafanana sana na miamba ya asili ndizo zinazoelekea kuwa zilitumika zamani zaidi, ilihali rangi nyepei ambazo zinatofautiana sana na rangi za miamba zinaweza kufikiwa kuwa zilitumika miaka ya karibuni zaidi. Hata hivyo, kila kitu kinategemeana na uimara wa mwamba, kwa mfano, kama ulipigwa na jua au upo. Vilevile jinsi nakshi zilizo katika mwamba zinavyomegeka kutokana na mmomonyoko kutoka umbo la V na kuwa umbo la U hutoa mwanga kidogo kuhusu umri wa kazi ya sanaa.

Kwa kiasi fulani, kazi za sanaa zinaweza kupimwa umri wake kutokana na spishi za wanyama zinazozwakilisha. Kwa mfano, paa wa Bubalusi, ni spishi kongwe na sanaa ambayo ilitoweka zamani sana. Lakini msanii angeliweza vilevile kuchora picha za wanyama maalum ambao walikwishatoweka kitambo sana.

Zaidi ya hayo, mtindo wa maumbile ambao hujaribu kuonyesha ukweli wa mambo kama msanii anavyoona, sio lazima uwe wa kabla ya mtindo dhahinia zaidi ambao haufungwi na vitu ambavyo unaviwakilisha. Zaidi ya hayo, japokuwa ni kweli kwamba michoro iliyochorwa juu ya mingine lazima iwe ya hivi karibuni, mara nyingi ni vigumu kutambua ni upi kati ya mistari miwili ni wa chini, na tena mistari ulioko juu unaweza kuwa ulichorwa na msanii yuleyule kwa sababu ambazo sisi hatuzijui.

Njia iliyosalia ni ya radio-kaboni (linganisha na Sura ya 9). Hata hii pia, lazima kuwa na uangalifu mkubwa ili kuepuka makosa; kwa mfano kwa kuhakikisha kuwa mabaki yanayofanyiwa uchunguzi hayakuchanganyika na mabaki ya hivi karibuni, au kwa kupima na kuona kama kielelezo cha kaboni hakikutokana na moto uliosababishwa na radi. Hata hivyo, idadi ya ukadiriaji umri kwa kutumia njia hii ni kubwa kuliko njia nyingine. Kwa mfano huko Menietti katika Sahara ya Kati, kipande cha kaboni kimekadiriwa kuwa na umri wa miaka 5,410±300 kabla ya sasa.

Wakati mwingine ukadiriaji umri unaweza ukaharibiwa na siasa, kama jinsi utawala wa watu wupe wa Afrika Kusini ulivyojaribu kupunguza umri wa ushahidi wa kiakolojia kwa kukadiriwa umri wa michoro ya Drakensberg kuwa ya karne ya kumi na saba, muda mrefu baada ya kufika kwa Wabantu, japokuwa michoro hii inaonyesha wanyama, watu na mandhari ya enzi za kale kabisa.

### Vipindi

Profesa J. Ruffie amesema kwamba 'awali kabisa binadamu alikuwa mnyama wa nchi za tropiki.' Akitokea Afrika, alikwenda na kutawala Ulaya ambako, kwa karne arobaini zilizopita, kulikuwepo na sanaa ya miambani iliyoshamiri sana katika mapango ya Ufaransa na Hispania.

Umri wa sanaa ya miambani ya Afrika unaanzia enzi za Neolithi, kipindi ambacho uchunguzi unaelekea, kukirudisha nyuma na nyuma zaidi katika Afrika hadi kati ya miaka 4000 na 10 000 kabla ya enzi ya Ukristo, kutegemeana na eneo.

Kumekuwa na kawaida ya kutofautisha aina nne kuu za sanaa ya miambani kutegemeana na mnyama ambaye anawakilisha zaidi ya kila moja ya aina hizo. Aina hizo zinafahamika kama enzi za Bubalusi, Maksai, Farasi na Ngania.

Bubalusi alikuwa aina ya nyati mkubwa sana anayeonekana katika vielelezo vya awali kabisa vya sanaa ya miambani takriban miaka 9000 kabla ya sasa. Tembo na kifaru walichorwa pia katika kipindi hiki, na spishi zote hizi zinaashiria mazingira yenye misitu minene.

Kuanzia kama miaka 6000 kabla ya sasa maksai, anaanza kuchorwa, katika maumbo mawili: *Bos-Ibericus* mwenye pembe fupi na nene na *Bos-Africanus* mwenye pembe ndefu zilizoachana sana.

Farasi alitokea takriban miaka 3500 kabla ya sasa, na wakati mwingine huonyeshwa katika mtindo wa 'kwenda shoti', miguu yake minne ikiwa imepanuliwa. Hadi wakati huu, ambao ulikwishaingia katika enzi ya historia, kiboko alikuwa amekwishapotea katika michoro ya miambani, ikimaanisha kwamba hakukuwepo tena mito au maziwa ya kudumu.

Ngamia aliletwa Misri na wavamizi wa Kiajemi yapata miaka 500 kabla ya enzi za Kristo na ni wa kipindi cha historia tu.

Kwa hiyo vipindi ambavyo vinaangukia katika kipindi kabla ya historia ni Bubalusi na Maksai. Jaribio la kuvigawa vipindi hivi katika vipindi vidogo zaidi limeshihika kuwa ni gumu sana. Kwa mfano, kondoo ameanishwa kuwa alitokea baada ya Bubalusi na tembo, japokuwa wakati mwingine anaelekea kuwa wa wakati mmoja na hao waliomtangulia. Wakati huo, inawezekana kuwa alifugwa nusunusu au aliwekwa kwa madhumuni ya kidini. Vivyo hivyo, nakshi inaaruifu za maksai zilizoko Dider huko Tassili, au maksai aliyevaa kidani, wa huko Wadi Jerat anaelekea ni wa kipindi cha Bubalusi. Kwa hivyo kulikuwepo na mwingiliano.

Katika sehemu nyingine, ukiondoa Sahara, vipindi muhimu mara nyingi ni vya miaka ya baadaye sana na hufafanuliwa kwa misingi ya vigezo kadha kama vile hali ya watu na wanyama waliowakilishwa, mbinu zilizotumika, na tanzu na mitindo.

## *Mbinu, aina na mtindo*

### Mbinu

#### *Ukataji nakshi*

Kwa kawaida, nakshi zilitokea mapema zaidi kuliko picha na mbinu za hali ya juu kabisa zinapatikana katika vipindi vya mwanzoni kabisa. Vipande vigumu sana vya miamba vilivyovunjwa kwa nyundo ya mawe, vielelezo ambavyo vimegunduliwa karibu na sehemu hizo, vilitumika kuchonga picha juu ya mawe ya mchanga au hata juu ya itale na kutoa modeli makini sana. Katika baadhi ya nakshi, mstari umechorwa kwa uhafifu tu kama ilivyo katika nakshi ya tembo iliyoko Bardai huko Chadi. Katika nakshi nyingine mstari mnene lakini unaoonekana waziwazi ulizama ndani katika mwamba, kama ilivyo kwa picha za tembo zilizoko Galjeien na za kifaru zilizoko Gonoa huko Tibesti. Mikato ni ya umbo la V au umbo la U na ilichimbwa kwa kutumia vishoka vya mawe au vipande vya miti migumu sana, na mchanga mbichi ulitumiwa kama msasa kusugulia sehemu za juu na kuzifanya laini.

Hapana shaka uhodari kama wa kisarakasi ulihitajika kuweza kukata baadhi ya nakshi hizi zilizokuwa na urefu wa mita 5 au zaidi.

Huko Afrika ya Kati na Kusini, matokeo mazuri yalipatikana kwa kuchimba sehemu za juu na kuzing'arisha ili kuonyesha alama ya ngozi ya wanyama au mizigo waliyokuwa wamebeba. Mbinu hii maashiria ile ya sanamu nakshi ya Misri ya wakati wa enzi ya Mafarao.

Aidha, miamba ya asili ilitumika kwa ufundi mkubwa ili kuongeza uzuri zaidi katika picha. Karibu na Lecufontein, Afrika Kusini, kifaru amechongwa juu ya mwamba usio laini na kingo zake kali hudhihirisha ngozi ya magamba ya mnyama huyu. Katika sehemu nyingine, taya la chini la pundamilia limeonyeshwa kwa kuvimbishwa kidogo katika mwamba wenye umbo linalofanana na taya halisi la mfupa. Kazi nyingine ya sanaa ambayo ni ya hali ya juu iliyofanywa kwa nakshi za mawe katika kipindi kabla ya historia ni kundi la twiga lililoko Blaka huko Niger, wakiwa na ngozi za rangi mbalimbali, miguu yao ikiwa katika hali halisi ya maumbile yao na hata kuonyesha jinsi wanavyopunga mikia yao. Lakini kadri wakati ulivyopita ndivyo ubora wa nakshi zao ulivyopungua na ustadi wa mwanadamu ukaendelea kuvia.

#### *Picha za rangi*

Vilevile ngazi au jukwaa wakati mwingine vilihitajika ili kuchora picha za rangi zilizoko urefu wa mita 4 toka ardhini, urefu usioweza kufikiwa na wanyama na watu. Wakati mwingine picha ni za rangi moja. Rangi mbalimbali zilipotumika, mchanganyiko wa rangi uliofanywa kwa ustadi sana ulikusudiwa kutoa sura halisi ya vitu kama vinavyoonekana katika hali yake ya kawaida. Kwa hivyo karakana za aina fulani zilizhitajika, na mabaki ya karakana hizi yameonekana huko I-n-Itinen, ikiwa ni pamoja na mawe ya kusagia, michi midogo na vidau vya rangi.

Rangi za kusliangaza ambazo zimeendelea kuwa zilivyo bila kuharibika hadi leo zinaonyesha ubora wa kustaajibisha wa michanganyo ya kemikali zilizotumika. Kulikuwepo na rangi kadha za msingi kama vile nyekundu, - kahawia, nyekundu iliyopauka na hudhurungi, zilizopatikana kutokana na ngegu na oksidi ya feri (eluma), rangi nyeupe iliyotokana na kaolini, utomvu mweupe, kinyesi cha wanyama na oksidi ya zinki; na rangi nyeusi iliyopatikana kutokana na mkaa, poda ya majivu ya mifupa, masizi au mafuta yaliyoungua. Njano, kijani na zambarau ni miongoni mwa rangi ambazo zilitumika pia. Vitu hivi vilisagwa kuwa poda laini kwa kutumia mchi na kinu na baadaye vikachanganywa na aina ya maziwa, mafuta yaliyoyeyuka, na sehemu nyeupe ya yai, asali au ubongo wa mifupa uliopikwa. Matokeo yakawa rangi kali anuwai ambazo zimedumu kwa miaka elfu nyingi. Rangi hizi zilipakwa kwa kutumia vidole au pengine manyoya, vijiti au vipande vya miti vilivyolainishwa, au brashi zilizotengenezwa kwa nywele za wanyama ambazo zilifungwa katika kijiti kwa kutumia kamba ngumu. Rangi hizi pia zilinyunyizwa kwa mdomo. Hapa vilevile sifa za asili ya mwamba zilitumiwa kwa ustadi mkubwa; kwa mfano huko Tibilahi mpasuko katika mwamba umetumika kuwakilisha shimo la maji ambalo mifugo inajitayarisha kunywa.

#### *Usonara*

Mbinu iliyotumika kutengeneza aina fulani ya sianga imeundwa upya kutokana na uchunguzi wa mabaki ya hatua kadha za kutumia jiwe gumu sana, hitwalo akiki (koneliani). Kwanza kilitengenezwa kisahani kwa kugongagonga jiwe, kujeya na kusaga. Sindano kubwa yenye

sehemu iliyo pembe mraba ilibanduliwa kutoka kwenye kiini cha flinti, na kwanza ilitumiwa kama chombo cha kutobolea pande zote mbili za kisahani na kisha ikatumiwa kama keeke ya kulimalizia tundu na kusawazisha kwa kutumia mchanga laini uliochanganywa na utomvu mzito wa mimea. Mawe mengine yenye kung'ara, mifupa, pembe za ndovu na makaka ya mayai ya mbuni, pia vilitumika kutengenezea vidani, bangili, metali, na marembo mengine. Jiwe la fuwawe lilitumiwa kung'arishia.

### *Ufinyanzi*

Udongo wa mfinyanzi unaotumiwa kutengeneza vitu vya udongo ulitayarishwa pamoja na kishikamanisho kilichotengenezwa kutokana na mavi ya ng'ombe. Kisha vyungu vilifinyangwa kwa njia ya kuviringisha udongo kwa kutumia vidole na kijiti cha kusawazishia. Shingo za vyungu zilitengenezwa katika maumbile mbalimbali wakati mbinu sahihi za uchomaji zilitumika ili kupata aina mbalimbali za rangi, kuanzia rangi ya waridi iliyokolea hadi kahawia. Ung'arishaji wa kutumia mimea ambao ulikwishakuwapo wakati huo bado unatumika barani Afrika hivi leo kutengeneza au kuremba vyombo vya ufinyanzi na nyumba kadhalika. Mbinu hizi zilikuwa tayari zinajulikana enzi hizo. Nakshi za vitana vya mifupa, mifupa ya samaki, chapa za masuke ya mahindi, kamba au mbegu zinadhahirisha ustadi mkubwa wa kubuni na wa kisani ambao waonekana wazi huko Esh Shahenab Sudani, na Wadi Echid nchini Mali, ambako majoko yaliyo karibukaribu huashiria kuwepo kwa maeneo makubwa ya karakana na kuzuka kwa tabaka la mafundi.

### *Uchongaji wa sanamu*

Uchongaji wa sanamu unawakilishwa na sanamu ndogo za ng'ombe waliolala, sungura ambaye masikio yake yamelalia nyuuna, kichwa cha kondoo kilichoko Tamentit huko Tuwat, kichwa cha bundi kilichochongwa kwa ustadi mkubwa kilichoko Tabelbalet, na vinyago vidogovidogo vya wanawake na ndege.

### *Aina na mitindo*

Katika Sahara, inawezekana kutofautisha aina na mitindo inikuu' mitatu ambayo karibu inalingana na kipindi kilichotajwa hapo juu.

Aina ya kwanza inaonyesha mwelekeo mkubwa wa hali inayokaribia hali ya asili ambamo hatua mbili tofauti zinaweza kubainishwa. Mtindo wa kwanza ni ule wa Bubalusi upatikanao huko Sahara ya magharibi na ya kati, Fezzan na Chadi. Vitu vinavyowakilishwa ambavyo vinatengenezwa kwa kuchongwa, kwa jumla ni pamoja na wanyama wakubwa waliochorwa maumbo yao kwa ustadi mkubwa. Mambo muhimu katika hatua ya pili ni picha za rangi za kondoo na paa wenye pembe, na wanaume wenye vichwa vya mviringo. Maumbo haya ya kuchorwa yawe katika picha ndogo za rangi au katika picha kubwa sana za ukutani hayana mapambo isipokuwa yanasisimua. Kisha inaonyesha kuwa kulikuwepo na inabadiliko katika mwelekeo kutoka hatua ya kwanza ya kutafakari na woga ulioibuliwa na mandhari halisi, kuingia katika hatua ya kujihusisha kiutendaji katika msisimko wa matambiko ambao watu ambao wakati mwingine huvaa maleba husujudia vizimu vyenye umbo la wanyama.

Aina ya pili ambayo ndiyo kuu ni picha za rangi na michongo ya maumbile ya asili. Mtindo huu wa kiufafanuzi unatumia aina nyingi za rangi na humwonyesha binadamu kama mfugaji wa wanyama. Mandhari ni magenge na vijiji vya Sahara; eneo bora zaidi la mandhari haya ni Jabbaren.

Mtindo wa tatu ni wa kidhahania na kikaida. Uhora wa ukataji nakshi unapungua lakini, katika picha, mstari mwembamba uliochorwa kwa urembo zaidi unafaa zaidi kwa kuleta hisia ya mtindo maalum au hali ya kuwa katika mwendo. Mtindo wa kusanafisha vilevile uliwezesha kutia kwa ustadi zaidi vivuli vya rangi. Picha zinawakilisha farasi na magari ya kukokota, na magari ya kuvutwa na ngamia, zote zikiwa zimechorwa kwa mtindo maalum ilihali binadamu wamechorwa kwa umbile lililotengenezwa kwa pembe tatu mbili au shingo ndefu, isiyokuwa na kichwa. Kwa hiyo mwelekeo ni kuchora picha kwa mtindo ambao ni makini zaidi lakini wakati huohuo kulikuwa na miclekeo ya kurahisisha maumbo ya kijiometri ambayo haikufaulu nyakati zote.

Baadhi ya kanuni za mitindo hii hazikubadilika, kwa muda mrefu, kama vile uchoraji wa ng'ombe akiwa na pembe kamili na kichwa kikiwa kinaonekana kwa upande, au michoro ya wachungaji, mkono mmoja ukiwa umenyooosha na mwingine umekunjwa na kugusa nyonga. Dhamira kadha za kidini zinaanza kujitokeza, kama vile kondoo dume huko Oran ya kusini, ilihali picha za kujamiiana zilikuwa za kawaida, hususa huko Fezzan na Tassili. Miongoni mwa zana, silaha na vito vya kipindi hiki, vielelezo vizuri kuliko vyote vinaonekana katika Neolithi ya Sudani huko Mauritania na Mali, ambako kunapatikana vilevile mapambo ya nguo, vyombo vya ufynyanzi vilivyorembwa na vigumba vya Tichitt pamoja na nakshi zake zinazong'ara na kumeremeta zenye umbo safi la pembe tatu.

Katika sehemu nyingine za Afrika aina ya sanaa ya, kipindi kabla ya historia bado hajajeweza kufafanuliwa kikamilifu. Huko Namibia, mtaalamu mmoja anadai kuwepo kwa matabaka ishirini yenye hatua nne muhimu: kwanza ni lile la wanyama wakubwa ambamo hakuna picha za binadamu, kisha mandhari zenye rangi moja za kuwinda na kucheza ngoma za matambiko na, mwisho kabisa, hatua yenye rangi nyingi, hatua ambayo ilijumuisha kazi nzuri sana za sanaa katika makazi ya Pango la Philip na Brandberg, ambazo zimekadiriwa kuwa za mwaka 1500 wa enzi za Ukristo. Frobenius, kwa upande wake, alitofautisha aina kuu mbili za mitindo ya sanaa huko kusini mwa Afrika. Katika ncha ya kusini kabisa, aliona mtindo wa maumbile ya asili wa rangi nyingi ukionyesha zaidi wanyama waliochorwa kwa ustadi mkubwa, ambao uliweza kuonyesha mikunjo halisi katika ngozi nene za wanyama au miili ya ngozi ya pundamilia, lakini haionyeshi mvuto mkubwa katika picha zinazoonyesha mandhari za kuwinda, kucheza ngoma, misafara na mikusanyiko.

Kwa upande mwingine, upande wa kaskazini kuanzia Transvaal hadi Zambezi, huko Zambia, Zimbabwe na Malawi, picha za rangi moja zinatoa fasiri ya uhalisi ulioomo katika sanaa iliyojaa fikra za uumbaji. Mwili wa binadamu na umbile lake la pembe tatu linaonyeshwa kwa upande, ilihali mikono na miguu inaonyeshwa kikamilifu, kama ilivyo katika sanamu za nakshi za Misri. Mandhari zilizochorwa labda hazikuhuishwa vya kutosha kama zile zilizoko kusini lakini zinavutia zaidi hisia. Kati ya madhari yanayoonyeshwa ni ibada za mazishi. Wanyama - kama ilivyo katika pango la Inoro, wanaofanana na madubwana ya kustaajabisha, ndege wake wakiwa na midomo ya mamba, tembo wenye migongo kama meno ya msumeno, wanyama wenye vichwa viwili; visaasili vya kawaida kama vile vya uganga wa mvua, na mandhari halisi au picha za mandhari zilichorwa kihalisia au kwa mtindo - kaida. Mtindo huu wa Kizimbabwe unaakisi utamaduni ulioendelea zaidi ambao, kadiri ulivyofikia, ulizuka mtindo ambao ulikuwa wa kawaida zaidi.

Michoro ya miambani iliyo kaskazini mwa Burkina Fasso ni za nusu-asilia na za kikaida ilihali zile za kusini mwa nchi hiyo zinaclekea kuwa na mtindo wa kijiometri zaidi.

Huko Jamhuri ya Afrika ya Kati, uchimbuzi umeonyesha ushahidi wa kuwepo makazi ya binadamu mapema sana, tangu kipindi kabla ya historia, kuanzia enzi kabla ya Asheuli. Idadi kadha ya vituo vya sanaa za miambani na picha nyekundu vimegunduliwa vikiwa na maumbo mekundu ya binadamu ya mtindo – kaida na maumbo meupe ya binadamu yaliyo na mikono iliyoshika nyongani. Sanaa hii inaonyesha uhusiano mdogo na ile ya Sahara na inafanana zaidi na picha za rangi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

### *Kusudi na maana*

Istilahi ‘petroglafia’ imebuniwa ili kueleza sanaa za miambani. Ama kwa hakika, sanaa hii ni aina ya maandishi ambayo lazima kwanza kielelezo chake kigunduliwe kabla ya kuweza kufasiriwa. Ndiyo maana ni muhimu kueleza alama kwanza kabla ya kufasiri na kuhakikisha maana yake.

Njia ambayo ingefaa hasa ni kukusanya takwimu ya data nyingi na bora za picha nyingi kadiri iwezekanavyo, kama msingi wa uchanganuzi fiunganishi, kwa kubainisha maendeleo mbalimbali kufuatana na wakati na mahali. Hata hivyo, lazima ieleweke kwamba alama si alama tu ya kitu fulani lakini pia ni alama ambayo ina maana fulani kwa mtu fulani na, kwa hiyo, ni aina ya ishara. Ili ishara hiyo iweze kueleweka, kuna haja ya kufahamu mambo yote ya kijamii na kiimani yanayowakilisha kundi la watu hao. Hatimaye ni muktadha mzima wa utamaduni tu ndio unaoweza kutupa mwongozo wa kufasiri ujumbe wa kiumbaji. Ni kwa kuunganisha tu vipande mbalimbali vya utamaduni ndipo tunapoweza kujenga upya ruwaza za kihistoria ambamo vipande hivi vimesukwa.

Ndiyo maana si vizuri kutumia michuuko au maelezo kama vile *Justice of the Peace*, (Hakimu wa Amani), *The White Lady*, (Mwanamke Mweupe), *The man-pulling teeth*, (Mtu anayevuta meno), *Josephine sold by her sisters*, (Josefina auzwa na dada zake), *The Martian* (Wamariti) kama majina ya sanaa za miambani za Kiafrika, kwani semi zote hizi zinaakisi fasiri za watu binafsi ambao wamelelewa katika ustaarabu tofauti na kwa hivyo zinapotosha maana halisi. Kimsingi, sanaa za Kiafrika ya kipindi kabla ya historia yabidi zifasiriwe kulingana na itikadi za watu za asili.

Kutokana na hali hiyo, kuna namna muhimu za kufasiri aina hii ya sanaa: mtazamo wa udhanifu na mtazamo yakinifu. Kwa mtazamo wa kidhanifu, sanaa ya kipindi kabla ya historia inaakisi fasiri ya binadamu kuhusu dunia. Erik Holm amesema kwamba sanaa ya kusini mwa Afrika inaweza kueleweka tu kama ikichukuliwa kuwa ni kitu kinachoelezea nguvu ya kidini na nia ya kuvuka upco wa hakika ya mambo. Hii ndiyo ilikuwa metafizikia ya watu wa kale. Alipendekeza pia kuwa turidhike na habari tunazozipata kutokana na visasili ambavyo, kwa maoni yake, ni wazi kiasi cha kutosha. Frobenius aliendeleza msimamo huohuo. Kwa maoni yake, simba wa Leeufontein amekatwa nakshi kwenye uso wake ukimulikwa na mionzi ya kwanza ya jua, kwa sababu anawakilisha jua, iihali kifarua ameelekea magharibi kwa sababu ni inzimu wa usiku na giza. Paa mwenye milia myekundu anawakilisha machafuko ya hali ya hewa, kivunjangungu anawakilisha umeme wa radi, na tembo anawakilisha mawingu ya mvua, kama inavyoonekana katika Mount St. Paul, huko Drakensberg. Kwa hivyo, inatosha kufahamu elimu zote za visasili na kosmogonia (asili ya madini, ulimwengu wa mimea na wanyama) ili kuweza kutambua viendawili vyote vya sanaa za miambani, ambavyo ‘vilianza kalc na kalc kama vilivyo visasili’.

Kwa upande mwingine, mtazamo yakinifu unaiweka sanaa hii katika muktadha wake wa kihistoria – kwamba inaonyesha kuwepo kwa watu katika jamii, na ni njia ya 'itikadi' ya binadamu ya kubainisha na kuendeleza nafasi yake katika dunia na maisha ya kijamii.

Yatubidi tuunganishe mitazamo yote miwili kama tunataka kuelewa vizuri zaidi sanaa hii ya kwenye miamba ya Afrika ambayo bila shaka yoyote, kwa kiasi fulani, ni kitabu kikubwa sana kilichokuwa na vielelezo, kinachotoa maelezo kuhusu dunia na kutoa ujumbe wa kuelimisha kwa kutumia ishara ya vielelezo, kama ilivyodhihirishwa na dhima ya michoro ya kipindi kabla ya historia katika elimu iliyotolewa kwa wasanii vijana. Katika muktadha huu michoro hii ni vielelezo vya 'historia kuu' vilivyojificha katika maleba ya visasili vinavyoeleza 'asili na mabadiliko ya viumbe vyote'. Hata hivyo, wakati huohuo, kisasili hutoa njia inayofaa kuendeleza nguvu za kuzalisha mali na mahusiano ya kuzalisha mali – au kuweza kuzikengeua. Kwa mfano, kijana wa Kisani ambaye anaomba nyota huku akinoa kigumba cha jiwe, anasema: 'Nisaidie kufuma lengo la ngu'. Huu ni mfano wa kutumia kisaasili katika kuzalisha mali. Ili kuendelea kuishi, binadamu anaomba na kutumia nguvu za dunia.

Kisasili kinaweza kutumika pia kama njia ya kuipanga dunia ili kuelewa vizuri zaidi na hivyo kuwa na uwezo zaidi wa kuimiliki. Kwa hakika, kuonyesha kiumbe wa kuogopesha ni njia mojawapo ya kukwepa kumilikiwa naye na kumchungu ni njia ya kumiliki. Kwa mfano, wawindaji watatu wenye kuvaa maleba katika picha iliyoko huko Jaret, ambao wanaonekana wakimzingira nyati mwenye chuma cha mViringo shingoni mwake, inaweza kuwakilisha mandhari ambamo wanamloga. Hadi leo wawindaji wa Sahel huvaa kichwa cha hondohondo ambacho hukichezesha juu na chini kwa kumwigiza ndege huyo, ili waweze kumnyemelea paa wakiwa wanatembea kwa miguu na mikono na kumpiga mshale kwa karibu. Wakati mwingine, michoro inayoonyesha mwanamke na mwanaume aliyevaa maleba mwenye dhakari kubwa wakicheza ngoma au kutimiza mila za unyumba huonyesha uhusiano dhahiri na ada za uwezo wa kuzaa. Ama kwa hakika, mnamo mwisho wa kipindi kabla ya historia wakati kila aina ya uhai katika majangwa ya Sahara na Namibia ilikuwa ikivia kutokana na maangamizi ya ukame, suala la uwezo wa kuzaa lilikuwa muhimu sana. Kipande cha pembe sita cha kito kutoka eneo la Neolithi huko Tin Felki kimetambuliwa na Hampate Ba kuwa ni hirizi ya uwezo wa kuzaa inayotumiwa na wanawake wa Kifulani. Vivyo hivyo, msalaba wa Agades inawezekana umetokana na alama kutoka Tanit, ishara ya uke.

Mwisho, pamoja na sababu za kidhanifu au za kimanufaa, suala la ujumi pia shurti litiliwe maanani. Furaha inayotokana na kuumba maumbo kwa madhumuni ya kuyatafakari tu au kama aina ya maelezo ya mtu binafsi ni moja ya tabia ya binadamu, kama ilivyo faraja katika kukumbuka na nia ya kuendeleza kumbukumbu ya mtu binafsi au ya jamii. Kwa asili binadamu ni mtarhi na wasanii wa kipindi kabla ya historia ambao waliumba sanaa hizi zilizohusisha vipengee vyote vya sanaa takatifu na sanaa ya kufuru ndio wanahistoria wa kwanza wa Kiafrika, kwani walichora katika mawe hatua mbalimbali za uhusiano wa Mwafrika na mazingira yake ya asili na ya kijamii.

### *Sanaa kama hati ya kihistoria*

Sasa hebu tufikirie ni kwa kiasi gani sanaa ya Kiafrika ya kipindi kabla ya historia inaweza kuwa toleo yenye vielezo ya kitabu cha kwanza cha historia ya Afrika.

## Mazingira ya Kickolojia

Ni kweli kwamba mabaki ya kipindi kabla ya historia kama yanavyowakilishwa na vifaa vilivyoonekana katika hali yake ya asili yanatuwezesha kujenga upya mazingira ya kipindi kabla ya historia. Lakini mada zinazoonekana katika picha za miambani pia zinaakisi mazingira hayo. Katika mambo ambayo pande hizi mbili zinakubaliana, zinatoa ushahidi mkubwa wa thamani ya hati za sanaa za kipindi kabla ya historia. Kwa mfano, katika eneo la Adrar Bous, ambalo limekadiriwa kuwa ni la mwaka 5140 kabla ya sasa kwa kutumia njia ya radio-kaboni limeonyesha mifupa ya kiboko ambayo ina usahihi wa kihistoria wa wanyama wa aina ileile waliochorwa huko Assajen Wan Mellen. Kama tembo, kiboko naye alihitaji misitu, na alama za kuwepo misitu kama hii zinaonekana hadi leo. Katika kipindi cha magari ya farasi kuna michoro ya michikichi ambayo labda ilitumika kuonyesha kuwepo kwa oasisi.

Huko kusini mwa Afrika mtindo wa kaskazini au wa Kizimbabwe una michoro mingi ya miti, na baadhi yake inaweza kutambulikana. Makazi katika sehemu ambazo sasa ni majangwa yana nakshi na picha za aina nyingi mbalimbali za wanyama wadogowadogo na kwamba kutembelea sehemu hizi ni kama kutembelea maonyesho ya wanyama. Licha ya aina nyingi za samaki, kuna Bubalusi, mwenye pembe kubwa zenye upana wa kufikia mita tatu kati yake na ambae sasa ametoweka, idadi kadha ya wanyama wawindaji, manyani na mbuni, bundi, n.k. Baadhi ya shughuli zinazoonyeshwa ni michoro mingi ya mandhari za uwindaji, kumbukumbu zisizokwisha za mapambano kati ya binadamu na wanyama wakali na ushindi wa akili dhidi ya maguvu. Huko Iheren, kuna mandhari ya simba anayewindwa, akiwa amezungukwa na mikuki.

Katika bonde la Nili na katika Sahara yote, kuna picha nyingi sana za mitego, zinazoonyesha umahiri wa binadamu kufanya mbinu zake zilingane na tabia na mazingira ya wanyama pori. Katika ustaarabu huu wa wawindaji, hata tembo walitishika, kama ilivyodhihirishwa na mandhari kubwa za uwindaji huko Mertuteki ya Juu. Alama za enzi hii zimedumu kwa maelfu ya miaka hadi enzi za kale wakati wawindaji walipoingia katika historia za falme nyingi za Kiafrika. Picha hizi pia zinaonyesha mabadiliko ya polepole kutoka wakati ambapo wanyama walikuwa wanategwa na kukamatwa mpaka walipoanza kufugwa. Mandhari moja huko Jabbaren inaonyesha mtu mwenye silaha akimnyemelea mnyamapori, akifuatiwa na mnyama mwingine, akiwa na hadhari lakini akionyesha pia ni wa kufugwa.

Aina mbalimbali za ng'ombe zinatofautishwa kutokana na jinsi pembe zao zilivyotengenezwa na kurembwa huku zikiwa zimepindwa na kusokotwa. Katika Sefar ya kipindi kabla ya historia picha ya mbwa mwindaji anayeonekana kama yu hai mwenye mkia wa mikunjokunjo ni saluki kama tunavyomfahamu hivi leo, na hivyo ndivyo ilivyo kwa upande wa punda aliyeko huko Tissukai. Hata mashua inaonyesha ikiwa na umbo linalokumbusha mitumbwi ya mafunjo iliyopatikana katika maziwa na mito huko Chadi na Nubia.

## Muktadha wa Binadamu

Baadhi ya michoro inaonyesha wanaume wameinama wakituunia zana, au wanawake wameinama mbele katika mkao wa kukusanya masuke ya nafaka. Si rahisi kujua kama picha hizo ni za watu wanaokusanya chakula kutokana na mimea ya porini au wanaolima nafaka,



kama inavyoashiriwa na baadhi ya mawc ya kusagia yaliyogunduliwa. Huko Battle Cave, kuna michoro inayoonyesha wasichana wadogo wa Kisani wakiwa katika safari ya kwenda kukusanya chakula na wakiwa na vijiti vya kuchimbia mabegani mwao.

Idadi ya michoro peke yake inasaidia kukisia wingi wa watu katika maeneo haya. Jambo hili likihusishwa na idadi kubwa sana ya zana za mawe zinazopatikana katika maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kaskazini-mashariki ya Bechar huko Algeria, inaweza kuonyesha kuwa uzalishaji mali ulikitwa katika mfumo wa nusu tasnia. Wanaume wanaonekana kuwa walikuwa wanajipamba zaidi kuliko wanawake hadi kipindi cha Maksai, wakati hali ya mambo ilipogeuka na kuwa kinyume. Nguo za wanaume zilikuwa zimetengenezwa kwa ngozi za wanyama. Walivaa tepe za kichwa zilizorembwa na makoti ya manyoya, pamoja na aina kwa aina za vidani, vikuku, bangili, na marembo mengine. Mwanzoni wanawake walivaa vipande vya nguo kusitiri scheinu za siri, lakini baadaye walivaa vikoi ambavyo vilikuwa na mikunjo katika sehemu ya chini iliyopangwa kwa namna mbalimbali, nguo zinazobana mwilini, sidiria na aina mbalimbali za vilemba, kama kile cha ushungi kinachoonekana huko Jabbaren.

Mara nyingi nyumba zilichorwa katika umbo la nusu mviringo zikionyesha vibanda na vifaa vyake vyote pamoja na shughuli za kifamilia zinazofanyika ndani ya nyumba hizo. Katika miteremko ya milima ya Tichit ulioko Mauritania, ambako vijiji 127 vimebainishwa, inaeneo ya makazi yalikuwa katika rasi zilizochelea upande wa kusini. Makazi mengi ya mawe yalijengwa katika misingi ya miamba mikubwa yakikumbushia yale ya Zimbabwe au makazi ya ngome katika dola ya Monomotapa, na kila makazi yalikuwa na uwezo wa kuwaweka watu 3,000.

Mandhari mbalimbali zilizochorwa katika sanaa ya miambani ya Afrika inaweza ikatazamwa kama filamu iliyoandikwa kuhusu maisha ya kila siku ya enzi za kipindi kabla ya historia. Kwa mfano huko Takedetoumatime, wanawake wazuri na wanene wameketi mbele ya vibanda vyao na watoto wao, na ndama wamewekwa katika mstari wakiwa wamefungwa kamba, ilihali wanaume wanajishughulisha na kukamua ng'ombe. Idadi ya wanawake waliopo inaashiria kwamba kulikuwa na ndoa za wake wengi. Huko Orange Springs katika jimbo la Natal, Afrika ya Kusini, wanawake wanaonyeshwa wakipiga makofi huku wamesimama wakiwazunguka wacheza ngoma waliovaa maleba. Picha ya ukuta iliyoko katika makazi ya Iheren, moja ya michoro ya kiwango cha juu ya kipindi kabla ya historia, inaonyesha msururu wa maksai waliopambwa vizuri, wakiwa na viriba vinavyoning'inia mbavuni mwao, wakiwa wamepandwa na wanawake waliovaa nguo za thamani. Baadhi ya wanyama wameinanisha vichwa vyao katika shimo la maji, wakati kundi lote lililobaki linakwenda mbele kwa mwendo wa madaha.

Huko I-n-Itinen, mandhari yenye wazee wakiwa wamevalia marembo yao ya morani wakiwa wamevaa sare inaonyesha kuwa jamii ilikuwa inaanza kuwa na mfumo wa utawalansonge. Pia inatushawishi kufikiri kwamba wapiga mishale waliovalia makoti walikuwa ni namna fulani ya jeshi la polisi.

Huko kusini mwa Afrika, kuna mandhari nyingi zinazowakilisha vita, hasa baina ya Wasani na Wabantu. Hata hivyo, mapenzi yalichukua nafasi yake, kama inavyoweza kuonekana katika picha nyingi za kujamiiana. Huko Acacous nchini Libya na Wadi Jerat huko Tassili, wanaume waliovaa maleba wakiwa na dhakari kubwa zilizodinda wanaonekana wakiwa tayari katika hali ya kuanza kujamiiana na wanawake.

Dini na sihiri vilichukua nafasi muhimu sana. Baadhi ya picha zinaakisi siri inayovizinga visasili na kuonyesha maksai mwenye vichwa viwili na motifu za mizunguko zinazohusiana

na wanyama - na pengine sihiri isiyodhuru - ambazo baadaye ziligunduliwa katika kazi za ufinyanzi za Misri mwanzoni mwa falme za Kifarao katika umbo la nyoka wa Mehen. Kadhalika kiungamwana kinachotoka katika mapaja ya mwanamke na kuungana na kitovu cha mpiga mishale akiwinda kinaonyesha imani ya kuwepo kwa nguvu ya siri inayotoka kwa mama, anayeomba dua huku mikono yake ikiwa imeinuliwa na kuelekezwa kwa mwanawe, ambaye amekabiliwa na hatari. Aidha huko Botswana, mnyama ambaye amekusudiwa kutolewa kafara ya mvua anaonyeshwa akiwa anatembezwa katika sehemu iliyowazi akiwa amefungwa kamba ambayo mwishoni imeshikwa na watu wa nyadhifa mbalimbali. Ufumbuzi wa baadhi ya vitendawili hivi unaweza tu kupatikana katika Afrika ya leo. Kwa mfano, Hampâté Bâ akifasiri mandhari ambayo hapo awali ilijulikana kama 'Maksai wa Kisanaa' (kwa sababu sehemu ya chini ya miguu yao haikuonyeshwa) aligundua kuwa ni kielelezo cha sherehe za lotori ambapo maksai huswagwa kwenda kwenye maji ili kusherehekea asili yao ambayo ilikuwa ni majini. Mkonu uliochorwa pamoja na mandhari hii umefasiriwa kama ni wa Kikala, mwanzilishi wa ufugaji.

### Athari na uhamaji - ustaarabu wa wenyeji

Kuna tabia ya kutaka kueleza vipengee vyote vya utamaduni wa Afrika kwa kutumia athari za kutoka nje. Tasnifu hii haina budi kukataliwa. Sanaa ya Ulaya ya kipindi cha kabla ya historia iliyogunduliwa katika sehemu mahsusi za Ufaransa na Uhispania ni ya mapema zaidi, yenye umri wa kuanzia enzi za Paleolithi, lakini inakubalika kwamba haikuwa na athari katika Afrika ambako Ncolithi na Paleolithi ni enzi mbili zilizotokea mapema kabla ya zile za Ulaya. Ni kutoka kusini mwa Atlas kwenda chini ambako sanaa ya Kiafrika ya kipindi kabla ya historia inadhihirika kuwa ilistawi.

Wala si kweli kwamba sanaa ya miambani ya kipindi kabla ya historia polepole ilisambaa kuelekea katikati ya Afrika ikitokea bonde la Nili katika Mashariki ya Afrika. Kinyume na madai hayo, sanaa ya Nili ya Misri ilistawi baadaye zaidi kuliko ile ya Afrika ya Sahara na Sudani. Picha za Sahara za maksai zenyenc visahani kati ya pembe zao ni za mapema mno kuliko zile zinazoonyesha Hathor mungu ng'ombe. Kadhalika, kipanga wa Sahara ni wa mapema zaidi kuliko watangulizi wa Horusi wanaoonekana katika makaburi ya Misri ya kabla ya enzi za ufalme. Vivyo hivyo kondoo aliyebeba tufe ni mtangulizi wa mapema sana wa kondoo wa Amon. Andre Malraux anafikiri kuwa vichwa vya wanyama vya Wadi Jerat ni watangulizi wa wanyama miungu wa Misri. Mashua za hali ya juu zisemwazo kuwa ni za 'aina ya Kimisri' zilizoonekana katika michoro huko Sahara kwa hakika ni za Sahara. Vivyo hivyo, michoro iliyodhaniwa kuwa ni kumbukumbu za Wahikso, Farao, na kadhalika - kwa sababu alama zao za utawala walizovaa ni sawa na zile zilizovaliwa na wafalme katika Bonde la Nili - zilikwishasambaa katika Sahara wakati Misri ilikuwa bado haikaliki kwa sababu ya kinamasi. Ilikuwa ni wakati wa enzi ya historia ambapo ustaarabu wa Misri ulishamiri kupita mwingine wote kiasi kwamba ulifikiriwa kuwa ndio asili ya vitu vyote hivi; na kuwa chimbuko lake la Sahara, Sudani, Afrika Mashariki na Mashariki ya Karibu lilisahaulika kabisa. Mahusiano baina ya kusini mwa Afrika na eneo la Sahara hayakuwa makubwa, na, kwa vyovyote vile, licha ya ukweli kuwa sehemu ya kusini ya bara hili ilijaa idadi kubwa ya watu tangu mapema sana, sanaa yake inaonyesha wazi kuwa ni ya baadaye sana kuliko ile ya Sahara. Kipindi peke yake ambacho kina sanaa inayofanana na zile za kusini mwa Afrika ni kipindi cha Maksai cha Sahara, vinginevyo sanaa ya kusini mwa Afrika inaonyesha sifa zake asilia kama vile mandhari ya ardhi yenye

mimea mingi, maumbo maalum ya miamba na mandhari za mazishi. Uchunguzi linganifu itabidi ufanywe ili kuielewa picha ya maendeleo haya kwa uwazi zaidi.

### Mtazamo finyu wa nadharia za jamia (mbari kuu)

Itakuwa ni makosa kuichukulia sanaa ya Afrika ya kipindi cha kabla ya historia kuwa ni kazi ya zile zidaiwazo kuwa ni 'jamia' kuu ambazo baadhi yake kama vile Waateri wa aina ya Neanderthal wa Afrika Kaskazini na Magharibi na Wakapsi wa Afrika Kaskazini na Sahara Kaskazini zilidhaniwa kuwa zilianza Mashariki ya Karibu.

Baadhi ya waandishi wanadai kuwa kazi za kipindi cha Bubalusi zinatokana na watu wajulikanao kama 'Watu wa Mediterania' ambao ama walikuwa weupe au machotara, ilibali sanaa ya 'kichwa mviringo' ilitokana na kundi la 'Wanegro' ambao wakati mwingine hudaiwa kuwa walioana na watu kutoka Mashariki ya Karibu na kuleta utamaduni unaojulikana kama wa mapokeo ya Neolithi ya Kisudani. Kutokana na fikra hii, kipindi cha Maksai kingekuwa ni kazi ya wahenga wa Kifulani na athari za mapokeo ya Guinea zingeneza hadi sehemu za makazi katika miteremko ya milima ya Tichitt huko Mauritania.

Juhudi zote hizi za kujaribu kuijenga upya kale ambazo zinashadidia athari toka nje ya Afrika zinatokana na misingi hafifu. Baadhi ya watu wamezungumzia kuwepo kwa 'athari za dhahiri za Kiafrika' katika michoro ya miambani katika Sahara.... Zaidi ya hayo, dhana za jamia, mbari, mtindo wa maisha na ustaarabu zinatumika tu kiholela, kiasi kwamba istilahi kama vile weusi, weupe, Wafulani, Waafrika, Wakapsi au watu wa Sudani, zinatumika bila liata kufafanuliwa kwa namna yoyote ile.

Watu wa Neolithi ya Kisudani wanaelezwa kuwa ni mbari ya 'wafugaji wawindaji ambao walikuja kutoka mashariki.' Sura zao 'nyororo, mbinu zao za ufugaji, vilemba vyenye shore vya wanawake na misuko ya wanaume vinadhaniwa kuwa ni uslahidi wa kutosha kuhusisha sanaa zote za miambani zinazoonyesha sifa hizo za Wafulani. Lakini, tofauti na Wasani, Wafulani hawakumbuki kuwa walitoa sanaa za aina hiyo. Ama kwa hakika maumbile yote ya Kiafrika yanaweza kuonekana katika michoro hii, kama vile yanavyoweza kuonekana karibu katika mbari zote za Afrika ya kitropiki hadi leo hii. Je, kuna aliyewahi kuona kikundi cha watu weusi wenye 'vichwa mviringo' tu? Zaidi ya hayo, hapakuwepo kizuizi kwa wasanii hao kubadilisha sura za mashujaa wao wa kiume na wa kike.

Vilevile hakuna uthibitisho iwapo tofauti kati ya wakulima na wafugaji ilikuwa kubwa kama hivi leo. Akiandika kuhusu watu wa Neolithi ya Kimauritania, H.J. Hugot anasema: 'Walipowasili, watu weusi wa Tichitt walikuwa na maksai wao,' na mahala pengine: 'ni katika kipindi cha ufugaji cha kati ndipo Wanegro walipoanza kuwasili. Hiki kilikuwa kipindi kikuu cha Maksai...' Kwa hivyo basi, si ufugaji wala vipimo vya fuvu vilikuwa vigezo vya kutosheleza. Vigezo hivi viwili ni sifa za kijuujuu za kiwiliwili<sup>1</sup>.

Wote hao waitwao 'wanawake weupe' katika michoro ya mianubani ya Afrika - na katika mfano wa Afrika Kusini, ni uso tu ulio mweupe - ambao baadhi ya wanazuoni wamedhania kuwa 'mlolongo wa watafutaji (wa madini) kutoka Ghuba ya Uajemi'; kwa hakika wanawakilisha wawindaji au wasichana wa Kiafrika wakitoka katika sherehe za unyago wakiwa wamejipaka rangi, kama ilivyo leo, kwa kutumia kaolini nycupe inayoanisha kutoweka kwa haiba iliyopita na kuingia katika hadhi mpya.

Usuli wa kihistoria wa sanaa ya miambani ya Afrika Kusini unadhihirika vizuri zaidi, kwa maana unaonyesha mahusiano kati ya Wakhoi-Khoi na Wasani, na hatimaye kati ya

1 Tazama Sura ya 10: Nadharia za 'jamia' na historia ya Afrika.



26.1 Utondoti wa piḡha za pango la 'Binti Mweupe' Afrika ya Kusini (A.A.A. Duverger)

Wakhoisani na Wabantu. Ukubwa wa alama za mikono zilizo miambani, nyamanyama za matako na kudinda nusu kwa uume – zote hizi zinatoa ushahidi wa kutosha wa watu ambao walizichora picha hizi.

### Ujumi

Japokuwa mambo mengi yamefuata mifano ya sanaa za Waarabu na Wazungu, sanaa ya kipindi kabla ya historia inachukua nafasi muhimu sana kati ya vyanzo vya sanaa ya sasa ya Kiafrika. Rangi zinazoonekana katika picha za miambani ni sawa na zile ambazo bado zinang'ara sana katika kuyaremba maleba na wachezaji ngoma.

Hii ni sanaa inayobainishwa kwa uchunguzi wa makini wa kila kipengee kama inavyoonekana katika picha ya maksai wa Ugusburg, wa huko Botswana, ambako hata yale maumbo madogo sana ya kianatomia yamechorwa vizuri na kwa uhakika kabisa. Mchoro wa twiga na mtoto wake wa huko Eneri Blaka umechongwa kwa ustadi huohuo. Hivyo ndivyo ilivyo pia katika picha ya ukutani ya Iheren. Ni mkusanyiko mkubwa wa kundi la watu lakini kila mtu anayehusika anaonekana wazi. Kuna kundi la twiga kumi na sita waliochanganyika kimaridadi, vikundi vya wanawake waliovalia nguo za rangi zilizokolea wakisafiri kwa maksai wao waliobeba mizigo; aina mbalimbali za paa na swala; mtoto wa twiga ambaye ndio kwanza amezaliwa akiwa bado ameunganishwa na utovute wake, simba akimnyakua kondoo hali akiwatazama watu wenye mikuki wanamfukuza, papo hapo kondoo wengine wakitawanyika kwa woga; na maksai anakuja bwawani kunywa maji na kuwafanya chura waruke. Ni mandhari ya kuvutia yenye kuonyesha hali halisi ya maisha.

Hata hivyo, kuzingatia kila kitu kufuatana na maumbile hakumzui msanii kufikiria kwa makini kiini cha wazo kuu: hii ni moja ya sifa isiyobadilika ya sanaa ya Kiafrika. Mhusika mkuu anaonyeshwa kwa ukaribu zaidi na kujitokeza zaidi kuliko wengine kama Farao au Oba wa Benin anavyoonyeshwa akiwa na maadui au watu wake.

## *Hitimisho*

Sanaa ya Kiafrika ya kipindi cha kabla ya historia ni sanaa inayojulikana katika maisha ya kila siku, ingawa imejaa mafumbo na maana zisizo dhahiri. Sanaa hii imetoa baadhi ya kazi bora sana ambazo ni urithi wa sanaa ulimwenguni, kama vile kondoo mwenye kisahani cha jua wa huko Bualen. Mtazamo huu wenye sifa hizi mbili unaonyesha vizuri pande mbili za maisha ya Mwafrika wa sasa: wepesi wake katika kukabili maisha ya kila siku na udhati wa matendo yake katika kucheza ngoma wakati wa matambiko.

Sanaa ya kipindi kabla ya historia bado inaishi. Kuna haja ya kuirudisha katika mihtasari ya shule na kuikabidhi kwa Waafrika wenyewe, ambao wanashindwa kuifikia kwa sababu ya umbali ambao ni watalii na wataalamu pekee kutoka nchi tajiri ndio wanaweza kuifikia. Orodha kamili ya sanaa ya Afrika yahitaji kukusanywa ili uchunguzi linganifu uweze kufanywa.

Kwa kuwa alama zinaweza kueleza kitu kwa ufasaha kama maandishi, sanaa ya miambani ya Kiafrika inaweza kuchukuliwa kama ni kitabu cha kwanza cha historia ya bara hili. Sanaa hii inatoa ushahidi ambao ni dhahiri lakini ambao pia ni kitendawili kinachohitaji kuthibitishwa na vyanzo kama vile paleontolojia, elimu ya tabia ya lali ya nchi, akiolojia na mapokeo simulizi.

Sanaa huakisi na vilevile huchochea tendo, na hii michongo na picha za kipindi kabla ya historia vinaeleza juhudi za mapambano ya Mwafrika kutaka kuyatawala mazingira, na pia kupanua hulka yake kwa kujipatia furaha ya kiungu yas uumbaji.

Kwa muda mrefu, waandishi wa vitabu wa Ulaya wameelezea asili ya kilimo kulingana na mtazamo wa Kizungu. Kwa mujibu wa maoni yao, kilimo kilianza Mashariki ya Karibu, hasa Mesopotamia. Hata hivyo, tangu Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, wakati nafasi muhimu ya eneo la rutuba lenye umbo la mwezi mwandamo *Fertile Crescent* katika mapinduzi ya Kineolithi bado inatambuliwa, mwanga umetupwa kuhusu uvumbuzi wa mazao katika mabara ya Amerika, ustawishaji wa mapema wa susu za kilimo katika sehemu za tropiki za kusini-mashariki mwa Asia, na mchango wa Afrika katika historia ya kilimo duniani.


Mapema zaidi, mtalaamu mashuhuri wa Kirusi wa mambo ya kilimo, N.I. Vavilov alikuwa ameonyesha kuwa kulikuwa na sehemu fulani katika Afrika ambako huenda mimea inayolimwa ilianza,<sup>1</sup> na mmojawapo wa wasaidizi wake, aitwaye A. Kuptsov, alionyesha hapo baadaye kuwa kwa hakika susu hizo za kilimo zilikuwepo. Lakini kwa muda mrefu kashfa za kikoloni zilizua wazo hili lisikubalike.

Katika miaka michache iliyopita kumekuwa na shauku kubwa sana ya kuchunguza zaidi suala hili kama inavyodhihirika katika makala yaliyochapishwa mwaka 1968 katika kitabu kiitwacho *Current Anthropology*; makala ambayo yaliandikwa na J.D. Fage na R.A. Oliver, na pia kazi ya W.G. Randles kuhusu historia ya ustaarabu wa Wabantu.

### *Mazingira ya asili na chimbuko la kilimo cha Waafrika*


Chimbuko na maendeleo ya mbinu za kilimo na mimea iliyolimwa vinahusiana sana na hali ya asili ya mazingira ya maeneo yale; kama vile udongo, tabia ya hali ya nchi, maji na mimea ya asili. Lakini maendeleo ya kilimo na ya ufugaji hutegemea mambo mengine yanayounda tamaduni na staarabu za watu mbalimbali kiasi kwamba shughuli zao za kilimo na ufugaji zinaweza kutofautiana hata katika mazingira yanayolingana. Ndiyo maana uhamaji wa watu ni muhimu sana katika kueneza au kupokea tabia mpya za maisha na hivyo kusnzisha mbinu ambazo zilikuwa hazijulikani, na hasa dhana za asili zinazohusu mahusiano yao na maumbile, matumizi ya maeneo n.k. Ndio kusema, basi, wakati Ulaya ilipokuwa ikianza kutoka katika enzi ya Paleolithi, kilimo na ufugaji tayari vilikuwa vimestawi huko Mashariki ya Karibu ambako bidaa za teknolojia na itikadi zinazoambatana nazo zilitapakaa kaskazini hadi Mediterania na kuchochea mapinduzi ya Kineolithi luko Ulaya. Afrika pia iliathiriwa na huu mjo wa bidhaa na watu na fikra zilizoandamana nao.


<sup>1</sup> Vavilov, N.I., 1951, *Chronica Botanica*, 13:1-6.



27.1 Mgawanyiko wa Kanda kilatitudo katika bara la Afrika (R. Portères)


27.2 Mifumo ya kiekolojia katika bara la Afrika (R. Portères)





27.3 Sehemu za asili ya kilimo katika bara la Afrika (R. Portères)

27.4 Ramani ionyeshayo utamaduni wa kilimo katika bara la Afrika (R. Portères)





Hata hivyo, isichukuliwe kuwa mambo haya yalifanyika katika muda mfupi. Ilichukua muda mrefu sana tangu binadamu atoke katika hatua ya kijungu meko ya uwindaji na ukusanyaji wa chakula mwisu hadi kufikia hatua ya uzalishaji kwa njia ya kilimo na ufugaji, kupitia awamu za kati kama vile kuwafuga wanyama pori na kupanda mazao kwa kubahatisha. Katika kuzifanya shughuli hizi, binadamu aliweza polepole kujitoa katika mashaka na hatari zilizotokana na kushindwa kwake kuyadhibiti mazingira alimokuwa akiishi. Hata hivyo, athari za mazingira hazikuweza kutoweka kabisa, hasa katika kipindi kabla ya historia.

Kwa mfano katika Afrika, kuwepo kwa kanda pacha za tabia ya hali ya nchi na ekolojia katika kila upande wa Ikweta kulisababisha ruwaza za kanda ambazo zilielekea kuathiri maendeleo ya kilimo. Baadhi ya kanda hizi kama vile Sahara, misitu ya Ikweta, mbuga za Tanzania na jangwa la Kalahari zilisababisha kuwepo kwa vikwazo wakati watu walipokuwa wakihamia sehemu za kaskazini au kusini ijapokuwa hakuna kanda ambayo ilikuwa haipitiki kabisa. Kanda nyingine kama vile mbuga za mtandao na savana za maeneo ya tropiki, zilikuwa ni sehemu zilizosaidia sana katika kueneza mawazo mapya.

Mbali na latitudo, mwinuko kutoka usawa wa bahari na sura ya nchi ya kijiografia, vilikuwa ni vitu muhimu sana katika kuweka mipaka ya kanda maalum za kiekolojia; baadhi yake zilikuwa hazifai kabisa kwa mimea na zingine zilikuwa zikifaa zaidi, kama vile nyanda za juu zilizokuwa ukingoni mwa Bonde la Ufa, ambazo zilikuwa kama ujia uliowezesha makundi mbalimbali ya watu yapite wakati wa kusuka Ikweta au milima ya kati ya Ethiopia.

Kwa jumla, Afrika inaweza kufikiriwa kama bara lenye sehemu muhimu ya msitu wa Ikweta isiyokalika kwa urahisi na kwamba eneo hili limezungukwa na eneo kubwa la nchi ya savana na mapululu sehemu za kaskazini, mashariki na kusini. Kaskazini na kusini zaidi kuna kanda mbili kame, ambazo ni jangwa la Sahara, upande wa kaskazini, na jangwa la Kalahari, ambalo ni jembamba zaidi, upande wa kusini. Mwisho, sehemu za pembezoni kabisa mwa bara hili kuna mazingira ya Kimediterania. Majangwa yaliyotajwa hapo juu hayakuwa kame wakati wote. Inawezekana kuwa wakati fulani yalikuwa pia ni susu za kilimo au ufugaji. Hapo mwanzoni, misitu ilimpatia binadamu mazingira yanayofaa kwa ukusanyaji wa chakula na uwindaji, mazingira ambayo yaliwapatia watu hawa waliotawanyika njia ya maisha bila ya kuhangaika sana.

Njia hii ya maisha inayotegemea uwindaji na ukusanyaji wa chakula bila shaka ilikuwa ikitumiwa pia katika mazingira makame kama inavyoonekana siku hizi katika ustaarabu wa Kung Sang huko Kalahari. Hata hivyo, katika sehemu kame chakula ni haba na cha namna, moja na hupatikana katika sehemu maalumu, kama vile kwenye visima vya maji.

Kati ya mwaka - 5500 na - 2500 kabla ya Kristo, kulikuwa na awamu ya umajimaji iliyojulikana kama enzi ya Makali. Awamu hii iliwezesha kuwepo kwa uhusiano kati ya eneo la Mediterania na misitu ya Ikweta iliyoko kusina mwa Sahara. Hii iliawezesha watu pia kufanya shughuli za uvuvi katika maziwa na miti ambayo ilikuwa na idadi kubwa ya samaki. Jambo hili liliwafanya watu waishi pamoja na kuanza polepole kubadili shughuli zao kuwa za kilimo. Ukweli ni kwamba, kabla ya wakati huo, kati ya mwaka - 9000 na - 5000 kabla ya Kristo, mkusanyiko mkubwa wa watu ulikwishaanza kuonekana katika ukanda uliokuwa kati ya jangwa na msitu, hasa katika nyanda za juu zenye majani za Afrika Mashariki, kuzunguka maziwa kando ya mito mikubwa kama vile Niger na Nili, na pia katika pwani ya Mediterania na kwenye ncha ya kusini ya bara hili. Hivyo si ajabu kwaamba sehemu hizi ambazo zilikalifiwa kwanza kuanzia Bonde la Mto Nili hadi kufikia nyanda za juu za Monomotapa, yakiwemo mabonde ya mito ya Niger na Senegal, maeneo yaliyo kando ya maziwa makubwa, sehemu za chini za Mto Kongo na nyanda za juu za Shaba, ndizo zilikuwa susu za staarabu zilizojulikana sana.

## Asili ya Kiafrika ya baadhi ya mimea inayolimwa

Vavilov alipambanua maeneo manane ambako mimea inayolimwa ilianzia. Ni eneo moja tu kati ya haya ndilo lilikuwa katika bara la Afrika, nalo ni eneo la *Abyssinia*, ingawa kulikuwa pia na eneo jingine la *Mediterrania* ambalo lilipakana na eneo moja la Mashariki ya Karibu. Maeneo haya mawili yalikuwa na uhusiano wa karibu sana.

Mbinu ya Vavilvo ilileta msukumo mkubwa katika kuchunguza asili ya kilimo, hasa kwa vile alionyesha kuwa ilikuwa ni lazima kutofautisha kati ya maeneo ya mabadiliko ya msingi ambapo mimea wa aina fulani inaweza kuonekana katika maumbo anuwai lakini bado maumbile yake muhimu yanaendelea kuonekana; na maeneo ya mabadiliko ya pili, ambapo sifa nyingi ambazo hazitokei zaidi bado zingalipo. Susu ya kilimo inaweza kusemwa kuwa ipo pale ambapo maeneo hayo mawili yana uhusiano mkubwa kwa vile hii ina maana kuwa mwanadamu amejishughulisha katika kazi ngumu na ndefu ya uchaguzi na ugeuzi unaoakisika katika sifa zinazofuatana za aina mbalimbali za mimea. Hata hivyo, shurti izingatiwe kwamba mahali ambapo mimea fulani unalimwa panaweza kuwa mbali kijiografia na mahali ulipoanzia, na huenda ulisambazwa na miguro ya watu.

Uchunguzi uliofanywa na Porteres umeweza kukamilisha picha kuhusu maeneo ya kilimo katika Afrika kwa kuonyesha kwamba mbali na eneo la *Abyssinia* na sehemu ya Afrika ya eneo la *Mediterrania*, kulikuwa pia na maeneo ya Afrika Magharibi na Afrika Mashariki; hili la mwisho pengine likiwa ni chane ya eneo la *Abyssinia*. Aidha eneo la Afrika ya Kati linaonyesha sifa za peke yake.

Hivyo susu za maendeleo ya kilimo katika Afrika zinaweza kuelezwa kwa muhtasari kama ifuatavyo:

1. *Susu ya Mediterania ya Afrika*, ambayo inaeneo kutoka Misri hadi Moroko na ambayo ilitumika kama njia ya kubadilishana bidhaa na susu ya Mashariki ya Karibu. Huu ulikuwa ndio mwanzo wa mimea ya nafaka kama vile ngano na shayiri, wa mimea ya jamii ya kunde kama vile dengi, wa mizetituni na kadhalika.
2. *Susu ya Nili -Abyssinia*, ambayo ilikuwa na ngano, shayiri na mimea ya jamii ya kunde. Vilevile kulikuwa na uwele na aina nyingine za mimea zilizoweza kuota katika sehemu hizo kama vile mibuni ya aina ya Arabika (*Coffee Arabica L*) na migomba ya *Abyssinia*.
3. *Susu ya Afrika Magharibi*, ambayo ilikuwa na mimea ya asili kama vile uwele, mtama na ulezi fonio (*Digitaria excilis Stapf*), mpunga na jamii ya viazi mishea (*Elaeis guineensis*) na pia mimea ya jamii ya kungu kama vile kokwa za kola.
4. *Susu ya Afrika ya Kati*, ambayo inaonekana kuwa mwendelezo wa susu ya Afrika Magharibi ambayo ina nafaka chache lakini mimea mingi zaidi ya jamii ya kunde kama vile njugu (*Voandzeia subterranea thon*).
5. *Susu ya Afrika Mashariki*, inayotanda Magharibi hadi Angola na ambayo ina uwele na aina anuwai za mtama na ufuta.


Hata hivyo, itakuwa si sahihi kufikiria kuwa hapo awali kilimo kilistawi katika Afrika bila kuwa na uhusiano wowote na sehemu nyingine. Ukweli ni kwamba palikuwa na mawasiliano mengi kati ya susu hizi, na ili kuelewa zaidi inafaa tulifikirie eneo la kati la msitu wa Ikweta kama 'Bustani ya Mimea' ingawa ina aina chache za mimea ukilinganisha na maeneo ya misitu ya tropiki yenye mvua nyingi yaliyoko Asia na Amerika. Ni sehemu ambayo ilitumia kilimo bustani (*hortus* katika lugha ya Kilatini) kuliko kilimo cha mashamba.




27.5 Uchomaji wa udongo wa juu katika sehemu za Futa Jalon; Pila, Timbi-Madina (R. Portères)

27.6 Ulimaji wa mashamba, Kadyendo, unaofanywa na Wadyula wa Ussuye (Kasanansi) hapa shamba linatayarishwa kwa ajili ya kupanda tena mpunga (R. Portères)





27.7 na 27.8 Njia mbili za ulinaji wa mpunga (R. Portères)



zilizokuwa kando za Afrika-Mediterrania na Nili-Abyssinia, zilizokuwa na mawasiliano zaidi na sehemu za nje ya Afrika; kupitia Misri na Ethiopia ndipo plau ya mkono ilifikia baadhi ya sehemu za kilimo zilizozalisha nafaka.

Ni eneo hili la kilimo kingi cha uwele na mpunga – kinyume na kilimo cha mazao mbalimbali yaliyokuwa yanapandwa katika eneo la bustani – ambalo polepole liliwezesha watu kuanza kustakimu kwenye kingo za msitu. Hii iliharakisha kuzifanya sehemu hizi ziwe savana, ingawa kwa upande mwingine, watu waliweza kuyazoca mazingira ya misitu ambamo walilima zaidi mimea ya jamii ya viazi na mimea mingine ambayo hapo awali ilikusanywa kwa chakula. Hata hivyo, zao muhimu katika mazingira haya ya savana ni mtama; zao lililopandwa Afrika na lenye aina kadha tofauti ambazo ni za asili mbalimbali katika sehemu za mashariki na inagharibi mwa bara hili, na katika Pembe ya Afrika. Mojawapo ya aina hizi za mtama imetawanyika katika eneo kubwa hadi kufikia sehemu za Iran na India. Hakuna shaka kwamba aina fulani za mtama ambazo zilianza kulimwa Afrika zilienezwa baadaye katika sehemu nyingine za dunia.

Hata hivyo, asili ya kilimo katika Afrika kimsingi inatokana na upandaji wa mpunga ulioendelezwa kutokana na aina zake mbalimbali za asili zilizokuwa katika susu ya Afrika Magharibi. Hapo zama za kale, Strabo alitaja kuwepo kwa kilimo cha mpunga katika Afrika, na katika karne ya kumi na nne Ibn Battuta alieleza kuwa mpunga ulikuwa ukilimwa kando ya Mto Niger. Kwa muda mrefu watu walidhani kuwa asili ya mpunga ilikuwa Asia (*Oryza sativa* R.) lakini baadaye ilikubalika kuwa mpunga ulikuwa ni zao mahsusi la Kiafrika (*Oryza Glaberrima Steudel*).

Ama kwa hakika, mpunga wa Kiafrika ni mfano mzuri wa hali ambazo kwa mujibu wa Vavilov zinahitajika kuwepo ili susu ya kilimo iweze kutambulika: eneo pana sana lenye kustawisha mmeapori mama; wingi wa aina zake, na sifa au tabia muhimu za ekolojia zinazolizwezesha zao hili kuota katikati ya delta ya Mto Niger (ambalo ni eneo la msingi), na aina za spishi zenye sifa pungufu huko Gambia na Kasamansi (ambalo ni eneo la pili). Kwa hiyo, aina mbalimbali za mpunga wa Kiafrika unaolimwa sasa ulienea kuanzia sehemu ya kati ya Mto Niger na kutapakaa Afrika Magharibi hadi kuifikia pwani ya Guinea. Ni kuanzia karne ya nane tu ndipo aina za mpunga za Asia zilianza kuingizwa barani Afrika na zilifika tu pwani ya Afrika Magharibi katika karne ya kumi na sita.

Vivyo hivyo, mimea mingi ya chakula ambayo asili yake ni Afrika inapatikana sehemu nyingi za bara hili, hata katika sehemu za pembezoni za Ethiopia, bonde la Mto Nili na Afrika Kaskazini.

## Uhusiano baina ya Afrika na Asia

Afrika iliipa Asia spishi nyingi za mimea inayolimwa kama vile aina mbalimbali za mtama. Afrika nayo imepokea mimea ya nafaka kama vile ngano na shayiri kutoka Mashariki ya Karibu, na ndizi, viazi vikuu na taro kutoka Arabia ya Kusini kupitia pwani ya Afrika Mashariki.

Inaonekana pia kuwa Afrika ilipokea kutoka Asia aina nyingi za mifugo ambayo wazazipori wake hawamo katika orodha ya wanyama wa Afrika ya Kusini mwa Sahara. Hata hivyo, kufugwa kwa wanyama hawa kunaweza kuwa kulifanyika wakati ambapo jangwa la Sahara na bonde la Mto Nili vilikuwa bado katika enzi za Neolithi.

### *Hitimisho*

Ni muhimu kutambua kuwa kustawi kwa kilimo katika kipindi kabla ya historia ni mwendeleo ambamo maeneo mbalimbali ya bara hili yalikuwa na uhusiano wa karibu. Kwa mfano ngano, uwele na mtama vinaota pamoja katika oasisi. Ethiopia ni eneo ambalo limekuwa muhimu katika kubadilishana mazao kutoka pande mbalimbali.

Eneo ambalo ni muhimu sana kihistoria kati ya maeneo yaliyohusika na maendeleo ya kilimo katika Afrika ni lile la savana na mapululu, hasa sehemu zilizo karibu na misitu na mito mikubwa na maziwa.

Ni vigumu sana kutaja tarehe sahihi ya kuanza kwa shughuli hizi za kilimo. Hata hivyo kipindi muhimu kinaonekana kuwa ni kuanzia - 9000, hadi - 5000, yaani wakati mmoja na kipindi cha kufanyika kwa bidaa za aina hiihii huko Mashariki ya Karibu.

28

## *Uvumbuzi na ueneaji wa metali na maendeleo ya mifumo ya jamii hadi karne ya tano kabla ya Kristo*

Huenda bonde la Mto Nili ndiyo kanda ambapo maendeleo ya makundi ya jamii za Kineolithi huweza kufuatiliwa vizuri zaidi hadi nyakati za historia. Mto Nili, ukiwa na urefu wa kilomita 6500 kutoka katikati ya Afrika hadi Mediterania, unafuata usawa wa maziwa makubwa na Bonde la Ufa na hivyo kufanya mhimili wa kaskazini hadi kusini kupitia bara la Afrika. Takriban katikati ya safari yake kuelekea baharini kwenye njia panda ambayo haina kifani kwingineko katika Afrika, Mto Nili hukutana na njia kuu ya Mashariki-Magharibi inayoiunganisha Bahari ya Shamu na Atlantiki na kuvuka mbuga zilizo kandokando ya milima ya Ethiopia na maeneo ya wazi ya Darfur na Kordofani, na kupitia mabonde ya Mto Niger na Ziwa Chadi.

Kwa bahati mbaya, kinyume na bonde la Nili ya chini ambalo akiolojia yake inafahamika vema, bonde la katikati baina ya Poromoko la Pili na la Sita, bonde la juu kutoka Khartoum hadi kwenye maziwa makuu, na hasa mabonde yaliyo nusu jangwa ambayo ni mito iingiyayo katika Nili, ni sehemu ambazo hazijafanyiwa uchunguzi wa kutosha.

### *Kutoka enzi za Neolithi kikwi cha tatu kabla ya Enzi za Ukristo*

Ueneaji wa metali katika bonde la Nili na kutokoa kwa vikundi vya kwanza vya kijamii ulianza katika kipindi cha tangu - 5000 hadi - 3000. Hii ilikuwa hatua muhimu lakini isichukuliwe kuwa inawakilisha mtengano wa ghafla baina ya wakati wa sasa na wa kale. Mabadiliko haya yalifanyika hatua kwa hatua katika wakati ambapo sifa za pekee za Neolithi na 'Enzi ya Metali' zilifungamana pamoja: zana zilizotumiwa, pamoja na sifa nyingi za jamii, zinadhihirisha kuwa mfalme wa kwanza wa nasaba ya Kithebe alikuwa mrithi halali wa machifu wa mwisho wa mbari za enzi za Neolithi.

### *Bonde la Nili ya chini*

Muundo wa kijamii ulioanzishwa tangu kikwi cha tatu na kuendelea, ulitokana na maendeleo ya bonde yaliyoletwa na umwagiliaji maji, mbinu ambayo ilianzishwa katika enzi ya Neolithi. Kuna mifano michache ambapo jiografia imekuwa mkunga halisi wa historia kama ilivyodhihirika katika kanda hii ya Nili hasa katika kipindi hiki tunachokizungumza. Kama Herodotus alivyosema: 'Misri ni zawadi ya Nili'. Iwapo maji ya Mto Nili yasingalikuwa yanasambaa katika eneo hilo kila mwaka, utanukaji wa jangwa la Libya kwa upande wa magharibi na jangwa la Negev kwa upande wa mashariki usingaliweza kuzuiwa na ukanda wa kijani ulio mbele ya bonde.

Hata hivyo, ili mafuriko ya kila mwaka yasilete maafa makubwa, ilibidi yadhitiwe kwa kuyajengea maboma yaliyo sambamba na yanayosulubiana na mto ili kufanya mabwawa ya kuzuia maji na kuyapeleka mbele zaidi.

Mfumo huu, ambao ulikuwa na maana ya kuwepo na makubaliano baina ya watu walioishi masafa marefu kandokando ya mto, ulihitaji muundo changamano na madhubuti wa kijamii. Maji yalipokuwa kidogo au iwapo mengi zaidi yalizuliwa huko juu, watu waishio sehemu za chini ya mto waliathirika sana. Huu ulikuwa mwanzo wa kuundwa kwa vikundi vya watu katika majimbo na baadaye kuungana kwao katika maeneo makuu mawili kaskazini na kusini na liatimaye kuunganika kwa falme hizi mbili na kuunda Misri ya Kifarao. Maendeleo haya ya kihistoria yalilingana na mahitaji makubwa ya kudhibiti Mto Nili. Msingi wa kutokea kwa kipindi cha historia katika Misri toka kale mashuhuri ya enzi za Neolithi ya Kiafrika zaidi ulikuwa kazi kubwa iliyofanywa na wakulima wa kawaida kudhibiti na kueneza manufaa ya mto kuliko kuanza kwa matumizi ya metali. Kwa hiyo jambo hili lilisababisha kuwe na haja ya kuwa na udhibiti wa kijamii na kisiasa katika sehemu kubwa ya bonde.

## Enzi za Neolithi

Sura ya 25 ya juzuu hili inaeleza kwa urefu sifa dhahiri za tamaduni mbalimbali za Kineolithi. Kusudi la sura hii ni kuonyesha maendeleo ya kijamii na kisiasa yaliyoandamana nazo. Kwa hakika hapakuwa na utengano katika mfululizo kati ya kipindi cha Neolithi na kile cha kabla ya ufalme. Mathalani; kipindi cha Badari, kilichochanganuliwa kwa urefu katika sura ya 25, ni hatua moja tu katika maendeleo ya utamaduni ulioanza tangu kipindi cha Tasa na kumalizika katika kipindi cha Nagada II na jamii zilizotangulia kipindi cha Thini.

Kwa bahati mbaya, kipindi cha Neolithi katika Misri kinafahamika tu kutoka maeneo machache ambayo mara nyingi hata hayakuwa ya wakati mmoja. Enco la kale kabisa linalojulikana liko katika Misri ya Kati, magharibi ya mto huko Fayum. Hata hivyo, yapo maeneo mengine huko Merimde-Beni-Salame katika delta ya Magharibi na katika Misri ya Kati na ya Juu huko Deir Tasa karibu na Asyut na katika kanda ya Thebe. Ukweli ni kwamba, tangu mwaka - 4000 hadi - 3300 yaani kwa muda wa karne saba hivi, hatujui lolote juu ya mabadiliko katika Neolithi ya Kimisri. Pia ni ukweli kuwa mwishoni mwa kikwi cha sita kulikuwepo na kituo katika mwendeleo wa ukaukaji huko Afrika ya kaskazini-mashariki kama matokeo ya awamu ya mwisho ya mvua nyingi iliyoitwa 'kipindi cha pumziko la unyevunyevu'.

Kutokujua mambo mengi kuhusu maeneo ya sehemu za mashariki ya delta hadi Memfisi, kunatufanya tusiweze kuikubali nadharia tete kwamba asili ya Neolithi ya Kimisri ilikuwa Mesopotamia na Palestina. Kwa upande mwingine, kuna ushahidi wa kuaminika zaidi wa kuwepo kwa uhusiano baina ya Neolithi ya Misri na Neolithi ya awali ya Sahara na Sudani kama ilivyodhihirika katika enco la Amekni huko Ahaggar. Inazidi kudhihirika kuwa Neolithi ya Sahara ilitokea mapema zaidi. Mathalani, ufinyanzi ulianza mapema zaidi huko Nubia kuliko Misri. Hata hivyo, lazima ikumbukwe kuwa delta ya Misri daima ilikuwa ikiunganishwa na kitovu cha taathira mbalimbali.

Lakini, mara Neolithi ilipotokea katika bonde la Nili ya chini, tamaduni za kaskazini na kusini mwa kanda hiyo zilianza kuachana. Huko kaskazini, nyumba zilisongamana zaidi na wafu walizikwa katika nyua za vijiji, ilithali huko kusini, nyumba zilikuwa zimesambaa zaidi na zilijengwa kikaya na makaburi yalikuwa ukingoni mwa jangwa. Katika shughuli za kifundi, watu wa kaskazini walikuwa stadi zaidi katika utengenezaji wa vitu vya mawe hasa katika



utengenezaji wa magudulia ya mawe, ambayo yalifanana kabisa na nakshi za Kifarao, ambapo huko kusini ufinyanzi ulishitadi zaidi. Kwa hiyo sifa bainifu za kitamaduni zinajitokeza ambazo hutofautisha kanda ya Memphis-Fayun na ncha ya kaskazini-magharibi ya delta huko kaskazini kuanzia eneo kati ya Asyut na Thebe katika Misri ya Kati na ya Juu huko kusini. Tofauti hizi ziliashiria kipindi kilichotangulia punde tu kabla ya Mafarao.

### Kipindi cha kabla ya Ufalme

Yafaa kusisitiza kuwa kuanza kwa matumizi ya metali katika kipindi hiki halikuwa tukio la kushangaza lililoleta mgawanyiko kamili kati ya kipindi hiki na vipindi vilivyotangulia. Kipindi cha mabadiliko kutoka matumizi ya mawe hadi matumizi ya metali kilitokea polepole sana na kilichukuwa muda mrefu. Wakati mwingine mabadiliko layo yalikuwenda kinyume; mathalani, shaba ilivumbuliwa kabla ya dhahabu, kwanza katika kundi la kusini kwenye eneo la Badari, na baadaye huko Fayum.

Kuna maoni tofauti kuhusu mahali teknolojia hii ilipotokea. Baadhi ya maoni hudai kuwa teknolojia hii tu ilitokea ng'ambo, hasa Mashariki ya Karibu. Huenda ilivumbuliwa katika maeneo yote mawili kwa wakati mmoja. Kwa vyovyote vile ni katika kipindi hichohicho ambapo watu wa Badari walivumbua enameli ya bluu au 'towe ya Misri' ambayo ndiyo ilikuwa chanzo cha utengenezaji wa shanga. Enameli ilitengenezwa kwa kuchoma malakite, aina ya mtapo wa shaba uhotumiwa kuremba macho. Hata hivyo, zana za mawe ziliendelea kutumiwa zaidi.

### Awamu ya Awali ya Kipindi cha Kabla ya Ufalme

Kipindi kilichotangulia ufalme, kiasi cha miaka -4000 hadi -3000 kinaweza kugawanywa katika awamu nne. Awamu hii, inawakilishwa na enzi ya Badari ya Fayum, enzi ya Badari ikiwa bado inafanana na Neolithi ya Tasia kama ilivyoonekana katika eneo la Deir Tasa. Vibanda bado ni vya umbo la yai, ingawa samani zake ni bora zaidi, zikijumuisha mkeka, mito ya ngozi na vitanda vya mbao. Kutokana na vifaa vya kila siku, magudulia na vyakula vilivyopatikana miongoni mwa vitu vilivyowekwa makaburini, inaonekana kuwa madhehebu ya wafu yalikuwa yanaanza kustawi. Kitani kilicholimwa, pamoja na ngozi, vilitumiwa kutengeneza nguo. Hali hii inadhahirisha kuwepo kwa uchumi mchanganyiko uliotegemea uwindaji kama ilivyokuwa hapo kale, lakini ambao ulikwishachanganya kilimo na ufugaji. Sifa zinazobainisha utamaduni huu ni pamoja na vyombo vyekundu vya ufinyanzi vikiwa na rangi nyeusi katika kingo zake, shanga za bluu zinazong'aa, vifaa vya urembo vya wanawake na chanuo za penibe za ndovu zilizochongwa kwa ustadi.

Enzi ya Fayum ni maarufu kwa matumizi yake ya flinti kuliko metali, na kwa utengenezaji wa magudulia ya kupendeza sana ya mawe meusi.

Katika kipindi hiki, inaonekana kuwa makundi ya watu wa kusini na kaskazini yaliishi katika jamii iliyokuwa na usawa ambamo hakukuwa na upendeleo uliotolewa kwa kuzingatia jinsi au umri wa watu.

### Awamu ya Kale ya Kipindi cha Kabla ya Ufalme

Awamu hii, ambayo pia inajulikana kama Amrati, kutokana na eneo la El Amrah karibu na Abydos, ipo sehemu za kusini zaidi kuliko ile ya Badari. Hata hivyo, awamu hii ni tawi la awamu iliyotangulia, kama inavyodhahirishwa na ufinyanzi wake unaonyesha ubunifu mkubwa wa umbo na nakshi za kijionetri za kiasili katika utengenezaji vifaa. Vijisanamu vya

wanaume wenye ndevu wakivaa nyuo za dhakari na wanawake wakicheza, pamoja na wanyama mbalimbali, pia vilianza kuonekana. Sifa moja ya kuvutia ya Amrati ilikuwa utumiaji wa rungu za mawe zenye umbo la pia iliyokatwa. Ingawa aina hii ya rungu ilitoweka kabisa baadaye, inaonekana kama alama mojawapo katika maandiko-picba, jambo ambalo linaashiria kwamba mtindo huu wa maandishi ulianza kutokeza katika kipindi hiki. Zaidi ya bayo, inaonekana kuwa ulikuwepo uhusiano fulani baina ya Amrati na eneo la delta, kwani magudulia ya mawe kutoka katika eneo hili yamepatikana sehemu ya kusini pia. Hali kadhalika, inaonekana kuwa hapakuwa na tofauti kubwa kati ya tabaka mbalimbali za kijamii.

#### *Awamu ya Kati ya Kipindi cha Kabla ya Ufalme*

Awamu hii ambayo inajulikana kama awamu ya Gerze kutokana na eneo la Gerzeh katika Misri ya Chini, inaonekana dhahiri zaidi upande wa kaskazini kuliko kusini ambako imechanganyika na sifa za Kiamrati. Sehemu ya kaskazini, vyombo vya ufinyanzi vilivyopo ni pamoja na magudulia ya rangi ya kahawia yaliyopambwa kwa mandhari za asili za milima, ndege au mashua, na vilevile magudulia ya mawe magumu zaidi kama vile basanti na dioriti. Aina ya silaha ya Gerze ilikuwa rungu yenye kichwa chenye umbo la yai. Desturi za mazishi zilikuwa changamano zaidi; maiti walizikwa katika makaburi ya mstatili, vichwa vyao vikielekea kaskazini na nyuso zilielekezwa mashariki badala ya magharibi.

Michoro ya mashua kwenye vyombo vya ufinyanzi inaonyesha beramu ambazo huenda zinawakilisha bendera za vikundi mbalimbali vya watu. Kulikuwa na ongezeko la zana na silaha za metali kama vile patasi, shoka, chusa na majambia. Vyombo walivyovikwa maiti vilikuwa ni pamoja na vitu vya dhahabu na mawe ya thamani ndogo. Majina ya baadhi ya miungu wa jadi wa Kimisri kama 'Horus Kipanga' na 'Hathor Ng'ombe' zilianza kuonekana.

Kwa hivyo, jamii inaonekana kuwa ilianza kuwa changamano zaidi na kuwa na makundi makubwa zaidi. Kutokana na hali hii, tamaduni za kaskazini na kusini zilizidi kuongana.

#### *Awamu ya Nyuma ya Kipindi cha Kabla ya Ufalme*

Hali ya kuongana iliendelea zaidi katika awamu ya nyuma ya kipindi kabla ya ufalme, au awamu ya Gerze ya nyuma, wakati utamaduni wao ulipotawaliwa zaidi na kuabudu Mungu Kipanga, ilihali hapo awali, wakazi wa kusini walikuwa wakimtukuza Mungu Seth, ambaye pia alijulikana kama mbwa mwitu ama twiga. Maelezo kuhusu ushindani baina ya miungu hawa wawili lazima yafasiriwe kuwa yanaakisi mgongano baina ya mashirikisho haya mawili mabayo tayari yalikuwa yameimarisha utaratibu wa kimuundo, yakiwa na machifu waliokuwa na uwezo mkubwa ambao umetokana na sihiri lakini ambao waliweza kuuua na raia wao pindi uwezo wao wa sihiri ulipoanza kufiia. Inafikiriwa kuwa katika hatua za mwanzo, upande wa kaskazini ulipata nguvu zaidi na kuliunganisha bonde, kazi ambayo inafikiriwa kuwa huenda ilifanyika wakati wa himaya ya Heliopolis, jambo ambalo lingesaidia kueleza kuenea kwa athari ya Gerze katika enzi ya Amrati ya Kati ya kipindi kabla ya ufalme.

Hata hivyo, wakati wa awamu ya nyuma ya kipindi kabla ya ufalme, miji mikuu ya kanda hizo mbili ilihamishiwa kaskazini zaidi na kusini zaidi, jambo ambalo linaonyesha hali ya mgongano baina yao. Na hapa pia miungu ambao waliabudiwa katika kipindi chote cha Mafarao walianza kutokea: mungu swda alikuwa kaskazini na tai jike kusini. Hata hivyo, kuabudu miungu kama vile Horus kulienea zaidi, ilhali wasanii walipendelea zaidi kutumia umbo la binadamu katika usanii wao. Wakazi wa Hierakonpolis, uliokuwa mji mkuu wa kusini, walianzisha mapambano dhidi ya wakazi wa kaskazini yapata miaka - 3000, na waliposhinda vita hivi waliziunganisha falme hizo mbili na bonde lote chini ya mamlaka ya

wafalme wa kusini kutoka eneo la This, karibu na Abydos, jina ambalo lilizaa jina la *Thini* linalotumiwa kumaanisha falme mbili za kwanza za Kifarao.

Kipindi kabla ya Thini, katika Awamu ya Nyuma ya Kipindi cha Kabla ya Ufalme, kimebainishwa huko Hierakonpolis kwa vitu kama, vifaa vikubwa vya kujiremba, pamoja na vichwa vikubwa vya rungu vya mawe ya chokaa. Kila kundi lilimthamini mungu wao na likiendesha shughuli zake katika majimbo au *nomes*, kila moja likiwa na nembo yake ya pekee iliyochukuliwa na mfalme wakati wa sherehe.

Utaratibu wa kuipanga jamii katika madaraja ambao ulikitwa katika inisingi ya uchumi na dini na baadaye kidogo katika misingi ya jeshi na utawala uliashiria ujaji wa kipindi cha historia. Kutokana na usuli huo uunganishaji wa bonde ulikuwa hatua ya kisiasa yenye dhamera na matokeo ya kiuchumi.

### Bonde la Nili ya Juu

Katika eneo la kusini mwa El Kab, makundi ya watu yalitofautiana na yale ya ukanda wa kati wa bonde. Hata hivyo, kadiri tunavyoihama Aswan na kuelekea kwenye maziwa makuu, habari juu ya watu hawa zinazidi kuwa chache. Kuna kumbukumbu chache za kiakiolojia zinazotuwzesha kupima mabadiliko katika ukanda huu mpana ambao umuhimu wake hauna budi utambulikane vilivyo.

### Utamaduni wa Neolithi ya Khartoum (- 5000 hadi - 3800)

Utamaduni huu pia unajulikana kama utamaduni wa Shaheinab, kutokana na jina la eneo kubwa la Es-Shaheinab. Katika eneo hili na lile la awali la Khartoum vifaa vingi vinavyohusiana na watu waliokuwa wawindaji na wavuvi vimegunduliwa, ikiwa ni pamoja na mashoka, rungu zilizotangulia zile za aina ya Amrati, zana za miti, nguo na ngozi. Ufinyanzi katika kanda hii unaonyesha kuwa utamaduni wa Shaheinab ulienca sana, kutoka *Blue Nile* katika upande wa mashariki na *White Nile* kwa upande wa kusini hadi Tibesti katika upande wa magharibi.

Hata hivyo, huko Abka, katika usawa wa Maporomoko ya Pili, umepatikana ushahidi wa tasnia za mawe na vyombo vya ufinyanzi ambao zinaonyesha kuwa kulikuwepo wawindaji na wavuvi walioishi katika mazingira yaliyokuwa kame na walijenga madema makubwa kwenye mifereji ya kudumu ili kuwazuia samaki wasipite na maji ya maporomoko. Ujenzi huu unaonyesha bayana kuwa jamii ilikuwa imepiga hatua kubwa katika mfumo wa maisha yake. Haifahariki vema juu ya uhusiano uliokuwepo baina ya Neolithi ya Abka na ya Khartoum, lakini hapana shaka kuwa ndiyo iliyoitangulia enzi ya Unubi ya kipindi cha kabla ya ufalme.

### Enzi ya Nubia ya Kipindi cha Kabla ya Ufalme (- 3800 hadi - 2800)

Ushahidi ulio katika hatua za awali zaidi za ufalme huu zilizodhihirishwa na kundi A la mwanzo hadi kufikia -3200, umeonyesha kuwa huko Nubia ya Sudani kulikuwepo kilimo na ufugaji, mambo ambayo hayakufahamika huko Abka, na kwamba mfumo wa ujenzi wa mabwawa ulitumika ili kuzuia mtiririko wa maji na hivyo kuongeza tope laini ambalo lilirutubisha ardhi. Mifupa ya ng'ombe na mbuzi iliyopatikana katika makaburi ni ushahidi kuwa watu hao walikuwa nusu - wanomadi, jambo ambalo linaeleweka, tukizingatia hali ya mapululu katika eneo hilo.

Kugunduliwa kwa zana za kupri kama vile sindano zilizotengenezwa kwa mbinu za Kibadari kunazua suala la usambazaji wa metali hii katika bonde la Nili ya Juu. Hata hivyo, kwa vile kulikuwa na mashapo ya mtapo wa kupri huko Unubi iliyokuwa ikichimbwa tangu kale, kuna kila sababu ya kutufanya tuamini kuwa ufuaji-metali huu ulianzishwa na wenyeji wa eneo hilo.

Mbinu za ufinyanzi zilikuwa za hali ya juu na ni magudulia ya mawe tu yaliyotengenezwa kwa alabasta na sleti ambayo yanaonekana yalitokea kaskazini.

Katika awamu iliyofuata, ile ya Kundi Rasimi A, watafiti wameshangazwa na mambo mawili: Kwanza ni kile tuwezacho kukiita mfuiko wa watu kama ilivyodhihirishwa na idadi kubwa ya makaburi. Pili, ni uagizaji bidhaa kwa wingi kutoka bonde la Nili ya Chini, jambo ambalo linaashiria kuwa biashara iliongezeka sana baina ya Misri ya Juu na ya Chini na kuwa pembe za ndovu kutoka kusini zilibadilishwa kwa mafuta kutoka kaskazini.

Baadaye katika hatua ya tatu, utamaduni huu wa mchanganyiko na ustaarabu ukaharibika, jambo ambalo pengine linaakisi ukoloni wa kinyama ulioingizwa katika eneo hilo na ufalme wa kaskazini.

### *Kipindi cha historia kuanzia mwaka - 3000 hadi karne tano kabla ya enzi ya Ukristo*

#### Maendeleo ya mifumo ya kijamii

Kutokana na uchiache wa nyaraka, maandishi ya Herodotus na Strabo juu ya kuwepo kwa makundi – awali au matabaka ya makubani, watunwa n.k. yasililiwe maanani sana. Ama kwa hakika mfumo wa kijamii wa Misri uliweza kugeuka kwa urahisi na ulikitwa zaidi katika utumiaji wa ardhi kuliko kwenye haki za watu binafsi. Kutokuwepo kwa fedha kulimaanisha kuwa watu hawa walithamini zaidi bidhaa walizopewa badala yake kama chakula, mavazi na nyumba, vitu ambavyo mtu alivipata kwa kuwa mmoja wa kundi fulani la kijamii ama familia ambayo ilipewa haki ya kulima shamba ambalo hatimaye lilimilikiwa na Farao au kikundi kilichoishi kwenye shamba la mfumo wa kidini au la mfalme.

Ujira wa mtu ulitegemea hadhi yake. Kwa mfano, waandishi walilipwa ujira mkubwa zaidi kuliko wakulima au wasanii, na hali hii iliwawezesha waliopendelewa katika jamii kupanua maashamba yao wenyewe. Njia pekee ya kuepuka mfumo huu ilikuwa kukimbilia jangwani. Mkuu wa himaya hizi alikuwa Farao ambaye ndiye aliyekuwa na mamlaka yote. Kutoka mwaka -1580 na kuendelea, askari walioajiriwa na Farao ili kuwafukuza Wahikso kutoka katika bonde, taratibu waliunda jeshi stadi ambalo maofisa wake walizawadiwa ardhi kubwa ambayo waliweza kuwaachia warithi wao. Mpaka kufikia mwisho wa kipindi hiki, hali hii ilisababisha kuundwa kwa tabaka – awali la wanajeshi.

Katika bonde la Nili ya Juu mfungamano wa kijamii ulikuwa na mshiksmano mdogo kwani ulijumuisha jamii zenye makazi ya kudumu na za wafugaji walioliamabama.

#### Usambazaji wa metali

Matumizi ya kupri pamoja na dhahabu na fedha na mbinu za ufuaji wake yalianza mwanzoni mwa kipindi cha historia. Shaba nyeusi, ambayo ni mchanganyiko wa kupri na bati, ilianza

kutumiwa katika kikwi cha pili, lakini hakuna uhakika juu ya kuwepo kwa ufuaji chuma wakati huo.<sup>1</sup>


Dhahabu kutoka migodi ya Misri na Nubia ilichanganyika na madini mengi ya fedha, na hii ndiyo sababu ya kutofautisha baina ya dhahabu nyeupe, yaani dhahabu iliyochanganyika na fedha, na dhahabu ya manjano, ambayo ilitwa *nub*.

Dhahabu iliyoibwa katika makaburi katika maelfu ya miaka ilitumiwa kwa kufujwa katika delta ya Nili na Misri ya Juu kwa ajili ya kupamba mazishi, mapambo binafsi, mapambo ya majengo na kadhalika.

Ingawa shaba nyeusi ni madhubuti zaidi kuliko kupri na ni rahisi kuyeyushwa, kamwe haikuchukua nafasi ya kupri ambayo inaweza kufanywa ngumu kwa kuipondaponda kwa nyundo. Kupri hii ilitumiwa kutengenezca vifaa vya mapambo (hasa vioo), silaha, zana, magudulia, vyombo vya mapambo, nakshi za samani.

Karibu, vitu vyote vya aina hii vilipatikana katika eneo la Kerma, Misri ya Juu. Vitu hivi vinadhihirisha kuwa eneo hili lilitoa mchango mkubwa katika usambazaji wa ufuaji chuma na kupri katika bonde la Nili na Afrika yote, hasa kuanzia falme za Napata na Meroe.

1 Tazama Juzuu la II.



## *Hitimisho: tokea mwanzo kabla ya ustaarabu hadi binadamu aliyejikomboa*

Sura zilizotangulia zinaonyesha wazi mchango mkubwa ambao Afrika ilitoa katika hatua za mwanzo katika hadithi ya mwanadamu. Ingawa mabara ya Afrika na Asia sasa yanahesabiwa kuwa nyuma sana yakilinganishwa na ulimwengu ulioendelea kiteknolojia, mabara haya yalikuwa katika mstari wa mbele wa maendeleo kwa miaka milioni na nusu ya kwanza ya historia ya ulimwengu, kuanzia wakati wa *Australopitheko* na *Pithekanthropo*. Kama tunavyojua sasa, Afrika ndipo mwanadamu alipoanzia kujitokeza kuwa spishi inayotawala sayari yetu na ndipo maendeleo ya siasa ya kijamii yalipoanzia. Lakini mchango mkubwa ambao Afrika ilitoa katika kipindi kabla ya historia ulifuatiwa, katika kipindi cha historia cha miaka 2000 iliyopita, na ruwaza ya maendeleo iliyodhihirishwa na unyonyaji na ambayo ililifanya bara zima libakie tu kuwa chombo cha kutumiwa na wengine.

### *Afrika, asili ya Mwanadamu*

Ingawa uchunguzi wa kiakiojia katika Afrika bado haujafika mbali sana, lakini ushuhuda wote uliopo sasa unaashiria kuwa bara hili ndilo lililokuwa kitovu cha kwanza na muhimu cha maendeleo ya mwanadamu. Hii ilikwibadhihirika miaka milioni 14 iliyopita, wakati wa Kenyapitheko - ambao aelekea kuwa chanzo cha spishi yetu. Lakini hakuna shaka kwamba Australopitheko (*Australopithecus africanus*) ndiye hominidi wa kwanza ambaye anaweza kuainishwa hivyo kutokana na muundo wa ubongo wake. Australopitheko alifuatiwa na *Zinjanthropi* - kutokana na neno *Zinj* au Afrika Mashariki - ambaye ndiye mhenga aliyezaa binadamu wa Ico. Baada ya huyo alifuata *Paleanthropi* au homo erekto na hatimaye homo sapi ambaye maumbile yake katika kilele cha enzi zake, hata katika Ulaya, mara nyingi yalikuwa ya Kinegro. Ndiyo kusoma uhusiano wote unaotunasibisha na hominidi wa kwanza na viumbe wa aina hiyo waliotangulia unapatikana Afrika. Kwa mujibu wa maelezo ya W.W. Howells jamii ya manyani wa Afrika, masokwe mtu na masokwe, inahusiana zaidi na binadamu kuliko na orangutang (aina ya manyani) wa Indonesia.

Sababu ya upendeleo huu wa maendeleo ni kwamba sehemu kubwa ya Afrika imetanda sana kusini katika latitudo za tropiki na za chini zaidi. Wakati mwanadamu alipoanza kutokeza, bara la Afrika lilikuwa na tabia ya hali ya nchi ya wastani ambayo iliwezesha kuongezeka kwa idadi ya wanyama. Aidha wakati wa miaka takribani 200 000 ya kipindi cha mvua nyingi ya

Kagera, tasnia ya zana za mawe ilikuwa inaendelea kusonga mbele katika Afrika wakati ambapo Ulaya ilikuwa bado imefunikwa na maki kubwa ya barafu na haijaweza hata kidogo kuonyesha dalili za kuwoko kwa mwanadamu wakati huo.

### Kujinasibisha na Mazingira

Maumbo ya Waafrika, ikiwa ni pamoja na ngozi zao za maji ya kunde zinazong'aa au nyeusi na zisizo na nywele, pua pana na midomo minene, yalitokea katika kipindi hiki muhimu cha kabla ya historia. Ama kwa hakika weusi wa ngozi yao na nywele za msokoto viliwakinga kutokana na jua. Kwa maoni ya baadhi ya waandishi, umbo la wima ambalo hominidi wa kwanza walilipata taratibu kutokana na kuendelea kubadilika kwa mifupa ya nyonga lilitokana na namna walivyoishi katika nyika za Afrika ambako mara kwa mara walilazimika kuinuka kuehungulia juu ya nyasi ndefu wakati wa kunyemelea mawindo yao au walipokuwa wakiwakimbia maadui wao. Lakini wanazuoni wengine wanafikiri kwamba maji ya maziwa makubwa na bahari kuu vina nafasi kubwa katika kuelezea vyanzo vya maisha, kutokea kwa hominidi na kutokea kwa sehemu za uzazi za mwanadamu.

Utundu wa mwanadamu wa kuvumbua mambo kutokana na vitu vilivyo katika mazingira yake pia hueleza mtindo na aina ya baadhi ya zana.

### Mazingira ya kiteknolojia

Mbali na mazingira ya kiasili, mazingira ya kiteknolojia yaliyoundwa na mwanadamu yalimwezesha kudhibiti maumbile ya asili baada ya kujiondoa katika kutawaliwa nayo. Kwa hakika uwezo wa kiakili wa mwanadamu uliendelea kuongezeka kwa kadri alivyoendelea kuzalisha vitu. Baada ya mikono yake kuwa huru kufanya kazi ambazo hapo awali zilikuwa ngumu, na ambazo yeye tu ndiye mwenye uwezo wa kuzifanya, taya zake hazikuhitajika tena kufanya kazi ambazo zilimweka katika kundi moja na wanyama wengine; ubongo wake pia ukaanza kukua. Akajifunza kuchunguza, kufanya uamuzi, kuelewa na kutafuta sababu. Mwanadamu amepewa uwezo wa kiakili kwa sababu ana mikono miwili.

Kwa mfano, tunapozichunguza karakana za zana za mawe zilizogunduliwa ardhini kama zile zilizoko katika eneo la Kinsbasa na kuona hatua mbalimbali zilizopitiwa katika utengenezaji wa zana, pamoja na mfululizo mzima wa zile zilizohesabiwa kuwa mbovu, tunaona kwamba mafundi wa kipindi kabla ya historia walikuwa na picua kamili ya vitu walivyotaka kutengeneza na mbinu zilizohitajika ili kufikia lengo lao. Maendeleo ya mwanzo ya mwanadamu yanadhahirishwa na kuongezeka huku kwa uwezo katika kutafuta njia bora zaidi za kufikia malengo mbalimbali. Hii ndiyo maana badala ya lile shoka la mkono la zama za kale na lililutumika kwa kazi mbalimbali kukatoka tasnia ya ujeja. Na baadaye kukatoka zana nyepesi zaidi na zenye maumbo bora zaidi na zilizotumika kwa kazi maalumu; hii ilikuwa kabla ya wakati wa Neolithi ambapo zana zilitengenezwa kwa makini zaidi kutokana na vitu mbalimbali kama vile mawe, mifupa, pembe, ngozi, miyaa, miti, udongo, n.k. Hata hivyo, ruwaza hii ya utengenezaji zana haiwezi kugawanywa kwa mipaka ya wazi kama sura za kitabu: utaratibu mzima ulisonga mbele polepole kila hatua ikiisha bila kuonekana na kuingiliana na hatua iliyofuata. Kwa hakika zana za nyakati tofauti ziliendelea kutumika pamoja kwa vipindi virefu sana. Kwa mfano tasnia ya Sango, ambayo ilipewa jina hilo kutokana na Sango Bay katika Ziwa Viktoria, ilianza katika Enzi ya Mwanzo ya Mawe na ikaendelea kuwepo mpaka Enzi za Neolithi.

Sifa nyingine iliyojitokeza katika utaratibu huo wa mabadiliko ilikuwa ni wingi wa mabadilishano na uigaji wa mambo toka kwa watu wengine. Matokeo yake yalikuwa ni

maendeleo ya mbinu za kilimo, ufugaji na ufinyanzi.

Mazao mbalimbali yalilimwa na kupatikana Afrika, kama ngano, shayiri, nyuzi za kufumia nguo kama vile kitani cha Fayum, aina mbalimbali za mtama, aina mbalimbali za mpunga, ufuta na *fonio*, na kusini zaidi kulikuwa na viazi vikuu, *dâ*, michikichi, kola, pengine aina fulani ya pamba, kahawa na mazao mengineyo yalipandwa na watu katika Afrika.<sup>1</sup> Kuanzia karibu miaka 6000 kabla ya Kristo vituo vitatu maalumu vya mazao na maendeleo ya kilimo - katika bonde la Nili, sehemu za kati kwenye Mto Niger na Ethiopia - vilianza kupanuka na kueneza athari zake. Vituo hivi viliunganishwa na mabadilishano ya wao kwa wao pamoja na ulimwengu wa mbali hasa kituo cha Mesopotamia, ambacho kilikuwa na ngano, dengu, vitunguu na jamii yote ya kunde, na kituo cha Mashariki ya Mbali ambacho kilikuwa chanzo cha mpunga, ndizi na wanyama wafugwao.

Uvumbuzi huu wa Kineolithi ulikuwa wa kimapinduzi kwa sababu athari zake nzuri juu ya idadi na hulka za watu wa Afrika ziliwashawishi watu kujenga makazi ya kudumu, jambo ambalo ni la kimaendeleo, kwani bila makazi ya kudumu ustaarabu hauwezi kusonga mbele. Kipindi cha Neolithi cha Sahara na Nili kilitokea yapata miaka 3000 kabla ya kipindi cha aina hiyohiyo huko Ulaya. Yaelekea kuwa ufinyanzi uliletwa katika utamaduni wa Kikhartoum wa Sudani na baadaye katika Sahara na Misri kutoka nyanda za juu za Afrika Mashariki. Huu ulikuwa uvumbuzi muhimu sana wa mwanadamu ambao ulisaidia kuongeza kasi katika ulimbikizaji rasilimali wa mwanzo, kama kuenca kwa ufugaji wa ng'ombe kulivyokuwa. Ufinyanzi pia ulichukua nafasi kubwa katika kuendeleza ufundi wa upishi, kitu ambacho kinamtofautisha binadamu na mnyama.

### Mabadiliko katika ubora wa jamii

Lakini mbali na mambo yaliyomwunganisha mwanadamu na maumbile ya asili na vitu alivyozalisha kulikuwa na mabadilishano muhimu zaidi - yale yaliyohusu mahusiano kati ya wanadamu - ambayo yalimwingiza mwanadamu katika matukio yasiyotegemewa, na majukumu ya historia. Ama kwa hakika kipengee cha kijamii kilichukua nafasi kubwa katika migongano iliyotokana na silika ya mwanadamu ya uchokozi ambayo matokeo yake yalikuwa kuwaangamiza wale waliokuwa wanyonge. Inafikiwa kwamba ni kutokana na utaratibu huu homo sapi alipoweza kumwangamiza mtu wa *Neanderthal* katika 'vita vya dunia', ambavyo ni lazima vitakuwa vimeendelea kwa maelfu ya miaka.

Lakini kipengee cha kijamii pia kilitoa mchango wenye manufaa, kwani polepole ubongo wa mwanadamu ulianza kufanya kazi ambazo zilihusiana na ufanyajikazi kwa madhumuni maalum, usemaji na urekebishaji wa tabia ya binafsi katika kundi alilomo.

Mahitajio ya kuwasiliana katika jamii yalikuwa na nafasi muhimu katika uundaji wa lugha ambao ulitokana na ishara za sauti na kelele zilizorithiwa kutoka kwa wanyama waliomzaa mwanadamu na hatimaye yakawa maneno. Uundaji huo wa lugha pia ulitokana na sifa fulani za kianatomia na kimaumbile - kama vile taya ndefu zaidi, ala za koromeo zenye nguvu zaidi na ulimi kushikizwa kwa chini.

Hata hivyo, bila kuwa na mwenzi wa kurudia zile sauti zake mwanadamu angebakia bila lugha. Kwa kuwa lugha humwezesha mtu kuwaathiri watu wengine, imepewa hadhi na nguvu inayojitegemea yenye uwezo wa kuathiri vitu pia. Katika Afrika - na kwa hakika si katika Afrika tu - neno ni sehemu ya uumbaji wa fikra. Aidha, lugha ni chombo cha maendeleo.

<sup>1</sup> *Fonio*: aina ya nafaka laini sana. *Dâ*: mmea wenye majani ya asidi na maua yake hutumiwa katika kupika mchuzi; nyuzi zake pia hutumiwa.



Ndicho chombo kitumiwacho kurithisha maarifa na mapokeo ya urithi wa masimulizi. Pia lugha ni chombo cha kutumilia maarifa ili mwanadamu aondokane na kutawaliwa tu na silika. Kwa kumalizia, kauli ilikuwa ndiyo chanzo cha mamlaka ya kijamii, yaani katika uongozi na madaraka.

### *Kutokea kwa jamii za Kisiasa*

Iwapo *Homo sapi* anaweza kusemekana kuwa mnyama anayetumia siasa, basi ni katika kipindi kabla ya historia ndipo alipoanza kupata sifa hiyo, na mbinu za uzalishaji na mahusiano ya kijamii vilichukua nafasi kubwa sana katika mabadiliko hayo.

### *Maendeleo ya Kiteknelojia*

Waafrica walioishi katika kipindi kabla ya historia walianza kwa kuishi katika makundi ya kuhamahama, kabla ya kuanzisha makundi maalumu, ambayo kwa pamoja yalifanya kazi ambazo zilikuwa za lazima katika kuishi kwao, au ambazo zilifutea ufanisi katika maisha yao, lakini ambazo zisingeweza kufanywa na mtu mmoja peke yake.

Kiunzi chao kilikuwa ni jamii ambayo ndiyo ilikuwa sehemu ya kuwaweka watu pamoja na mahala pa kupumzikia, pa kupatia mahitaji yao na ulinzi, na baadaye ikapata moto ambao kwao watu wote walijikusanya ili kujilinda kutokana na wanyamapori na pia kuondokana na woga wa giza.

Katika bonde la Omo, huko Ethiopia, kumepatikana mawe ambayo yamepangwa makusudi ili kuweka msingi wa vibanda vilivyokaliwa na hominidi wa mwanzo kabisa. Mitindo na mbinu za ujenzi polepole vilizidi kuwa bora na hatimaye kukatokea vijiji vya Kineolithi kama vile vilivyopatikana huko Tichitt Walata, nchini Mauritania. Vijiji hivi vilijengwa juu ya magenge ya milima karibu na schemu za maji; kwa namna hii wakazi wake wakawa wamecupukana na mashambulio ya ghafla na mafuriko ya mito.

Wahenga wetu wa kipindi cha kabla ya historia walikuwa hodari wa kujipanga katika makundi ya kuwinda wanyama; wengine waliwafukuza wanyama hadi juu ya magenge na katika mabonde. Lakini kumwua mnyama, kumkatakata vipande na kubeba nyama kupeleka nyumbani kulihitaji mgawanyo wa kazi. Utaratibu huu ukawa wa kawaida katika nyakati za Neolithi.

Wakati wa Enzi ya Mwanzo ya Mawe, hapakuwa na uchaguzi mkubwa kati ya kukusanya chakula, kuwinda na kuvua. Lakini kuanzia kipindi cha Neolithi na kuendelea, uchaguzi uliongezeka, ukajumuisha kilimo, ufugaji na ufundi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ufundi wa kuchonga mawe, ngozi, miti, pembe na mifupa, ufinyanzi na baadaye kidogo ufuaaji vyuma.

### *Mahusiano ya Kijamii*

Maendeleo ya ubora wa zana walizotumia ndiyo yaliyowawezesha Waafrica kulimbikiza chakula na bidhaa mbalimbali. Kwa kufanya hivyo walijipatia ziada kubwa ambayo iliwafanya baadhi yao waache shughuli za kuzalisha mali na badala yake wawe watoa huduma tu. Mahusiano ya kijamii yakawa ya namna nyingi na yakawa yamecemezwa kwenye kuwapo kwa daraja mbalimbali za kijamii.

Wakati huu pia ndipo jamia (mbari kuu) zilipoanzishwa na kugawanyika kijiografia; ya kwanza kabisa kujitokeza ikawa ni jamia ya Wakhoisani na Mbilikimo. Jamia ya watu warefu wa Kisudani au Wanegro wa Kibantu, watu ambao wanawakilishwa na mtu wa Asselar katika Mali, ilijitokeza baadaye. Kwanza Wanegro walizagaa katika mabara kadhaa, lakini huko

Ulaya ilibidi wapatoke na kupaachia jamia zilizozoea tabia ya hali ya nchi ya huko. Lakini katika Asia walifukuzwa na kurudishwa nyuma hadi nchi ya Wadravidi na Visiwa vya Papua. Kuchanganyika kwa jamia ukingoni mwa bara hili tangu zama za zama ndiko kulikosababisha kuwepo kwa watu wenyewe sura zisizo za Kinegro sana kama vile Wafulani, Waethiopia, Wasomali, Waniloti, Wasonghai na kadhalika.

Halikadhalika, katika kipindi hiki Waafrika walidhihirisha stadi zao za kubuni mambo katika picha za kipindi cha kabla ya historia walizochora kwenye mawe, na sanaa za maumbo walizozitengeneza. Kwa kuwa mtu wa kwanza alitokea katika Afrika, halitakuwa jambo la kushangaza kuona kuwa sanaa ya Kiafrika katika kipindi cha kabla ya historia ni za hali ya juu kuliko sanaa zote ulimwenguni' hasa tukizingatia selemu za Sahara, Mashariki na Kusini mwa Afrika, Misri na nyanda za juu za milima ya Atlas. Ni kweli kwamba sanaa hii inatoa picha ileile ya wingi wa wanyama wa wakati huo, lakini pia ni rekodi za jamii ambazo zinaonyesha maisha ya kila siku ya watu, kazi zao, burdani zao, migongano na maadui wao, mambo waliyoyaogopa, matambiko yao na michezo yao. Kwa ufupi, kazi hizi za sanaa zinaonyesha mageuko ya taratibu katika kuelekea kwenye jamii yenye siasa kama ambavyo ukuhani ulivyoondoka katika uongozi wa watu na badala yake kukawa na utawala wa machifu.

Maendeleo ya nguvu za kuzalisha mali katika wakati wa Neolithi yamkini yalileta ongezeko kubwa katika idadi ya watu, na kusababisha luja ya uhamaji kama inavyoonekana katika 'karakana' za kipindi cha kabla ya historia ambazo zilikuwa katika sehemu zenye maeneo ya umbali wa kutosha kutoka 'karakana' moja hadi nyingine lakini zote zikiwa na aina za zana za mawe zilizohusiana sana. Uhamaji wa aina hii wa watu ulizidi kuonekana kuyamkinika kadiri uzito wa zana ulivyozidi kupungua na ufanisi wake kuongezeka.

Watu daima wamekuwa wakija na kutoka katika maeneo makubwa na ya wazi yaliyotanda Afrika, kutokana ama na kufaulu au kushindwa kukabili mazingira ya nyumbani kwao. Hii ndiyo sababu ya kuwepo sasa kwa ramani za mbari ambazo wakati mwingine zinaonekana kama vipande vidogovidogo vilivyounganishwa. Ushuhuda wote unaonyesha kuwa uhamaji wa mwanzo ulianzishwa na watu walioishi mashariki na kaskazini-mashariki mwa bara la Afrika, ambamo nao walizidi kusonga mbele kuelekea magharibi na kaskazini. Kisha, kuanzia wakati wa Neolithi na kuendelea, uelekeo umekuwa mashariki kuelekea bonde la Nili na pia kusini, labda kwa kuzuiwa na jangwa la Sahara. Uhamaji huu wa jumla kuelekea kusini wa Wasudani, Waniloti na Wabantu, ulifanyika kwa kipindi cha maelfu ya miaka na ukaendelea wakati wa kipindi cha historia hadi karne ya kumi na tisa ambapo ulifikia nyanda za juu za kusini mwa Afrika ambazo zilikwishakaliwa na Wakhoisani tangu mwanzoni kabisa mwa kipindi cha kabla ya historia.

Kwa kulinganisha faida ya kutafuta maisha mazuri na hatari za kutangatanga ovyo, viongozi wa misafara hii ambao miili yao ilijaa hirizi walihesabiwa kuwa mababu wa kundi lao, na kutokana na mtazamo huo watu hawa walikumbukwa kwa muda mrefu na jamii. Hata hivyo matokeo ya mwisho ya uhamaji huu yaweza kusemwa kuwa yana faida na hasara. Mahali ambapo idadi ya watu ni kidogo mazingira ndiyo yanayotawala.

### *Maendeleo ya Kihistoria*

Mojawapo ya mambo ambayo hujitokeza sana katika Afrika ni ulc ukweli kwamba toka zama za kale jamii zinakuwa zikiishi maisha ya namna moja pasi na kuingiliwa na namna nyingine ya maisha. Kwa mfano, hata sasa, tukiwa katikati ya karne ya ishirini, mbinu za uwindaji zinazotumiwa na Mbilikimo ni zilezile zilizotumiwa na mababu zao maelfu ya miaka iliyopita.

Ingawa kulikuwa na maendeleo ya hali ya juu sana yaliyoletwa na ustaarabu wa Misri na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika falme na dola mbalimbali katika Afrika, bado ni dhahiri kwamba namna ya maisha ya Waafrika imebaki vilevile na hii ndiyo sababu jamii za Kiafrika zimeendelea kuwa na uelekeo wa namna moja wa maendeleo.

Historia ya mwanadamu hasa ikoje? Hili ndilo swali ambalo watu wenye busara kama vile akina Marx na Teilhard de Chardin wamekuwa wakijaribu kujibu. Kuanzia wakati wa Mt. Agustino (354- 430), ambaye alikuwa Mwafrika, historia ilipiga hatua kubwa kwenda mbele toka kwenye dhana iliyotangulia ya 'mzunguko' kuelekea kwenye dhana ambayo inaitazama historia ya ulimwengu kama kitu kilicho katika mstari kinachoanzia kwenye Uumbaji hadi kwenye Hukumu ya Mwisho; kuanzia kwenye mji wa kilimwengu hadi kwenye Mji wa Mungu.

Mwafrika mwingine, Ibn Khaldun (1332 - 1406), japo aliamini kuwa maisha ya mwanadamu humtegemea Mungu, hata hivyo aliweka misingi ya historia kuwa sayansi ambayo imekitwa kwenye ushahidi unaohitishwa na hoja za kirazini. Badala ya kuitazama historia kama mlolongo tu wa matukio, alifanya uchanganuzi wa njia mbalimbali za uzalishaji mali na mitindo ya maisha, na uhusiano wa uzalishaji mali kwa jumla - kwa ufupi, ustaarabu (al-umran al-Bashari). Hata alitoa nadharia kamambe ya kuelezea utaratibu uwezeshao historia kusonga mbele.

Alipotoa hoja kwamba tofauti zinazojitokeza katika mila na asasi za watu mbalimbali hutegemea namna watu wanavyojikimu, kwa hakika Ibn Khaldun alikuwa tayari ameanzisha mojawapo ya itikadi za uyakiniifu wa kihistoria ambayo ilielezwa kwa undani na Karl Max kama kadhaa zilizofuatia. Marx alitoa uchanganuzi wenye kina wa ruwaza yote ya maendeleo katika Ulaya Magharibi, halafu baadaye akachunguza taratibu za uzalishaji mali nje ya Ulaya, kama kitu cha pembeni tu. Alibainisha 'utaratibu wa uzalishaji mali wa Kiasia'.

Hata hivyo habari za kiakiolojia na kiantropolojia zilizokwihapatikana tokea wakati wa Marx, zinaashiria kuwa baadhi ya jamii hazikupitia hatua zote ambazo alizihusisha na watu wote kule Ulaya. Kweli hii pia inajitokeza kwa upande wa Waafrika, angalau kulingana na data zilizopo.

Kwa mfano katika jamii za awali za Kiafrika, nafasi ya umilikaji mali kwa pamoja haikuchukuliwa na umilikaji mali binafsi katika namna alivyoona Marx kuhusiana na zama za kale na katika jamii ya kale ya Kijerumani. Hali kadhalika, sifa muhimu za mbinu za uzalishaji mali za Kiasia hazikuweko katika jamii za Kiafrika ambako dola, ambayo ndicho chombo cha mamlaka ya juu kabisa, haikuwa na haki zaidi juu ya ardhi kuliko mtu binafsi. Tena basi jamii zenye dola kama hizo hazikuwa na watawala 'dhalimu' wala hazikuwa zincaanzisha miradi mikubwa ya ujenzi katika jamii. Katika Afrika ya watu weusi, madaraka ya mfalme yalikuwa yakitazamwa kwa makini na vyombo maalumu vilivyochaguliwa kijadi na ambavyo vilijaribu kuepukana na udhalimu. Zaidi ya hayo, utawala wa kufuata mfano wa Kimashariki ulikwazwa kwa sababu maandishi yalikuwa hayajaenea sana, na njia za usafiri hazikuwa nzuri sana. Aidha ziada za uzalishaji za jamii katika Afrika hazikuwa kubwa hata katika dola zilizohodhi bidhaa za thamani kama vile dhahabu katika Ghana na Asante, pembe za ndovu, ehumvi n.k. Yafaa ikumbukwe kwamba sehemu kubwa ya kodi na mirabaha mwingine iliyotozwa iligawanywa tena kwa watu na mamwinyi ambao hawakuuheshimu tu nifumo uliokuwepo wa kumiliki ardhi, lakini pia walikuwa na wajibu juu ya huduma za kawaida kama vile kulinda usalama, haki na utaratibu wa masoko. Tukiacha hali ilivyokuwa hivi karibuni, ni dhahiri kwamba mfumo wa uzalishaji mali kwa kutumia watumwa vilevile ulikuwa na athari ndogo katika maendeleo ya historia ya Afrika.

Kuwa mateka hakukumpunguzia hadhi mtu na kumfanya awe kitu tu (kama neno hili lilivyocoleweka Urumi). Ama kwa hakika mara nyingi watumwa wa Kiafrika walikuwa na kiasi fulani eha haki ya kumiliki mali. Pale ambapo mateka wa vita hawakutolewa kama sadaka katika matambiko, walihesabiwa kuwa schemu ya familia mpaka hapo walipoachiwa huru. Mateka waliposajiliwa katika jeshi walitokea kuwa nguvu kubwa iliyotegemewa, katika jamii na waliwakilishwa katika ngazi za juu za serikali. Katika jitihada za kuhimiza umoja, katika ufalme wa Asante kabla ya ukoloni ilikuwa mwiko kabisa kuzungumzia asili ya utumwa wa mtu fulani. Hii ni kusema kwamba katika Afrika 'kuwa mateka au intumwa hakukuashiria kuwa na nafasi maalumu katika uzalishaji mali ambayo ilionyesha sifa za kitabaka katika jamii'<sup>2</sup> Katika schemu ambazo utumwa ulifanyika kwa wingi na tkawa na sura tofauti, kama ilivyokuwa katika Dahomey, Asante na Zanzibar katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa, miundo ya kijamii ililetwa na ubepari, ambao ndio ulikuwa mfumo wa uzalishaji mali uliotawala sana wakati huo.

Wala haiwi rahisi kupambanua mfumo wa kikabaila wa uzalishaji mali katika Afrika, ambako kwa kawaida hakukuwa na kujitwalia mali au kumiliki ardhi binafsi, yaani hakukuwa na utaratibu wa miliki ya kabaila. Iliyoyo ni kwamba watamalaki mara nyingi waliacha ardhi katika mikono ya viongozi wa asili wa wananchi wenyewe, yaani makuhani wa ardhi, ambao walikuwa tofauti na viongozi wa kisiasa. Hii ndiyo maana tabaka za mamwinyi katika Afrika hazikujishirikisha katika biashara. Umwinyi ulikuwa haki ya kuzaliwa, na hivyo haingewezekana kuhamishwa au kutanguliwa.

Mwisho, siarti pia tuzingatie miundo kama mfumo wa familia unaorithi kukeni ambao kwa muda mrefu umekuwa ni sifa ya jamii za Kiafrika, na ambao kwao wanawake walikuwa na nafasi kubwa katika urithi wa mali na ufalme. Inaelekea udugu wa kufuata mkondo wa mama umekuwepo tangu kipindi kabla ya historia wakati ambapo uelekeo katika makazi ya kudumu katika kipindi cha Neolithi uliitulia mkazo mkubwa katika kazi za akina mama nyumbani kiasi cha kuwafanya wawe ndio watu muhimu katika jamii. Tabia nyingi za kijamii katika Afrika zimetokana na maendeleo haya - kwa mfano 'uhusiano wa utani', kuoana kwa maumbu, mahari (ambayo yanalipwa kwa wazazi wa binti aliyeposwa), n.k.

Nini, basi, kinachoweza kusemwa kuwa ndiyo ruwaza bainifu za maendeleo katika jamii za Kiafrika za kipindi cha kabla ya historia? Hapa yafaa tusisitize kwamba Afrika ya kipindi cha kabla ya historia ilikuwa ndiyo chanzo cha utundu wa kiteknolojia, na kwamba ugunduzi uliotokana nayo ulisambazwa mbali kupitia mabara yanayopakana nayo. Lakini baadaye hali hii ikageuka na kwa muda wa maelfu ya miaka bara hili lilinyang'anywa utajiri wake. Kwanza katika Zama za Kale wakati ambapo, baada ya kuporomoka kwa Misri, bonde la Nili na mikoa ya Rumi katika Afrika Kaskazini vilinyonywa kwa kufanywa kuwa ndio mahala pa kupatia chakula cha Dola ya Rumi na mahali pa kupatia wanyama pori, watumwa na wapiganaji kwa ajili ya jeshi, namwinyi na viwanja vya michezo ya kuua wanyama na kuuana; pili katika karne ya kumi na sita, wakati ambapo walichukuliwa watu wengi sana katika biashara ya utumwa; na mwisho katika karne ya kumi na tisa, ambapo polepole wakoloni walianza kulitawala bara hili. Ulimbikizaji wa rasilimali luko Ulaya na kutokea kwa mapinduzi ya kitasnia visingewezekana bila ya na gharama kubwa iliyolipwa na Asia, Amerika Kaskazini na Kusini na, zaidi ya yote, Afrika.

Wakati huohuo maendeleo katika Afrika yalizuiwa na vikwazo kadhaa vya kijamii na kiteknolojia; vikwazo ambavyo vilisababisha jamii kushindwa kupata nguvu ambazo

2. J. Suret-Canale, 1964.

zingewawezesha ama kulimbikiza mali au kuleta mapinduzi halisi ya kijamii. Zaidi hasa ni kwamba kwa kuwa katika Afrika ni mara chache sana ardhi ilimilikiwa na watu binafsi, bara hili lilinyimwa mojawapo ya viambajengo muhimu sana vyenye kusababisha mgongano wa kitabaka na maendeleo ya kijamii. Halikadhalika kiwango cha chini cha mafanikio ya kiteknolojia na udhaifu wa nguvu za kuzalisha mali vilitokana na ukweli kwamba kulikuwa na watu wachache tu waliotawanyika katika eneo (kubwa) la kuishi lililokuwepo.

Kutokana na viziuzi vya asili vya bara lili, biashara haikufika mbali wala haikufanyika kwa wingi; mara nyingi ilihusu tu bidhaa za anasa kwa ajili ya mamwinyi. Kwa upande mwingine katika sehemu ambako viziuzi hivyo havikuwa vya kutopitika kabisa - bonde la Nili, Sahel, mbuga zinazopakana na Mediterania, nyanda za juu za Shaba, na sehemu yenye maziwa makubwa ya Afrika Mashariki - mabadiliko makubwa yalianza kutokca kadri idadi ya watu ilivyo zidi kuongezeka na kadri watu walivyo zidi kumiliki mali binafsi.

Ndiyo kusema katika Afrika (ya watu weusi) hakukuwahi kutokea hatua ya utumwa au hatua ya ukabaila, kama inavyoeleweka Ulaya. Hata hivyo hii haina maana kwamba maendeleo ya mwanadamu katika Afrika yalikuwa na mwelekeo tofauti na kwingine. Nguvu za uzalishaji mali katika Afrika zilikuwa na athari zilezile juu ya uhusiano wa kijamii kama zilivyokuwa kwingineko; jamii za Kiafrika zilikuwa na kubadilika kama jamii nyingine, kuanzia miundo isiyokuwa na matabaka badi kufikia miundo mbalimbali ya mapambano ya kitabaka katika jamii. Lakini haiwezekani kuilazimisha historia ya Afrika, kwa namna yoyote ile, iingie katika imani zilizotokana na mazingira mengine. Kuitumilia mbinu ya Marx kuna manufaa zaidi kuliko kuamania mawazo na imani yake kama msahafu. Kwa ufupi, kwa muda mrefu zaidi kuliko bara jingine Afrika ilikuwa na kuendelea bila kuwa na umilikaji mali wa binafsi au wa kidola; hali hii ililifanya bara hili lichukue sura ya kipekee katika maendeleo yake.

Dola ya kikoloni na ya kibepari ikawa ndio mtawala wa utajiri wa Afrika - utajiri ambao uliendelea kuchukuliwa na wakoloni kwa manufaa yao na hatimaye kukazaliwa serikali za nchi zilizokuwa ama za kikabaila au za kisoshalisti.

Hata hivyo, ingawa nguvu za uzalishaji mali zilisimama kabisa kutokana na sababu mbalimbali za ndani na nje, maendeleo ya ajabu ya kujieleza kisanaa na ubora katika uhusiano wa binadamu havikuzuliwa.

Kwa ufupi ustaarabu wa vitu yakinifu ulianza katika latitudo za tropiki za Afrika na Asia katika kipindi cha kabla ya historia. Baadaye ukahamia katika latitudo za kaskazini zaidi katika Ulaya ambako kutokana na maendeleo makubwa ya tekuolojia na kujilimbikizia rasilimali matokeo yake yamekuwa makubwa. Ni historia pekee itakayoweza kuamua kama mageuzi ya mfumo huu wa ulimwenguni kote yataanzia kwenye kitivo chake huko Magharibi au yataletwa na watu walio pembezoni mwake kama ambavyo vuvumko la Dola ya Rumi lilivyo zimwa na 'washenzi'. Vyovyote itakavyokuwa, historia ya Afrika ya kipindi cha kabla ya historia ni hadithi inayocheza jinsi kiumbe aliyetokana na spishi ya manyani alivyoendelea kupata mageuko hadi kufikia hali ya mwanadamu, na jinsi mwanadamu kama nguvu iliyo nyuma ya maendeleo yote alivyodhibiti mazingira yake.

Lakini kwa kadiri nguvu za kuzalisha mali zinavyozidi kuwa madhubuti, ndivyo migongano itokanayo na maslahi ya binafsi na kutaka madaraka vinavyozidi kuongezeka. Harakati za kujikomboa kitaifa na kijamii zinazotokca kote katika bara hili zinadhihirisha jinsi Waafrika wanavyokataa kufungwa katika minyororo ya ukoloni iliyokuwepo kwa muda mrefu.

Ni harakati hizi za kujikomboa, kiu hii ya kutamani vitu bora na hamu ya kujiondoa katika

mkengeuko, ambavyo vimewafanya binadamu wajipambanue kutoka wanyama wengine tokea wakati ambapo walianza kusimama wima na kutembea.

Katika Afrika kuzaana kwa binadamu, ambako kulianza maelfu ya milenia zilizopita, bado kunaendelea. Kwa namna fulani historia ya Afrika ya kipindi cha kabla ya historia bado haijafikia ukomo wake.

---



## Bibliografia

---

- Aitken, M.J.** (1961), *Physics and Archaeology* (New York: Interscience Publishers).
- Alimen, H.** (1955), *Prehistoire de l'Afrique* (Paris: Boubee) tr. *The Prehistory of Africa* (London: Hutchinson), 1957.
- Alimen, H.** (1976), 'Variations climatiques dans les zones désertiques de l'Afrique nord-equatoriale durant les quarante millénaires', *Actes VII Congr. PPEQ*, Addis Ababa, kur. 337-47.
- Alimen, H. Chavaillon, J. and Margat, J.** (1965), 'Contribution à la chronologie préhistorique africaine. Essai de corrélation entre les dépôts quaternaires du bassin Guir-Saoura (Sahara) et du bassin du Tafilat (Maroc)', *Congress Préhistorique de France*, Monaco, 1959, kur. 161-267.
- Arambourg, C.** (1949), 'Sur la présence dans le Villafranchien d'Algérie de vestiges éventuels d'industrie humaine', *CRAS*, 229, kur. 66-7.
- Arambourg, C.** (1962), 'Etat actuel des recherches sur le Quaternaire en Afrique du Nord', *Actes IV Congr. PPEQ*, 40, kur. 255-77.
- Ayache, G.** (1961), "Les archives marocaines", *HT*, 2.
- Ba, A.H.** (1972), *Aspects de la civilisation africaine (personne, culture, religion)*. (Paris: Presence africaine).
- Ba, A.H. and Cardaire, M.** (1957), *Tiemo Bokar, le sage de Bandiagara*. (Paris - Presence africaine).
- Ba, A.H. and Daget, J.** (1962), *L'empire peul du Macina au XVIIIe siècle*. (Paris : Mouton).
- Balandier, G.** (1971), *Sociologie actuelle de l'Afrique noire*. (Paris : PUF), chapa ya 3.
- Balandier, G. and Maquet, J.** (1968), *Dictionnaire des civilisations africaines*. (Paris : Hazan).
- Balout, L.** (1955), *Préhistoire de l'Afrique du Nord, essai de chronologie* (Paris : AMG).
- Barry, B.** (1974), La chronologie dans la tradition orale du Waalo. Essai d'interprétation, *Afrika Zamani*, 3, kur. 31-49.
- Bayle des Hermens, R. de** (1967), 'Premier aperçu du Paléolithique inférieur en République Centrafricaine', *Anthropologie*, 71, kur. 135-66.
- Bayle des Hermens, R. de** (1975), Recherches préhistoriques en République Centrafricaine. (Laboratoire d'ethnologie et. de sociologie comparative, Université de Paris, Série Recherches oubanguiennes, Paris, Kilincksieck). na. 3.
- Bebey, F.** (1969), *Musique de l'Afrique*. (Collection Expressions, Horizons de France).
- Berger, R.** (1970), 'Ancient Egyptian Chronology', *PTRS*, 269, 1193, kur. 23-36.
- Berggren, W.A.** (1973), 'Correlation and Calibration of late Pliocene and Pleistocene Marine and Continental Biostratigraphies', *Acts IX INQUA Congr.*
- Bishop, W.W. and Clark, J.D.** (eds) (1967), *Background to Evolution in Africa*

- (Chicago/London : University of Chicago Press).
- Bloch, M.** (1949), *Apologie pour l'histoire ou le Mettier d'historien*. (Paris : Colin).
- Bonnefille, R.** (1972), 'Associations polliniques actuelles et quaternaires Ethiopie (vallees de Awash et de l'Omo)', *Tasnifu*, Juz. 2. (University of Paris).
- Bonnefille, R.** (1976), 'Végétation et climats des temps oldowayens et acheu leens á Melka Kunturé (Ethiopie).' *L'Ethiopie avant l'histoire*, Juz. 1 kur. 55-71.
- Bounak, V.** (1972), 'Du cri au langage', *Le Courrier* (August-September).
- Braudel, F.** (1969), *Ecrits sur l'histoire*. (Paris : Flammarion).
- Brézillon, M.N.** (1969), *Dictionnaire de la préhistoire* (Paris : Larousse).
- Bucha, V.** (1970), 'Evidence for changes in changes in the earth's magnetic field intensity', *PTRS*, 269, pp. 47-55.
- Bucha, V.** (1971), 'Archaeomagnetic dating', in H.N. Michael and E.K. Ralph (eds), *Dating Techniques for the Archaeologist* (Cambridge, Mass : MIT Press), kur. 57 - 117.
- Butzer, K.W., and Hansen, C.L.** (1968), *Desert and River in Nubia; Geomorphology and Prehistoric Environments at the Aswan Reservoir* (Madison : University of Wisconsin Press).
- Butzer, K.W., Richardson, J.L. and Washbourknakamau, C.** (1972), 'Radio-carbon dating of East African Lake Levels', *Science*, 1975, kur. 1069-76.
- Caley, E.R.** (1949), 'Validity of the Specific Gravity Method for the Determination of the Fineness of Gold objects' *OJS*, XLIX, kur.76-92.
- Chamla, M.C.** (1968), 'Les populations anciennes du Sahara et des region limitrophes : etude des restes humains néolithiques et protohistoriques' *MCRAPE*, 9.
- Chamot, E.M. and Mason, C.W.** (1938), *Handbook of Chemical Microscopy*, chapa ya 2 (New York : Wiley/London : Chapman and Hall).
- Clark, J.D.** (1960), *The Prehistory of Southern Africa* (Harmondsworth : Penguin).
- CNRS (ed.)** (1974), 'Les Méthodes Quantitatives d'étude des Variations du Climat au Cours du Pléistocène', *Col. CNRS*, na.219.
- Cooke, H.B.S.** (1958), 'Observations relating to Quaternary environments in East and Southern Africa', *TGSSA*, Appendix to Juz. 61.
- Cooke, H.B.S.** (1972), 'Pleistocene Chronology: Long or Short', *Maritime Sediments*, 8, (1), kur. 1-12.
- Cuoq, J.** (trans.) (1975), *Recueil des Sources Arabes Concernant l'Afrique Occidentale du VIIIe au XVIe Siecle*, Bilad al-Sudan, (Paris : CNRS).
- Cuvelier, J. and Jadin, L.** (1954), *L'Ancien Royaume du Congo d'apres les Archives Romaines 1518-1640*. (Brussels : Academic Royale des Sciences Coloniales).
- Dalby, D.** (1965), 'The Mel Languages: A Reclassification of Southern "West Atlantic"', *ALS*, 6, kur. 1-17.
- Dalby, D.** (1970), *Language and History in Africa* (New York : African Publishing Corporation; London : Cass).
- Davidson, B.** (1965), *Old Africa Rediscovered*. (London: Gollancz).
- Davies, O.** (1967), *West Africa Before the Europeans: Archaeology and Prehistory*. (London: Methuen).
- Davison, C.C.** (1973), 'Glass Beads in African Archaeology', *AATA*, 10,2.
- Deschamps, H.** (ed.), (1970-1), *Histoire General des l'Afrique Noire, de Madagascar et des Archipels*, Juz.2. (Paris: PUF).
- Dimbleby, G.W.** (1963), 'Pollen Analysis"', in D. Brothwell and E. Higgs (eds), *Science in*



- Archaeology*. (London: Thames and Hudson), kur. 139-49.
- Diop, C.A.** (1955), *Nations Nègress et Culture*. (Paris: Presence Africaine).
- Diop, C.A.** (1959), *L'Unité Culturelle de l'Afrique Noire; Domaines du Patriarcat et matriarcat dans l'Antiquité Classique* (Paris: Presence Africaine).
- Dorize, L.** (1974), 'L'Oscillation Pluviométrique récente sur le bassin du lac Tschad et la Circulation atmosphérique Génératrice' *Revue de Géographie Physique et de Géologie Dynamique*, 16, 4, kur. 393-420.
- El-Kettani, M.** (1968), "Les Sections d'archives et de manuscrits des bibliothèques marocaines", *HT*, 9, (3), kur. 459-68.
- Fægri, K. and Iversen, J.** (1950), *Textbook of Modern Pollen Analysis*. (Copenhagen: Munksgard).
- Fage, J.D. and Oliver, R.A.** (eds.) (1970). *Papers in African Prehistory (Journal of African History)*. (Cambridge University Press).
- Farag, N. and Iskander, Z.** (1971). *The Discovery of Nefertiti* (Cairo: Government Printing Office).
- Faure, H.** (1962), 'Reconnaissance géologique de formations sédimentaires Postpaleozoïques du Niger Oriental', *Tasnifu* (University of Paris).
- Faure, H.** (1967), Evolution des grands lacs Sahariens à l'Holocène, *Quaternaria*, 15, kur. 167-75.
- Faure, H.** (1969), 'Lacs quaternaires du Sahara', *Internationale Vereinigung für theoretische und angewandte Limnologie* (Stuttgart), 17, kur. 131-48.
- Faure, H. and Elouard, P.** (1967) 'Schema des variations du niveau de l'océan Atlantique sur la côte de l'Ouest de l'Afrique depuis 40,000 ans' *CRAS*, 265, kur. 784-7.
- Faure, H. and Williams, M.A.J.** (1980), *The Sahara and the Nile*, Rotterdam, A.A. Balkema.
- Flint, R.F.** (1947), *Glacial Geology and the Pleistocene Epoch* (New York: Wiley; London: Chapman and Hall).
- Flint, R.F.** (1959), 'Pleistocene climates in eastern and southern Africa', *BGSA*, 70, kur. 343-74.
- Frobenius, L.** (1952), *Histoire de la civilisation africaine*, trans. H. Back and D. Ermont. (Paris: Gallimard).
- Gabel, C. and Bennet, N.R.** (1967), *Reconstructing African Culture History*. (Boston, Mass: Boston University Press).
- Gardiner, A.H.** (1947), *Ancient Egyptian Onomastica* (London: Oxford University Press).
- Gardiner, A.H.** (1957), *Egyptian Grammar: Being an introduction to the study of hieroglyphs*, chapa ya 3. (London: Oxford University Press).
- Gasse, F.** (1975), 'L'évolution des lacs de l'Afrique Centrale (Ethiopie et TFA) du Plio-Pléistocène à l'Actuel', *Tasnifu*, Juzuu la 3. (Paris: University of Paris).
- Giegengack, R.F.** (1968), 'Late Pleistocene history of the Nile valley in Egyptian Nubia', Ph.D. Dissertation. (New Haven: Yale University).
- Glele-Ahanhanzo, M.** (1974), *Le Danxome, du Pouvoir Aja à la Nation Fon*. (Paris: Nubia).
- Greenberg, J.H.** (1948), 'The Classification of African Languages', *American Anthropologist*, 10.
- Greenberg, J.H.** (1966), *The Languages of Africa* (The Hague: Mouton).
- Griaule, M. and Dieterlen, G.** (1951), 'Signes graphiques soudanais', *L'Homme*.
- Grove, A.T., Street, F.A. and Goudie, A.S.** (1975) 'Former lake levels and climatic change in the rift valley of southern Ethiopia', *GJ*, 141, (2), kur. 177-202.
- Guernier, E.L.** (1952), *L'apport de l'Afrique à la Pensée humaine*. (Paris: Payot).
- Hall, E.T.** (1965), 'Recent research at the Research Laboratory for archaeology and the history of art', *Proceedings of the Seminar on Application of Science in Examinations of Works of Art*,

- Boston, Mass.
- Hall, E.T. (1970), 'Analytical techniques used in archaeometry', PTRS, 269, 1195, kur.135-41.
- Halpern, J.W., Harris, J.E. and Barnes, C. (1971), 'Studying skulls in Egypt' *Research News* XXII, 1. (ann Arbor: University of Michigan).
- Hamilton, E.I. (1965), *Applied Geochronology*. (London/New York: Academic Press), kur. 47-79.
- Harlan, J.R., Wet, J.M. de and Stemler, A.B.L. (eds.) (1976), *Origins of African Plant Domestication*. (Paris/The Hague: Mouton).
- Hayes, W.C. (1964), *Most Ancient Egypt*, cd. K.C. Seele. (Chicago: University of Chicago Press).
- Heinzelin de Braucourt, J. de, Brown, F.E. and Howell, F.C. (1971), 'Plio-Pleistocene formations in the lower Omo Basin (Southern Ethiopia)'. *Quaternaria*.
- Homburger, L. (1930), 'Les dialectes copte et mande', BSL, 3, (1).
- Homburger, L. (1941), *Les langues negro-africaines et les peuples qui les parlent*. (Paris: Payot).
- Houis, M. (1971). *Anthropologie linguistique de l'Afrique noire* (Paris: PUF).
- Huard, P. and Beck, P. (1969), *Tibesti, carrefour de la Préhistoire Saharienne*. (Paris: Arthaud).
- Hugot, H.J. (1974), *Le Sahara avant le désert*. (Paris: Edition des Hesperides).
- Iakmov, V.P. (1972), 'Deux grandes théories sur l'apparition des races', *Le Courrier* (August-September).
- Iskander, A. (1960), 'The scientific study and conservation of the objects and materials found in the discovery of the wooden boat at Giza', *The Cheops Boats*, pt 1 (Cairo: Antiquities Department of Egypt), kur. 29-61.
- Kagame, A. (1969), *Introduction aux grands genres tyriques de l'ancien Rwanda*. (Butare: Editions Universitaires du Rwanda).
- Kesteloot, L. (1978), *Da Monzon de Segou. Epopée Bambara*, Juzuu la 2 (Paris: Nathan).
- Kiwanuka, M.S.H. (1967), 'Some reflections on the role of oral tradition in the writing of the pre-colonial history of Africa', *Acta Africana* VI, (1) kur. 63-74.
- Ki-Zerbo, J. (1964), *Le Monde africain noir histoire et civilisation*. (Paris: Hatier).
- Ki-Zerbo, J. (1969), 'La tradition orale en tant que source pour l'histoire Africaine', *Diogene*, 67, kur. 127-42.
- Ki-Zerbo, J. (1978), *Histoire de l'Afrique noire*, chapa ya 2. (Paris: Hatier).
- Kolhoff, I.M., Sandell, E.B. Meehan, E.J. and Bruckenstein, S. (1969), *Quantitative Chemical Analysis*, chapa ya 4. (New York: MacMillan).
- Kouyaté, N. (1969-70), 'Recherches sur la tradition orale au Mali (Pays Manding)', Mem. de recherche non edite. (Algeria: University of Algeria).
- Kukla, G.J. and Mathews, R.K. (1972), 'When will the present inter-glacial end?', *Science*, 178, kur. 190-1.
- Laroui, A. (1970), *L'Histoire du Maghreb*. (Paris: Maspero).
- Laude, J. (1966), *Les Arts de l'Afrique noire*. (Paris: Le Livre de Poche).
- Lawson, A.C. (1927), *The Valley of the Nile*. (Berkely: University of California Press), 29, kur. 235-59.
- Leakey, L.S.B. and M.D. et al (1965-71), *Olduvai Gorge*, Juzuu la III. (Cambridge University Press), more vols. in preparation.
- Leroi-Gourhan, A. (1943), *L'Homme et la Matière, Evolution et Techniques*, Juzuu la 1. (Paris: Albin Michel).
- Lhote, H. (1958), *The Search for the Tassili frescoes*, trans., A.H. Porodrick. (London:

- Hutchinson).
- Lhote, H.** (1976), *Vers d'autres Tassili: Nouvelles découvertes au Sahara*. (Paris: Arthaud).
- Libby, W.F.** (1970), 'Radiocarbon dating', *Phil Trans. Roy. Soc.*, Vol. A, 269, no.1193, kur. 1-10.
- Linington, R.E.** (1970), 'Techniques Used in archeological field surveys', *Phil. Trans. Roy. Soc.* Vol. A, 269, no.1193, kur. 89-108.
- Lucas, J.O.** (1938), 'Der hamitische Gehalt de Tschadchamistischen Sprachen', *ZES*, 28, kur. 286-99.
- Lucas, J.O.** (1948), *The Religion of the Yoruba in Relation to the Religion of Ancient Egypt*. (Lagos: CMS Bookshop).
- McCall, D.F.** (1964), *Africa in Time-Perspective*. (Boston: Boston University Press).
- Maley, J.** (1973), 'Mecanisme des changements climatiques aux basses latitudes', *PPP*, 14, kur.193-227.
- Maquet, J.J.** (1970), *Pouvoir et société en Afrique*. (Paris: Hachette).
- Marx, K.** (1972), *Contribution à la critique de l'économie politique*. (Paris: Editions Sociales).
- Mauny, R.** (1960), 'Reviews of Chekh Anta Diop's `Nations negres et cultures and `Afrique noire precoloniale', *BIFAN*, B,22, kur. 544-5.
- Mauny, R.** (1961), *Tableau géographique de l'Ouest africain au Moyen Age, d'après les sources écrites, la tradition orale et l'archéologie*. (Dakar: IFAN).
- Mercier, P.** (1966), 'Histoire de l'anthropologie'. (Paris: PUF).
- Morgan, E.** (1973), *La Fin du Surmali*. (Paris: Calmann-Levy), trans G. Fradier. *The Descent of Woman* (New York: Stein and Day; London: Souvenir Press).
- Mori, F.** (1965), *Tadrart Acacus: Arte rupestre e culture del Sahara preistorico* (Turin: Einaudi).
- Morner, N.A.** (1975), 'Eustatic amplitude variations and world glacial changes'. *Geology*, 3, kur. 109-10.
- Morner, N.A.** (1973), 'Climatic changes during the last 35,000 years as indicated by land, sea, and air data. *Boreas*, 2, kur. 33-53.
- Murdock, G.P.** (1959), *Africa: Its Peoples and their Culture History*. (New York: McGraw Hill).
- Muzur, A. and Nosek, E.** (1974), 'Metal examination of iron objects from Niani'. *AATA*, 11, I. National Academy of Sciences, Washington, DC (1975), 'Understanding climatic change. A program for action', *United States Committee for the Global Atmospheric Research Program*. (Washington).
- Niane, D.T.** (1960), *Soundjata; ou L'épopée mandingue*. (Paris Presence Africaine).
- Nilsson, E.** (1952), 'Pleistocene climatic changes in East Africa', *Proc. II PCPQS*, kur. 45-55.
- Nketia, J.H.** (1975), *History and the Organisation of Music in West Africa*. (Legon: University of Ghana, Institute of African Studies).
- Noten, F., van Cahen, D. Maret, J., de Moeyersons, J. and Roche, E.** (in press), *The Archaeology of Central Africa* (Graz: Akademische Druck-u. Verlagsanstalt).
- Obenga, T.** (1970), 'Methodologie en histoire africaine: sources locales', *Africa*, XXV.
- Organ, R.M.** (1968), *Design for Scientific Conservation of Antiquities*. (London: Butterworth).
- Payddoke, E.** (1963), *The Scientist and Archaeology*. (London: Phoenix House).
- Pelletier, A. and Goblou, J.J.** (1973), *Matérialisme historique et histoire des civilisations*. (Paris: Editions sociales), chapa ya 2.
- Perlman, I. and Isaro, F.** (1969), 'Poetry analysis by neutron activation', *Archaeometry*, II, kur. 21-52.
- Petrie, W.M.F., Mackay, E. and Wainwright, G.** (1912), *The Labyrinth, Gerzeh and Mazghuneh*. (London: School of Archaeology in Egypt).

- Philipson, D.W.** (1977), *The Later Prehistory of Eastern and Southern Africa*. (London: Heinemann).
- Plenderleith, H.J.** (1962), *The Conservation of Antiquities and Works of Art; Treatment, Repair and Restoration*. (London: Oxford University Press).
- Presence Africaine** (1971), *Perspectives nouvelles sur l'histoire africaine*. (Paris).
- Ranger, T.O.** (1962), Emerging themes of African history. International Congress of African Historians, Dar es Salaam.
- Rognon, P.** (1974), 'Modifications naturelles du cycle hydrométéorologique depuis 10,000 ans. Leur utilisation pour la prevision climatique a long terme'. In *Influence des Activités de l'homme sur le cycle hydrometeorologique - 13<sup>e</sup> Journee de l'hydraulique*, Société hydrotechnique Francaise.
- Ruffie, J.** (1977), 'Genetique et anthropologie', Science et vie...(Paris), na.120.
- Said, R.** (1962) *The Geological Evolution of River Nile*.
- Saleh, S.A., George, A.W. and Helmi, F.M.** (1972), 'Study of glass and glass-making processes at Wadi-El-Natrum, 1st part. Fritting crucibles, their technical features and temperature employed'. *Studies in Conservation*, Journal of the International Institute for the Conservation of Museum Objects. (London), 17, kur. 143-70.
- Savage, G.** (1967), *The Art and Antique Restorers' Handbook*. (London: Barrie and Rockliff).
- Servant, M.** (1973), 'Séquences continentales et variations climatiques: évolution du bassin du Tchad au Cenozoique superieur', CORSTOM.
- Servant, M.** (1974), 'Les variations climatiques des regions intertropicales du continent africain depuis la fin du pleistocene', in 13<sup>e</sup> Journee de l'hydraulique, Societe Hydrotechnique Francaise.
- Seydou, C.** (ed.) (1977), *La Geste de Ham-Bodedio au Hama le Rouge*. (Paris: Colin).
- Sibrava, V.** (ed.) (1975), *Quarterly Glaciations in the Northern Hemisphere*. (Prague: UNESCO).
- Simpson, W.K.** (ed.) (1972), *The Literature of Ancient Egypt. An Anthology of Stories, Instructions and Poetry*, trans. R.D. Faulkner, E.F. Wente and W.K. Simpson. (New Haven/London).
- Soga, T.B.** (1929), *Intlalo ka Xosa*. (Lovedale).
- Stross, F.H. and O'Donnel, A.E.** (1972), *Laboratory Analysis of Organic Materials*. (USA: Addison-Wesley ), Module 22.
- Tricart, J.** (1956), 'Tentative de correlation des periodes pluviales Africaines et des periodes glaciaires', RSGF, kur.164-7.
- Ucko, P.J. and Dimbleby, G.W.** (eds.) (1969), *The Domestication and Exploitation of Plants and Animals*. (Chicago: Aldine).
- UNESCO** (1974), *Colloque sur le peuplement de l'Egypte ancienne et le déchiffrement de l'écriture meroitique*. (Cairo, 28 January - 3 February).
- Vansina, J.** (1961), *De la tradition orale: essai de methode historique*. (Tervuren: Memoire na. 36 de Musee Royal d'Afrique Centrale).
- Vansina, J., Mauny, R. and Thomas, L.V.** (eds.) (1964), *The Historian in Tropical Africa*. (London: Oxford University Press).
- Vavilov, N.I.** (1935), *Base theoriques de la selection des plantes, I: Selection generale*. (Moscow/Leningrad).
- Werner, A.E.A.** (1970), 'Analysis of Ancient Metals', PTRS, 269, 1193, kur. 179-85.
- Willett, F.** (1960), 'Ife and its archaeology. JAH,2, kur. 231-48.
- Willett, F.** (1964), 'Spectrographic analysis of Nigeria Bronzes'. *Archaeometry*, 7, kur.81-93.
- Willett, F.** (1968), 'New Light on the Ife-Benin Relationship'. *African Forum*,3, (4),4,1.

- Philipson, D.W.** (1977), *The Later Prehistory of Eastern and Southern Africa*. (London: Heinemann).
- Plenderleith, H.J.** (1962), *The Conservation of Antiquities and Works of Art; Treatment, Repair and Restoration*. (London: Oxford University Press).
- Presence Africaine** (1971), *Perspectives nouvelles sur l'histoire africaine*. (Paris).
- Ranger, T.O.** (1962), Emerging themes of African history. International Congress of African Historians, Dar es Salaam.
- Rognon, P.** (1974), 'Modifications naturelles du cycle hydrométéorologique depuis 10,000 ans. Leur utilisation pour la prevision climatique a long terme'. In *Influence des Activités de l'homme sur le cycle hydrometeorologique - 13<sup>e</sup> Journee de l'hydraulique*, Société hydrotechnique Française.
- Ruffie, J.** (1977), 'Genetique et anthropologie', Science et vie...(Paris), na.120.
- Said, R.** (1962) *The Geological Evolution of River Nile*.
- Salch, S.A., George, A.W. and Helmi, F.M.** (1972), 'Study of glass and glass-making processes at Wadi-El-Natrum, 1st part. Fritting crucibles, their technical features and temperature employed'. *Studies in Conservation*, Journal of the International Institute for the Conservation of Museum Objects. (London), 17, kur. 143-70.
- Savage, G.** (1967), *The Art and Antique Restorers' Handbook*. (London: Barrie and Rockliff).
- Servant, M.** (1973), 'Séquences continentales et variations climatiques: évolution du bassin du Tchad au Cenozoïque supérieur', CORSTOM.
- Servant, M.** (1974), 'Les variations climatiques des régions intertropicales du continent africain depuis la fin du pleistocène', in 13<sup>e</sup> Journee de l'hydraulique, Société Hydrotechnique Française.
- Seydou, C.** (ed.) (1977), *La Geste de Ham-Bodedio au Hama le Rouge*. (Paris: Colin).
- Sibrava, V.** (ed.) (1975), *Quarterly Glaciations in the Northern Hemisphere*. (Prague: UNESCO).
- Simpson, W.K.** (ed.) (1972), *The Literature of Ancient Egypt. An Anthology of Stories, Instructions and Poetry*, trans. R.D. Faulkner, E.F. Wente and W.K. Simpson. (New Haven/London).
- Soga, T.B.** (1929), *Inlalo ka Xosa*. (Lovedale).
- Stross, F.H. and O'Donnel, A.E.** (1972), *Laboratory Analysis of Organic Materials*. (USA: Addison-Wesley), Module 22.
- Tricart, J.** (1956), 'Tentative de corrélation des périodes pluviales africaines et des périodes glaciaires', RSGF, kur.164-7.
- Ucko, P.J. and Dimbleby, G.W.** (eds.) (1969), *The Domestication and Exploitation of Plants and Animals*. (Chicago: Aldine).
- UNESCO** (1974), *Colloque sur le peuplement de l'Égypte ancienne et le déchiffrement de l'écriture méroïtique*. (Cairo, 28 January - 3 February).
- Vansina, J.** (1961), *De la tradition orale: essai de méthode historique*. (Tervuren: Mémoire no. 36 de Musée Royal d'Afrique Centrale).
- Vansina, J., Mauny, R. and Thomas, L.V.** (eds.) (1964), *The Historian in Tropical Africa*. (London: Oxford University Press).
- Vavilov, N.I.** (1935), *Base théoriques de la sélection des plantes, I: Sélection générale*. (Moscow/Leningrad).
- Werner, A.E.A.** (1970), 'Analysis of Ancient Metals', PTRS, 269, 1193, kur. 179-85.
- Willett, F.** (1960), 'Ife and its archaeology. JAH, 2, kur. 231-48.
- Willett, F.** (1964), 'Spectrographic analysis of Nigeria Bronzes'. *Archaeometry*, 7, kur.81-93.
- Willett, F.** (1968), 'New Light on the Ife-Benin Relationship'. *African Forum*, 3, (4), 4.1.

- Willett, F.** (1969), 'New Radiocarbon Dates from Ife'. WAAN, 11, kur. 23-5.
- Williams, M.A.J., Clark, J.D., Admson, D.A. and Gillespie, R.** (1975), 'Recent Quaternary research in central Sudan'. BASEQUA, 46.
- World Meteorological Organisation** (1975), 'WMO/IAMAP Symposium on long-term climatic fluctuations', Proc. Norwich, WMO, na. 421.
- Young, W.J.** (1958), 'Examinations of works of art embracing the various fields of Science', *Proceedings of the Seminar on Application of Sciences in Examination of Works of Art.* (Boston), kur. 18-19.
- Zaki, A. and Iskander, Z.** (1942), 'Ancient Egypt cheese'. ASAE, XLI, kur. 295-313.

# FARAHASA

- A. Ruffe - 101  
A.N. Tucker - 92  
A.P. Newton 13  
A.R. Radcliffe-  
Brown 14  
A.T. Bryant 47  
A.W. Schlegel 5  
Australopitheko -  
188  
Abasidi 36  
Abbe 51  
Abbeville - 181,  
Abbevillian - 186  
Abidjan, 22  
Abka, - 311  
*Abki* - 279  
Aboey 5  
Abu Hagar. - 278  
Abu Simbel - 279  
Abuja 51  
Abyata, - 147  
Abydos - 283, 309, 311  
*Abyssinia*, - 302  
Acacus, - 104  
Accra, 29  
Acheuli - 133  
Ackermann - 103  
Adaima, - 274  
Adamawa 31, 115  
Adamawa  
Mashariki: 115  
Addis Ababa - ix,  
47, 169, 177  
Adrar Bous - 255, 256,  
260, 292  
Aegyptopithecus -  
168  
Aelophithecus, - 168  
Afalū-bu-Rhummel, -  
246  
Afar - 156, 157, 170,  
176, 194 Afar  
ya Kati - 165  
Afrikanaizesheni 28  
Afro-Asia 120  
Agades - 291  
Agano la Kale 38  
Aghawa ya Kancin.  
41  
Agordat - 208  
Ahaggar - 255, 256,  
.257, 308  
Ahel - 244  
Ahmad Baba 3, 50  
Ahmad majid, 48  
Ahmadu Seku, 52  
Ahmed Gran 46  
Ain Dokkara - 248  
Air - 28, 284  
Ajami 3  
akilojia ix, 2, 3, 7,  
14, 15, 26, 29, 31,  
39, 86, 141, 147,  
149, 297,  
Akori - 81240, 250, 255  
Aksum 14  
Aktiki - 153, 162  
Al Biruni Ya kubi 41  
Al Tabari 41  
al-Baghdadi 43  
Al-Bakri - 1, 140  
Albert - 124  
Aldai - 154  
Alexandria 11,40  
Algeria - 16, 45,  
104, 181, 182,  
186, 240, 241, 244,  
246, 248, 254,  
255, 263, 293  
Al-Haji Askiya  
Muhammad 22  
Al-Haji Umar, 52  
al-Hinyari 43  
Ali 6  
Al-Idris 11,43  
Alimen  
*Al-Inkishafi* 51  
al-Jabarti 45  
Almohadi 37,, 42  
Almoravidi 42  
Al-Nasiri al-Slawi 45  
Alpine - 152

- Alps - 182  
 al-Sa'di 50  
 al-Shmmakhi 45  
 Altamira, - 244  
 al-Tunisi 48  
 Al-Umari, 11, 43  
 alumini - 184  
 al-umran al- Bashar. - 319  
*Al-Wafibi-L-  
 Wafayati* 43  
*Al-Wasit* 46  
 al-Zarikashi 45  
 Al-Zayyani 45  
 Ainadou Hampâté  
 Ba 55  
 Ananzi - 214  
 Amina 21  
 Amkoulel 72  
 Amon. - 294  
 Amrati - 310  
*anato*, 34  
 Anderson - 82  
 Andre Malraux - 294  
 Anfa - 181  
 Angola - 11,12,33,44,48,95,  
 131,109,112,221,226,228, 232  
 233,234,237,238  
 Antaktiki - 149, 153,  
 156, 157,162  
 Antalanthropo - 241  
 Antananarivo - 128  
 Antera Duke, 51  
 anthropolojia 2, 5, 7,  
 9, 14 ,15,26,  
 anthroponomia 5  
 Apidium, - 168  
 Arabia ya Kusini - 305  
 Arambog - 104  
*Ardo* 68  
 Arkanthropo - 182  
 Armant. - 280  
 Armenia 3  
 Arturo Labriola vii  
 Aruj 45  
 Asante - 19,51,58,270,  
 319,320 Asantehene  
 Osei Bonsu 23  
 Asheuli - 150, 177,  
 241,182, 184, 185,193,  
 199,201, 212, 214,  
 215,218, 221, 225,  
 226,227, 239, 240,  
 254, 255, 266,268,  
 274, 275, 277, 290  
 Asheuli ya kale, -  
 222,234  
 Asia- 8, 40, 52, 74,  
 103, 104, 107, 125,  
 134, 135;156, 166,  
 177, 180, 193,  
 201,298, 302,305,  
 318, 320,321 Asia  
 Magharibi. - 147,  
 Asia ya Kusini  
 29,108, Asia ya  
 Kusini-Mashariki.  
 - 124 ,Asia ya  
 Mashariki 29  
 Askiya Muhammad  
 22  
 Askiya wa  
 Songhay 52  
 Assajen Wan Mallen.  
 292  
 Asselar - 317  
 Aswan - 311 Aswani  
 na Khartoum 117  
 Asyut - 308, 309  
 Atbara, - 128, 275  
 Ateri - 150,244, 255,  
 256, 260 275, 277  
 Atlantiki - 9 33, 40,44,  
 91,93, 110, 115,117,  
 120,125,126,149,  
 153,156,161, 182,  
 184  
 Atlantis 15  
 Atlasi - 54,124,294  
 Atlas ya Kusini, - 122  
 Ankar, - 256  
 Aulef, - 254  
 Aurignac - 182  
 Australia - 101,159  
 Australopihitheko -  
 182, 185, 194, 195,  
 314  
*Australopithecus  
 prometheus* - 179  
 Australopitheko  
 grasili 176  
 Australopitheko  
 robusto - 170  
 Australopithesi - 183  
 Australopithesini -  
 104, 168, 170,  
 178,199, 210,212  
 Austria - 104,186  
 Avatika Bagdasarian,  
 48  
 Azores - 125,126  
 B. Malinowski 14  
 Bachar - 293  
 Badari, -281,309  
 Bafulero - 18  
 Baghdad. - 273  
 Bahari - 279  
 Bahari Kuu ya Hindi  
 11,48, 125, 126,  
 130, Bahari ya  
 Atlantiki - 37, 124,  
 28,238,241, 250,  
 263, 266 Bahari ya  
 Erythrea 39 Bahari  
 ya Hindi - xi, 33,  
 50, 52,125 Bahari  
 ya Mediterani  
 viii,128 Bahari ya  
 Msumbuji - 125  
 Bahari ya Pacific x



- Bahari ya Sham  
 11,31, 32, 36, 124,  
 125, 149, 150, 154,  
 157, 282  
 Bahr el Ghazal. - 2,127,  
 128  
 Bakker - 157  
 Balandier - 140  
*balla* 5  
 Bamako - 64,72,268, 269  
 Bambata vya Zimbabwe -  
 133  
*bambaado*, 70  
 Bamum 3,32, 52  
 Banangolo 66  
 Bandari - 280,279,308  
 Bandari ya Fayum, - 309  
 Bandiagara 71,73  
 Bandy, - 162  
*bankulu mpangu* 33  
 Banzaoumana 64  
 Banzoumana 70  
 Bara- 2, 5, 13, 14,  
 16,19, 24 33, 35,  
 36, 43, 44, 47, 49,  
 135,137, 150  
 Bara Arabu - 126  
 Bara Arabuni - 95,  
 125 bara Hindi -  
 125 Bara la Afrika  
 -vii,viii, xiv, 1, 37,  
 48, 107, 109, 118,  
 122, 124,127, 129,  
 133, 143,1 145,  
 146, 147, 188,190,  
 93,302, 307, 314,  
 318 Bara la Asia -  
 v, 196, 201 bara la  
 Siberia. - 157  
 Barabarossa 45  
 Barbot 12  
 Bardai - 286  
 Barth, 6  
*Bassa Ahsadee* 12  
 Battle Cave, -293  
 Baule, 67  
 Bauinan - 92,94  
 Bavaria - 185, 186,  
 187  
*Baylo* 67  
 Beja, 41  
*bekhen* 78  
 Belime, 72  
 Bello 22  
 Bellum Civile 39  
 Bemba 110  
*bendre* 5  
 Benezet, 13  
 Benguela - 126  
 Beni Abbes - 254  
 Beni Hilal 9  
 Benin - 5, 34,44,126,  
 270  
 Benjamini Anderson,  
 51  
 Bentley Glass - 101  
 Benue Kongo 115,  
 120  
*Berbers* 6 Sunjata: 6  
 Berlin 40  
 Berne; 13  
 Besset - 92  
 Biber, - 152  
 Biberson - 185  
 Bijago 117  
 Bilad al-Sudan 11  
 Binger 50  
 Bir el Ater - 241  
 Bir el Ater, - 181  
 Birmingham, 28  
 Bishop na Miller, -  
 162  
 Bizerta, - 124  
 Black - 186  
 Blaka - 287  
 Blande, - 269  
 Bluden 51  
 Blue Nile - 128,147,  
 208,311  
 Bobo, - 141  
 Bodo - 176  
 Boilat, 51  
 Bomoun - 95  
 Bonde la Benue 11  
 Bonde la Chad - 3,  
 148, 154 bonde  
 la Chad kalc- 111  
 Bonde la Dead -  
 112 bonde la  
 Fayum - 280  
 bonde la juu la  
 Awash (Afar) -  
 161 bonde la Kasai  
 na Shaba - 234  
 Bonde la Kati -  
 233 bonde la  
 Kongo - 4,22,221,  
 225,227, 228, 232,  
 233, 234, 229  
 Bonde la  
 Kubango-Zambezi - 233  
 Bonde la Mto Kongo - 233  
 bonde la Mto Naili 3,9,15,  
 32,38,104, 107, 111, 138,  
 274,277 278, 280, 283,  
 292, 294, 301, 305,307, 308,  
 311,312,313, 316, 320, 321,  
 bonde la Mto Niger - 268,  
 272, bonde la Olduvai- 147,  
 170, 185, 201, 240  
 bonde la Omo - 177, 176,179,  
 190,193, 199, bonde la, 318  
 Pleistosini la Ziwa Turkana - 177  
 - Bonde la Ufa - 2, 147, 165,190,  
 199, 201,206, 207,208, 209,  
 210,301 Bonde la Volta - 142  
 bonde la Zaire - 1, 10 ,124, 147,  
 207,126,137, 206, 227,  
 bonde la Zambezi , 233

- Bonnefille - 161  
 Bono Mansu 8  
 Bordeaux, 28  
 Bormeo 117  
 Bornu 37,52  
*Bororo* 70,105  
 Botswana - 214,  
 284, 294, 296  
 Bouar, - 231  
 Boubou Hama 55  
 Bougouni, 72  
 Bour - 238  
 Bowdich, 13  
*bowe* - 128  
 Bowler - 159  
 A. Brasio 53  
 Brazil 28,49  
 Brazilia - 102  
 Breuil - 181,182,  
 184, 184  
 Broken Hill - 193  
 Bronislaw  
 Malionowski 26  
 Broom - 187  
 Brunhesi - 146  
 Bryan - 93  
 Bualen. - 297  
 Bubalusi - 288  
*bubu*  
 Bucha, - 84  
 Buchari - 275  
 Buhen, - 88  
 Burkina Faso, 5, 9,  
 18, 56,65,71, 142  
 Bukini 44,88,89, 168  
*Buldan* 41  
 Burton 49  
 Buru - 238  
 Burundi - 136,232  
 Busman 12  
 Bussa - 268  
 Byantium, 39  
 Byzantine 40  
 C. Conti Rossini 13  
 C.G. Seligman - 14,94  
 C.H. Stigand, 15  
 C.L. Lepsius, - 92  
 C.S. Reindorf, 51  
 Cadmosto 12  
 Calabar 51  
 Calame-Griule 140  
 Caley<sup>5</sup> 76  
 Cana, 21  
 Canada. 29  
 Cape Hangklip - 214  
 Cape Manuel - 268  
 Cape Province -  
 187,217  
 Cape Verde - 124, 126  
 Cardonega 12  
 Carl Christian  
 Reindorff 15  
 Carr Saunders, - 135  
 Carribean 28  
 Carter G. Woodson  
 28  
 Catican 53  
 Cavazzi 12,62  
 Cavazzi de  
 Montecudolo - 95  
 Cenozoic, - 162  
 Cerko 21  
 Chad - 30, 34, 110,  
 135, 156, 157, 162,  
 182, 110, 260, 263,  
 265, 270,286,284,  
 288,292  
 Charles Darwin - 188  
 Charles Lucas 13  
 Charles Monteil, 15  
 Chavaillon - 177  
 Chavuma, - 217  
 Cheikh Anta Diop -92,  
 118  
 Chelles - 185, 186  
 Cheops 80  
 Chephren - 87  
 China - 137,186  
 Chonge, - 228  
 Choukoutien - 186  
 Churchill<sup>2</sup> 2  
 Ciroma, 8  
 Clacton-on-sea - 184  
 Cladius Ptolemy 11  
 Cohen - 93,109  
 Conakry - 126, 269  
 Cordillera - 157  
 Cosmas  
 Indicopleutes 39  
 Crescent Island 208  
 Cro magnon - 244, 278  
 Cuba. 28  
 Curtis - 83  
 Czechoslovakia 28  
 D. Dalby 93,117  
 D.F. Wolberg - 179  
 Da Monzon 4  
 da Silva Regon 53  
*daaru* - 94  
*Dahomey* 13,21, 320  
 Dakar - 15, 16, 26,  
 50, 169,268,269  
 Dakodonu - 95  
 Dambos - 214  
 Danfo Sine 65,72  
 Danxome 33,34  
 Dapper 12  
 Dar es Salaam  
 26,183  
 Darfur - 46,52,307  
 Dart - 180, 182  
 Darwin - 5,104  
 David Livingstone,  
 47  
 David Reubeni 46  
 Dayfallab, 46  
 Deir Tasa - 308, 309  
 Deir-Bahri, 32

- Delafosse – 6,93,109,114  
 delta ya Magharibi - 308  
   delta ya Misri - 308  
   delta ya Mto Niger – 7,  
   44,265,305 delta ya  
   Nili - 313  
 Deng, 108  
 Desmond J. Clark - 139  
 Dhar Tichitt – 260,284  
 Diarra wara, 64  
 Dider - 286  
*diel-faama*, 70  
*Dieli*, 70  
 Dieterlen. - 95  
 Dietrich  
   Westermann. 14  
 Dingaana Catshwaye,  
   47  
 dini 19,22,27,23,36,  
   38, 40,49,57, 58,  
 Diodorus 38,39  
   Diodorus Siculus  
   40  
 Diredawa - 206  
 Djelgodji 71  
 Dizek 13  
 Do, 64  
 Dokodonu wa Dahomey –  
   95 *dokunno*  
 Doleriti. - 217  
 Dolgopolskij - 93  
*doma* 64,65,70, 152.  
 Dongola - 278  
 donon. - 278  
 Dordogne - 185  
 Dorize - 153  
 Drackensberg – 285,  
   290  
 Dubois - 186  
*dugu* - 94  
 Dussel Basin - 185  
 Dyars - 157  
*dyatigui* - 142  
 E. Cartailhac - 182  
 E.J. Wayland - 183  
 E.W. Blyden, 15  
 E.W. Bovill, 15  
 Edinburgh 28  
 Edward W., 51,135  
 Eemian – 159,161  
 El Amrah - 309  
 El Beyes - 254  
 El Kab, - 311  
 Elementeita - 182  
 El-Khiam, - 278  
 Enameli - 309  
 Eneri Blaka- 296  
 erekto. - 255  
 Erg Admer, - 128,255  
 Erik Holm - 290  
 Eritera, 37, 208  
 Esh Shaheinab –  
   208,254,256, 288  
 Esna - 277  
 Esternmann - 93  
 Ethiopia – 2,11,12,36,  
   37,39,41,42,44,48,,45,  
   46,48,57,79,95,104,  
   107,108, 113,120, 128,  
   143,149,150,165,170,  
   176,148,177,179,190,  
   193, 194,199, 201,206,  
   208,209, 240,301,305,  
   306, 316, 317  
 Etrusean 15  
 Eurasia - 161  
 Eva L.R. Meyrowtz  
   15  
 Evans-Pritchard 6  
 Evenden - 83  
 F. Braudel, 2  
 F. Muller 113  
 Faid Bour, - 248  
 False Bay - 214  
 Fan; 67  
 Fante 51  
 Farao – 38,136, 294,296,  
   Farao Hor'Aha 78,  
   Farao Narmer.<sup>3</sup> - 95  
   Farao Nefer-Ka-Re  
   (Pepi II) 32 Farao  
 Pepi wa Pili 108, Fasso - 145  
 Fate 67  
 Fatimidi 36,41, 42  
*Fauresmith* - 215  
 Fayum, - 168, 279,  
   281, 282,308,316  
 Fayun 79  
 Fernando - 238  
 Fezani 55, 288, 289,  
   377  
*Fief*, 34  
 Flint, - 154  
 Flora Shaw, 14  
 Florisbad, - 217,218  
 Fort Ternan - 186  
 Fourah Bay 16  
 Freetown 113  
 Frobenius – 6,94,289,  
   290  
 Fu Kiau, 55  
 Fuhlrott - 185  
 Fula Ardo Dembo,  
   64  
 Fula, 50  
*Fulani* 72  
 Fulfulde 64  
 Funj 46  
 Futa Djalon 50 Futa  
   Toro 50 Futa ya  
   Senegal, 50  
 G.M. Theal 47  
 G.P. Murdock 14,26  
 G.W. Murray - 92  
 Gabli - 184  
 Gabon – 108, 226,  
 312228, 231, 232, 233,

- 234,  
 Gabriel Hanolaux 13  
 Gafsa – 183,241,246,  
 galago - 168  
*Galena* 79  
 Galjeien - 286  
 Gambia – 186, 187,  
 222, 225,227, 233,  
 272,305  
 Gan - 143  
*gando* 64  
 Gao – 18,42,140,269  
 Garamantes, 40  
 Gardner  
 Gargora - 206  
 Garonne - 182  
 Gasse – 156, 161  
 Gauss - 146  
 Ge'ez , 113  
 Genge Kuu – 214,  
 217  
 Geniza 42  
 Georges Hardy 15  
 Germaine Bieterlen 7  
 Gerza – 280, 310  
 Ghana – 6,14,28,48,  
 51,140, 141, 143,  
 266, 268,269,270,  
 273,319  
 Ghuba ya Benin 59  
 ghuba ya Guinea –  
 37,122,126,128,  
 221,233 Ghuba ya  
 Sango – 186 Ghuba  
 ya Uajemi, 36  
 gibbon, - 168  
 Gigantopitheko - 169  
 Gignoux - 183  
 Gilbert Viellard 50  
 Gilbert-Gauss - 147  
 Gilsa - 162  
 Giza 80,89, 277  
*Glele* 13,34  
 glotokronolojia 54  
 Glotz 13  
 Gold Coast 16,51  
 Gondar - 206  
 Gonja 50,*Gonja*  
*Chronicles* 12  
 Gonoa - 286  
 Goody 57  
 Gossolorum - 260  
 Graba III - 206  
 Gran Arab-Faqih, 46  
 grasilii – 170, 180  
 Greenberg – 5,93,110,  
 113,114,117,120  
 Gregersen 110  
 Griule - 95  
 Guinea –12,13, 28,77,  
 95,131,145,257,  
 266, 295 Guinea  
 Bissau 117  
 Gunz, - 152, 183  
 Gur 110, 115,120  
 Gustav Natchigal 13  
 Gustavus Vasa 51  
 Guthrie – 92,110, 117  
 Gwisho – 134, 238  
 H.A. Wieschoff, 15  
 H.H. Johnston, 110  
 H.J. Hugot - 295  
*haala* 64  
 Hadar – 165, 177,  
 194  
 Haiti 28  
*hal* 64  
 Halfa - 277  
 Ham 113  
 Hamamia, - 280  
 Hamburg – 103, 104  
 Hamidun 46  
 Hânipaté Bâ 7, 291,294  
 Hannibal – 39,135  
 Harmattan, - 126  
 Harry Jonston 14  
 Hatshepsut 32  
 Hawari - 277  
 Hays, - 154  
 Hearths - 218  
 Hegel – 13,21,103  
 Heinrich Barth 13,49  
 Heliopolis. - 283  
 Helwan – 282,283  
 Henri Labouret 15  
 Henrik Witbooi, 47  
 Henry Johnston 114  
 Herkhuf - 32, 108  
 Herman Baumann,  
 14  
 Herodotus 11,38,40,  
 43, 312  
 Hersini - 122  
 Hierakonpolis –310, 311  
 Hiliobatidi - 169  
 Hill – 214, - 218  
 lobatide - 166  
 Hinze. - 93  
 Hispania – 182,186,  
 244, 285  
 Hitler - 102  
 Holosini – 146, 150,  
 153, 186, 233  
 Homburger, 118  
 Hominidi – 168,169,  
 170, 177,182, 190,  
 194, 99,210, 210,  
 212, 214,218, 220,  
 315  
 Homo – 177, 85,186,  
 210, 255 Homo  
*ereko*–,170, 176,  
 177, 179, 186, 193,  
 195, 201, 201, 214,  
 218, 234, 254, 263  
 Homo faber - 178

- Homo habili – 301, 302  
 170, 176, 193, 194,  
 195, 199, 210, 263,  
 254 Homo  
 rhodesia – 214,  
 215 Homo sapi –  
 188, 193, 201,  
 212,218, 244, 317,  
 244 *Homo sapiens*  
 – 178 Homoerecto.  
 - 241  
 Honea – I04  
 Horon 68,71  
 Horusi - 294  
 Houis - 140  
 Howard 28  
 Hungaria – 169,186  
  
 I.A. Akinjogbin 8  
 Ibadan 16  
 Iberia – 244, 246, 257,  
 248  
 Ibn Abd al-Hakam  
 41  
 Ibn Adwar, 50  
 Ibn al-*adhari* 43  
 Ibn al-Saghir 42  
 Ibn Battuta – 21,31,43,  
 141  
 Ibn Khadun – 11,35,66,  
 319  
 Ibn Lyas, 45  
 Ibn Sa id al-Gharnati  
 43  
 Ibri, 9  
 Idris 52  
 Idris Alaoma, 50  
 Ife 25  
 Ignatius Sancho, 51  
 Iheren, - 292, 293, 296  
 Ikweta – 5,237,263,  
  
 301, 302  
 Iman Ibn Fartuwa 50  
*Imbo Zabantusundu*  
 47  
 In Salah - 254  
 Inchiria - 161  
 India – 48,137, 114,  
 156, 169, 186  
 Indonesia – 168, 176,  
 186  
 Ishango – 229,238  
*Isidigini* 47  
 Isimila – 201, 214  
*isnad* 71  
 Isnadi 56  
 Israeli - 162  
 Istanbul (Uturuki) 3  
 Italia – 42,169,183,  
 187  
 Ivor Wilks 23  
 Ivory Coast, - 9,57,  
 268,265, 270  
  
 J. Cuvelier, 53  
 J. Hiernaux 9  
 J.A.B. Horton, 15  
 J.B. Danquah, 15  
 J.D. Clark – 133,256  
 J.D. Fage - 298  
 J.de Morgan - 183  
 J.E. Casely-Hayford  
 15  
 J.H. Greenberg, 14,  
 92  
 J.M. Sarabah, 15  
 J.M. Stewart 120  
 J.O. Lucas 15  
 J.V. Egharevba 15  
 J.W. de Graft  
 Johnson 15  
 Jabbaren. – 288, 293  
  
 Jabrudia - 218  
 Jacobus Capitein 51  
 James Africanus 51  
 James Africanus  
 Horton, 13  
 James Bruce 13, 46  
 Jamhuri Afrika Kusini, - 284  
 Jamluri ya Afrika ya  
 Kati – 108,231,232,23,  
 32,39, 290  
 Jamhuri ya Guinea, 266, 269  
 Jamhuri ya Watu wa  
 Kongo – 232, 233,238  
 Jan Vansina 26  
 jangwa – 127, 137  
 Jangwa la Kalahari –  
 107, 108, 127, 301 jangwa la  
 Libya – 307,254 jangwa la  
 mashariki, - 280  
 jangwa la Namibia –  
 126 jangwa la  
 Negev – 307 jangwa  
 la Sahara – 2,36,42,43,  
 111, 124, 128, 135, 149, 153,  
 186, 196, 208,222, 250, 270,  
 301, 318  
 Java – 177, 186  
 Jebel Ijerane, - 254  
 Jemai - 277  
 Jenne 50  
*Jihad* ya wafulani 51  
 jimbo la Cape – 210,  
 214, 218 jimbo la  
 Shaba – 131,133  
 Job Ludoulf, 12  
 John Philip 47  
 Jos – 266,268  
 Joseph Ki-Zerbo 53  
 Juba II 39, 40  
  
 K.O. Dike 16

- Kabwe. - 218  
*kaçella* 8  
 Kadero - 279  
 Kadi Nu'man 41  
 Kafu - 180, 226  
 Kagera - 184, 222, 233, 315  
*kaigamma*, 8  
 Kairo - 168, 277, 117, 274, 275, 277, 282, 283,  
 Kaisari, 39  
 Kakontwe - 162, 183, 229  
 Kalahari - 2, 125, 126, 129, 220, 222, 301  
 Kalambo - 134, 214, 215, 218  
 Kamara 27  
 Kamasia - 165, 183, 186, 187, 233  
 Kambabai, - 269  
 Kamerun; 3, 110, 118, 226, 228, 231, 232, 233, 234, 238  
 Kamoã - 238  
 Kampala (Makarere College), 16  
 Kanapoi - 176,  
 Kanari - 246  
 Kanjera - 165, 183, 193, 227  
 Kano 51, 72  
 Kanta wa Kebbi, 52  
 Kapsi - 181, 183, 244, 246, 248, 257, 249  
 Kapsia - 133, - 207  
 Kariandusi - 201  
 Kariba - 104, 127  
 Kariteji 39, 125  
 Karkarichinkat, - 269  
 Karl Marx 12  
 Karnak, - 85  
 Kamelia - 184  
 Karoo - 214  
 Kasai - 128, 184, 187, 227, 237  
 Kasamansi - 305  
 Katanga - 166, 168, 184, 221  
 Kathago - 95, 125  
 Katla, 115  
 Katsina, 51  
 Katwinkel - 185  
*Kayes*, 69  
 Kenchala - 246  
 Kenya - 32, 57, 131, 165, 169, 170, 176, 179, 182, 183, 184, 185, 193, 194, 199, 206, 207, 208, 209, 225, 240, 278  
 Kenya pitheko - 169, 314  
 Kenyapitheko  
 Africana - 169  
 Kenyapitheko  
 Wikeri - 169  
*ker* - 94  
 Keremi, - 246  
 Keringet - 208  
 Kerkopitheko - 184  
 kerkos - 184  
 Kerma, - 313  
 Kerzaz, J. Chavaillon - 254  
 Keyla, 4  
Khaldun 12, 43  
Khalifa bin Khayyat 41  
 Kharaga - 254, 275  
 Khartoum - 16, 45, 46, 47, 127, 256, 278, 279, 307, 311  
 Khayruddin 45  
 Khet' 79  
 Khitab 42  
 Khoi-Khoi 108  
 - Khor Abu Anja - 275  
 Khor Daud, - 279  
 Khwarizni, 41  
 Kiafrika - xi, xii, xiii, xiv, 3, 4, 6, 7, 8, 10, 3, 14, 19, 21, 22, 23, 25, 26, 27, 33, 34, 47, 48, 49, 50, 51, 53, 54, 63, 64, 70, 91, 94, 95, 101, 103, 110, 112, 113, 114, 139, 140, 141, 142, 143, 183, 229, 257, 260, 269, 290, 291, 292, 294, 296, 297, 305, 308, 318, 319, 320  
 Kiafrikaans 7, 47, 117  
 Kiafrika-Kiasia, 33  
 Kiajei, 37, 38, 40, 48, 50, 117, 286  
 Kiakan-Guang, 115  
 - kiakiolojia- 1, 38, 74, 75, 78, 84, 85, 104, 140, 141, 169, 178, 231, 238, 240, 263, 283, 285, 311, 314, 319,  
 Kiamazoni 21  
 Kiambara 70  
 Kiamharia - 12, 95, 113  
 Kiamrati. 310  
 kianthropolojia 31  
 Kiarabu - xiv, 2, 3, 5, 7, 12, 13, 25, 41, 44, 45, 48, 50, 51, 71, 91, 92, 07, 112, 113  
 Kiarabu na  
 Kiajemi viii  
 Kiarmania 117  
 Kiarya 13

- Kiasheuli – 206, 214,  
 215, 218  
 Kiasia' - 319  
 Kiateri. - 241  
 Kiazerbaijani 48  
 Kibadari - 312  
 Ki-Bambara 22,66,  
 68,142 Kibambara  
 Danfo Sine 64  
 Kibambara -Dyula  
 115 Kibambara-  
 Dyola, - 92  
 Kibantu – 5,94,109,110,  
 112, 113,114,117,118,  
 120,317  
 Kibariba, 115  
 Kibasari 115  
 Kiberiberi – 92,93, 95,  
 109 118, 114  
 Kibiiru 58  
 Kibijago 117  
 Kibisa, 115  
 Kibohairi 117  
 Kiboza 32  
 Kibsaga, 115  
 Kibusa 115  
 Kibwamu, 115  
 Kichadi, - 93, 109  
 Kichamba 115  
 Kichina– ix,xiv,37,  
 55  
 Kidachi 117  
 Kidagari, 115  
 Kidagbane, 115  
*Kidjerma* 106  
 Kidogomba - 142  
 Kidrogoni 115  
 Kidrauid 114  
 Kidyula, 50,115  
 Kiedo, 115  
 Kiethiopia – 26,38,42,  
 112, 113,260  
 Kifaransa 2,15,27,28  
 Kifarao - 294, 309, 311  
 Kifarsi 117  
 Kifulani 4, 37, 68,  
 72, 105, 106, 291  
 Kifulefulde– ix, 12,  
 50,51,66,67,90, 92,  
 93,94,114,115  
 Kiga-Adangme, 115  
 Kigala, - 93  
 Kigani, 115  
 Kigbeya, 115  
 Kige'cz 12,46  
*Kigicandi* 32  
 Kigiriki – 11, 37, 38,  
 39,182, 185, 186  
 Kigrusi 115  
 Kiguinea - 257  
 Kigujarati, 107,117  
 Kiguna, 115  
 Kihadza - 109  
 Kihamiti 14, 33, 93,  
 109,114, 117, 120  
 Kihausa – ix,xiv,5,12,  
 14,37,50,51,92,93, 94, 118  
 Kihibrania 37  
 Kihindi 48,92,117  
 Kihindi-Kiajemi  
 112 Kihindi-  
 Kizungu 112, 117,  
 113  
 Kihispania - ix,xi xiv  
 Kiibo, - 92, 115  
 Kiidoma, 115  
 Kiifa - 95  
 Kiikala 64  
 kiikolojia – 122, 127,  
 136,  
 Kiingcreza –ix,7,16,26,  
 28,54, 91,94,110  
 Kiislam 11,21, 22,  
 28, 35 36, 52,71,  
 145  
 Kiitaliano xiv, 37  
 Kijapani xiv  
 Kijerumani – ix,  
 xiv,2,13,94,103,  
 112, 319  
 Kikala, - 294  
 Kikanuri 5, 51  
 Kikhariji, 43  
 Kikhartoum - 316  
 Kikhoi-Khoi 114,118  
 Kikhoisan  
 108,110,114  
 Kikisi 115  
 Kikoa 118  
 kikoloni – 13,25,26,27,  
 28,47,120,298,,321  
 Kikongo 54,107,  
 Kikopti, - 37,95, 117  
 Kikorodofan 110  
 Kikotoko 51  
 Kikrioli (Krio) 117  
 Kikristo 43, 49  
 Kikronolojia 3,7, 33  
 Kikru, 115  
 Kikulango, 115  
 Kikusase - 142  
 Kikushi, 109  
 Kikushiti – 93,113, 114, 118  
 Kikwadi 109  
 Kilatin – 37, 39,44,  
 182, 183, 184  
 Kilevallois – 241, 254,  
 255  
 Kilimanjaro - 148  
 Kilingala, - 92  
 Killoginon - 244  
 Kilobiri, 115

- Kilwa Chronicle* 12  
 Kimaanya 117  
 Kimalay 112  
 Kimalaya-Polinesia  
 113, 117  
 Ki-Mande - 6,94,110  
 Ki-Mandingo - 94  
 Kimaninka, 115  
 Kimano, 115  
 Kimariana, 113  
 Kimasai 114  
 Kimbun, 115  
 Kimediterani - 107,  
 127,149,301  
 Kimende Kusini 32  
 Kimerciana 51,112,  
 117  
 Kimeroc, 32  
 Kimeroit 117  
 Kimesolithi. - 133  
 Kimisri - 32,79,93, 94,  
 114,117,118  
 Kimore - 22,115,142  
 Kimorocco 48,50  
 Kimsari 46  
 Kimusteri, - 268,277  
 Kinailoti Kimasai,  
 117  
 Kindi 41  
*Kinegro* viii, 114,118,  
 133, 270,318,314  
 Kineolithi - 298, 307,  
 316,317  
 Kingonde 6  
 Kiniloti 92, 110, 117,  
 221,225  
 Kinshasa - 227, 315  
 Kinsibidi, 52  
 Kinuba-fulh 114  
 Kinubi - 5,117  
 Kinupe, 115
- Kioldowani - 274  
 Kipanga, 310  
 Kipapua 114  
 Kireno - ix,xiv,7,53,  
 112,117,142  
 Kirumi, 11, 31, 39,  
 40, 51,88  
 Kirusi, ix, xiv,298  
 Kisabe ya Kusini - 95  
 Kisamo 22  
 Kisani 108, 114,  
 118, 115, 291, 293  
 Kisasili - 3,7,14,67,291  
 Kisemiti - 33,94, 109,  
 113, 114,117,118  
 Kisemitiki, - 93  
 Kisemiti-Kiyahudi  
 112  
 Kisenufo, 115  
 Kisereri, - 93, 94, 115  
 Kisidamo, - 93  
 Kisimia - 182  
 Kisiwa cha Fernando  
 Po 110  
 Kislavu 112  
 Kisomali, - 93  
 Kisonghay. - 92  
 Kisoninke, 115  
 Kisovieti 48, 93  
 Kisto. - 260  
 Kisu - 65,67  
 Kisudan- 5,46, 50,  
 94, 102, 104, 107,  
 109,114,118,256,  
 Kisufi, 71  
 Kisundi - 317  
 Kisunni, 43  
 Kiswahili -ix,xiv, 5,  
 12,37, 51,91,92,  
 Kita 4  
*Kitab al-Ghunja* 50
- Kitala 52  
 Kitaliano 48  
 kitamaduni - 141,  
 166, 207,218, 220,  
 309  
 Kiteme, 115,  
 Kithebe - 307  
 Kitigriniya - 95, 113  
 Kitshitolo. - 237  
 Kitukolor al-Haji  
 Umar Tall, 51  
*Kitukuloor* 69  
 Kituruki 48,52  
 Kitwi, - 92  
 Kiurupa, 15  
 Kivai - 52,95  
 Kivai-Kono 115  
 Kivolta - 92  
 Kivu Edward, Mobutu - 124  
 Kiwolof - 90, 91,92, 93  
 94,115  
 Kiyahudi 113  
 Kiyoruba au  
 Kilingala ix, 92,  
 115  
 Kiyuda-Kisiria. 14  
 Kiyunani - 107,182,  
 184  
 Kizande 115  
 Kizimbabwe - 292  
*Kizulu* 106  
 Kizulu 66  
 Kizungu 11,25,27,  
 33, 42,44, 45, 48,  
 50,51,52,62, 91,92,  
 93, 103, 298  
 Klaktonia - 184  
 Klip - 212  
*Kloisani* 117  
 Koalib, 115  
 Koelle - 54, 93



- kol* - 142  
 Kollignon - 246, 246  
 Kolumnata - 244, 246  
 Kom Ombo. - 277  
 Kombewa - 241, 255  
 Komdraai. - 212  
*Komo* 64,65, 70  
*Kondofani* 115  
 Kongo - 7,33, 34,  
 44, 48,53,95, 106,  
 112,184, 187, 229,  
 231,233, 234,237,  
 238, 239, 234  
*Kono Chronicle* 12  
 Koobi Fora - 179,  
 194  
 Kopti 43  
 Kordafani 117, 307  
 Kore, 64  
 Kornelia - 214  
 Korotoro - 210  
 kosmogonia, 62  
 Koullél mdogo 72  
 Koullél, 72  
 Koumbi Saleh 60  
 Koumbi Saleh 61  
 Kristeli - 246  
 Kristo - 11, 31,32,  
 34, 36, 38, 39,  
 41,207, 209, 214,  
 217,220, 232,  
 269,270, 301,316,  
 215, 218, 246  
 Kromdraai - 170,  
 185, 210  
 Kronolojia - 8, 22.  
 159  
 Krugersdorp, - 210  
 Kubbel 41  
*Kuma*, 64  
*Kuma-nyon*,
- Kumbi 7  
 Kumbi Saleh, - 140  
 Kumbukumbu - vii,  
 viii, ix 3, 17, 36,  
 36, 38, 41, 42,  
 45,46, 52, 55,  
 56,70, 220  
 Kundi Kuu la  
 Khoisani 118  
*Kundi Zindj* 110  
 Kuñg Sang - 301  
 Kuptsov, - 298  
 Kurani 71  
 Kwa 115, 120  
 Kwañe Nkrumah 29  
 Kwango - 231, 237  
 Kwatenari - 153,  
 159, 162,168, 182,  
 183, 184, 186,274
- L. Jadin 53  
 L'Honore Naber 47  
 La Condition humaine -  
 144  
 La Mouillah - 244, 246  
 Laetolil - 170,176,  
 194  
 Lake Abay - 156  
 Lapi Lazuli - 184  
 Largeau, - 263  
 Lars Dunstrom, 14  
 Lartet - 185  
 Lascau - 244  
 Lat Dior, 52  
 Lateriti - 184  
 Latif - 64, 72  
 Latini Amerika, - 134  
*lawol fulfulde* 68  
 Leakey - 169,176,  
 177,181, 183, 185  
 Lebna Dengel, 46
- Lecufontenin, - 287,290  
 Lemurs - 168  
 Leo Africanus 11, 48  
 Leo Frobenius -  
 15,103  
 Leopoldville  
 Lovanium 19,54  
 Lepsius 113,114  
 Leptis Magna - 88  
 Leroi-Gourhan - 142  
*Les Eyzies* - 184  
 Leslau - 93  
 Lesotho 47, 284  
 Levallois - 184,185,  
 186,217,222, 227,  
 228, 229,237, 275,  
 277, 278  
 Levallois-Perret -  
 184  
 Levi-Strauss - 140  
 Lewin, - 88,89  
 Liberia - 3,16,95,117,  
 145, 269  
 Libya. - 3, 31,40,88,  
 104,241,255,93  
 Lidianiti - 184  
 Liñpopo - 127  
 Linnaeus - 183  
 Liptako, 52  
 Lirue - 268  
 Livingstone -  
 101,157, 214  
 Livy, 39  
*Lo Wasenoufo* 22  
 Loango, 33  
 Lobengula 47  
 Lobi, - 142  
 Loire - 186  
 London - 13,28,103  
 Longana - 147  
 Lopez 12

- Lothagam - 176  
 Louis 25  
 Lualaba - 128  
 Luba 110  
 Lubbock - 185  
 Lubu 33  
 Luis Moriano 112  
 Luja - 104  
 Lukuliro - 201  
 Luleji 19  
 Lunda - 237  
 Lupemba - 134, 184,  
 187, 206, 225, 227,  
 228, 229, 237, 239,  
 268  
 Luxor 80, 85  
 Iwa 70  
 Lwandjili, 33  
 Lyell - 186  
 Lyon 28
- M. Guillain; 13  
 M.C. Chamla, - 256  
 Maa Ngala 64, 66  
 Maabo 66  
 Maadi - 282, 283  
 Macina 72  
 Madagascar - 16, 51,  
 112, 122, 125, 126  
 128, 129  
 Madara 31  
 Mafarao - 8, 32, 33,  
 35, 37, 95, 107, 108,  
 129, 150, 274, 283,  
 287, 309, 310  
 Mafunjo 37, 38, 41,  
 79  
 Maghrib - 31, 35, 37,  
 39, 40, 41, 43, 42,  
 44, 48, 124, 127,  
 129, 240, 241, 244,  
 248, 275, 278, 366  
 Maghrib Maghrib  
 na Sudan 43  
 Maghribi ya Kale  
 39  
 Magosi - 184, 229  
 Mahasna, - 280  
 Mahdiyya 46  
 Mahmadu Lamine,  
 52  
*Mahram* 37, 50  
*Makalia* - 184, 225,  
 233  
 Makapani - 210,  
 215, 218, 212  
 Makapansgat - 170,  
 176, 177, 179, 180,  
 185  
 Maksai, - 293, 295  
 Malagasi, 113  
*Malakiti* - 184  
 Malawi, - 134, 284, 289  
 Maley - 153  
 Mali 4, 5, 6, 7, 9, 12,  
 17, 21, 31, 43, 58,  
 64, 65, 66, 67, 69,  
 70, 71, 135, 141,  
 145, 265, 268, 269,  
 270, 288, 289, 317  
 Maliki 43  
 Malindi 48  
 Malinke, 4  
 Malka Konture - 177  
 Malom Gaolo, 71  
 Mamadou Molom 71  
 Mame-Bantu: 33  
 Mame-Stillbaya, -  
 229  
*Mande* 115, 117  
 Maneseya 110  
 Mangala - 227
- Manient - 257  
 Manoel de Almeida,  
 12  
 Mansa Musa, 17  
 Mansa Uli 6  
 mapokeo - 4, 317  
*Mapokeo hai* - 63,  
 mapokeo simulizi 2, 3, 4,  
 5, 6, 7, 16, 26, 30, 31,  
 33, 40, 49, 53, 55, 56, 61,  
 62, 63, 65, 66, 72, 73, 140,  
 141, 297, Mapokco ya  
 Kapsi, - 269  
 Maprosimia - 166,  
 168  
 Maqdish al-Safaqusi  
 45  
 Maqrizi 42  
 Marc Block 12  
 Marekani 28, 29, 47,  
 49, 53, 74, 102,  
 107, 142  
 Marlaux, - 144  
 Marx 34, 319, 321  
 Mary Leakey - 180  
 Mas'udi na Ibn  
 Khaldum 38  
 Mas'udi 42  
*Masalik al-absar* 43  
 Masalik, 41  
 Masayidi 48  
 Mascara, - 241  
 Masen - 165  
 Mashariki 2, 13, 33,  
 44, 48, 53, 102,  
 133, 148, 165, 193,  
 195, 201, 212,  
 218, 229 mashariki  
 mwa  
 Madagascar. - 129  
 mashariki mwa

- Mediterania, 162  
 Mashariki na  
 Kusini mwa  
 Afrika - 31, 170  
 Mashariki ya  
 Adamawa, 118  
 mashariki ya  
 Afrika 294  
 Mashariki ya  
 Amerika Kaskazini  
 - 156 mashariki ya  
 bara la Afrika 42  
 Mashariki ya  
 Karibu - 129  
 Mashariki ya  
 Karibu - 41, 109,  
 246, 256, 294,  
 295, 298, 302, 305,  
 309 Mashariki ya  
 Kati 2, 3, 41  
 Mashariki ya  
 Mbali - 316  
 Mashariki ya  
 sudani 46  
 Mashariki-  
 Magharibi - 307  
 Masimia - 166, 168,  
 169, 170  
*masimulizi* 9, 48  
 masimulizi ya  
 mapokeo 57  
 Masimulizi ya  
 ngano 40  
 Masul 45  
 masuria, 6  
 Mataria 80  
 Matmar. - 279, 280  
 Matupi Cave, - 237  
 Matuyama - 146  
 Matveiev 41
- Maurice Delafosse  
 14  
 Maurice Glele 34  
 Mauritania - 40, 46,  
 60, 105, 133, 161,  
 241, 257, 260, 266,  
 284, 289, 256, 293,  
 317, Mauritania  
 Kusini - 93,  
 Mauritania  
 ya Kaskazini, 94,  
 255  
 Maurusi - 244,  
 246, 248, 254, 257,  
 278  
 Mazer, - 254  
 Mazeri - 184  
 Maziwa Makuu 59  
 maziwa ya Sahara -  
 157  
 Mbali - 193  
 Mbwe - 180, 181  
 McGaffey 59  
 Mdaga 34  
 Mdogoni 65  
 Mechta el Arbi - 244  
 Mechta-Afalou. - 248  
 Medina 41  
 Mediterani 11, 39,  
 102, 114, 125, 127,  
 128, 135  
*Mediterania* -  
 156, 161, 162, 241,  
 244, 248, 256, 301,  
 302, 307, 321  
*megalith i* - 231  
 Mehander 38  
 Mehen. - 294  
 Meinhof - 92, 104,  
 114
- Mel 110, 117  
 Melika Konture -  
 199, 201, 206  
 Memfisi, 308  
 Memphis- Fayun - 309  
 Menelik II 46  
 Meniet - 260, 285  
 mer - 95  
 Merimde-Beni  
 Salame - 308  
 Merimdi - 281, 282  
 Meroe 117, 272, 313  
 Mesolithi - 134, 135,  
 184, 196, 229, 250,  
 256,  
 Mesopotamia - 104,  
 137, 298, 308, 316  
 Mfalme Napoleon<sup>1</sup>  
 2 Mfalme wa  
 Segou 4  
 Miguel Cervantes 45  
 Mile Homburger - 92  
 Milima Kenya - 148  
 Milima Kenya na  
 Kilimanjaro - 124  
 Milima ya Alps -  
 122, 183, 185,  
 186, 187, milima  
 ya Atakora - 266  
 Milima ya Atlas  
 148, 250, 318  
 milima ya  
 Drankensberg, -  
 220 milima ya  
 Ethiopia - 307  
 Milima ya Futa  
 Jallon - 266  
 milima ya  
 Kameruni. - 265  
 milima ya  
 Maghrib, - 122

- milima ya Tibesti  
 – 284  
 Mindel, - 152, 181,  
 183  
 Miosini – 166, 168  
 Misri – ix, 1, 32, 33,  
 35, 37, 38, 40, 41,  
 42, 43, 44, 78, 80,  
 85, 92, 98, 107,  
 129, 133, 136, 143,  
 149, 270, 278, 281,  
 282, 289, 302, 305,  
 308, 312, 313, 319,  
 320,  
 Mji wa Mungu. - 319  
 Mlima Elgon – 148,  
 Mlima Ruwenzori  
 – 148 mlima wa  
 Mlima wa  
 Kilimanjaro, - 122  
 Mncgro 13, 14, 104  
 Mokhtar Sussi 45  
 Molo - 208  
 Molon Gaolo, 71  
 Momolu Duwela  
 Bukele 52  
 Monomotapa. – 129,  
 293, 301  
 Monrovia 16  
 Morice 52  
 Moroko 3, 181, 184,  
 187, 240, 241, 244,  
 246, 255, 284, 302  
 mosaics -184  
 Moscow 13  
 Moshesh 47  
 Mossi wa Yatenga - 143  
 Mosteri - 150  
 Moulouya - 185  
 Mount St. Paul, - 290  
 Mount Wilhelm -  
 159  
 Moussou, 22  
 Movius - 180  
 Msumbuji - 124  
 Mt. Agustino 39, 39,  
 40, 319 Mt.  
 Cyprian 39 Mt.  
 Helena). – 125,  
 126  
 Mtawa Bahrey 46  
 Mto Dhar Tichitt-  
 Walata. – 260  
 Mto Gambia – 265  
 Mto Gambia, - mto  
 Kafu – 180, 183 mto  
 kagera – Mto Kamoa –  
 227, 234, Mto  
 Kongo – 231,  
 301 Mto Naili Mto  
 Niger – 2, 48, 72,  
 127, 128, 265, 266,  
 273, 305, 307,  
 316, Mto Nile –  
 127, 128, 148,  
 149, 256, 270, 275,  
 307, Mto Omo  
 148, Mto Orange –  
 47, 215, mto  
 Senegal, 266, Mto  
 117 Tefassasset –  
 Mto Ubangi 238,  
 mto Vaal – 212,  
 Mto wa Benue.  
 128 Mto Wadi,  
 Mto Saura, 254  
 Mto Zaire 27, 128,  
 Mto Zambezi 12,  
 44, 127  
 Mtukoko 14  
 Mtume 56  
 Muhammad 22  
 Muhammad al  
 Tilimsani 45  
 Muhammad Ali 45  
 Muhammad  
 Ghalbun 45  
 Mukarvovsky 117  
 Mukhtar Wuld 46  
 Muller 114  
*mumuya* 68  
 Mungo Park 49  
 Mungu, 32, 64, 66,  
 67, 136, 310, 319  
 Mustajidda – 279, 280  
 Muster – 181  
 Musteri – 184, 185,  
 218, 237, 241, 244,  
 246, 255, 275,  
*Musteri ya Kinubi,*  
 - 275,  
*mvet* 5  
 Mwafrika 6, 8, 71,  
 90, 108  
 Mwami 18  
 Mwanganda - 214  
 Mwene Mutapa - 44  
 Mwislainu- 48  
 Myoruba- 51  
 Mzilikazi, 47  
 N.I. Vavilov - 298  
 N' Ajjer - 284  
 Nachikufa - 133  
*Nagada* – 279, 280  
 Nagada I – 282, 283  
 Nagada II - 308  
 Naivasha - 148  
 Nakuru – 135, 148,  
 182, 208, 225, 229,  
 233

- Nama , 64  
 Namibia 47, 108,  
 131, 217, 220, 284,  
 289, 291  
 Napata - 313  
 Napier - 183  
 Napoleon 45  
 Nara 71  
 Narosura - 208  
 Natal 47, 215, 293  
 nathari 4  
 Nazi 19  
 Ndutu - 165  
 Neanderthal - 193,  
 244, 295, 316  
*ned (a)* - 91  
*neddo* - 91  
*neds* - 91  
 Neferwptah 79  
 Nema 46  
 Neolithi - ix, 85, 133,  
 134, 135, 150, 184,  
 185, 196, 208, 229,  
 231, 238, 244, 246,  
 248, 256, 257, 260,  
 260, 265, 269, 274,  
 275, 277, 278, 281,  
 283, 286, 289, 291,  
 307, 308, 311, 318,  
 320,  
 Neolithiki 43, 250  
 New Guinea - 101,  
 159  
 Ngai (Mungu) 18  
 Ngwane - 284  
 Nhampassere - 269  
 Niafunke 71  
 Niani, 77  
 Nicolas Guillani 28  
 Niger 9, 21, 40, 70,  
 105, 127, 156, 157,  
 255, 256, 265, 269,  
 284, 287, 301  
 Niger-Chad - 91,  
 Niger-Kongo 33,  
 110, 115, 117, 118,  
 120, Niger-  
 Kordofan 115  
 Nigeria 9, 14, 16, 59,  
 71, 72, 77, 145,  
 266, 268, 270  
 Nigeria Kusini 32,  
 58, 95 Nigeria ya  
 kaskazini 50  
 Nigeria ya Kusini  
 Mashariki, 52  
 Nile - 135, 137, 301,  
 302, 316 Nili nycupe -  
 233 Nili ya Kati -  
 208 Nili ya Misri -  
 294 Nili-Abyssinia,  
 305 NiloI-Sahara 110,  
 117, 118  
 Nimba - 126  
 Njarassi - 218  
 Njoya 52  
 Nsibidi 32  
 Nsongezi - 201  
 Ntereso, - 270  
*ntinu* 33  
 Nubia 104, 120, 274,  
 275, 280, 284,  
 292, 311, 313  
 Nubia ya Misri -  
 277, 283 Nubia ya  
 Sudani, - 283  
 Nuhu 113  
*numusira* 68  
 Nungunungu - 206  
 Nuri. -- 75, 275  
 Nuwayri 43  
 Nyanda za juu za  
 Afrika Mashariki  
 120 nyanda za  
 juu za Jos, 120  
 Nyanda za nyasi  
 - 134 nyanda za  
 nyasi za Nyani 4  
 nyaraka viii  
 Nyawoole 64  
*nzo* 34  
 O.E. Vida 113  
 Oasisi ya Kharga. - 277  
 Oba wa Benin - 296  
 Obenga, - 96, 98  
 Obligosini, - 168  
 Occiptali torus - 176  
 Ohemhit. - 279  
 Olaudah Eqino 51  
 Olderogge 117  
 Oldowani - 177,  
 185, 199, 201, 212,  
 214, 215, 226, 265  
 Olduvai, - 83, 165, 176, 177,  
 179, 180, 185, 193, 199, 218,  
 226, 234  
 Oligopithecus, - 168  
 oligosini - 183  
 Ologopitheko - 169  
 Oloregsailie - 201  
 Oinari A - 282  
 Omo - 170, 176, 177  
 Oran - 289  
 Orange - 127, 284, 218, 293  
 Orange Free State - 182  
 Oranois - 284  
 Oreopitheko  
 bambolii - 169  
 Osei Tutu 19

- Osteodontokerati - 177, 179  
ostrakani<sup>1</sup> 37, 38  
Ottobach Cugoano 51  
Ouassoulou 6  
Oxford. - 87  
Oyo 8, 21
- P:V. Tobias - 176  
Pacheco Parreira, 7  
Padri Teilhar de Chardin - 186  
Paiva 53  
Pakistan - 169  
Paleolithi - 187  
paleobotania 30  
Paleolithi - 134, 180, 181, 184, 185, 196, 218, 246, 250, 254, 255, 256, 268, 275, 277, 281, 298,  
Paleolithi ya chini - 184  
Paleolithi ya kale - 181, 183  
Paleolithi ya Kati - 182, 241  
Palestina - 104, 278, 283, 308  
Pango la Hearth - 215  
Pango la Philip na Brandberg, - 289  
*Parapithecus*, - 168  
Paraustral-  
Paris ix, 13, 27, 28, 137  
Patrice Lumumba 29  
Pedro Paez 12  
Pei - 186
- Pembe ya Afrika 36, 37, 39, 48, 102, 120, 305  
Periplus of the Erythraean Sea 11  
Peter Kolb 47  
Peters 2  
Pigafetta 12  
Pignari 65  
Pithekanthropo - 182, 183  
pitheko - 185  
Plaeothi - 150  
Platirrina - 166, 168  
Pleistosini - 146, 147, 148, 149, 150, 154, 156, 161, 170, 183, 185, 190, 193, 194  
Pliny Mkubwa 11, 38, 39  
Pliny, 40  
Plio-pleistosin - 194, 185  
Pliosini - 147, 168, 170, 183, 194,  
Plotemi, 37  
Plutarch 39  
Po, - 238  
Pointe Kalina - 228  
Poland, 28  
Polybius, 38, 40, 39,  
Pongidi - 166, 169  
Port Elizabeth. - 215  
Porteres - 302  
*Pragmateia* 39  
*Présence Africaine* 16  
Prester John 46  
Price-Mars 28
- Primata - 166, 168, 169, 177, 178, 179, 181, 186, 194  
Procopius 40  
Promongwan, - 220  
Propliopithecus, - 168  
Pseudo-Scylax 40  
Ptolemy 35, 38, 39  
Ptolemy 1 - 82  
Puniki 39  
Punpun - 269  
Punt, 32  
pwani ya Afrika - 154  
Pwani ya Afrika Mashariki 117  
pwani ya Atlantiki - 113, 126, 154, 157, 270,  
Pwani ya Atlantiki ya Afrika 39  
pwani ya Guinea. - 305  
pwani ya Israeli. - 162  
Pwani ya Kaskazini 39  
Pwani ya Mashariki 9, 36, 37,  
pwani ya Mediterania - 301  
pwani ya Sahara, - 125  
Pwani za Msumbiji - 126
- QunareI samba Dondo 72  
R.A. Oliver - 298  
R.C. Lepsius, 113  
R.C. Lewontin - 101  
R.N. Cust 113  
Rabili 52

- Rahaniraka 51  
*rakire* - 142  
 Ramapitheko - 169  
 Ramendo, P.  
   Biberson - 180  
 Raombana 51  
 Rasi ya Agulhas, - 124  
   Rasi ya Guardafui. -  
   124 Rasi ya Juby 40  
   Rasi ya Khoi 47  
   Rasi ya Kusini mwa  
   bara - 22 Rasi ya  
   Vende (Kiwolof) 118  
 Recade<sup>2</sup> - 95  
 Redeyef, - 241  
 regs - 128  
 Rehoboth 47  
 Rhodesia - 53, 193  
 Richard Burton, 13  
 Richard Palmer 14  
 Rif - 124  
*Rimah Hizb al-*  
*Rahim* 51  
 Rio Muni, - 232, 233  
 Riss - 152, 161, 183,  
   187  
 Riss-W\_rm  
 Riyadh 43  
*Rkiz*, 105  
 Robert Moffat 47  
 Robinson - 187  
 Roche - 180  
 Roma 27, 38, 39  
 Rudolf - 124, 165  
 Ruffie - 101, 285  
 Rufisque - 268  
 Rumi. - 135, 320  
 Rundo - 272  
 Rwauda - 58, 60, 136,  
   179, 206, 207, 232,  
   234, 233  
 S. Robert 33  
 S.W. Koelle, 113  
*saare* - 94  
 Sabratha, - 88  
 Sadfa - 93  
 safu za milima, - 134  
 Sahara - vii, 2, 3, 11,  
   14, 21, 31, 41, 48,  
   55, 92, 102, 104,  
   107, 126, 127, 129,  
   130, 131, 134, 136,  
   150, 153, 154, 156,  
   157, 184, 186, 187,  
   207, 208, 218, 232,  
   240, 241, 244, 246,  
   248, 250, 254, 255,  
   256, 257, 260, 266,  
   268, 269, 270, 275,  
   284, 286, 288, 290,  
   291, 292, 294, 295,  
   305, 308, 316, 318,  
 Sahara ya Algeria,  
   - 254 Sahara ya  
   Chad 31 Sahara ya  
   kaskazini - 127,  
   266 Sahara ya kati,  
   - 127, 285, 268  
 Sahara ya kusini -  
   127, 255 Sahara ya  
   Mauritania - 257  
 Sahara ya Sudan  
   45 Sahel 2, 3, 7,  
   11, 12, 36, 43, 50,  
   104, 108, 126, 129,  
   137, 140, 153, 154,  
   250, 263, 269, 291  
 Saheli ya Kisudani  
   - 141  
 Sai, - 275, 279  
 Saint Acheuli  
 Saite 38  
 Sakkara - 283  
 Saldanha - 218  
 Salil ibn Razik 48  
 Salust, 39  
 Samuel Crowther 51  
 Samuel Johnson, 51  
 Samweli Johnson, 15  
*sanakuya* - 142  
 Sango - 206, 215,  
   218, 222, 225, 227,  
   228, 237, 239, 268,  
   275, 315 Sango  
   Bay - 227, Sango-  
   Lupemba - 207  
   sango -Lupemba -  
   237  
 Sansanding 72  
 Sao 34  
 Saone - 186  
 Sapir - 93, 117  
 Saqqara, 78, 80  
 Saura - 186  
 Savana - 68, 108, 109, 129,  
   133, 134, 148, 150, 194, 233,  
   263, 270, Savana ya Afrika 126  
 savana ya Kisudani, - 137, 64, 66,  
   70, 72  
 Scandinavia 27  
 Schruz. - 103  
 Scipios 39  
 Sebua, - 279  
 Sefar - 292  
 Segou 7  
 Sekopithesidi - 166  
 Selgman - 104  
*Semi za Mtume* 55  
 Semiti-Hamiti 110  
 Senegal 27, 51, 71,  
   72, 94, 108, 127,  
   135, 265, 266, 268,

- 269, 270, 272,  
Senegal-Guinea, -  
91  
Senegambia, 44  
*seret* - 78  
Servant - 157  
Sesopithedi - 169  
Shaba - 111, 221,  
225, 226, 227, 229,  
232, 233, 237, 238,  
301, 321 Shaba  
Kusini 117  
*Shahenabi* - 278, 279  
Shaka - 19, 143, 144  
*Shamaki* - 279  
Shanga - 128  
Shara, - 240  
Shaykh Musa 27  
Shaykh Salah, 71  
Shekh Osman dan  
fodio 71  
Shele - 266  
Shem 113  
Sherda, - 254  
*shisti*, 78  
Shoka la Mkono -  
199  
Shungura - 165  
Siculus 38, 39  
Sierra Leone - 16, 32,  
93, 117, 145, 269,  
273  
Silaniaka 4  
*silatigi* 64, 68  
*silsila* 71  
Silsile - 277  
Silva Correia, 12  
Sire-Abbas Sow, 50  
Sirenaica, - 246  
Siwaliks - 186  
Skandinavia - 156,  
157  
*Skundjata (Sundiata  
Fasa)* 19  
*Societe Africaine de  
Culture* 16  
Soga 47  
Sokoto, 52  
Soltani - 183  
Solutre - 187  
Somalia 32, 126  
Somme - 181  
Songhay 22, 50, 270  
Sonianke wa  
Wasonghay 21  
Sonni Ali 18  
Sonni Mkuu 18  
Sorbonne, 28  
Soro 70  
Sphinx - 89  
Springs - 293  
St. Louis 51  
Stanley 49  
Stanley Pool - 127,  
228, 231  
Steinbeck, - 144  
Sterkfontein - 170,  
176, 180, 210, 212  
Stillbay - 187, 206,  
229  
Stow - 103  
Strabo - 11, 38, 39, 40,  
312  
Stuhlmann, - 103,  
104  
Sudan 8, 11, 12, 18,  
36, 37, 41, 42, 43,  
44, 52, 59, 88, 94,  
126, 128, 129, 135,  
156, 208, 220, 233,  
250, 260, 272, 274,  
275, 277, 278, 279,  
288, 289, 295, 311,  
316, Sudan na  
Afrika ya Kati 9  
Sudan ya  
Magharibi 37, 41,  
46, 48, 50, 51, 129  
Sudan ya  
Mashariki 46, 110  
Suez 2  
*Suidae* - 177  
Sultani 52  
Sultani Njoya - 52, 95  
Sultani wa Kilwa 52  
Sultani wa Morocco  
52  
Sunaooro Kante - 143  
Sundjata, 2, 4, 21,  
62, 143  
Sungwaya 53  
Suriama 51  
Sussex 28  
Swadesh - 92  
Swana Mulunda 19  
Swartkrans - 170,  
187, 210, 212  
Swaziland, - 218  
*Ta'rikk* 15, 41  
*Ta'rikk al-Fattash*  
12, 22, 50 *Ta'rikk  
al-Sudan* 12, 22,  
50 *Ta'rikk Say* 50  
Tabaat 42  
tabaka 4  
*Tabakat* 43, 46  
Tabelbalat-Tachenghit - 241  
Tabelbalet, - 288  
Tachenghit, - 254  
*Tafineq*, - 95  
Taforalt, - 246



- Tahert 42  
*Tahoua*, 105  
 Takedetoumatime, - 293  
 Talodi, 115  
*Tamaduni* - 229,  
 283, 308  
 Tamaduni za  
 Afrika x tamaduni  
 za kale ix  
 Tamara Hat - 244  
*tambipwalo*, - 95  
 Tamentit - 288  
 Tangasi - 275  
 Tangiers - 244  
 Tamit, - 291  
 Tanzania - 83, 131,  
 147, 165, 170, 176,  
 177, 183, 185, 194,  
 199, 201, 206, 207,  
 208, 214, 226, 234,  
 240, 301  
*Tarihi* 41, 42, 45, 51,  
 161, *Tarihi* 51  
*Tarihi ya Funj* 46  
*Tarihi ya Kilwa* 51  
*Tarihi ya Ngome*  
 ya Adeni 48  
*tarsiere* - 168  
 Taruga, - 270, 272  
 Tasa - 279, 280, 308  
 Tassih - 7, 284, 286,  
 289, 293,  
 Tassili N'Ajjer, - 104,  
 256,  
 Taung - 210  
 Taylor - 94  
 Tcitus, 39  
 Tebessa - 241, 248  
 Tegali, 115  
 Tegdaoust, J.,  
 Dcvisse 33  
 Teilhard de Chardin -  
 319  
 Tell - 124  
 Tenere - 134, 260, 284  
 tengsoba - 142  
 Tensift - 187  
 Ternifine - 182, 241  
 The Martian - 290  
*The Zimbabwe-*  
*Monomotapa*  
*Culture* 15  
 Thebe. - 308, 309  
 Thebes, - 274, 275  
 Theodosius 39  
 Thianaba 72  
 Thini. - 308  
 Thomas B. Freeman,  
 51  
 Thomas Mofolo, - 144  
 Tiaret - 244  
 Tibesti. 286, 311  
 Tibilahi - 287  
*tibo* 18  
 Tichitt - 260, 289, 293,  
 295 Tichitt  
 Walata, - 317  
 Tidikelt - 255  
 Tidjami, 72  
 Tiemassas, - 268  
 Tierno Bokar 71, 73  
 Tihodaine, - 254, 255  
 Tilemsi - 256  
 Timbuktu, 3, 12, 50,  
 52,  
 Tin Felki - 291  
 Tipolitania, 45  
 Tissukari - 292  
 Tit Mellil na Ain  
 Fritissa, - 241  
*toba* 18  
 Tobias - 183  
 Togo - 120, 126, 268 Togo  
 ya Kaskazini - 140  
 Togo/ Atakora, - 266  
 Tondidaru, - 272  
 Tor Irstam, 14  
 Tougan, 65  
 Transvaal - 170,  
 179, 185, 210, 215,  
 217, 220, 284,  
 289, 131  
 Tripoli 14, 45, 52  
 Tropiki ya Ikweta 36  
 Tshitolo - 225, 229,  
 234, 239 Tshitolo  
 ya Kale - 237  
 Tshitolo ya Nyuma  
 - 237  
 Tucker - 93  
 Tumtum 115  
 Tunis 11, 46  
 Tunisia - 45, 124,  
 133, 183, 241, 244,  
 246  
 Turkana - 124, 135, 170,  
 Turkana (Rudolf), - 148  
 Tuscancy - 169  
 Tutankhamen 79  
 Tuwat, - 288  
 Uchina - 125, 176, 177, 193  
 uchunguzi 1, 5, 6, 7,  
 17, 26, 27, 28, 29,  
 31, 36, 41, 52, 53,  
 60, 74, 75, 78, 79,  
 80, 81, 84, 87, 92,  
 146, 149, 154,  
 157, 162, 165, 177,  
 188, 195, 199, 210,  
 212, 220, 286,  
 287, 295, 296, 302  
 Uele - 238

- Ufaransa -24, 25, 27,  
28, 53, 103, 181,  
182, 184, 184, 185,  
186, 187, 244,  
285, 294,  
Ufilipino - 168  
Uganda - 15, 18,  
148, 169, 180, 183,  
184, 186, 201, 206,  
226,  
Ugiriki - 162, 186  
Ugiriki ya kale,  
vii  
Ugusburg, - 296  
Uhispania -42, 294  
Uholanzi, 53  
uhuru viii, xi,, 6, 16,  
25, 28, 56  
Uingereza - 24, 53,  
104, 184  
Uislamu 23, 27, 38,  
40, 43, 45, 50, 55,  
70,  
Ujerumani - 19,  
182, 185, 186  
ukoloni ix, 2, 6, 9,  
15, 16, 19, 26, 27,  
28, 34, 53, 61, 93,  
117, 135, 284,  
Ukristo. - 3, 23, 27, 32  
39, 231, 233, 234, 238  
239, 244, 248, 256, 260,  
265, 268, 286, 289  
272, 273, 266, 307,  
312,  
Ulaya - ix, 3, 11, 12,  
13, 23, 24, 25, 28,  
29, 34, 45, 46, 47,  
48, 51, 52, 53, 74,  
103, 104, 124,  
145, 146, 147,  
149, 150, 157, 181,  
182, 183, 184, 186,  
193, 196, 201,  
218, 241, 285,  
294, 298, 314,  
315, 316, 318,  
320, 321 Ulaya  
Kaskazini. - 152  
Ulaya magharibi -  
53, 185, 319 Ulaya  
ya Mashariki na  
Kati 27 Ulaya ya  
Mediterrania. - 248  
*Ule* 6  
Umar bin Shabba, 41  
Umayyadi, 36  
Unubi - vii, 31, 38, 41,  
42, 48, 129, 208,  
280, 311 Unubi ya  
Misri - 27, 275, 279,  
280, Unubi ya  
Sudani - 275  
Upemba - 233  
Ureno, 53  
Urusi 28, 113  
Usonali 9  
utamaduni - 3, 5, 15,  
140, 201, 207, 208,  
227, 229, 231, 254,  
255, 257, 269,  
272, 274, 278, 279,  
280, 281, 282,  
283, 290, 294, 311  
utamaduni wa  
Mbwe - 254  
Utamaduni wa  
Zana za Mbwe -  
199  
Uthman dan Fodio  
51  
utumwa, viii, 1, 2, 7,  
13, 19, 34, 321  
Uturuki 45, 52, 169,  
186  
  
Vaal - 284  
Vai, 3  
valdai - 159  
*Valih* 69  
Vana Zinderen  
Vasco da Gama 48  
Vavilvo - 302, 305  
Vereemiging. -212  
Victoria, - 124  
Victoria West - 222,  
226, 275  
Vienna 40  
Vilafansia - 162  
vilima vya Atakora - 268  
vilima vya Togo. - 266  
Villafranca d'Asti,  
Piedmont, - 187  
Villafransiani -  
185  
visaasili 17, 18, 19,  
67, 141, 290, 293  
Visiwa vya - Papua. 318  
visiwa vya Cape Verde 120,  
177 vita kuu vya kwanza -  
103 Vita Kuu vya Pili  
viii, 2, 16, 24, 25, 298, 104  
Vita vya Msalaba 27, 46 Vita vya  
Vanda 40 Volta Kongo 120  
  
Würm - 233  
W.E.B. Dubbois 28  
W.F. Libby - 82  
W.G. Randles - 298  
W.H.I. Bleek 92, 113  
W.L. Hansbury 28

- W.W. Howells - 314  
 W.W. Rostow 27  
 Waadeni, 49  
 Waafrika - vii, viii,  
 6, 12,16, 17,  
 18,19, 22, 23,  
 24,25, 26,27, 28,  
 41, 47, 49, 50, 51,  
 53,100, 102,  
 107, 129, 131,  
 135, 136, 298, 315,  
 317, 318, 319,  
 Waakan 23  
 Waalda, 34  
 Waalladiani 22  
 Waarabu - 14,,36, 38,  
 40, 90, 95,131, 296  
 Waarmenia 48  
 Waaryeni - 102  
 Waasiria - 143  
 Waateri - 244, 246  
 Wabambara - 7,94,95  
 Wabantu - 7, 9 36,  
 53,92,104, 109,  
 111,220, 232, 285,  
 293,296, 318  
 Wabariba 34  
 Wabassa 52  
 Wabateke 59  
 Waberiberi - 31, 40,  
 102, 107, 130,273  
 Wabisa - 92  
 Wabubi 110  
 Wabumi 31  
 Wabyzentine 40  
 Wacheki, 46  
 Wadachi - 36, 48, 49,  
 277,499  
 Wadachi Wadi -  
 277  
 Wadi Echid - 288  
 Wadi Halfa. - 275  
 Wadi Jerat - 286,- 293  
 Wadi Saura - 255, 256  
 Wadi-el-Natrum 80  
 Wadi-Hammamat 78  
 Wadinka 108  
 Wadogoni 58, 68,  
 68, 71,95  
 Wadravidi - 318  
 Wadyola, - 145  
 Wadyoro - 145  
 Waefik 32  
 Waambu 57  
 Waethiopia, - 102,  
 107,318  
 wafalme 4  
 Wafan - 101  
 Wafangi 5  
 Wafaransa 49  
 Wafoni, 34  
 Wafulani - 6,7,14,  
 31, 56, 66, 68, 68,  
 70,71, 72,90,92,  
 94,102, 104,  
 136,318  
 Wagadugu - 143  
 Wagala 46  
 Wagaramante - 272  
 Wagiriki 28,90  
 Wagogon; 8  
 Wagouro 57  
 Wagurma - 95  
 Wahabeshi - 104  
 Wahadza 108  
 Wahadzapi 109  
 Wahaiksosi - 104  
 Wahamiti - 9, 104,  
 143  
 Waharatini - 102  
 Wahausa - 9, 21, 56,  
 102, 135,144  
 Waherero 47  
 Wahikso - 294,312  
 Wahilali 36  
 Wahiso 31  
 Waiberia - 224, 278  
 Waibo - 95,145  
 Waibrania - 104  
 Waidonia 59  
 Waingereza 49  
 Waislamu - 14,46,94  
 Wajerumani 49  
 Wajuda, 34  
 Wakabre - 140  
 Wakapsi - 248, 295  
 Wakariteji 40  
 Wakaspi - 278  
 Wakhoikhoi - 104,  
 109, 295  
 Wakhoisani - 296, 317, .  
 318  
 Wakikuyu 18,32  
 Wakiroi 31  
 Wakongo 59  
 Wakuba 58, 59  
 Wakulango. - 142  
 Walata, 46  
 Walobi  
 Waluba 56  
 Walunda 21  
 Waluo 9  
 Wamacinanke 72  
 Wamaahi, 34  
 Wamamluki 37  
 Wamande - 144  
 Wamangbetu, - 143  
 Wamarekani weusi  
 29  
 Wamarka - 72,92  
 Wamasai - 57,104,136  
 Wambochi 33  
 Wamende 52,68

- Wamoor 9  
 Wamosi - 5,9, 18,  
 21, 56,94,135  
 Wanachikufa - 134  
 Wanailoti 37  
 Wanama 47  
 Wanegro - 92, 93,  
 94, 104, 109, 114,  
 207, 218,273, 295,  
 317  
 Waneolithi - 257, 278  
 Wangoni 6  
 Waniloti - 102,318  
 Wanomadi - 12,124,  
 278  
 Wanubi - 95  
 Wanyakyusa 6  
 Wanyoro 18  
 Waoromo 57, 104  
 Waotavi 109  
 Waporo - 22,145  
 Wapuniki - 95  
 Wareno 36,46, 48,  
 49, 51,110  
 Warga. 48  
 Warmenia 46  
 Warumi - 80,135  
 Warusi - 46,118  
 Wasandawe - 109  
 Wasani - 47,92,108,  
 109, 218 220, 293,  
 295  
 Wasarakole 72,- 92  
 Wasavi, 34  
 Wasemiti, - 104  
 Wasenoufo, 9, 145  
 Waserer, - 92  
 Washanti 52  
 Washiluk 18  
 Washington - 152,  
 162  
 Wasiddi, 107  
 Wasomali - 102,  
 104, 318  
 Wasonghay - 72,94,  
 102,318  
 Wasonianke - 18,19  
 Waswidi 46  
 Wataliani, 36, 49  
 Watilemsi, - 260  
 Watokolor, - 72,92,102  
 Watoma, Wagueze  
 52  
 Watonga 57  
 Watt 57  
 Watuaregi, - 95,102,135  
 watumwa 6, 8,12,  
 51, 25, 26, 49,  
 51,52  
 Wawa - 275  
 Wawarsingili 9  
 Wawolof 108  
 Waxhosa 6  
 Wayahudi 42  
 Wayland - 184, 186  
 Wayoruba - 51,141, 272  
 Wayunani 28  
 Wazarma 18  
 Waziridi 36  
 Wazulu 47, 143  
 wazungu - 13, 15,  
 24, 26, 28, 36, 45,  
 46, 49,50, 52, 64,  
 95, 104, 136, 296  
 Weichelien, - 159  
 Weidenreich - 186  
 Westermann - 94,109,  
 110,114  
*White Nile* - 208,  
 311  
 wikeri - 181,186  
 William Amo, 51  
 Wilson, - 93  
 Wilton - 187,207,  
 220  
 Wisconsin, - 159  
 wo - 142  
 Yacub Bauchi 22  
 Yafeti, 113  
 Yagala, - 269  
 Yakut 11,43  
 Yangama - 269  
 Yatenga 17  
 Yemen 14  
 Yorubaland 15  
 Yusuf Kamal, 53  
 Yves urvoy 14  
 Zaire 12, 55, 5658,60, 108,  
 110, 111, 124,126, 131  
 Zambezi - 48,135, 233,  
 289  
 Zambia - 7,57,133,134, 193,  
 214, 215,217,218, 220, 233,  
 238, 289  
 Zandj 41  
 Zanzibar - 36,52,20  
 Zaria 21  
 Zawi. - 147  
 Zimbabwe - 14, 28, 53, 215,  
 217,220129, 141, 220, 289, 293,  
 131,  
 Zinjanthropo - 83,185,314  
 Ziwa Abay, F,  
 ziwa Chad - 37,  
 48,221, 256, 257,  
 265,268, 307, ziwa  
 Edward - 207  
 Ziwa Eyasi  
 (Tanzania) 108  
 Ziwa Kisale 60, 61

Ziwa Lisan - 162  
Ziwa Malawi -  
214 Ziwa  
Naivasha, - 208  
Ziwa Nakuru -  
185, 207 Ziwa  
Tana - 206, 147  
Ziwa Tanganyika  
- 134, 234, 237,-  
238 Ziwa Turkana  
- 148, 176, 181,  
194, 199, 201,  
207, Ziwa Victoria  
- 148,186, 206,  
227, 315  
Zumri - 255

---



## ***SHEREHE***

---

Abidjan: Abijani  
Abyssinia/Uhabeshi: Abyssinia  
Afrika Kusini: South Africa  
Afrika Magharibi: West Africa  
Afrika Mashariki: East Africa  
Afrika ya Kusini: Southern Africa  
Afrika ya Magharibi: Western Africa  
Afrika ya Mashariki: Eastern Africa  
Ajemi/Uajemi: Persia  
Ajjer: Adjdjer  
Akkra: Accra  
Aksun: Axum  
Aktika: Arctic  
Amerika: America  
Antaktika: Antaretica  
Antiokia: Antioch  
Asia Ndogo: Asia Minor  
Assajen: Assadjen  
Augustio: Augustine  
Aurinyaki: Aurignac  
Awjila: Awdjila  
Azugui: Azougui  
Bahari ya Mediterania:  
...Mediterranean Sea  
Baleari, visiwa vya: Balearic  
islands  
Bara Hindi/India: India  
Barselona: Barcelona  
Bijay: Bidjay  
Bizante: Byzantium  
Bizasena: Bizacena  
Bonde la Ufa: Lift Valley  
Buar: Bouar  
Bukini/Madagaska: Madagascar

Bussura: Boussoura  
Chokwe: Cokwe  
Daud: Daoud  
Diula: Dioula  
Efurata: Ephrates  
Ekwado: Equador  
Ethiopia/Uhabeshi:  
Ethiopia/Abbysinia  
Filandia: Flanders  
Grikwa: Griqua  
Gwadalkivir: Guadalquivir  
Hijaz: Hidjaz  
Hispania: Spain  
Hungaria: Hungary  
Irak: Iraq  
Jabal: Djabal  
Jadid: Djadid  
Jadu: Djadu  
Jaja: Djadja  
Jalil: Djalil  
Jalu: Djalu  
Jalula: Djalula  
Jama: Djama  
Janet: Djanet  
Jannan: Djannan  
Jaret: Djaret  
Jarid: Djarid  
Javal: Djaval  
Jerba: Djerba  
Jibralta: Gibraltar  
Jil: Djil  
Jilmi: Djilmi  
Judalla: Djudalla  
Judham: Djudham

Kairo: Cairo	Nyoro (ya Afrika magharibi): Nioro
Kajor: Cajor	Pasifiki, Bahari ya: Pacific Ocean
Kalabari: Calabar	Pembe ya Afrika: The Horn
Kalabria: Calabria	Punti: Punt
Kameruni: Cameroon	Rumi/Roma: Rome
Kanari, visiwa vya: Canary Islands	Sabta: Ceuta
Kanton: Canton	Saheli: Sahel
Kantor: Cantor	Saura: Saoura
Karibiani: Caribbean	Shamu, bahari ya: Red Sea
Karteji: Carthage	Shamu: Syria
Kasamansi: Casamance	Shelif: Chelif
Kastile: Castile	Shiroda: Schroda
Kilimani: Quelimane	Silsile: Silsileh
Koloni la Rasi/Cape: Cape Colony	Sirenaika: Cyrenaica
Kontonu: Contonou	Sirta: Cirta
Kordoba: Cordoba	Sisilia: Sicily
Krete: Crete	Songhai: Songhay
Krioli: Creole	Sudani: Sudan
Kuba: Cuba	Suezi: Suez
Kumbi: Koumbi (mji)	Tanja: Tangiers
Kupros: Cyprus	Tegdaust: Tegdaoust
Kushi: Cush	Theba: Thebes
Laghwat: Laghouat	Tilimsan: Tlemecen
Levanti: Levant	Tissukai: Tissoukai
Lwango: Loango	Tondidaru: Tondidarou
Maka/Makka: Mecca	Transoksania: Transoxania
Maldive: Maldives	Ubizenti; Byzantium
Marekani: U.S.A	Udachi: Germany
Mashariki ya Karibu: Near East	Ugriki: Greece (Modern)
Mashariki ya Mbali: Far East	Uhabeshi: Abyssinia
Memfisi: Memphis	Uholanzi: Netherlands/Holland
Meroe: Meroe	Ujerumani/Udachi: Germany
Metuteki: Mertoutek	Ulasia: Eurasia
Misri: Egypt	Ushelisheti: Scyelles
Mmoori/Chotara wa kiberiberi: Moor	Ussuye: Oussouye
Monte Kassino: Monte Cassino	Uturuki/-a Kituruki: Turkey/ Ottoman
Moroko: Morocco	Uyunani: Greece (Ancient)
Najid: Najid	Wahiguya: Ouahigouya
Ngazija/Komoro: Comoro	Wajaksanke: Jaxaanke
Nili: Nile	Walata: Oualata
Njimi: Ndjimi	Wan: Ouan
Nova Skotia: Nova Scotia	Warjilan: Wardjlan
Nubia/Unubi: Nubia	Wassulu: Ouassoulou
Nyamina: Niamina	Yerusalemu: Jerusalem
Nyani: Niani	Zallaka: Zallaca

## A

- (mwelekeo) tovu: centripetal  
 (Mwelekeo) pewa: centrifugal  
 -a ardhini: sub-terranean  
 -a Asheuli (kipindi kilichotangulia enzi za kale za mawe): Acheulian  
 -a Ateri: Aterian  
 -a barafuto: glacial  
 -a baridi: passive  
 -a biashara: merchantlist  
 -a kadiri: moderate  
 -a Kafua: Kafuan  
 -a kale sana: primeval  
 -a kando ya mto: riverine  
 -a karibu na ikweta: sub-equatorial  
 -a karibu na tropiki: sub-tropical  
 -a kati ya maziwa: interlacustrine  
 -a kienyeji/kijanibu: local  
 -a kifahari/-a juu: loft  
 -a kiinjili: evangelical  
 -a kikaida: stylized  
 -a kina: profound  
 -a kiosteodontokerati: osteodontokeratic  
 -a kipindi cha tatu: tertiary  
 -a Kirumi: romance  
 -a Kiyunani: Hellenic  
 -a kudhuru pande zote: internecine  
 -a kukeni: matrilineal  
 -a kulazimisha/a kudhibiti/ -a mabavu: coercive  
 -a kupenda usawa: egalitarian  
 -a kupokezana: relay  
 -a kustakimu: sedentary  
 -a kuumeni: patrilineal  
 -a Lupemba: Lupemban  
 -a majini: aquatic  
 -a makali-kuwili: biface  
 -a maumbile: physical  
 -a mawe: lithic/stone  
 -a Mosteri: Mousterian  
 -a msingi: rudimentary  
 -a mviringo: spheroid  
 -a mvua nyingi: pluvial  
 -a mwisho: terminal  
 -a mzunguko: cyclic  
 -a mzunguko: spiral  
 -a namna moja/-a hali moja: homogeneity  
 -a ncha mbili: two-pronged  
 -a pande mbili: bilateral  
 -a Sango: Sangoan  
 -a siri/-a kificho: clandestine  
 -a siri: covert  
 -a sulubu: arduous  
 -a taaluma fungamano: interdisciplinary  
 -a titio: tectonic  
 -a uchokozi: aggressive  
 -a udongo mwekundu: terracota  
 -a Ulaya Magharibi/-a Magharibi/-a Kizungu: Western  
 -a wastani/-a kiliberali: liberal  
 -a wima: vertical  
 Abiri: navigate  
 Aboti: Abbot (mkuu wa nyumba ya watawa)  
 Adilifu, -enye haki: impartial  
 Afrocentric: a mwelekeo wa Kiafrika  
 Agoni: argon  
 Agua/uaguzi: divine/divination  
 Aina awali: prototype  
 Akiki: cornelian  
 Akiolojia: archaeology  
 Akisi: reflect  
 Akropolis: Acropolis  
 Alabasta/jasi: alabaster  
 Alama: sign  
 Alluvial: - kitope  
 Amali/kazi: career  
 Amazoniti: Amazonite  
 Ambari: ambergris  
 Amiri(1): Amiri/Emir  
 Amiri(2): Amirian  
 Analojia: analogy  
 Anatomia: anatomy  
 Anfa: Anfatan



Angahewa: atmosphere  
 Anthropolojia: anthropology  
 Anthropometa: anthropometric  
 Anza/anzisha: embark  
 Arabisha: arabize  
 Arami: Aramaic  
 Asheuli: Acheuli  
 Asilia/-a mapokeo: orthodox  
 Askari wa farasi: cavalry  
 Askari wa Kituruki: janissary  
 Askofu: Bishop  
 Ateri: Aterian  
 Athari: implication  
 Atlanthropo: Atlanthropos  
 Australopitheko: Australopithecus

## B

Baa: disaster  
 Babu/inababu: ancestor (s)  
 Baganda/jamii ya Baganda: Baganda  
 Bahari Kuu: ocean  
 Bara(1)/kontinenti: continent  
 Bara(2): hinterland/inland  
 Barafuto: glacier  
 Barakala: opportunist  
 Baraza: palaver/court  
 Bari: barium  
 Basanti: basalt  
 Batli: ship's log  
 Bedui: Beduin  
 Bepari: capitalist  
 Biashara: commerce; trade  
 Biashara ya watumwa: slave trade  
 Biasharanje: exports  
 Bidaa: innovation  
 Bidhaa: commodity  
 Bidhaa: goods  
 Bidhaa za matumizi: consumer goods  
 Biokemia: biochemistry  
 Bluu iliyoiva: indigo  
 Bobari: gouge  
 Boma: compound; kraal  
 Bonde: basin  
 Bresia: Breccia  
 Bubalusi (aina ya paa): bubalus

Bubu: boubou  
 Buchari: cleaver  
 Buhuri: frankincense  
 Burini: burin

## C

Chadanthropo: Chadanthropus  
 Chama/tapo/vuguvugu: movement  
 Changamani/ a mseto: syncretic (adj)  
 Changamano/tanzo:  
 Changarawe za milimani: scree  
 Changuka: disintegrate  
 Chanzo/chimbuko: origin; source  
 Chavua: pollen grains  
 Chaza: oyster  
 Chifu/mtemi: chief  
 Chimere: Cimere  
 Chochca: agitate  
 Chonge/jino la mbele: incisor  
 Choroa: oryx  
 Chotara: mulatto  
 Chotara wa iberiberi/Mmoori: Moor

## D

Dalali: broker  
 Darubini: telescope; binocular  
 Demografia: demography  
 Dhahiri/thabiti: tangible  
 Dhalimu: despot  
 Dhibiti: control  
 Dhima/amali: function  
 Dhuria: descendant  
 Diabasi: diabase  
 Diaspora/sehemu za mtawayiko: Diaspora  
 Dini: religion  
 Dini ya kimasihhi: messianic religion  
 Dioriti: diorite  
 Diskoidi: discoid  
 Dogna: dogma  
 Dola/ nchi/ jimbo: State  
 Dola unganifu: centralized state  
 Doleriti: dolerite  
 Duara: circle  
 Duhuli: import

Dunia: earth  
Durusu: revise

## E

Ekolojia: ecology  
Eledi: shrewed  
Elektroni: electron  
Elemeo: tendency  
Endeleza(1): protract  
Endeleza(2): develop  
Endeleza(3)/kuza: enhance  
Enea: diffuse  
Eneolithi: Aeneolithic  
Enye kudandia: brachial  
Enye kuzunguka/tembezi: itinerant  
Enye mabonde na miinuko:  
undulating  
Enzi ya mawe: stone age  
Enzi/zama (1): age; era; epoch  
Enzi (2): sway  
Enzi Mpya ya Mawe: New Stone Age  
Enzi ya Chuma: Iron Age  
Enzi ya Kati ya Mawe:  
Middle Stone Age  
Enzi ya Mwanzo ya Mawe: Early Stone Age  
Enzi ya Nyuma ya Mawe: Late Stone Age  
Eosini: eocene  
Epidemolojia: epidemiology  
Epidoti: epidote  
Erevu, -epesi kung'amuta: astute  
Ethnografia: ethnography

## F

Fahiwa: sense  
Falsafa: philosophy  
Falsafa ya sheria: jurisprudence  
Famakolojia: pharmacology  
Fanasia: pharmacy  
Faraka: sect  
Fasithi: literature  
Fauna: wanyama  
Fauresmithi: Fauresmith  
Fedha/ajenti: silver  
Fenomena: phenomenon

Fenza: faience  
Ferikriti: ferricrete  
Fidia(kt): recoup  
Fidia(n): restitution  
Fifia(1): decline  
Fifia(2)/oza: decay  
Fikia (upeo au hatua fulani) ulminate  
Filolojia: philology  
Fizikia: physics  
Fiziognomia: physiognomy  
Fiziolojia: physiology  
Flinti: flint  
Flora: mimea  
Foeniki: Phoenician  
Fonolojia: phonology  
Fuawe: anvil  
Fundi-mchundo: artisan  
Fundistadi: craftsperson  
Fungu la/mfululizo wa milima: massif  
Funguvisiwa: archipelago  
Funo: duiker  
Fununu: clue  
Fuwawe: punic stone  
Fuwele: crystal

## G

Galena: galena  
Gamblia: Gamblian  
Gastropodi: gastropod  
Gesi: gas  
Geuza/badilisha: reform  
Ghafi: crude  
Gliseroli: glycerol  
Gramina (aina ya nyasi): gramineae  
Gudulia: vase  
Gumba/baa la njaa: famine  
Gunzi: Günz

## H

Hadithi/masimulizi: tale  
Hadubini: microscope  
Hagiografia/uandishi kuhusu maisha ya  
watakatifu: hagiography  
Hai: active

Hajira: migration  
 Hakiki: vet  
 Halijoto: temperature  
 Halki ya hewa: climate  
 Hamatani/pepo za kipupwe: harmattan  
 Hami/Wahami: Hamite (s)  
 Hangaiko/ uchungu wa moyoni: chagrin  
 Harakati/mapambano: struggle  
 Haram: pyramid  
 Haramia: pirate  
 Harimu: Harem  
 Harunia: Harounian  
 Hatarisha: expose  
 Hataza: patent  
 Hati unganishi: cursive script  
 Hati(1)/waraka: document  
 Hati(2) (ya maandishi): script  
 Hatua kwa hatua: piece-meal  
 Hawilisha: transfer  
 Hazimu: appropriate (?)  
 Heba/haiba kubwa: charisma  
 Hegemonia: hegemony  
 Hematiti: hematite  
 Hidrografia: hidrography  
 Hierografia/hatimchoro: hieroglyphy  
 Hilobatidi: hylobatidae  
 Himaya: empire  
 Himaya: stronghold  
 Himiza: encourage  
 Hirimu/rika: age group  
 Historiografia: historiography  
 Holosini: Holocene  
 Hominidi awali: pre hominid  
 Hominidi: hominid  
 Homo: homo  
 Homo faberi: Homo faber  
 Homo habili: Homo habilis  
 Homo sapi: Homo sapiens

## I

Ikulu/jumba la  
 mfalme/kitala: palace  
 Ikweta: Equator  
 Ihamu/kariha: inspiration  
 Iliochanganywa: compounded

Iliyogawanyika: segmentary  
 Imani za kiroho: mysticism  
 Inadi/udogma: dogmatism  
 Ingilia (mali ya mtu mwingine):  
 encroach  
 Ingiliana/mwingiliano: interact/interaction  
 Iosini: Eocene  
 Ishara: symbol  
 Isiodhahiri: Indirect  
 Isiokikomo: timeless  
 Isiokwisha/-a kurudiwarudiwa:  
 incessant  
 Isiopevuka: naive  
 Isiyopenyeka/isiyolingilika: impregnable  
 Itale/graniti: granite  
 Itikadi: ideology

## J

Jaala: fate  
 Jabrudia: Jabrudian  
 Jadeiti: jadeite  
 Jaha: glory  
 Jalizi: auxiliary  
 Jalizia: supplement  
 Jalo: Djalo  
 Jamaa: relations  
 Jamaa/familia: family  
 Jamia/mbari kuu: race  
 Jamii: society  
 Jamii ya kijadi: traditional society  
 Janibu: locality  
 Jarabati: empirical  
 Jasperi: Jasper  
 Jasuri: adventurer  
 Jenasi: genus  
 Jenetiki: genetic  
 Jeramna/Wajeramna: Djeramna  
 Jerontokrasia: gerontocracy  
 Jibu/jibizo/itiko: reaction  
 Jimbi: cocoyam/taro  
 Jimbo/mkoa: canton  
 Jinasibisha: adapt oneself  
 Jiolojia: geology  
 Jiomofolojia: geomorphology  
 Jiosumaku: geomagnetic

Jiwemoto: silex  
 Jumuiishi: encompassing  
 Junuiya: community  
 Juso/kizuizui/kinyago: mask  
 Jusura: adventure  
 Juula: Dyula

## K

Kabaila: aristocrat; big landowner  
 Kabila/mbari/jamii: ethnic group  
 Kabla ya Sasa (KS):  
     Before Present (BP)  
 Kaboni dioksidi: carbon dioxide  
 Kaburi: Tomb  
 Kadiria umri: date  
 Kafara: sacrifice  
 Kafiri: infidel  
 Kaharabu: amber  
 Kainozoiki/senozoiki: Cenozoic  
 Kaka: shell  
 Kalabria: Calabrian  
 Kalautala: stereotype  
 Kaledoni: Caledonite  
 Kali/potasi: potassium  
 Kalisi(1): calcium  
 Kalisi(2): chalice  
 Kalisidoni: chalcedony  
 Kalsite: calcite  
 Kaunbi: encampment; camp  
 Kauri: energy  
 Kantara: bridgehead  
 Kanuni: principle; code  
 Kanzi: repository  
 Kaolini: kaolin  
 Kapsia: Capsian  
 Kariha/muhu/uhanasisho/  
 Msukumo: inspiration  
 Karne: century  
 Karnelia: carnelian  
 Kata nakshi: engrave  
 Katalogi: catalogue  
 Katarrina: cartarrhina  
 Kategoria: category  
 Kauri: porcelain; ceramics  
 Kaya: homestead; household

Kemia: chemistry  
 Kerkopitheko: Cercopithecus  
 Khalifa: Caliph  
 Khufu/Kopti: Coptic  
 Kiafrika-Kiasia: Afro-Asiatic  
 Kiafrikaana: Africaans  
 Kiambishi: affix  
 Kiambishi awali: prefix  
 Kiambishi-tamati: suffix  
 Kibantu-mama: proto-Bantu  
 Kibaraka: collaborator  
 Kibaraka: vassal  
 Kibuyu: calabash  
 Kichocheo: motivation  
 Kichokoo/kipengele: factor  
 Kideni: Danish  
 Kidoko: click  
 Kifani: model  
 Kifinyange: ceramic; pottery  
 Kigange: Ostracow  
 Kigezo: standard  
 Kigoda: stool  
 Kigoda cha Dhahabu: Golden Stool  
 Kigumba: arrow-head  
 Kijikundi: subgroup  
 Kijisanamu: figurine  
 Kikiasi/kisifa: quantitative/qualitative  
 kikinga upepo: wind break  
 Kikombo: scraper  
 Kikwi/milenia: millenium  
 Kilindi (cha bahari): deep sea  
 Kimelea: parasite  
 Kina: rhyme  
 Kinu: mortar  
 Kinubi: lyre  
 Kinyago: mask; sculpture  
 Kinyang'anyiro/kugombania: scramble  
 Kiolezo: template  
 Kionjo: taste  
 Kipindi kisichokuwa na tawala:  
     interregnum  
 Kipindi cha kati ya barafu: interglacial period  
 Kipindupindu: cholera  
 Kisakale: legend  
 Kisasili: myth  
 Kisawe/sinonimu:

- synonym  
 Kishoka/kichanjia: chopper  
 Kisifa: qualitative  
 Kisimbwi: continental shelf  
 Kisukuku: fossil  
 Kiswidi: Swedish  
 Kita/imarisha: entrench  
 Kitala/ikulu: royal court  
 Kitanguakimbunga: anticyclone  
 Kitenzi: verb  
 Kitu yakinifu: material thing  
 Kituo cha kuhifadhi na kusambaza bidhaa: entreport  
 Kiunga: plantation  
 Kiunzi/skeletoni: skeleton  
 Kiunziakili: mental framework  
 Kiviga: rite  
 Kivinginyo/duara: gyre  
 Kivuli cha maana: shade of meaning  
 Kiwakilishi: pronoun  
 Kiwanda/shughuli ya biashara: enterprise  
 Kiwesley: Wesleyan  
 Kizalia/vizalia: offspring  
 Kizazi: generation  
 Kizimu: totem  
 Kizuizui: mask  
 Klaktonia: Clactonian  
 Kliori: Creole  
 Kodi isiyodhihirika/  
 kodi ya kificho: indirect tax  
 Kola: kola nut  
 Koloni la kifalme: crown colony  
 Komasha/futa: eradicate  
 Kongamano: symposium  
 Konsonanti: consonant  
 Konstantini: Constantine  
 Korongo: gorge  
 Kosmogonia: cosmogony  
 Kotama: sickle  
 Kronolojia: chronology  
 Kronostratigrafia: Chronostratigraphy  
 Kufuru: profane  
 Kugawa/kuunganifua/madaraka: decentralization  
 Kuingia kwa wingi: influx  
 Kuingilia/kujitia kati: intervention  
 Kujihini: self denial  
 Kujitawala: autonomy; self rule  
 Kujitawala/mamlaka/uhuru: sovereignty  
 Kukua/kubadilika/ukuo: evolution  
 Kundi la miungu: pantheon  
 Kupoteza imari: disenchantment  
 Kupri: copper  
 Kurani: Qoran/Koran  
 Kuruba: curve  
 Kusimi mwa Sahara: sub-Saharan  
 Kutawaliwa/kugangamizwa: subjection  
 Kutiisha/kutumikisha: subjugation  
 Kutotengemaa/kuyumba-umba: instability  
 Kuyumba/kutanganga: vacillation  
 Kwa kuashiria: indirectly  
 Kwaga (mnyama kama pundamilia): Qwagga  
 Kwapua: annex  
 Kwatenari: Quaternary  
 Kwatzi: quartz  
 Kwatzi: quartzite  
 Kweh tupu/halisi: down-to-earth  
  
 L  
 Lahaja: dialect  
 Lamela: lamella  
 Latitudo: Latitude  
 Leksika: lexical  
 Lidianiti: Lydianite  
 Linganifu: consistent  
 Linganishi: comparative  
 Liturujia/litujia: liturgia  
 Lodi: Lord  
 Longitudo: Longitude  
 Lugha ambishi: agglutinative language  
 Lugha ya toni: tonal language  
 Luja: wave  
  
 M  
 Maada: matter

Maafa: disaster	Manju mtembezi: troubadour
Maarufu/mashuhuri: prominent	Mapadre Weupe: White Fathers
Maasi/uasi: rebellion	Mapenzi juu ya binadamu/filantropia: philanthropy
Maasi/upinzani: insurrection	Mapigano ya wenyewe kwa wenyewe: civil conflicts
Maathura/mwathirika: victim	Mapinduzi: revolution
Mabadiliko/evolusheni: evolution	Mapokeo huru: independent tradition
Mabadiliko ya kupanda na kushuka: fluctuations	Mapokeo simulizi: oral tradition
Mabaki: vestiges; remains	Mapululu: steppe
Mabishano/ubishani: disputation/ polemics	Masegego: premolar
Madhehebu/ada ya uzazi: fertility cult	Masihi/Kimasihi: Messiah/Messianic
Madodoso (ya awali): overtures	Masihiya/-a Kikristo: Christian
Maduhuli/bidhaa zinazoingia: import(s)	Maslahi: interest
Maelezo/masimulizi: account	Matamano/matakwa: aspirations
Maenzi: anchorage	Matbaa/kiwanda cha uchapaji: press (printing)
Mafundo: initiation	Mateka: captive
Mafunjo: papyrus (reeds)	Matini simulizi: oral text
Mafuta ya mawese: palm oil	Matini: text
Mageuzi: reforms	Mauaji (ya mtu mashuhuri): assassination
Mahitajio: demands	Mauaji ya baba: patricidal
Mahuraji: export(s)	Maudhui: content
Maji ya kunde: light skinned	Mawanda: scope
Majina: nomenclature	Mazingira ya kinamasi: swampy habitat
Majusi (1): Zoroastrian	Mbari kuu: race
Majusi(2)/msihiri: inagian	Mbari/kabila: ethnic group
Makabaila/malodi: nobles	Mbinu za kujeya: flaking techniques
Makabifiano ya ana kwa ana: confrontation	Mbirikimo: Pygmy
Makamu Mkuu wa Jeshi la Wanamaji: Vice Admiral	Mbuga (ya nyasi): grassland
Makimbilio: refuge	Mbuga chachu: sourveld
Makutano/ndagano: confluence	Mbuga/pululu: steppe
Malakite: malachite	Mbuga tamu: sweetveld
Malale: trypanosomiasis	Mcha Mungu: Murabit (holy man)
Malalo: lair	Mchakato: process
Maliki: emperor	Mchangamani: syncretic (n)
Mama: proto	Mchanganyo: compound
Mama-Malkia: Queen Mother	Mchanguko: disintegration
Mamalia: mammal	Mchawi: witch doctor
Mame-Bantu: proto Bantu	Mchokozi: aggressor
Mamlaku unganifu: centralized authority	Mchoro wa mapangoni/ miambani: rock painting
Mamlaka-pacha: diarchy	Mdachi/Mjerumani: German
Mandhari: terrain/setting/landscape	Mdeni, wa-: Dane(s)
Manemane: myrrh	Medani: Theatre (of conflict)
Mangani: niangnese	

Melanini: melanin	Mkuo (wa shaba, dhahabu, n.k.): bar, ingot, nugget (copper, gold, etc)
Melczi/maczi: anchorages	Mla mizoga: scavenger
Menyu: pure	Mlangobahari: channel
Metalujia: metallurgy	Mlangomto: estuary
Meza/funika kabisa: engulf	Mlumba/mbugu: bark cloth
Mfalme mkuu: paramount king	Mnara: minaret
Mfalme: monarch/king	Mnara wa ukumbusho/kumbukumbu: monument
Mfanano/mshabaha: affinity	Mnasaba: symbiosis
Mfanya biashara/mchuuzi: trader	Mnasihi: mentor
Mfanya biashara: merchant	Mnomadi/wanomadi/wahamamaji: Nomad/Nomads
Mfekane: Mfecane	Mnyweo: evaporation
Mfoko (wa wasiwasi): upsurge	Mode of production: mtindo wa uzalishaji mali
Mfua: smith	Modeli: model
Mfuasi: disciple	Mofolojia: mophology
Mfugaji: pastoralist	Momonyoa: erode
Mfumo/mtandao: network	Monofisita: Monophysite
Mfumu/kahini: oracle	Monografia: monography
Mganga: medicineperson; healer	Morali: morale
Mgimba/mganga wa mvua: rain maker	Motifu: motif
Mgogoro/zahama: crisis	Moyo wa kujituma: initiative
Mgogoro/ingongano: conflict	Mozarabi/Wa- : Mozarabs
Mhariji/wahariji: exporter(s)	Mpangilio/mtandazo: layout
Mhashamu: Monsignor/Mgr	Mpelelezi: explorer
Mhazeli: hazel (plant)	Mpiganaji/askari: warrior
Mholanzi: Dutch	Mpini/kutia mpini: haft, handle/ to haft
Mikrokemikali: microchemical	Mpito/uhawili: transition
Mikrolithi: microlithic	Mporaji/mteka nyara: marauder
Mila ya unyumba: ritual intercourse	Mrindimo: vibration
Milenia/kikwi: millennium	Mrumi: Roman
Miosini: miocene	Msamati: lexicon/vocabulary
Mirathi: legacy	Msanii: artist
Mise/kokwa za mawese: palm kernel	Msharasi: awl
Misri ya Chini: Lower Egypt	Mshea: shea tree
Misri ya Juu: Upper Egypt	Mshikamano: solidarity
Miwati: wattle	Mshindani: rival
Mizengwe/kutawala kianza: manipulation	Msimamo: stance
Mjasirimali/mwekezaji: entrepreneur	Msimbo: code
Mji mkubwa/makao makuu: metropolis	Msimulizi/mtambaji: narrator
Mjube: jube plant	Msonge wa madaraka: political hierarchy
Mkabala: approach	Msukosuko: upheaval; instability
Mkatoba: treaty	Msukumo, kichocheo: impetus
Mkingamo: intersection	Mswidi, wa-: Swede
Mkinzani/adui: adversary	Mtabiri: seer
Mkoa/jimbo: province	
Mkongano: cohesion	

Mtafaruku/zahama: crisis	Mwelekeo/mchakato/wend/mwende/leo: process
Mtaji, rasilmali: capital	Mwelezi: cedar
Mtambaachi: reptile	Mwendeleo: continuum
Mtandao: network	Mwiba wa kigumba/ndaka: barb
Mtapo chuma: iron ore	Mwimo: column
Mtapo: ore	Mwinuko: relief
Mtarihi: chronicler	Mwinyi: lord; aristocrat
Mtawala mkuu: central ruler	Mwondoko/mguro: movement (moving)
Mtazamo: outlook	Myunani: Ancient Greek
Mtetemo: vibration	Mzingiro: siege
Mtindo wa uzalishaji: mode of production	Mzingo/pindi: bend
Muamala/mapatano ya biashara: transaction	Mzozo/ugomvi: wrangle
Muda wa kumiliki/kushika chco: tenure	
Mujarabu: tested	N
Muktadha: context	
Mumi: mummy; maiti iliyohifadhiwa kwa kutiwa mumiani	Nadharia tete: hypothesis
Mungu: God; Allah	Nasaba(1): lineage
Muongo: decade	Nasaba(2) (tawala): dynasty
Murabiti/warabiti: mara bout	Nasabu: genealogy
Muswada: manuscript	Natija: outcome
Muundo: structure	Natiri: sodium
Muungu: deity	Natiri kabonati: sodium carbonate
Mvinginyo: gyration	Nchi: country
Mvutano/fadhaa: tension	Nchi/tawala: principality
Mvuvumko/mzinduko: Renaissance	Ndagano/makutano: confluence
Mwachano wa kijeni: genetic drift	Ndani: characteristic; aspect
Mwainisho: classification	Nembo: emblem
Mwaloni: oak	Neolithi/Zama Mpya za Mawe: Neolithic
Mwamba: rock	Neolithisha: Neolithize
Mwanba masapo/tabaka: sedimentary rock	Ngegu: laterite
Mwamba wa volkano: tuff	Ngeu/ngegu: ochre
Mwamili: functionalist	Nguvu/ari: dynamism
Mwana mapinduzi: revolutionary; revolutionist	Nguvu za uzalishaji: productive forces
Mwanamageuzi: reformer	Nguvu-uzima: vital force
Mwanana: delicate	Nikeli/madini ya fedha: nickel
Mwanashajara/mnasabu: genealogist	Nitrojeni: nitrogen
Mwanasilia/mwanajadi: traditionalist	Nomino: noun
Mwanazuoni: scholar	Nukuu/unukuzi: transcribe/transcription
Mwangalizi: regent	Nusu-kipenyo: radius
Mwasho/mwako: ignition	Nutroni: neutron
Mwavi: nettle tree	Nyumba ya watawa: monastery
Mwekezaji: investor	Nyumbu: wildebeeste
	Nywele: hair



Nywele za singa: straight hair  
 Nywele za kitani/msokoto: fuzzy hair  
 Nywele za kipilipili: wooly hair  
 Nyweshea: irrigate

## O

Oana kimseto: intermarry  
 Oasisi: oasis  
 Obsidi: Obsidian  
 Ojite: Augite  
 Ombwe: void  
 Onamastika: onamastics  
 Ottomani: Ottoman

## P

Palae-: pale-  
 Paleakiolojia: palaeoarchaeology  
 Paleobotania: palaeobotany  
 Paleolithi: paleolithic  
 Paleontolojia: palaeontology  
 Paleosini: Paleocene  
 Palinolojia: palynology  
 Pambana: contend  
 Pangilia/panga/ratibu: organize  
 Papuri/karatasi za sisha: papyrus (paper)  
 Parish/parokia: parish  
 Pedolojia: pedology  
 Pembezoni: periphery  
 Pepo za msimu: monsoon (winds)  
 Petroglafia: petroglyph  
 Pigo, mshtuko mkubwa: brunt  
 Pindi/mzingo: Bend (of river)  
 Piramidi/haram: pyramid  
 Pithekanthropi: Pithecanthropine  
 Plani: plan  
 Planktoni: plankton  
 Platirrina: Platyrrhina  
 Plau: plough  
 Plaubemba: swing plau  
 Pleistosini: Pleistocene  
 Plioplestosini: pliopleistocene  
 Pliosini: pliocene  
 Plumbi sulfidi: lead sulphide  
 Pogo: lopsided

Polihedroni: polyhedron  
 Pongide: pongidae  
 Pongidi: pongid  
 Pongo: bushbuck  
 Pora/teka nyara: plunder  
 Potosha: distort  
 Primata: primate  
 Production: uzalishaji mali  
 Propaganda: propaganda  
 Prosimia: pro-Simian  
 Pundela: pundela

## R

Radiografia: radiography  
 Radiokaboni: radiocarbon  
 Radiometa: radiometre  
 Raghba/shauku: interest  
 Raghba, ari: zeal  
 Raia: subject  
 Rasi: cape/promontory  
 Regalia/nembo: regalia  
 Rejesha (katika hai/maisha ya  
 kawaida): rehabilitate  
 Rejimenti/kikosi: regiment  
 Rekebishu: adapt  
 Rika/hirimu: age group  
 Rikabu (wanyama wa  
 kusafiria): mount  
 Rudisha hadhi: rehabilitate  
 Ruwaza/sulubu: pattern

## S

Safari ndefu/treki: trek  
 Sagagego: premolar  
 Saikolojia: psychology  
 Saisi: groom  
 Sambaratika: disintegrate  
 Sanaa za maumbo: plastic arts  
 Sanaa ya ukutani: mural  
 Sanaajadiya/fanijadiya: folklore  
 Sandarusi: gum  
 Sasisha/fanya ya kisasa: modernize  
 Sawidi (kt): draft (v)  
 Sedimentolojia: sedimentology

Sekopithesidi: Cercopithecidae  
 Semiti/Wasemiti: Semite (s)  
 Sentimeta/sentimita: centimeter  
 Septa: septum  
 Serikali unganifu/ kuu: central government  
 Serikali ya wachache: oligarchy  
 Setla/mlowezi: settler  
 Shaba nyeusi: bronze  
 Shaba nyekundu/kupri: copper  
 Shadi: intensive  
 Shahidi (wa imani): martyr  
 Shajara(1): diary  
 Shajara(2)/nasabu: genealogy  
 Shamba: country; rural area; cultivated land  
 Sharia: Islamic law  
 Shazia/msharasi: awl  
 Shehe/sheikh: Shaykh  
 Shellea: Chellean  
 Sheria za mila/jadi: customary law  
 Sheria: lex (k.m.Lex Hadriana: Sheria ya Hadriana)  
 Sheria: law  
 Shinda/tiisha/teka: conquer  
 Shindwa: succumb  
 Shirikisho: confederation; confederacy; federation  
 Shisti: schist  
 Shoka: axe  
 Shoka la mkono: handaxe  
 Shore: crest  
 Shujaa: hero  
 Siagi ya mshea: sheabutter  
 Sifa bainifu: trait  
 Silabi: syllable  
 Silikati: silicate  
 Simba: codify  
 Simbi/kauri: cowry  
 Simia: Simian  
 Similisha: assimilate  
 Simulizi: oral  
 -Siokalika: uninhabitable  
 -Siokeza: recessive  
 Sisha: papyrus pith  
 Sitara: shelter

Sokota pamoja: entwined  
 Sokwe: chimpanzee; ape  
 Sokwe-mtu: orangutang  
 Sosiolojia: Sociology  
 Spektografia: spectograph  
 Spishi: species  
 Stratigrafia: stratigraphy  
 Sufii: sufi; holy person; monk  
 Sufuri/shaba nyekundu: brass  
 Suhula/nyenzo: facility/facilities  
 Suhulisha: facilitate  
 Sulubu/ruwaza: pattern  
 Susu: cradle

## T

Taaluma ya Misri ya Kale/ Misriolojia: Egyptology  
 Taamuli: meditation  
 Taathira: impact  
 Tabaka la wakwasi: leisured class  
 Tabaka la kiamali/tabaka- anili: caste  
 Tabaka (la dhahabu): seam (of gold)  
 Tabaka la makabaila: aristocracy  
 Tabakisha: stratify  
 Tafiri: frustrate  
 Tahafifu/unafuu: concession  
 Taja: cite; mention  
 Tajiriba/uzoefu: experience  
 Takadiri: destiny  
 Takriban (t.): circa (c.)  
 Takua: piety  
 Tamadunisha: acculturate  
 Tamalaki/mtamalaki: conquer/ conqueror  
 Tambulisha: characterize  
 Tangaza rasmi: promulgate  
 Tangua: abrogate  
 Tanzo/changamano: complex  
 Tao (dogo): lobate arc  
 Tapo/shule ya mawazo: school of thought  
 Tarihi: chronicle  
 Tarihia/kronolojia: chronology

Tarika/udugu: brotherhood  
 Tasia: industry  
 Tasia ya Wilton: Wilton Industry  
 Tata: complex  
 Tawala: dominant (mf. tabaka tawala)  
 Tebo/jedwali: table  
 Teka/twaa: annex  
 Telegrafu/simu ya kuandika: telegraph  
 Tendeza: activate  
 Teokrasia: theocracy  
 Teolojia: theology  
 Thabiti: strong; valid  
 Thori: thorium  
 Tia akilini: imbibe  
 Timamu: detail  
 Timbe/mtapo: ore  
 Toa utumwani: manumit  
 Tohoa: adapt  
 Tokeo: result  
 Tondoti: detail(s)  
 Toni: tone  
 Topografia: topography  
 Toponimia: toponym  
 Towashi: eunuch  
 Towe: clay  
 Trapezoidi: trapezoid  
 Tukio: episode  
 Tuliza: placate  
 Tumbawe: coral  
 Tumiliwa/tumilizi: applied  
 Tungamanisha: integrate  
 Tungazi: terrace  
 Ture: Toure (name of person)  
 Tuta la mchanga: sand dune  
 Twaa: conquer  
 Typology: uainishi

## U

Uamili: functionalism  
 Uamsho/mzinduko/mvuvu mko:  
 Renaissance  
 Uasi/maasi: rebellion  
 Uarakala: opportunism

Ubishani: controversy  
 Ubwe/mbwe: pebbles  
 Uchamungu: piety  
 Uchangamani: syncretism  
 Uchanganuzi: analysis  
 Uchanjaji chale: scarification  
 Uchifu: chiefdom; chieftaincy  
 Uchimbuzi: excavation  
 Uchochezi: agitation  
 Udhalimu: despotism  
 Udhanifu: idealism  
 Uelekeo: direction  
 Ufalme: kingdom  
 Ufalme Mkongwe (wa Misri): Old Kingdom  
 Ufalme wa Zama za Kati (wa Misri): Middle Kingdom  
 Ufalme Mpya (wa Misri): New Kingdom  
 Ufanano: homogeneity  
 Ufinyanzi/infinyanzi: pottery/potter  
 Ufugaji: pastoralism  
 Ufuo: shoreline  
 Ugasumaku: magnetic field  
 Uhai: vitality  
 Uhalisia: realism  
 Uharibifu mkubwa: depredation  
 Uhuru/kujitawala: independence  
 Uimara/ wepesi wa kujirekebisha: resilience  
 Ujeya (njeya): flake(s)  
 Ujirani: proximity  
 Ujumlisho: generalization  
 Ujusi/sihiri: magic  
 Ukabaila: feudalism  
 Ukadiri: moderation  
 Ukali/ukatili: ferocity  
 Ukali/inkazo: intensity  
 Ukanda/zoni: zone  
 Ukanda/eneo: region  
 Ukhalifa: caliphate  
 Ukilia: determine  
 Ukinzano: contradiction  
 Ukiritimba/uhodhi: monopoly  
 Ukomesaji utumwa: abolition (of slavery)

Ukoo: clan  
 Ukuo/ukuzi: evolution  
 Ukwapuzi: annexation  
 Ukwasi: opulence  
 Ulikaji: weathering  
 Ulimwengu: universe  
 Ulinganifu: equilibrium  
 Ulokole: fundamentalism  
 Ulumbi/ufasaha wa lugha: rhetoric  
 Umiundo: structuralism  
 Umma: populace  
 Unasaba/udugu wa damu: kinship  
 Unasi: populism  
 Unda upya: reconstruct  
 Unda: construct; manufacture  
 Unganifu/enye mamlaka kuu: centralized  
 Unganifua: de-centralize  
 Ungaunga wa dhahabu: gold dust  
 Unyevuhewa: humidity  
 Uongozi: helm  
 Uowevu/unyevu: moisture  
 Upatanishi: mediation  
 Upungufu/uhaba: dearth  
 Urani: Uranium  
 Urari hafifu: delicate balance  
 Urasimi: classicism  
 Urazini: consciousness  
 Urea: urea  
 Urithi (wa utawala): succession  
 Usawa: equity  
 Usawa wa bahari: sea level  
 Usemi: saying  
 Ushahidi/ushuhuda: testimony  
 Ushuhuda simulizi: oral testimony  
 Usimilishaji: assimilation  
 Ustaarabu: civilization  
 Ustadi/ubunifu: ingenuity  
 Usuli: background  
 Utamaduni: culture  
 Utamaduni yanikinifu: material culture  
 Utamakani wa watu: peopling  
 Utamalaki: supremacy; conquest  
 Utambulisho: identity

Utambuzi: enlightenment  
 Utando: crust; patina  
 Utando barafu: ice sheet  
 Utangamano: harmony  
 Utani: joking relationship  
 Utanzo: complex  
 Utanzu: genre  
 Utata: ambiguity; complexity  
 Utawala wa kidini: theocracy  
 Utawala huria: anarchy  
 Utawalamsonge: bureaucracy  
 Utendi: epic  
 Utengemano/uthabiti: stability  
 Utengemano: stability  
 Utengenezaji/usindikaji: processing  
 Uteuzi asili: natural selection  
 Utondoti: detail(s)  
 Utumwa: slavery  
 Utumwa wa viungani: plantation slavery  
 Utwazi: supremacy  
 Ukilizizi: determinism  
 Uundaji miji: urbanization  
 Uunganifishaji: centralization  
 Uvamizi wa ghafla: incursion  
 Uvamizi: incursion  
 Uwanda wa juu: plateau  
 Uwekezaji: investment  
 Uwili: dual; duality  
 Uzoefu/tajiriba: experience

## V

Vekta: vector  
 Vertebrata: vertebrate  
 Viazi mishea: tubers  
 Vikundi (ndani ya kundi kubwa): factions  
 Vita vya msalaba: crusade  
 Vuguvugu la ukomeshaji: utumwa: abolitionist movement  
 Vuka mpaka/kiuka: transcend  
 Vuruga: disrupt  
 Vurugu: disruption

## W

Waali: elite  
 Waasaki: Asax (people)  
 Waayubi: Ayubids  
 Wadachi: Germans  
 Wadhishsha: weka wazi  
 Wadi: wadi  
 Wafunji: Funj  
 Wagothi: Goths  
 Wahafsi: Hafsids  
 Wahemcaji: gatherers  
 Wahka: insecurity  
 Waholanzi: Dutch  
 Wajabal: Djabals  
 Wajaksanke: Jaxaanke  
 Wajuula: Dyula/Juula (people)  
 Wakati/wakaa: duration  
 Wakazi walowevu/wastakimu:  
 sedentary people  
 Wakelwi: Kel Wi (people)  
 Wamaliki/Kimahiki: Maliki/Malikitte  
 Wamarini: Marinids  
 Wamethodi: Methodists  
 Wamoravi: Almoravids  
 Wangwa: lagoon  
 Waottoman: Ottomans  
 Waraka: document  
 Wari/waliofundwa: initiates  
 Wasaffari: Saffarids  
 Wasanhaja: Sanhadja (people)  
 Wasenufu: Senoufo people  
 Wasirkassi: Circassians  
 Wasta: intermediary  
 Wattasi: Wattasids  
 Wazawa: autochtons; indogens  
 Wekeza: invest  
 Wendo/machakato: process  
 West Indies: West Indies  
 Woto/mimea: vegetation

## Y

Yeli: griot

## Z

Zaka: toolkit  
 Zama za Mawe: Stone Age  
 Zambarau: violet  
 Zana: tool  
 Zana ya wajihhi tatu: trihedral  
 Zana za ujeya: flaked tools  
 Zebu: smallhorned cattle  
 Ziada: surplus  
 Zidua: extract  
 Zima/zuia: suppress  
 Zingia/zuia: blockade  
 Zinjanthopi: Zinjanthrope  
 Zinjanthropus: Zinjanthropo  
 Zuio: blockade  
 Zumaridi: emerald

## Historia Kuu ya Afrika

*Historia* hii inatoa mwanga juu ya umoja wa kihistoria wa Afrika pamoja na uhusiano wake na mabara mengine, hasa Amerika na Karibian. Kwa muda mrefu aina zote za taarifa za kubuni na hisia pendelevu zimeficha historia ya kweli ya Afrika kwa ulimwengu kwa jumla.

Kwa kujumuisha maarifa yetu juu ya Afrika, tukiweka bayana maoni mbalimbali kuhusu tamaduni za Afrika na kwa kupitia upya historia, *Historia* hii ina manufaa ya kutoa mwanga na uvulivuli na kueleza bayana tofauti za mawazo ambazo zinaweza kuwepo baina ya wasomi.

## Mapitio ya Majuzuu yote

"Mazau ya mwanzo ya UNESCO ni lazima yasifiwe kuwa ni mchango mkubwa wa kitaaluma."

Roland Oliver, *Times Literary Supplement*

"Ni mojawapo wa miradi mikubwa ya kitaaluma iliofanyika katika karne hii."

*West Africa*

"Majuzuu haya yametolewa kwa unadhifu mkubwa lakini yana bei nafuu sana ... Yanawakilisha matumizi mazuri kabisa ya pesa ambayo mnunuzi yeyote wa vitabu anaweza kuyapata ..."

Basil Davidson, *Third World Quarterly*

## I Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika

Juzuu la 1 linahusu Historia ya Awali ya Afrika na mbinu zake. Sehemu ya mwanzo ya juzuu hili inaangalia umuhimu uliowekwa na jamii za Kiafrika kuhusiana na mambo yao ya kale na maendeleo katika taaluma ya historia ya Afrika, pamoja na maelezo ya jumla ya vyanzo na mbinu. Hii inafuatiwa na maelezo ya kumbukumbu za awali za kimaandishi, simulizi zilizopo na akiolojia ya Kiafrika na mbinu zake. Sura 10 - 12 zinajadili isimu na uhamaji. Baada ya hapo, kuna sura mbili kuhusu jiografia ya kihistoria na mjadala wa kiunzi cha tarihi kilichotumika.

Nusu ya pili ya juzuu hili inahusu hasa watu wa mwanzo na historia ya awali ya Afrika kulingana na maeneo ya kijiografia: Kaskazini, Kusini, Mashariki, Magharibi na kati, Bonde la Nili likiwa limepewa umuhimu wa pekee. Sura zinachunguza sanaa, mbinu za kilimo na maendeleo ya kusana chuma ya kipindi hicho.

**TUKI • CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM • UNESCO**

S.L.P 35110, Dar es Salaam

ISBN 9976 911 40 8